Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 29 Juni, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA NA OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**

Randama ya Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri**.**

Na. 99

## Halmashauri za Ushetu na Msalala Kuanza Kazi

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI)** aliuliza:-

Kati ya Halmashauri tatu katika Wilaya ya Kahama ni Halmashauri moja tu ya Mji wa Kahama ndiyo imepata Hati ya kuanza kazi:-

(a) Je, ni lini Halmashauri za Ushetu na Msalala zitaanza rasmi?

(b) Kwa kuanzishwa kwa Halmashauri ya Ushetu na Msalala. Je, ni nini hatma ya Halmashauri ya Wilaya ya Kahama?

(c) Je, wapi yatakuwa Makao Makuu ya Halmashauri hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, taratibu za kuanzisha Halmashauri za Msalala na Ushetu zinafanywa kwa mujibu wa Sheria Na. 7 ya Serikali za Mitaa ya Mwaka

1982 kifungu cha 7 (1- 4) kinachoeleza kuwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa atatangaza kusudio la kuanzisha Halmashauri katika Gazeti la Serikali na magazeti ya kawaida na atatoa siku sitini (60) kwa wadau kuwasilisha kwa maandishi maoni, ushauri, au pingamizi kuhusiana na uanzishwaji wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza tarehe 18 Juni, 2012 wakati najibu swali Na. 25 lililoulizwa na Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, kwamba Halmashauri za Msalala na Ushetu ni miongoni mwa Halmashauri mpya ambazo zipo katika hatua ya uhakiki wa maeneo ya kijiografia (*geographical boundaries*) kwa maana ya mgawanyo wa Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji/Mitaa ili kuweza kutangaza. Hivyo Halmashauri za Msalala na Ushetu zitaanza rasmi sambamba na Halmashauri nyingine mpya zinazotarajiwa kuanzishwa baada ya kukamilika kwa taratibu za uanzishaji wake kwa mujibu wa Sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Serikali ilitangaza kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama katika Halmashauri zingine tatu za Msalala, Ushetu na Halmashauri ya Mji wa Kahama. Halmashauri ya Ushetu itajumuisha eneo lote la Jimbo la Uchaguzi la Kahama ukiondoa eneo la Halmashauri ya Mji wa Kahama. Halmashauri ya Msalala inayopendekezwa itajumuisha eneo lote la jimbo la Uchaguzi la Msalala.

Kwa maelezo hayo ni dhahiri kuwa baada ya kuanza kwa Halmashauri hizo tatu, hapatakuwapo

tena na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, kutakuwepo na Wilaya ya Kahama tu.

(c) Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, lengo la Serikali kuzigawa au kuanzishwa Halmashauri mpya ni kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi. Hata hivyo, jukumu la kujua wapi yawepo Makao Makuu ya Halmashauri ni la Uongozi wa Halmashauri husika ukishirikiana na wananchi wake.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anasema Halmashauri za Ushetu na Msalala zitaanza mara baada ya kukamilika taratibu. Sasa naomba kujua hizo taratibu zitakamilika lini maana inawezekana zikawa mwaka mmoja, mwaka mzima hizo taratibu zitakamilika lini ili wana Usheti na Msalala waweze kupata huduma kama alivyosema Waziri tunataka tuwasogezee huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kwa sababu tuna Halmashauri pia nyingi sana katika nchi za miji midogo ambazo zimeanza nyingine miaka minne mitano ikiwepo Halmashauri ya Mji Mdogo wa Vwawa kule Mbozi. Je, hiyo Halmashauri yenyewe itaanza lini sambamba na Halmashauri zingine ambazo ziko katika hatua ya Miji Midogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hizi Halmashauri ninazozingumza hapa pamoja na zile nyingine ambazo zinazungumzwa haziwezi kuanza bila ya kupitia kwenye huu mchakato ninaouzungumza hapa.

Juzi nilijibu hapa na naomba nirudie na kusema hapa sasa hivi tunayo timu ambayo imeundwa pale TAMISEMI ambayo inazunguka katika maeneo yote mapya ambayo yanakusudiwa kuanzishwa. Nia na shabaha ya mpango ule ni kufananisha yale yaliyoandikwa katika makaratasi ambayo yamekuja kama mapendekezo na hali halisi iliyoko pale kwenye *ground.*

Mheshimiwa Spika, kuanzisha Halmashauri hapo unaanzisha kwa ajili ya watu na watu ni lazima waseme sisi tuko tayari Halmashauri hii ianze na lazima useme vijiji vitakavyoingia mle ni hivi. Useme mitaa itakayoingia mle ni hii, Tarafa zinazoingia mle ni hizi na Kata zinazoingia mle ni hizi na wote waafiki waseme kwamba naam barabara!!! Atatangaza Waziri mwenye dhamana ataweka kwenye ukuta, atawapa siku 60 waseme kama wanataka kuanzisha Halmashauri hizo au hawataki.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana inaniwia vigumu, lakini nataka niseme hapa kama mlivyosikia katika hotuba zote Waziri wa Nchi atakaposimama hapa na Waziri Mkuu ataeleza hili la mchakato unaendelea hapa. Habari ya Kahama au Ushetu pamoja na Msalala wala hakuna *debate* tena. Kwa sababu ni

jambo ambalo linajulikana kwamba tunaanza, lakini kwa kuzingatia hili ninalosema.

Mheshimiwa Spika, sasa anazungumzia habari ya Vwawa. Vwawa nimefika pale naifahamu. Nilieleza juzi nilipokuwa nazungumza habari ya Itigi na wale wengine. Tunachowaomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmeomba muwe na Mamlaka za Mji Mdogo wote kabisa na kina Lwanji ahakikisheni kwamba mnatuletea.

Juzi nimekwenda kutafuta Mheshimiwa Godfrey Zambi tukakuta kwamba kweli wanakiri Mkoa wa Mbeya pamoja na wale wengine wote kwamba zile *documents* hazikufika zimefika ofisini kwetu.

Kwa hiyo, nawaomba sana wote hata wewe Mheshimiwa Spika kama una mji wako mdogo unataka kuanzisha wewe tuletee hizo takwimu hapa.

**SPIKA:** Mimi nina mji mkubwa lakini hamjui kama kuna vijiji 44. Ndiyo hilo tu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa naomba niulize swali moja dogo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa baadhi ya Halmashauri hapa nchini ambazo zimetangazwa na Serikali kwamba ziweze kuanza nyingi baadhi zimeshakamilisha vigezo vyake kama Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Kwa kuwa katika majibu yako ya msingi umeeleza kwamba itabidi

kuweza kusubiri Halmashauri zote ambazo zimeanzishwa ziweze kukidhi vigezo.

Je, hatuoni kwamba ni kuwachelewesha maeneo mengine ili suala zima la kusogeza huduma kwa wananchi kutokana na kutokuanzishwa Halmashauri ambazo tayari zimeshakidhi vigezo, Serikali inatoa kauli gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hii Halmashauri ya Kasulu, Masasi, Nzega, Handeni wala tusizungumzie, yaani nawaambia kabisa tusizungumze kwa sababu hizo najua kabisa kwamba zinakuja, hizi zilishakuwa zimetamkwa kutoka kule nyuma. Ninachosema hapa kama kuna watu ambao tunawasema hivyo tunavyosema halafu watachelewa hawakuleta treni imepita, itakuwa imekwenda.

Mheshimiwa Spika, nina hakika hataweza kusema kwamba mimi naanzisha hapa kama hatujajiridhisha hapa kwamba hivi tunavyosemwa na wananchi wameridhika na jambo hilo linalosemwa. Hii itatuondolea migogoro ambayo tunayo katika Tanzania ya mahali unaanzisha maeneo ya utawala kesho unakuta watu wanalalamika kusema kwamba sivyo.

Nataka nikuthibitishie kwamba sisi hapa tumeshaeleza na kwamba tunawasiliana kwa karibu sana na Halmashauri zote hii ni pamoja na zile Halmashauri 19 ambazo zitaanzishwa baadaye.

Kwa sasa hivi Mheshimiwa Rais alichofanya ameanzisha Wilaya na ameteua Wakuu wa Wilaya na Mikoa mipya ili wasaidie kusimamia mchakato huu tunaozungumza hapa. Kwa hiyo unaweza ukaiona kabisa dhahiri nia ya Serikali ya kutaka kufanya kazi hii lakini kwa kufuata taratibu hizi ambazo nimesema hapa za kisheria.

**SPIKA:** Ahsante hili suala limejibiwa sana sana.

Na. 100

**Barabara Toka Ihumwa – Chuo Kikuu Hombolo**

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE** aliuliza**:-**

Mji wa Dodoma unakua kwa kasi sana na uwepo wa Vyuo Vikuu hivyo inalazimu miundombinu ya barabara iwekwe vizuri ili kufikia Vyuo hivyo kwa urahisi:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuweka lami kwenye kipande cha barabara inayotoka Ihumwa hadi Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ihumwa – Hombolo ni sehemu ya barabara ya Ihumwa-Hombolo-Gawaye-Mayamaya yenye jumla ya urefu wa kilometa 55.75.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo, Serikali ilipandisha hadhi mwaka 2009 kuwa barabara ya Mkoa. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Dodoma, iliifanyia matengenezo ya kawaida, muda maalum pamoja na matengenezo ya madaraja barabara hiyo yenye gharama ya jumla ya shilingi 58,632,150.00.

Pia katika mwaka wa fedha 2011/2012, barabara hiyo imefanyiwa matengenezo ya kawaida, muda maalum pamoja na matengenezo ya madaraja yenye gharama ya jumla 122,632,440.00. Hali kadhalika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shillingi 269,190,000.00, zimeombwa ili kuifanyia matengenezo ya aina hiyo kwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali kwa sasa haijapanga kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo kutoka Ihumwa hadi Chuo Kikuu cha Serikali za Mitaa Hombolo. Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo kwa kiwango cha changarawe ili iendelee kupitika vizuri kipindi chote cha mwaka.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Nashukuru kwa kazi nzuri ambayo Serikali inaendelea kuifanya ya kukarabati barabara hiyo ili iendelee kupitika wakati wowote. Je, ni lini sasa Serikali itajipanga kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa kuzingatia kwamba Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo ndio Chuo Kikuu pekee kilichopo katika nchi yetu ya hapa Tanzania.

Pili, nimeenda mwendo wa kasi sana kukagua barabara tunazokwenda Dodoma/Iringa na Dodoma/Babati na kwa kweli kazi inaendelea vizuri na bila shaka lami itaingia hapa mjini kwa muda ambao sio mrefu kuanzia sasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuona kwamba wakati barabara ya Iringa/Dodoma itakapoingia hapa basi muweze pia kufikisha lami kwenye Chuo Kikuu cha Saint John's ambacho kiko karibu sana na barabara hiyo? Kwa upande pia wa Kaskazini kwa barabara inayotoka Babati kuingia hapa Dodoma Je, Serikali pia ina mpango gani kuweza kuona kwamba mnafikisha lami kwenye Chuo cha Mipango, Chuo cha Ufundi John Bosco na Chuo cha Madini ambavyo vyote viko karibu sana na barabara hiyo?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwa kuishukuru Serikali kwa waliyofanya. Ninachotaka tu kujibu hapa kwa Mheshimiwa Mbunge kupanga ni kuamua. Kwa sasa hivi katika mkoa wa Dodoma *Trunk road* zote zinajengwa kwa kiwango cha

lami. Ukitoka Dodoma hadi Iringa kuna wakandarasi wanatengeneza kwa kiwango cha lami na Dodoma kwenda Singida nayo inajengwa kwa kiwango cha lami na katika Bajeti ya mwaka huu kuna zaidi ya shilingi bilioni 62 na kitu zimepangwa.

Sasa wakati tukiendelea kujenga barabara za lami za Dodoma ni lazima Mheshimia Malolle ajue kwamba kuna maeneo mengi ya Tanzania ambayo hayajajengwa kwa kiwango cha lami ikiwepo Mpanda hadi Uvinza, kutoka barabara ya kutoka Masasi hadi Ruvuma hadi Mbambabay na maeneo mengine, ikiwepo pia kutoka Njombe kwenda Makete. Kwa kuzingatia hiyo na kwamba hiyo *resources* tuliyonayo tutaendelea kujenga barabara zingine za *trunk road* hizi za kwenda kwenye Vyuo Vikuu vya Dodoma visubiri mpaka tutakapomaliza kujenga barabara zingine katika nchi hii.

**SPIKA:** Hiyo ya Njombe mpaka Makete ni ahadi ya Ilani iliyopita. (*Makofi/Kicheko)*

**MHE YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kama ilivyo kwa Mkoa wa Dodoma kwamba unakua kwa kasi na kadhalika Mji wa Korogwe nao unakua kwa kasi. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na ahadi ya Mheshimiwa Rais ya barabara za mji wa Korogwe zafikia kilomita mbili na nusu?

**SPIKA:** Sasa Korogwe na kule kwingine ni wapi? Dodoma.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahadi ambazo ziko kwenye Ilani ya Uchaguzi ni nyingi na ahadi ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais ni nyingi. Tutaendelea kuzitekeleza kulingana na upatikanaji wa fedha na kwa bahati nzuri katika fedha za Mfuko wa Barabara zimeweza kuongezeka kutoka shilingi bilioni 300 hadi 400. Kwa hiyo, hizi kilomita ndogo ndogo ambazo ziliahidiwa na Mheshimiwa Rais katika Wilaya na kadhalika zitazingatia kwa kutumia fedha za Halmashauri za Wilaya.

Kwa hiyo, nimshauri tu Mbunge wa Korogwe, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe iombe fedha kupitia Mfuko wa *Road Fund* ili waweze kuanza kutengeneza barabara ya Korogwe na maeneo mengine ikiwa ni pamoja na barabara hizi za Dodoma zinazoenda kwenye Vyuo Vikuu kwa kutumia fedha za *Road Fund* zinazopangwa kupitia Mfuko wa Barabara.

**MHE. JAMES F. MBATIA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa taaluma ya ujenzi kwa miundombinu (*Construction Management*) kwenye *classfication theory* inasema *maintenance* ni jambo la msingi, yaani barabara ambazo zimeshakuwa *Class A* ziendelee kuwa *maintained* kubaki *Class A* wakati una *upgrade* zile nyingine za *Class B* inaweza kuwa A na C kuwa B.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kuna barabara nyingine ambazo zinatakiwa kuanza wakati suala la msingi linahusu vilevile ku-*maintain* barabara

za mji wa Dodoma ziendelee kuwa *maintained* kwenye *Class A* wakati hizo nyingine kutoka *Class B*.

Je, Serikali haioni ni vyema badala ya kutoa ahadi za kisiasa zaidi ikatoa ahadi ikatekeleza matakwa ya kitaalam ya ujenzi wa barabara?

**SPIKA**: Kwa kweli nilimwita aulize swali la nyongeza kwa sababu nilimsikia kwenye kipindi alisema vizuri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahadi zinazotekelezwa si za kisiasa, lakini ni ukweli pia kwamba barabara ambazo zinatakiwa kufanyiwa *maintenance* zinakuwa *maintained* na ndiyo maana katika mwaka wa 1998 kupitia *amendment act Na. 2* ilitungwa Sheria ya Kuanzishwa Mfuko wa Barabara *(Road Fund.*

Katika miaka hiyo makusanyo ya fedha za *Road Fund* ambazo zilikuwa zinakusanywa zilikuwa ni shilingi bilioni 13, lakini katika Bajeti ya mwaka huu makusanyo ya fedha za *Road Fund* ni shilingi bilioni 400 na katika sheria ile pamoja na mabadiliko yake kifungu na. 220 kinasema: "*All the money should be used for the main road maintenance only".*

Kwa hiyo, *status* kwa yale anayoyazungumza kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kusimamia suala la *maintenance* ya barabara zake

itaendelea kulisimamia kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 inavyosisitiza.

**SPIKA:** Tumechukua muda mwingi sana kwa swali moja, tumechukua zaidi ya dakika 15 sivyo ilivyo. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Moza Abeid atauliza swali. *(Makofi)*

Na. 101

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu - Kondoa**

**MHE. MOZA A. SAIDY** aliuliza:-

Pamoja na Wilaya ya Kondoa (Mjini) kupata umeme tangu 1982 bado haina mawasiliano ya simu yanayoridhisha:-

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwaboreshea miundombinu ya mawasiliano ya simu wananchi hao ili wapate mawasiliano ya simu yanayoridhisha?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma ya mawasiliano ya simu katika maeneo yote nchini. Kwanza kwa ajili ya kupeana taarifa na

pia katika kufanikisha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, Serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha kuwa maeneo yote nchini yanafikiwa na huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itawasiliana na Kampuni za Simu ili kuyashawishi yaboreshe kiwango cha upatikanaji wa mawasiliano katika Wilaya ya Kondoa Mjini kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Serikali sasa inapitia upya utaratibu mzima wa kupeleka mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali nchini kwa nia ya kuharakisha zoezi hili.

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY**: Mheshimiwa Spika. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini napenda kuuliza swali. Ndani ya vijiji ambavyo umevitaja. Je, na Kondoa imo?

Swali la pili. Je, ni lini Serikali itafanya ushawishi kwa kampuni hiyo ili iweze kuja kuboresha mawasiliano katika Wilaya ya Kondoa, Chemba na kwingineko kwenye shida ya mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba Serikali imefanya utafiti na kubaini kwamba vijiji 2,175 aidha havina mawasiliano au havina mawasiliano ya kuridhisha na naamini kwamba katika tathimini hiyo vijiji vilivyomo katika Wilaya ya Kondoa vimo na ni lini Serikali itawasiliana na makampuni ya simu ili kuboresha huduma katika Wilaya ya Kondoa. Jibu ni kwamba tutafanya hivi

karibuni na tukimaliza kikao hiki l eo nitakutana na Mheshimiwa Mbunge tutawasiliana na makampuni tukiwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutoa taarifa kwamba leo baadaye tutagawa karatasi kwa orodha. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba mwaka jana waliorodhesha vijiji katika maeneo yao ambayo havina mawasiliano au havina mawasiliano ya kuridhisha.

Lakini imebainika kwamba aidha baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawakuorodhesha au hawakuorodhesha vijiji vyote.

Kwa hiyo leo tutagawa orodha tena upya ya vijiji vyote ambavyo mliviorodhesha na pale itakapobainika kwamba aidha baadhi ya vijiji vilisahaulika basi tutaomba mviongeze kwenye orodha ile ili tuhakikishe kwamba kila Mbunge na kila eneo lake limezingatiwa ili tusiwe na maswali tena la kwamba je, eneo langu limo au halimo na tutapenda orodha hiyo mturudishie ndani ya wiki moja kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Lukuvi.

**SPIKA:** Hiyo inatosha, mkaorodhe wote mliosimama kuuliza maswali kusudi muweze kusaidiwa. Mheshimiwa Kapt. John Chiligati swali linalofuata badala yake atauliza Mheshimiwa John Lwanji.

Na. 102

**Huduma za Simu za Mkononi Kata ya Sanza na Iseke**

**MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI)** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vingi Wilayani Manyoni havijapata huduma ya Simu za mkononi:-

Je, ni lini Makampuni ya simu yatapeleka huduma ya simu katika vijiji vya Makanda na Ngaiti, Tarafa ya Kintinku, Majiri na Hika Tarafa ya Kilimatinde, Sanza na Iseke Tarafa ya Nkonko?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayani na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kalpt. John Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote *(UCAF)* imehakiki mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini na kubainisha vijiji 2,175 havina mawasiliano au havina mawasiliano ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo umejumuisha Wilaya ya Manyoni katika maeneo ya Kitalalo, Magasai, Magasai A na Makanda A, katika kijiji cha Makanda ambapo inaonyesha kuwa tayari Kampuni za *Airtel* na *Vodacom* ziko katika hatua ya kuboresha huduma katika maeneo hayo. Aidha imebainika kuwa kampuni za *Airtel* na *Vodacom* zina minara katibu maeneo ya Chichecho, Ikasi, Ntope vilivyo katika kijiji cha Sanza na

maeneo ya Igwamadete, Isseke, Mpapa na Simbanguru katika kijiji cha Isseke. Hivyo mfuko utaendelea kushirikiana na makampuni husika ili kuhakikisha kwamba huduma hii inaboreshwa katika maeneo hayo. Utafiti zaidi utafanyika katika vijiji vya Ngaiti, Majiri na Hika ili kuona uwezekano wa kufikisha huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango kazi wake, mnamo mwezi Novemba 2011, Mfuko ulitangza zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza iliyojumuisha vijiji 140 nchi nzima ambapo uchambuzi wa zabuni na matokeo ya zabuni hiyo ulikamilika mwezi Machi, 2012. Aidha kwa zabuni aliyewasilisha maombi hakushinda zabuni hiyo kutokana na gharama kubwa tofauti na fedha halisi zilizotengwa na mfuko wa kazi hiyo. Kufuatia hilo, utafiti zaidi unaendelea kufanywa na Mtaalam Mwelekezi ili kufanya tathmini ya kitaalam ya mahitaji ya fedha na mbinu bora zenye gharama nafuu za kufikisha mawasiliano katika maeneo yote. Tathimini hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2012 na zabuni mpya zinatarajiwa kutangazwa mwezi wa Septemba 2012 kwa kuzingatia mapendekezo ya mtaalam na kwa ajili ya hatua zaidi za utekelezaji.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza katika Wilaya hii ya Manyoni na hasa hizo tarafa zilizotajwa za Kintinku na Nkonko tuliwasilisha kwa pomoja kwa upande mwingine wa Wilaya upande wa Magharibi

tuliwasilisha maombi kwa Kata ya Mamaghembe Ipandye na Idondyandole.

Sasa napenda kujua hali ya hizi Kata katika huo mchakato unaozungumza ikoje maana utafiti ulifanywa na imeonekana kabisa hawa watu kiuchumi wanaweza kupatiwa huduma hiyo?

Swali la pili, ni kweli kwamba mwaka jana au mwaka juzi tulijaza fomu. Wakuu hawa wa Makampuni walikuwa kwenye Ukumbi wa Msekwa tukajaza fomu hizo lakini hali halisi inavyoonekana kwa kweli utoaji wa huduma hii ya minara unasuasua sana. Sasa napenda nieleweshwe ni nini hasa mahusiano haya? Ni ushawishi tu mahusiano kati ya Serikali na haya makampuni, uhusiano wake hasa ni upi katika kushawishi haya makampuni? Maana inaonekana kwa upande mwingine Serikali kama vile haina *control* kabisa katika eneo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitakapoleta ile orodha tutatazama kama maeneo ya Jimbo lako yamo na kama hayamo basi utaongeza na tutayafanyia kazi.

Kuhusu hili la pili, msingi wa biashara ya mawasiliano ni biashara ya faida na makampuni haya hayalazimishwi kupeleka mawasiliano katika maeneo ambayo wanaona hayana mvuto wa kibiashara. Ndiyo maana Serikali ilianzisha mfuko wa *UCAF,* Mfuko wa Mawasiliano kwa wote msingi wake ni kutoa ruzuku kwa makampuni ya simu kupeleka mawasiliano katika

maeneo ambayo hayana mvuto wa kibiashara. *(Makofi)*

Sasa mwanzo tulikuwa hatuna hakika kwamba moja, gharama halisi za kupeleka mawasiliano kwenye eneo mahususi ni kiasi gani. Kwa hiyo, ruzuku inayohitajika ni kiasi gani. Hizo taarifa hazikuwepo. Tulichofanya sasa hivi ni kufanya tathimini ya kila kijiji na kujua gharama halisi za kupeleka mawasiliano kwenye kila kijiji na kutangaza *tender* kwa kila kijiji mahususi na ambacho tunajaribu kufanya ni kwamba katika yale maeneo ambayo makampuni ya simu yana minara inayozunguka katika maeneo haya inawezekana kampuni ya Vodacom tayari imewekeza katika maeneo ambayo ni jirani na Manyoni magharibi na kampuni ya *Airtel* imewekeza katika maeneo jirani na Wilaya ya Liwale kwa hiyo tunajaribu kutoa ruzuku kulingana na uwepo wa Makampuni katika maeneo mahususi.

Mheshimiwa Spika, tunaamini njia hii na utafiti tulioufanya upya na *model* hii mpya ambayo tumeitengeneza itasaidia kuharakisha zoezi hili na tayari tumepata fedha shilingi bilioni 45 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kugharamia awamu ya kwanza ya kazi hii.

Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba baada ya kutengeneza utaratibu huu mpya zoezi hili litaenda haraka. Pale mwanzo tulikuwa tunachelewa kwa sababu tulikuwa hatuna

hakika na kiwango cha ruzuku na utaratibu tuliouweka. Kwa hiyo, sasa hii sio ahadi tu. Hii sasa ni utekelezaji.

Na. 103

## Kuchomwa Moto kwa Ofisi ya OCD Tandahimba

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Tarehe 17 Aprili, 2012 Ofisi ya *OCD* Tandahimba ilichomwa moto na watu wasiojulikana na kuleta hasara kubwa sana kwa wananchi na wafanyabiashara wenye maduka yanayozunguka eneo hilo.

(a) Je, kwanini Serikali haiundi Tume huru ili ipate ukweli wa chanzo cha moto huo?

(b) Kwa kuwa hasara iliyopatikana inawaacha wananchi katika hali mbaya. Je, Serikali inawasaidiaje waathirika wa tatizo hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tarehe 17 Aprili, 2012 Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Tandahimba

na maduka 65 ya wafanyabiashara wa eneo hilo vilichomwa moto na kusababisha hasara kubwa. Kufuatia tukio hilo jumla ya watu 9 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani na kesi zao zinaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hilo lipo Mahakamani ni kinyume na utawala wa Sheria Serikali kuunda tume huru kabla ya Mahakama kutoa uamuzi wake. Aidha kuhusu suala la fidia kwa waathirika hili litategemea uamuzi wa Mahakama kwenye suala hilo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, asante. Pamoja na kuwepo jambo hili Mahakamani lakini yapo mambo, administrative actions zinazotakuwa zifanywe ili kuleta amani ya kudumu pale Tandahimba ikitiliwa maanani kwamba wananchi wameathirika sana lakini hata Polisi walioko pale wanaishi kwenye ma-tent tena vijana wadogo tu wametoka depo wamekuja pale wanaishi katika maisha mabaya kiasi cha kuleta athari kwa pande zote. Kwanini Serikali haitaki kwenda kukutana na wananchi wale pamoja na Polisi wakawasilikiza vizuri ili tukapata ufumbuzi wa kudumu na kuleta amani pale Wilayani Tandahimba.

Pili, kwa kuwa mimi niliona dalili fulani za hali mbaya na kwa sababu hiyo kwanza nilikutana na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Nahodha nikamshauri mambo mengi ya msingi ya kufanya lakini pia nilimwona *IGP* naye nikamshauri mambo mengi ya kufanya na kwa sababu nilikuwa najua *OCD* aliyekuwepo pale alikuwa na mtandao

wa utendaji wa hovyo wakiwemo baadhi ya Polisi na wale Polisi bado wapo. Hata juzi hapa namshukuru Mheshimiwa *DC* wangu Mheshimiwa Pansiano Nyami ameweza kutuliza amani kwa sasa.

**SPIKA**: Uliza swali, sio kutoa hotuba tena.

**MHE. JUMA A. NJWAYO**: Mheshimiwa Spika, umenitoa kwenye *track.* Sasa kwanini basi Serikali isafanye utafiti wa kina nje ya Mahakama ile niliyosema *administrative action* ili isiwe tu suala la kuwaondoa wale Polisi ambao kwa namna au nyingine wamechangia matatizo wapewe adhabu zinazostahili ili tuweze kujenga utawala bora wa kisheria kama ambavyo tungetarajia iwe? ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 104

**Askari wa Usalama Barabarani Kutoa Faini Bila Kutoa Risiti**

**MHE. VICENT J. NYERERE** alijibu:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa askari wa Usalama Barabarani wanaotoza faini bila kutoa risiti (Stakabadhi) ya malipo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kinachotozwa na askari wa Usalama Barabarani sio faini bali ni tozo la papo kwa papo (Notification) na dereva kwenda kulipa faini. Hii inafanyika kwa mujibu wa kifungu 95 cha Sheria ya Usalama Barabarani Na. 68 ya 1973 na Kanuni Na. 257 ya mwaka 2011. Kazi ya askari ni kumwandikia notification (PF.101) ikianinisha kosa/makosa aliyoyatenda na kiasi cha fedha anachotakiwa kulipa.

Mheshimiwa Spika, dereva anapoandikiwa Notification hutakiwa kwenda kulipia kwenye ofisi za Wakuu wa Polisi wa Wilaya ambako kuna wahasibu wenye jukumu la kupokea fedha na kutoa stakabadhi.

**MHE. VICENT J. NYERERE**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nasikitika kwa jibu ambalo halifanani na swali. Nilikuwa napenda kujua Waziri anataka kutuambia hakuna askari anayekusanya fedha barabarani na kama wapo na tukaleta vilelelezo yupo tayari kuwajibika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu ambao upo kuna Askari katika maeneo yaliyoko mbali sana na vituo vya Polisi wa Wilaya wanakusanya fedha na utaratibu unaotumika ni kwamba baada ya kukusanaya anamwandikia dereva kituo gani au eneo gani aende akachukue risiti yake baada ya safari. Kwa sababu wakati mwingine siyo rahisi kumtoa mtumishi wa kwenye safari yake halafu ukamwambia arudi kituo cha polisi cha Wilaya akalipe tozo.

Hili jambo ninakubaliana naye kuwa lina tatizo na tumejipanga kuhakikisha kwamba sasa tunataka kulirekebisha kwa kutumia mabenki na tehama ili tuhakikishe kuwa askari hawatazigusa fedha na kwa sababu hiyo sidhani kama nina wajibu wa kuwajibika kwa hili.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba nimwulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, askari wa barabarani hutoza *fine* barabarani waliko ambayo risiti huonyesha gharama ya shilingi ishirini elfu tofauti na anayetozwa *fine* hiyo kwa kulipa shilingi thelathini elfu na risiti ishirini elfu na risiti inaonyesha shilingi ishirini elfu na hapo hupelekea mtafaruku baina ya mtozwa *fine* na mtoza *fine.*

Je, Serikali iko tayari kuandaa risiti halali ya shilingi elfu thelathini ili kuondoa mtafaruku huu baina ya mtoza *fine* na mtozwa *fine?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge aliuliza kama Serikali iko tayari kurekebisha risiti na jibu ndiyo kuwa tuko tayari na tutabadilisha**.** *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini Mheshimiwa Gaudence Kayombo, atauliza swali hilo.

Na. 105

## Kiasi cha Makaa ya Mawe Katika Kijiji cha Mtunduwalo

**MHE.GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Je, ni kiasi gani cha makaa ya mawe kipo katika maeneo ya Ngaka, Mbuyura, Mbalawala na Mkapa katika kijiji cha Mtunduwaro, Wilayani Mbinga?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassin Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kubaini kiasi cha makaa ya mawe katika maeneo ya Ngaka, Mbuyura, Mbalawala na Mkapa ilianza 1949 na Serikali ya Uingereza wakati huo kupitia *Colonial Development Corporation (CDC)* ilifanya kazi ya uchorongaji wa miamba. Baada ya Uhuru, Serikali ya Tanzania iliendeleza kazi ya utafiti na kwa sasa kuna makampuni yanayoendeleza utafiti kwa ajili ya kuchimba makaa ya mawe katika maeneo tajwa.

Mheshimiwa Spika, tafiti za kijiolojia zimebaini bonde lenye makaa ya mawe *(coalfield)* la Ngaka ambalo linajumuisha maeneo ya Mbuyura, Mbalawala na Mkapa na Kijiji cha Mtunduwaro kimo katika eneo

la Mbalawala Wilayani Mbinga na Kampuni inayofanya kazi ya utafutaji *(exploration)* katika eneo hili ni *Tancoal Energy LTD.* ambayo ni kampuni ya Ubia kati ya *NDC* na kampuni ya *Intra Energy* kutoka Australia .

Mheshimiwa Spika, bonde la Ngaka lina takribani tani milioni 286.99 za makaa ya mawe, kati ya hizi:

- Mbuyura, tani milioni 11.1;
- Mbalawala, tani milioni 251;
- Mkapa, tani milioni 19.81; na
- Nyakangunda tani 5.08.

Mheshimiwa Spika, mradi huu umekadiriwa kuzalisha MW 250 pindi uzalishaji wa umeme utakapoanza mwanzoni mwa mwaka 2015.

**MHE.GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninapenda kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri ya mradi huu hasa wenzetu wa *NDC* na Wizara ya Viwanda kwa ujumla. Lakini pia napenda kumshukuru Dkt. Milton Makongoro Mahanga, ambaye alikuwa Naibu Waziri wa kwanza kabisa kufika katika eneo hilo wakati lilipokuwa likiungua moto sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa sababu Serikali inasema kutakuwa na umeme utakaozalishwa wa MW 250 na kwasababu katika Mkoa wa Ruvuma na Wilaya ya Mbinga hakuna

kijiji chenye umeme ukiondoa Makao Makuu ya Wilaya ya Mbinga, Songea na Tunduru.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa umeme huu unaanza kwanza kwa kuwekwa katika vijiji vinavyozunguka eneo la mradi kwenda katika Tarafa na Katika Wilaya na baadaye katika Mkoa?

(b) Katika eneo hili kuna baadhi ya wananchi ambao wamehamishwa na wamepewa fidia lakini fidia hiyo ni ndogo na kwa kweli ukifika ukionyeshwa nyumba ambayo unaweza kudhani ni milioni ishirini kumbe mtu amelipwa milioni tano.

Kwa vile Mheshimiwa Makamu wa Rais alitembelea pale na Mkuu wa Mkoa na mimi pia tulifika pale na Mkuu wa Mkoa aliahidi kushughulikia jambo hili.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kama dharura kuonana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na Wabunge na  Mkuu wa Mkoa yuko hapa kwenya *gallery* sasa hivi anasikia baada ya kipindi cha maswali na majibu tukutane ili tuweze kuweka mkakati kuhakikisha kuwa wananchi hawa wanapata haki iliyo sawa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hamuwezi kuonana labda saa saba kwa sasa ni kipindi cha maswali na majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Napenda kujibu maswali ya nyongeza ya

Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia fidia hii ya wananchi wa Mbinga. Nikianza na swali lake la kwanza Serikali katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukiangalia kitabu cha Ilani ya CCM ukurasa wa 68 D ina itaja wazi Wilaya ya Mbinga kwamba ni sehemu ambayo itapelekewa umeme na hivi sasa Wizara ya Nishati na Madini kupitia *TANESCO* tunao mradi mkubwa wa kupeleka umeme Mbinga kutokea Makambako kupitia Madaba – Songea na Wilayani Mbinga mpaka *Mbamba Bay.*

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mbali ya uzalishaji wa MW 250 utakaotokana na makaa ya mawe ya Ngaka lakini pia Serikali ina mradi unaoendelea hivi sasa wa kupeleka umeme katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Mbinga ikiwamo *Mbamba Bay.*

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba mimi niko tayari kukutana na Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma hususani Mbinga na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ili kujadili na kuona kitu gani kilitokea mpaka wananchi wakapunjwa kulipwa fidia.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa *time* ya maswali ni *limited.* Mheshimiwa Mangungu, ni *limited* kabisa kwa hiyo hatuwezi kufanya mambo ya habari hayo na nini.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Unakumbuka kuwa uliunda Kamati kwa ajili ya kufuatilia umeme wa uhakika unaotokana na makaa ya mawe Serikali kupitia Bunge hili imekuwa ikitoa ahadi kila siku kwamba mradi utaanza na utatekelezwa wakati hatujaona jitihada zozote za kujenga *transmission line* kutoka Mbinga kwenda Makambako kuptia Njombe hadi Mufindi kwa nini ahadi hii isiendane sambamba na utekelezaji kulikoni kutoa ahadi tu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ahadi hii ya utekelezaji wa mradi wa kujenga *transmission line* kutoka Makambako kwenda Songea na Mbinga iko kwenye utekelezaji. Serikali kupitia Shirika la *TANESCO* tayari imeshapata fedha kupitia *SIDA* Shirika la msaada la Sweden ambako zaidi ya *krona* milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu na tayari mshauri anaendelea na kazi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge siyo kwamba ni ahadi tayari kazi hii inaendelea na fedha zimepatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika swali la nyongeza. Si ulisimama? au *oky* Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, imebainika kwamba pale ambapo mashirika yetu kama *NDC* na *STAMICO* yenyewe yamefanya *exploration* yanapata nguvu za kuweza kuingia ubia na makampuni kutoka nje. Kwa mfano hivi karibuni *STAMICO* waliweza kuingia ubia na kampuni na kuweza kupata 40% wakalipwa *cash money* kama dola milioni tatu *NDC* kwasababu haikufanya *exploration* imeingia ubia kwa 30%.

Je, Serikali ina utaratibu gani na mpango wa kuyaweza mashirika haya mawili *NDC* na *STAMICO* kuwapa fedha za kutosha ili wenyewe wakafanye *exploration* wakajua ni kiasi gani cha migodi iliyopo ili hatimaye wakaweza kuingia ubia na makampuni kutokana na *information* walizo nazo wao badala ya wao kuwakaribisha watu kuingia ubia ambao wao wanaenda kwenye *stock exchange* wanauza hizo taarifa wana – *raise money* wakati mashirika yetu yanaweza kufanya hiyo kazi na ku- *raise money* zaidi Serikali ina mpango gani wa kufanya hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid, Mbuge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini imelitambua hilo na hivi sasa tumejipanga kabisa kuhakikisha kwamba tuna iwezesha *STAMICO* pamoja na *NDC* ambayo iko chini ya Viwanda na Biashara. Tuna mashirikiano ya karibu kuangalia haya mashirika yetu ambayo yako *strategic* kusimamia

biashara ya Madini kwa niaba ya Serikali tunayawezesha ili tuweze kupata *shares* kubwa na kusimamia uchumi hasa katika gunduzi mbalimbali zinazoendelea. Kwa hiyo, siyo tu *NDC* na *STAMICO* lakini pia hata TPDC tumejipanga kuhakikisha tunaziwezesha ili ziweze kufanya kazi zaidi na kwa tija.

Na. 106

**Uhitaji wa Umeme- Mbamba Bay**

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa nimekuwa nikiiomba Serikali kupeleka umeme kwenye mji wa *Mbamba Bay,* baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kutoa jenereta la kuzalisha umeme kwenye mji huo.

(a) Je, jambo hili litatekelezwa lini?

(b) Kwa sababu mji wa Mbamba Bay sasa umekuwa Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Nyasa. Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka kupeleka umeme kwenye mji huo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John Damiano Komba, Mbunge wa

Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme kwenye Mji wa Mbamba Bay, unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 33 yenye urefu wa kilomita 167 kutokea Songea kupitia Mbinga kwenda *Mbamba Bay.* Mradi huu unafadhiliwa na shirika la Maendeleo la Sweden (Sida) na inakadiriwa kugharimu *Swedish Crona (SEK)* milioni 500.

Hatua iliyofikiwa mpaka sasa ni kuwa mshauri mwelekezi wa mradi, ambayo ni kampuni ya *SWECO International* ya Sweden, yuko na *site* na anaendelea na kazi tangu Agosti, 2011; maandalizi ya ukamilishaji wa maeneo ya ujenzi wa vituo vya kupozea umeme vya Madaba na Songea pamoja na kulipa gharama za uthamini kwenye Halmashauri husika yamekamilika.

Tumekubaliana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kutoa jenereta, miundombinu ya kusambaza umeme huo, hivyo pindi ujenzi wa njia za kusambaza umeme katika maeneo hayo utakapokamilika, jenereta yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa *Kv 250* itatumika kupeleka umeme kwenye Mji wa *Mbamba Bay.*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inalitambua hilo na ninapenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatekeleza mradi huu kwa kasi kubwa kwa kuwa na malengo ya kuunganisha Wilaya zote za zamani na mpya kwenye gridi ya Taifa na hii ni katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Mkandarasi

Mshauri kwa ajili ya mradi wa Makambako – Songea, ambao utafikisha umeme *Mbamba Bay,* ameshapatikana na anaendelea na usanifu wa mradi huu wa kufikisha umeme Songea, Mbinga, *Mbamba Bay* na maeneo mengine. *(Makofi)*

**MHE. KPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Jambo hili la kupeleka umeme kutoka Makambako kuelekea Songea na Mbinga sasa hivi ni miaka karibu nane na ilikuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya miaka mitano iliyopita. Sasa kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imetoa jenereta na liko tayari na imetoa kuanzia mwaka 2008, kuna ugumu gani wa *REA* kwenda pale na kufanya *network* ya umeme ili mji ule upate umeme?

(b) Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu tu hivi inaingia akilini au ama haiingii akilini kwamba makaa ya mawe yanachumwa pale Ngaka, yanapelekwa Malawi kuimarisha umeme wa Malawi na sisi pale hatuna umeme hivi inaingia akilini, ama haiingii akilini? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na niwapongeze Madiwani wote wa Halmashauri ya Mbinga kwa kukubali na kuridhia kuachia jenereta moja ambayo ilikuwa ikitumika kwenye Kiwanda cha Kahawa itumike kupeleka umeme eneo la *Mbamba Bay.*

Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kuwa Mheshimiwa Rais ameweza kutoa jenereta mbili katika Wilaya ya Mbinga ili kutatua tatizo la umeme Wilaya ya Mbinga na ni kweli kabisa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imeweza kutoa jenereta iliyokuwepo kuipeleka *Mbamba Bay,* tayari tunafanya mazungumzo na nimekwisha iagiza *TANESCO* pamoja na *REA* watafute fedha kwa ajili ya kujenga miundo mbinu ya kusambaza umeme kwa wateja, kazi ambayo ingefanyika baadaye baada ya mradi wa kutoa umeme kutoka Makambako- Songea kwenda Mbinga *Mbamba Bay* ingekamilika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kupitia Halmashauri ya Mbinga wamekwenda hatua mbele zaidi ya kupata jenereta. Kwa hiyo, kazi yetu sisi ni kuhakikisha kwamba tunajenga miundombinu haraka ya kuwasambazia wananchi umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katika swali lake la pili, jibu ni haiingii akilini. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Kitu gani hakiingii akilini nini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua hilo na tunafanya kazi sasa hivi ya kuhakikisha kwamba rasilimali za makaa ya mawe zinatumika kwanza kutosheleza mahitaji ya umeme wa ndani kabla hatujafikia kuuza nje.

Kwa hiyo, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge makaa ya mawe yale hayapelekwi tu Malawi

lakini pia viwanda vyetu vya Sementi vya Twiga, Mbeya pamoja na kiwanda cha Chai kinatumia makaa ya mawe haya yanayotoka Mbinga. Lakini pia tukijitosheleza kiu-meme, siyo vibaya pia kuuza kwa wenzetu. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi ili niungane na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Ruvuma kuwakilisha kilio hiki cha umeme katika Mkoa wetu wa Ruvuma.

Kwanza niishukuru Serikali kwa sababu baada ya muda mrefu sana wa matumaini yaliyokuwa hayana matarajio sasa zimetengwa fedha kwa ajili ya umeme wa gridi kutoka Makambako mpaka Songea na kwa kuwa, tayari katika kijiji cha Madaba ambao *REA* wanatakiwa kuufanyia kazi wa maporomoko ya Lingatuta na umeme mwingine wa maji katika kijiji cha Lilondo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ananihakikishia kwamba sasa yuko tayari kuhakikisha *REA* wanafanya kila linalowezekana umeme ule unapatikana ili uweze kuongeza nguvu kwenye gridi ya Taifa umeme kutoka Madaba na ule unaotoka katika kijiji cha Lilondo kama walivyoniahidi miaka yote iliyopita?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo hayana umeme yanapata umeme hasa Wilaya za zamani na Wilaya mpya na hii

tunaifanya katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Ni kweli huko nyuma miradi hii ilipaswa itekelezwe siku nyingi lakini kwasababu ya upungufu wa fedha ilishindwa kutekelezwa lakini sasa hivi Mheshimiwa Mbunge amekiri kabisa kuwa fedha zimepatikana na *REA* tumeiongezea fedha ambayo tutaleta Bajeti yetu hapa nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wa Mbinga na maeneo mengine ambayo wanahitaji umeme watuunge mkono kwenye Bajeti yetu ili tuweze kutekeleza miradi hii. *(Makofi)*

Na. 107

**Fedha Zilizochukuliwa Toka Kampuni ya DECI**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliifungia Kampuni ya *DECI* ikiwa ni pamoja na kukamata mali, fedha na kuwafungulia mashataka Wakurugenzi Wakuu wa Kampuni hiyo:-

(a) Je, Serikali ilifanikiwa kuokoa kiasi gani cha fedha na fedha hizo ziko wapi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani na fedha hizo?

(c) Je, nini mustakabali wa fedha zilizowekezwa na Watanzania waliopanda mbegu zao wakitarajia kupata zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba nijibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliweza kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 14.81 kati ya shilingi bilioni 39.27 zilizokuwa zinadaiwa na washiriki wa *DECI.* Fedha hizi zimezuiliwa katika akaunti zinazomilikiwa na Wakurugenzi wa *DECI* katika mabenki mbalimbali hapa nchi.

Mheshimiwa Spika, hatma ya fedha hizi itategemea hukumu ya kesi 109/2009 iliyofunguliwa tarehe 12 Juni 2009 katika mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Aidha, mnamo Julai 17 mwaka 2012 Mahakama itatoa uamuzi kama washtakiwa wana kesi ya kujibu au la.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Kwa kuwa Serikali imechukua zaidi ya miaka mitatu kuweza kujua kama washtakiwa wana kesi ya kujibu ama la, na kwa kuwa utaratibu huu ukiachwa ukiendelea maana yake kesi ya msingi inaweza ikachukua zaidi ya miaka mitatu mpaka minne, na kwa kuwa suala la *DECI* linahusu maslahi ya Watanzania wengi maskini.

Je, Serikali haioni kwamba baada ya kujulikana kama kuna kesi ya kujibu ama la, kuweka muda maalum ambao kesi ya *DECI* inatakiwa iishe?

La pili, mwaka 2009 aliyekuwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mkulo alikiri kwamba kuna vigogo wa Serikalini wanaohusika na *DECI,* lakini vile vile kuna fedha za umma ambazo ziliingizwa kwenye *DECI* kwa malengo ya kuvuna ili kile kiasi cha Serikalini kirudishwe Serikalini. Lakini kwa taarifa ambazo tunazo, kesi iliyopo inayohusika na *DECI* ni ya wale wachungaji watano. Nilitaka Serikali iniambie kufuatia tamko lile la Mheshimiwa Mkullo, ni vigogo wangapi wa Serikali wameshachukuliwa hatua ambao walihusika na suala hili la *DECI* kwa mantiki ya kuweka fedha za Umma. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala zima la kuwa washutumiwa wana kesi ama hawana hiyo itabidi Mahakama yenyewe iamue na ndipo hatua zinaotakiwa kuendelea za kisheria zitaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuiwekea Mahakama kikomo cha kesi hii isikilizwe kwa muda upi naamini hiyo ni juu ya Mahakama yenyewe, sisi kama Serikali hatuwezi kuingilia muhimili huo na kuwashurutisha wafanye hiyo kazi kwa shinikizo letu sisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vigogo wangapi waliochukuliwa hatua, naomba nikiri kuwa sina taarifa kuwa kuna vigogo waliohusika. Lakini naamini kutokana na kesi kuwa ipo Mahakamani hata wao watachukuliwa hatua zinazopaswa kufuatana na sheria zinavyosema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muangalie tu saa, muda umekwisha na maswali ya msingi yameisha.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwatambue wageni tulionao leo katika ukumbi wetu. Wapo wageni watano wa Waziri Mkuu kutoka *NGO* iitwayo *Friends and Family Community connection* ya California nchini Marekani na ina tawi lake Singida, hawa wageni *wherever they are*, kuna Phil Harris, kuna Joe Anne Shau, *they are five of them, Steven Luther, Happy Philemon and Grace Emmanuel,* hawa ni wageni wa *NGO* inaitwa *Friends and Family Community Connections* nasikia iko Singida. Ahsanteni sana tunafurahi kwamba mmekuja.

Tuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi hamsini pamoja na Walimu wao kutoka shule ya Sekondari ya Bihawana naomba wasimame mahali walipo, ahsanteni sana, tunawatakieni msome vizuri na kwa bidii. Tuna madiwani wanne na wakulima nane wa kahawa wakiongozwa na Mheshimiwa Samweli Mtawa kutoka Jimbo la Mbozi Mashariki. Madiwani na wakulima wa kahawa wapo wapi?

Nadhani ni hilo suala la kahawa kununuliwa mbichi, ahsanteni sana karibuni. Mbunge wenu anapigania hili suala nasikia na wenzake pia wanaolima huko suala hilo wanalifanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge kuna Wajumbe 25 kutoka kikundi cha Wakaguzi *foundation* cha Arusha wapo

wapi hao. Mimi sikifahamu Wakaguzi *Foundation*, karibuni sana. (Makofi)

Kuna Wanafunzi hamsini pamoja na walimu kutoka shule ya msingi ya Chamwino hawa wapo wapi na walimu wao, ahsanteni sana, karibuni sana ninyi ni wenyeji hapa Dodoma. Tunao Madiwani tuliowatambulisha jana, nafikiri 35 kutoka Wilaya ya Handeni, Tanga wasimame huko waliko, tuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, ambaye ni Mzee Vitalis Aiyemba, kutoka Musoma, Karibu Mzee Vitalis. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Kessy ni wanafunzi 8 kutoka *UDOM* wakiongozwa na Ndugu Mansoor Kessy, ashanteni sana wanafunzi wa *UDOM* tunaomba msome kwa bidii. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni ambao wengine wapo *basement* watasubiri kuingia baadaye, hawa ni wanafunzi hamsini kutoka shule ya Sekondari ya Buigiri, wanafunzi 57 kutoka shule ya Sekondari ya wasichana ya Huruma, Dodoma.

Wengine ni wanakwaya 60 kutoka Kanisa la Kiinjili la Kikristo Tanzania (KKKT) Mkoa wa Manyara. Wapo pia Watunza Kumbukumbu na Makatibu Muhtasi 48 kutoka Halmashauri mbalimbali hapa nchini wanaosoma katika Chuo cha *Leadership Training Center* Dodoma, wanaongozwa na Mratibu wao Ndugu James Imambi. Hawa watapata nafasi baadaye kuingia sasa hivi wapo *basement*.

Wageni wengine wote tunawakaribisha kwa sababu hapa ni mahali pa kuwasikiliza Wabunge wenu wanapojadili mambo yao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma *(POAC),* Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 219. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa John Lwanji anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa nane kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika Ukumbi Namba 231.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo huo ndio mwisho wa matangazo. Katibu endelea na *Order Paper.*

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Haya Waheshimiwa Wabunge akina Mwongozo, nianze na Mheshimiwa Mnyika. (*Kicheko*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 64 (1) (c) ambayo nitaomba niisome. Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatazungumza jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahsusi, na vile vile hatapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahsusi inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, naomba niweke mkazo kwenye maneno hatazungumza jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kuhusu maswali na masuala mawili yaliyojitokeza mapema leo na jana yanayogusa mambo ambayo yapo Mahakamani. Leo kumekuwa na maswali mawili, Swali Namba 103 na Swali Namba 107 ambayo yamegusa masuala yaliyopo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Bunge hili linaongozwa na Kanuni na ninaomba nisome Kanuni ya 5(1) inayosema, katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa

Bunge pamoja na Mila na Desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati swali Namba 103 linajibiwa, Serikali ilitoa jibu kwamba haiwezi kuunda Tume huru ya kuchunguza hili suala la Tandahimba kwa kuwa suala lipo Mahakamani. Lakini mimi nimekwenda Tandahimba, suala lililopo Mahakamani ni tofauti na malalamiko ya wananchi. Sasa Bunge kazi yake ni kuisimamia Serikali, Serikali imeacha kujibu kwa sababu suala lipo Mahakamani ni tofauti na suala lililoulizwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye swali Namba 107 sehemu (c) ya swali ilihusu mustakabali wa fedha hizi za *DECI* ambazo tayari Serikali imekwishazikusanya bilioni 14 na kwamba imeeleza mustakabali wa hili itabidi lisubiri kwanza uamuzi ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna *precedence,* kulitokea kesi maarufu sana kama samaki wa Magufuli, samaki walikamatwa, samaki wakahifadhiwa, kesi ikawa inaendelea, baadaye ukafanyika uamuzi na taarifa ikatolewa hapa Bungeni ya kuwagawa wale samaki kabla ya kesi haijahukumiwa. Sasa kama fdha za wananchi zimekaa kwa miaka mitatu na zinashuka thamani na kadhalika. Ni kwa nini Serikali inatumia kivuli cha mambo ambayo hayahusiani kuacha kuamua mambo ambayo inaweza kuamua, inaweza ikaamua zile pesa zikagawanywa.

Mheshimwia Spika, niombe mwongozo wako kwa kurejea na kwa ruhusa yako naomba ninukuu, Nyaraka ya *The Separation of Powers* kwa sababu kwenye Kanuni niliyoisoma ni kwamba unaongozwa kwa Kanuni. Lakini vile vile kwa uzoefu wa Mabunge mengine, kwa sababu neno hakuna tafsiri kwenye Kanuni zetu ya maneno haya yaliyotamkwa hapa ambayo yametuzuia vile vile kujadili masuala yanayohusiana na Madaktari, wakati mengine hayahusiani kabisa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, mbona unaenda nje ya utaratibu?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Sawa, naomba basi nimalizie.

**SPIKA:** Tafadhali naomba tukae chini tuelewane. Naomba ukae chini kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, tunachogomba hapa ni kidogo tu, ukisema Mwongozo kama ulivyosema yale maswali yaliyoko Mahakamani ni sahihi kujadiliana hapa kwa mujibu wa Kanuni zetu. Mimi nitasema siyo sahihi na kama nimeruhusu hapa basi sikujua *details* zake lakini siyo sahihi. *(Makofi)*

Sasa ukiyafanya hivyo unajadili na huo siyo mwongozo. Maana sasa umeanza *DECI* ukaenda Tandahimba, ukaenda kote huko, huo siyo Mwongozo naombeni sana tuelewane. Kama kuna suala zito kama hilo unalotaka kuleta wewe leta kwa utaratibu

mwingine, lakini siyo kwa utaratibu wa Mwongozo, tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge naomba sana, tunatumia vibaya mwongozo. Mwongozo ukisoma pale unasema. Je, suala lililotokea karibuni sasa hivi liko sahihi ama siyo sahihi, ndiyo hivyo tu. Sasa mimi ni lazima nikiri kama ni masuala yanayohusu mahakamani hapa kuzungumza siyo sahihi. Kwa hiyo, hili nimemaliza.

Mwingine nani mwongozo, Mheshimiwa Nassari, unatoa msimamo wa mwongozo maana yake hatupendi kubishana bila sababu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68 kanuni ndogo ya 7 naomba nisiisome kuokoa wakati.

**SPIKA:** Isome maana yake unaanza kujifunza.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, wakati Naibu Waziri wa Nishati na Madini akijibu swali Namba 105 nilisimama nikaomba taarifa kwa mujibu wa ile Kanuni ya 68(8). Alipokuwa akijibu swali Namba 105 alitaja Mkoa wa

Mbinga na Mkoa wa Songea. Tunavyofahamu hakuna Mkoa wa Mbinga wala Mkoa wa Songea. Kwa hiyo tunaomba mwongozo wako au pengine Serikali ituambie kama kuna mikoa mingine ambayo imeongezwa na hatuifahamu, ili kuweka *record clear* kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwanza kabisa aliposema Songea akasema Ruvuma, katika maswali ya kupoteza wakati mengine ndiyo haya. Tuendelee na Mheshimiwa Dkt. Mbassa.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wa kiti chako kwa Kanuni ya 68 (7) kuhusiana na suala sasa ambalo linaendelea.

Mheshimiwa Spika, jana ilikuwa itolewe Kauli ya Serikali.

**SPIKA:** Samahani kuhusu nini?

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Madaktari linaloendelea.

**SPIKA:** Nilishakwambieni toka jana maswali haya hatuzungumzi hapa, naomba ukae, Mheshimiwa Mkosamali (*Kicheko*)

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, mimi ni fupi tu, mwongozo wangu ni hiyo 68 (7).

**SPIKA:** Siyo mwongozo wako umeniomba mwongozo mimi. (*Kicheko*)

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika naomba mwongozo. Jana Kanuni ya 64 (1) (a) na Kanuni ya 64 (1) (g) zilikiukwa. Mbunge wa Babati alitudhalilisha vijana na ukaahidi kwamba utatoa *rulling* kwa sababu alitudhalilisha vijana na kusema kwamba sisi tunafanya vitu ambavyo siyo vya kiutaratibu.

Mheshimiwa Spika, nilitaka mwongozo wako utatoa hii *rulling* lini na ulisema utafuata *Hansard* ili aweze kufuta kauli yake kwa sababu alikiuka Kanuni kwa mujibu wa Kanuni ya 64 (2). (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali humwongozi Spika kufanya kazi yake, Mheshimiwa Ezekia Wenje.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mapema jana kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu aliulizwa swali akajibu kwamba moja ya *measures* ambazo Serikali inachukua kusaidia wananchi kwenye matibabu kipindi hiki cha mgomo wa madaktari ni kwamba wame-*organise* wagonjwa waende kwenye hospitali za Jeshi kama maeneo ya Dar es Salaam ambako kuna hospitali za Jeshi.

Sisi Mwanza hatuna hospitali za Jeshi na ni kweli kwamba mgomo wa Madaktari umeathiri huduma zinazotolewa kwenye hizo hospitali, napenda nipate mwongozo wako ili tupate kauli ya Serikali kwamba wananchi wanaoishi Mwanza na maeneo mengine

ambapo hakuna hospitali za Jeshi, tufanye nini ili tupate matibabu kwa sababu watu wanaumia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Wenje soma habari ya mwongozo swali hilo ni sahihi au siyo sahihi, basi. Sasa wewe unataka mimi nianze kufanya kazi ya Serikali hapa, mimi siiwezi hiyo kazi. *(Kicheko/ Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mnaona, dakika tulizotumia hapa ni *literary* kupoteza muda ambao watu wengine wangefanyakazi ambayo ni mahususi. Ninaomba sana tabia yetu hii si njema, maana ni kupoteza muda na kanuni yetu inakataa mtu kuanza kuuliza swali la kupoteza muda na haya ndiyo mnayofanya sasa. Mnayafanya maksudi ili kusudi mwonekane mnavyopoteza muda. (*Kicheko*)

Lakini rafiki zangu huku Waandishi wa Habari wanasema Spika anawagandamiza Wapinzani, jamani mimi hapa nakaa kwa mujibu wa Kanuni hii. Hizi *statement* za kusema tunapingana na Wapinzani ni upuuzi tu ambao hauna maana, kwa sababu bila Kanuni hii hatuwezi kufanya kazi inayostahili heshima ya Bunge hili itatunzwa tu kwa kutumia Kanuni vizuri naomba Waandishi wa Habari mlielewe hili. Maana yake mnachochea tu uwongo, Spika, Naibu Spika wanapendelea sijui nani.

Waheshimiwa Wabunge hapa waliouliza mwongozo ni akina nani sasa. Siwezi kumjibu mtu ambaye hajauliza mwongozo. Kwa hiyo, naomba Wabunge tujifunze kutumia muda wetu vizuri nimesema wananchi wanatusikiliza na *note* ninazopata

wengi wanasema hawapendi hata kusikiliza kipindi chetu kwa sababu ya utundu unaofanyika hapa ndani. Tafadhali sana mjifunze Kanuni zetu na tuendelee na kazi tuliyodhaminiwa na wananchi waliotuchagua. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 – Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ABIA MUHAMA NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pesa za walipa kodi zimekuwa zikitafunwa kama mchwa bila kujua ni nani aliyehusika na malipo hayo. Sasa ni muda mwafaka wa kuwa na mfumo wa utambuzi kama ule wa Kibenki katika Halmashauri zetu zote nchini ili kuzuia mfumko wa wimbi lililokithiri la wizi wa mali ya umma kwa kutumia *system* za Kibenki ambayo *Data Base* yake itakuwa Makao Makuu ya Wizara. Tukifanya hivyo, kila mlipaji atafahamika kwa *pass word* yake moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi wa Mahesabu waangalie malipo ya Vikao vya Wabunge vinavyofanyika kwenye Halmashauri zao kama kweli Wabunge walihusika katika vikao hivyo kama

Madiwani au pesa husainiwa bila wao kujua. Naomba lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtu wa Kigoma lakini kwa bahati mbaya tumepakana na Nchi ya Burundi iliyoingia kwenye mapigano ya wao kwa wao miaka ya 1972 na kwa bahati mbaya mipaka ya nchi ilipowekwa tuliambiwa sisi ni Watanzania lakini mtu wa Kigoma anapowabebea watu mizigo au kulima mashamba ya watu katika mikoa mingine, hupewa sifa tele za utendaji kazi bora za kusema Waha ni wagumu, Waha ni wachapakazi na kadhalika. Inapofikia Muha amesoma na amepata kazi na kushika cheo fulani ili na yeye sasa akae kwenye kiyoyozi, historia zisizokuwa na maana zinaanza; huyu Mtumishi ni Mrundi alikimbilia Tanzania na matokeo yake Mheshimiwa Spika, watu wengine wanapoteza kazi na wengi wamepata misukosuko ya kikazi, wengine wamekaa nje ya kazi kwa miaka miwili mpaka mitatu, uchunguzi unafanyika wanapokuwa wametuhumiwa; mimi mwenyewe nilipoonekana nimeshinda kura za maoni, nilipata hekaheka mpaka wazazi na majirani hawakulala wakiulizwa uraia wangu, simu za hapa na pale nilipigiwa kuulizwa habari zangu.

Mheshimiwa Spika, sasa watoto wetu wamesoma watafanya kazi katika nchi gani; na wao si wataendelea kuambiwa kuwa ni Warundi? Ikiwa fitina inazidi kipimo na wanaopelekea uongo huo inapothibitishwa kuwa ni uongo hawachukuliwi hatua yoyote na matokeo watu wa Kigoma wanaishangaa Serikali hii, ikiwa Mmanyema au Mbembe, Mbwani, Mgoma ni watu kutoka Zaire, wao hawana shida katika

nchi ya ugenini akihalalishwa kuwa yeye ni Mtanzania halisi. Serikali iache uonevu huo, wote ni Watanzania, lakini tuambiwe ni lini mateso hayo yatakoma. Wanaopakana na Zambia, Malawi, Zaire, Kenya, Msumbiji na Uganda, wao hawana shida ya kuwa wakimbizi, naomba Serikali itoe ufumbuzi wa wazi kwa watu wa Kigoma. Pia elimu ya uraia itolewe katika ngazi za Vitongoji na Kijiji kwa Viongozi wa Serikali na Chama ili kuleta ufanisi wa uongozi bora katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Sumbawanga Mjini eneo la Jangwani wakati wa masika nyumba hujaa maji na watu wanalala na maji kama vyura; je, Serikali imepanga kujenga mifereji mikubwa mingapi katika bajeti hii kwani eneo hilo ni tishio watu wanang'atwa na mbu usiku kucha utafikiri inzi kwenye kidonda? Je, bajeti hii ina makusudi ya kuwaokoa watu wa Sumbawanga wanaokufa ovyo kwa ajili ya malaria na kuhara mara kwa mara? Lini mifereji itajengwa ili Wanasumbawanga nao waone kama wanaishi na Serikali makini?

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ina mkakakati gani wa kumwinua Mtu wa Kala – Nkasi anayeishi kuzimuni bila matarajio ya barabara inayopitika wakati wa masika? Wampembe pia nao huishi shimoni, Watu wa Kala na Wampembe wanaitaka Serikali hii kuziingiza barabara hizi kwenye Barabara za *TANROAD* ili ziweze kushughulikiwa na Serikali kwani hakuna Halmashauri inayoweza kutunza barabara hizo za umbali wa km 67 na 68. Tunaomba barabara hizo zipokelewe na Serikali hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wasaidizi wake, kwa kuendelea kuendesha utawala vizuri na kwa ufanisi, lakini pia kwa maandalizi na uwasilishaji mzuri wa Bejeti ya Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo au Wilaya Mpya ya Kyerwa, ninashukuru kwa kutupatia Wilaya Mpya ya Kyerwa. Tuna imani kuwa ujenzi wa Wilaya hii Mpya ya Kyerwa utaharakishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu posho za Madiwani, ninaipongeza Serikali kwa kuona ukweli kwamba, Madiwani wanafanya kazi kubwa na mchango wao katika kusimamia maendeleo ni mkubwa na nyongeza ya posho wanaistahili.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie baadhi ya maeneo katika Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu, Serikali imesema kwamba, itaongeza posho kwa ajili ya Madiwani. Wenyeviti wa Vijiji hawajatajwa katika kulipwa posho. Naomba ieleweke kuwa Wenyeviti wa Vijiji ni Viongozi muhimu sana katika shughuli za maendeleo ya kila siku. Mathalani, Mbunge anashirikiana na Diwani katika shughuli za kimaendeleo lakini mtekelezaji, msimamizi wa shughuli za kila siku ni Mwenyekiti wa Kijiji. Kutokuwajali kwa posho

kutawakatisha tamaa Wenyeviti wa Vijiji katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Nashauri Serikali iangalie ombi hili la kuwalipa posho Wenyeviti wa Vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mvomero kuna uhaba mkubwa wa walimu wa shule za msingi na sekondari. Katika Jimbo la Mvomero kuna shule zingine zina mwalimu mmoja na hivyo hivyo kwa shule za sekondari, uhaba wa walimu na pengine uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, mwaka uliopita niliiomba Serikali ipeleke umeme katika Kata za Doma, Melela, Kanga na Kibati na Vijijini vya Kidudwe, Husanga, Ngabo, Kisala, Mgudeni na Makuyu. Niliandika barua za maombi na Wizara ilijibu kuwa itapeleka umeme kupitia Wakala wa Umeme Vijijini *(REA).* Naomba sasa Serikali itekeleze ombi langu na ahadi yake kwa kupeleka umeme maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM imetamka bayana kuwa, kila Kijiji kiwe na Zahanati na kila Kata iwe na Kituo cha Afya. Jimbo langu la Mvomero lina uhaba wa Zahanati katika Kata za Sungamji, hakuna Zahanati hata Kijiji kimoja, Kata ya Itembebi Vijiji vya Mndela na Kisinagulu, Kata ya Mtibwa, Vijiji vya Kidudwe na Kunke, Kata ya Maskati, Vijiji vya Maskati na Tarafa ya Mgeta kuna uhaba wa Zahanati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Hotuba kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2012/2013, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni tabia ya Serikali kuchelewesha pembejeo kwa wakulima. Sasa nataka kujua je, mwaka huu Serikali itahakikisha kwamba mbolea na mbegu zitapelekwa kwa wakulima mapema? Aidha, Serikali inatarajia kuboresha mfumo wa usambazaji pembejeo. Nia ni kuondoa upungufu ambao umekuwa unajitokeza katika mfumo wa sasa. Nataka kujua mfumo huo unaokusudiwa utaanza lini? Je, mfumo wenyewe utafanya kazi namna gani? Nataka pia kujua ni mpango wa Serikali wa kuongeza kiwango cha mbolea na mbegu ya ruzuku ya Serikali kinachotolewa sasa?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mpango wa matrekta makubwa kwa madogo na pampu za umwagiliaji. Mpango huo una nia ya kuongeza uzalishaji wa chakula nchini. Hata hivyo, pamoja na nia hiyo nzuri ya Serikali, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba, Watanzania wengi au wakulima bado hawana uwezo wa kununua matrekta hayo. Rai yangu kwa Serikali ni kuiomba iendelee kupunguza bei ya zana hizo. Aidha, naishauri Serikali iendelee kuhamasisha matumizi ya jembe la kukokotwa na maksai (Ng'ombe).

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, katika ukurasa wa 31 wa Kitabu cha Hotuba ya Waziri Mkuu, Serikali

inasema na inalihakikishia Bunge kwamba hakuna Kampuni ya Madini ambayo itakwepa kulipa mrabaha kwa kiwango kipya na kodi zote kama inavyotakiwa. Naipongeza Serikali kwa hatua hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa Bunge ndicho chombo kinachoisimamia Serikali, nashauri Serikali itoe taarifa kwa Bunge katika kila Mkutano wa Bunge kuhusu ulipaji wa malimbikizo yote ya kodi tangu Sheria Na. 14 ya Mwaka 2010 ilipopitishwa. Aidha ni vyema Serikali ikalieleza Bunge ni kiasi gani cha fedha ambacho Makampuni ya Madini yanapaswa kulipa kama mrabaha.

Serikali kupitia kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu na kufuatia swali lililoulizwa na Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb), sasa Naibu Waziri, Waziri Mkuu aliahidi kwamba Deni la TAZARA kiasi cha shillingi bilioni 22 kingelipwa kwa awamu. Nataka kujua hadi sasa Serikali imeshalipia kiasi gani na lini itamaliza kulipa deni hilo?

Mheshimiwa Spika, suala la Ustawishaji Makao Makuu Dodoma lina zaidi ya miaka 30 sasa. Hata hivyo, mamlaka inayohusika na Ustawishaji Makao Makuu Dodoma imekuwa inapewa pesa kidogo sana! Kutokana na hali hiyo, uendelezaji wa Mji wa Dodoma umekuwa siyo wa kuridhisha hata kidogo. Tatizo ninaloliona sasa ni Viongozi wa Serikali kutokuwa tayari kuhamia Dodoma. Viongozi wetu hawana utashi, hawana utayari.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kwa Mwaka huu wa Fedha 2012/2013 ni Wizara ngapi zinatarajiwa kuhamia Dodoma? Nataka pia kujua hivi ni kwa nini

Serikali inaendelea kujenga majengo ya Wizara kule Dar es Salaam; je, hii siyo dalili ya kutosha kwamba Serikali haipo tayari kuhamia Dodoma?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na utendaji mbaya kwa baadhi ya Watumishi wa TAMISEMI; kinachosikitisha ni kuona kwamba Serikali haichukui hatua za haraka katika kurekebisha hali hiyo. Nashauri Serikali ichukue hatua za kinidhamu kwa watumishi watakaopatikana na hatia na *CAG*, yaani ubadhirifu wa mali ya umma. Pia wale watakaohusika na ubadhirifu basi wafilisiwe mali husika. Inaweza kusaida kujenga nidhamu ya matumizi kwa pesa za Serikali.

Mheshimiwa Spika, upo ugonjwa katika Halmashauri nyingi nchini wa Watumishi wengi kukaimu. Kwa mfano, Halmashauri za Arusha, Monduli, Rombo, Arusha Jiji, zipo nyingi nataja chache tu. Ni dhahiri kwamba, mtu anayekaimu mara nyingi hukosa kujiajiri, hukosa kujiamini na utendaji hauwi mzuri sana. Nashauri TAMISEMI iondokane na hali hiyo ya Watumishi kukaimu muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nashauri Serikali iachane na kigezo cha mtumishi kufikisha miaka saba ili apate sifa ya kuwa Mkuu wa Idara. Nashauri sifa hiyo iwe miaka mitatu, lakini pia kigezo cha utendaji mzuri kizingatiwe. Vinginevyo, tutaendelea kudidimiza utendaji kazi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake wakati akiwasilisha Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi yake na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2012/13. Hotuba hiyo imefafanua mambo yote kwa uwazi na inaleta matumaini kwa kuwa inaonesha ni kwa kiasi gani Serikali imejiandaa kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia mambo machache yafuatayo:-

Naipongeza Serikali kusikia kilio cha Wabunge na Madiwani na sasa imeamua kuongeza kiwango cha posho ya Madiwani. Ingawa kiwango hakikutajwa, ninaamini kiwango hicho kitakuwa ni kile kitakachomfanya au kumsaidia aweze kukopesheka. Madiwani wengi hawana vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuzungukia maeneo yao ya kazi. Kiwango cha sasa ni kidogo sana. Kwa kutambua uwezo wa Taifa kiuchumi, kwa kile kilichopatikana tunashukuru sana. Hata hivyo, kundi la Wenyeviti wa vijiji, Mitaa na Vitongoji nao wafikiriwe kulipwa posho kwani wanafanya kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa Mikoa duni kiuchumi. Pamoja na juhudi za Wananchi katika uzalishaji wa njia ya Kilimo, Uvuvi, Biashara na kadhalika, Mkoa wetu unakabiliwa na bei kubwa sana za bidhaa za viwandani; saruji, mabati, nondo na vingine vyote.

Mheshimiwa Spika, kipekee, mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya taa, tunayapata kwa bei ya juu sana kuliko Dar es Salaam, Morogoro na mikoa mingine iliyo jirani na Dar es Salaam. Kukosekana kwa njia rahisi ya kusafirisha bidhaa kama treni na meli ndicho kinachofanya bei za bidhaa hizo kuwa juu. Hivi haiwezekani mpango wa kujenga bomba la mafuta Dar es Salaam – Mwanza ukafufuliwa ili kupunguza bei ya mafuta? Uliwahi kusikika mpango au mawazo ya kujenga viwanda cha saruji katika Mkoa mmojawapo wa Kanda ya Ziwa. Tunaomba mawazo hayo yawekwe katika vitendo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa vijana, hili litaendelea kuwa tatizo na mzigo mkubwa kwa taifa. Ni ajabu kila anayezungumzia ajira kwa vijana anaonesha uchungu sana lakini hatoi ushauri nini kifanyike. Kila mwaka vijana wanamaliza shule za msingi lakini si wote wanaendelea na masomo ya sekondari. Hawa hawaajiriki lakini mpango mizuri ikiandaliwa, wanaweza kuajiri baada ya kuhamasishwa na kupewa mafunzo na stadi mbalimbali kama vile ufundi mbalimbali; ufyatuaji wa matofali, kilimo cha mboga, ufugaji wa kuku, mbuzi na hata samaki na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa Bajeti nzuri iliyowasilishwa na kupitishwa katika Bunge hili. Tunayo matumaini kuwa ikitekelezwa kwa makini, Taifa litapiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. HEZEKIAH NDAHANI CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Hotuba ya Waziri Mkuu, pamoja na maelezo ya kiutendaji ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi (TAMISEMI).

Naunga mkono hoja na ninaomba yafuatayo yapokelewe kama mchango wangu:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua umuhimu wa *CDA,* chombo hiki cha Serikali, Wananchi wa Dodoma wengi wao wanashindwa kuelewa ni kwa nini Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imenyimwa haki yake ya kumiliki Ardhi kwa niaba ya Wananchi wa Manispaa ya Dodoma. Hali inayojidhihirisha dhahiri ni kwamba, *CDA* inamiliki Ardhi ya Wananchi wa Manispaa ya Dodoma wakati Manispaa yenyewe imebakiwa na watu bila Ardhi. Jambo hili linaleta mgongano mkubwa sana kiutendaji.

Tunapenda kushukuru sana kwa jitihada za Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kuliona hilo na tunasubiri matokeo ya hatua alizoziweka kunusuru hali hiyo ya mgogoro. Serikali imesema inafanyia kazi mapandekezo ya Mshauri Mwekezaji kuhusu Muundo wa *CDA* na kutatua mwingiliano wa utendaji uliopo kati ya Manispaa ya Dodoma. Hili ni jambo jema, lakini naomba liharakishwe na kulitolea maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile itakavyokuwa imependekezwa na Mshauri Mwelekezi, naomba Wananchi wa Dodoma wapewe Mamlaka ya kusimamia Ardhi iliyo chini ya Mamlaka ya Manispaa

ya Dodoma kama ilivyo kwa Mamlaka zingine za Miji. Jambo linaloleta mgongano ni lile la Manispaa ya Dodoma kuwa haina Mamlaka juu ya Ardhi ya Dodoma, ambayo inasimamiwa na chombo kingine. Kisheria Serikali haiwezi kukosa Ardhi na ikaendelea kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali isimamie Ustawishaji wa Mji Mkuu wa Dodoma kipitia *CDA* kwa njia ya kupanga Mji na kushauri jinsi ya kuujenga kupitia Manispaa ya Dodoma. Hapa Dodoma tunashindwa kujua nani anawajibika na ujenzi wa Barabara za Mji na miundombinu mingine, kwa sababu kuna kutupiana mpira juu ya nani mwajibikaji. *CDA* inawajibika kupitia Bodi ya Wakurugenzi kwa mamlaka iliyoiteua Bodi hiyo. Kwa hiyo, kwenye Vikao vya Kimkoa *CDA* haina wajibu wa moja kwa moja na wala hata kwenye Vikao vya Mkoa kama *RCC, CDA* hawana wajibu wa kujibu hoja kama ilivyo Manispaa.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri zinazofanywa na *CDA* na zile zitakazoendelea kufanywa kuendeleza Mji Mkuu wa Dodoma; mwananchi wa kawaida anayeishi Dodoma atatumia njia gani ya moja kwa moja kuzijua kazi hizo na kama ikibidi apate fursa ya kukosoa.

Mheshimiwa Spika, Wanadodoma wangependa mgogoro na mwingiliano uliopo baina ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma umalizike haraka.

**MHE. MANSOOR SHANIF HIRAN:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono Bajeti ya Waziri Mkuu. Naomba kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya pembejeo ni makubwa Wilaya ya Kwimba, naomba Vocha za Pembejeo ya Mpunga iongezwe kutoka 603 – 6000.

Mheshimiwa Spika, naomba Ofisi ya TAMISEMI itoe mwongozo kwenye Halmashauri kuhusiana na Miradi ambayo imepangiwa fedha kutoka Mfuko wa Jimbo, ambayo Kamati imeshapanga, lakini utekelezaji wake inachukua takriban miezi mitatu mpaka sita Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Spika, nashauri trekta za pembejeo zingesambazwa kwenye Halmashauri zote nchini na zikifikishwa huko zitauzwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu naomba Wakala wa Umeme Vijijini waniletee umeme Tarafa ya Wanashimba na hususan Mji Mdogo wa Hungumarwa. Miaka mingi wananchi wanasubiri umeme na usanifu umeshafanywa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia mambo matatu kama ifuatavyo:-

Nianze kwa kusema kwamba, nimefarijika sana kusikia adhabu ya mtu anayekamatwa na madawa ya kulevya ni kifungo cha maisha. Tunapoteza nguvu kazi ambao ni vijana, vijana wengi wamejiingiza kwenye

madawa ya kulevya na kila kukicha idadi ya wanaotumia madawa ya kulevya inazidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwa imejitahidi sana kuzuia uingizaji wa madawa ya kulevya kwani tunasikia kila siku watu wanakamatwa na madawa ya kulevya licha ya kuwa siku hizi unatumika ujanja wa kuwatumia wanawake lakini Serikali imeweza kuwabaini hao wanawake na kuwakamata.

Mheshimiwa Spika, jambo ninaloliomba kwa Serikali, itafute mbinu zaidi za kuwakamata hawa waletaji kwani kufanikiwa kwa vijana kutotumia madawa ya kulevya ni kudhibiti huu uingizaji wa madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato *TRA;* nasema bado Wafanyakazi wa *TRA* siyo waaminifu, mapato mengi tu yanakusanywa lakini yanavuja. Wafanyakazi ambao hawana uchungu wa nchi yetu huwa wanatumia hizi pesa kwa matumizi yao. Kuna suala ambalo limejitokeza siku nyingi, mfanyabiashara analeta makontena ya nguo yenye thamani ya dola 100,000 na yule mfanyabiashara hutakiwa kulipa Sh. 60,000 kwa mzigo wake lakini *TRA* zinakwenda Sh. 20,000 tu na Sh. 40,000 wanagawana Wafanyakazi wa *TRA* na Wakala wa Forodha. Kuna mambo mengi ya ubadhirifu yanafanyika *TRA,* imefika wakati sasa *TRA* ije na mfumo mzuri wa ukusanyaji wa hizi kodi.

Mheshimiwa Spika, mtu ameajiriwa *TRA* kipindi kifupi utamwona anavyobadilika maisha yake haraka

sana. Lazima wafanyakazi wawe wanabadilishwa sehemu zao siyo kumwacha karani au ofisa kukaa sehemu moja kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna wataalam wa kutosha kwenye Wizara ya Fedha ni jukumu lao kutafuta vyanzo vingine vya mapato.

Mheshimiwa Spika, namaliza kwa kusema kwa makusudi paajiriwe watu waaminifu sana ambao wataweza kukusanya kodi za uhakika na pia muwape na majukumu wakawafuatilia wale wote ambao siyo waadilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji na uwekezaji, ili tupate wawekezaji wengi lazima tuwajengee mazingira mazuri, maeneo yapimwe kabisa na yaelekeze kuwa ni Mradi gani unafanyika kwenye maeneo hayo. Pia pafanyike *fesibility study* kabisa ili mwekezaji ajue haraka tu anapofika hapa atawekeza Mradi gani.

Maeneo ambayo yamemilikiwa na wananchi, Serikali ikitaka kuyachukua wayalipie wao kabisa kabla ya kumpa mwekezaji kuepuka migogoro mingi ambayo tunaishuhudia baina ya Serikali na Wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara isimamie mikopo vizuri ili iweze kuwafikia walengwa. Kuna huu Mfuko wa JK unalalamikiwa sana haujawafikia walengwa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake ya Bajeti. Niseme tu kuwa uzuri wa Hotuba uendane na utekelezaji wa Mipango yote ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, dhana nzima ya *D by D* ni nzuri lakini haikuwa na matayarisho kule Wilayani na Vijijini. Kwa mfano, Wizara ya Mifugo inatengeneza Sera ya Kuendeleza Mifugo lakini watekelezaji ni Halmashauri, ambayo ndiyo yenye pesa ya kuchimbia mabwawa na malambo au majosho na kadhalika. Kwa kuwa Halmashauri nyingi zina upungufu mkubwa unaolalamikiwa sana ni bora Serikali itafakari upya dhana hii ya *D by D* kwa mustakabali wa nchi na kwa ufanisi wa mipango yote ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa mahabusu, nikiwa Mjumbe wa Kamati inayohusiana na Masuala ya UKIMWI, tulitembelea Gereza la Ukonga na Segerea mwezi Februari na Mei mwaka huu. Tulishuhudia wenyewe msongamano wa kutisha katika mabweni ya mahabusu. Kwa mfano, bweni linalotarajiwa kuchukua mahabusu kumi na tano tulikuta wamelala mahabusu 75. Hili tuliliona *live* maana waliamua kutuonesha hali halisi ya msongamano pale. Hata mahabusu wakitaka kugeuka upande wa pili wanapolala haiwezekani mpaka wapewe amri wote wageuke kwa pamoja. Hali hii pia inafanya wasiweze kujisaidia vyooni ambavyo pia ni vibovu na badala yake wanajisaidia kwenye ndoo. Hali hii inachochea mahabusu

kujamiiana; hivyo, kufanya maambukizi ya UKIMWI kuwa ni tatizo linaloendelea.

Mheshimiwa Spika, hivi inashindikana vipi kupunguza idadi ya mahabusu kama suala la ubambikizwaji wa kesi litakomeshwa na kama mahakama itaendesha kesi kwa haraka? Naomba hili liwe suala la dharura kuwanusuru vijana wetu ambao ni nguvu kazi kubwa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la vijana wanaoishi katika mazingira hatarishi ni kubwa hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Hawa ni vijana wanaohitaji elimu, afya bora na makazi; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa inawatambua vijana hao na kuwapatia huduma muhimu kwa maisha yao?

**MHE. ENG. GERSON HOSEA LWENGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri. Naiunga mkono na nawatakia kila la kheri ili waweze kuyatekeleza kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati kwa kupewa Wilaya Mpya ya Wanging'ombe na kuidhinishiwa Makao Makuu ya Igwachanya. Najua kabisa mwanzo ni mgumu, lakini ni vizuri tukasisitiza uanzishwaji wa Halmashauri uwe wa haraka ili wasimamie ujenzi wa majengo ya Makoa Makuu wakati wa majumuisho itafaa na hasa kwa Wilaya na Mikoa Mipya utolewe mchanganuo wa fedha zilizotengwa kwenye Bajeti ya 2012/13 ili sisi Wabunge tufuatilie utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ilani ya CCM 2010, tuliahidi kuwa kila Wilaya itakuwa na Hospitali ya Wilaya ya Serikali. Wilaya ya Wanging'ombe naomba itengewe fedha za kujenga Hospitali ya Wilaya ya Wanging'ombe.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi, ambalo ndiyo hiyo Wilaya ya Wanging'ombe, wamehamasika sana katika kuchangia maendeleo ya afya, elimu na kadhalika lakini cha kusikitisha yapo majengo mengi wananchi wametoa mchango wao lakini yale yanayotakiwa kufanywa na Serikali yanachukua miaka mingi, sehemu nyingine zaidi ya miaka mitano bila kumiliki. Hii inakatisha tamaa wananchi.

Mheshimwa Spika, wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa Mwaka 2010, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokea maombi ya gari la Kituo cha Polisi Ilembula na akaahidi kuwa atawapatia lakini mpaka sasa ahadi yake hiyo hajaitekeleza. Naomba sana kwa niaba ya wananchi atimize ahadi hiyo, wananchi wamekuwa wakinisisitizia kila ninapofanya ziara maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize juu ya ujenzi wa Vyuo vya *VETA* kwa kila Wilaya. Elimu ya *VETA* inaweza kuanzia katika majengo ya Vyuo vya Wananchi ambapo maeneo mengi hayatumiki kwa Wilaya ya Wanging'ombe. Naomba majengo yaliyokuwa ya Mradi wa Maji pale Soliwaya, Wanging'ombe, tunaweza kuanzisha Chuo cha *VETA*

pale ili kupunguza adha ya vijana kuhusu kupata nafasi ya kujiajiri katika fani mbalimbali za kiufundi.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLACK:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii. Aidha, napenda nichukue nafasi hii, kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeniwezesha afya na nguvu ya kuzungumza mbele ya Bunge lako Tukufu kuwawakilisha Watanzania wengi wanaoendelea kuteseka na kukosa huduma za kimsingi ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuiomba Serikali kwamba, tuwe tunaangalia kwanza mafanikio na upungufu wa bajeti iliyopita, ndiyo tuingie kwenye Bajeti nyingine kuangalia vipaumbele na maainisho ni yapi tumefanikiwa na yapi hatujafanikiwa ili tusiendelee kuwahadaa wananchi kwa maneno matupu yasiyozaa matunda.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 2011 Juni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa Hotuba kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi.

Mheshimiwa Spika, tumeingia sasa kwenye Bajeti mpya huku matatizo ya Watanzania ndiyo kwanza yanazidi kuongezeka. Nitolee mfano Mkoa wangu wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la Elimu ya Msingi. Kwa upande wa elimu Mpanda, sidhani kama kuna Kiongozi wa Juu kama Mkurugenzi wa Wilaya,

Waziri, Mbunge na kadhalika, anayeweza kusomesha mtoto wake katika Shule za Mkoa wa Katavi. Tukianzia na shule za msingi, hazina madawati, watoto wanakaa chini tena kwenye sakafu iliyochimbuka ovyo. Darasa moja wanasoma watoto zaidi ya mia moja na hamsini, mapaa yanavuja mvua ikinyesha, walimu wanahaha kwa kuhama kuokoa vitabu visilowe, kuta zimepasuka ovyo kiasi cha kuhatarisha maisha ya watoto wetu, maji safi na salama ya kunywa shule hazina bomba la maji au visima. Je, watoto wetu watafaulu masomo kwa hali hii? Walimu wao hawana nyumba za kuishi wala vyoo vya kutumia na wanatembea umbali mrefu bila usafiri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekondari, shule ni nzuri kwa majengo na vifaa vya kufundishia havitoshi, maabara hakuna na watoto wanapanga nyumba. Mabweni hakuna badala ya kufaulu masomo wanafaulu kubeba mimba.

Mheshimiwa Spika, naongea kwa uchungu kwa sababu nimetembelea shule nimejionea. Naiomba Serikali katika Bajeti hii itenge fungu la Wakaguzi wa Elimu ili waweze kuzungukia shule kuzikagua, tofauti na sasa Wakaguzi wamesahaulika sana hata usafiri hawana, wanategemea kunyang'anyana na Mkurugenzi, kitu ambacho kinafanya kazi yao idorore. Elimu ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, mpaka chaki sasa hivi inakosekana; hii ni elimu bora au ni bora elimu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, tukumbuke kilimo ni uti wa mgongo, pia ndiyo ajira kuu kwa Mtanzania wa kawaida. Leo hii mkulima huyu mdogo hajaliwi, hapewi kipaumbele, mbolea haiji kwa wakati na hata ikija mfuko unauzwa Sh. 70,000 Je, Serikali inategemea mwananchi anainuka vipi? Haya ndiyo Maisha Bora kwa kila Mtanzania?

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu, Mkoa wa Rukwa na Katavi ikiwa bado Wilaya ni Mkoa mkongwe. Tunaomba sana tukumbukwe kuletewa umeme wa uhakika wa Gridi ya Taifa. Umeme utoke Nyakanazi - Kigoma, Mpanda, Sumbawanga, Tunduma – Mbeya Makete, Makambako na Iringa. Tunazalisha sana kilimo; hivyo, tunahitaji viwanda sasa.

Mheshimiwa Spika, tuna ardhi nzuri sana tunahitaji kukuza zao la miwa ili tufungue viwanda vya sukari badala ya kutegemea Zambia na Malawi. Uwezo huo tunao ila tunarudishwa nyuma kimaendeleo kwa kukosa umeme wa uhakika. Tamko kwa Serikali, tunaomba umeme wa Gridi ya Taifa sasa ili tuamue mwone.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Afya; vijijini ni sehemu ambako Watanzania wengi bado wanapoteza maisha kwa wingi. Bado wananchi wanatembea umbali zaidi ya kilomita tano, madawa hakuna, wananchi wananunua kwenye maduka ambako bei ni kubwa wagonjwa hawamudu hasa wa kipato cha chini pia dawa nyingi zimepitwa muda, Watanzania wanapata madhara, wahudumu katika vituo hawatoshi, maji hakuna wagonjwa mpaka wafuate mtoni, mawasiliano

ni duni kwa mgonjwa anayetaka kupelekwa Hospitali ya Wilaya, watumishi hawana nyumba za kuishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ilipe deni la *MSD* shilingi bilioni 41 ili wasambaze dawa za kutosha na ziwe na Nembo ya Serikali ili kuepusha wizi wa dawa kwenye maduka binafsi

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jitihada kubwa alizozionesha katika kupanga mikakati mizuri ambayo imemgusa kila mtu, kila sekta.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja hii, nianze na Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba, Bunge tulipitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8 ya Mwaka 2011 (Sura ya 85). Aidha, Bunge lilifanya Marekebisho ya Sheria hiyo katika Mkutano wa Sita, mwezi Februari 2012. Sasa swali langu; Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo ndani yake kuna Tume itakayoratibu na kukusanya maoni kwa wananchi kuhusu Mabadiliko ya Katiba au Katiba waitakayo; cha kushangaza hadi leo Sheria hiyo bado haijapelekwa katika Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika ili Baraza lipate kutilia mkazo.

Kama Katiba ya Zanzibar inavyosema, naomba kunukuu kifungu 132(1) na kifungu 132(2): "Sheria yoyote inayopitishwa na Bunge la Jamhuri itatumika Zanzibar mpaka Sheria hiyo iwe kwa mambo ya

Muungano tu na ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano 132(2). Sheria kama hiyo lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika." Mwisho wa kunukuu.

Je, hili limefanyika na mbona tumeshaanza kufanya kazi tarehe 1 Mei, 2012 hatuoni kwamba Tume hii inaweza kukosa ushirikiano wa aina moja au nyingine? Hali iliyoko sasa Zanzibar ya Jumuiya ya Uamsho kama wanavyosema hatuwezi kujadili Katiba bila ya kujadili kwanza Muungano.

Mheshimiwa Spika, sasa ninakuja katika huo Muungano. Kama ilivyosemwa tarehe 26 Aprili, 2012 Muungano wetu ulitimiza miaka 48 Watanzania kuishi pamoja kwa amani na utulivu chini ya Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal. Zipo kero ambazo mmekaa Vikao vya Mawaziri na Makatibu Wakuu na kuna kero mbili ambazo mmezifanyia kazi nazo ni kuhusu ongezeko kubwa la ankara za umeme kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO* na Mfuko wa Jimbo sasa ni faraja kwa wananchi ila kuna kero nyingine nazo hizi pia zinataka ufumbuzi wa haraka. Kero hizo ni kero ya *TRA,* Bandari kwa wafanyabiashara, mafuta na kero ya mipaka ya Bahari Kuu.

Wazanzibari wanataka kujua ufumbuzi wa kero hizi. Kwa nini mambo muhimu yanayohusu maslahi ya wananchi yanachukua muda mrefu sana kuyatatua na ndiyo maana hivi sasa kuna vikundi vya uamsho ambavyo vinatishia amani na utulivu uliodumu kwa muda wa miaka 48. Nakumbuka nilimwambia

Mheshimiwa Waziri kuwa, Muungano wetu ni kama koti, likikubana unalivua na maneno hayo niliyanukuu tu. Sasa wamekuja Jumuiya ya Uamsho na wanataka Zanzibar yao. Naomba kundi hili msilidharau kwani kwa wenzetu kulianza hivi hivi kidogo kidogo mpaka moto ukawaka. Mkae nao ili kutafuta ufumbuzi amani iendelee kwa utulivu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, Muungano wowote Duniani unakutana na changamoto mbalimbali; Jumuiya ya Uamsho ni moja ya changamoto ya Muungano huu tulionao.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu bado haijawa tayari kumwezesha mwananchi wa kawaida kiuchumi kwani kuna Programu na Sera nyingi zinakuwa zinaandaliwa lakini huishia vitabuni tu. Kwa kweli kuna Mifuko mingi tu ya kumwezesha mwananchi lakini mmemwandaaje huyo mwananchi; je, amepata elimu? Hamwoni kuwa pesa au Mifuko hiyo huishia kwa wajanja? Wanaolima kilimo cha umwagiliaji mmewatayarishia mabwawa? Hamwoni bado tatizo litakuwa pale pale kilimo chetu kitakuwa duni?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa Bunge la Bajeti, Serikali ilisema imejizatiti kukabiliana na tatizo la madawa ya kulevya na mwaka huu imesema hivyo hivyo. Waathirika wa madawa haya ni watoto wa maskini ambao hawana ajira. *Solution* ya tatizo hili siyo kujenga vituo ila ni adhabu kwa yeyote atakayekamatwa na madawa hayo anyongwe tu kama nchi za wenzetu ili iwe fundisho kwa mwingine. Wanaofanya biashara hii ni wa watu wakubwa na

matajiri na siyo maskini kama hao wavutaji, Vyombo vyetu vya Usalama havifanyi kazi kwa uzalendo kwani rushwa imetawala katika biashara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwe makini sana kwa hili au mwisho wa siku Taifa hili litakuwa na waathirika wengi wa madawa hayo na Serikali itakosa watendaji kazi hasa vijana, kwani tunaamini vijana ni nguvu ya mabadiliko. Ahsante.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, katika Hotuba hii imesemwa kwamba bandari inaboreka lakini bila wafanyakazi mahiri, wanaopata mafunzo kila sekta hii inapoamua kuleta vyombo vipya vya kisasa, hakuna kitakachoendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi, hivi vyombo vyetu vinavyoingiza meli kila siku na kutupatia mapato ya bandani zetu kwa wingi; je, vinafanyiwa *service* kila vinapofikia muda wake au tunasubiri mpaka *TAG* hizo zilale kabisa baadaye zipigwe mnada? Naiomba Serikali na Wizara husika iliangalie hili kwa kina ili vyombo hivi visife kwa uzembe na baadaye kuja kupigwa mnada.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pesa za Rada; kwa kuwa Zanzibar nayo inahusika, naiomba Serikali isimamie suala hili ili nasi tufaidike, kwenye elimu tupatiwe madawati, vifaa vya kufundishia masomo ya sayansi, kompyuta na vifaa vyote vya elimu. Naiomba Serikali hii sikivu, pindi itakapokuwa tayari sisi Viongozi hasa wa Majimbo tueleweshwe ili baadaye pakitokea

masuala kuhusiana na fedha hizi tupate majibu ya kuwajibu wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, Serikali haikuwatendea haki wananchi wangu kwani haikutekeleza haki yao ya Kikatiba ya kulinda maisha yao na mali zao.

Mheshimiwa Spika, asilimia mia moja ya Wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wanategemea kilimo ili waweze kuishi. Kilimo chao ni cha mazao makuu mawili; mpunga na tangawizi. Mazao yote haya yanategemea umwagiliaji. Licha ya mazao haya, Jimbo langu lina kila aina ya mboga mboga kwani lina mito mikubwa minne.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Same Mashariki lina Msitu wa Shengena wa asili ambao ndiyo unaozaa mito mikubwa sana mine; mto wa kwanza mkubwa sana unaozaliwa na Msitu wa Shengena ni Mto Saseni. Mto huo ndiyo chanzo kikuu cha kilimo cha tangawizi katika Kata ya Mpinji, Miamba, Kihurio, Mkomazi, mpaka kufikia Pangani. Mto mkubwa wa pili ni Mto wa Yongoma (maana ya yongoma ni kelele). Mto huu maji yake ni mengi mno na wingi huo unaosababisha kelele kubwa maji yanaposafiri. Mto huu unahudumia Kata ya Mtii Milimani lakini kubwa katika yote Mto huu ndiyo chanzo cha Skimu ya Umwagiliaji ya Ndungu ambayo tulizawadiwa na Wajapani na ni Skimu yenye

uwezo mkubwa sana ya umwagiliaji wa kilimo cha mpunga na kuwawezesha wananchi kuvuna mpunga mara mbili kwa mwaka. Mto huu ndiyo unaotengeneza Bwawa kubwa la Kalemawe lililoko Kata ya Ndungu.

Mto wa tatu unaozaliwa na Msitu wa Shengena ni Mto Hingilili. Mto huu unatumika kumwagilia Kata za Mbaga, Vuje, Ntenga, Bombo na Kata kubwa ya Tambarare ya Maore, ambayo inaongoza kwa kilimo cha nazi Mkoa wa Kilimanjaro.

Mto wa nne ni Mto Nakombo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Msitu wa Shengena ni mpana mno, bila ya Msitu wa Shengena hakuna maisha kabisa kwenye Jimbo la Same Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Msitu wa Shengena umeharibiwa kabisa na majangili wanaovuna dhahabu kwa njia haramu. Msitu wa Shengena umesheheni miti mikubwa sana na ni Msitu wa asili. Wavunaji hawa wa dhahabu wanaikausha miti hii kwa kemikali kwani siyo rahisi kuikata. Miti hii inapokauka ndipo wanapoiangusha na kuvuna dhahabu kwa kuzoa kwa mabeleshi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuvuna dhahabu hii wanaisafisha huko huko kwa kutumia *mercury* ambayo imejaa kemikali kali sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu na Serikali liko hapa: Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Maige, alikwenda Shengena tarehe 23 Desemba 2010, aliona tatizo hili lilipoanza. Alikwenda na *delegation* kubwa akiwepo na Kaimu Mkurugenzi wa Misitu na Viongozi wengine Waandamizi wa Wizara hii. Hawakuchukua hatua yoyote hapa. Wananchi waliendelea kulalamika kunywa maji yenye kemikali na Wizara hii haikuchukua hatua yoyote na ikawa inajua kinachoendelea. Tatizo likaendelea kuwa kubwa, ndipo mimi mwenyewe nikaamua kuingia ndani ya Msitu tarehe 9 Mei 2012, takriban mwaka mmoja na nusu bila ya Serikali kuchukua hatua yoyote ya kutatua matatizo ya uharibifu wa vyanzo vya maji na wananchi wangu wakiachwa wanaendelea kunywa maji yenye kemikali ambayo ni chanzo cha magonjwa mengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mimi kwenda, nilitoa kwenye Vyombo vya Habari na hili likamfanya Mkurugenzi wa Misitu astuke na tarehe 10 Juni 2012 akaenda Shengena. Swali; alikwenda kufanya nini na yeye alijua uharibifu wote tangu Desemba 2010? Anamdanganya nani?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Wizara iliachia uchimbaji huo wa dhahabu ukaathiri Jimbo langu kwa muda wa mwaka mmoja na nusu bila kuchukua hatua ya kuepusha uharibifu huu?

Mheshimiwa Spika, jibu; inasemekana na mimi nashawishika kuamini kwamba, kuna baadhi ya Viongozi Wakuu waliokuwa wanafaidika na uchimbaji huo haramu ambao umemaliza vyanzo vya maji na

kuua afya za maisha ya wananchi wangu. Wananchi wangu wametumia maji ya sumu kwa muda mrefu sijui hatima yao ni nini.

Mheshimiwa Spika, ninaisihi Serikali sasa ifanye kazi ya dhati na iweze kuutambua mtandao wa waliopewa dhamana ya kuhudumia wananchi badala yake wakajinufaisha wao. Nashawishika kuamini hili ni kwa sababu kwa nini Serikali ilizibwa macho kulishughulikia hili?

Mheshimiwa Spika, ukimya wa Serikali ulisababishwa na nini? Hiyo dhahabu ilipelekwa wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii nami kuchangia hoja kwa kusema kwamba katika Jedwali la Orodha lililoambatana na Hotuba ya Waziri Mkuu kuna fedha zinazoonesha kupangwa kwa ajili ya ama ujenzi wa madarasa, ujenzi wa nyumba za walimu, vyoo na kadhalika, lakini ujenzi pengine haukufanyika mwaka uliopita na fedha hazijaonesha kutumika. Je, fedha hizo bado zipo ama hazikupelekwa au la na kwa nini ujenzi haukufanyika?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata kwa wingi siyo ufaulu katika Sekta ya Elimu. Tatizo la maabara na maktaba katika shule hizo ni kubwa sana na tunajidanganya tunaposema vijana wetu wanafaulu vizuri na tunaliangamiza Taifa kwani kijana anamaliza darasa la kumi na mbili hajui hata *test tube*;

tunatarajia nini kuhusu Taifa letu na Ulimwengu huu wa Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, leo inashangaza kusikia kwamba hata Chuo Kikuu cha Dodoma hakuna maabara!

Mheshimiwa Spika, walimu na mazingira magumu ya kazi: Hivi kusomea ualimu imekuwa ni adhabu? Kwani vijana sasa wanasema ualimu ni daraja tu la kupita na kuelekea kwenye mafao zaidi. Hii inatokana na kutokuwajali walimu. Tunampeleka mwalimu kijijini ambako ni mgeni, hana nyumba ya kuishi, miezi mitatu hajapata mshahara. Shule anayofundisha iko mbali naye, hana usafiri, hana nauli na hayo mazingira magumu hayakuzingatiwa kabla. Je, tunalisimamiaje hili ili kuwafanya vijana wetu waipende kazi ya ualimu na tuzalishe Taifa la Wasomi wa kweli na siyo Taifa la Wajinga.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani mara hii limevunja rekodi, kwani wanafunzi wanafanya mtihani siku moja lakini matokeo yanatoka kwa awamu. Baya zaidi wanafunzi wa darasa moja matokeo yanakuja ya wanafunzi watatu na wengine wanafutiwa kabisa. Sasa mimi sitaki niende mbali zaidi, ila ukweli ni kwamba Baraza hili haliko sawa. Mkubali mkatae, pale pana tatizo kubwa sana. Serikali ituambie kuna nini pale; inakuwaje watu wanafutiwa matokeo na wanaofaulu wengine hawajui kuandika majina yao?

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda na biashara; naomba kwa dhati kabisa niipongeze Serikali kwa

kuanzisha Sheria ya Ubia Katika Sekta Binafsi na Serikali *(PPP),* ambayo ilipitishwa na Bunge hili mwaka 2010. Kwa kuzingatia kuwa mfumo huu tulielezwa kwamba utaipunguzia kazi Serikali na kuifanya iweze kuzingatia vipaumbe vingine, lakini bado vipaumbele vyetu havijabadilika; kwa nini?

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka jana na ya mwaka huu hazina tofauti. Je, kuwepo na Sheria hii na utumikaji wake kuna tofauti gani? Tumekuwa na viwanda na makampuni mengi ambayo kabla ya Sheria hii yalikuwa yakiendeshwa kwa ubia, ikiwemo Kiwanda cha Urafiki. Kiwanda hiki sasa naona ni muda mwafaka kubadili jina lake na tukiite kiwanda cha Chuma Chakavu maana kule ndani hakuna kitu zaidi ya *scrapers* tu kwani hata ule mtambo ambao Serikali ilitoa shilingi bilioni 27 haumo tena. Pamoja na mazuri mengi ya *PPP,* naomba Serikali itueleze ni hasara kiasi gani tumepata katika Kiwanda cha Urafiki.

**MHE. MOSES JOSEPH MACHALI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Halmashauri ya Mji wa Kasulu itaanza utendaji?

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ilishatangaza Kasulu kuwa Halmashauri ya Mji wa Kasulu tangu 2010. Leo inaelekea miaka miwili tangu kutangazwa kwa Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Ninaomba kujua kwa niaba ya Wananchi wa Kasulu ni lini eneo hilo litakuwa Halmashauri Kamili; yaani kuwa na Mkurugenzi wake, Wakuu wa Idara zote na Mameya wake? Kwa kifupi, Uongozi wake kamili na hivyo kuondoka mikononi mwa Halmashauri ya Wilaya

ya Kasulu na kuwezesha wananchi kupata huduma kwa ukaribu. Nnaomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kumteua *DC* wa Wilaya Mpya ya Buhigwe, ambayo ilikuwa sehemu ya Wilaya ya Kasulu. Ni wazi kuwa baadhi ya Madiwani wa Wilaya Mpya wanapaswa kwenda kuanzisha Halmashauri yao ya Buhigwe. Kwa mantiki hiyo ni wazi pande zote mbili zitapaswa kufanya chaguzi upya, yaani kupata Wenyeviti wa Halmashauri za Kasulu na Buhigwe baada ya kugawanyika. Nataka kupata Kauli ya Serikali juu ya lini Madiwani wa Buhigwe wataanzisha Halmashauri yao na kuwaacha wale wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kufanya uchaguzi wa uongozi wake? Pia bila kusahau Halmashauri ya Mji wa Kasulu ambyo ni mpya na haijaanza.

Mheshimiwa Spika, sijaona mahali katika Hotuba ambapo pameeleza ni lini Halmashauri Mpya ya Mji wa Kasulu itaanza kujitegemea. Rejea majibu ya Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), alipoahidi kuwa, Hotuba itaeleza kila kitu. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi njema na utumishi wake uliotukuka kwa Taifa na Watanzania wote. Pia nampongeza Waziri wa Nchi,

Ofisi wa Waziri Mkuu (TAMISEMI), Naibu Mawaziri na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia umuhimu wa Sekta Binafsi katika kukuza uchumi wa chini yetu. Sekta Binafsi duniani kote ndiyo mtoa ajira kwa wananchi wengi na ndiyo mchangiaji mkubwa katika kuchochea ukuaji wa uchumi. Hata hivyo, naiomba Serikali iendelee kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta hii. Miundombinu ya umeme wa uhakika ni muhimu kwa Sekta Binafsi. Pia Taasisi za Fedha, yaani Mabenki na Mifuko mingine iwakopeshe wawekezaji wa ndani kwa riba nafuu isiyokuwa na masharti magumu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu uwekezaji hapa nchini. Kwa kuwa Serikali yetu imeweka Sera ya KILIMO KWANZA, nashauri tutafute wawekezaji wakubwa katika Sekta ya Kilimo. Kilimo kwa maana ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mifugo, uvuvi, misitu na ufugaji wa nyuki ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na maji ya maziwa, miti na kadhalika; hivyo ni lazima tuwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji. Nashauri Serikali yangu ihamasishe wawekezaji katika Sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niongelee kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi. Nashauri Serikali yetu ihakikishe vijana wote wa kike na wa kiume wanawezeshwa kiuchumi ili kuwaondolea kero za kimaisha. Serikali imejenga Vyuo vya *VETA* takriban kila Mkoa hapa nchini, naomba vijana wetu wakishamaliza

mafunzo yao wapewe vifaa na mitaji yenye masharti nafuu ili waanzishe vikundi vyao vya uzalishaji. Vile vile naomba watafutiwe masoko ya bidhaa zao watakazozalisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzalishaji unaofanywa katika Sekta ya Kilimo, viwanda vianzishwe ili kusindika mazao ya kilimo na kuyaongezea thamani ili kupata faida kubwa. Wakati umefika, Tanzania iondokane na utaratibu wa kuuza *unprocessed goods or products.* Viwanda vyote vya Wazalendo vifutiwe kodi ili viweze kuhimili ushindani na bidhaa zitokazo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Sekta ya Utalii. Sekta hii ni mojawapo ya Sekta ambayo ikikuzwa ipasavyo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi katika Taifa. Sekta ya Utalii ina *wider multiplier effects*; kwanza, hutoa ajira, pili, hutoa soko kwa wananchi mfano wakulima, wavuvi na kadhalika na tatu, huongeza mapato ya ndani na fedha za nje. Naishauri Serikali iweke mazingira wezeshi katika Sekta hii. Muhimu sana ni kuongeza amani na utulivu. Watalii hutembelea maeneo yenye amani na utulivu; vinginevyo, siyo rahisi kuvutia watalii. Uwepo wa umeme wa uhakika, miundombinu bora na ya kisasa ya barabara, viwanja vya ndege na taasisi za kifedha ni muhimu kwa Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea juu ya utendaji mbovu unaoendelea katika Halmashauri zetu nchini. Watendaji wengi katika Halmashauri zetu hawatimizi wajibu wao hasa katika kusimamia utii wa

sheria. Sheria zinazotungwa na Halmashauri zetu hazipewi umuhimu stahiki; hivyo, naomba utii wa Kanuni, Sheria Ndogo na Taratibu zilizowekwa na Halmashauri upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, akiwa ndiyo Mtendaji na Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali, siku hadi siku ahakikishe suala la ulinzi na usalama linazingatiwa. Wananchi wenye asili ya Tanzania Bara na Wakristo wa Madhehebu mbalimbali wanateswa huko Zanzibar. Naishauri Serikali ya Muungano ilinde mali na maisha ya wananchi wanaobaguliwa huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati wa kufanya majumuisho ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, asisitize umuhimu wa wananchi kuheshimu Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano, inayoruhusu Watanzania kuishi sehemu yoyote ya nchi yetu madhali hawavunji sheria.

Mheshimiiwa Spika, naunga mkono hoja

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametueleza katika Hotuba yake kwamba, suala la uvuvi tunatumia kiasi cha fedha kuzalisha vifaranga vya samaki, jambo ambalo litakuwa la kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, sikuona Serikali inafanya nini katika Uvuvi wa Bahari Kuu na pia mipango gani wa kuanzisha Uvuvi wa Bahari Kuu hasa kwa kuwa tuna samaki wengi na kila siku tunalalamika kwamba meli za

kigeni zinaiba samaki wetu. Je, ili tusiwe Tanzania ni joka la mdimu tuna utaratibu upi wa kuvua katika Bahari Kuu?

Mheshimiwa Spika, inasadikika kwamba kuna samaki aina ya vibua ambao wanavuliwa na meli za kigeni katika bahari yetu na wanapakiwa kwenye maboksi tunauziwa Watanzania kama vibua kutoka Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna vivutio vingi vya utalii lakini ukilinganisha kati ya nchi zetu za Afrika Mashariki za Kenya, Uganda na Tanzania, sisi tuko nyuma sana. Je, kwa nini au ni sababu gani Tanzania tunapokea watalii wachache lakini pia tunaingiza fedha kidogo za kigeni kwa faida ya nchi yetu? Naomba nipate majibu kwamba ni kwa nini tunapokea wageni kidogo wakati tuna vivutio vingi vya kitalii kulinganisha na wenzetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati; hivi sasa nchini kwetu pamoja na kwamba tumekuwa na madini kwa miaka mingi, lakini kwa miaka yote hiyo, wananchi wamekuwa duni na hawafaidiki kabisa na rasilimali ambazo zipo katika nchi yao. Wageni ndiyo ambao tunashuhudia kwamba wanakuja kuvuna rasilimani zetu (mali za Watanzania) na kwenda kujifaidisha wao na nchi zao.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Watanzania wanajua kwamba, tuna gesi nyingi ambayo ipo nchini na nchi nyingine duniani ambazo kuna mafuta na gesi imetokea kuwa na migogoro ya wenyewe kwa

wenyewe. Chanzo kinaonekana ni wahusika ambao ni wananchi kukosa mgao (maslahi), yatokanayo na kinachopatikana kutokana na Nishati hiyo. Kwa wasiwasi huo na kwa kuwa pia Taarifa ya Jopo la Wachumi Duniani inaonesha kwamba chanzo cha machafuko katika nchi zenye mafuta na gesi ni mgawanyo mbaya, pengine Serikali haitoi mgao kwa wananchi wao. Je, Serikali imejipanga vipi katika kugawana mapato yatakayotokana na gesi hii iliyokwisha gunduliwa ili na sisi tusiingie katika vurugu za wenyewe kwa wenyewe kama ilivyotokea kwa wenzetu?

Mheshimiwa Spika, Watu wa Pwani tuna usemi tunasema kwamba: “Kivuli cha mvumo kinawafaa walio mbali.” Sasa kwa masikitiko makubwa, naomba niseme kwamba, Tanzania tumekuwa mvumo, kivuli kinawafaa waliombali.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tuna rasilimali nyingi, mfano; madini, maeneo ya kitalii, rasilimali watu, gesi na kadhalika, lakini kwa bahati mbaya sana, pamoja na sura hiyo inayoonesha kwamba kumbe Tanzania ni tajiri, lakini wananchi wengi sana ni maskini wa kutupwa na tunashuhudia wageni wakichukua rasilimali zetu na kwenda kufaidisha nchi zao.

Mheshimiwa Spika, hata matumizi ya rasilimali watu bado hatujatoa kipaumbele. Inashangaza sana kwamba, kutokana na mtikisiko wa kiuchumi duniani ambao hata nchi kubwa Marekani nayo uchumi wao umeyumba sana. Marekani katika kuhakikisha

kwamba wanajenga upya uchumi wao na kuimarisha, wametafuta ni wapi wanaweza kupata rasilimali itakayosaidia kujenga uchumi wao na wamemwona Profesa Lipumba wa Tanzania anao uwezo mkubwa wa kuwasaidia kuinua uchumi wao, wamemfuata ili akawasaidie kujenga uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, Lipumba ni Mtanzania, ni Mnyamwezi wa Tabora, hahitaji kulipwa kwa dola kushauri na kufanya upembuzi yakinifu ndani ya Tanzania katika kuisaidia Tanzania yak, lakini swali ni je, Serikali ya CCM imemtumia vipi Mchumi huyu tuliyenae hapa kwetu kuishauri Serikali kujenga uchumi wetu?

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM imejifungia katika chumba na mawazo yale yale ya mwaka 47 na haitaki kutoka nje kupata mawazo ya Watanzania wengine. Naiomba Serikali itumie rasilimali zote tulizonazo hapa hapa nchini kwa faida ya wananchi wetu wote na kwa kuwa mjenga nchi ni mwananchi, watumieni wananchi wenyewe ili wajenge nchi yao na wala isiwe kwa ubaguzi wa kiitikadi; hatutafika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOSHI SELEMANI KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwasilisha Bajeti ambayo inagusa maeneo ya walala hoi walio wengi katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kilimo pekee ndicho kitakachobadili maisha ya Watanzania walio wengi lakini hakuna mpango mkakati wa vitendo

unaotekelezwa na Serikali. Ili kilimo kiweze kufanya kazi, lazima tupeleke zana za kurahisisha kilimo kwa kuwawezesha wakulima waweze kupata zana zingine za kuwsaidia waweze kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kupeleka umeme vijijini, utakaowasaidia wakulima hawa kusindika mazao yanayozalishwa na wakulima hao ili mazao hayo yapate thamani ya juu. Sambamba na hilo, tuongeze wataalamu wa kusimamia kilimo ili wakulima wazalishe mazao yenye ubora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi; eneo ambalo Serikali inatakiwa ilifanyiwe kazi kwa ukaribu zaidi ni kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji. Kuna bomu kubwa ambalo litasababisha mapigano kati ya wakulima na wafugaji. Ninaishauri Serikali ishughulikie kwa haraka kutenga maeneo ya wafugaji na ya wakulima.

Mheshimwa Spika, kuna vijiji vingi vilivyopo Mpanda havina huduma ya maji, tunaomba Serikali iangalie kwa upana wake tuwasaidie Wananchi wa Vijiji vya Igagala, Vikonge, Mpembe, Kamsanga, Ilebula, Kasekese, Katuma na Kabungu; hawana maji kabisa Serikali iwasaidie kupata huduma hii.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa sana kati ya wakulima na Hifadhi zinazozunguka maeneo yafuatayo: Kijiji cha Kabage, Kijiji cha Kasekese, Kapalamsenga, Sibwesa, Kungwi na Kaseganyama. Maeneo haya yana mgogoro mkubwa sana wa kugombea ardhi. Naishauri Serikali wakae na wafikirie

kwa ukaribu kurudia mipaka ili wananchi wapate maeneo ya kufanyia kazi.

Eneo lingine lenye mgogoro ni la Kijiji cha Vikonge, Kitongoji cha Kalukilo au Mnyamasi. Kitongoji hiki kilianzishwa mwaka 1995 na kupata hadhi zote ikiwemo na Uongozi unaotambuliwa na Serikali. Cha kushangaza, sasa wananchi hawa wanatakiwa wahame ili kuruhusu upanuzi wa Hifadhi ya Tongwe. Naiomba Serikali iangalie umuhimu wa mfumo wa kurejesha ardhi ya wanakitongoji hao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT SENKAMBA KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi, naipongeza Serikali ya CCM kwa nia yake njema ya kuhakikisha kwamba, wananchi wanawezeshwa kiuchumi. Kwa bahati mbaya sana, pamoja na nia njema hii, haiwafikii wananchi wa maeneo yote ya Tanzania na hasa walio vijijini ambao ndiyo walio wengi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(Mwananchi Empowerment Fund),* umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 7.3

kwa wajasiriamali 7,187 katika mikoa tisa na Rukwa ikiwa miongoni.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kalambo lililoko Mkoa wa Rukwa na sehemu yote ni vijiji. Nami nikiwa napita vijiji vyote sijapata bahati ya kuona wananchi waliofaidika na mpango huu; hivyo, nashauri mipango mizuri kama hii sisi Wabunge tukiwa wadau ni vizuri tukashirikishwa ili nia njema ikawafikie walengwa.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kujiunga na *SACCOS* na *Vicoba* imekuwa ikichukuliwa kwa *assumption* ambayo siyo sahihi kwa kuwasihi Waheshimiwa Wabunge watoe hamasa lakini bila kuzingatia kwamba ni suala la kitaalamu, linalohitaji kuelezwa kwa ufasaha na weledi uliobobea.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimekuwa muumini mkubwa wa uanzishaji wa vikundi vya uzalishaji mali lakini siyo mtaalamu wa uanzishaji wa madarasa ya hamasa. Naishauri Serikali ihakikishe kwamba, elimu ya ujasiriamali inaenezwa mikoa yote na hususan mikoa yote ya pembezoni ili waweze kuchangamkia fursa za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ukimnyima mwananchi elimu ya ujasiriamali halafu ukamwambia eti hayuko tayari kujiunga na vikundi vya uzalishaji mali, utakuwa unamwonea.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine nalazimika kulisemea hili baada ya ahadi iliyotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwamba, mgogoro

baina ya Wananchi wa Kijiji cha Katapulo na NARCO, ungepata ufumbuzi katika bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilituma Watendaji wake kuja kufuatilia mgogoro huu na kwa bahati mbaya sana, Watendaji walipofika walishindwa hata kubaini mipaka kati ya Kijiji na NARCO.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi wananchi wanachodai ni kwamba, ardhi hiyo waliitoa bure kwa Serikali na bahati nzuri walikuwa wameruhusiwa kuendelea kulima kwenye ardhi hiyo. Baada ya kuamua kubinafsisha baadhi ya mashamba yake, walifanya makosa ya kubinafsisha kwa kukodisha hata ardhi ambayo siyo yao kwani haijawahi kuwa ya kwao, ile ardhi ilichukuliwa kwa kufuata Sheria, fidia stahili ilitolewa kwa vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa nia yake njema ya kuhakikisha kwamba, ardhi inapimwa na Hati za Kimila zinatolewa na zitumike kama Hati za Kisheria katika kupata mikopo katika Taasisi za Kifedha. Naishauri Serikali ihakikishe zoezi hili linafanyika kwa kasi ili kuleta maendeleo ya haraka kwa kwenda kupima na kubaini matumizi bora ya ardhi kwa Wilaya Mpya ya Kalambo na Jimbo la Kalambo.

**MHE. PAULINE PHILIPO GEKUL:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa vijiji na vitongoji vingi vipo wazi, Wakurugenzi wamekuwa wakijitetea kuwa hawana fedha, *OC* ni ndogo. Ofisi ya Waziri Mkuu, itoe kauli ya haraka kwa Halmashauri na maeneo yote ambayo yapo wazi uchaguzi uitishwe.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kilio cha muda mrefu kwa Wabunge wa Viti Maalum kuendelea kudharaulika kwa kutoingia kwenye Kamati za Fedha za Halmashauri. Nini kinachosababisha Ofisi ya Waziri Mkuu isitoe tamko juu ya hili? Ameshatuahidi kuwa atalishughulikia mbona bado? Wenzetu Wanawake wa Kiganda wanapewa shilingi milioni kumi kwa mwaka kuhudumia Wilaya wanazozisimamia, sisi tunasimamia Mikoa hata kwenye mgao wa mafuta tunapewa sawa na wale wa Majimbo. Tunaomba kauli ya Waziri Mkuu katika hili.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na zoezi la kutupiana mpira kati ya TAMISEMI na Wizara mbalimbali kuhusu Fedha za Maendeleo za Elimu na Afya. Fedha za MMES na MMEM zinazopelekwa Halmashauri hazitumiki ipasavyo; mfano, zile za msingi hadi leo hakuna majengo mapya ni yale yale ya Enzi za Mwalimu. Nashauri Fedha za Maendeleo kwa Shule za Msingi na Sekondari na nyumba za walimu zijengwe.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa MMAM 2007 ulianzishwa chini ya Sera ya Afya iliyolenga kujenga Zahanati kila Kijiji na Vituo vya Afya kila Kata. Nashauri kuwa, iitishwe Ripoti kwa nchi nzima ya fedha hizo za wafadhili tuone mafanikio yake; vinginevyo, 2017 itafika wakati Zahahati nyingi zitakuwa hazijajengwa; ni vizuri Serikali ikapitia tena utekelezaji wa Sera ya Afya ya Msingi, bado hali siyo shwari.

Mheshimiwa Spika, hakuna sababu ya msingi ya Wizara ya Elimu kupanga fedha za rada katika mikoa mitatu (Mwanza, Morogoro na Dar es Salaam). Nashauri fedha hizo zipelekwe kwenye ujenzi wa nyumba za walimu nchi nzima. Kupeleka fedha hizo kwenye vitabu ni kukaribisha ufisadi. Wale waliosababisha Taifa likaingia hasara kwenye zoezi zima la ununuzi wa rada wameshughulikiwa au kuwajibishwa kwa kiasi gani?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 Pato halisi la Taifa limeshuka kwa asilimia 0.6 ukilinganisha na mwaka 2010, ambapo mwaka 2010 ilikuwa 7.0 na mwaka 2011 ni asilimia 6.4. Suala kubwa lililoelezwa na sababu zilizotolewa ni ukame na umeme.

Mheshimiwa Spika, sioni kama tatizo hilo linatosha, ukweli ni mipangilio mibaya ya kiuchumi ndiyo iliyosababisha hali hii.

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu unategemea sana kilimo; hivi kuchelewa kwa mbolea kufika kwa wakati kwa wakulima ni tatizo la ukame na umeme?

Mheshimiwa Spika, swala la kuchelewa kwa mbolea na pembejeo kutopatikana kwa wakati imekuwa tatizo kubwa sana. Mbolea inapatikana wakati wa palizi kama siyo wakati wa kuvuna, kwa namna hii hakuna kitu kitakachopatikana, matokeo yake watu watakosa mavuno na kubaki na madeni ya mikopo waliyokopa kuendesha shughuli za kilimo.

Swala hapa siyo ukame wala umeme ni mipangilio mibaya ya Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeajiri Maafisa Ugani kibao lakini waulize nini kinafanyika kama si kusubiri mishahara tu mwisho wa mwezi, wengi wao hawajui la kufanya kama wanajua hawataki kutimiza wajibu wao. Hivi kweli kuna Afisa Ugani yupi anayepita vijijini na kuelekeza wananchi nini cha kufanya kuhusu kilimo bora? Namna ya kupanda, kupata mbegu bora na kadhalika, pia kama wangeelimishwa vyema wangepanda mazao yanayovumilia ukame na wangelivuna; hili lingefanyika swala la ukame lingekuwa halipo wala la umeme.

Mheshimiwa Spika, Maafisa wa Kilimo wa Wilaya saa zote wako ofisini na hata Mbunge ukienda kwenye ziara ukawaalika visingizio vya kazi nyingi ofisini, bado wanajivuta wanataka posho, wakati hiyo ni kazi yao. Ukiwauliza habari za Kata wanasema hawana mafuta, Mbunge ukiwa na mafuta ya kwenda nao wao wanatoa visingizio. Je, kazi ya Afisa Kilimo inafanyikia ofisini au ni shambani? Je, hii nayo ni ukame au umeme? Swala zima hapa ni uwajibikaji na nani amuwajibishe nani?

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mikakati ya zao gani lilimwe kwa wakati gani na linachukua muda gani: Kutokana na hali ya tabia ya nchi kubadilika, bila mikakati ya makusudi ya kubadilisha tamaduni zetu za majira ya kilimo, hatuwezi kufikia tunakotaka kwenda na kilimo. Wakulima wanahitaji elimu ya badiliko la

majira na misimu; haya yakifanyika yatabadilisha lugha ya ukame na umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali kutoa miradi mikubwa kwa upendeleo hasa kwa Ukanda wa Kusini. Zimetengwa shilingi bilioni 7.177 kwa ajili ya kilimo na umwagiliaji kwa Ukanda wa Kusini na hata mwaka jana fedha zilitengwa. Ni vyema Kasungura haka tukagawane sawa; lini Ukanda wa Ziwa utatengewa fedha za Miradi ya Kilimo ukizingatia Ukanda huo hasa Kagera mvua ni Januari mpaka Desemba, hakuna ardhi yenye mabonde kama Ukanda wa Ziwa mfano Mkoa wa Kagera hasa Misenyi hatujawahi kuwa na ukame; kwa nini Serikali isielekeze nguvu ya kilimo kama vile kutupa pembejeo, matrekta, ruzuku na mbolea na kadhalika? Serikali lazima igawe keki vizuri, ukifuatilia utaona jinsi ambavyo wengine wanasahaulika.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Uchumi ni mibaya; Kahawa ni Zao Kuu la Biashara la Mkoa wa Kagera, lakini linapoteza thamani kwa wakulima kila kukicha wanaambiwa leo Soko la Dunia mambo ni mazuri. Mwaka 2011 kahawa mauzo ya nje iliongezeka kwa asilimia 40.3 kufikia Dola za Kimarekani 146.6 milioni, ukilinganisha na 2010 Dola za Kimarekani 101.6 milioni. Mauzo ya tani mwaka wa 2011 ni dola 3,654.9 ukilinganisha 2,853.1 ya mwaka 2010. Kahawa iliyouzwa nje mwaka 2010 na kahawa iliyouzwa nje mwaka 2011 ni tani 39,000 ukilinganisha na tani 35,600 mwaka 2010; ni ongezeko la asilimia 9.5. Hivi kweli Serikali inaweza kunielewesha kwa nini imeshusha bei ya Zao la Kahawa; sasa hivi Nkenge kilo moja ni Sh.

1,100 wakati mwaka jana iliuzwa kwa Sh. 1,350 lakini Waganda wananunua kilo moja kwa wakulima Sh. 1,500 na Uganda wanauza soko gani? Naomba Serikali ije na majibu wakati inajibu hoja hizi kuhusu bei ya uhakika ya kahawa. Ni ajabu sana wakati bei imepanda kwenye Soko la Dunia ninyi mnashusha bei kwa wakulima wenu.

Mheshimiwa Spika, kama kweli Wabunge tupo ili kuishauri Serikali ifanye vyema, basi naomba wakubali ushauri; kuna nafasi watu wanapewa kuliko uwezo wao, matokeo yake wanaelemewa na wanasababisha malengo ya maendeleo kutofikiwa. Lazima Serikali itoe nafasi kwa watu kulingana na uwezo wao, Serikali lazima ijiwekee vigezo vya kugawa nafasi nyeti za Uongozi si kila mtu anaweza. Nafasi zingine zinahitaji weledi wa kutosha, miradi ya kibiashara na hata kutafuta wafadhili au wawekezaji. Ninasikitika kusema nafasi zingine si za kutoa tu bali uwezo ni muhimu zaidi.

Mheshimiwa Spika, natoa angalizo, Watanzania wa leo wako makini sana; hivyo, wanategemea Serikali yao iwe makini pia. Unapokuwa na Mtendaji asiye na weledi wa kutosha katika kazi aliyopewa unategemea kukuza uchumi gani katika eneo husika? Mfano, *DAS* kama hana uwezo wa kutosha kumudu kazi hiyo unategemea nini katika Wilaya husika; hii ni pamoja na *DC, RAS* na kadhalika? Nafasi hizi ziwe na vigezo, bila hivyo swala la maendeleo litakuwa historia na wimbo wa kila siku ni kufukuzana kazi kila siku, maana kama Serikali itafanya bila kujali mtazamo wa Watanzania wa leo itakuwa aibu kila siku maana hawatanyamaza.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na vuguvugu la Madaktari kugoma, kwa sababu ya kudai malipo makubwa kuliko uwezo wa Serikali, kitu ambacho hata wao wanajua ila kwa sababu zisizojulikana wanaitikisa Serikali kuona kama kiberiti kimejaa. Kwa sababu hawana sababu ya kutosha kugoma.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kuwapongeza *Medical Assistant Officers* kwa kutojiunga katika mgomo huo unaoanzishwa na *Medical Officers,* japo kazi zao ni hizo hizo na siyo ajabu *Medical Assistants* wanafanya kazi kubwa kuliko wao. Ningeliwashangaa kama wangelijiunga kwa sababu wao hawawaiti Madaktari na kwa hili wameliona basi hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize hivi hapa nchini tuna *Medical Officers* wangapi na *Assistant Medical Officers* wangapi? Muda wa masomo ya watu hawa wawili ni muda gani? Katika utoaji wa huduma zao za kila siku kuna tofauti gani?

Mheshimiwa Spika, *Mediacl Doctors* ni kama asilimia kumi ya Madaktari wote Tanzania. *Assistant Medical Officers* ni kama asilimia 90. Muda wa masomo kwa watu hawa wote ni miaka mitano chuoni lakini *Assistant Medical Officer* anakuwa ameshafanya kazi miaka miwili au mitatu kabla hajajiunga na Chuo Kikuu cha Udaktari na pia kabla ya kazi anakuwa amepitia Chuo cha *Medical Assistant* miaka miwili au mitatu ndiyo anakwenda Chuo Kikuu. Huyu *Medical Doc*tor anakwenda chuo moja kwa moja akimaliza

Kidato cha Sita anasoma miaka mitano kama kawaida, baada ya hapo anakwenda *Internship* mwaka mmoja ambayo huyu *Assistant Medical Officer* hahitaji maana yeye kabla ya chuo ameshafanya kazi miaka miwili au mitatu.

Mheshimiwa Spika, Mikoa mingapi ina *Medical Officers* na wapo wangapi? Mikoani *Medical Doctors* ni wachache labda mkoa mzima unao wawili au watatu, waliobaki wote ni *Assistant Medical Officers* na Watendaji au Wafanyakazi wakubwa ni *Assistant Medical Officers.*

Ndugu zangu Watanzania, wanaotutibu kila siku ni *Assistant Medical Officers,* maana *Medical Officers* Wilayani hawapo, lakini watu hawa wote ni sawa, majina tu ndiyo yanatofautiana. Mfumo tuliouweka ndiyo unasababisha wengine kuwa jeuri na kuwanyanyapaa wenzao wakati kazi kubwa wanafanya *Assitant Medical Officers*. Ninawashauri Madaktari wasijisumbue kuwashawishi wengine, tena wanaopita kushawishi mgomo hawajaajiriwa na Serikali, likitokea la kutokea wao watendelea na kazi zao.

Mheshimiwa Spika, naomba niongee na Watanzania wasitishike na swala hili, tulio wengi kila siku tunahudumiwa na waganga ambao hawapo kwenye mgomo na hivyo wasiogope, Serikali hii inaelewa kinachoendelea. Ninawasihi sana Madaktari wafikirie tena, kwa kuwa kazi yao siyo ya kawaida ni ya wito, bora wasitishe malumbano walihurumie Taifa lao, kama kweli hawajachochewa na mtu yeyote maana

Serikali imejitahidi. Nashauri Serikali itazame tena huu mfumo kama una maana yoyote maana hawa kazi zao za kila siku ni zile zile bali majina ndiyo tofauti, tena kuna *Assistant Medical Officers* wanawafundisha kazi *Medical Officers;* Mungu awasaidie.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuifanya Tanzania kuwa Njia Kuu ya Biashara ya Usafirishaji kwa nchi jirani kama njia ya kuongeza pato, itakuwa ndoto kama yafuatayo hayatabadilika:-

Mheshimiwa Spika, swala la rushwa babarabani limekuwa sugu, kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma kuna vituo kama 15 vyote vinapiga mkono lori moja. Hivi mtu anayekwenda Burudi akisimama mara kumi na tano Dar es Salaam mpaka Dodoma, Burundi atafika lini? Kwa nini tusiweke utaratibu Trafiki wakae kati ya Wilaya na Wilaya mpakani au kwenye mizani? Hivi *checking* za kila kilomita 20 ni nini kinakaguliwa kama siyo uonevu na rushwa ni nini? Adha hii haivumiliki kibiashara.

Mheshimiwa Spika, ina maana swala la rushwa barabarani limeshindikana? Barabara ni nzuri, zimejengwa, tunaishukuru Serikali, lakini hazipitiki kwa wafanyabishara hasa wenye malori, mabasi na rushwa yao ni ya wazi wazi; hivi kweli Serikali haioni kuwa hii ni kero kubwa sana?

Mheshimiwa Spika, kama kweli Serikali imekusudia kufufua bandari zote nchini kama ilivyo kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa ni vyema

ikashughulikia tatizo hili kwa kina maana barabara hazipitiki kwa rushwa. Swala hili halihitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, kama kuna ahadi ya ongezeko la mishahara wapewe ili barabara zipitike kwa amani.

Mheshimiwa Spika, mzalishaji mkuu wa nchi hii ni mwanamke lakini mwanamke huyu hapati maji safi na salama na siyo hilo tu hata afya ya mwanamke huzorota kwa uchovu mkubwa anaoupata; maeneo mengine mwanamke hutembea mwendo mrefu kwenda kutafuta maji. Sehemu zingine mama huondoka asubuhi na hurudi jioni; je, huyu mama atazalisha saa ngapi?

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuna ahadi ya kuhakikisha nchi nzima tunapata maji safi na salama. Suala hili lingetekelezwa wanawake wangepata muda mrefu wa kuzalisha na hivyo uchumi ungelikua.

Mheshimiwa Spika, kuna Mradi wa Vijiji Kumi kila Halmashauri vilivyo kwenye Mpango wa *World Bank;* sehemu nyingi *World Bank* wamemaliza lakini wananchi hawana hela ya kuchangia, michango yao inasuasua; hivyo basi kwa nini Serikali isiwakopeshe wakawa wanalipia kidogo kidogo mtu anapokuja kuchota maji mpaka wakamaliza deni kuliko sasa mitambo itachakaa kwa kutotumika na itakuwa hasara kubwa?

Mheshimiwa Spika, ukimwezesha mwanamke umeliwezesha Taifa zima. Mikopo iliyotajwa kupitia

Halmshauri ni shilingi milioni 88; hizi ni za Halmashauri au Tanzania nzima? Kama ni Tanzania nzima huo ni utani, wanawake ndiyo wazalishaji wakubwa kweli katika kiwango hiki tunaweza kusingizia umeme na ukame?

Mheshimiwa Spika, sikubaliani na utaratibu huu kabisa, mimi naomba kushauri; kuna bilioni mbili zinazotolewa kwa Benki ya Wanawake wakati Benki hii haitoi huduma kwa Wanawake wote, bali ni Wanawake wa Dar es Salaam tu ndiyo wanaofaidi Benki hiyo. Je, kwa nini tusiite Benki ya Wanawake wa Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, nashauri kama ni Benki ya Wanawake wote, wanufaike kama ilivyokuwa imekusudiwa kuwahudumia Wanawake wote basi ifungue dirisha la kuhudumia wateja wake wakubwa ambao ni Wanawake kupitia *NMB* kwa kuwa Benki hii ipo kila Wilaya nchi nzima. Bila hivyo sikubali hela hizi za Serikali kwenda Benki ya Wanawake kwa sababu Benki hii haijatimiza ahadi iliyoombea fedha hizi, ukizingatia wanawake wengi zaidi wako vijijini na huko huduma za kibenki ni chache, mjini wao wana njia nyingi za kufikia mikopo na hata kimaisha wao ni nafuu. Bado nguvu nyingi inatumika kuwawezesha wanawake waliopo mijini. Naomba maelezo ya kutosha kutoka Serikalini kuhusu Benki hii ya Wanawake lini mtawafikia Wanawake wa Vijijini na Miji mingine ambayo ipo nje ya Dar es Salaam ili Wanawake wote wa Tanzania wanufaike.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu elimu, viwango vya ukuaji katika utoaji wa huduma za elimu ni mdogo sana, na

hii inasababishwa na mipango yetu ya elimu kutokaa sawa.

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini tunaimba wimbo huu siku zote na Serikali haichukui hatua hata kama tafiti zimesema? Mfano, utafiti uliofanyika 2010 chini ya *MOEVT PETS* ulionesha yafuatayo:-

Lazima iwepo posho maalumu ya walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. *Allowance* hizo ziangalie eneo na eneo, kama shule zilizo milimani, sehemu za ndani ndani kabisa ambapo hata miundombinu ya jamii ni shida, shule za visiwani na kadhalika; walishauri vivutio kama *hardship allowance, promotion* za haraka, kupandishwa mishahara haraka, *transport allowance, housing allowance, special study leave* na *training opportunities* na fursa hizi zitolewe kulingana na mazingira ya sehemu mfanyakazi alipo, itaongeza mvuto kwa walimu na watafika vituoni mwao watakakopangiwa kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie yale yaliyokuwa imeyakubali kama walivyo wenzetu wa Uganda, Malawi, Lesotho na Mozambique, tutapunguza kero hii kwa kiasi kikubwa na walimu wataomba kwenda vijijini wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Serikali iwe na Mikataba na kila mwanafunzi anayejiunga na Chuo Kikuu na kupata mkopo, akubali kuwa kwa kipindi cha miaka mitano ataitumikia Serikali popote itakapompeleka na baada ya hapo awe huru kwenda

kokote anakotaka, la sivyo kila siku tutafundisha walimu na bado wataondoka hawana kibano. Kwa misingi hiyo ni ngumu sana kufanikisha maendeleo ya elimu.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu (S.W.), kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuandika machache kuchangia Bajeti hii kwa maslahi yetu na mustakabali mwema wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, amani, utulivu na maelewano ni jambo la kwanza na muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote duniani. Mfano mzuri wa hapa kwetu Tanzania ni utulivu na maelewano yaliyopelekea kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Ni mwaka mmoja tu sasa tokea Serikali hii iundwe na pato la wastani la Wananchi wa Zanzibar limepanda kutoka Sh. 782,000 kwa mwaka na kufikia Sh. 884,000. Hii imetokana na kuongezeka kwa bei ya Zao la Karafuu kutoka Sh. 3,000 kwa kilo hadi Sh. 15,000 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa letu. Kilimo kinatoa ajira za kujikimu kimaisha kwa robo tatu ya Watanzania wote (asilimia 75). Kwa mantiki hiyo ni lazima umuhimu wa pekee uwekwe katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyotengwa haikidhi haja ya KILIMO KWANZA. Hakuna fursa kwa wakulima wadogo wadogo; mikopo ya fedha, pembejeo, matrekta na zana za kilimo haziwafikii wakulima wadogo. Wapewe mbegu bora na mafunzo ili waweze kuvuna magunia 30 – 35 kwa ekari moja badala ya

magunia mawili au matatu wanayovuna kwa ekari moja. Wajengewe maghala ili waweze kuuza mpunga, mahindi, korosho na kadhalika, kwa bei ya soko na siyo hivi sasa wanauza kwa *throw away price.* Vile vile wakopeshwe mashine za kukobolea ili kuongeza thamani ya mazao yao.

Mheshimiwa Spika, asilimia 42 ya watoto wenye umri wa miaka mitano na kushuka wana utapiamlo. Kuwawezesha wakulima wadogo wadogo, kutasaidia kupunguza tatizo la utapiamlo, kujenga nguvu kazi imara na kuwa na Taifa lenye watu wenye afya njema.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza mfumko wa bei ni lazima tuongeze uzalishaji hasa wa chakula. Watanzania wanatumia asilimia 50 ya mapato yao kwa ajili ya chakula. Uongezaji wa kuzalisha ni lazima uende sambamba na uimarishwaji wa miundombinu ya uchukuzi, bandari, reli na barabara.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kupunguza mfumko wa bei na kufikia tarakimu moja *(single digit)*, ifikapo Desemba 2012. Kwa miezi mitano (Januari – Mei 2012), mfumko wa bei umepungua kwa asilimia moja na nusu tu. Kwa mwenendo huu wa kusuasua wa kupungua kwa mfumko wa bei, itachukua miaka miwili na nusu mfumko wa bei kupungua na kufikia tarakimu moja *(single digit).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano, Mafuta na Gesi na mgao wa mapato: Suala la mafuta na gesi limekuwa likizungumzwa Bungeni tokea 2006 ili kupatiwa ufumbuzi kero hii. Kwa bahati mbaya sana,

imekuwa ni mikakati tu, uchambuzi, michanganuo, lakini uamuzi bado haujafikiwa.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa mafuta na gesi yatolewe kwenye Mambo ya Muungano ili kuweka ustawi ulio bora wa kiuchumi katika pande zote mbili za Muungano. Pia mgawanyo wa mapato asilimia 4.5 iliyopewa Zanzibar ni udhalilishaji. Wakati umefika sasa Zanzibar iachiwe ijitafutie misaada ya maendeleo kivyake. Hii itasaidia kujenga na kuimarisha Muungano, kwani Zanzibar pia itakuwa na afya ya kiuchumi.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na maelezo mazuri ya Serikali katika suala la uwekezaji, ukurasa wa 14 hadi 21, kipengele cha 31, lakini ninashindwa kuamini kwa kuwa ni tofatuti na hali halisi inayofanyika katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, mfano ni uwekezaji wa kilimo cha miwa unaotarajia kufanyika Jimboni kwangu Kasulu Vijijini katika Vijiji vya Kitanga, Kigadye, Nyarugusu na Mvungwe. Mpaka leo hii mimi Mbunge ambaye ndiye sauti ya wakulima hao sijashirikishwa; je, nitaamini vipi kuwa wananchi wameshirikishwa? Hili ni tatizio kubwa sana kwa Watendaji wetu katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii; kama Mwakilishi wa Kasulu Vijijini sikubaliani kabisa na Mikataba mibovu ambayo inatolewa nchini kote hasa Mkataba uliopitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na

Mwekezaji mwenye Kitalu cha Kagera Nkanda (Ranchi ya Kasulu), kwa sababu hakuna ushirikiano na wananchi; wananchi wanaozunguka Kitalu hicho hawajui chochote juu ya faida na hasara itakayopatikana kwa kusaini Mkataba huo; mbaya zaidi, hata mimi mwakilishi wao sikushirikishwa juu ya Mkataba huo; na kundi dogo la wawakilishi kupitia Mwenyekiti wa Halmashauri, Mkurugenzi na wenzake ndiyo wanaojua kila kitu.

Mheshimiwa Spika, itambulike kwamba, wananchi ndiyo wenye maliasili za nchi hii; iweje Mkurugenzi anaingia Mikataba bila wao kujua? Kimsingi ni kuwakosea na hawajatendewa haki hata kidogo. Hivyo basi, Mkataba huu siutambui na siyo haki kwa Watanzania wa Kasulu.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ni wa muda mrefu sana, miaka 30 ni mingi sana. Ukizingatia tunaishi kwenye dunia ya utandawazi, kila mwaka mambo yanabadilika; hivyo basi, Mkataba huu wa miaka 30 ni sawa na kupokonywa haki za vizazi vijavyo. Hali hii ni hatari na inaweza kusababisha kuwa na kizazi cha kulaumu na hasa kikachukua maamuzi yanayoweza kupelekea machafuko.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Serikali; ikiwa mambo yote haya yamefanyika na Mbunge ambaye ni kisemeo cha wananchi wa eneo husika sijahusishwa ni wazi kwamba, asilimia 99 ya Wakazi wa Jimbo la Kasulu hawajashirikishwa na hawajui kitu kuhusu Mkataba huu wenye usiri mkubwa kwa kulinda maslahi ya watu wachache. Naiomba Serikali Kuu, iingilie kati

suala hili ikiwa ni pamoja kubatilisha Mkataba huu ili ushiriki wa kupitia Mkataba huo uwe wazi kwa maslahi ya wananchi na vizazi vijavyo. Hii itakuwa ndiyo njia pekee ya kujenga mahusiano mazuri kati ya wananchi na mwekezaji wetu.

Mheshimiwa Spika, rasilimali za nchi hii ni mali ya wananchi na siyo kundi dogo kama ilivyofanyika Kasulu kupitika Mkataba huo mbovu. Pia wananchi wanayo haki ya kupata taarifa zinazohusu namna ambayo rasilimali zinatumika na wananufaika vipi. Kitu ambacho kimekiukwa waziwazi na Viongozi wachache wa Halmashuri dhidi ya Wananchi wa Kasulu na hasa Vijiji vya Kagera Nkanda na Mvinza, ikiwemo Kitongoji cha Katoto ambacho mpaka sasa wanalalamika sana kuhusu mpaka wa Kitongoji cha Kitara ambacho hakina uzio wowote ambao ungepunguza kero ya wananchi kuingia eneo la Hifadhi ya Wanyama Pori. Uwekezaji tunauhitaji sana kwa ajili ya ustawi wa wananchi ila uwe wenye tija.

**MHE. DKT. DAVID MCIWA MALLOLE:** Mheshimiwa Spika, napenda ku-*declare interest* kwa sababu mimi ni mmiliki wa Shule ya Sekondari City, Dodoma. Napenda kuchangia kuhusu Elimu (Hoja ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 42 na Hotuba ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ukurasa wa 28), kuhusu Elimu ya Msingi na chenji ya rada.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwa fedha yote ya rada, Sh. 72 bilioni itumike kununulia madawati na fenicha za ofisini, meza za walimu na makabati makubwa ya kutunzia vitabu na vifaa vingine vya

shule. Mbao zote za shule *(blackboards)* pia zikarabatiwe ili ziweze kuandikika vizuri.

Mheshimiwa Spika, vinunuliwe vitabu vichache vya masomo yote kwa ajili ya walimu. Walimu kwa kutumia ujuzi wao wa maandalio *(Schemes of Work* na *Lesson Plans),* pia ubunifu *(improvisation),* watatoa elimu nzuri kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, baadaye vinunuliwe vitabu vya watoto vya masomo yote.

Watoto wakiwa na madawati, watakaa vizuri na kusoma vizuri. Makabati yakiwepo, yatatumika kutunza vizuri vitabu vya shule ili visitupwe ovyo chini na kuharibika haraka.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya kompyuta pia yaanzishwe toka shule za awali hadi msingi na sekondari. Kompyuta ndogo yenye size ya *calculator (kindle)*, inaweza kuhifadhi zaidi ya vitabu 10,000, wakati Simu ya *Smart Card* inaweza kuhifadhi zaidi ya vitabu 1,000,000 bila ya kubeba vitabu vingi mkononi.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimeanza kutoa mafunzo ya kompyuta kwa walimu 920 (watu 25 kutoka kila Kata kwa Kata zote 37 za Dodoma Mjini). Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ipo tayari kuwapokea Walimu hawa 920 ili wafundishe kompyuta shule zetu za msingi za hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu isadie kutoa kompyuta za kutosha katika Shule zetu za

Msingi za Dodoma Mjini ili kutoa ajira na kusaida kuleta maendeleo ya kiteknolojia katika mafunzo ya elimu nchini. Mtindo wa vitabu vya magamba *(hard copy)* umepitwa na wakati. Badala yake mtindo wa kutunza vitabu kwa njia ya *soft copy*, yaani kwa njia ya kompyuta ndiyo mtindo mpya na safi, tena wa kimaendeleo zaidi kwa kizazi kipya cha sayansi na teknolojia ya kisasa ya Karne ya 21.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA:** Mheshimiwa Spika, ninataka kuchangia kwenye eneo la Sekta ya TEHAMA. Ni jambo la kufurahisha kusikia ya kuwa *video conferencing facilities* zimefungwa kwenye kila Sekretarieti ya Mkoa; hongereni sana. Kufunga mitambo hii ni jambo moja na matumizi ya mitambo hii ni jambo lingine. Ninashauri Mikoa ya Tanzania iendelee kuhamasishwa matumizi ya kutumia mitambo hii. *Video conference facilities* zina faida kubwa. Kwa kutumia mitambo hii, Watendaji wa Mikoa wanaweza kushiriki kwenye matukio (mikutano, mihadhara na *interviews*) mbalimbali bila ya wao kusafiri wenyewe kuhudhuria matukio hayo. Hii itapunguza gharama kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ili mradi huu uwe endelevu ni lazima kila mkoa utenge bajeti kwa ajili ya ununuzi wa *band width*; vinginevyo, mitambo hii haitofanya kazi. Pia ni muhimu kwa mikoa ijenge uwezo wa kutumia mitambo hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa vile Halmshauri zote zimeunganishwa kwenye mtandao wa TEHAMA, ni vyema kuendelea kuwahamasisha wafanyakazi watumie mtandao huo. Vinginevyo, faida ya kuwekeza kwenye mtambo huo haitaonekana.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MARIAM REUBEN KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kutoa mchango wangu wa maandishi kutokana na Hotuba nzuri aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, inayohusu Bajeti ya 2012 – 2013.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Masasi lina changamoto nyingi sana ambazo zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi kama vile Sekta ya Afya, Maji, Barabara, Kilimo na Elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuwazungumzia Wakulima wa Jimbo la Masasi. Wakulima hawa wamekuwa wakijishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara na mazao ya chakula. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, wakulima katika msimu huu wa kilimo hawakupata mvua za kutosha na hazikunyesha kwa wakati; hivyo, wakulima wamekosa kuvuna chakula cha kutosha kukidhi mahitaji ya kila kaya. Kwa ujumla, Jimbo hili litakuwa na upungufu mkubwa wa chakula; hivyo, naiomba Serikali ifanye tathmini haraka ili kubaini mahitaji yanayohitajika na Serikali kupeleka chakuka kulingana na mahitaji hayo kabla hazijatokea athari zozote.

Mheshimiwa Spika, Wakulima wa Masasi wanajihusisha pia na Kilimo cha Biashara kama Korosho, Ufuta na Mazao ya Mikunde. Korosho ni zao ambalo huingiza pato kwa Serikali na kuwawezesha wananchi kujikimu kimaisha. Katika msimu uliopita zao hili liliyumba sana kwa ajili ya kukosa wanunuzi wenye nia ya dhati kabisa ya kununua korosho. Je, Serikali hadi hivi sasa inachukua jitihada gani ili kuhakikisha kuwa msimu huu wa 2012 – 2013 wakulima hawapati adha kama ulivyojitokeza usumbufu mkubwa ili kuwarudishia imani wakulima wetu? Naomba Serikali ilifanyie kazi haraka kabla msimu haujaanza.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Afya, pamoja na matatizo makubwa sana ambayo nitayazungumzia wakati wa Bajeti ya Wizara ya Afya, naomba nizungumzie suala la Chuo cha Wasioona kilichopo Masasi, ambacho kwa zaidi ya miaka kumi hakina mwanafunzi yeyote na majengo yamekuwa yakiendelea kuharibika huku watumishi waliopo wakiendelea kulipwa mishahara bila kufanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sana Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliomba majengo haya yabadilishwe matumizi ili yatumike kama Sekondari ya Mwenge Mtapika ambayo ipo hapo hapo yalipo majengo hayo, lakini Wizara ilikataa kutoa majengo hayo na yanaendelea kuharibika sana. Pamoja na Halmashauri kuchukua jitihada hizo ili kunusuru majengo, mimi Mbunge wa Jimbo hilo nimejitahidi sana kuishauri Serikali ibadilishe matumizi ya majengo hayo ili kiwe Chuo cha Ufundi ambacho

kitajumuisha na jamii yenye ulemavu, lakini hadi sasa Wizara haichukui hatua yoyote.

Mheshimiwa Spika, haya ni matumizi mabaya ya rasilimali za Taifa na ni hujuma kubwa sana. Leo naleta ombi rasmi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, aridhie kutoa kibali cha kubadili matumizi ya majengo hayo ili yawe Chuo cha *VETA* kama Sera yetu inavyotaka kuanzisha Vyuo vya *VETA* kila Wilaya. Tafadhali sana, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie sana swala hili la kubadilisha matumizi ya majengo ya Chuo cha Wasioona na kuwa Chuo cha *VETA* ambacho kitachukua wanafunzi wa aina zote; walemavu na wasio walemavu, kwa manufaa ya nchi yetu na kuwawezesha vijana wetu kupata ujuzi ambao utawasaidia kujiajiri na kuondokana na umaskini. Tafadhali, naomba katika majumuisho nipate jibu lenye kunusuru majengo haya na kuleta tija kwa wananchi hasa vijana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mwaka huu ya Waziri Mkuu, inayohusiana na Bajeti ina upungufu wa maelezo yanayohusiana na nyumba na makazi kinyume na Hotuba ya mwaka 2011/12. Kutokana na upungufu huo, ninaomba katika Hotuba ya Waziri Mkuu ya Mwaka huu kiwemo kifungu hicho na badala yake kiwe kifungu cha 124 badala ya kifungu cha 123.

Mheshimiwa Spika, Nyumba na Makazi ni Sekta muhimu kwa maisha ya binadamu katika nchi yetu. Taasisi ya Serikali inayoshughulikia ujenzi wa nyumba ni Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC).*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa baada ya kufanya mabadiliko ya Uongozi chini ya Mkurugenzi Mkuu, Ndugu Mchechu, limedhihirisha kuleta maendeleo makubwa katika suala la ujenzi wa nyumba za kuuza na kukodisha.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili katika ufanisi wa utendaji wake limeongeza pato la pango kwa mwezi kutoka Aprili 2010 kuwa Sh. 2.9 bilioni na kufikia Sh. 4.9 bilioni wakati wa sasa. Hivyo ni hatua kubwa sana na hapo kuna ongezeko la shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Spika, uzoefu uliopo wa Mashirika ya Umma ni kupewa ruzuku kutoka Serikalini ambapo Shirika la Nyumba kwa hatua ya maendeleo ilifikia wao wanatoa mchango kwa Serikali. Kwa mwaka 2011/12, mchango wa Shirika kwa Serikali ni Sh. 11.47 bilioni na kwa mwaka wa 2012/13 wanategemea kuichangia Serikali Sh. 24.18 bilioni.

Mheshimiwa Spika, pia kutokana na maendeleo ya Shirika hilo, wanategemea pato la Shirika kuongezeka kutoka Sh. 44 bilioni kwa mwaka 2011/12 na kufikia Sh. 75.05 bilioni kwa mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio hayo, Shirika la Nyumba la Taifa pia linakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo mahitaji ya mabadiliko ya Sheria Na. 2

ya Mwaka 1990 iliyorekebishwa mwaka 2005 na ughali wa nyumba zinazouzwa na Shirika kutokana na Ongezeko la Kodi ya Thamani. Mfano, nyumba inayouzwa kwa Sh. 99.99 milioni bila ya *VAT,* ikiingizwa *VAT* itafikia Sh. 118,000 milioni.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iondoe *VAT* kwa nyumba za Shirika ili nyumba hizo ziwe bei nafuu na wananchi wawe na makazi yaliyo bora na kuhusu Sheria Na. 2 ya Mwaka 1999 ifanyiwe marekebisho ya haraka.

Mheshimiwa Spika, Utalii ni Sekta muhimu katika uchumi wa nchi yetu, unachangia asilimia 17.2 Pato la Taifa na unachukua asilimia 25 ya fedha za kigeni zinazopatikana na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, licha ya vivutio vilivyoko hapa nchini petu vya utalii, bado ujaji wa watalii ni mdogo ukilinganisha na Nchi ya Kenya ambayo haina vivutio vya kitalii kama hapa Tanzania; uingiaji wa watalii wa kigeni kwa mwaka 2010 kwa Tanzania ni 782,699 na Kenya 1,600,000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto nyingine za Sekta ya Utalii inazozikabili, pia ipo changamoto ya fedha kidogo za utangazaji wa utalii. Mfano hai mwaka 2010, Kenya ilitumia Dola za Kimarekani milioni 24 wakati Tanzania ilitumia Dola za Kimarekani milioni 2.78.

Mheshimiwa Spika, gharama za utangazaji wa kitalii nashauri zitoke katika Bajeti ya Serikali na siyo Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa kuishauri Wizara itoe

fedha, matokeo yake fedha za utangazaji zitakuwa kidogo. Mwaka huu utangazaji wa utalii kwa kupitia Bodi ya Utaliii ya Tanzania haizidi bilioni sita. Wakati fedha hiyo Kenya kwa mwaka 2010 ilitumia Sh. 36,000,000,000; sasa iweje leo Tanzania mwaka 2012/13 itatumia chini ya bilioni sita?

Mheshimiwa Spika, naomba suala hilo la fedha za utangazaji lizingatiwe. Ahsante.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la fedha za rada. Nchi yetu iliingia katika kashfa kubwa ya ufisadi katika ununuzi wa rada. Baada ya Serikali na Bunge la Uingereza kuingilia kati, Serikali ya Tanzania imerudishiwa shilingi bilioni 72.3 ili zitumike kuboresha Sekta ya Elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwanza, sikubaliani na jina ambalo Serikali ya Tanzania inazipa hela hizo zilizorudishwa baada ya kubainika ufisadi mkubwa. Serikali yetu inaziita fedha hizo kuwa ni chenji ya rada. Sote tunajua kuwa chenji ni fedha halali inayorudishwa unapofanya malipo halali, lakini katika suala la rada hakukuwa na malipo halali bali ni ufisadi uligubika suala zima. Sasa inakuwaje fedha hizi zinarudishwa baada ya amri ya Mahakama ziitwe chenji? Huku ni kujaribu kuficha uozo wa ununuzi wa rada na kuwahifadhi waliohusika ili wasichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, ninaitaka Serikali iwachukulie hatua za kisheria wote waliohusika na kashfa hii na pia fedha zote zilizorejeshwa zitumike katika Sekta ya Elimu iliyokubaliwa na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha za maendeleo kwa Mikoa na Halmashauri umeendelea kuwa si wa haki kwa mikoa ile ile ambayo iko nyuma kimaendeleo. Tumekuwa tukitaka Serikali ichukue hatua za makusudi, kwa kutenga fedha za kutosha kwa mikoa ambayo iko nyuma kimaendeleo, lakini cha kuchangaza Mikoa kama Singida, Lindi na Rukwa, ambayo iko nyuma kimaendeleo kila mwaka ndiyo inayoongoza kwa bajeti ndogo. Utaratibu huu unajenga matabaka ya kimaendeleo katika nchi yetu. Cha kusikitisha ni kwamba, fedha hizi pamoja na kuwa ni kidogo, haziendi zote na haziendi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, matumizi yasiyo ya lazima na yasiyo na tija yanayofanywa na Serikali, yameendelea kutafuna fedha za walipa kodi. Tunahitaji kuona utekelezaji na nia ya Serikali kudhibiti ama kuondoa matumizi ya magari ya kifahari kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameahidi katika Hotuba yake. Nchi zote majirani zetu wameacha kutumia magari ya kifahari Serikalini; Tanzania kuna nini? Imefika wakati sasa Viongozi wetu waache fahari zinazowaumiza wananchi na waweke maslahi ya wananchi kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijikite moja kwa katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua ukweli kwamba maji ni uhai, bado wananchi wengi nchini na hususan Jimbo la Mwibara, hawapati maji safi na salama. Ukame unazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kusababisha hata mito kukauka, visima vifupi vya asili kukauka na malambo/mabwawa. Jimboni kwangu kuna Miradi miwili tu kati ya kumi ya visima virefu vya Benki ya Dunia katika Wilaya ya Bunda. Nataka kujua ni kigezo gani kilitumika kwa kupata visima viwili tu. Aidha, nilishaomba Bungeni hapa kupanua uwezo wa pampu za maji za Kasahunga, Kibara na Isanju ili kuunganisha vijiji vingine lakini hadi leo hakuna kilichofanyika wakati pampu hizo ziko katika maji ya Ziwa Viktoria. Naomba kujua tatizo liko wapi? Aidha, nilishaomba pampu ya Kasahunga iwekewe umeme badala ya kuendelea kutumia dizeli kwani umeme umepita mita 200 tu.

Mheshimiwa Spika, umeme umepita Jimboni kwani kutoka Bunda kwenda Ukerewe, lakini ni vijiji vitatu tu katika vijiji 50 ndiyo vina umeme. Mwibara tunataka umeme, hatuwezi kukubali ardhi yetu itumie kuwapa watu wengine umeme wakati sisi hatuna umeme. Nimeomba mara kadhaa katika michango yangu mingi hapa Bungeni na pia nimeuliza swali na kujibwa fedha zitatengwa katika Bajeti hii. Naomba niambiwe kama kweli umeme tutapata Bajeti hii kwani Wanamwibara wanahitaji umeme na siyo porojo.

Mheshimiwa Spika, Barabara yetu ya Bunda – Kisorya – Nansio, tumeipigia kelele miaka yote ambapo Wabunge waliopita walifanya hivyo. Hii ni barabara ya kiuchumi kwa uchukuzi wa mazao ya pamba, samaki, matunda, biashara na safari za kijamii. Aidha, barabara hii inahusu viwanda vitatu vya kuchambua pamba na hivyo kuzalisha marobota mengi yanayosafirishwa na malori makubwa. Pia barabara yetu iko namba moja katika orodha ya barabara zilizoko katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010 kwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Mwibara tunataka lami na cha kushangaza sioni fedha iliyotengwa kwa ajili ya barabara yetu. Tunahitaji maelezo ya kina juu ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, ili kupambana na mfumko wa bei na njaa ya Mwibara ya kila mwaka, lazima Serikali ipanue wigo wa Miradi ya Kilimo cha Chakula. Katika Bajeti ni mabonde machache tu yalipata Miradi kama Mabonde ya Mto Wami, Ruvu, Kilombero na Rufiji. Naomba tuwe na Mradi Ziwa Victoria kwenye Bonde zuri la Vijiji vya Kabainja, Karukekere, Muranda na Nansimo Jimboni Mwibara. Maji ya Ziwa yana uhakika mkubwa. Wanamwibara tumechoka kuhemea chakula hasa kusubiri msaada wa chakula cha mahindi toka Rukwa, Ruvuma, Iringa na Mbeya. Mwibara tunaweza kujilisha wenyewe endapo tutapewa Miradi ya Kilimo kando kando ya Ziwa Victoria. Tunaomba majibu juu ya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati Jimboni hauridhishi kwani bado wananchi wanatembea zaidi ya kilomita kumi kutafuta

matibabu mathalani kutoka Kijiji cha Mchigondo hadi Igunda ni kilomita 13 ndani ya Kata moja. Hali hii haikubaliki; ni aibu, hata Makao Makuu ya Jimbo pale Mji wa Kibara hakuna Kituo cha Afya wala Zahanati. Nasema hii ni aibu na haikubaliki. Nashauri Serikali iwe na Mpango wa Operesheni ya Kujenga Zahanati kila Kijiji kwa kushirikisha nguvu za wananchi kama tulivyofanya katika kujenga shule za sekondari kila Kata na kila Kijiji Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake nzuri, japokuwa ina changamoto, pesa zilizotengwa mikoani ni kidogo hasa za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimechangia kwa kuongea lakini sikumaliza, hivyo nimeona bora niandike haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu, Mkoa wa Tanga pia kuna upungufu wa walimu wenye fani ya ufundi stadi katika Vyuo vya Ufundi. Pia kuna uhaba wa Vyuo vya Ufundi ambavyo vipo vitatu tu Mkoa wote wa Tanga; *VETA* - Tanga, Mnyuzi na *FDC* – Handeni. Mbali ya uchache wa vyuo, hao wanafunzi waliopo hawapati muda wa mafunzo kwa vitendo, ukizingatia Tanga viwanda vimefungwa kwa sera ya ubinafishaji.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itekeleze azma yake ya kujenga Vyuo vya Ufundi – *VETA* kila Wilaya ili kuwaandaa vijana kuweza kuwa na sifa za kuajiriwa lakini pia kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, namshukuru tena Waziri Mkuu, kwa kuona umuhimu wa kuongeza posho za Madiwani, lakini bado ningeomba angalau ifikie shilingi laki tano. Pia wafikiriwe Madiwani hao kwa siku zijazo badala ya kupewa posho wapewe mishahara.

Vile vile naiomba Serikali iwafikirie Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Jiji kwa mambo mawili; posho zao ziongezwe na wapewe mafunzo ili waweze kujua majukumu yao na kuyasimamia kwani wao ndiyo wenye watu huku chini.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo katika Idara nyingi katika Halmashauri zetu ambapo wafanyakazi wengi wakienda kuongeza ujuzi wanaporudi hawatendewi haki kwa sababu zifuatazo; hawaitambui elimu yao waliyoiongeza, wakirudi ofisini wanawarudisha kwenye Kata, hata kama wilayani wapo watu wenye *level* ya *advanced diploma,* wakati wenye *post graduate diploma* na *masters* wanapelekwa kwenye Kata. Hivi siyo haki kabisa, inapelekea watumishi wengi kuondoka kwa sababu ya kunyanyasika na kuacha Halmashauri kukosa Wataalamu mfano Maendeleo ya Jamii. Je, Wizara ina utaratibu gani juu ya hili kwani baadhi ya Wakuu wa Idara wanapanga wapendavyo na si kuangalia taaluma ya watumishi. Naomba Waziri akija kufanya majumuisho nipate ufafanuzi kwenye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba kuongelea ardhi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Hotuba yake ya Bajeti, ukurasa wa 34 alisema, nanukuu: "Ardhi ni rasilimali muhimu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini." Katika Jiji la Tanga tuna tatizo la ardhi hasa ukizingatia maeneo mengi yalikuwa Mashamba ya Mkonge. Katika Bunge la Aprili wakati wa Taarifa za Kamati tuliomba sana hasa Kamati ya Mashirka ya Umma *(POAC)* kuwa wamiliki wote wanyang'anywe mashamba hayo hasa wale walioyatelekeza na kuacha mapori tu, Serikali iyachukue na kuyagawa kwa wananchi kwani ardhi ni rasilimali muhimu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iharakishe mchakato huo wa kuyarudisha mashamba hayo kwenye miliki yao na kuyagawa kwa wananchi, kwani kwa taarifa za uhakika *Master Plan* ya Jiji inaonesha kuwa hairuhusiwi Jiji kuwa na *estate* kama hizo na mashamba hayo ya mkonge. Ambapo Halmashauri tumeshapitisha hati kumi za mashamba hayo yarudishwe Serikalini na tumeshapeleka kwa Mkuu wa Mkoa na pia Kikao cha Mkoa kimeshabariki. Tunaomba Wizara husika iharakishe mchakato huo hasa ukizingatia Wananchi wa Kitongoji cha Mkembe na Kijii cha Marungu wanateseka sana, kuna wawekezaji mchwara wanawasumbua sana wakazi hao.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa Wananchi hawa walikuwa wanafanya kazi kwenye mashamba ya mkonge tangu enzi za ukoloni kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mwekezaji huyo

anataka waondoke, watakwenda wapi na hawana hata pa kwenda; hivyo, naiomba Serikali ifanye haraka sana suala hili ni muhimu sana.  Ahsante.

**MHE. DEOGRATIAS ALOYS NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake yenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ni hodari sana kwa kuandaa Mipango mizuri na hata Bajeti nzuri lakini tatizo kubwa tulilonalo ni utekelezaji wa Mipango hiyo. Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ndiyo Serikali yenyewe – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. TAMISEMI ndiyo ina watendaji ambao wako karibu na wananchi katika utekelezaji wa Mipango mbalimbali ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuwawekea Mikataba ya Utendaji *(Performance Contracts)* watendaji hawa na kuwasimamia kikamilifu ili wafanye kazi yao vizuri ya kuwashauri na kuwaelekeza wananchi namna ya kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri na Watendaji sharti wabadilike kifikra waache mtindo wa *business as usual* kama kweli Serikali ipo *serious and committed* katika kuelekea Nchi ya Uchumi wa Kati *(Medium Income Economy).* Nchi ya Uchumi wa Kati ni nchi ambayo kilimo chake kimekuwa *mechanised*, ni nchi ambayo ina viwanda vya msingi *(semi industrialised),* ina *industrial base* ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, ni nchi ambayo watu wake wamefikia kiwango cha elimu ya hali ya juu na *continuous learning* kwa watu ni jambo la kawaida. Ni nchi ambayo ina miundombinu mizuri na umeme wa uhakika. Ni nchi ambayo wananchi wake wanapata maji safi.

Mheshimiwa Spika, kama tunaendelea na tabia ya uswahili, tabia ya kutowajibika na tukaendeleza rushwa, Nchi ya Uchumi wa Kati itaendelea kuwa ndoto tu. Mpango wa Miaka Mitano na ule wa Muda Mrefu *(The Tanzania Long Term Perspective Plan - LTPP)*, umetayarishwa vizuri. Tuweke mikakati ya utekelezaji na tuwe na Programu zitakazosaidia tufikie hiyo ndoto.

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI imekabidhiwa jukumu la kusimamia elimu ya msingi na ile ya sekondari. Uwekezaji katika *Human Capital* unaanzia kwenye *Primary* na *Secondary Schools,* hatufikii nchi ya ahadi inayotiririka maziwa na asali kama hatutawekeza vizuri kwenye elimu. Kwa nini TAMISEMI haiwachukui wataalam walioko Wizara ya Elimu kuja TAMISEMI kuongeza nguvu? Wao ndiyo wana *Institutional Memory* ya elimu.

Mheshimiwa Spika, *Capitation Grant* sina hakika kama TAMISEMI inapeleka ya kutosha kwenye Shule za Sekondari na *Primary* kwa ajili ya ununuzi wa vitabu, chaki na kadhalika. Sina hakika kama mnapeleka Sh. 25,000 kwa kila mwanafunzi wa sekondari na Sh. 10,000 kwa kila mwanafunzi wa *primary school.*

Mheshimiwa Spika, kwetu Ngara shule hazina vitabu, ninahangaika kutafuta Vitabu vya Kiingereza na Sayansi. *Headmasters* wanaishi vizuri sana sijui kama hali hiyo inatokana na hiyo ruzuku ya vitabu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali izingatie ushauri wangu wa kuwawekea Mikataba ya Utendaji *(Performance Contracts),* Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mkoa, *DCs* na Watendaji na uwepo utaratibu wa Rais kukaa na Mawaziri na Wakuu wa Mikoa mara mbili kwa mwaka, kupitia mikataba hiyo. Viongozi na Watendaji wazembe waondolewe kwenye madaraka. Huo ni utaratibu endelevu kuliko Rais kushinikizwa na Bunge kuwaondoa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa kuwateua Viongozi na Watendaji kwa kuzingatia uwezo, sifa, uzoefu, uadilifu na uzalendo kuliko udini, urafiki, ushemeji na ukabila.

Mheshimiwa Spika, zingatieni *Principle* ya *Peter Principle – Never promote somebody to his highest level of incompetence."* Usimteue mtu na kumpa majukumu ambayo hana uwezo nayo.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Hivi karibuni tulitembelea maeneo mengi ya Tanzania kukagua Miradi ya Maendeleo inayohusiana na miundombinu zikiwemo barabara, madaraja, bandari, reli na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na wimbi kubwa la wizi katika Miradi hii ya Maendeleo. Kila Mradi tulioutembelea tumekuta malalamiko hayo, hata kusababisha kupunguza kasi ya kutekeleza Miradi hii. Mfano, katika Mradi mmoja jumla ya Sh. 300 milioni na vifaa vilivyokuwa vikisafirishwa kwenda kwenye Mradi kutoka Dar es Salaam viliibiwa. Kubwa ni kuwa vifaa hivyo vilisamehewa ushuru.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa wana nyezo kamili za kudhibiti wizi huu, kwani Kamati ya Ulinzi na Usalama ina Askari Polisi, Askari wa Usalama wa Taifa, Sungusungu na Ulinzi Shirikishi. Ikiwa nyombo hivi vitatumika vizuri, wizi huu utadhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, upo ucheleweshaji wa kutoa vibali vya aina mbalimbali kama ulipaji fidia, vibali vya kuhamisha makaburi na vibali vya ruhusa ya kuchimba mabwawa ya kuwekea maji kwa ajili ya Miradi ya Ujenzi inayohitaji maji mengi hasa katika Mikoa isiyopata mvua za kutosha.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, awaagize Wakuu wa Mikoa kusimamia Miradi hii hasa wizi wa vifaa kwani haya ni mambo yanayosababisha aibu kwa kwa Taifa na hasara.

Mheshimiwa Spika, taarifa za Serikali hazioneshi kuwa Zanzibar itafaidika na fedha za chenji ya rada. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze kama Zanzibar itafaidika na chenji hii.

**MHE. ALBERT OBAMA NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na hayo, naomba nitoe mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nashauri tupewe *data* za ukuaji wa hali ya uchumi pia kwa Mikoa na Wilaya ili iwe kichocheo cha kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, tulipoingia Bungeni simu zilikuwa haziiti ndani ya Bunge, lakini sasa hivi simu zinalia ndani. Je, ni kitu gani kimesababisha? Tunaomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, nashauri mbinu mpya za ugawaji wa pembejeo zibuniwe kwani imekuwa ni kero kwa sababu pembejeo haziendi kwa wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, masharti ya Wafadhili ya *Procurement* yanasababisha kero hii; hivyo ni vizuri *to re-negotiate again* na Wafadhili kurejesha na kutoa *tender for two years.*

Mheshimiwa Spika, ninayo maeneo mazuri ya umwagiliaji katika Wilaya ya Buhigwe ya Mabonde ya Mugera, Migongo, Kilelema, yenye ukubwa wa hekta 800 na Bulemanyi, Biharu, lenye hekta 700. Ninaiomba ofisi yako, wataalamu waweze kuiona na kushauri ili tuweze kulitumia kwa uzalishaji mpunga. Katika wilaya hiyo mpya haya ndiyo maeneo tunayoyapa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Manyovu, katika Tarafa ya Muyama, Serikali ilikataza na kufunga Mnanda wa Mifugo na wananchi wanahangaika kwa kukosa wapi waweze kuuzia mifugo yao. Taarifa ya maombi ya kufunguliwa kwa Mnada huo zipo Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo lakini hatujajibiwa juu ya ombi hilo. Hii ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutupatia nishati katika Wilaya Mpya ya Buhigwe katika Jimbo la Manyovu. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kusukuma nia hiyo kwa kuweka umeme Makao Makuu ya Wilaya mapema. Wilaya ya Kasulu imepata umeme hivi karibuni; je, kwa nini isiletwe mashine nyingine ili iongeze uwezo wa kusambaza umeme ambao ni km 20. Wananchi wa Manyovu wanataka umeme. Ninaiomba Serikali yetu iweke kipaumbele kwa Mikoa iliyoachwa nyuma kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano; Jimbo la Manyovu linazo Tarafa mbili Manyovu na Muyama. Tarafa ya Muyama yenye vijiji 13 ambavyo vyote viko mpakani, hawana mawasiliano kabisa na hivyo kushindwa kuwasiliana na kutoa taarifa zozote za kiulinzi. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, upelekwe mnara wa mawasiliano ili nchi yetu ipate ulinzi uliotukuka. Namwomba awasilliane na Serikali ya Wilaya atapewa uhakika huo. Silaha, risasi na wakimbizi, wanapita sana na raia hawawezi kuripoti kwa sababu hakuna simu inayofanya kazi maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali juu ya barabara zinazotekelezwa Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Barabara ya Mnanila mpaka Kasulu, km 42, ijengwe kwa kiwango cha lami kwani Mkoa wa Kigoma barabara imekuwa ndiyo siasa. Kwa nini siasa? Wananchi wanaamini kwamba, sehemu yenye Wabunge Wapinzani ndipo barabara za lami zinajengwa. Naomba eneo langu la Chama cha Mapinduzi liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa barabara hii: Inaunganisha nchi ya Burundi; inaunganisha Mikoa na Wilaya; inaunganisha Masoko ya Kimataifa yanayoanzishwa; inaunganisha kupitia Wilaya Mpya ya Buhigwe; *cost effective* kwa kufupisha kwa mfano toka Burundi kuja Kasulu na kuendelea; kuokoa ajali zinazotokana na milima iliyopo njia hiyo kwa wananchi kufa kwa ajali zinazotokana na utelezi mkubwa; na kuokoa Chama cha Mapinduzi kwenye majukwaa ya siasa ambapo kila siku wananchi wanaona sehemu zenye Upinzani zinajengwa. Ninaamini ramani ya nchi hii unayo, nakuomba unisaidie mimi Obama na Chama changu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa Bajeti iliyotengwa kwa Wilaya Mpya. Naomba fedha zitolewe haraka Wilaya ya Buhigwe ili miundombinu ianze kujengwa. Halmashauri Mpya za Wilaya zianzishwe haraka ili kutotegemea Wilaya Mama.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja,

**MHE. HERBERT JAMES MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na kuwapongeza wote.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa maoni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo Kiongozi na Msimamizi wa Serikali wa Wizara. Ofisi hii ichukue jukumu la kuratibu utekelezaji wa ahadi mbalimbali za Mheshimiwa Rais. Watendaji wanasahau ahadi hizo na mabadiliko ya Mawaziri pia yanachangia kupunguza kasi ya usimamizi wa utekelezaji wa ahadi hizo.

Katika Wilaya ya Muheza, Mheshimiwa Rais, ametoa ahadi zifuatazo:-

- Kufuta Hati za Mashamba ya Mkonge yasiyoendelezwa. Hili ni jukumu la Wizara ya Ardhi halijatekelezwa.

- Ahadi ya kujenga Barabara ya Muheza hadi Amani (km 35) kwa kiwango cha lami 2004 – 2012. Hili ni jukumu la Wizara ya Miundombinu halijatekelezwa.

- Ahadi ya kuupatia maji Mji wa Muheza kutoka Mto Ziggi (2005 – 2012). Hili ni jukumu la Wizara Maji halijatekelezwa.

- Ahadi ya kujenga upya Mradi wa Maji wa Mbambara Kata ya Songa ili kuwezesha Sekondari ya Mtindiro kupata maji 2005 – 2012. Jukumu la Wizara ya Maji halijatekelezwa.

- Kupandishwa Daraja Barabara ya Mbaramo – Kicheba – Misozwe – Maramba 2004 – 2011. Jukumu la Wizara ya Miundombinu limetekelezwa mwaka 2011.

- Kujenga Kituo cha Afya Kata ya Kicheba 2004 – 2012. Jukumu la Wizara ya Afya na TAMISEMI, halijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa utendaji wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani kuwa chini ya Mkurugenzi Mtendaji, unachangia kuficha hoja muhimu zenye dosari. Mkurugenzi anapopewa taarifa hizo kabla ya kupelekwa kwenye Kamati ya Fedha ha Baraza la Madiwani, anachambua na kuondoa baadhi ya hoja hasa za wizi na matumizi mabaya ya fedha. Kamati ya Usimamizi inayohusisha Wajumbe huru nje ya Halmashauri hazifanya kazi. Hila zinatumika kutoa fedha kati ya *DT* na Mkuu wa Idara huku *DED* akiwa hajui hasa *DED* anapokaimisha nafasi wakati akisafiri. Taarifa za Kamati ya Bunge inayosimamia Mahesabu ya Serikali za Mitaa hazifanyiwi kazi kwa ukamilifu wala Taarifa za Ukaguzi wa Mkaguzi Mkuu wa Serikali hazifanyiwi kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, taarifa za mapokezi ya fedha hazitolewi kwa usahihi na kwa wakati. Mfano mdogo ni fedha za Mfuko wa Jimbo la Muheza, Hazina walipeleka Sh.18,800,000 zaidi ya miezi sita iliyopita na

fungu la pili pia limepelekwa lakini hakuna taarifa ya kukiri kupokelewa fedha hizo hadi leo tarehe 27 Juni, 2012.

Mheshimiwa Spika, shaka ya wizi wa fedha zaidi ya Sh. 1,800,000 imetokea na Mkuguzi wa Ndani kumwarifu *DED* tangu Februari 2012, lakini taarifa hiyo haikutolewa kwenye Kamati ya Fedha na imekuwa kificho hadi Juni 2012.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Nishati (Umeme), baada ya kuongezeka upatikanaji wa gesi asilia, ipo haja kurejea mapendekezo ya awali kama ifuatavyo:-

(a) Kurejesha Kampuni ya *GASCO* iliyoundwa kabla ya mwaka 1998 chini ya Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)*. Kampuni hiyo ipewe jukumu la kusimamia usambazaji na uuzaji wa gesi badala ya kuweka jukumu hilo kwa Kampuni ya nje.

(b) Kampuni ya Taifa ya Usambazaji wa Mafuta *(COPEC)* irejeshwe na kupewa dhamana na uwezo wa kusambaza mafuta nchini badala ya kuachia kampuni za nje licha ya kuwa zimeaandikishwa nchini.

(c) Ili kujihakikishia uwezo mkubwa wa kukidhi mahitaji ya umeme, utekelezaji wa Miradi Mikubwa ya Umeme ya *Striglers Gorge Mg* 2000, Mradi wa Kiwira *Mg 300* itekelezwe sambamba na Miradi ya Gesi asilia.

(d) Miradi ya Dharura ya Uzalishaji Umeme isitishwe.

- Mradi wa Dharura wa Umeme wa *IPTL* ni mzigo mkubwa Kitaifa. Utakuwaje na Mradi wa Dharura kwa miaka 20?

- Kwa nini Mkataba wa *IPTL* unabebeshwa *TANESCO* gharama za matengenezo ya mashine zake na kulipia gharama za mafuta ya kuendeshea mashine hizo na baadaye kununua umeme uliozalishwa?

- Kwa nini *IPTL* wanachelewesha mapendekezo ya kutumia gesi kuendesha mashine zao badala ya mafuta mazito na mafuta ya ndege *(JET A1)* ambayo ni ghali?

Mheshimiwa Spika, tutaendelea hadi lini kubeba mzigo huo mkubwa wa gharama? Ninaunga mkono hoja ili ushauri uliopo utekelezwe.

**MHE. GOODLUCK JOSEPH OLE-MADEYE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu, kwa Uongozi wake mahiri. Pia nampongeza Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb), kwa kuteuliwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Nawapongeza pia Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa kazi nzuri wanayofanya kumsaidia Waziri Mkuu kuongoza Sekta zote zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nawatakia kila la kheri na pia nawahakikishia ushirikiano ili kwa pamoja tuweze kutimiza azma ya Chama cha

Mapinduzi ya kutumikia Wananchi wa Tanzania ili kupata maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, pili, nawapongeza sana Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote na Watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tatu, nathibitisha kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, naishukuru sana Serikali kwa namna walivyosaidia Wananchi wa Jimbo langu wanaokabiliwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame kupata chakula cha msaada. Nawapongeza sana Watendaji wote wakiongozwa na Bw. Peniel Lyimo, Katibu Mkuu, kwa kuwa wavumilivu na wasikivu wakati wote ambao tuliwasiliana na wakati mwingine tukiomba huduma kwa dharura.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa imedhihirika kuwa mvua katika Wilaya karibu zote za Mkoa wa Arusha imepungua sana na hivyo kuendelea kulima mahindi na mazao yaliyozoeleka kama maharage na mengineyo haitakuwa kwa manufaa ya jamii kwani hunyauka kabla ya kuchanua. Nashauri kuwa, Serikali itoe agizo kwa Uongozi wa Mkoa wa Arusha kuwa kuanzia sasa iwe ni lazima kwa wakulima wote kulima walau ekari mbili za mazao yanayostahimili ukame ikiwemo mtama na alizeti.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuongeza mitaji kwenye benki mbalimbali hapa nchini ili kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mikopo. Hata hivyo, nina shaka na utaratibu unaotumika kutoa mikopo ambayo hukwaza watu wa kawaida kupata mikopo hiyo. Mfano, ingawa lilianzishwa Dirisha la Kilimo *TIB* imekuwa vigumu kwa wakulima wadogo kupata mikopo. Benki huwataka wakulima hao kuwa na dhamana *(collateral)*, ambayo wengi hawana. Hatimiliki za Kimila ambazo hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999 hazithaminiwi na Mabenki ikiwemo *TIB.* Serikali iiagize Benki Kuu ya Tanzania itoe Mwongozo kwa Mabenki na Taasisi zote za Fedha kuwa ziheshimu hatimiliki hizo na kutoa mikopo kwa wananchi bila ubaguzi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi haujulikani kwa wananchi walio wengi nikiwemo mimi mwenyewe. Ni vizuri taratibu za kutoa mikopo ziwekwe wazi ili wananchi wote waweze kunufaika. Kama inavyoeleweka vijina wengi hawana ajira, vile vile hawana mtaji wa kuanzisha miradi wala dhamana ya kuwawezesha kukopa; nashauri hatua zichukuliwe kuwahamasisha na kuwasaidia vijana kupata mitaji kwa kuwawekea masharti nafuu. Mfano, Shahada ya Kuhitimu Chuo Kikuu itumike kuwa dhamana kwa mkopo mdogo usiozidi Sh. 50,000,000 ilimradi mkopo huo uwekewe bima.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Nishati: Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali ya madini ya urani. Nishati ya umeme itokanayo na madini hayo ndiyo yenye

uhakika zaidi kuliko vyanzo vingine vyote. Badala ya kuuza madini hayo yakiwa ghafi ni vizuri tukapanga kushirikiana na nchi zenye uzoefu katika ujenzi na usimamizi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa nyuklia kama vile Marekani ili kuzalisha umeme wa kutosha nchi nzima na sehemu yote ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya gesi asilimia kuendesha: Katika Hotuba ya Waziri wa Fedha, Serikali iliainisha maeneo yatakayosamehewa kodi ambayo ni pamoja na vifaa vya *CNG Vehicles Conversion Kits.* Mpango huu ni mzuri sana kwani utasaidia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni kuagiza mafuta ya kuendeshea magari. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kuwa marekebisho ya magari ya petroli au diseli ili yaweze kutumia gesi hayajawa na mafanikio makubwa kwa sababu uwezo wa kuunganisha vifaa hivyo na kufanya kazi bila gesi kuvunja unaonekana kuwa na upungufu hapa nchini. Ushauri wangu ni kwamba, ili kupunguza uagizaji wa mafuta ya petroli, Serikali ishawishi na kutoa motisha kwa waagizaji wa magari watakaoagiza na kuuza nchini magari yanayotumia gesi asilia na mafuta yaliokamilika. Magari yakiunganishwa kiwandani uvujaji hautakuwepo. Vile vile magari yote ya Serikali yatakayoagizwa kuanzia sasa yawe ni yenye kutumia gesi asilia na mafuta kwa pamoja. Sababu ya kufanya yatumie mafuta na gesi ni kutambua kuwa gesi asilia bado haijasambazwa nchini kote hivyo magari yakiwa ni ya gesi tu yatapa matatizo yakifika maeneo ambako hakuna vituo vya kujazia gesi. Katika mipango yetu ya miaka ijayo tujiandae kusambaza gesi maeneo yote ya

nchi hadi vijijini kwa sababu ndiyo nishati tuliyopewa na Mungu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo; napongeza Mpango wa Kuendeleza Kilimo cha Mpunga na Miwa kwenye Mabonde yaliyoainishwa. Ni vizuri tukatumia kila fursa iliyopo ili kuondokana na kero ya kuagiza chakula toka nje ya nchi. Vile vile nashauri kuwa mabonde madogo yaliyo kwenye mikoa yote nchini yatumike kwa kilimo cha umwagiliaji kadiri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna uwiano wa maendeleo ya viwanda vidogo katika Wilaya zote nchini. Zipo Wilaya hasa za Mijini zenye viwanda vingi wakati baadhi ya Wilaya hazina hata kiwanda kimoja cha kusindika mazao yazalishwayo Wilayani humo. Nashauri kuwa hatua za makusudi zichukuliwe kuchochea uwekezaji kwenye viwanda vidogo kwa Serikali kutoa motisha kwa wale watakaowekeza kwenye Wilaya za Vijijini.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana hatua ya Serikali kuweka kiwango cha chini cha kipato kwa wafanyabiashara kitakachotozwa kodi ya mapato iliyotangazwa na Waziri wa Fedha wakati wa kuhitimisha mjadala wa Hotuba yake ya Bajeti ya 2012/13. Ili uamuzi uliochukuliwa na Serikali uwe na manufaa kwa wananchi wote, nashauri kuwa Serikali iweke kiwango cha chini cha mapato ya wakulima ambacho hakitatozwa kodi. Watendaji wa Serikali za Mitaa wamekuwa wakiwatoza wakulima fedha nyingi sana kwa mazao yao wanayopeleka gulioni hata

kabla ya kuuza. Hii imekuwa kero kubwa sana. Kwa kuzingatia msamaha uliopendekezwa kutolewa kwa wafanyabiashara, wakulima wengi wadogo (wauza ndizi, mbuzi mmoja na kadhalika), wanapaswa kusamehewa ushuru wa mazao na mifugo midogo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wananchi wa Arumeru wajulishwe mustakabali wa Utawala wa Wilaya yao. Kwa muda mrefu sana wamekuwa wakiomba Tawala za Mikoa iigawanye Wilaya ya Arumeru ili kusogeza huduma za kiutawala karibu zaidi na wananchi na hivyo kuharakisha maendeleo. Wilaya imekwishagawanywa Kichama na Halmashauri. Kwa kuzingatia ukubwa, uhafifu wa miundombinu na uduni wa huduma kulinganisha na idadi ya watu, naomba Serikali iigawe Wilaya hiyo mapema iwezekanavyo ili wananchi wapunguziwe usumbufu wanaopata kufuata huduma mbali sana kutoka kwenye makazi yao.

Mheshimiwa Spika, ardhi kwenye Wilaya ya Arusha na Arumeru inaendelea kuwa haba kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu, kwa sababu ya kuwepo kwa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Jijijni Arusha, pamoja na fursa ya kibiashara zilizopo. Mahitaji ya ardhi yameendelea kuongezeka na hivyo ardhi inayofaa kwa kilimo imeendelea kubadilishwa matumizi kuwa ya makazi na biashara. Kama hali hii ikiendelea kuna hatari kuwa muda siyo mrefu ardhi yote nzuri iliyotengwa kwa ajili ya kilimo na kumilikishwa wawekezaji walioomba kwa ajili hiyo itakwisha na hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa chakula. Miaka ya 1970, Mwalimu Nyerere aliagiza

kuwa Mji wa Arusha ujengwe kuelekea Kusini kwenye maeneo yasiyo na rutuba sana. Mheshimiwa Rais Kikwete wakati akitoa tamko la kugawanywa kwa Wilaya ya Arumeru kuwa Halmashauri mbili, vivyo hivyo alirudia agizo hilo. Hata hivyo, maagizo haya ya Viongozi Wakuu wa Nchi wanapuuzwa na Uongozi na Watendaji wa Halmashauri ambao kazi kubwa inayofanywa sasa kwenye Halmashauri hiyo ni kununua mashamba na kugawa viwanja kisha kuuza.

Hali hiyo imeathiri utoaji huduma kwa wananchi kwani hata wanapoomba kuwa wapimiwe ardhi yao wanayomiliki kimila hawapati huduma kwa Maafisa wanaohusika wanashughulikia viwanja vya biashara. Naomba Waziri Mkuu aingilie kati hali hiyo na kuagiza kuwa mashamba yote yabakie kuwa mashamba na ikiwa waliomilikishwa wamechoka kulima, warejeshe Serikalini au wauze kwa wawekezaji wengine wenye nia ya kulima na siyo kugawa viwanja au kubadilisha matumizi kienyeji.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Olkokola kilijengwa yapata miaka mitano iliyopita. Kituo kina majengo ya kutosha kutoa huduma za kutwa na kulaza wagonjwa. Hata hivyo, hakijaweza kufanya kazi kulingana na uwezo wake kutokana na upungufu wa watumishi. Hadi kufikia juma lililopita, Kituo hicho kilikuwa na mtumishi mmoja tu. Tatizo kubwa kwenye Kituo hicho ni kutokuwepo kwa nyumba za watumishi. Pamoja na Kituo cha Olkokola, zipo zahanati katika Jimbo la Arumeru Magharibi ambazo hali yake kimajengo, watumishi na vitendanishi ni mbaya sana. Vituo hivyo ni pamoja na Oldonyosambu, Musa, Oljoro

na Losinoni. Naomba waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), atembelee zahanati hizo ili ajionee mwenyewe hali ilivyo na kutusaidia kuelekeza rasilimali zitengwe kwa ajili ya kuziimarisha.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kumwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), aingilie kati na kumwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kuwa atekeleze agizo la Mheshimiwa Rais kuwa, Halmashauri iandae Mpango Kabambe wa Maji kwa Wilaya yote na kuwasilisha Serikalini ili fedha zitengwe na kumaliza kero ya maji kwenye Wilaya hiyo. Mheshimiwa Rais, alitoa agizo hilo tarehe 17 Septemba, 2010 lakini hadi leo mchakato wa maandalizi haujaanza.

Mheshimiwa Spika, shule nyingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha hazina walimu. Hii inasababishwa na mazingira magumu yanayowakabili walimu kwenye Vijiji mbalimbali vya Wilaya hiyo. Naomba Serikali itoe kipaumbele kwa Shule za Sekondari na Msingi katika Wilaya hiyo ili kuvutia walimu wanaopangwa huko kuanza kazi na kubaki huko. Aidha, nashauri kuwa kwa kuzingatia ugumu wa mazingira ya kufundishia kwenye Wilaya hiyo, Serikali ikubali kuwapanga wahitimu wanaotoka maeneo hayo au wale wanaoonesha nia ya kutaka kwenda kufundisha maeneo hayo. Mwaka huu niliwasilisha majina ya walimu walioomba kupangwa maeneo hayo, lakini maombi hayo hayakuzingatiwa na matokeo yake waliopangwa na kuripoti ni wachache.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kusikia kilio cha Wananchi wa Jiji la Mwanza, kupandisha hadhi kwa Halmashauri na Ilemela kuwa Manispaa. Nasema hongera sana, tatizo litakalojitokeza ni kwamba fedha zilizotengwa kuianzisha Manispaa hiyo ni kidogo sana. Eneo la Utawala linabaki hivyo hivyo au mipaka itaongezwa au kupanuliwa ikiwemo Kisesa ambayo kwa sasa eneo hilo liko Wilaya ya Magu?

Mheshimiwa Spika, walimu kwa walimu wao ni viongozi, waelimishaji, waratibu na kadhalika. Masuala ya malalamiko yao yanapaswa kusikilizwa mapema iwezekanavyo. Kwa mfano, mishahara iboreshwe, ujenzi wa nyumba za kuishi, usafiri nao waweze kukopeshwa, wapewe posho ya mazingira magumu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Bunge hili Tukufu, Waziri Mkuu alijibu swali toka kwa Wabunge kuhusu malalamiko ya walimu na kusema nanukuu: “Mara Walimu watakapokuwa na Uongozi tayari wa CWT tutazungumza.” mwisho wa kunukuu. Je, Chombo hicho (CWT) kipo tayari? Maana yangu, kuna fukuto ambalo siyo zuri ndani ya Taasisi hii iitwayo Walimu.

Mheshimiwa Spika, Mwanza ni Mji wa viwanda vingi vya matumizi ya malighafi mbalimbali. Mwanza ina viwanda vya nguo, samaki, vyuma (nondo), vioo

na kadhalika. Matatizo ya viwanda hivi ni; vingi vimechakaa, hativumiki kama ipasavyo, vimebinafsishwa kwa wawekezaji kwa matumizi tofauti na mikataba mfano, Kiwanda cha Ngozi Ilemela kimekuwa ghala la tajiri mmoja na vingine vimefungwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri vifufuliwe virudishwe Serikalini kwa vile wawekezaji wamekiuka Mikataba. Serikali itolee tamko hapa Bungeni jinsi gani wanafufua au kuvibinafsisha kwa wawekezaji halali na Mikataba iangaliwe upya.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake na Wataalam, ambao waliochangia kuandika Hotuba hii ambayo leo tunaichangia kwa upeo mzuri zaidi. Hata hivyo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chenji ya rada, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati atakapokuwa anajibu hoja, suala hilo lazima atoe ufafanuzi wa Zanzibar ili kuondoa Kero ya Muungano. Kama ilivyokuwa kwa Tanzania Bara, wao wameingiza katika Elimu ya Msingi, Tanzania Zanzibar tumo katika Muungano kwa kupitia Elimu ya Juu, sasa itabidi tupate fedha hizo kwa ajili ya Sekondari na Vyuo hapo ndiyo tunadumisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pango za ofisi; nina masikitiko makubwa kwa Serikali kuendelea kukodi Ofisi za Serikali na kulipa pango. Mfano, Msajili wa Vyama

vya Siasa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hizi ni ofisi nyeti lakini zimekosa Majengo ya Serikali ya kufanyia kazi. Ukiangalia Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa, imepanga katika Majengo ya Posta na Simu na Majengo ya Wakala wa Manunuzi kwa ajili ya kutunza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Vifaa vya Uchaguzi. Huku ni kuipa hasara Serikali na kupoteza fedha za Wananchi walipa kodi kwani fedha hizo za pango wangepewa *investors* wa nyumbani ili kutujengea ofisi na hizo fedha tulizokuwa tunalipa pango zingelipa deni na Serikali kumiliki jengo lake na kuwa Ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mabasi ya Ofisi ya Bunge ni machakavu mno na yamekuwa hayana mvuto kutumiwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wanapofanya kazi za Bunge na wanapofanya Ziara za Kikazi Mikoani. Hata hivyo, Ofisi ya Bunge huingia hasara pale wanapokodi mabasi kwa ajili ya shughuli za kazi za Wabunge. Uchakavu wa mabasi hayo Kiserikali yana haki ya kuuzwa ili Bunge linunue mabasi mengine mapya au kama Bunge ni lazima kubakia na mabasi hayo, basi ni bora kuwataka Wabunge watumie magari yao na Bunge liwapatie mafuta wanapofanya Ziara za Kikazi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, itaisaidia Ofisi ya Bunge kutumia fedha kidogo kununua mafuta ya magari ya Wabunge badala ya kukodi mabasi ya nje kwa gharama kubwa na kulitia hasara Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa kuongeza Hati Safi na

kupunguza Hati zenye Mashaka na huo ni mwanzo mwema.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado elimu inahitajika kutoa mwamko mkali kwa baadhi ya Halmashauri zetu ambazo bado utendaji kazi wake siyo wa kuridhisha. Tunazidi kuangalia tunakoelekea ili kuleta sura nzuri ya Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, naiomba ofisi ya Waziri Mkuu ayatazame kwa umakini zaidi masuala matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu ubora wa elimu, ili kuimarisha elimu kwa vijana wetu, Idara ya Ukaguzi iimarishwe, fedha ziongozwe ili Wakaguzi waliopo kwenye Idara hiyo waweze kuzipitia shule zetu za sekondari na za msingi ili waweze kukagua utendaji wao wa kazi. Idara ya Ukaguzi iimarishwe kwa kuongezewa fedha za kutosha. Lakini pia utungaji wa mitihani ubadilishwe kutoka huu wa *'mutiple choice"* unaofanywa sasa. Wanafunzi wetu hawafikirii kwani wanafumba macho na kutia vyema.

Mheshimiwa Spika, pili, maadhimisho ya sherehe mbalimbali. Napendekeza kwa sasa tusimamishe kufanya sherehe kwa miaka mitano ijayo na fedha zake zipelekwe kwenye shughuli nyingine za kimaendeleo, tusimame kufanya sherehe. Tuache kufanya sherehe na maadhimisho kwa miaka mitano

(5) ili tufanye shughuli nyingine kwanza. Fedha za maadhimisho ya sherehe zinatuumiza vibaya, nchi hii na Watanzania hawahitaji kofia na *T-shirt*.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu mwenge. Miaka 50 imepita toka nchi yetu ipate uhuru, wananchi wa mwambao kule Ziwa Nyasa hawajawahi kuuona mwenge. Kama kweli mwenge ni kwa ajili ya watu wotem basi ninaomba mwenge kupita Ziwa Nyasa kuanzia Lumbila, Kolondo, Makonde na Lupingu. Mwenge ni nuru ya matumaini. Wananchi wa Ziwa Nyasa tumewatelekeza. Wananchi wa Kata hizo nilizozitaja hapo juu nao wanahitaji nuru ya matumaini inayoletwa na mwenge.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya bajeti. Pia napenda kuishukuru Serikali kwa kutangaza rasmi kuanzishwa kwa Wilaya mpya ya Nyang'hwale na Makao yake Makuu kuwa (Khalumwa) na baadhi ya viongozi tayari wamesharipoti kama Mkuu wa Wilaya *(DC), OCD, OSC, DSO,* Katibu wa Chama na kadhalika. Swali ni lini Halmashauri ya Nyang'hwale itaanzishwa?

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa ya hali ya chakula Jimboni Nyang'hwale, ni mbaya sana, sasa hivi debe moja la mahindi linauzwa Sh.15,0000 – 16000. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ijipange haraka kutatua tatizo hilo au kupunguza makali hayo kuepusha vifo kwa wananchi wangu wa Wilaya mpya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ahadi za Mheshimiwa Rais katika mkutano wake wa kampeni Jimboni Nyang'hwale aliahidi mambo mengi kama:-

(a) Barabara itokayo Busisi – Busolwa-Nyitundu-Kalumwa-Bukwimba- Nyang'holongo–Kahama, kujengwa kwa kiwango cha lami lakini hadi leo hatua zozote hatujaziona. Je, mpango huu utaanza lini? Naomba ufafanuzi wako.

(b) Mheshimiwa Rais aliahidi umeme kuwashwa Jimboni Nyang'hwale haraka iwezekanavyo lakini hadi leo hatua za kuleta umeme zinasuasua sana hadi wananchi kuanza kukata tamaa na ahadi za Mheshimiwa Rais.

(c) Mheshimiwa Rais aliahidi kupunguza tatizo kubwa la maji kwa kufufua mtandao wa maji utakao Ziwa Victoria uliokuwepo tangu miaka ya 1975 kuwa utafufuliwa ili wananchi wapate maji lakini hadi leo hii hakuna hatua zozote za mradi huo kuanza. Wananchi hadi sasa wanahoji ahadi ya Mheshimiwa Rais mbona kimya kabisa?

(d) Mheshimiwa Rais aliahidi kukipandisha Kituo cha Afya Khalumwa kuwa Hospitali ya Wilaya ili kupanua wigo wa matibabu na kupunguza msongamano uliopo hivi sasa kwa sababu kituo hicho kinapokea wagonjwa wengi sana hadi Wilaya za jirani kama Kahama, Shinyanga Vijijini, Geita na Sengerema. Ahadi hiyo mpaka sasa hakuna dalili zozote za kuanzishwa upanuzi huo.

Wananchi wanahoji ni lini sasa ahadi za Mheshimiwa Rais zitaanza kutekelezwa?

(e) Mheshimiwa Rais aliahidi kupunguza tatizo la upungufu wa Walimu kwenye shule zetu. Kwa hili tunashukuru sana kuwa sasa Walimu shule nyingi za msingi na sekondari wanaongezeka, kiasi tunampongeza Rais kwa hilo. Pamoja na hilo, bado tuna upungufu mkuwa wa nyumba za Walimu, madawati, vitabu, maabara na vyoo, tunaomba Serikali itusaidie kupunguza tatizo hilo upande wa elimu.

Mheshimiwa Spika, tatu, tatizo la soko la pamba kuyumba, wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale tayari wameshakata tamaa na kilimo cha pamba kuwa kinawapotezea muda na uduni wa maisha yao kwa mategemeo yasiyo na matumaini. Tunaiomba Serikali ifufue viwanda vya kuchambua pamba kama cha Kasamwa Ginerry, Buyagu Ginerry, Chato Ginerry na kadhalika na kufufua viwanda vya nguo kama Mwatex, Mutex na kadhalika ili kupandisha zao hilo la pamba kuwa na thamani ili wakulima wafaidike na zao hilo.

Mheshimiwa Spika, nne, wafugaji wa Jimbo la Nyang'hwale hawaoni sababu ya kuendelea kuwa wafugaji na kuwa watumwa wa mifugo hao bila kufaidika nao. Sababu kuu za kukatisha tamaa ni upungufu wa malambo ya maji ya kunyweshea mifugo, upungufu wa majosho ya kuogeshea, soko la mazao ya mifugo kama ngozi, samaki, ng'ombe na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tano, naomba kujua Serikali imechukua hatua gani kwa dharura iliyotokea huko vijiji vya lyenze na Mwasabuka katika Kata ya Mwingiro kwa milipuko ya migodi ya *Kahama Mine* na kusababisha mpasuko mkubwa na nyumba nyingi kupata nyufa na kutia wasiwasi kwa wakazi wa maeneo hayo. Je, Serikali ina mpango upi wa kutoa fidia kwa wahaga hao? Naomba Serikali itoe tamko.

Mheshimiwa Spika, sita, naipongeza Serikali kwa kuongeza posho kwa Madiwani. Naomba wapate mshahara, pia naomba Serikali iwafikirie Wenyeviti wa Mtaa na Vitongoji wapate mshahara.

Mheshimiwa Spika, saba, nauliza kwa nini Serikali hairuhusu Waislam kujiunga na *OIC* na kuwa na Mahakama ya Kadhi ili na Waislam wawe na chombo chao cha kisheria cha dini yao?

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitoe shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia kwa maandishi kwenye hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nichangie kwenye maafa ukurasa wa 58 na 59 wa Kitabu cha Hotuba ya Waziri Mkuu, inasema katika mwaka 2011/2012, Serikali imeshughulikia matukio ya maafa ambayo yametokea, mafuriko, magonjwa ya mlipuko, upepo mkali pamoja na ukame. Huo ni katika ukurasa wa 58. Ukurasa wa 59, Serikali hiyohiyo imetaja waathirika wa milipuko ya mabomu yaliyotokea kwenye Kambi ya Jeshi ya

Gongo la Mboto. Masikitiko yangu ni kwamba hata kule Zanzibar kulitokea maafa makubwa, maafa ambayo yalishtua Tanzania nzima na dunia kwa jumla. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kufanya majumuisho atuambie ni kwa nini maafa haya ya Meli ya *Spice Island* ya Zanzibar haikuonyeshwa katika bajeti hii au ndiyo Waziri anatuonyesha maafa haya hayakuwa katika nchi hii?

Mheshimiwa Spika, muungano wowote duniani hutegemewa kuongeza nguvu kwa walioungana na sio kupopotoa nguvu zote za upande mmoja na upande huo ubaki bufuru tupu (kwa maneno ya Profesa Shivji). Kwa muundo wa muungano huu, Zanzibar imepoteza nguvu, uwezo na madaraka yake yote kama nchi na yametumbukizwa katika himaya ya Tanganyika lakini Tanganyika ilipoteza jina tu nguvu, uwezo na madaraka viliongezeka. Ukweli katika jambo hili ni pale viongozi wa nchi hizi mbili walipokutana kwa siri kule Zanzibar kukubaliana kuziunganisha nchi zao bila umma haujaelezwa kuhusu Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mkataba wa muungano huu ulipelekwa katika vyombo vya kutunga sheria vya nchi hizi mbili ili kuridhiwa, uridhiwaji wa mkataba huo uliridhiwa na upande mmoja wa Bunge la Tanganyika, upande wa Bunge la Zanzibar haukuridhia mkataba huo. Aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dourado ndiye aliyeibua hoja ya jambo hilo. Kwa maelezo ya Dourado hakuna sheria yoyote ya mamlaka za Zanzibar zilizowahi kutungwa na kuonyesha uridhiaji wa Mkataba wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, naye Profesa Shivji katika kupekuapekua kwake alibahatika kuliona Tangazo la Serikali ya Zanzibar la Mei 1 – 1964 lililochapishwa na Gazeti la Tanganyika Namba 243 (GN 243 Tanganyika Gazeti) ambalo lilitolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Tanganyika. Tangazo hili lilisema kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba mkataba wowote wa kimataifa uwe kwa maandishi au katika mdomo, ni lazima uwe umeingiwa katika hali ya ukweli na uwazi na usio na shinikizo na kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, Tangazo likaendelea kusema:-

Uwepo wa lolote katika mambo yafuatayo utabatilisha mkataba; udanganyifu katika kufanya jambo, upotoshaji unaotokana na hila au upotoshaji katika kufanya jambo, ama udanganyifu unaotokana na kutokuweka jambo husika bayana.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ina haki ya kupanga mipango yake ya kiuchumi, huduma za jamii, miundombinu, haya yote si mambo ya muungano lakini haiwezi kupanga hayo bila kujua idadi ya watu wake na makisio ya wageni wake, Zanzibar haina uwezo wa kudhibiti lolote. Uingiaji wa Zanzibar unaoeleweka ulikuwepo kabla ya muungano na hata baada ya muungano ulifanyiwa nongwa ya kisiasa hadi kuondolewa. Leo Zanzibar imekithiri kwa matukio ya wizi wa kutumia silaha wakati Zanzibar raia hawaruhusiwi kutumia silaha. Naomba Waziri Mkuu atakapokuja kujumuisha, atuambe ni lini sasa Serikali

itarudisha utaratibu wa kuingia Zanzibar uliokuwepo hasa ukizingatia sasa hivi dunia imejaa vitendo vya ugaidi na ili Zanzibar iweze kudhibiti wageni wanaoingia?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa niaba ya wananchi wa Musoma kutupatia Wilaya mpya ya Butiama. Pamoja na mvutano uliokuwapo ndani ya Wilaya kupata mahali pa kuweka Makao Makuu ya Wilaya na hatimaye maamuzi yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais ya kumuenzi Baba wa Taifa na kuamua kuwa Makao Makuu yawe pale pale Butiama.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kuweka kumbukumbu za Taifa, naomba sasa eneo la Mwitongo na mashamba ya Mwalimu yawe *ring fenced* na kuingizwa kwenye *National Heritage Site* ili uharibifu wowote wa mazingira hasa miti au msitu uliopo hapo Mwitongo isikatwe bali eneo zima lihifadhiwe kama *National Heritage*, Butiama Mwitongo iwe kumbukumbu ya vizazi vijayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ombi la kuitenga Butiama Mwitongo kuwa Hifadhi au National Heritage, naomba Serikali izidishe juhudi zake kuanza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere. Natambua juhudi Serikali inazozifanya kuhusu kuwaleta wawekezaji kutoka Thailand kuwekeza kwenye kilimo, uvuvi na ufugaji pale Butiama. Tukifanya hivyo basi

kweli tutakuwa tumemuenzi Mwalimu Nyerere, alikuwa mkulima na mfugaji. Iwapo Butiama itaingizwa kwenye mpango wa uwekezaji wa *CPF Thailand* ambao sasa wako nchini basi ninahakika kuwa hata Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere kitajengwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba ili kuhifadhi mazingira ya Butiama, yale mabwawa makubwa ya maji ya Kyarano na Rwamkoma yafufuliwe tayari kwa kuanza kilimo, ujenzi wa Chuo Kikuu na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maombi ya kuifufua Butiama na kumuenzi Mwalimu kwa juhudi zake za kuendeleza kilimo, naomba Butiama imegewe fedha kutoka fedha zilizotengwa na nchi nane tajiri duniani kwa ajili ya kilimo Tanzania kwa ajili ya kilimo Butihama na maeneo jirani kama vile shamba la Bugwema ambalo limekosa mwekezaji wa hakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo niliyoyataja, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. AMINA N. MAKILLAGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naungana na Wabunge wenzangu kukushukuru wewe na Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango na mawazo yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na wale wote walioshiriki kwa hali na mali kuandaa

Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Serikali kwa kusikiliza kilio cha Wabunge wa Mara kwa niaba ya wananchi na kutenga fedha kwa ajili ya uendelezaji wa Hospitali ya Rufaa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Singida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya afya, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Mara, Singida, Mtwara na Lindi, pia napenda kujua mchango wa Serikali kukamilisha miradi hiyo ili kuondoa adha ya wananchi wa Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya maji, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ya kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama kwa kiwango cha asilimia 86 mijini na vijiji 65, naomba nitoe ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa maji vijijini kasi iongezeke. Kasi ya usambazaji maji vijijini bado si ya kiwango kikubwa cha kuridhisha. Naomba Serikali iongeze bidii katika kuongeza kasi ya kutenga fedha kwa ajili ya kusambaza maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Shinyanga, Nzega, Igunga na Tabora, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kufikisha maji maeneo ya Igunga, Nzega, Tabora kutoka Mkoa wa Shinyanga (Ziwa Victoria). Naishauri Serikali ifanye kila linalowezekana kuongeza fedha

katika Wizara ya Maji ili mradi huo uweze kutekelezwa kabla ya mwaka 2015 Ilani, Ibara 86.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijitahidi kuongeza na kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji ili kupunguza upotevu wa maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa maji Mgango, Kiabakari na Butiama, naomba Serikali ifanye kila linalowezekana kusambaza maji kutoka chanzo cha maji cha Mgango katika vijiji vinavyozunguka chanzo cha maji pia maji yafike katika Kata ya Kiabakari – Butiama bila kusuasua.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uchimbaji wa maji ya visima na kutoa maji, Serikali ichukue hatua. Maji vijijini, hapa Serikali haikueleza ni kiasi gani kimefikia katika usambazaji wa maji vijijini. Hali siyo nzuri, jitihada ziendelee. Mradi wa maji katika vijiji 10 bado unasuasua. Napenda kujua pia Serikali inatoa kauli gani juu ya mishahara ya wafanyakazi katika chanzo cha maji Mugambi, Butiama?

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Serikali kuhusu mradi wa maji wa vijiji 10. Serikali ijitahidi kutenga fedha za ndani kwa ajili ya kuendeleza mradi wa maji vijiji 10 badala ya kutegemea wafadhili wa nje. Aidha, bajeti ya maji vijijini naomba iongezwe ili kuongeza upatikanaji wa maji na kuwapunguzia adha wanayopata wanawake kwa kutembea masafa marefu kilomita 1 – 2 wakitafuta maji (Maji ni Uhai).

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Dar es Salaam. Pongezi kwa Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya mradi wa maji. Naomba Serikali ijitahidi kupeleka fedha hizo kwa wakati ili kazi ya kukarabati miundombinu ya Ruvu Chini na Ruvu Juu, ujenzi wa visima vya Mpera, Bwawa la Kidunda uweze kuendelea ili ifikapo 2015 Dar es Salaam tatizo za la maji libaki kuwa historia.

Mheshimiwa Spika, ombi kwa Serikali. Kwa kuwa matanki ya kusambaza maji Dar es Salaam yatawekwa kwenye mlima wa Ruvu ambao ni kilomita moja kufika Kisarawe, vilevile vyanzo vya maji vya Mpiji na Mpera viko karibu na Wilaya ya Kisarawe na chanzo cha maji cha Mpera kilichopo Wilaya ya Mkuranga, mradi huu wa maji Dar es Salaam kuhudumia wananchi wa Dar es Salaam, Bagamoyo na Kibaha tu, sasa tuongeze wigo ili mradi huu pia uhudumie wananchi wa Mkuranga na Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya, Zahanati na Vituo vya Afya. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kushirikiana na wananchi kwa kujenga Zahanati na Kituo cha Afya kila Kijiji na kila Kata, naiomba Serikali ijitahidi kuweka msimamo mpya wa kuhamasisha wananchi kuona umuhimu wa kujenga Zahanati na Kituo cha Afya kila Kata kwa sababu itasaidia kupunguza vifo vya wanawake wanaojifungua na watoto wanaokufa kabla ya miaka mitano, pia itawapunguzia mzigo wanawake wajawazito wanaopata adha ya kutembea masafa marefu ya kilomita 5 – 8 kutafuta huduma ya afya. Aidha, Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua madawa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupanga na kutenga fedha za ujenzi wa Hospitali za Rufaa kwa Mikoa ya Mara, Mtwara, Lindi na Singida. Naomba Serikali itenge fedha za kutosha ili mradi huu uendelee kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo, naipongeza Serikali kwa kukarabati na kujenga majosho na malambo. Pamoja na kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji, Serikali ijitahidi na ihakikishe inatenga fedha kwa ajili ya majosho na marambo, inatenga ardhi kwa ajili ya wakulima na wafugaji ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji na kwenye Halmashauri za Wilaya, Serikali izielekeze Halmashauri kutunga Sheria Ndogo itakayofuatwa kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, sekta ya miundombinu ya barabara. Barabara za Bunda, Kisonya hazikutengewa fedha, napenda kupata maelezo fedha za barabara hizi zitatoka wapi? Serikali pia ione uwezekano wa kujenga barabara ya Kiwango cha lami Musoma – Majita kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Mkapa ya mwaka 2000, 2009 na 2010.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo na napenda kupewa majibu kwa maswali nitakayouliza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nchini, napenda kuishauri Serikali ianze kutupatia taarifa Waheshimiwa

Wabunge juu ya fedha ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri kila mwezi au robo tatu ya mwaka ili Wabunge wawe na taarifa ya fedha zilizoingia kwenye kila mradi na kufuatilia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zimekuwa zinaitisha vikao vya Madiwani ambapo Wabunge ni wajumbe na ratiba zao zinagongana na ratiba ya Bunge. Napenda kupata majibu ni lini (TAMISEMI) itatoa mwongozo ili Halmashauri na Manispaa zisiitishe vikao wakati wa Kamati za Bunge au vikao vya Bunge?

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Napenda kupata majibu kutoka Serikalini ni lini itatenga fedha za ujenzi wa ofisi ya Msajili wa Vyama ili tuache kutumia fedha nyingi za walipa kodi kulipia pango/kodi ya ofisi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, napenda kupata majibu ya mambo yafautayo: Moja, ni kuhusu afya. Napenda kupata majibu, ni lini vijiji visivyo na zahanati vitapata zahanati mfano Kigina Magarama, Nyarulanga na kadhalika. Pia nataka majibu fedha za *CHF* zilizotumiwa na *DMO* wa Wilaya ya Kibondo zaidi ya shilingi milioni 76, akatumia fedha za afya pia shilingi milioni 42 na pia ametumia tena shilingi milioni 22. Nataka kupata majibu ni hatua zipi zimechukuliwa kwa ufisadi wa namna hii?

Mheshimiwa Spika, pili, kilimo. Nataka kupata majibu ni lini mawakala waliosambaza mbolea

watalipwa? Pia nataka kuishauri Serikali ilete mbolea kwa wakati. Pia wananchi wanahitaji mbegu za alizeti.

Mheshimiwa Spika, tatu, uvuvi. Katika pori la Moyowosi lililoko Wilayani Kibondo; kuna mabwawa yaliyoko kwenye *game reserve*, wananchi wamekuwa wakipewa vibali lakini nataka kupata majibu kwa nini wananchi kwa sasa hawapewi vibali vya kuingia kwenye hifadhi kama ilivyokuwa awali na watapewa vibali tena lini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu soko la mpakani. Wilaya ya Kibondo inapakana na nchi ya Burundi. Serikali iliahidi kujenga soko la mpakani (Mabamba) katika kijiji cha Mkalazi na Benki ya *TIB* ilikubali kutoa fedha. Je, soko hilo kwa nini halijengwi mpaka sasa? Je, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, sekta ya ujenzi. Napenda kupata majibu ya Serikali ni lini barabara ya Nyakanazi - Kidahwe itajengwa kwa lami? Tumekuwa tunapewa ahadi ya ujenzi kila mwaka, je, ni lini barabara hii itajengwa. Pia napenda kujua lini ahadi ya Rais ya ujenzi wa kilometa 1½ ya lami Kibondo Mjini, je, ujenzi huu utaanza lini, soma Kitabu cha Ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, matumizi makubwa ya Serikali, napenda kuiuliza Serikali, ni lini itapunguza posho za vikao ambazo zinaongeza gharama kwa Serikali? Pili napenda kupata majibu, magari ya kifahari yanayotumia gharama kubwa kufanyiwa matengenezo, je mnada wa magari haya utafanyika lini?

Mheshimiwa Spika, sensa ya watu na makazi 2012, napenda kuishauri Serikali, kwa Mikoa ya mipakani, sensa ifanyike baada ya Operesheni Maalum ya kuwaondoa wahamiaji haramu. Jambo hili lilifanyika kabla ya sensa mwaka 2002, hii itasaidia kuhesabu Watanzania tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya madini, napenda kuishauri Serikali kupitia upya utaratibu wa kodi katika madini kwani bado Taifa halijanufaika na rasilimali hii, zingatia taarifa ya Kamati ya Bomani. Pia Watanzania wapewe kazi za kuhudumia migodini ili kutoa ajira mfano kuhudumia vyakula na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, napenda kuishauri Serikali uwekezaji katika viwanda vya alizeti, ufuta, michikichi na Korosho na kadhalika kwani hadi sasa tunaingiza (*import*) zaidi ya 60% ya mafuta ya kula toka nje. Maeneo kama ya Kibondo yanaweza kuzalisha mazao hayo, naomba Serikali izingatie haya.

Mheshimiwa Spika, mitandao ya simu, tumekuwa tunapoteza mapato mengi kwenye mitandao ya simu. Tumekuwa tukitoza *corporate tax* peke yake, hii inapoteza mapato makubwa. Mfano mtando wa Vodacom peke yake umefanya *transaction* za M-pesa kwa shilingi 6.6 trilioni, fedha zote hizi hazijatozwa kodi, acha *Zain, Tigo, Zantel* na kadhalika.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono na kuipongeza hoja ya Waziri

Mkuu, kwa kujali maslahi ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Waziri Mkuu imewapa moyo na kwa kuitambua Korogwe kuwa ndiyo Mkoa tarajiwa hasa pale mipango ya Halmashauri ya Korogwe ilipotamkwa rasmi kuingia kwenye programu ya maboresho ya miji saba nchini. Hakika hii ni hatua kubwa sana ya matumaini. Nimetumwa na wananchi wa Korogwe nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake ya TAMISEMI. Zaidi ya hayo ni mafao ya wahanga wa Mkonge ambao sasa wameanza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Korogwe inakabiliwa na changamoto ya magonjwa ya mlipuko hususan kipindupindu na homa ya matumbo. Hali hii inachangiwa sana kutokana na Mji huu kuwa chini ya mlima na ardhi yake eneo la makazi ni (teke) majimaji kwani kina cha maji *(water table)* kiko juu sana.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji Korogwe imeomba magari ya taka ngumu na maji taka ili kukabiliana na hali hii. Kwa kuwa wakati wa bajeti tulipewa mwongozo wa kutovuka kikomo *(ceiling)* na hivyo kufanya mahitaji haya kufuata mfumo wa maombi maalum mara zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mji Korogwe bado ni changa, haina uwezo na Mji huu unakuwa kwa kasi na hivyo kupelekea kushindwa kukabiliana na uzalishaji mkubwa wa taka. Mrundikano wa takataka maeneo ya sokoni, stendi ya basi na mtaani, ndiko

kulikopelekea sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati maombi yetu wakati tukisubiri utekelezaji wa Mpango wa Benki ya Dunia wa Uendelezaji wa Miji Mipya.

Mheshimiwa Spika, juhudi binafsi za watu waliotoa vitendea kazi, magari, zimekuwa ni za muda mfupi tu hivyo bado tatizo liko pale pale. Aidha, Halmashauri ya Mji wa Korogwe haina mfumo maalum wa maji taka na vyoo kwenye makazi ambavyo viko kwenye viwanja vidogo ni vya aina ya mashimo. Hali hii ni ya hatari kwa usalama wa afya ya wakazi na wananchi kwa ujumla. Kwa nyakati mbalimbali nimejaribu kufanya mawasiliano na Ofisi ya TAMISEMI kuhusiana na maombi haya bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naleta ombi kwa niaba ya wananchi wa Korogwe ili tusaidiwe kupatiwa gari la taka na majitaka ili kunusuru hali iliyopo. Basi hata kwa kuanzia na taka ngumu, naomba japo matrekta mawili na matrela yake kama juhudi za awali za kupunguza kadhia iliyopo.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuandaa na kuwasilisha hotuba na mpango mzuri kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sana mgawanyo wa fedha za maendeleo na *OC* umekuwa na tofauti kubwa sana kati ya Mkoa na Mkoa, Wizara na Wizara, Taasisi na Taasisi. Mikoa mingine imekuwa inapata asilimia 8.9 ya *OC* bajeti nyingine ikipata

asilimia 0.98 na kwa *Development Fund* baadhi ya Mikoa inapata asilimia 6.39 (Mwanza) na Mikoa mingine inapata asilimia 1.44 (Katavi). Kwa upande wa Wizara tofauti ni kubwa sana. Wakati mgao wa baadhi ya Wizara umefikia asilimia 18 (Ujenzi) – *OC* na *Development Funds* kufikia asilimia 6.73 (Ujenzi), *OC* mgao wa Wizara nyingine ni mdogo sana kama Mifugo na Uvuvi mgao wake ni asilimia 0.83 (*OC*) na asilimia 2.67 (*development*). Kuna haja ya kutazama upya mgao huu ili kuwepo na uwiano na kupunguza tofauti hii kubwa kati ya Mkoa na Mkoa, Wizara na Wizara.

Mheshimiwa Spika, fedha zaidi itafutwe na iwekwe katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kutenga, kupima na kuweka miundombinu wezeshi kwa ajili ya maeneo ya ufugaji ili kupunguza na hatimaye kuondoa au kumaliza migogoro kati ya wafugaji na wakulima, migogoro inayoshamiri hivi sasa katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, jitihada zifanyike ili kuunda *Budget Designated Fund* ama *Budget Endowment Fund* kwa ajili ya ku-*fund budget* iliyoidhinishwa na Bunge. Hii itahakikisha kuwa fedha zitahamishwa zitumike kwa wakati. Mfuko huu utatunishwa na fedha za *reserves*, mikopo ya ndani na nje ya nchi na misaada ya nchi rafiki; mirabaha toka kwenye madini, uchimbaji gesi na mafuta, vitalu vya uwindaji na kadhalika. Pesa ya kodi na tozo ikusanywayo iende kwenye mfuko huu kwa *replenishment* na kuandaliwa kugharamia *budget* ya mwaka unaofuata. *Target* ya mfuko huu iwe ni shilingi trilioni 20.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia kwa mdomo, napenda kuendelea kuchangia kwa maandishi ili kuona Serikali inatekeleza yale iliyowaahidi wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutoa ufanunuzi wa kina kuhusu ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Morogoro Vijijini (Mvuha). Hadi leo tumepokea Sh.500,000,000 ambazo zimetumika kwa uandaaji wa michoro, upimaji wa maeneo na uidhinishaji wa michoro. Maandalizi ya kufungua maeneo (miundombinu) na uchunguzi wa udongo *(soil test)* yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tupatiwe fedha shilingi 1,000,000,000/= kama tulivyoomba katika Maombi Maalum ili tuweze kuwakaribia kwa karibu wananchi ambao tunawaongoza. Naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu atatuangalia kwa jicho la huruma wananchi wa Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pili, ujenzi wa Bwawa la Kidunga, ufafanuzi wake ni kuwa mambo muhimu ambayo yalikubaliwa kati ya wananchi, *DAWASA* na Serikali ni kwanza, DAWASA, Serikali kulipa fidia stahili chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 kwa mali na maendeleo yote ya waathirika wa ujenzi wa bwawa. Pili, *DAWASA* kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro iandae eneo la kuhamia wananchi na *DAWASA* itagharamia upimaji wa makazi mapya na uwekaji miundombinu. Tatu, *DAWASA* na Halmashauri ya Wilaya itajenga majengo ya umma

yanayotoa huduma, majengo hayo ni zahanati, shule, ofisi za Serikali na majengo ya ibada.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa, tathmini ya mali na maendeleo ya wananchi imekamilika. *DAWASA* wameshakabidhiwa rasimu ya uthamini. Aidha, tunasubiri *approve* ya Mthamini Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nini kinaendelea? Eneo la kuhamishia wananchi limeshatengwa katika kijiji cha Bwakila Chini ambako kutakuwa kijiji cha kisasa. Makadirio yameshatumwa *DAWASA* na hatujapata pesa, Halmashari tunasubiri utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu Hati Chafu ambayo imepata Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ukurasa wa 14, sababu ambazo zinasababisha Halmashauri kupata Hati Chafu ni kuwepo watumishi wanaokiuka maadili na kujihusisha na ubadhirifu wakishirikiana na watumishi wa benki na kutotolewa kwa mafunzo ya kutosha kwa watumishi wa umma katika sekta ya fedha. Nachotaka kusema ni kuwa kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kazi kuu ambayo ameianza katika kusafisha Wizara hii mama ambayo ndiyo uti wa mgongo wa nchi. Si haki kwa Serikali kunyima haki wananchi ambao Halmashauri yao imepata Hati Chafu kwa matendo ya watu ambao wamefanya ubadhirifu. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa TAMISEMI, Serikali iendelee kutoa pesa ya ruzuku ya maendeleo kwa

Wilaya zote hata kama zimepata Hati Chafu kwani kutotoa ruzuku hiyo ni kutesa wananchi ambao hawana hatia. Ni vizuri kila wakati Hazina wanapopeleka pesa ya aina yoyote kwenye Halmashauri Wabunge tukapewa kopi ya barua inayoonyesha pesa hiyo na kitu ambacho kitafanyika. Aidha, sheria za utumishi wa umma ziangaliwe upya ili ziendane na wakati huu.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji. Migogoro hii inahitaji ufumbuzi wa haraka kabla maafa hayajatokea. Nimeendelea kusema toka Bunge lililopita, Mkoa wa Morogoro ni Mkoa wa Kilimo na katika kuthibitisha hili Mheshimiwa Rais ameuandaa kuwa ghala la kitaifa la chakula. Mkoa una uhakika wa kulisha Taifa na cha ziada kuuza kutokana na mabonde mengi mazuri na makubwa tulionayo. Kuendelea kuachia mifugo iendelee kuzagaa bila utaratibu Mkoani Morogoro na hususani Jimbo la Morogoro Kusini, Wilaya ya Morogoro ni kuufanya Mkoa wa Morogoro kupoteza uhalisia wa asili wa Mkoa wa Morogoro na hatimaye kuufanya jangwa na vilevile kuchochea mapigano na hatimaye vifo kati ya wakulima na wafugaji wakati wafugaji wakilisha mifugo katika mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anapokuwa anahitimisha bajeti yake atueleze ni jinsi gani Serikali imejipanga katika kutatua tatizo hili. Pendekezo langu ikibidi ipangwe Mikoa ya kilimo na Mikoa ya ufugaji. Ni kweli vyote ni muhimu kwa wananchi lakini ni vizuri tukumbuke tukipeleka nchi katika jangwa, nchi itaingia katika njaa.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii ili nami niweze kuchangia mchango wangu katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nachangia katika Kilimo kwa sababu karibu asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na hata wananchi wa Mkoa wa Rukwa na wa Jimbo langu la Kwela zaidi ya asilimia 95 ni wakulima. Kilimo ni uti wa mgongo katika Taifa letu na ndiyo maana kumekuwepo na kauli mbiu za kila wakati zikiashiria ukweli huo kwa mfano Kilimo cha Kufa na Kupona, Kilimo ndiyo Ngao yetu, Azimio la Siasa ni Kilimo – kauli iliyotolewa na hayati Baba wa Taifa katika Azimio la Iringa mwaka 1972 na kwa sasa Kilimo Kwanza. Maazimio yote haya yanaendelea kutoa msimamo kuwa kilimo ndiyo kinaweza kusaidia Watanzania kwa sehemu kubwa. Kwa maana hiyo, naomba bajeti ya kilimo iongezwe.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji ndiyo kinaweza kuleta ukombozi mkubwa. Kilimo hiki hakijatiliwa maanani kwa mfano tunazo hekta 29 milioni zinazoweza kutumika katika kilimo cha umwagiliaji lakini katika hekta hizo ni hekta 354690 sawa na asilimia 1.19, hicho ni kiwango kidogo mno. Hivyo nashauri bajeti ya kilimo cha umwagiliaji iongozwe.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2011/2012, aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo aliahidi

kuingiza mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika sehemu ya Maleza yenye hekta 7500 katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Naomba sasa kupata majibu kama sehemu hiyo imetengewa fedha, naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa mazao, naomba Serikali ijitahidi kununua mazao ya wakulima ili wananchi wasikate tamaa na jitihada za kuendelea kulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo, Serikali inatakiwa kuharakisha zoezi la kurasimisha rasilimali walizonazo wakulima ili zitumike kama dhamana katika mikopo yao kwa taasisi za fedha kama vile mashamba yao na nyumba zao. Jambo hili halina msukumo wa kutosha, naomba ufafanuzi juu ya juhudi gani za Serikali zinafanyika ili kuharakisha zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matrekta, wakulima wakopeshwe matrekta makubwa kwa madogo na hasa kwa Mikoa inayozalisha chakula kwa wingi (Rukwa). Matrekta yasogezwe karibu na wakulima, yapelekwe katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku iwafikie mapema wakulima na itolewe kwa mazao yote kama mahindi, alizeti, mtama, ufuta, mpunga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mawakala wa pembejeo walipwe fedha zao. Ni kitendo cha aibu Serikali kutowalipa mawakala wa pembejeo mapema kwani wao walishatoa huduma, tatizo ni nini? Naomba Serikali itakapolipa madeni hayo, walipe na riba

wanayodaiwa na taasisi za fedha maana Serikali ndiyo imewasababishia riba hiyo kwa kuchelewa kuwalipa fedha zao.

Mheshimiwa Spika, bei za mazao zieleweke mapema kabla ya msimu wa kilimo kuanza ili mkulima aweze kuamua zao gani alime kwa kuwa na uhakika na faida baada ya kutoa gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, janga la njaa, kutakuwa na upungufu wa chakula katika Tarafa ya Kipeta, hii ni kutokana na kukatika kwa mvua mapema na kusababisha mazao kukauka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji katika kilimo, kabla Serikali haijawekeza ingalie kwanza utoshelezi wa eneo la kulima wananchi katika eneo husika. Kumekuwa na migogoro mingi inayojitokeza kutokana na wakulima wazalendo kukosa eneo la kulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa. Muda unaotumika kutoa mafunzo ni mfupi sana hivyo muda uongezwe. Mafunzo yatolewe hadi ngazi ya chini kwa Wenyeviti wa Vijijini, Wenyeviti wa Vitongoji na Watendaji wa Vijiji.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuliona tatizo la Mabaraza ya Kata na kutoa mapendekezo mazuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za nafasi za watendaji wa Kata na Vijiji, zipo Kata na Vijiji ambavyo havina Maafisa hao katika ngazi hizo. Nafasi hizo

zitajazwa lini maana hata nafasi za kazi zilizoelezwa na Serikali sijaona ajira ya Maafisa hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi nitaunga mkono hoja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema inayoniwezesha kushiriki michango mbalimbali katika Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kubwa kwangu aliyoionyesha kupitia uteuzi wake kwangu wa Ukuu wa Wilaya ya Muheza. Naaahidi kuchapa kazi kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa fursa hii, naomba nipongeze hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na naunga mkono hoja hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa utendaji wake wa kazi. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu na watendaji wote kwa uandaaji wa hotuba hii ambayo imejumuisha mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nielekeze mchango wangu kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni uwezeshaji wananchi kiuchumi. Napongeza jitihada zote zilizochukuliwa katika suala zima la uwezeshaji

wananchi kama inavyoonekana katika ukurasa wa 20 wa Kitabu cha Hotoba ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, naomba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika kuhakikisha kuwa sheria ya kutenga asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri zetu kwa ajili ya kuchangia Mifuko ya Wanawake (asilimia tano) na Vijana (asilimia tano) ili kukopesha makundi hayo ili waweze kufanya shughuli za uchumi na kujiletea maendeleo. Hali ilivyo kwenye Halmashauri mbalimbali hapa nchini, ni ukiukwaji wa sheria. Kiasi kinachotengwa hakikidhi hitaji la asilimia kumi ya mapato yote ya ndani.

Mheshimiwa Spika, pili, sekta za uzalishaji, kilimo. Napongeza jitihada zote za Serikali kuhakikisha sekta za uzalishaji zinatimiza wajibu wake wa kumtetea mwananchi maendeleo kama ilivyoelezwa kwenye ukurasa wa 22 wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hata hivyo, naiomba Serikali ivitazame Vyuo vya Kilimo hasa vinavyohusiana na masuala ya utafiti. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuelekeza kuwa asilimia moja ya Pato la Taifa litengwe kwa ajili ya shughuli za utafiti. Pamoja na maelekezo hayo, utekelezaji wa maelekezo hayo ni wa kusuasua. Baadhi ya Vyuo vya Utafiti wa Kilimo vina hali mbaya sana. Mfano Chuo cha Utafiti wa Kilimo Mlingano kilichopo Wilaya ya Muheza Mkoa wa Tanga. Kati ya maombi ya chuo hicho ya shilingi milioni mia tatu (300,000,000) kwa ajili ya shughuli za utalii ni kiasi cha milioni thelathini (30,000,000) zilizopelekwa kwenye chuo hicho mpaka tarehe 16 Juni 2012. Hali ya vyuo hivyo ni mbaya sana. Pia naiomba Serikali iwatazame

sana wataalam watafiti wa vyuo hivyo, wengi wa watafiti hao ni watu wazima, kutokana na maslahi duni hakuna vijana wanaojiunga na vyuo hivyo vya utafiti. Kwa kuboresha maslahi ya watafiti hasa wa eneo la kilimo itavutia vijana kujiunga na Vyuo vya Kilimo hasa vinavyoshughulikia utafiti.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa uagizaji wa pembejeo na zana za kilimo kupitia SUMA JKT, matrekta makubwa 1,860 na zana zake, matrekta madogo ya mkono 400 na pampu za umwagiliaji 1,100. Ni wazi uingizaji wa zana hizi za kilimo zitapelekea uhitaji mkubwa wa mafundi wa kutengeneza zana hizo. Naishauri Serikali kusaidia Chuo cha Kilimo Mlingano, Muheza Tanga, ni chuo pekee kinachotoa kozi inayohusiana na matengenezo ya zana za kilimo. Wahitimu wa kozi hii watasaidia sana kutengeneza zana hizo za kilimo ili ziweze kutumika kwa muda mrefu. Utoaji wa kozi hii unaathiriwa sana na ukosefu wa vitendea kazi vya kujifundishia. Hakuna kabisa zana yoyote ya kilimo isipokuwa *powertiller* moja tu, hivyo wanafunzi wanafundishwa kinadharia tu.

Mheshimiwa Spika, tatu, mafunzo ya ufundi stadi. Naishukuru sana Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi – *VETA* Kongowe kilichojengwa Kibaha. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuja kutufungulia Chuo hicho na hotuba aliyotoa ambayo ilituelekeza viongozi wakiwemo viongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa vijana wengi ndani ya Mkoa wa Pwani wanapata fursa ya kukitumia Chuo cha *VETA* Kongowe Pwani.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa na naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Nchi kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kutoa mawazo yangu kwa njia ya maandishi katika hotuba hii ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb). Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, shukrani na pongezi za dhati pia nazitoa kwa Waziri Mkuu kwa kuwakumbuka Madiwani kwa kuwaongezea posho kwa 100%. Hakika hali hii itaongeza ufanisi makini kwa Madiwani katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusikia kilio cha Watanzania wanyonge wanaotaabika katika lindi la umaskini kwa kupunguza na kubana matumizi ya Serikali. Ni ukweli usiopingika kuwa kuna matumizi mabaya sana ya fedha za umma katika uhujumu wa fedha za umma. Kwanza kabisa, kuna rushwa kila kona ya nchi! Kuna rushwa katika Halmashauri zetu. Kuna rushwa katika Mashirika ya Umma! Kuna rushwa katika taasisi zetu! Kila kona kuna harufu ya rushwa. Hata TAKUKURU kwenyewe kuna rushwa. Hali hii inasababisha kukosekana kwa haki na usawa kwa watu maskini.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba uendeshaji wa mashangingi katika Wizara, Taasisi, Mashirika, Halmashauri na kadhalika huigharimu sana Serikali. Kwa mfano shangingi moja linanunuliwa kwa Sh. 300,000,000, gharama ya kuliendesha kila mwezi si chini ya Sh. 1,000,000/= na kulipeleka gereji ndiyo usiseme. Kwa hakika hali hii ilikuwa inaligharimu sana Taifa. Hivyo, kitendo cha Waziri Mkuu kutangaza/kuutangazia umma kuwa Serikali itaangalia magari mbadala, ni dhahiri kuwa Serikali imedhamiria kupunguza na kubana matumizi ya Serikali. Nashauri magari haya yauzwe kwa Watanzania watakaohitaji ili fedha zitakazopatikana zipelekwe kwenye shughuli ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu kwa kulinganisha na hali halisi ya Wilaya ya Tarime. Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Watendaji walioko chini yake, wanagusa maisha ya kila Mtanzania hasa wa hali ya chini kama wakazi wangu wa Tarime, tafadhali ninayoyaandika hapa, naomba yazingatiwe na kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, suala la miundombinu mibovu ya barabarani Wilayani Tarime si ya kuridhisha. Kwanza Barabara ya Nyamwaga Road inayoanzia Tarime – Nyamwaga – Nyamongo hadi Mto Mara yenye urefu wa km 53 haijawekewa lami ingawa kuna ahadi kemkem. Naiomba Wizara iingilie kati suala hili. Naomba nijulishwe ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami? Hii ni barabara muhimu kwa

uchumi wa Mkoa wa Mara. Pia itasafirisha watalii wengi wanaotoka Kenya kuelekea Serengeti.

Mheshimiwa Spika, pili, ahadi ya Waziri Mkuu kuipandisha hadhi barabara ya Mangucha – Misanga – Katewasi – Gibaso hadi Mrito kuwa barabara ya Mkoa. Ahadi hii itatekelezwa lini kwani taratibu zote zimekwisha kukamilika.

Mheshimiwa Spika, tatu, madaraja mawili ya Kyoruba na Mori ambayo yalijengwa na Wakoloni na baadaye yakaharibika, yamekuwa ni kero kubwa sana kwa wakazi wa Tarime. Ifahamike wazi kuwa Halmashauri haina uwezo wa kujenga madaraja hayo. Hivyo, naomba Waziri Mkuu kupitia Wizara ya Ujenzi isaidie kutujengea madaraja haya.

Mheshimiwa Spika, nne, barabara ya *security road* iliyoko mpakani mwa Tanzania na Kenya, kwa nini haipitiki muda wote? Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina mpango wa kuiwekea lami barabara hii?

Mheshimiwa Spika, suala la umeme wa *REA* Wilayani Tarime. Nianze kwa kutoa shukrani kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuvipatia umeme vijiji vifuatavyo: Nyamwigura – Kemakorere – Nyerere – Rozana – Nyamwaga – Keisangura – Tagare – Muriba – Kumwika – Kobori – Itiryo na Getena. Ombi langu ni kwamba gharama za kuweka umeme zipunguzwe ili wananchi wengi waweke umeme kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Waziri Mkuu kukipatia umeme kijiji cha Maanga hasa kwenye kile kituo cha Kurya *Cultural Centre*, naomba ahadi hii itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *REA* katika vijiji vya *Security Road* toka Rorya – Susuni – Kubiterere- Remagwe – Gwitryo – Nyabisaga- Borega- Gonyange – Kimusi – hadi Nyantira. Umeme huu ni muhimu ili kuongeza uzalishaji na hivyo kuongeza kipato kwa wakazi wa Tarime. Namwomba Waziri Mkuu asaidie.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *REA* katika vijiji vya Nyakunguru – Kibasuka – Kembwi – Manga hadi Komaswa. Umeme huu unaweza kuunganishwa na ule wa mgodi wa *North Mara* (Nyamongo).

Mheshimiwa Spika, mradi wa *REA* katika vijiji vya Kata za Nyandoto, Susuni, Mwema, Bumera, Gorong'a, Kiore, Gibaso na kadhalika nao ushughulikiwe ili kuwasaidia wananchi wa Tarime kujishughulisha na shughuli za uzalishaji mali. Ni imani yangu kuwa watakuwa na uwezo wa kulipia luku na gharama nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini hasa dhahabu ya North Mara (Nyamongo), naomba Waziri Mkuu anijibu swali hili kwa uhakika. Wananchi wa Tarime wanalalia dhahabu, wanakalia dhahabu, wanatembea juu ya dhahabu lakini wanakabiliwa na umaskini wa kutupwa, kwa nini? Je, ni ujinga na upumbavu wa wakazi wa Tarime? Je, ni Serikali imeshindwa kutoa fursa kwa wananchi wa Tarime ili wafaidi rasilimali hiyo? Tujiulize, nini kifanyike? Kwa nini

Serikali isiwashirikishe wawekezaji ili kuimarisha miundombinu ya barabara Wilayani Tarime? Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba tufikiri kwa makini! Tufikiri kwa makini zaidi! Nasisitiza hatuwezi kukubali wawekezaji wanafaidi dhahabu yetu lakini wananchi wetu wanaambulia umaskini wa kutupwa pamoja na mahandaki ya mashimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kizuizi cha Magena, nina hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu anakifahamu vizuri kizuizi hiki. Je, kina faida gani kwa wananchi wa Tarime? Je, anafahamu kuwa kizuizi kile ni mradi wa Polisi? Anawaahidi nini wananchi wa Tarime kuhusu kizuizi hicho? Au wananchi wa Tarime watumie nguvu kukiondoa? Mkuu wa Mkoa wa Mara, John Tuppa anamshauri nini juu ya kizuizi hiki? Mkuu wa Wilaya ya Tarime, John Henjewele anamshauri nini juu ya kizuizi hiki?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mkoani Mara, iitwayo Mwalimu *Nyerere Memorial Hospital* itaanza lini na kukamilika lini? Mheshimiwa Waziri Mkuu anafahamu kuwa Serikali ya Awamu ya Nne itapata heshima Mkoani Mara kwa kuijenga hospitali hii. Nashauri Serikali iwashirikishe wadau mbalimbali ili kuhakikisha kuwa hosptiali hii imejengwa na kukamilika haraka iwezekanavyo ili iweze kuwahudumia wakazi wengi wa Mkoa wa Mara ambao hawana hospitali ya Mkoa tangu enzi za Ukolini hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa uwanja wa ndege wa Magena, Wilaya ya Tarime inapakana na

nchi ya Kenya ambayo ina watalii wengi wanaoingia Serengeti kupitia Sirari nchini Tanzania. Hivyo, namshauri Mheshimiwa Waziri asimamie ule uwanja wa ndege wa Magena ulioko Wilayani Tarime ujengwe haraka ili kuwezesha ndege za utalii kutua kirahisi na hivyo kuweza kuingiza watalii wengi Wilayani Tarime na hivyo kusaidia kuchangia kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mji Mdogo wa Sirari, nina swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, ahadi yake ya kuufanya Mji Mdogo wa Sirari kuwa Mamlaka ya Mji imefika wapi?

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji safi na salama katika Mji wa Tarime ni la muda mrefu, tangu enzi ya ukoloni, uhuru hadi sasa. Mji wa Tarime una mto mkubwa wa Mara na pia upo karibu na Ziwa Victoria, kwa nini unakabiliwa na tatizo la maji? Hivi kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu inaingia akilini kuwa maji yanatoka Ziwa Victoria hadi Shinyanga karibu takribani umbali wa km 500 na kuacha Mji wa Tarime takriban umbali wa km 30? Je, hii ni sawa? Je, Wakurya wa Tarime wameikosea nini Serikali za Awamu zote zilizopata kuiongoza Tanzania pamoja na Awamu hii ya Jakaya Kikwete? Mheshimiwa Waziri Mkuu tuzidi kuzama katika fikra.

Mheshimiwa Spika, miundombimu mibovu ya Hospitali ya Wilaya ya Tarime. Hii ni hospitali ya zamani sana na ilijengwa tangu mwaka 1942 mpaka sasa hakuna mabadiliko yoyote. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa kauli gani ya uhakika juu ya aibu hii?

Tunaelekea wapi au tuna utani na wananchi wa Tarime?

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ardhi Tarime, kwa nini hati za kimila hadi sasa hazijatolewa Wilayani Tarime? Mheshimiwa Waziri Mkuu anafahamu wazi kuwa mapigano ya mara kwa mara yanayotokea Wilayani Tarime pamoja na mambo mengine yanasababishwa na suala la umiliki wa Ardhi – Fikiri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za Rada, naungana na Wabunge wenzangu kuwa fedha zote za Rada zinunue madawati hapa nchini, Zanzibar ipate mgao, fedha Sh. 30,000,000,000 toka Canada ndizo zinune vitabu. Halikadhalika vifaa vya elimu maalum kwa viziwi, vipofu na kadhalika viwekewe mgawo.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu nchini Tanzania, je, Sera hii ya mwaka 2010 imetekelezwa kwa kiwango gani? Je, Sera hii itatekelezeka au haitekelezeki? Je, kitengo cha *EMAC* katika Wizara ya Elimu kina manufaa yoyote katika nchi yetu? Tuzame katika fikra.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora, je, Mheshimiwa Waziri Mkuu ana taarifa kuwa Watendaji Wakuu wa Serikali na Mawaziri wa Wizara hawana ushirikiano na hali hii hupelekea ufanisi kuwa hafifu katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu Wizara zao?

Mheshimiwa Spika siungi mkono hoja hadi nipate majibu ya uhakika toka kwa Waziri Mkuu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima sina budi kukupa pole kwa majukumu mazito ya utendaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia bajeti ya ofisi hii, nataka nijikite na kutoa mchango wangu kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu maafa, ni masikitiko yangu kuona hadi leo Jiji la Dar es Salaam lina kituo kimoja ambacho magari ya kuzimia moto hukaa. Kutokana na kasi ya ukuaji wa Jiji letu la Dar es Salaam, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa kutenga maeneo mapya na kuanzisha vituo vipya ambapo magari za kuzimia moto yatakaa viwe karibu na makazi au katika maeneo ya viwanda na hata karibu na maeneo ya hoteli za kitalii ili pale majanga ya moto yatakapotokea iwe rahisi kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Spika, zao la bangi (madawa ya kulevya), wakulima wengi katika baadhi ya maeneo ambayo mmea wa bangi huota na kukua, ni kilimo chao ambacho kinawapatia riziki yao. Kwa bahati mbaya wakulima hawa mara nyingi mashamba yao huchomwa moto na wao kuchukuliwa hatua za kisheria. Napendekeza kwa Serikali, kwa kuwa nchi yetu ina wataalam wengi na watafiti au kupitia *COSTECH*, waangalie njia nyingine mbadala ya kuyachunguza majani haya aidha yasindikwe na kutoa mafuta au aina yoyote ya madawa kwa ajili ya binadamu au hata mashambani kwani ni imani yangu bangi kama itafanyiwa utafiti wa kitaalam, inaweza kuwa ni tija na ukombozi kwa baadhi ya wananchi

wetu na kuondokana na kuwasumbua wakulima hawa ambao hutegemea kilimo hicho hata kusomeshea watoto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam, kwa kuwa Wizara nyingi za Serikali ziko Dar es Salaam na Wizara hizi hutumia fedha nyingi kwa ajili ya kufanya usafi katika ofisi zao. Kwa mfano, katika *budget* ya mwaka 2012/2013 katika Idara ya Utawala, ndani ya Wizara ya Sayansi na Teknolojia wamepanga kutumia Sh. 600,000 kwa ajili ya usafi wa ofisi kwa mwezi vilevile Sh. 60,000,000 kwa ulinzi na kuzoa taka. Nashauri Halmashauri zizungumze na Wizara ili kazi hizi zifanywe na Halmashauri zetu ili kuongeza kipato kwa Halmashauri zetu kulikoni kazi hizi kupewa makampuni binafsi, makampuni ambayo mengi yao hukwepa kodi. Namwomba Mheshimiwa Waziri suala hili aliangalie kwa undani na aangalie makadirio ya matumizi ya Wizara zote katika vipengele hivi vya uzoaji taka na usafi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, katika uwekezaji wa kilimo unaofanyika nchini, tunaomba uwashirikishe vijana kwa kiasi kikubwa. Vijana wengi hawana ajira, hivyo tumaini lao pekee ni ardhi. Katika maeneo yanayofaa katika kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha kawaida, kutokana na changamoto ya ajira inayowakabili vijana, ni wakati mwafaka kwa Serikali kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya vijana ili wawezeshwe na kujishughulisha katika kilimo na kujikwamua katika tatizo la ajira kupitia kilimo.

Mheshimiwa Spika, mbali na Serikali kuendea kukabiliana na tatizo la ubadhirifu wa fedha za umma katika Halmashauri zetu bado vitendo vya ubadhirifu wa fedha katika Halmashauri zetu unaendelea. Mbaya zaidi watu wanaofanya ubadhirifu badala ya kuchukuliwa hatua wamekuwa wakihamishwa katika vituo vingine.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ina mkakati gani wa kuhakikisha Serikali inakuwa na vyanzo vingine vya mapato ya ndani ili kuepuka utegemezi wa wafadhili ambao mara nyingi hawaleti fedha wanazoahidi kuleta na mwisho miradi mingi ya maendeleo inakwama?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri haikueleza suala la michezoni nchini na mikakati ya kuinua vipaji na kuendeleza soka nchini.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali izuie ujenzi wa nyumba za makazi katika njia kuu za mito hususani Mkoa wa Dar es Salaam ili kuzuia tatizo la mafuriko. Lakini pia maeneo ya Mabwepande walikopelekwa vilikuwa ni viwanja vilivyotolewa fomu na wananchi wakatoa pesa kuchukua fomu, leo hii vimegawiwa kwa tatizo lingine lililojitokeza, nini hatma ya wale waliochukua fomu za Serikali na kulipia lakini mchakato mzima haujafanyika?

Mheshimiwa Spika, pili, maji yamekuwa tatizo kubwa sana Mkoa wa Kigoma, bei imepanda kutoka shilingi 6,500 hadi shilingi 17,500 na watu wa Mkoa wa Kigoma hali yao ya kiuchumi si mzuri hivyo imekuwa kikwazo kwao. Tunaomba muwasaidie wananchi hawa ili maji isiwe ni biashara bali iwe huduma.

Mheshimiwa Spika, tatu, katika uwekezaji kumekuwa na tatizo la ulipwaji wa fidia hususan Mkoa wa Kigoma, Manispaa ya Kigoma Ujiji, kumekuwa na uchakachuaji katika fidia za wananchi. Kwanza kabisa, kanuni za fidia hazifuatwi, zile siku ishirini na moja za kubandika thamani ya awamu ya kwanza ili wananchi waone kama fidia zipo sahihi hazikubandikwa. Hivyo wakati wa fidia kulikuwa na malalamiko mengi kwamba baadhi ya mashamba makubwa, viwanja, mimea havikuorodheshwa na ofisi ya Mkoa haikuonyesha ushirikiano wowote wa kusikiliza dhuluma kwa wananchi hawa. Sasa mwaka huu wananchi hawatakubali, tunaomba haki itendeke.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, kwanza natanguliza pongezi kwa hotuba ya Waziri Mkuu kwani imejitosheleza. Nachoomba ni utekelezaji kwa vitendo ili azma ya Waziri Mkuu iweze kukidhi haja ya Watanzania.  Naomba kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo kwa kutoa maoni.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nashauri Wilaya mpya ambazo zinaenda kuanza sasa pamoja na Mikoa mipya ianze kujengwa kwa utaratibu mzuri wa miji iliyopangwa.  Maafisa Mipango Miji wajitahidi kupanga ili kuepuka ujenzi holela na baada ya muda kuanza

kubomoa nyumba za watu na kupoteza fedha nyingi kwa kulipa fidia. Ningefurahi zaidi kuona Wilaya mpya ya Mkalama inajengwa kwa *plan*.

Mheshimiwa Spika, pili, Makao Makuu ya Wilaya ya Mkalama (Nduguti) hakuna miundombinu ya maji, umeme na kadhalika, naamini Serikali itapeleka huduma hizo haraka. Pamoja na hayo, napenda kushukuru kwa kupatiwa Wilaya mpya za Ikungi na Mkalama.

Mheshimiwa Spika, tatu, Mkoa wa Singida umepata bahati ya kuwa na zao la alizeti ambalo nina imani kuwa asilimia kubwa ya mafuta ya alizeti yanatoka Mkoa wa Singida hususani Wilaya ya Iramba. Zao hili limeinua sana uchumi wa kipato cha wananchi wakiwemo wakulima wakamuaji wadogo wa mafuta (viwanda vidogo) pia wenye viwanda vikubwa. Pamoja na yote pia wanunuzi/wafanyabiahsasha ambao ndiyo waliosaidia kuinua kilimo cha alizeti kwani wao huwafuata wakulima majumbani mwao na wao kupeleka kuuza kwa wenye viwanda. Ni ukweli usiopingika kuwa wanunuzi hawa wamekuwa ama wakinunua kwa bei ya makubaliano na mkulima na huenda huwapunja, lakini ndiyo walioshikilia njia ya soko la mkulima na hivyo kuinua kilimo cha alizeti na kuinua vipato vya wakulima hawa pia kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, sasa jambo la kusikitisha, Mkuu wa Mkoa alitoa amri halali ya kupiga marufuku wanunuzi binafsi wa zao la alizeti kununua moja kwa moja toka kwa wakulima na kwamba wakulima wakauze kwenye Vyama vya Ushirika na kuwa

atakayekiuka amri hii atafungwa jela miaka miwili. Mimi sina tatizo na amri hii, bali naona kama haikuja kwa wakati mwafaka, ni kama imeshtukiza. Pia maandalizi ya kuwaandaa wakulima na wadau wa zao hili hayakufanywa na elimu kutolewa. Hivyo jambo hili linaleta utata kiasi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Waziri baada ya kupitisha bajeti (hoja) hii, afanye ziara ya makusudi ili apate kukutana na wananchi/wakulima, wanunuzi binafsi, wenye viwanda vidogovidogo na wenye viwanda vikubwa bila kuacha Vyama vya Ushirika na wadau wengine.

(ii) Naomba uwekwe utaratibu wa zao hili la alizeti kuwa na Bodi ya Alizeti ili litakapokuwa linawekewa taratibu angalau zifanane na Mikoa inayolima.

(iii) Kuwe na utaratibu wa soko huria au ushindani ili Vyama vya Ushirika na Binafsi washindane kwa bei ili mkulima na wadau wote wanufaike.

(iv) Elimu itolewe kwa wakulima ili wajue faida ya kuuza kwenye ushirika.

(v) Amri iangaliwe upya ili kutoa fursa kwa wale wakulima wakubwa ambao wao wana uhuru wa kuuza moja kwa moja kwa mteja watakayemtaka au kiwandani. Wenye

viwanda vidogovidogo wapewe ruhusa ya kununua toka kwa wakulima kwani inaongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, nne, mradi wa maji wa Mwankoko Singida umekwama kuanza kutokana na *TANESCO* kutopeleka umeme ili kuwezesha mashine kuanza kufanya kazi ya kusambaza maji mjini. Naomba umeme *(TANESCO)* wapeleke umeme Mwankoko ili kuondoa tatizo la maji Mjini Singida.

Mheshimiwa Spika, tano, naomba Zilikoni inayochimbwa Luzilukulu Kata ya Ndago, ipimwe kwani inasemekana inaambatana na almasi, lakini wanunuzi huwapunja wachimbaji kwani wanawalipa kwa bei ya Zilikoni lakini kama ni Almasi hawaambiwi.

Mheshimiwa Spika, sita, *TMAA* imewekwa kufanya kazi za *TRA*, *NEMC* na kadhalika maana anakagua uwekezaji katika masuala ya kodi, kwa nini kazi hiyo isifanywe na *TRA?* Halafu anakagua mazingira, eti kuangalia mahesabu yaani fedha zinazotumika kwenye mazingira wakati kazi hiyo inatakiwa ifanywe na *NEMC*. Kisha wanakagua ukusanywaji wa mrahaba wakati kazi hiyo inatakiwa kufanywa na Makamishna wa Madini wa Kanda. Bado anaangalia uzalishaji kwenye migodi ukweli ni kwamba, kazi hiyo inatakiwa ifanywe na Mkurugenzi Mkuu aliyeko chini ya Kamishna wa Madini kwa kutumia Kanda. Kuna sababu gani za msingi za kuanzisha taasisi ya kufanya kazi za wengine na ambazo ziko kisheria? Hii ni matumizi mabaya ya fedha. Napendekeza wataalamu waliopo *TMAA* wapelekwe *TRA* na kuwe na Idara ya Ukaguzi wa

migodi tu. Pia wataalam wa mazingira wapelekwe *NEMC* ili kupunguza matumizi ya fedha na *TMAA* ivunjwe. Ianzishwe Idara ya Ukaguzi wa Uwekezaji katika migodi ili kuona kama kampuni itatakiwa kulipa kodi kiasi gani na iwe chini ya Kamishna wa *TRA* na tuwawezeshe ili kuokoa fedha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, je, ni fedha kiasi gani Serikali imeshaokoa tangu Waraka wa Kuuziwa magari watumishi wa Serikali enzi za Mheshimiwa Rais Mstaafu, Mzee Ali Hassan Mwinyi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Naomba kumpongeza Waziri Mkuu na kumpa pole kwa yote yaliyojitokeza katika kipindi hiki cha miaka miwili iliyopita na kumpongeza kwa ujasiri wake alionao kuhimili mikiki na mitihani mbalimbali ya yaliyotokea. Pili, naomba kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi nayo kwa jitihada zake kuendelea na kuhuisha uhuru wa wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa ya ukusanyaji wa mapato, bado Watanzania hawachangii, tunahitaji usimamizi thabiti wa malipo katika:-

(i) Bidhaa zinazoingia kutoka nje na kubadilisha utaratibu wa malipo kwa wafanyabiashara kulipa *"cash"* bali watumie *Bank A/C* zao kufanya malipo.

(ii) Wigo wa tozo za *taxation* upanuliwe zaidi, wafanyabiashara hasa wenye maduka, wanauza bidhaa, wanakusanya kodi – hawatoi risiti. Kwa hiyo mfumo wa mashine za *electronic* kwa watoa risiti uhamasishwe na kuwe na ufuatiliaji.

(iii) Taasisi za utalii kama vile *TANAPA*, mahoteli na nyumba za wageni, hawa nao wanapaswa wasimamiwe kikamilifu. Mfano kwenye utalii tozo zinakuwa ndogo sana au hata kukwepa kulipa kodi ndogo zinazotozwa.

(iv) Taasisi ya Fedha isimamie malipo na watalii walipe fedha za kigeni kwenye asasi zinazowatumikia, sio hilo tu bali Watanzania tuache tabia ya kutumia *'dollar"* kwenye maduka ya rejareja nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi, pamoja na kuwa Tanzania eneo kubwa tumezungukwa na maji, ama bahari au mito, au maziwa na umuhimu wa sekta hii katika uchumi wa taifa, lakini bado jitihada za makusudi zinatakiwa zichukuliwe ili sekta hii iweze kuchangia uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, baharini kuna meli nyingi za kigeni zinapora mali za Tanzania hasa bahari kuu na Serikali haifanyi jitihada za kutosha kudhibiti uvuvi huo na wanaingia na kutoka bila ya kulipa malipo stahili. Taasisi hii nayo ichunguzwe vya kutosha na watakiwe kulipa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo mengine ya jumla, tunaiomba Serikali izidishe usimamizi kwenye matumizi hasa kwenye Halmashauri zetu. Naomba kutoa rai kuanzia sasa Serikali itoe tamko au itunge sheria ya pale *AG (Auditor General)* anapotoa ripoti yake kwa Bunge ya upotevu na utumiaji mbaya wa fedha za Serikali basi ripoti hiyo iwe ni kielelezo cha moja kwa moja na uwe ni ushahidi wahusika wakajibu hoja hizo Mahakamani. Kesi hizi ziwe za aina yake na zishughulikiwe katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja. Kwa usimamizi mzuri, maamuzi ya hatua zilizojitokeza za kimahakama ziwasilishwe Bungeni kabla ya mwaka wa fedha unaofuata. Nadhani utaratibu huu ungeambatana na vilevile na kesi zinazohusu wahujumu uchumi (akina TAKUKURU), kesi za wanaoingiza/kusafirisha unga (mihadarati), wanaohujumu nyara za taifa (wezi) kama vile pembe za ndovu na wanyama kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nguvu zake zote aangalie suala la kilimo cha pamba na viwanda, kilimo cha korosho na viwanda, madini na mikataba, ardhi na ugawaji wake na suala la masoko ya bidhaa mchanganyiko hasa mahindi, mchele na zaidi kilimo cha miwa na sukari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Idara ya Uratibu wa Maafa ya Tanzania Bara kwa ushirikiano wa kazi wa karibu na Idara ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar na naziomba Serikali

zote mbili ziendeleze ushirikiano huo katika kuratibu maafa.

Mheshimiwa Spika, imekuwa kawaida kunapotokea majanga au maafa hasa ya chakula cha njaa, hakuna mpangilio au utaratibu maalum unaofanyika katika kufanya tathmini. Je, ni nani hasa anayetakiwa kufanya tathmini ya upungufu wa chakuka katika Mikoa? Pia kuna malalamiko kwamba utaratibu wa upelekaji wa chakula cha maafa au njaa umekuwa si mzuri. Je, ni nani hasa anayetakiwa kusambaza chakula hicho au utaratibu gani unatumika? Tunafahamu kuwa Idara ya Kuratibu Maafa imeshatayarisha Mpango wa Taifa na Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa *(Emergency Preparedness and Response Plan - EPRP).* Je, ni lini mpango huu utaletwa Bungeni kwa Wabunge ili waweze kuujua na kuuchangia? Pia ni lini Watanzania wakiwemo Wanahabari wataelimishwa juu ya mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maelezo tokea bajeti ya mwaka 2010/2011 na pia mwaka huu 2012/2013 kuhusu kukamilika maandalizi ya Sheria mpya ya Menejimenti ya Maafa na Sera husika. Naomba sasa kupitia Idara hii kuharakisha Sera na Sheria ya Maafa ili iweze kutumika kwani kuna mkanganyiko wa shughuli yanapotokea maafa kutokana na kukosekana miongozo na kanuni ya nani afanye nini *(Distribution of Responsibities).*

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii nichangie katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya, Mwenyezi Mungu ambariki. Pili natoa pongezi kwa Waziri wa TAMISEMI, Naibu wote wawili pamoja na Mawaziri wote na viongozi wote waliohusika na bajeti hii nzima. Naomba Mwenyezi Mungu bajeti ipite bila matatizo kusudi kazi za kuleta maendeleo Mikoani zianze mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo mmoja naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, takriban asilimia 75 ya wananchi wanaishi vijijini na wananchi hawa wanategemea kilimo. Nashukuru Serikali kutoa kipaumbele kwa kilimo, Serikali inajali wananchi wake. Ombi langu na ushauri, ni kuhusu pembejeo. Naomba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, iweke mkakati na mpango ulio wazi, kusudi vocha ziletwe Mikoani kwetu mapema. Pembejeo zifike kwa wakati kwa walengwa/ wakulima.

Mheshimiwa Spika, bado nazidi kutoa ombi kwa niaba ya wakulima, hususan wa Iringa na Morogoro kuwa wanufaika wa ruzuku, wananchi waongezeke. Hii itasaidia uzalishaji zaidi kwani wanufaika watakuwa wengi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya tabia nchini, Mkoa wa Iringa umegawanyika katika sehemu yenye ukame na sehemu zingine zenye mtawanyiko wa mvua ya kutosha. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ruzuku kwa mbegu za mtama mweupe pamoja na alizeti. Mwaka huu 2011/2012 sehemu hizi tumelima mtama kidogo na alizeti. Wananchi baadhi yao wamevuna, wengine wamevuna kidogo, kutokana na ukame au wengine walilima sehemu ndogo (mtama) kwani ilikuwa ni mwanzo wa kilimo hiki.

Wananchi hawa wakipatiwa ruzuku ya mbegu za mtama na alizeti, watakuwa wamepata chakula, wataacha kuomba chakula cha kila mwaka na watapata pato la kutosha. Lishe bado ni tatizo katika Mkoa wa Iringa. Kwa hiyo, kutokana na mavuno mazuri ya mtama na mahindi sehemu yenye mvua ya kutosha, wananchi watapata chakula cha kutosha, watapata lishe nzuri na wataendelea kufanya kazi zao za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro na Iringa kilimo cha umwagiliaji ni muhimu. Hasa Mkoa wa Iringa bila ya umwagiliaji, hakuna kilimo. Fedha za umwagiliaji hasa fedha za *DADPS,* naomba zifike kwa wakati bila kuchelewa, kusudi wananchi/wakulima wengi wanufaike na kilimo cha umwagiliaji kwa mwaka mzima hasa katika kilimo cha mpunga na mbogamboga.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine chini ya kilimo ambalo naiomba Wizara ni kuhusu utafiti wa udongo. Kwa urahisi, kwa sababu kuna tafiti ambazo zilishafanyika katika Mikoa yote, taarifa za tafiti ziletwe Mikoani kwetu. Tafiti zinaoonyesha hali ya udongo, aina na kiasi gani cha mbolea kitumike na mazao gani yastawishwe. Hii itasaidia kulima mazao sahihi kufuatana na aina ya udongo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zana za kilimo, napenda kutoa shukrani zangu kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwajali wananchi wake kuhusu zana za kilimo. Bei ya matrekta imepunguzwa ili kuwasaidia wakulima wapate kununua zana hizi. Licha ya Serikali kupunguza bei, lakini bado bei iko juu. Bei kuwa juu pia ni kwa pembejeo na hasa mbolea. Wakulima wanaomba bei ya pembejeo hususan mbolea pamoja na matrekta zipunguzwe kusudi wananchi wapate unafuu na uwezo wa kununua zana hizi. Ni vyema zana hizi zinunuliwe kusudi zitumiwe na wananchi katika kuzalisha mazao hususan mazao ya chakula (mahindi na mpunga).

Mheshimiwa Spika, kwa mazao yatakayonunuliwa na *(NFRA)* baada ya kuvuna, ombi langu ni kuwa bei hii elekezi itolewe mapema. Jambo hili litasaidia wananchi kupata msukumo wa uzalishaji kutokana na masoko na bei za kuvutia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali imelenga katika Kilimo cha kisasa na chenye tija. Mambo yote niliyoyataja hapo awali yakikubalika na kutekelezwa, wananchi wengi watanufaika, chakula kingi

kitazalishwa, pato litapanda/litakuwa, lishe kwa familia itakua nzuri, afya ya wananchi itakuwa nzuri na maisha bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Ofisi ya Waziri Mkuu na Manaibu Waziri wote, pamoja na watendaji wa ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu kama malimbikizo ya madeni ya watumishi Serikalini yatalipwa? Je, hatua gani zinachukuliwa dhidi ya viongozi kwenye Taasisi ambao wanasababisha watumishi kucheleweshewa malipo yao endapo fedha hizo zimefika kwenye taasisi mapema?

Mheshimiwa Spika, imefika wakati sasa Serikali kuleta Sheria itakayodhibiti taasisi ndogondogo za fedha (*microfinance*) ili kudhibiti shughuli zinazofanywa na Taasisi hizi. Kwani wako ambao wamekuwa wakitoza hadi asilimia 30 kwa mwezi na imepelekea wakopaji wengine kuwa mafukara kabisa.

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo madai ya wizi wa kura kwenye chaguzi mbalimbali zinazofanyika nchini. Ingawa si rahisi kuamini madai haya, lakini panapokuwa na tuhuma ni muhimu kuzishughulikia. Ili kuepuka tuhuma hizo, nashauri uanzishwe mfumo wa "*Electronic Voting system*" ambapo kitambulisho cha

mpigakura kitapotambuliwa au kuchanjwa kwenye *register* ya kielekroniki itaonesha taarifa zote za mhusika. Kidole gumba kitumike kuthibitisha taarifa hizo na ndipo mhusika ataruhusiwa kupiga kura. Utaratibu huu utasaidia kupunguza uwezekano wa kura kuibiwa au watu ambao hawajaandikishwa kutumia vitambulisho vya wengine kupiga kura. Aidha, utaratibu huu utapunguza gharama za uchapishaji wa makaratasi na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya machache, naunga mkono hoja hii ya bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wake makini wa hotuba yake. Nawapongeza pia Naibu Mawaziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na watendaji, wataalamu na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa juhudi zao na kwa kushirikiana kuandaa bajeti ya Waziri Mkuu yenye mwelekeo mzuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuipongeza Ofisi ya Waziri ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa kazi nzuri ya kusimamia maendeleo katika Halmashauri zetu zote nchini. Kazi ni kubwa na nzito lakini Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imejipanga vizuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imedhamiria kuboresha kilimo ili tuondokane na aibu ya njaa na kuomba misaada ya chakula. Jimboni Bagamoyo tuna

tatizo kubwa la uwezeshaji mdogo katika sekta ya kilimo. Mfano, miradi yetu michache ya kilimo cha umwagiliaji haipati tengeo zuri la fedha kuwawezesha wakulima kulima kwa kiwango cha tija. Miradi hii ni ile ya *BIDP*, Kidogozero (Vigwaza) na Chauru (Vigwaza). Nashauri Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI isisitizie tengeo bora zaidi kwa ajili ya kilimo na hasa kilimo cha umwagiliaji. Wananchi wengi zaidi wangependa kushiriki katika kilimo cha umwagiliaji lakini miundombinu katika skimu hizo hairuhusu.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo tulipata kadhia ya watendaji kutuhumiwa na ubadhirifu wa fedha za umma; na mwaka 2010 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwavua madaraka, watendaji hao ni pamoja na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Cha kusikitisha, kesi za watendaji hao mpaka leo hazionyeshi dalili ya kupiga hatua yoyote. Nashauri Ofisi ya Waziri Mkuu iiombe Mahakama iharakishe usikilizaji wa kesi za watendaji wanaotuhumiwa ili haki itendeke na ili wengine wapate masomo kwa hatua za kisheria zitakazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye Rehema, ambaye ametuwezesha kufika hapa tukiwa hali ya uzima.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja katika ukurasa wa (15) katika kitabu cha Waziri

Mkuu alipoelezea uwekezaji. Katika eneo hili la uwekezaji, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awe makini sana kwani kumekuwa na wawekezaji ambao wanapenda kukwepa kodi, kitu ambacho kinaikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 29 umezungumzia viwanda, bado nchi yetu haijawekeza katika sekta ya viwanda jambo ambalo linazorotesha maendeleo ya watu pamoja na nchi. Nchi ambayo haina viwanda, wakulima wa nchi hiyo watakuwa maskini kwani wanaweza kuwa wanalima sana mazao ya vyakula lakini wanashindwa wapi wakauze mazao yao. Tumeshuhudia Tanzania ina wakulima wengi wa mazao ya vyakula kama mahindi, mchele, alizeti, kahawa, pamba na kadhalika lakini wakulima hao hawajui nani wa kumuuzia mazao yao.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 53 umegusia ajira, ajira katika nchi yetu bado ni kitendawili, hata elimu zinazotolewa nchini hazikujikita katika ujuzi zaidi ndiyo maana kila anayemaliza Chuo Kikuu anataka kuajiriwa Serikalini. Kama Serikali itatoa elimu ya ujuzi zaidi, tatizo la ajira litapungua nchini kwani kila anayemaliza Chuo Kikuu angeweza kujiajiri mwenyewe na pia kuweza kuwapatia ajira na wenzake. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aelekeze maoni yangu haya kwa Waziri wa Elimu ili aweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchangia kuhusu huduma za kifedha. Mfumo wa biashara ya ubadilishaji wa fedha za kigeni nchini umeacha mianya ya wenye Maduka ya Fedha za Kigeni (*Bureu De Change*) kukwepa kodi na kutorosha fedha za kigeni nje ya nchi. Hali hii imetokana na hali ya kuwa wanaofanya biashara hii hawalazimiki kutoa risiti kwa wateja wanaonunua au kuuza fedha za kigeni hivyo kuwepo kwa uwezekano wa kutolipa kodi *TRA*. Lakini pia wanaobadilisha fedha za kigeni hawalazimiki kutambulika na kuleta uwezekano wa kuwepo kwa *"money laundering".*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zikiwemo Afrika Kusini, Uingereza, nchi za Shengeni (Ulaya ya *Continent*) hulazimisha wanaobadilisha/kununua fedha za kigeni kutambulika kwa kutoa kitambulisho au pasi ya kusafiria na pia maduka hayo hutoa stakabadhi (risiti) ya ununuzi au mabadilishano hayo. Naishauri Serikali kuweka udhibiti kwenye biashara ya kubadilisha fedha za kigeni ili kuongeza mapato ya Serikali kwa kuhakikisha kila *transaction* imekatiwa stakabadhi. Ni vizuri mfumo wa *electronic* wa biashara unaotayarishwa na *TRA* ufike kila duka. Serikali pia iweke utaratibu wa lazima kuwa kila anayebadilisha fedha za kigeni atoe kitambulisho na kitambulisho hicho kichukuliwe nakala na mwenye duka. Hali hii itaondoa uwezekano wa wizi wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu njaa Wilaya ya Igunga. Katika msimu wa mvua uliopita haikupata mazao ya chakula kama mahindi, mtama na mpunga kutokana na mvua isiyotabirika. Tayari

wananchi hao sasa wanahemea mahindi na nafaka zingine kwa bei ya juu. Wengine na hasa wale wa vijijini wenye asilia ya ufugaji hawana chakula kabisa. Naiomba Serikali ipeleke chakula kwenye Wilaya ya Igunga ili wananchi hao wasipate madhara zaidi ya kuteseka kwa njaa.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, Tarafa ya Igurubi katika Wilaya ya Igunga hawana umeme. Upembuzi yakinifu wa mradi huo ilishafanyika, kilichobakia ni utekelezaji wake. Naiomba Serikali iharakishe umeme kwenye Tarafa hii ambapo ni kati ya Tarafa zinazozalisha pamba kwa wingi. Umeme utawawezesha wananchi wa Tarafa hiyo kuanzisha *Ginnery* kwa ajili ya kuchambua pamba. Aidha, wananchi wataweza kuanzisha viwanda vidogovidogo kwa ajili ya usindikaji wa mazao mengine na pia kuwa na karakana ndogondogo. Umeme pia utaharakisha biashara za vinywaji na machine za kusaga na kukoboa nafaka. Umeme ni nyenzo itakayoweza kuboresha maisha ya wananchi wa Tarafa hiyo. Naomba tena mradi huu uharakishwe.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwanza kuhusu suala la mafuta na gesi ya asili kutokuwa katika masuala ya Muungano. Kumekuwa na vikao vya muda mrefu ambavyo vina miaka isiyopungua 10 mpaka sasa ambavyo huitwa Vikao vya Kero za Muungano na katika vikao hivi kila siku Wazanzibari huahidiwa lakini maamuzi hayafanyiki ambapo kuna kero ambazo hazijapatiwa ufumbuzi mfano suala la mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika vitalu vilivyopo kwenye kisima cha Zanzibar, Kitalu namba 9, 10, 11 na 12 vimesimamishwa na hakuna shughuli inayoendelea mpaka sasa. Kwani kuchelewa kufanya maamuzi juu ya suala hili, ni kuliletea hasara Taifa letu kwani ni jambo la msimu na lina muda wake wakati kwa upande wa Bara shughuli za utafutaji na uchimbaji unaendelea, hivyo ni kuifanya Zanzibar kudumaa kiuchumi hususan katika suala hili. Hivyo basi Wazanzibar hawafurahishwi na jambo hili na kuazimia kupitia Azimio la Baraza la Wawakilishi kwamba jambo hili liondolewe katika Orodha ya Masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya uchimbaji na utafutaji inaingiliwa na Waziri wa Nishati na Madini, Wizara ambayo siyo ya Muungano na hakuna hata eneo ambalo lipo chini ya himaya ya Wazanzibar na kuwekewa taratibu kuwa mikataba isainiwe na Mawaziri kutoka katika pande zote za Muungano. Pendekezo, mikataba pia iseme wazi kuwa itasainiwa na Mawaziri wa pande mbili za Muungano na kampuni inayofanya utafiti itatoa taarifa za utafiti sawia kwa Mawaziri wote kwa mujibu wa vipengele vya mkataba.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la muda mrefu, eneo la uchimbaji na hasa kugawana mapato ya mafuta na gesi lisimamiwe na kila upande wa muungano kivyake. Pia biashara ya mafuta isiwe jambo la muungano na hivyo kila upande wa muungano uwe na Shirika lake la Mafuta na Gesi Asilia ambalo litashiriki kama mbia wa Mashirika ya Kimataifa katika uchimbaji, usafirishaji na uuzaji wa mafuta na

gesi asilia kwani mafuta kuwa jambo la muungano halafu kusimamiwa na Shirika la Tanganyika na Wizara ya upande mmoja wa Muungano ndiyo chanzo cha mgogoro na suluhu sio *TPDC* kuwa Shirika la Muungano bali kila upande upewe uhuru wa kusimamia uchimbaji, biashara na mlolongo mzima wa tasnia ya mafuta isipokuwa utafutaji. Pia shughuli za utafutaji kwenye vitalu vyenye mgogoro ziendelee haraka zaidi bila ya kupoteza muda, ziendelee mara moja. Katiba mpya inapaswa kutoa uamuzi wa mwisho katika suala hili kama ambavyo tulivyoeleza katika hotuba ya Kambi ya upinzani.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, hali ya Zanzibar sio nzuri kwa ujumla kwani imekuwa ikionekana kuwa fujo zote hizo chanzo chake ni Uamsho. Naishauri Serikali na kumwomba Waziri Mkuu kwamba ipo haja ya Serikali kukaa na watu wa Uamsho na kuwasikiliza nini wanataka ili kutatua matatizo na pia kuleta hali ya utulivu kwani kutumia Jeshi la Polisi kwa kutuliza fujo bila ya kuwasikiliza wananchi nini wanataka sio jambo la burasa. Kwani matokeo yake ni fujo, vurugu na watu kuuwana na kuteseka bila ya sababu mfano wiki iliyopita katika Msikiti wa Mahonda Askari walivamia watu katika nyumba ya ibada na kuwapiga mabomu na wengine kujeruhiwa sio suluhisho kutumia nguvu katika kutaka kuleta amani bali naishauri na kuitaka Serikali kukaa kitako na watu wa Uamsho na Wazanzibar kwa ujumla kwa kuwasikiliza ni nini wanahitaji na kukipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa Zanzibar kumekuwa na

malalamiko makubwa kwa wananchi hususan wa Pemba walioko jirani na *Mecy* ya Jeshi ambayo inaonekana ni tatizo kwa *Mecy* hiyo kuwa katikati ya makazi ya watu. Imekuwa kero kubwa kwa wananchi waishio jirani na eneo hilo kwa kupiga muziki kwa kupitiliza na kujisahau kuwa wapo watu katika maeneo hayo. Mfano mzuri wiki iliyopita kuna mtoto amepigwa na Askari wa Jeshi la Polisi na mpaka sasa yupo katika Hospitali ya Rufaa ambapo ni kinyume na Sheria za Haki za Binadamu ambazo huzuia kufanya hivyo. Ili kuondoa uhasama kati ya wananchi na JWTZ ni kuitaka Serikali iamuru hiyo *Mecy* ya Jeshi irudi au iwe ndani ya Kambi yao ya Alhamisi iliyopo Matrekta (Machomane).

Mheshimiwa Spika, suala la nne ni kuhusu *master plan* ya *industrialization.* Kuboresha viwanda na kufufua viwanda vyetu vya ndani na kufanya hivyo kutapelekea wakulima kupata nguvu na mori wa kuzalisha kwa wingi ili kupata mazao ya kutosha, ya chakula na *raw material* katika viwanda na kufanya hivyo kutapelekea wananchi wengi kuwa na mapenzi na kilimo na kuzalisha kwa wingi ili kupata *raw materials* katika viwanda. Pia uzalishaji ukiwa mwingi na viwanda vikafanya kazi vizuri na kuzalisha kwa wingi tayari tutakuwa tumetoa fursa za ajira kwa vijana *direct* na *indirect* na pia waliosoma na wasiosoma nao kuweza kupata ajira kupitia viwanda na hata katika sekta ya kilimo, kufanya hivyo tayari tutasaidia vijana kupata ajira.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mungu kwa zawadi ya uzima hadi

nimeweza kuchangia kwa maneno na kwa maandishi hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa 100% kwa sababu ina majibu yote ya maswali mengi ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuzungumzia tatizo la maji Geita, ni tatizo la muda mrefu sana, inashangaza kuona Serikali imekuwa ikitoa ahadi tu kisha inakaa kimya. Naomba Serikali itoe zile shilingi 9.5 bilioni ambazo iliahidi kuzitoa kusudi mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria uanze mara moja. Mradi huu ni wa jumla ya shilingi 15.3 bilioni ambao utaleta maji Geita, ambapo shilingi 6.99 zitatolewa na *GGM*. *GGM* tayari imeshatoa pesa hiyo kwa upande wake kwa nini Serikali inashindwa kutimiza ahadi hii?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itenge maeneo ya wachimbaji wadogo ili kuongeza ajira kwa vijana na kupunguza malalamiko yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, naomba uwekwe utaratibu mzuri kwa makubaliano kati ya *GGM* na Serikali wa kuwapatia wananchi wa Geita Magwangala ambayo yanasemekana yana mabaki ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Serikali iweke utaratibu wa kuongea na *NGOs* hapa nchini kwani naamini mchango unaotolewa na asasi zisizo za kiserikali ni mkubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Hivyo si vizuri kuziacha zifanye kazi bila hata mwongozo na ushauri wa jinsi gani zitafanya kazi vizuri. Naomba

pia *NGOs* zipatiwe msamaha kwa asilimia 80 badala ya asilimia 20 iliyopo sasa, kwani misamaha hii ya kodi itasaidia kuwatia moyo wahisani kuzidi kututumia misaada zaidi kwa kuamini mizigo wanayotutumia tunaweza kuitoa bandarini kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja hii mkono, ahsante.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba Waziri Mkuu afikirie yafuatayo kwa Mkoa wa Kilimanjaro:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, wakati wa mdororo wa uchumi mwaka 2009/2010, Serikali iliahidi kufidia *KNCU* shilingi bilioni 1.3 ili ifidie madeni waliyokuwa nayo kwenye Benki ya *CRDB*. Fedha hizo hazikutolewa hadi leo.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa bei ya kahawa imefika shilingi 10,200 kwa kilo katika Soko la Dunia, naomba yafuatayo:-

(a) Serikali iangalie makato yanayokatwa katika kila kilo ya kahawa. *KNC* inakata Sh.40 kwa kilo na Bodi ya Kahawa inakusudia kukata Sh. 9 kwa kilo.

(b) Serikali ipunguze gharama ya kuzalisha kahawa kwa kuimarisha *TACRI* na fedha nyingi zitolewe kwa *TACRI* ili waweze kuzalisa miche mingi ya kahawa na kupambana na magonjwa sugu.

(c) Serikali iangalie sera yake badala ya kuwauzia walanguzi kahawa mbichi, wanachama wahamasishwe kuvuna kahawa yao wao wenyewe, waipukuchue wao wenyewe, waianike wao wenyewe na waiuze wao wenyewe kama wanavyofanya katika Vyama vya Msingi vya *Mwika North East – Lole, Mwika Msae Company Society, Kirua Vunjo West Company Society na Kibongoto Wauri Company Society.*

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba Waziri Mkuu achunguze jinsi viongozi wa Wilaya ya Moshi wamekuwa ni madalali wa kupora na kuuza ardhi ya wananchi Vunjo. Maeneo yenye mgogoro na wananchi ni:-

(i) Himo Mieresini. Eka zaidi ya 100 zinadaiwa kutolewa kwa wananchi waliohamishwa kwenye maporomoko ya mto. Naomba Serikali ifuatilie kwa majina watu hao waliopewa eneo hilo. Aidha, naomba kujua kwa nini maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali, Mahakama, Benki, Kituo cha Posta, Shule za Msingi na Sekondari (*Form Six*) wanapewa watu binafsi ambao tayari ni matajiri?

(ii) Kahe Mawala. Kuna mgogoro mkubwa kati ya wakulima na wafugaji. Aidha, kuna mgogoro kati ya viongozi madalali waliojimilikisha ardhi yao na nyingine kupewa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, nne, Mahakama Kuu ya Tanzania Moshi katika Kesi Na. 3 ya 2005 inayowahusu Masista wa *Holy Spirit Sisters* Marangu dhidi ya wavamizi kwenye shamba lao lililopo Sanya Juu. Naomba hukumu hiyo itekelezwe kwani ni ya tangu 2008.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata fursa ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza niseme naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo yaliyopo Mkoa wa Shinyanga, naomba sana kwenye huduma ya afya, Serikali iweze kutuangalia kwa macho mawili. Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga inakabiliwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa na hii ni kutokana na kwamba Wilaya tatu hazina Hospitali za Wilaya. Wilaya hizo ni Kishapu, Halmashauri ya Wilaya Shinyanga na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Halmashauri ya Kishapu ina Vituo vya Afya vinne (4) kwa Kata 20 na hawana hospitali ya Wilaya hivyo kulazimika kwenda Hospitali ya Mkoa. Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ina Vituo vya Afya vinne na ina Kata 26. Hivyo, wagonjwa wote hulazimika kwenda hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Shinyanga imeanzisha ujenzi wa Vituo vya Afya vingine vinne, Zahanati 14 na Hospitali ya Wilaya ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi kwenye Hospitali hiyo ya Wilaya ambayo ina majengo yafuatayo – *OPD*, nyumba moja ya mtumishi na misingi ya nyumba nne za watumishi, wodi ya wanawake,

wodi ya watoto na wodi ya wanaume. Naishauri Serikali iwaunge mkono wananchi hawa ambao kwa makusudi mazima wameanzisha ujenzi huu kutokana na namna wanavyopata tabu. Serikali haioni kuyaacha majengo haya bila kuyamalizia kunawakatisha tamaa wananchi hawa? Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ina vituo vitano (5) vya afya ina Kata 55. Hospitali ya Wilaya wanayo. Namwomba Waziri Mikuu akiwa anajibu aniambie anafikiria nini kuhusu Hospitali ya Mkoa Shinyanga na Wilaya zake ili tuweze kuwanusuru wagonjwa wanaopoteza maisha kwa kuwa mbali na huduma ya afya?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye udhibiti wa matumizi ya Serikali na napenda kujikita katika ubadhirifu wa fedha ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anafanya majumuisho aweze kuniambia Kamati za *Auditing* ndani ya Wizara, Halmashauri na Mashirika ya Umma zina kazi gani na zina nguvu kiasi gani? Hoja yangu ni kwamba hawa *Chief Internal Auditors* wawe wanaripoti ndani ya Kamati za *Auditing* ambazo zipo ndani ya Wizara, Halmashauri sababu kitendo cha *CIA* kuripoti kwa Makati Wakuu, Wakurugenzi wao, naona kinawanyima uhuru wa kufanya kazi vizuri na matokeo yake mianya ya rushwa inakuwa mikubwa sababu kunakuwa na kuogopana,

wakati *CIA* ni chanzo kikubwa cha kuibua ubadhirifu wa fedha ndani ya Idara zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, tunapokuwa kwenye mazingira ya *campas*, mahusiano ya kujamiana yanakuwa ya karibu na tumeona kwamba maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI yameongezeka. Hivyo naishauri Serikali na Viongozi wa Vyuo kuendelea kwa kasi kuweka mazingira wezeshi ya kupata elimu na fursa ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI kwa ajili ya vyuo kwani waathirika wakubwa ni vijana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake nyingi kwetu, naomba niishukuru Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushughulikia masuala yanayowagusa wananchi kupitia TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi Tanga ilikuwa ni mhimili wa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi, kielimu na kisanaa na Mji wa Tanga ulikuwa ni Mji wa pili kwa umaarufu ukitanguliwa na Dar es Salaam. Katika siku za karibuni Tanga imepoteza nafasi na hadhi yake kiasi cha kupitwa na Miji mingi mingine na Wilaya nzima ya Tanga kudumaa kwa kila hali. Hata hivyo, dalili zote za mipango ya maendeleo ambayo Serikali inazifanya haziashirii hata kidogo kuisaidia Tanga irejee hadhi yake angalau ipige hatua kimaendeleo kama sehemu nyingine Tanzania.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Wilaya ya Tanga yamechimbika katika Wilaya ya Tanga nzima, ni jimbo moja la Tanga Mjini ambalo lina Halmashauri moja ya Jiji la Tanga. Tatizo ni kuwa Tanga ni Jiji bila faida na fursa za Jiji lakini pia Wilaya ya Tanga ambayo ni Jiji la Tanga imepoteza faida na fursa zinazopatiwa sehemu za vijijini.

Mheshimiwa Spika, viwanda vilivyokuwepo Tanga Mjini vimekufa na baadhi ya sehemu zilizokuwa na viwanda hivyo kama Kiwanda cha Tanzania Fertilizer Company ambacho siyo tu hakitumiki hivyo bali pia sehemu hiyo imekuwa ni pori linalofuga nyoka na hata nguruwe katikati ya Jiji la Tanga, sehemu ya Raskazone ambayo ni sehemu bora ya makazi.

Mheshimiwa Spika, tangu Mei, 2010 hadi leo Juni, 2012, Jiji la Tanga halina Mkurugenzi na wamekuwepo wanaokaimu na ambapo kwa sasabu moja au nyingine imechangia maendeleo ya Jiji kudorora. Ombi langu ni Jiji hili kupatiwa Mkurugenzi haraka iwezekanavyo, kama haiwezekani kupatiwa Mkurugenzi basi yule anayekaimu athibitishwe ili awe na hamasa na kujiamini kufanya kazi hiyo kinyume ya ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tanga ambayo ndiyo Jimbo la Uchaguzi la Tanga Mjini ina wakazi wanaokaribia 500,000 eneo la hekta 600, Tarafa nne (4), Kata 24, Vijiji 23, Vitongoji 129 na Mitaa 146 na baadhi ya Kata kama ile ya Mabawa ina wakazi zaidi ya 40,000. Kata 10 ambazo zimesambaa kwenye urefu wa takriban kilomita 130, ni sehemu ya vijiji ambako

shughuli zake kubwa ni ukulima. Kwa bahati mbaya sana vijiji hivyo havipewi fursa za kuendelea kama sehemu za ukulima kama ilivyo kwa vijiji vingine Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wilaya nzima ya Tanga ina Vituo vya Afya vinne tu na kati ya hivi ni Kituo cha Afya kimoja tu ndicho kiko vijijini. Hii imepunguza sana kiasi cha huduma za afya kwa wananchi hawa wa vijijini na imefanya Hospitali ya Bombo iwe inaongoza nchini kwa vifo vya wazazi, mwaka 2011 vilikuwa zaidi ya 430. Hii ni kwa sababu wengi wao inabidi wakimbizwe Bombo kutoka mbali. Ushauri wangu kwa Serikali ni kuvipa kipaumbele Vituo vya afya katika kata hizo za vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwenye ukulima ingawa ardhi ipo na wakulima wapo, Jimbo la Tanga Mjini halionekani kufikiriwa kabisa kwenye kuwezeshwa kiukulima. Hawapewi mbolea, hawakufikiriwa kupatiwa *Powertiller* kiasi ambacho hadi 2011, Wilaya nzima ya Tanga ilipangiwa *powertiller* mbili tu wakati baadhi ya Wilaya Mkoani Tanga zilikwishapatiwa *powertiller* zaidi ya 25.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kupatia vijiji hivi maji na umeme haitiliwi nguvu kama kwa vijiji vya Wilaya nyingine kwa kuwa Mji wa Tanga una mfumo mzuri wa maji na umeme ingawa huduma hizi zinapatikana katikati ya Wilaya hiyo ambako ni Mji wa Tanga wenyewe.

Mheshimiwa Spika, wanavijiji hawa na wakazi wa Tanga kwa jumla hawafaidiki kwa misaada ya *VICOBA, SACCOS* na hata mabilioni ya Mheshimiwa Rais. Wanaofaidi kwenye hili ni wafanyabiashara ambao wanakuja Tanga kwa makusudi ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Tanga ndiyo chimbuko la elimu Tanzania hadi Novemba, 2010, Wilaya ya Tanga haikuwa na Chuo Kikuu cha aina yoyote, si cha Serikali wala binafsi. Mwaka jana mtu binafsi alianzisha Chuo Kikuu kinachoitwa *Eckenforde University*. Ombi langu kwa Serikali ni kuweka mikakati ya makusudi kuanzisha Chuo Kikuu Tanga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri niliotoa hapo juu pia ili kutatua matatizo mengi yanayotokana na Wilaya ya Tanga kuwa Jiji la Tanga, napenda kushauri kutiliwa mkazo Wilaya ya Tanga kugawanywa kuwa Majimbo matatu ya Uchaguzi ambayo nitaishauri Halmashauri ya Tanga ipendekeze tena. Majimbo yanaweza kuwa na Kata zifuatazo:-

(i) Tanga Mjini, Kata zake ziwe Mabawa, Mzingani, Makorora, Msambweni, Usagara, Ngamiani Kusini, Ngamiani Kati, Ngamiani Kaskazini, Majengo, Mwanzange na *Tanga Central.*

(ii) Tanga Kaskazini, Kata zake ziwe Pongwe, Chumbageni, Nguvumali, Maweni, Mzizima, Kiomoni, Mabokweni na Chongoleami.

(iii) Tanga Kusini, Kata zake ziwe Tangasisi, Mwambao (Magaoni, Ndumi, Mnyenjawi na kadhalika), Duga, Tongoni, Kirare, Malungu na Mwakidila.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza Serikali kuongeza posho za Madiwani. Pia ninashukuru posho hizo zilingane na mishahara ya Watendaji wa Serikalini katika ngazi ya Wilaya yaani *DED* kama vile mishahara ya Wabunge inavyolingana na ya *DC*. Vilevile Wenyeviti wa Vijiji walipwe posho/mishahara ya kuwawezesha watekeleze majukumu ya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na pia naunga hoja nikiamini kabisa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu itayatilia maanani na kuyafanyia kazi maombi yangu inavyostahili.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchangia hoja kwa kutounga mkono hoja hii mpaka nikifahamishwa na Serikali ni hatua gani inayochukua kuhusu masuala makubwa mawili yanayowakabili Wananchi wa Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ni kuhusu mgogoro mkubwa uliopo baina ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Rufiji. Mgogoro huu ulianza tangu mwaka 2007 mara Serikali ilipowahamisha wafugaji toka Ihefu Mbeya na kuletwa katika Wilaya ya Rufiji. Wilaya hii kutokana na uwezo wake ilitaka ipewe ng'ombe wasiozidi 50,000 katika maeneo ambayo mipango bora ya matumizi ya ardhi imekamilika. Aidha, katika kikao cha *RCC* kilichofanyika Kibaha,

Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani mwaka 2006 kiliitaka Serikali itoe elimu kwa wananchi wa maeneo ambayo mifugo inapelekwa ili kuepusha migogoro baina yao na wafugaji pindi mifugo itakapopelekwa pamoja na kujenga miundombinu. Jambo la kushangaza ni kuwa mifugo ilipelekwa zaidi ya laki mbili na miundombinu kutokamilika hatimaye mifugo yote ikahama toka maeneo tengefu na kuingia katika Bonde la Mto Rufiji ambalo ni maarufu sana kwa kilimo cha mpunga, mahindi na kunde. Mifugo hii imeenea kwenye bonde hili hadi maeneo ya Delta.

Mheshimiwa Spika, tangu mifugo iingie, ugomvi baina ya wakulima na wafugaji imekuwa mingi na vifo vingi vimetokea ambapo wanaouwawa ni wakulima wenyeji. Wafugaji hawa pia wamesababisha kudumaza kilimo kwani kwa sasa kilimo kimepungua kwa zaidi ya asilimia hamsini (50%). Wafugaji hawa wamekuwa wakiharibu uoto na asili kwa kufyeka misitu na hatimaye kuweza hata kumuua Mzee Shamte kwa kumpiga. Naiomba Serikali iweke wazi ni lini wafugaji hawa wataondolewa katika Bonde la Mto Rufiji ili Bonde hili litumike kwa shughuli za kilimo. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aeleze kwa kina mkakati ambao Serikali umeuweka ili wananchi hawa waweze kulima bila bugudha kilimo cha vuli na kile cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni malipo ya wakulima wa zao la korosho katika Mkoa wa Pwani. Wakulima hawa waliuza mazao yao mwezi Septemba na Oktoba 2011 na kupewa asilimia sabini na kubaki asilimia 30 hadi sasa pamoja na tamko la Waziri Mkuu kuwa Serikali italipa deni hilo mwezi Mei, 2012.

Naiomba Serikali ieleze kwa kina ni nini kinachosababisha hadi sasa wakulima hao washindwe kupewa fedha zao ambazo zinahitajika mno kwa ajili ya matumizi yao ya kila siku na pia kuweza kuyaandaa mashamba yao kwa msimu huu wa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali, ieleze ni vikwazo gani vilivyosababisha watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kuendelea kukaimu kwa zaidi ya miaka mitatu. Viongozi hawa wanaokaimu kama hawana sifa ni vizuri kuwaondoa na kama wana sifa kwa nini wasithibitishwe?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali kwa bajeti nzuri, napenda kugusia masuala mawili.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutokuwahamisha Watendaji wa Halmashauri wanaofuja fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwaongozea Madiwani posho kwani wao wanajitolea sana kufanya kazi ngumu ya kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao lakini bado kuna haja ya kuwawekea posho Wenyeviti wa Serikali ya Kijiji ili na wao wapate hamasa ya kusimamia majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kazi nyingi ambazo ni nzuri lakini umma wa Watanzania haupewi

taarifa ya kutosha. Pamoja na kwamba ajira kwa vijana ni tatizo lakini Serikali inaajiri vijana wengi kila mwaka. Nashauri ofisi ya Waziri Mkuu itenge siku maalum kila mwaka itangaze ajira zote zilizotolewa na Serikali au tuwe na Siku ya Ajira Tanzania. Kwa kufanya hivyo, umma wetu utapata taarifa za ajira ambazo zinatolewa kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, zao la tumbaku linaongoza kuingiza pato la Taifa lakini bado mkulima wa tumbaku hanufaiki kwa sababu:-

(i) *WETCU* inasimamia usambazaji wa pembejeo ambapo wanawaibia sana wakulima kwa mfano mfuko mmoja wa pembejeo (NPK kg. 50) unatoka Dar es Salaam mpaka kumfikia mkulima alipo, unatozwa jumla ya US$ 16 mpaka kumfikia mkulima kwa gharama hii, je, tunamkomboa mkulima au tunamkomoa mkulima?

(ii) Zao la tumbaku limewekewa *grade* 68 kwa kila jani jambo ambalo limeweka mpenyo kwa wanunuzi kuweza kumkandamiza mkulima kwa kushusha *grade* na hivyo malipo kupungua kwa mkulima.

(iii) Mkulima anakatwa kilo moja kwa kila belo la tumbaku kama uzito wa gunia ambapo gunia lina gramu 700 – 800 tu gramu zinazobaki hazifanyiwi marejesho ya malipo.

(iv) Mwaka jana bei ya wastani ya tumbaku ilikuwa US$ 1.60 lakini wakulima wamelipwa bei ya wastani US$ 1.30, wakulima wameibiwa.

(v) Licha ya bei ya tumbaku kuporomoka mwaka jana lakini ushuru wa Serikali umeongezwa kwa nini?

Mheshimiwa Spika, mradi wa *WMA* katika mpaka wa Wilaya ya Uyui na Urambo. Kuna unyanyasaji mkubwa unaofanywa wa *WMA* ambapo wanawachomea nyumba na kukamata mifugo ya wananchi waishio kijiji cha Katunda, Kitongoji cha Mwamashiga, Kata ya Maboma, Wilaya Uyui. Eneo hili la Mwamashiga halimo kwenye hifadhi ya *WMA* lakini bado wananchi wanasumbuliwa na anayewapa ujasiri huo ni Mkuu wa Wilaya ya Urambo aitwaye Anna Magoha. Kama amani ikivunjika na watu kuuwana, chanzo atakuwa *DC* wa Urambo kwani wananchi wa Uyui mateso wanayopata, *DC* Urambo anayajua lakini huwa hayuko tayari kutoa msaada eti anasema Askari wa *WMA* wako sahihi na baadaye mfugaji anatakiwa kulipia kiasi kikubwa cha fedha ili akomboe mifugo yake hali hii ni mbaya, amani itapotea muda si mrefu.

**MHE. DKT. PRUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashauri kwanza, Shirika la *STAMICO* lipewe mamlaka kamili ya kusimamia madini pamoja na bodi husika ikiwa ni pamoja na kuangalia upya mikataba iliyopo na itakayofuata ili kuongeza tija katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, asilimia nne ya mrahaba inayotajwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria mpya ya Madini Na. 14 ya mwaka 2010. Kiwango hicho ni kidogo na hivyo sheria hiyo ni vyema ikapitiwa upya ili kuangalia kiwango kinachoendana na thamani ya madini yetu.

Mheshimiwa Spika, tatu, asilimia hiyo yaani (asilimia nne) ni vyema ikaenda moja kwa moja katika Halmashauri husika ili ziweze kusaidia katika kutatua matatizo ya kijamii kama shule, dawa na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, nne, makampuni yote yanayokuja kuwekeza nchini yashiriki moja kwa moja katika jamii katika kuleta maendeleo kwa mfano kusomesha na kutoa ufadhili kwa watoto wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini badala ya ilivyo sasa makampuni mengi yamekuwa yakitoa vifaa vya michezo kama mipira na *jazzy* badala ya kutoa vifaa hivyo tu, ni vyema makampuni kama hayo yakaendeleza michezo kwa kuchagua aina ya mchezo na kuuendeleza kwa kiwango cha kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, wakazi wa Kilimanjaro wamechoka kuzika ndugu zao kutokana na ajili za barabarani. Wanaomba kujua ni lini Serikali itafufua Reli ya Tanga – Moshi na Mombasa – Moshi – Arusha?

Mpeshimiwa Spika, pia wakazi wa Moshi wangependa kujua ni lini Serikali itatange pesa za

kukarabati *runway* ya Kiwanja cha Moshi ili ndege ziweze kutumia kiwanja hicho ambacho ni muhimu sana kwa utalii; hasa wapanda Mlima wa Kilimanjaro?

Mheshimiwa Spika, wakazi wa Moshi wamechoka kuona mji wao ambao ni maarufu kwa usafi unaharibiwa kwa makusudi, hasa ujenzi holela usiofuata taratibu ambao una baraka zote za Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi kwa tabia yake ya kudharau na kutofanyia kazi maazimio ya Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Spika, tunaomba *VAT* na kodi yoyote inayotozwa kwenye maji ya kunywa ifutwe, kwani inafanya maji yawe ghali na kufanya watu kunywa maji machafu ambayo ni hatari kwa afya zao.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pawe na mpango maalumu wa kuokoa Mlima Kilimanjaro kwa kutoa pesa za kutosha kulinda mazingira. Jambo hili lipewe kipaumbele kwani hali ya sasa ni mbaya na mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la Udini, Ukanda na Ukabila, linajitokeza kwa nguvu sana hata ndani ya Bunge hili; hii ni hatari, Serikali inalinyamazia. Hii ni mbegu mbaya inapandwa ndani ya Taifa hili. Tutajuta. Serikali ichukue hatua kudhibiti hali hii badala ya kuibariki.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake

nzuri lakini pia napongeza Jeshi letu la Ulinzi na Usalama, linafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuchangia kuhusu suala la barabara ya lami toka Lamadi – Bariadi, barabara hii itafungua Mkoa wetu wa Simiyu na Mikoa mingine kama Mwanza na Mara. Inasikitisha sana barabara hiyo ya kutoka Lamadi kwenda Bariadi wakati inaanza kujengwa ilianza kwa kasi sana, kwa sasa imesimama, haina mwelekeo, mkandarasi ameshaondoka, amehamisha na vitendea kazi akidai hajalipwa hela yake. Wananchi wetu ni wasikivu, wamebomolewa nyumba zao bila malipo yoyote wakipitisha barabara lakini cha ajabu mpaka muda huu hakuna kinachoendelea, barabara imezidi kuchimbika sana kiasi kwamba haipitiki. Wananchi wanalia wanadai ni bora ingebaki barabara yao ya zamani kuliko kuharibiwa na kuachwa. Wabunge wa Mkoa wa Simiyu tuna shida sana, mara kwa mara tunakumbana na hayo maswali kuhusu barabara tunashindwa kujibu, hata Waziri Mkuu wakati wa ziara yake ya Wilaya ya Bariadi alikumbana na hayo maswali.

Mheshimiwa Spika, mimi nina wasiwasi sana kuhusu msimu wa pamba, magari yatasombaje pamba, barabara ni mbovu kuliko maelezo na hiyo barabara inaweza ikasababisha ajali. Malori yanayosomba pamba kutoka Bariadi kwenda Musoma na kutoka Mkula kwenda Bariadi watapita wapi? Naishukuru Serikali nimeona kwenye kitabu imetenga pesa shilingi bilioni saba, naiomba ipeleke haraka

Mkoani Simiyu ili iweze kujengwa barabara hiyo inayotoka Ramadi – Bariadi - Mwigumbi. Zao la pamba, naiomba Serikali iweke mazingira rafiki kwa wakulima wote lakini pia wanunuzi. Bei itakayopangwa iwe yenye tija kwa wote wakulima na wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji, bwawa la Mwanjoro lililopo kule Meatu liishe. Tunaomba pia Serikali sasa ifikirie kuvuna maji toka Ziwa Victoria kuja kwenye Wilaya zetu za Bariadi, Maswa, Itirima na Meatu. Huu utakuwa mradi pekee utakaoondoa tatizo la maji Simiyu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri pesa nyingi zinazopelekwa huko zinapotea bila kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Kwa mfano, pesa nyingi hupotea kwenye mafuta ya magari, huko ndipo pesa zinakopotelea, watu wenye vituo vya mafuta ambao wanatenda za kuiuzia mafuta Halmashauri ndiyo wanaoshirikiana na watendaji katika Halmashauri zetu na huko kwa wafanyabiashara hao ndiko cheki hewa za malipo ya mafuta zinakopitishiwa. Watendaji katika Halmashauri zetu, ndiyo wenye makampuni yanayofanya kazi katika Halmashauri kwa kuwatumia ndugu zao au marafiki zao. Sasa kama kweli Serikali imedhamiria kwa dhati kusimamia pesa za Serikali, iliangalie jambo hili ili watendaji au Madiwani katika

Halmashauri husika wasijihusishe katika tenda za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba mbolea iwafikie wakulima kwa wakati kabla ya msimu kuanza, mbolea na mbegu vyote viende sambamba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuongelea kuhusu TAMISEMI, kuna tatizo kubwa linalotokana na *"appointments"* kwa nafasi mbalimbali za uongozi Serikalini kutokana na Serikali ya Awamu ya Nne kuamua kuondoa ushindani kwa kutangaza nafasi za uongozi. Nashauri nafasi hizo zitangazwe hata kwa *"Internal Circulars"* ili wanaoomba nafasi hizo wawe ni watumishi waajiriwa tu ndani ya Serikali popote pale walipo nchini, hii itaondoa upendeleo, udini, ukabila, ukanda, kuweka milolongo ya waliojipanga kifisadi ili kuhujumu fedha za Serikali. Matarajio ni kwamba kutakuwepo *panels* za kuchuja na kushauri nani apewe cheo gani na wapi.

Mheshimiwa Spika, pili, utumishi Serikalini; nashauri ukiondoa waajiriwa katika Sekta za Ulinzi na Usalama wa Taifa, yaani Polisi, Magereza, JWTZ na Usalama wa Taifa; waajiriwa wengine wote Serikali wapewe ajira za mikataba kati ya miaka mitatu, mitano na *maximum* saba. Hii itatoa fursa kwa Serikali kuweka taratibu za *"Pay for Performance (P4P)"* ambapo kila mwajiriwa atapewa masharti ya kazi ambayo yatatathminiwa kabla ya *"Redeployment"* pia Serikali itatoa fursa kwa

Serikali kujivua gamba kwa kuondoa maelfu na malaki ya watumishi wa kada mbalimbali ambao ni mzigo kwa Taifa na wanapata mishahara hewa bila ya kuwajibika. Wengi wa watumishi hawa wanakuwepo tu hadi wafike miaka 60. *This is wrong,* Serikali inabadilisha Baraza la Mawaziri na Makatibu Wakuu na wengine wachache; watumishi wengine wote ni *static*, wapo tu hadi wafikie miaka 60 ya kustaafu, *no*! Sasa tuna wataalamu kila kada, tutangaze nafasi watu washindanie, *we should retain in Government only but the Best.*

Mheshimiwa Spika, tatu, fedha za Rada. Kama kweli fedha ya Rada katika elimu zinaenda katika baadhi ya Mikoa, hiyo si sawa hata kidogo. Zigawiwe nchi nzima hata kama ni kwa uwiano bila kutofautiana.

Mheshimiwa Spika, nne, nishati ya umeme Kongwa. Tunaomba nishati za umeme kupitia *REA* kwa vijiji vya karibu kama ifuatavyo:-

(i) Mlali – Nghumbi – km 5;
(ii) Mbande – Sejeli – Banyibanyi – km 15;
(iii) Zoissa – Chitego – km10; na
(iv) Pandambili – Chiwe km 8.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ni ofisi muhimu sana katika kuratibu utaratibu wote katika Halmashauri zetu ili kusimamia maendeleo ya Mikoa na Halmashauri zote

nchini Tanzania, naomba kutoa ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Katika Halmashauri kuna mali nyingi sana za Serikali lakini usimamizi wake bado duni kwa mfano Kitengo cha Manunuzi bado hakijaimarishwa. Fedha nyingi sana zinapotea kupitia kitengo hiki. Kwa hiyo, Serikali iimarishe usimamizi madhubuti katika kitengo hiki kwa kufuata Sheria ya Manunuzi.

(ii) Naomba Halmashauri zetu kuwa na miradi ili kupata mapato ya ndani siyo kutegemea ruzuku kutoka Serikali kuu.

(iii) Halmashauri zina wawekezaji ambao wana miradi mikubwa kwa mfano viwanda vya chai, viwanda vya mbao na viwanda vya karatasi ambavyo vipo katika Jimbo la Mufindi Kusini, Wilaya ya Mufindi. Kwa hiyo, Halmashauri inaweza kufaidikia kupitia viwanda hivi kwa kupewa mrahaba kutoka katika viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, suala la maji, katika vijiji vingi hapa Tanzania wana tatizo la maji, ndiyo maana Wabunge wengi sana wanauliza maswali ya maji hasa miradi wa *World Bank* bado haitekelezeki. Naomba Serikali itafute njia nyingine ili kutatua tatizo hili la maji. Katika Jimbo la Mufindi Kusini, kuna Vijiji vya Sawala, Kibao, Rufuna na Kipande. Wananchi wanapata shida ya maji, wananchi wameshachangia fedha mpaka sasa fedha zao zipo benki lakini Serikali bado haijapeleka maji kwa mradi huu wa *World Bank*.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo kubwa sana katika Jimbo la Mufindi. Serikali kwa kushirikiana na wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini walijenga matanki ya maji katika vijiji vya Sawala, Kibao, Igowole, Nyololo, Maduma na Nyigo lakini miundombinu yake imechakaa sana mpaka sasa hivi matanki hayo hayatumiki sababu miundombinu yake imechakaa. Naiomba Serikali kuchukua hatua za haraka ili kukarabati miundombinu ya maji katika Jimbo la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kujenga barabara kwa kiwango cha lami, barabara ya Nyololo – Igowole – Kibao – Mtwango – Mgololo. Ni barabara muhimu sana katika uchumi wa Taifa kwa ujumla sababu imepita katika viwanda vikubwa vya chai, mbao, karatasi na viwanda vidogovidogo vya wajasiriamali. Pia kuna idadi ya watu wengi wanaoishi katika barabara hiyo. Naiomba sana Serikali kulichukulia hili kuwa ni tatizo kubwa katia Jimbo la Mufindi Kusini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango ufuatao kuhusu maelezo ya kiutendaji ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu mapitio ya kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na mwelekeo wa kazi kwa mwaka 2012/2013 pamoja na Fungu 56 katika makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1998 na

utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa; Wizara ifanye mapito ya Sheria za Serikali za Mitaa kuhusu Muundo wa Kamati za Mitaa Mijini na majukumu ya Wenyeviti na Watendaji wa Mitaa ili kuwe na mfano thabiti na ushirikishwaji mpana kama ilivyo kwa Halmashauri na mikutano mikuu ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2011/2012 yameshuka ukilinganisha na makadirio. Mapato yalikuwa shilingi bilioni 142.8 hadi mwezi Machi 2012 wakati makadirio yalikuwa shilingi bilioni 350.5 sawa na asilimia 40.7. Sababu mojawapo ikiwa ni kuchelewa kutungwa kwa kanuni na kuwekwa kwa mfumo baada ya marekebisho ya Sheria ya Biashara kufanyika. Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara Fedha wafidie kiwango cha upungufu wa mapato uliojitokeza kwenye Manispaa ya Kinondoni. Aidha, Serikali iharakishe kuweka mfumo husika kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2011/2012, naomba maelezo ni kwa nini fedha za barabara ya Kibangu mpaka Makoka, Kata ya Makuburi, Manispaa ya Kinondoni hazikutolewa mpaka sasa? Naomba barabara hii ifanyiwe matengenezo kama Waziri wa TAMISEMI alivyoahidi. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu ishughulikie ombi lililowasilishwa na Mkuu wa Mkoa la ujenzi wa daraja la Ubungo Kisiwani linalounganisha Ubungo Maziwa na *Mabibo External* na kuchangia katika kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu sababu ya kutotoa kiwango cha fedha za ruzuku ya MMEM na MMES (*Capitation*) kama ilivyopitishwa kwenye bajeti. (Jumla ni shilingi bilioni 17.8 tu badala ya shilingi 72.9 bilioni).

Mheshimiwa Spika, naomba kupatiwa nakala ya Taarifa ya Ukaguzi wa Elimu ya Shule ya Msingi na Sekondari katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kifungu 2005, maendeleo ya miji, kasma 270620 – *DART*, matumizi ya fedha hizo yazingatie pia kuboresha mfumo wa kutoa taarifa kwa wananchi na wawakilishi wa wananchi ikiwemo Madiwani na Wabunge kuhusu utekelezaji wa mradi kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, aidha, mpango wa maendeleo kasma 4285- *DART*, kutotenga fedha za maendeleo kabisa kutakuwa na athari kwa mradi. Ofisi ya Waziri Mkuu itenge fedha za kumaliza fidia ya shilingi bilioni 500 kwenye kituo cha mabasi ya Ubungo, shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya eneo mbadala la kupaki mabasi na shilingi bilioni 1.5 za matengenezo ya barabara za mchepuo za kupunguza foleni wakati wa utekelezaji wa mradi. Ikiwa hakuna chanzo mbadala, Ofisi ya Waziri Mkuu ichukue kiasi cha fedha kutoka kwenye kasma 4170 – Programu ya Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maboresho ya Sekta ya Fedha, naomba kuletwe Bungeni Muswada wa Sheria

ya Taasisi Ndogondogo za Fedha ili kuboresha mfumo mzuri wa kuendeleza *SACCOS, VICOBA* na taasisi zingine pamoja na kudhibiti viwango vya riba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sensa ya watu na makazi, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu katika majumuisho itoe kauli kuhusu kutofautiana kwa kauli kunakoendelea kwenye vyombo vya habari kati ya baadhi ya Mawaziri wa Serikali na baadhi ya viongozi wa dini kuhusu mfumo na utaratibu wa sensa ya watu na makazi kwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko ya Katiba, Ofisi ya Waziri Mkuu itoe kauli ya kuendelea kupokea mapendekezo ya kuboresha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8 ya Mwaka 2011 (Sura ya 83), kuhusu Bunge la Katiba na kuhusu kura ya maoni. Bila kuboresha utaratibu wa utungaji na uhalalishaji wa Katiba, kazi iliyoanza kufanywa na Tume ya kuratibu na kukusanya maoni haitaweza kujenga mwafaka wa kitaifa na kuipatia nchi Katiba mpya na bora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muungano, Ofisi ya Waziri Mkuu itoe taarifa ya kina zaidi kwa Wabunge na Bunge kuhusu hoja kumi na mbili (12) ambazo hazijapatiwa ufumbuzi; ili Kamati za Kudumu za Bunge ziweze kuishauri na kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge, ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu na Bunge) ishirikiane na uongozi wa Bunge kuwezesha marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwenye mwaka wa fedha

2012/2013. Aidha, itoe kauli imejipanga vipi kushirikiana na uongozi wa Bunge kuweka mfumo mzuri zaidi wa Kikanuni na kirasilimali kuweka mazingira bora ya utendaji wa Wasemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani (Baraza Kivuli) kama ilivyo katika nchi zenye wigo mpana wa demokrasia. Naomba pia kupata majibu ya Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya maombi yangu ya mwaka 2011 ya kuingizwa katika orodha ya ujenzi wa Ofisi ya Mbunge katika Jimbo la Ubungo. Kwa kuwa kwa sasa Ofisi ya Mbunge wa Ubungo ipo katika Jimbo la Kinondoni. Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Katibu wa Bunge zianze mawasiliano na Manispaa ya Kinondoni kwa ajili ya kupata eneo la kujenga Ofisi ya Mbunge katika Jimbo la Ubungo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya sekta binafsi, uwekezaji na uwezeshaji, Waziri wa Nchi atoe nakala kwa Mbunge na Manispaa ya Kinondoni kuhusu uchambuzi unaofanyika kuhusu ujenzi na upanuzi wa barabara ya Chalinze na Morogoro *(express line)*. Aidha, atoe nakala kwa Mbunge kuhusu wananchi wa vikundi kutoka Jimbo la Ubungo na fedha za *TASAF* na mifuko mingine ya uwezeshaji inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, kufuatia mkutano wa Waziri Mkuu na wadau wa viwanda vya nguo; naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ifuatilie kwa karibu Kiwanda cha Nguo cha Urafiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya juu, pamoja na kuunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu kusimamishwa kwa wanachuo wa UDOM; Ofisi

ya Waziri Mkuu itakapotoa majibu ieleze pia hatua ya wanachuo waliosimamishwa UDSM.

Mheshimiwa Spika, naomba pia majibu ya mchango wa Mkutano wa Nne wa bajeti 2011 ikiwemo kuhusu fidia ya ardhi ya wananchi wa Kwembe - Mloganzila.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mkuu kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi yake kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanda Peter Pinda (Waziri), kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi uliotukuka. Pili nampongeza kwa utendaji makini wa majukumu yake na uvumilivu wa hali ya juu alionao. Nampongeza pia Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia kwa utendaji mzuri na ameonyesha kuwa ni jinsi gani yupo makini maana ni kipindi kifupi tangu uteuzi wake.

Mheshimiwa Spika, tatizo la bomoabomoa limekuwa ni kero ya kwanza na ni la kipaumbele kabisa kwa nchi nzima na malalamiko ni makubwa. Naiomba Serikali isikie kilio hiki kwa kuzingatia haki.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Jimbo la Kilwa Kaskazini mathalani, wananchi wamejenga kabla hata ya sheria iliyotajwa haijatungwa na kuridhiwa na Bunge ama kuidhinishwa na mamlaka husika na hii

inathibitishwa na histora ya nchi yetu kwamba wakoloni wamekuwepo kuanzia karne ya 18 na kabla ya hapo walikuwapo Waarabu na Washirazi katika maeneo ya Kilwa. Hivyo sikubaliani kabisa kuwa uwepo wa wananchi hawa katika maeneo hayo ni kuvunja sheria kwa tafsiri kwamba wamekuwapo kabla. Lakini haitoshi itakuwa pia Katiba inakikukwa kama Ibara ya 13 (1) ambayo inatamka watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Pia Ibara ya 24(1) inayosema kila mtu anayo haki ya kumili mali na haki ya kuhifadhi mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ujenzi wa barabara gharama zinaongezeka kila siku, ifike wakati sasa tuwe na mpango mkakati kuhakikisha tunamaliza ujenzi wake haraka na kuepuka gharama ambazo zinaongezeka kwa kasi sana. Kwa kipindi kirefu sasa tumekuwa tunazungumzia barabara ya Nangurukuru – Liwale, Njia Nne – Kipatimu zijengwe kwa lami ili zipitike wakati wote. Pia tumeleta maombi maalum kwa ujenzi wa barabara ya Kipatimu – Mpopera bila ya majibu yoyote. Kipindi kilichopita pia nilizungumzia suala la ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete kwa ujenzi wa barabara ya Kipatimu hadi Nyamwage ambapo hata dalili ya utekelezaji wake haijaonekana. Licha ya jitihada za Serikali kuwawezesha Watanzania kiuchumi na kiutendaji kwa kiasi kikubwa sasa tuhakikishe makampuni ya kitanzania yanapewa (yanajengewa) uwezo ili yaweze kushiriki kikamilifu katika miradi, kwa maana kuwa tunaposhirikisha kampuni za nje tunatoa

pesa zetu nyingi na tunaimarisha uchumi wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufuatiliaji mzuri wa viongozi wa Wizara hizi, naishauri Serikali ihimize na kuhakikisha barabara ya Ndundu – Somanga inakamilika kwa wakati, ili iwe ni pumziko kwa wananchi wa Kilwa na Mikoa ya Kusini kwa ujumla ambao kwa kipindi kirefu wameteseka kwa kutopata kuitumia vyema fursa za kiuchumi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa miradi, kumekuwa na tatizo kubwa la wananchi kucheleweshewa fidia zao pale ambapo wanatakiwa kupisha miradi. Naishauri Serikali itafute namna bora zaidi ya kutekeleza zoezi la fidia kwa maana linakera na kusumbua sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana la mfumuko wa bei haswa kwenye vyakula. Tumekuwa na tunapendekeza hatua mbalimbali ili kuweza kukabiliana na tatizo hili. Tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali ushauri wa mara kwa mara ila sasa naishauri Serikali iweke mkazo kuhakikisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko inapewa mtaji na kushiriki soko na wafanyabiashara ambao wamekuwa wakaidi kusaidiana na Serikali. Katika kutekeleza hili, pamoja na Baraza la Mawaziri kuridhia toka mwaka 2008 kwa Waraka Na. 40 ambao uliagiza kuwa mali zote zilizokuwa za *NMC* zikabidhiwe kwa Bodi, zoezi hili halijakamilia hadi leo.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo kubwa sana la huduma kwa wazee ambao wametimiza umri wa miaka sitini kutopata tiba stahiki, licha ya Waziri Mkuu kutoa agizo kuwa wazee watibiwe bure kama sera inavyoelekeza. Tunaiomba TAMISEMI iandae Waraka ili usambazwe katika vituo na zanahati zote nchini ili kuondoa kero kwa wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, mpangilio wa bajeti imefikia wakati uangaliwe upya kwa maana hii inapelekea maeneo mengine kudumaa kabisa. Ukiangalia kwa kipindi cha miaka mingi, Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Kigoma na Rukwa imekuwa imepunjwa sana bajeti ya maendeleo hasa katika sekta za afya, elimu, maji na barabara ambapo ukiangalia kwa makini bajeti za Mikoa hii inalingana kabisa na bajeti ya Mkoa mmoja wa Dar es Salaam au Mwanza. Kigezo cha idadi ya watu si sahihi kwa maana hakuna ambaye anakubali kuishi kwenye shida, tuwekeze vijijini maana hali hii inapelekea watu wote kutoka vijijini na kukimbilia mijini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ngumu ya maisha na mazingira magumu ambayo watumishi wamekuwa wanakumbana nayo haswa Wilayani Kilwa, naishauri Serikali ihakikishe mpango wa kuwalipa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu haswa kwenye afya, elimu na kilimo. Si sahihi watumishi hawa kulipwa viwango sawa na wale ambao wanaishi kwenye maeneo ya miji.

Mheshimiwa Spika, kwa sekta ya elimu pia tunaiomba Serikali irejeshe utaratibu wa kutoa chakula

mashuleni ili kusaidia kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi. Hali ya lishe na utapiamlo ni mbaya sana nchini na tukiacha iendelee basi ni janga kubwa kwa Taifa letu kwa maana hata ufaulu wa watoto hauwezi kuongozeka.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na madai mengi ya watumishi kwa kipindi kirefu mno. Naelewa kabisa jitihada kubwa ambazo Serikali imekuwa ikifanya ili kutatua tatizo hili lakini ieleweke kuwa matatizo mengine yanatokana na mahusiano mabaya yaliyopo kati ya watumishi na viongozi wao maeneo ya kazi. Serikali ifanye jitihada za makusudi ili kujenga mahusiano mazuri na mazingira mazuri baina ya watumishi na viongozi wao.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu tumekuwa tunaiomba Serikali igawanye Wilaya ya Kilwa kutokana na ukubwa lakini pia jiografia yake ni ngumu mno. Ombi hili halijapatiwa majibu mpaka sasa. Tunaomba kama ikiwezekana tuanzie japo kuwa na Halmashauri mbili ili kusaidia kupeleka karibu huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupokelewa maoni yangu, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inayohusiana na mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa hotuba nilizungumzia sana kuhusu kilimo. Yapo masuala ya msingi pia ambayo kutokana na ufinyu wa muda sikuweza kuyawasilisha. Mambo hayo ni pamoja na kutumia vizuri wataalamu, watafiti wa kilimo, kujenga viwanda vya usindikaji wa mazao kwa kutumia mbegu bora, pembejeo bora na kuboresha huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kumsaidia mkulima ili anufaike na bei ya mazao yake. Ni vyema kukafanyika utafiti wa gharama za uzalishaji ili kutoa bei itakayompa mkulima faida kutokana na jasho lake.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Ipo hoja ambayo imetolewa hapa Bungeni kuhusu wingi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hivyo kuomba mifuko hii iunganishwe, na ubakie mfuko mmoja utakaohudumia wanachama. Sababu iliyotolewa ni kwamba, kuwepo kwa mifuko hii, kunaongeza gharama ya kuendesha mifuko.

Mheshimiwa Spika, haya ni mawazo tu, yanaweza kutazamwa kwa upande mmoja. Napenda kutangaza maslahi yangu kwa mujibu wa fasili ya 61(1) ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge kwamba mimi nimekuwa mtumishi wa moja ya Hifadhi za Jamii hapa nchini. Ningependa pia kutoa mawazo yangu kwa mujibu wa uzoefu wa kufanya kazi katika mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa hapa nchini ni mfano, *PPF, NSSF, LAPF, GEPF*

na *PSPF*. Kila mfuko kabla ya kuanzishwa kwa wakala wa mifuko hii *(SSRA)* ilikuwa ina wanachama wa aina mbalimbali kutokana na masharti ya ajira ya kila mwananchama.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya mifuko hii ni kutoa huduma ya kulipa mafao ya aina mbalimbali kwa wanachama. Ili kutoa huduma bora, inahitaji idadi ya watumishi iwiane na idadi ya wanachama wanaohudumiwa katika mfuko mmoja wa hifadhi ya jamii (nilikokuwa nafanya kazi) kwa wastani mtumishi mmoja anahudumia wanachama 7,500. Kwa aina ya kazi zinazohusiana na huduma kwa wanachama wa mfuko, ni dhahiri kwamba kuna mzigo mkubwa sana wa kazi na hivyo mtumishi anatingwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mifuko hii inaendelea kukua na hivyo idadi ya wanachama wake itaendelea kuongezeka, hivyo gharama za kuiunganisha mifuko hii kwa pamoja inaweza ikawa kubwa zaidi ikilinganishwa na hali ilivyo kwa sasa. Kwa maana ya kwamba idadi ya watoa huduma kwa wanachama italazimika kuwa kubwa. Inaweza ikashindikana kutoa huduma bora (kwa maana ya kulipa mafao kwa haraka) lakini pia inaweza ikashindikana na kuwa na idadi kubwa na iliyokithiri ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spkika, naomba Serikali iliangalie wazo hili kwa pande zote kwa kuwa azma ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni kutoa huduma bora na kwa haraka. Tukisema gharama za uendeshaji ya mifuko hii ni kubwa, maana yake, idadi ya wafanyakazi pia

ipunguzwe. Kwa hali halisi ya Taifa letu, tuna ukosefu mkubwa sana wa ajira na hivyo sioni haja ya kupunguza watumishi kama sehemu ya kupunguza gharama za uendeshaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa vile Serikali itakuwa imeongeza tatizo la ukosefu wa ajira na vilevile mifuko hii itashindwa kutoa huduma bora na hivyo kusababisha ugumu wa maisha ya wanachama wanaostahili kupata mafao yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kwamba ilipe madeni ambayo inadaiwa na mifuko hii ili mifuko iweze kuimarika kifedha na kulipa mafao ya wastaafu na wanachama wengine. Ili mifuko hii iweze kulipa mafao, inahitaji kuwa na fedha za kutosha. Fedha hizi ni michango ya wanachama wenyewe. Siyo haki kwa Serikali kuendelea kutumia fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ilhali Watanzania ambao wamewekeza kwa kuchangia kutoka kwenye mishahara yao, wasinufaike na mafao yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kuitaka Serikali ya chama changu ilipe madeni yote inayodaiwa na mifuko hii. Serikali ilikopa kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii mabilioni ya fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na ulipwaji wa wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Matumizi hayo ni ya muhimu kwa vile yanawahusu wananchi wetu, lakini ukweli ni kwamba fedha hizi zinatokana na michango ya wanyonge, wafanyakazi waliotumikia Taifa letu kwa moyo. Hivyo ni lazima kuheshimu, kutunza na kulinda michango yao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaomba Serikali ifuatilie na iyafanyie kazi maoni yangu.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, hakuna asiyefahamu kuwa hukumu dhidi ya kampuni ya Uingereza ya kutengeneza silaha, *British Aerospace Systems Limited (BAE)* ambalo ilikiri kuhusika katika uuzaji tata wa rada ya kijeshi na kukubali kulipa faini ya paundi milioni 30 imekuwa ni dhihaka za walipa kodi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo jambo lenyewe ni la utata mtupu, na malipo hayo ya chenji yanaonekana nayo yanataka kuleta sintofahamu ndani ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bunge lililopita, aliliambia Bunge kwamba fedha hizo za chenji za rada tayari zimeshapatikana na zimepangiwa kugaiwa kama utaratibu unavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuzielekeza fedha hizo kwenye Sekta ya Elimu ikiwemo kununua vitabu milioni 4.4 kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi, kununua vitabu 192,000 vya kufundishia kwa ajili ya Walimu wa Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imesema watanunua madawati 200,000 kwa ajili ya wanafunzi 16,000 wa Shule za Msingi na kujenga nyumba 1,996 za Walimu wa Shule za Msingi vijijini na kujenga vyoo 200,000 kwenye Shule za Msingi nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mipango hii katika ripoti ya Serikali haioneshi mahali popote kama Serikali ina mpango wowote wa kupeleka fedha hizi Zanzibar ambapo kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya nchi, ulinzi ni mambo ya Muungano na rada hii ni ya kijeshi, hivyo Zanzibari walihitaji kupewa gawiwo la chenji hiyo iliyopatikana.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha kabisa, fedha hiyo ya chenji ni fedha ya Muungano, ilihitaji ushiriki wa pande zote za Muungano kukaa pamoja na kujadili hatima ya chenji hiyo, kinyume chake ni kutengwa kwa Zanzibar na Serikali ya Muungano kama vile sio wahusika wa Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *BAE Systems* iliamuriwa na mahakama Nchini Uingereza kulipa faini hiyo ya bilioni 72.3 baada ya kugundulika kwamba ilikwenda kinyume katika kuizuia Tanzania rada mwishoni mwa miaka ya 1990.

Mheshimiwa Spika, kwa kujali na kuheshimu makubaliano ya Muungano wetu na kutunza kumbukumbu sahihi za waanzilishi wa Muungano huu, naamini chenji hiyo itakwenda Zanzibar kwa gawiwo stahiki kwa kulingana na makubaliano yetu kikatiba. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni na ushauri wangu kwenye hoja

na hotuba ya Waziri Mkuu katika maeneo makuu matano kwa maana ya kilimo kama chanzo muhimu cha kuweza kuinua uchumi wetu, changamoto tulizonazo kwenye Sekta ya Afya na sera ya afya; tatu, nitazungumza juu ya kuzorota kwa elimu yetu ya Tanzania; nne, ni kuhusu kodi wanazokatwa wafanyakazi; na mwisho nitazungumzia suala zima la fidia mbadala kwa wananchi wanaopisha matumizi mapya ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia, Wananchi wengi wa Tanzania wanaishi vijijini kwa takribani asilimia 75. Hawa ni watu wanaojishughulisha na kilimo na ufugaji ili waweze kuendesha maisha yao. Ili tuendane na dhana bora ya Kilimo Kwanza, kwa maana ya *green revolution*, basi ni vyema kundi zima la Serikali limiliki kwenye uwezeshaji wa wananchi wa kawaida ili aweze kuwekeza kwenye kilimo. Hapa ndipo tutakuwa tumetimiza kwa vitendo dhana ya kumwezesha mwananchi wa kada ya chini kabisa kuliko ilivyo sasa nadharia *(theory)* zaidi ya kuwa Watanzania wanawezeshwa kupitia mifuko kedekede, lakini kiuhalisia hizi pesa zinaishia kwa wajanja wachache. Ndiyo maana hadi leo hatuna kanzidata *(database).*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuwa na uchumi unaokua ni lazima Taifa lijikite kwenye *rural growth*. Tuinue kilimo kwa kupeleka miundombinu kwa maana ya umeme vijijini, tuwezeshe kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga mabwawa ili wakati wa mvua tuweze kuyavuna, na pia mabwawa ya kunyweshea ng’ombe. Tukishaimarisha kilimo cha umwagiliaji

ambacho ni endelevu, ni lazima kuwepo na umeme vijijini.

Tukiwezesha hili, tutakuwa na misimu ya kilimo kwa misimu yote ya mwaka, na ukizingatia nchi yetu ya Tanzania ina rutuba nzuri sana na inastawisha mazao mengi sana. Ukitembelea nchi za wenzetu utatamani kulia, kwa sababu mazao mengi yanapandwa kila eneo, ukikuta msitu ni wa miti yenye manufaa, ya mbuga au hifadhi ya jamii. Mfano ukitembea maeneo mengi ya Afrika Kusini, ni mashamba tu, huoni ardhi iliyokaa, *supermarket* zao zote zimejaa mazao yao yenyewe. Hivyo, nashauri uwezesho wa miundombinu yote kwa maana ya maji, barabara, umeme, mikopo na kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ni juu ya Sekta ya Afya ambayo tumeendelea kushuhudia changamoto nyingi, licha ya Sera ya Afya na kuwa na Kituo cha Afya katika kila Kata na Zahanati, kuna utekelezaji wa sera hii, lakini pia kwenye maeneo yaliyojengwa Zahanati, basi ni majengo bila hata dawa, wahudumu wa afya na vitendea kazi vingine kwenye hospitali. Ukizingatia miundombinu ya maeneo yetu, ni mibovu na unakuta Zahanati hazina huduma yoyote inayowalazimu Eatanzania wasajiri umbali mrefu ili waweze kupata huduma za afya kwenye Kituo cha Afya au hospitali ya Wilaya. Hili ni tatizo na kama tulivyosema, Watanzania wengi ndiyo wanaoishi vijijini, basi Serikali haina budi kuboresha zaidi na kwa upendeleo kabisa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya elimu yetu. Tumeendelea kushuhudia kusuasua na kushuka kwa kiwango cha elimu. Licha ya kwamba Serikali imeelekeza kwenye majengo na kuangalia idadi kubwa ya watoto wanaojiunga na Sekondari na Shule za Msingi, kwangu mimi idadi kubwa ya majengo na idadi kubwa ya wanafunzi siyo tija, kwa sababu mwisho wa siku elimu tunayoitoa ni bora elimu na siyo elimu bora kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, ili tuwe na elimu bora, tunahitaji viwezeshi *(inputs)* kama walimu wa kutosha, majengo, maabara, vitabu, madawati na kwa ujumla mazingira bora ya ufundishaji na usikilizaji unaohitajika ili mwanafunzi awe na uelewa mzuri. Kwa kufanya hivi, tutapata *product (output)* nzuri, maana ulewa na ufanisi wa mwanafunzi utaongezeka na nchi itapunguza idadi ya watu wasiokuwa na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kuzungumzia juu ya kodi ya mapato, yaani *PAYE*. Tumeshuhudia wafanyabiashara wakipewa unafuu wa kulipa kodi ambayo wafanyakazi wataanza kukatwa kuanzia kipato cha Shilingi milioni nne kwa mwaka ambayo ni sawa na Sh. 333,333.33 kwa mwezi. Wakati mfanyakazi yeye anaanza kukatwa kodi kwa kipato cha Sh. 170,000/= kwa mwezi ambayo ni sawa na Shilingi milioni 2.04 kwa mwaka. Naomba Serikali iwapunguzie kodi hawa kwa wao pia kukatwa kodi kuanzia Sh. 333,333,33 kwa mwezi kama wafanyabiashara, kwani wao ni wachache kuliko wafanyabishara. Vile vile kuna marekebisho kwenye vipato vingine vya mshahara ili kuweza kutoa unafuu.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya fidia mbadala kwa wananchi wanapopisha matumizi mapya ya ardhi, inabidi tuwape haki wananchi hawa kwa kuwapa fidia mbadala na kwa wakati. Huwezi kumhamisha mwananchi anayeishi kwenye ardhi yenye madini na kumlipa Shilingi milioni nne au mbili. Hii ni fedheha sana. Tumeshuhudia hili kule Bunda kupisha mradi wa *EPZ*, kule Rowolt... kupitisha JWT. Sasa miaka inakwenda, wananchi wanakuwa *domant* kwenye shughuli za maendeleo na uchumi. Hii siyo sawa kabisa. Vile vile Waziri Mkuu arejee kauli yake ya kuunda Tume juu ya mauaji ya raia na ubambwikwaji kesi kwenye Wilaya ya Tarime. Tumeendelea kushuhudia mauaji kule Nyamongo yanayofanywa na aidha askari wa migodi au na Jeshi la Polisi, kisha Jeshi la Polisi kulazimisha familia kuzika maiti tena kwa kutoa kifuta jasho, mchele, gari la kubebea maiti na kusimamia Marehemu azikwe. Huu ni udhalilishaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kauli juu ya haya, vinginevyo siungi mkono hoja.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake kwa kazi nzuri yenye kuleta matumaini juu ya bajeti iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe yangu mawazo juu ya bajeti hii. Kwanza napenda nizungumzie juu ya kilimo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amegusa akisema kilimo itakuzwa Kusini mwa Tanzania. Sasa ili

kukuza, ni budi pawe na vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na matrekta na pembejeo. Kulingana na hayo, naomba wakulima wakopeshwe matrekta kwa wale wenye uwezo ili kurahisisha utendaji wa kazi. Pembejeo pia zikopeshwe. Pia zitolewe kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa stakabadhi ghalani unaotumika siyo mzuri kwa hali ile ya kulipa nusu nusu, unamkosesha mkulima kutimiza azma yake, kwani katika palizi za mashamba hutumika mikopo ya nguvu za watu, yaani vibarua. Hii hufanya mipango isitimizwe, maana ile nusu ya kwanza huishia kwenye madeni na mahitahji madogo madogo kama vile chumvi, sabuni, mafuta, matibabu na kadhalika. Zijapo nusu ya pili hukuta zile za mwanzo zimekwisha na hivyo kukosa kutimiza lengo. Hivyo basi, ni vyema ikiwa zinalipwa zote kwanza na zijapo zile za baada ya mauzo, yaani zile za bonsai, ndipo makato yafanyike kwa hizo. Hivyo naomba Serikali ichunguze ili kupatikana njia mbadala.

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie juu ya Elimu Kwanza. Napenda nizungumzie juu ya Walimu. Kama ujuavyo, ualimu ni wito. Kazi yake kubwa ni kuzielekeza akili za watu ambazo ni ngumu sana. Mtumishi yeyote hufanya kazi ikiwa maslahi yake yanakwenda vizuri na kumfanya aipende. Maslahi hayo ni pamoja na mishahara, makazi na marupurupu, vile vile kama vitendea kazi vinakuwapo. Kwa upande wa wapokea elimu, nao huwa wanapokea vizuri kama vifaa vinatimia. Vile vile walimu wakiwapo wa kutosha kwa masoko yote, pawe na maktaba na maabara. Kwa upande wa Shule za Kata ambazo mara nyingi huwa na mapungufu makubwa na aina zote. Kwa

hawa, naomba Serikali iwafikirie sana pale wakosapo kupata alama zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, suala la maji Wilayani hata Nanyumbu na Newala hali ni tete sana. Kwa Masasi visima ni vingi, ila pampu ziliharibika. Hivyo vipatiwe matengenezo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hotuba ya bajeti ambayo ina matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la Muungano, katika hotuba ya Waziri Mkuu, amesema kuwa kuna vikao 14 vya Mawaziri na Makatibu Wakuu kutoka Zanzibar na Tanzania Bara, pamoja na Kamati ya pamoja baina ya *SMT* na *SMZ* ili kutatua changamoto za Muungano. Jambo la kusikitisha hoja hizo zinazoendelea kujadiliwa kila siku na kwa miaka mingi zinafanywa kama ni hoja mpya na zinazoanza kujadiliwa sasa. Kuna mambo mengi na ya msingi ambayo kwa Wazanzibar ndiyo kero hasa, lakini hakuna kilichowasilishwa hapa. Nashauri kusiwe tena na vikao wala Kamati, hazina maana yoyote isipokuwa kupoteza na kuharibu fedha za Serikali na badala yake ni bora sasa tusubiri Katiba mpya tu.

Mheshimiwa Spika, ajenda yangu ya pili ni kuhusu utendaji wa Halmashauri za Wilaya. Nasikitika kuona kuwa bado utendaji wa Halmashauri zetu nchini ni mbovu katika dhana zote.

Mheshimiwa Spika, hayo yamethibitishwa na ripoti ya *CAG* kuwa, Halmashauri 47 zina ulegevu mkubwa katika usimamizi wa mapato; Halmashauri 88 zimeonekana zina udhaifu katika usimamizi wa mapato; na Halmashauri 32 zinafanya malipo bila hati ya malipo ambapo zaidi ya Shilingi bilioni hazina hati hizo za malipo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa, Halmashauri zina matatizo mengi na hakuna ufanisi. Hivyo, ni muhimu hatua za haraka zikadiriwe ili kupunguza ubadhirifu na upotevu wa pesa za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie kuhusu sera na sheria zetu. Tanzania tuna sifa ya uandishi wa sera na sheria nzuri na vitabu vizuri, lakini tatizo kubwa la sheria zetu hazieleweki na jamii kubwa ya Watanzania ambapo jamii hii ndiyo wadau wakubwa wa sheria na sera hizi. Kwa sababu hizi, ufanisi wa maendeleo inakuwa haufikiwi kwa sababu hakuna ushirikishwaji wa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, uelewa wa jamii kuhususiana na sera na sheria ni ndogo sana na hivyo inathibitishwa na tafiti za uelewa wa baadhi ya sera kama ifuatavyo:-

- Sheria ya Mazingira - 7.5%;
- Sheria ya Madini - 3.8%;
- Sheria ya Ardhi - 3.8%
- Sheria ya Maji - 2.5%;
- Sheria ya Uvuvi - 12.5%; na
- Sheria ya Misitu - 11.3%.

Mheshimiwa Spika, ndiyo sababu kukawa na migogoro mingi katika jamii zetu kutokana na uelewa mdogo. Hivyo ni muhimu na kuna haja kubwa juhudi za makusudi zikachukuliwa ili kuongeza uelewa wa sheria kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda - Waziri Mkuu kwa kukabiliana na changamoto nyingi za nchi yetu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia - Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Muu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuonyesha kuyatekeleza majukumu yake vizuri kwa manufaa ya Watanzania wote. Napenda pia kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada zao za kusaidia kuboresha na kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nina maoni yafuatayo:-

Mosi, naomba bajeti ijayo Madiwani wasiendelee kupewa posho, badala yake wapewe mshahara. Aidha, Wenyeviti wa Vijiji wafikiriwe kupewa posho; Katiba mpya iweke wazi kuhusu nafasi ya Madiwani katika nchi yetu.

Pili, naomba Serikal ipitie upya mpango wake wa awali wa kuwaruhusu madaktari kuendesha hospitali na maduka ya dawa, binafsi. Niaminivyo mimi, lengo la utaratibu huu ulikuwa ni kuwaongezea kipato nje ya

kazi zao za kawaida. Lakini kwa kuwa *demand* zao zimekuwa zikiongezeka kila siku, basi ni vyema mtazamo wa *demand* hizo uangaliwe kwa kuangalia pia ruhusa wanazopata kwa kupata vyanzo vyao vingine vya mapato.

Mheshimiwa Spika, nashauri posho mpya zizingatie Daktari afanyae kazi kwenye hospitali za umma na hana *private hospital* ili mchango wao kwa umma uwe mzito na mkubwa, kuliko sasa ambapo kazi kwa umma ni ya muda mfupi kuliko kwao, yaani kwenye *private* huko wakitaka Serikali kuwalipa zaidi.

Tatu, napenda kupata maelezo kuhusu maendeleo ya Hospitali ya rufaa ya Mtwara. Serikali imejipangaje kumalizia ujenzi wa hospital hii? Wananchi wa Kanda ya Kusini wamechoka kusikia wimbo usiokwisha wa Hospitali ya Rufaa, kwa fedha chache. Ni vyema fedha za ujenzi za kutosha zitengwe ili kazi imalizike.

Nne, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imetenga ekari za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi *(VETA).* Ni maoni kwa bajeti ya mwaka 2013/2014 ili ujenzi uanze kama ilivyo kwa baadhi ya Halmashauri zilizopata fedha.

Tano, Halmashauri nyingi nchini, baadhi ya Watendaji wake hujihusisha na mambo ya siasa. Kwa ajili ya kuhakikisha utawala bora, ni vyema utaratibu uwekwe ili kubaini Watendaji wa namna hiyo na hatua za kuwathibiti zichukuliwe.

Sita, kuna tatizo kubwa la kutopatikana kwa pembejeo za korosho huku msimu wenyewe ukiwa sasa. Naomba Ofisi ya Waziri mkuu kusaidia kumaliza kero hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nami kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujikita hasa kwa maeneo ya vijijini. Kwa kuwa kigezo kinachotumika hivi sasa kuandaa na kupanga bajeti ni kuzingatia zaidi idadi ya watu, imekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo vijijini ambako kuna idadi ndogo, kulingana na mijini. Licha ya ukweli kwamba mjini kuna fursa nyingi za huduma za kijamii kulinganisha na vijijini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umesababisha mlundikano wa huduma na mahitaji ya maendeleo ya Mjini na Makao Makuu ya Wilaya huku wananchi wanaoishi pembezoni wakitaabika kwa kukosa huduma au kulazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hizo mijini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, Wilaya ya Ngorongoro kama zilivyo Wilaya nyingi nchini, ina uhaba mkubwa wa huduma za afya, lakini kuna tatizo la ziada limejitokeza Wilayani humo. Kumekuwa na mlundikano wa huduma za afya katika Makao Makuu ya Wilaya eneo la Loliondo, Sakala na Waso ambayo haizidi umbali wa kilometa tano, kwa

kuwa na Hospitali ya Wilaya na Vituo viwili vya Afya huku sehemu kubwa ya Wilaya ikiwemo Kijiji cha Naan, Kata ya Enguserusambu kilichopo umbali na zaidi ya km 70 ikiwa haina hata Zahanati na kusababisha wananchi kutegemea tiba asili itokanayo na mitishamba.

Mheshimiwa Spika, pale Waso, kuna hospitali inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, Jimbo Kuu la Arusha ambayo inatumika kama Hospitali ya Wilaya kwa Serikali kutoa ruzuku ya dawa na watumishi kama madaktari, wauguzi na wakunga.

Mheshimiwa Spika, ukitoka Waso hadi kijiji kingine cha Oloipiri, zaidi ya kilometa sita, pia kuna Kituo kingine cha Afya na hivyo kufanya eneo lenye umbali usiozidi kilometa 15 kulundikwa vituo vitatu vya afya na Hospital ya Wilaya wakati wananchi wa maeneo mengine hawana hata huduma ya msingi ya Zahanati. Huu ni mgawanyo wa rasilimali usiozingatia usawa hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, sio kama napinga uwingi wa huduma za afya, sehemu moja kama uwezo unaruhusu, ninachopinga ni kulundika huduma hiyo Makao Makuu ya Wilaya au Vijiji vinavyokaribiana nayo huku sehemu nyingine zikikosa.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, katika miaka ya 2000, Serikali iliamua kujenga Kituo cha Afya katika eneo la Sakala, ambalo liko na haja ya kujenga kituo Kingine cha Afya eneo la Sakala kwa sababu kile cha Holando na Hospital ya Wilaya vingetosha kabisa

kuwahudumia wakazi wa Makao Makuu ya Wilaya Ngorongoro. Fedha hizi zingetumika kujenga Zahanati kwenye vijiji vingine visivyo na huduma ya afya kama Naan na Enguserusambu.

Mheshimiwa Spika, hii imekuwa kero sana kwa Nagonjira wanaotoka maeneo ya Naan hasa akina mama, kwani wao ndiyo wauguzi na pia wajawazito wamekuwa wakiishia kutokuhudhuria kliniki na bado, kuishia kujifungulia kwa wakunga wa jadi na kutokupata huduma za chanjo ya magonjwa ambukizi ya surua na *chickenpox* na kuongeza idadi ya vifo kwa akina mama wakati wa kujifungua hasa wale wanaoshindwa kujifungua kawaida, kwani wanakuwa hawana huduma ya *operation*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka jana tu walikufa watoto kumi kutokana na ugonjwa wa Surua. Je, kwa hali hii tutapunguza vifo kwa akina mama wajawazito na vifo vya watoto wachanga kutokana na magonjwa ambukizi au vifo vitokanavyo na malaria?

Mheshimiwa Spika, naomba pia nionglee suala la msongamano wa magari katika Mkoa wa Arusha. Siku za hivi karibuni kumekuwa na msongamano mkubwa wa magari kutokana na ufinyu wa barabara, idadi ya watu kuongezeka na pia magari haya kuongezeka kwa idadi kubwa siku baada ya siku. Imefikia wakati sasa ukitoka Arusha mjini kuelekea *KIA*, inachukua muda wa zaidi ya saa moja tofauti na zamani dakika 45 tu au pungufu unakuwa umeshafika *KIA*.

Mheshimiwa Spika, Arusha ni mji ambao umekua ukiongezea nchi hii pato kubwa kutokana na utalii, lakini msongamano huu umekuwa kikwazo sana kwa watalii na pia wakati wa Mikutano ya kimataifa ambayo mingi imekuwa ikifanyika ndani ya Mkoa huu. Mfano, Mkutano wa *AFDB* ambao ulifanyika Arusha kwa siku tano ulikuwa na wahudhuriaji 3000.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara ya *TBL,* kontena ijengwe kwa kiwango cha lami ili iweze kupunguza msongamano huu. Kwanini barabara hii inaungana na barabara ya *ESSO* - Ngarenaro hadi uwanja mdogo wa ndege Kisongo na kuelekea Mbuga za Wanyama.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia uhaba wa watumishi katika Wilaya za pembezoni kumekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi kwa sababu ya kusingizia mazingira magumu ya vijijini kana kwamba huko hakuna watu wengine wanaoishi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia ya watumishi kusema uongo na kutumia hila na ujanja ili kuhamia katika maeneo ya mijini. Hili limefanyika katika Wilaya ya Longido kati ya Septemba na Oktoba mwaka 2011. Baada ya kuripoti kazini, watumishi hawa walitoweka, mmoja kwa kutoroka kazini na hadi leo hakuna taarifa zozote zinazosema yupo wapi; na mwingine kwa kushirikiana na baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Arusha kupata uhamisho wa muda kwenda Tanga kwa kile kinachodaiwa kazi maalum.

Mheshimiwa Spika, kinachozua utata kwa mtumishi huyu aliyehamia Tanga, ni kitendo cha Katibu Tawala Mkoa *(Evaline Hamisa)* kutokua na habari ya uhamisho huo. Inadaiwa kutolewa na ofisi yake, kwa mujibu wa habari, barua ya mtumishi huyo ilisainiwa na Elgin Nkya.

Mheshimiwa Spika, watumishi hawa wamehama vituo vyao vya kazi bila kufikisha hata kipindi cha miezi na kwa mujibu wa *RAS* mbele ya Mkuu wa Mkoa (Muhongo Magesa) aliyetembelea Longido hivi karibuni, yeye alishakataa ombi la mtumishi huyo kuhama, lakini akazungukwa na mmoja wa Maafisa wake ofisini kwake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Ofisi ya Mkoa, Arusha imeshaanza uchunguzi wa jambo hili, lakini naomba Waziri Mkuu wakati anahitimisha, aeleze Bunge hili Tukufu kama Ofisi yake ina taarifa hizi na je, hatua gani zimechukuliwa dhidi ya Afisa aliyehusika kutoa uhamisho kinyume cha sheria? Je, watumishi hao bado wanaendelea kupokea mishahara?

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo ni ya muhimu sana hasa katika kipindi hiki ambacho taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali inapoeleza kuwa Taifa linapoteza mabilioni ya fedha kwa malipo ya mishahara hewa kwa watumishi wasiokuwepo kazini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ila napenda kuchangia kuhusu

kilimo cha umwagiliaji. Kilimo hiki ndiyo njia pekee ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Kwa mantiki hii, kuna haja ya kufafanua maamuzi ya makusudi ya kuwekeza katika ujenzi wa mabwawa ya kati na mabwawa makubwa ili tuwe na uhakika wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, vile vile tuwekeze katika ujenzi wa *schemes* za umwagiliaji. Waheshimiwa wabunge, tumekuwa tunasita kutoa maamuzi, Serikali iwekeze kwenye *schemes* za umwagiliaji na kuzifufua zilizokufa. Mfano, Wilaya ya Mkalama zina mabonde mazuri ya umwagiliaji na *schemes* zilizokufa zikifufuliwa zinaweza kulisha Wilaya ya Mkalama na tukajikomboa na upungufu wa chakula bonde la Msingi, Mpambala na Mwangeza.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iwapeleke baadhi ya Wabunge kwenda  na Mawaziri wa Wizara husika, kujifunza katika nchi za Japani, India, Vietinam, China, kilimo cha umwagiliaji. Wakishajifunza waje waanze utekelezaji na kusambaza teknolojia hii hatimaye kuenea nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, nimeona kama nchi tajwa hapo juu ina uwezo wa kulisha takribani bilioni 1.3. Sisi idadi ya watu bado ni ndogo na bado tuna eneo kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukaua nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda kwa kazi nzuri anayoifanya katika kusukuma maendeleo na Ustawi wa Tanzania. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Hawa A. Ghasia - Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Katibu Mkuu wa Wizara - Ndugu Hussein Ketanga, Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania, Makatibu Tawala wa Mikoa, *DCs* na Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara hii. Aidha, tunawashukuru wananchi wote kwa kuunga mkono juhudi zote zinazofanywa na Serikali inayoundwa na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, suala la amani ni suala muhimu sana. Madaktari wameamua kwa makusudi kabisa kufanya mgomo ambao ni ukatili dhidi ya raia wa Tanzania. Ni uvunjifu wa Katiba sehemu ya tatu ya utangulizi juu ya haki na wajibu muhimu, namba 14, inazungumzia haki ya kuwa hai. Katika sura ya sasa, baadhi ya watu, vikundi vya watu ikiwemo baadhi ya wanasiasa wamejiingiza katika kutetea zaidi maslahi ya watu binafsi tena yaliyo katika lengo la kutopata suluhu na kutozingatia na kujali uhai wa binadamu wenzao waonyimwa matibabu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pole sana kwa Daktari aliyepatwa na janga la kihalifu, kama madaktari wenzake wangeendelea na mgomo angetibiwa na nani? Hali hiyo inaleta hisia kali

miongoni mwa jamii na hakika kuhatarisha maisha ya madaktari wenyewe. Yawezekana baadhi ya watu wanaoshuhudia ndugu zao kutothaminiwa na kutibiwa hospitali, wakifikia kulipiza kisasi, hiyo ni mbaya sana. Lakini pia Vyama vya Siasa vinavyoshabukia, vikundi binafsi, watu binafsi wanaoshabikia migomo hiyo, pia nao wachunguzwe kama Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Martha Mlata alivyoshauri, isije ikawa kuna mchezo mbaya wa baadhi ya vikundi kujihusisha na hali hiyo ili kuleta chuki kwa Serikali.

Kiongozi wa Chama cha Madaktari alisema, ameomba Polisi ifanye kazi ya uchunguzi ili kubaini uhalifu huo. Ni jambo jema, lakini: Je, kama Polisi nao wangegoma, nani angechunguza? Maisha yetu yanategemeana, hivyo ni vyema kuepuka mambo yasiyo na tija kwa jamii kwa maslahi mapana ya jamii. Serikali iendelee kufanya jitihada kubwa kuhakikisha kuwa watu hao wamebainika (wahalifu na majambazi) wa Daktari Ulimboka, wanakamatwa.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa hawajafika kukaa kwenye viyoyozi kama Wabunge wa Chadema walivyodai. Wamekuja kutimiza wajibu wa dhana ya utawala bora wa kusikiliza Wawakilishi wa wananchi, Waheshimiwa Wabunge kupata ushauri na hisia za Wabunge juu ya kero zinazowakabili wananchi ili kuzifanya kazi kama Chama cha Mapinduzi kinavyotaka.

Juu ya Bwawa la Kawa, suala lililotolewa na Mheshimiwa Keissy nikiwa kama Kiongozi wa Serikali, Mkoa wa Rukwa, suala hilo tulikaa kikao cha pamoja

kati ya Uongozi wa Mikoa wa Rukwa, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mbunge Mipata mwenye Jimbo na mwekezaji, Mheshimiwa Mbunge mstaafu - Dkt. Mzindakaya na tukafikia mwafaka kuwa Wizara itakwenda eneo linalohusu kuzunguka chanzo cha maji cha bwawa la Kiwa na kulitengeneza kwa mujibu wa sheria. Hivyo, mradi huo uendelee kwa faida ya wananchi wa vijiji vya Ntendo, Nkundi na Fyengereza. Serikali za vijiji pia vilihusishwa.

Mheshimiwa Spika, mbolea kufika kwa wakati mwafaka (mwezi wa Tisa) ni muhimu kwa Mikoa ya Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Iringa ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri na kilimo chenye tija. Wananchi wa Kata ya Kihagara Mbinga (Nyasa) walijitolea kufyatua matofali 370,000 kwa ajili ya Kituo cha Afya, lakini hadi leo hamna kilichofanyika pamoja na mchango wangu wa bajeti ya mwaka 2011/2012, inakatisha tamaa ya wananchi kujitolea, hata mimi Mbunge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na neema kwa kumjalia Waziri Mkuu kuwaamsha Wazanzibari ambao walikuwa wamejisahau pale alipowaeleza mbele ya Bunge lako hili Tukufu kwamba Zanzibar siyo nchi na kwa hilo likapelekea Wazanzibari waliolala kushtuka na kuelewa kosa lao.

Mheshimiwa Spika, kadri muda unavyozidi kwenda, masuala ya Muungano pamoja na kero zake

zinazidi kuleta matatizo na kwa mujibu nilivyoisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, haikutilia maanani kero za msingi ambazo zinautetereshа Muungano wetu. Imekuwa hadithi za Abunuwasi kwamba kuna vikao ambavyo vinafanyika eti kutatua kero za Muungano, lakini ni dhahiri kwamba hakuna chochote kinachoonyesha ukweli juu ya kupatikana ufumbuzi wa utatuzi wa kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kutokana na misingi hii inayofanywa kwa makusudi kabisa juu ya kupuuza jambo hili, natahadharisha kwamba huko tunakokwenda siyo kuzuri kama vile Waswahili walivyosema kwamba: “Nyota njema huonekana alfajiri.” Inavyoonekana, wenzetu wa upande wa pili hawana nia njema na Muungano huu na mnaonekana kuichukulia Zanzibar kama sio mshirika wa Muungano, bali ni sehemu tu ya Tanzania wakati hilo ni kosa. Bila ya kuungana kwa Tanganyika na Zanzibar, Tanzania isingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, kupuuzwa kufanyiwa marekebisho kero zitokanazo na Muungano kumeanza kuleta viashiria vya yale yanayotokea Zanzibar. Nachelea kusema kwamba hali ni njema. Siwezi kusema hivyo hata kidogo, na haya yote yanachochewa na Muungano huu ambao umechukua mamlaka yote ya Zanzibar na kuyaweka mgongoni mwa Tanganyika kwa kutumia kivuli cha Muungano.

Mheshimiwa Spika, Muungano unaweza ukawa jambo zuri sana, hasa ikiwa faida zake zitagusa pande

zote za Muungano, lakini ilivyo sasa, kero na changamoto zake zinafunika faida zake kwa upande mmoja wa Muungano huu. Hivyo basi, ni vyema kabisa kero hizi za Muungano zikaangaliwa kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Wizara zisizohusiana na Muungano ndani ya Serikali ya Muungano ni kuonesha dhahiri kwamba kuna Serikali ya Tanganyika ndani ya Serikali ya Muungano. Hoja hii inasababishwa na mkanganyiko huu wa masuala ya Muungano. Kwa mfano, ikiwa kuna Wizara 26 zilizoundwa na Rais Kikwete, lakini Wizara za Muungano kwa ujumla wake ni sita tu ikiwa ni pamoja na Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Elimu ya Juu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, na Wizara ya nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano. Wizara 20 zinazobakia zinaongozwa na Serikali gani? Je, hiki si kiini macho na kuonesha kwamba kuna Serikali ya Tanganyika ndani ya Serikali ya Muungano ambayo iko wazi wazi, lakini haitaki kutamkwa kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, naelewa katika hili mtakimbilia kifungu cha 64 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini hata hivyo, litakuwa siyo jibu sahihi litakalomaliza kiu ya upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielezee nafasi ya Rais wa Zanzibar katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *Articles of Union* inasema kuwa Rais wa Zanzibar atakuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, lakini imepindishwa pindishwa

na sasa Rais wa Zanzibar ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri. Je, hii siyo dharau kwa Wazanzibar? Ni kwanini hili lilitokea? Je, Wazanzibar walihusishwa vipi katika majadiliano yaliyobadilisha kuondoa nafasi ya Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano? Hivyo huu si uonevu tunaofanyiwa Wazinzabar, hivyo tuseme Mheshimiwa Waziri Mkuu hili hamlielewi, kwamba huu ni Muungano wa nchi mbili huru, na siyo nchi na Jimbo? Zanzibar ni nchi iliyo huru, lakini pamoja na hayo yote, kero za Muungano zinakuwa kama zinazotiwa *petrol* na hili suala la mafuta yaliyogunduliwa Zanzibar ambayo yote yalikwishawekwa wazi katika orodha ya mambo ya Muungano. Lakini cha kusikitisha, madini yote yaliyoko Tanzania Bara siyo ya Muungano. Suala hili ni sawa na ule msamiati usemao: "Chako chako, changu chako." Yaani cha Tanganyika ni cha Tanganyika, na cha Wazanzibar kuwa cha Tanzania nzima. Haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lazima ijue kuwa kadri siku zinavyokwenda, Muungano huu unapoteza umaarufu wake hasa kwa sababu ya kubadilisha makubaliano ya Muungano yanayofanywa mara kwa mara kiholela. Ieleweke kwamba, Muungano huu ni wetu sote. Ni lazima tufike mahali tukubaliane kwamba Muungano huu uwe wa hiari, usiwe wa lazima na mabavu kwa upande mmoja kujiona kuwa una nguvu zaidi kuliko upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sikuwatendea haki Waislam ambao kwa namna moja au nyingine, ikiwa sitawaomba kurejeshwa kwa Mahakama ya Kadhi kwa upande wa Tanzania Bara. Huu ni unyanyasaji wa

kidini, ni kinyume na uhuru wa kuabudu jambo ambalo limetamkwa katika Katiba. Kwanini suala hili la Mahakama ya Kadhi lipingwe Tanzania Bara ambapo pana idadi kubwa ya Waislamu kuliko Kenya, Uganda, India na hata Uingereza? Kama hili siyo ubaguzi, ni nini? Waislamu wenzetu walioko Chama Tawala na hata Chadema wanaogopa kulisemea jambo hili kwa kuogopa vyama vyao, Mjue kwamba suala hili msipolitetea, mtakwenda jibu nini kesho mbele za Mungu na Waislamu wote ambao hamwatetei kupata haki zao juu ya kuundwa Mahakama ya Kadhi? Wanayoyafanya na wanayofanyiwa yatakuwa ndani ya shingo zenu, pamoja na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima alionijalia katika siku ya leo na mimi nichangie.

Mheshimiwa Spika, nachangia kuhusu UKIMWI. Ingawa katika hotuba ya Waziri Mkuu ukurusa wa (61) unaeleza Tanzania imepata mafanikio makubwa kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI kwa asilimia 25, ni sawa na ni habari njema. Naipongeza juhudi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maendeleo haya, bado juhudi za makusudi zifanyike. Mimi mawazo yangu, UKIMWI unaonekana umezoeleka na sasa hautishi tena, umekuwa ni kitu cha kawaida tu.

Mheshimiwa Spika, vishawishi bado ni vingi sana ambavyo Serikali inashindwa kudhibiti. Miongoni mwa vishawishi ni kutokuwa na utamaduni wa kitaifa juu ya

maadili ya Mtanzania. Tanzania hatuna maadili ya mavazi, wanaume na wanawake.

Mheshimwa Spika, leo Tanzania mwanamke kuvaa nusu uchi ni jambo la kawaida. Huu ni ushawishi kwa wanaume wengi, nguvu zao walevi na wala unga wamekuwa chanzo kikubwa kwa ongezeko jipya la magonjwa ya UKIMWI. Hawazingatii kulinda afya zao. Sasa nakwenda ukurasa wa nne kuimarisha demokrasia na Muungano.

Pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kusifu ukuaji wa demokrasia kwa kushiriki wananchi kwenye masuala ya kisiasa, bado yapo mambo mengi ambayo ni pingamizi zinazokosesha wananchi wengi haki za msingi. Mfano, mtu anajiandikisha kwenye daftari la kudumu, jina lake linakuwemo ndani ya daftari. Ikifika siku ya uchaguzi ndani ya daftari jina lake linakosekana, hata akiwa na kadi ya kujiandikisha haruhusiwi kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote. Katika mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu kwa kuzungumza, nilieleza mambo mengi juu ya kwamba Serikali ilisaidia Shirika la Nyumba la Taifa katika kutimiza malengo yake. Lakini Serikali pia itimize jukumu lake la kulisaidia shirika hasa katika madeni ya wapangaji wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika madeni ya Shirika kwa wateja wake, wastani wa Shilingi bilioni 6.6 zinadaiwa.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa wadaiwa sugu ni baadhi ya taasisi za Serikali zaidi ya Shilingi bilioni mbili zinadaiwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isiwe miongoni mwa wadaiwa sugu, ilipe na inaweza kuwasaidia watu wa shirika kuweza kujenga nyumba za bei nafuu zaidi ya 100.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, katika utatuzi wa changamoto za Muungano, mwaka uliopita kati ya hoja 13 ni mbili tu zilizopatiwa ufumbuzi kwa hesabu za haraka haraka chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iharakishe katika utatuzi wa kero hizi za Muungano ili Serikali itimize jukumu lake la kutenda haki kwa upande wa pili wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, rada ni suala la Jeshi. Jeshi ni ulinzi na ulinzi ni jambo la Muungano na Muungano ni kati ya nchi mbili huru Tanganyika na Zanzibar. Hapa naiuliza Serikali, ni kwa mazingira gani au ni vigezo gani vilivyotumika kugawa au kuzitumia pesa hizi na Zanzibar isihusishwe? Je, huko ni kuutendea haki upande wa pili wa Muungano? Aidha, pesa za *EPA* zote zimeelekezwa kwenye Kilimo Kwanza: Je, fungu la Zanzibar katika haki hii liko wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa imani kabisa, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anipe majibu maridhawa kwa mustakabali wa nchi yetu.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuandika yale ambayo sikuweza kuyagusia katika mchango wangu wa kusema.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, jambo la msingi na muhimu sana ni kutafuta njia ya kudhibiti fedha zilizokusanywa, kudhibiti matumizi mabaya, kuhakikisha ukusanyaji bora wa kodi, kuwa na mipango mizuri ya maendeleo hasa kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzingatia mambo haya manne, jambo kubwa sana na muhimu sana kuliko yote, ni kuwa na utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji na utawala bora ndiyo unaoleta nidhamu ya ukusanyaji wa kodi zaidi, ya matumizi mazuri ya fedha za umma, ndiyo unaoleta usawa wa haki na sheria.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuangalia rasilimali watu kwa maana ya vijana. Vijana ndiyo tegemeo kubwa la Taifa letu na ndiyo wenye nguvu za kuliendesha Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni lazima kuwe na *programme* maalum ya ajira kwa vijana, na kulisimamia kifedha ili kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, hali ya makazi ni jambo muhimu sana, lakini ujenzi umekuwa mgumu mno. Mtu wa kawaida hawezi kujenga nyumba kutokana na ughali wa vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Miji, Vijiji tuangalie upya bei za saruji na bati ili vijana wengi waweze kujenga nyumba za kuishi. Hili ni vyema liangaliwe kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Waziri Mkuu kuandaa mpango maalum wa usafiri wa ndege katika kufufua lile Shirika la Ndege na liwekeze katika kusimamia kwa umakini sana suala hili la usafirishaji. Hili litatupati fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, elimu ni kila kitu? Lakini cha kusikitisha, elimu yetu imeendelea kuporomoka. Hii ni kwa sababu Kitengo cha Ukaguzi kimekuwa hakipati fedha hata kidogo, wakati ina kazi kubwa sana. Lakini cha kushangaza, baada ya ugawaji wa elimu kutoka Wizarani kwenda TAMISEMI, Kitengo cha Ukaguzi kimebakia Wizarani. Hivyo, wamebakia, hawapati fedha za kutosha, athari zake ni pamoja na kutofanya ukaguzi. Hivyo Walimu kutofanya kazi zao vizuri na watoto pia kutofanya vizuri. Ni lini basi kitengo hicho kitapewa fedha na ama kuwa katika TAMISEMI, au Elimu ya Msingi na Sekondari kurudi Wizarani?

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi iliyo na hekta milioni 44.3, lakini cha ajabu 24%, yaani hekta milioni 11 hazitumiki au hazijawekezwa kwa kuwa kuna mabadiliko makubwa ya tabia nchi, hatuna kimbilio lingine zaidi ya kilimo cha umwagiliaji. Uzuri ni kwamba nchi hii imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya maji ikiwa ni pamoja na maziwa na mito. Tuna eneo la hekta milioni 29.4 za kilimo cha umwagiliaji, lakini ni hekta 344,000/= tu zinazomwagiliwa sawa na asilimia 1.1. Tukiweza kumwagilia, ina maana hatutakuwa na tatizo la chakula, lakini ajira zitakuwepo na lishe bora. Hakuna jambo baya kama kuomba chakula. Tanzania ni nchi iliyopo katika *strategic area*, kwamba tunazungukwa na nchi sita zisizo na bahari ambapo tungeweza sana kusaidia kusafirisha bidhaa mbalimbali zikiwemo chakula.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kwa *strategic area* tuliyonayo na maji yaliyotuzunguka tuwe ombaomba wa chakula. Maji ni uhai na bila maji hatuwezi kuishi. Maji imekuwa ni tatizo sugu na wote tunajua ni jinsi gani magonjwa yatokanayo na maji machafu yanavyowasumbua wananchi. Fedha nyingi zinatumika katika hospitali zetu kutibu magonjwa haya, fedha ambayo ingeweza kutumika kwa sekta ya kuboresha maji. Moshi Vijijini Kata ya Mbokomu kwa miaka 20 sasa hatuna maji, kisa wananchi wa Rau ambapo chanzo cha maji kipo, wamekatalia maji hayo kwenda eneo lingine na hata kutishia kuwadhuru wote watakaokwenda kufanya shughuli pale.

Mheshimiwa Spika, hivi ingekuwa penye chanzo cha maji ni mali hodhi ya wakazi hao, leo Misri ingekuwa wapi? Wakazi wa Dar es Salaam wangepata wapi maji?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia Waziri wa maji wafuatilie jambo hili.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuipongeza sana Serikali kwa hatua inazochukua kuboresha huduma za jamii na maendeleo kwa ujumla, licha ya changamoto nyingi zinazokabili uchumi wetu. Hivyo naunga mkono bajeti hii. Aidha, natoa wito kwa Serikali ishughulikie yafuatayo:-

Naomba Wilaya ya Kahama igawanywe kuwa Wilaya tatu za Vishetu, Kahama na Msalale, mapendekezo yalishapitishwa katika vikao. Naomba Majimbo ya Uchaguzi, Kahama yaongezwe kwa kuunda Jimbo jipya la Halmashauri ya Vijiji Kahama. Pendekezo hili lilishapitishwa na vikao vya Wilaya. Naomba Serikali itambue mtando mpya wa barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na Halmashauri ya Msalala. Naomba Halmashauri ya Msalala ianze mwaka huu wa fedha 2012/2013. Naomba maeneo mengine ya kisekta yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kusema naunga mkono bajeti hii. Naunga mkono kama wananchi wa Msalala walivyoniagiza kwa matarajio kwamba kuanzia sasa na siku za usoni,

Serikali itatumia bajeti hii na nyingine zijazo kujibu changamoto za umasikini Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kuna *contradiction* kubwa sana ya utajiri wa Mikoa na maendeleo katika Mkoa. Kwa taarifa tu, Mkoa wa Shinyanga una sifa zifuatazo: Una idadi kubwa ya wananchi kuliko Mkoa mwingine wowote. Watu ni nguvu kazi ambayo ingekuwa *productive* kama wanavyoitumia Wachina, Shinyanga ingekuwa na utajiri mkubwa wa kipato kwa wananchi wake. Mkoa unaongoza kwa uzalishaji wa madini ya almasi na dhahabu, uzalishaji wa pamba, unaongoza kwa idadi kubwa ya mifugo, na Mkoa huu ni miongoni mwa Mikoa mitatu inayozalisha tumbaku kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa zote hizi, Mkoa una sifa mbaya zifuatazo: Mkoa unaongoza kwa mauaji ya albino na mauaji ya vikongwe kwa imani ya ushirikina, kutokana na elimu duni na huduma mbaya za afya; Mkoa umekuwa wa mwisho mtihani wa Darasa la Saba miaka mitano mfululizo; unaongoza kwa uwiano mbaya kati ya idadi ya Shule za Msingi na Sekondari; unaongoza kwa uwiano mbaya kati ya idadi ya shule za *'O' level* na *'A' level;* unaongoza kwa kuwa na uwiano mbaya kati ya idadi ya shule na idadi ya shule za bweni; unaongoza kwa kuwa na uwiano mbaya kati ya idadi ya shule za sekondari na shule za sekondari zenye umeme; unaongoza kwa kupata njaa na kuhitaji msaada wa chakula kila mwaka na Mkoa huu unaongoza kwa kuzalisha wakimbizi wa ndani kwa jina la wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huo, *it is no wonder* kwamba Mkoa unaongoza kwa kuwa na uwiano mbaya kati ya idadi ya watu na idadi ya viongozi kwenye nafasi za maamuzi za kisera na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hali hii haifai na haipaswi kuachwa kiendelee. Naomba Serikali kuanzia bajeti hii, ianze kujibu hii *human development paradox in* Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ijengee uwezo Mkoa wa kunufaika na rasilimali zake, yaani watu, mifugo, mazao, madini na kadhalika, kwa kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa msingi wa umasikini wa wananchi Mkoa wa Shinyanga ni ukosefu wa elimu, Serikali iweke msukumo katika elimu kwa Mkoa wa shinyanga kwa kufanya yafuatayo:-

Kutoa fedha zote za chenji ya rada kuendeleza elimu Shinyanga kwa kukamilisha majengo ya nyumba za walimu, mabweni, umeme, vitabu na maabara. Kwa mfano, Jimbo la Msalala pekee lina maboma 200 ya nyumba za Walimu na maboma 250 ya vyumba vya madarasa toka mwaka 2004 wakati wa Mradi wa MMEM. Maboma haya hivi sasa yanabomoka na wananchi wamegoma kuchangia miradi mingine mipya ya elimu kwa kudai kwamba nguvu zao zilizotumika kujenga maboma hayo zinapotea bure bila Serikali kukamilisha miradi hiyo. Kuongeza bajeti ya elimu kwa Mkoa wa Shinyanga kwa kuhakikisha ahadi

ya kujenga *VETA* kila Wilaya, hasa Kahama ambayo ina migodi miwili mikubwa ya Buzwagi na Bulyanhulu, lakini wananchi wake hasa vijana hawapati kazi kwa kukosa utaalamu na ufundi.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya madini *(MDA)* iwekwe wazi na zipitwe upya ili kama taifa tunufaike. Mikataba hii imekuwa ikilalamikiwa sana. Serikali iruhusu Mkoa kunufaika na rasilimali zake za madini kwa kukubali mapendekezo ya Tume ya bomani ya kugawa mrahaba kati ya Serikali kuu na Wilaya, upo mgodi kwa uwiano wa 60 kwa 40 kama ilivyotoa kipaumbele na ilivyohusu wananchi wa Lindi na Mtwara kupatiwa umeme wa gesi kwanza kabla ya wengine. Halmashauri ziruhusiwe kutoza *service levy* toka migodini kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982.

Msimamo huu wa kutoruhusu *service levy* kutozwa migodini imepotezea Kahama zaidi ya Dola la Kimarekani 8,000,000 tokea mgodi wa Bulyanhulu ulipoanza uzalishaji rasmi mwaka 2001 na Dola la Kimarekani 1,200,000 tokea mgodi wa Buzwagi ulipoanza uzalishaji mwaka 2008 kwa wastani, kwa Kahama kulipwa Dola za Kimarekani 400,000 tu kwa mwaka kutokaa migodi hii miwili kama, *"consolidated local levies"* badala ya *service levy* ambayo ni 0.3% *of gross turnover,* Kahama inapunjwa zaidi ya Dola za Kimarekani 2,100,000. Aidha, kwa kuwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 imeruhusu Halmashauri kutoza *service levy* toka mwaka 2010. Serikali inaombwa iruhusu Kahama kutoza ushuru huo *retrospectively* na hivyo ipatiwe chenji yake, yaani Dola za Kimarekani 4.2

za miaka miwili toka mwaka 2010. Serikali iendelee na juhudi za kutatua migogoro kati ya wananchi na wawekezaji wanaovuna rasilimali za Shinyanga hasa madini. Naomba Serikali ilipatie ufumbuzi tatizo sugu la wachimbaji wadogo kukosa maeneo ya kufanyia kazi. Serikali kwa kushirikiana na mgodi wa Bulyanhulu imalize mgogoro wa fidia ya wananchi waliohamishwa kupisha mgodi wa Bulyanhulu mwaka 1966 kwa kuwalipa wadai.

Mheshimiwa Spika, Shinyanga inapata mvua za kutosha kwa muda wa mfupi, Serikali isaidie kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Mabonde ya Chela, Ntobo, Bulige, Kabondo na Ngogwa (Jimbo la Msalala) na Mwakitolyo na Salawe (Jimbo la Solwa) yanafaa kwa kilimo cha mpunga na yanaweza kulisha Mkoa mzima wa Shinyanga. Agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mtemi Nkumbi la kupanua *scheme* ya umwagiliaji ya Chela litekelezwe sasa. Ni aibu kwa Shinyanga kutokuwa na *scheme* hata moja ya umwagiliaji yenye kufikia Shilingi bilioni moja. Aidha, ni aibu kwa kufanya Mkoa wa Shinyanga kuwa *permanent food dependent*. Nguvu kazi kubwa iliyoko Shinyanga inapotea bure na hii ni hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe viwanda vya kuongeza thamani kwa mazao yanayozalishwa Shinyanga hasa pamba na mifugo. Hivyo, Serikali ianzishe au iwezeshe kuanzishwa viwanda vipya vya nguo na nyama Shinyanga. Siyo haki kwa wafugaji wa Shinyanga kuendelea kutangatanga na mifugo yao mingi kwa kukosa malisho bila kuwasaidia kupata soko la uhakika la mifugo yao. Ni aibu kwa zao la pamba

kuendelea kuwa zao la wafanyabiashara kutajirika huku bei ikiporomoka kila mwaka. Tunaomba viwanda vya nguo na mafuta ya pamba Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianze kutekeleza miradi mikubwa ya miundombinu ya maji, umeme na barabara ili kuchochea maendeleo Shinyanga kwa kutekeleza kwa kipaumbele miradi ifuatayo: mradi wa maji ya Ziwa Victoria kwenda Kagongwa na Isaka na vijiji vitakavyopitiwa na bomba hilo vya Mondo, Penzi, Banhi, Mwalugulu, Gembe, Sungamile, Kishima, Kagongwa, Iponya, Isagehe, Malenge, Sangilwa, Mashigini, Mwakata, Itogwanholo, Isaka stesheni na Ntungulu uanze mwaka huu. Ahadi ya kuwapatia maji wananchi waishio jirani na bomba kuu la maji toka Ziwa Victoria kwa umbali usiozidi kilometa 12, vijiji vya Kabondo, Mwanase, Magobeko, Izuga, Matinje, Nduku, Busangi, Mhama, Bulige na Butegwa itekelezwe mwaka huu.

Mradi wa ujenzi wa barabara ya lami kuunganisha Kahama na Geita uanze mwaka huu. Nasikia mgodi wa Geita wamekubali kugharimia ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami upande wa Geita. Naomba Serikali izungumze na kukubaliana na *ABG* ili nao wagharimie ujenzi wa barabara hiyo upande wa Kahama. Kubalianeni mtakatana kwenye kodi na mrabaha siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, miradi ya umeme vijijini ambayo maombi yalishapelekwa *REA* toka 2010 itekelezwe. Miradi iliyoombewa kwa Jimbo la Msalala ni kupeleka umeme Vijiji vya Busangi, Nyamigege,

Nyambura, Ngongwa, Ngaya, Bulige, Chela na Ntobo. Mradi wa umeme kwenda Bukombe kupitia vijiji vya Lunguya, Shilela, Ikinda, Nyikoboko na Segese vilivyoko Jimbo la Msalala nao uanze mwaka huu maana umeahidiwa toka mwaka 2004, enzi za awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla. Ningepewa na ningetakiwa kuchangia mjadala mzima (wote) wa bajeti ya Serikali kwa sentensi moja tu ningesema 'tutekeleze mpango wa maendeleo wa miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016) kikamilifu tupime mafanikio, tubaini changamoto, tuboreshe na kuendelea kutekeleza, mengi ya yanayopigiwa kelele na Waheshimiwa Wabunge yamo katika Mpango. Nitayagusia machache kama ifuatavyo:-

Kuongeza Pato la Taifa ili kuongeza uwezo wetu kibajeti (ukurasa wa 74 mpaka 84). Kwa mifano michache, suala la kukusanya kodi na kudhibiti misamaha ya kodi (ukurasa wa 74 hadi 75), na *super profit tax on minerals* (ukurasa wa 82) na mengi mengineyo. Nashauri kwamba tuandae majedwali ya utekelezaji na upimaji mafanikio kitaalamu *(on smart style).*

Mheshimiwa Spika, kudhibiti matumizi (ukurasa wa 84 hadi 86) njia mbalimbali zimeainishwa. Maoni mahsusi na maalum *(specific),* (ukurasa wa 78) nanukuu: *"the whole issue of strenghthening LGAs revenue collection and administration."*

Mheshimwa Spika, matumizi ya utaalamu zaidi hasa sayansi na teknolojia, chombo maalum kilichogunduliwa na Tume ya Sayansi na teknolojia ambacho kimetumika Kinondoni Dar es Salaam na kuongeza makusanyo mara nne, kifuatiliwe na kitumike katika Halmashauri zake.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mapato katika Halmashauri zikiwemo fedha za ruzuku mbalimbali, udhibiti zaidi kwa ujumla, matengenezo ya barabara za udongo na za kokoto *(earth roads and gravel roads)* kwa namna yanavyofanyika sasa hayazisaidii Halmashauri wala Taifa kwa ujumla wake. Ni matumizi mbaya ya fedha za Serikali. Sababu ni ukosefu na upungufu wa wataalamu, ukosefu wa maadili miongoni mwa baadhi ya wataalamu, ukosefu wa makandarasi makini na wenye sifa stahiki, ufinyu wa bajeti, kutawanya fedha chache katika miradi mingi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mapendekezo ya ufumbuzi kama ifuatavyo:-

- Kukamilisha kuundwa kwa wakala wa barabara za Halmashauri. Chombo hicho kitasaidia kuratibu vyema ukubwa wa kazi katika eneo kwa wakati kisha kugawa rasilimali chache zilizopo *(resource sharing).* Kwa mfano, hakuna haja kutawanya *resources* ambazo mwishowe hazileti tija.

- Fedha zipelekwe katika Halmashauri chache kila mwaka.

- Wahandisi na mafundi sanifu wagawanywe kule ambako kuna miradi.

- Usanifu *(design)* wa barabara huko uwe unaotosha kujenga barabara za kudumu angalau kwa *(standard design period),* barabara tunazojenga nyingi zinadumu kwa takribani miezi miwili au mitatu. Mzunguko uendelee kila mwaka au baada ya miaka miwili kugawa rasilimali na kuendelea na ujenzi wa barabara kimkakati.

Mheshimiwa Spika, nidhamu kwa wataalamu isimamiwe kwa kushirikiana na vyombo vya Serikali husika kwa mfano na Bodi ya Usajili wa Wahandisi. Kuanza kufanya ukaguzi kabla *(pre audit)* badala ya kusubiri *Post Audit results and effects.* Hii ituwezeshe kubaini na kuamua kupeleka fedha au la kwa matumizi fulani ili kujirishisha na uwezo wa kutumia kwa tija *(absorption capacity).*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kuu, Namtumbo – Tunduru, ujenzi wa barabara hii lilipaswa kutekelezwa na Kampuni *ya M/S Progressive* ambayo dalili zote zinaonyesha kuwa wameshindwa kazi. Ushauri *Tanroads* watumie vifungu sahihi vya Mkataba wawalazimishe kutekeleze mradi huu haraka sana. Vinginevyo, kwa Mkataba huo huo wawasimamishe na kuwanyang'anya kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tunduru – Mangaka - Mtambaswala iko katika hatua ya kutafutwa Mkandarasi. Ushauri wangu ni kwamba,

Serikali iharakishe kupatikana kwa Mkandarasi na Makandarasi. Lakini muhimu zaidi mradi wa Namtumbo na Tunduru utumike kama darasa kutupatia fundisho ili makosa yasirudiwe. Mchakato uwe makini ili apatikane mkandarasi makini, na barabara hiyo ijengwe kwa wakati kwa kiwango na kwa gharama mwafaka.

Mheshimiwa Spika, Tunduru imeacha kuwa Kisiwa, *National Grid*, imeikwepa.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza thamani ya Korosho (*value addition)*, nashauri kiwanda cha korosho bora kianzishwe. Kilichopo hakieleweki faida zake. Pia nashauri kwamba uzalishaji uongezwe, pembejeo zipunguzwe bei na zimfikie mkulima kwa wakati, bei ya korosho na malipo kwa wakulima kwa wakati liwe ni jambo la kipaumbele kwa Serikali.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, matumizi hasa yapo katika ununuzi wa samani za Ofisi hususan vyombo vya ofisini na nyumbani, magari na kadhalika. Naomba ufafanuzi wa juu ya azma ya Serikali katika suala zima za kupunguza gharama kwenye mambo yasiyo ya lazima na kuelekeza fedha hizo kwenye miradi ya maendeleo na huduma za kijamii.

Kwa mfano, katika *program* 10, kifungu cha utawala, *sub vote1001 items* ya Shilingi milioni 454 kwa kipindi cha mwaka 2012/20213, hata hivyo utaona matumizi ya namna hiyo hiyo yamefanyika mwaka 2011/2012, jumla ya Shilingi milioni 729 na kipindi cha mwaka 2010/2011 jumla ya Sh. 549,674,047/=

zilitengwa. Takwimu hizo ni kutoka katika Kitabu cha *Estimates of Public Expenditure Consolidated Fund Services (Section1) and Supply Votes (Ministerial) volume lll.*

Hoja hapa ni: Je, Serikali haioni haja ya kuangalia upya ni kwa namna gani udhibiti wa matumizi ya rasilimali? Kwa maana ya samani za ofisi kwa kuwa haingii akilini, kiti cha ofisi au hata samani nyingine za namna hiyo kununuliwa kila mwaka wa fedha. Uwajibikaji katika ofisi unaolenga ufanisi ni pamoja na ulinzi wa rasilimali za nchi zetu zile asilia, bali hata hizi zinazonunuliwa kwa pesa za walipa kodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa muda mwingi imekuwa ikipanga mipango na ku-*allocate fund* kwenye Halmashauri bila kufikia malengo tarajiwa. Hii husababisha Halmashauri nyingi kutotekeleza mipango ya maendeleo kama ilivyopangwa, kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni 55% tu ambazo zilipelekwa, hivyo kufanya 45% kutopelekwa. Hii inamaanisha kuwa tunakuwa na mipango mizuri katika makaratasi bila kulenga uhalisia wa kuleta maendeleo katika jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, suala la upandishaji wa madaraja kwa watumishi wa Serikali nalo limekuwa na urasimu mno na hata kuwa kero. Kwa sasa mtu hupanda daraja kila baada ya miaka mitatu, kimsingi kama mtumishi akiwa na umri wa miaka 30 mpaka afike daraja ‘H’ atakuwa ndiyo yupo/anafika kwenye

kipindi cha kustaafu. Hivyo naishauri na kupendekeza miaka ya kupandishwa madaraja ipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya Halmashauri nchini kumekuwa na mahusiano yasiyoridhisha ya kiutendaji kwa kuwa wakati fulani Madiwani hukataa ushauri wa kitaalamu katika baadhi ya masuala, hivyo Madiwani kuwa na maamuzi ya kisiasa zaidi ambayo yanaathiri wananchi, kwa kupelekea vikao kutoa maamuzi yasiyokidhi haja kwa wananchi, na katika baadhi ya Halmashauri, Wenyeviti wa Halmashauri wamekuwa na ubavu wa hata kuingilia maamuzi ya Watendaji na kushawishi Watendaji watekeleze baadhi ya masuala kwa manufaa *(interest)* yao.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itazame upya muundo wa Halmashauri zetu, hususan katika vikao vya maamuzi ili kudumisha mahusiano mazuri kati ya Watendaji na viongozi wa kisiasa ambayo yataleta tija kwa wananchi.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kunijalia afya njema kuweza kuchangia kwenye mjadala wa hoja ya Ofisi za Waziri Mkuu. Naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuboresha maisha ya wananchi kupitia Wizara na taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo na hasa TAMISEMI, ambayo ndiyo inayoshughulikia kwa karibu sana matatizo ya wananchi kwa kupitia Halmashauri zilizosambaa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo Serikali imeridhia kuyashughulikia na pia kuyatatua, naorodhesha yafuatayo: utawala bora na suala zima la kuzipa uhuru mamlaka ya Serikali za Mitaa ili ziweze kushughulikia na kutatua matatizo ya Wilaya zao kwa karibu sana. Kuzipatia Halmashauri 62 magari ili kuziwezesha kufanya ukaguzi wa ndani vilivyo. Pia napongeza uamuzi wa kuwakopesha Madiwani vyombo vya usafiri.

Vile vile naipongeza Serikali kwa kuwachukulia hatua za kinidhamu Wakurugenzi 24 wa Halmashauri mbalimbali pamoja kuwavua madaraka nane. Ombi langu lilikuwa, Serikali isiishie hapo, bali iwapeleke Mahakamani wale wanaostahili kushughulikiwa, ili hatua za kisheria zichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iharakishe kuzipatia wakurugenzi Halmashauri ambazo hazina Wakurugenzi. Kama kuna ugumu wa kutafuta Watendaji wa kupewa nafasi hizo kutoka nje, basi wale wanaokaimu wathibitishwe, kwani haiingii akilini kumwachia mtu kukaimu kwa muda mrefu kama kuna imani ya uwezo wake wa kuifanya kazi yenyewe. Vinginevyo, Halmashauri ziruhusiwe kuajiri Wakurugenzi wao. Vile vile mchakato wa kuajiriwa Maafisa Tarafa 145 ambao tayari vibali vya kuwaajiri vimepatikana, uongezewe kasi.

Mheshimiwa Spika, Mji Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Mji ambao ni mkongwe na ambao uko katika ukanda wa bandari nzuri ya kitalii, ukulima na uvuvi na unganisho lake na dunia ni kupitia Tanga kwa

barabara ya Tanga, Pangano. Barabara hii yenye urefu wa kilometa 51.7 tu imeendelea kuwa finyu na pia ya udongo miaka yote. Ahadi ya kuijenga kwa kiwango cha lami imetolewa mara nyingi hadi kumfanya Mheshimiwa Rais kuiweka kwenye ahadi zake wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2005. Barabara hii imo kwenye ilani ya CCM ya mwaka 2010/2015, lakini hadi leo Juni, 2012 bado dhamira ya kutekeleza ahadi hiyo haionekani.

Naiomba Serikali itujulishe hatima ya barabara hiyo ambayo inaunganisha Wilaya za Tanga, Muheza na Pangani, ifikapo Desemba, 2015, na ni nini kinafanyika sasa hivi, ukiachia barabara hiyo kuu, ahadi za barabara zinazounganisha vijiji vingi na Mji wa Tanga hazijaanza kutekelezwa pamoja na kuwa barabara hizo ni muhimu kwa maendeleo ya viwanda na ukulima katika vijiji hivyo? Kwa mfano, vijiji vya Majojoni, Kibafuta, Chongokani, Pande, Mwarongo, vinahitaji barabara, maji na umeme kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kujengwa barabara ya Tanga – Horohoro, lakini ninasikitika sana kuwa tangu mwaka 2009 hadi leo wananchi waliojitolea kubomoa nyumba zao kuwezesha ujenzi wa barabara hiyo bado hawajalipwa haki zao wakati wenzao ambao hawakujitolea hivyo wamelipwa. Serikali ielewe kuwa siku za mbele hakuna mwananchi atakayejitolea, tena hakuna fadhila za kufanya hivyo ni haya mnayoyatenda. Nilifuatilia suala hili mwaka 2011 kwa karibu, bali badala ya kupatiwa

ufumbuzi, Serikali kupitia Naibu Waziri wa Ujenzi, ilinieleza kuwa wamejenga misikiti 35.

Mheshimiwa Spika, Misikiti ni nyumba za ibada na Mwenyezi Mungu Sub-hanah-wa-taala naye anajua atazilinda vipi kwa anayezibomoa. Mimi ninachoomba ni fidia za wananchi wanyonge.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha elimu katika Wilaya ya Tanga kimerudi nyuma sana, kwani Shule nyingi za Kata kiwango cha kufaulu kwenye mtihani kwa Kidato cha Nne mwaka 2011 ambapo Shule nyingi waliofaulu, wachache ni daraja la Nne. Shule hizi hazina maabara na Walimu hawatoshi na hata zile ambazo zina hao Walimu wachache, Walimu hawa hawataki kukaa vijijini au hawawezeshwi kuishi huko.

Mheshimiwa Spika, suala la chenji za rada napendekeza zigawanywe kwenye Wilaya ya Tanga pia kwa kuchangia ujenzi wa maabara kwenye Shule za Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wa Wilaya ya Tanga, hali zao ni duni sana pamoja na nia zao thabiti za kujiendeleza kimaisha. Ninaiomba Serikali isimamie utoaji wa mikopo katika Wilaya hii ili mikopo hiyo iwafikie wananchi hao. Wenye mashamba wawezeshwe kwa kupatiwa nyenzo stahili zikiwa mbolea na matrekta.

Mheshimiwa Spika, narejea kusisitiza kuwa suala la kutokuwepo Mkurugenzi mwenye Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa takriban miaka miwili sasa tangu Mei, 2010

limedumaza sana maendeleo ya jiji hili. Mimi nitaunga hoja mkono pale tu nitakapohakikishiwa kwa vitendo kuwa Halmashauri hivyo imepatiwa Mkurugenzi. Nimelifuatilia sana suala hili bila jibu. Mwanzoni mwaka huu ilitulazimu Madiwani wa Halmashauri ni kumbadilisha aliyekuwa akikaimu kwa kuweka mwingine. Serikali isitufanye tukarejea rejea kitendo hiki.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye kuamsha ari ya maendeleo kwa Watanzania. Nawapongeza pia Waziri wa TAMISEMI na Manaibu wake wote, pamoja na Mawaziri wengine. Katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Watendaji Wakuu wa Wizara na viongozi wote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri ya bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninayo maeneo machache ya kuweka msisitizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika sera yake ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ya mwaka 2004 inayo programu na mifuko kadhaa inayogharimu shughuli za kilimo ikiwemo umwagiliaji. Lakini miradi mingi ya umwagiliji inalalamikiwa sana kuwa haina tija sana kwa wananchi. Changamoto iliyopo inaonekana ni namna ya miradi ya umwagiliaji inavyoratibiwa, *KHC* kanda, badala ya Halmashauri za Wilaya husika. Hali hii inaletea utatanishi katika utekelezaji na usimamizi wa miradi hiyo. Katika maeneo mengine, miradi ya

umwagiliaji inajegwa/inaanzishwa na kuwepo kama picha/mlima uliooteshwa bila kufanya kazi na maeneo mengine wananchi hawashiriki kikamilifu katika kuitunza kwa kuwa wanaiona kama sio ya kwao.

Kwa ujumla, miradi ya umwagiliaji ni mikubwa, inatumia fedha nyingi ambapo zisiposimamiwa vizuri itakuwa inapoteza dhamira nzuri ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Nashauri kwamba miradi ya umwagiliaji ifanyiwe uratibu, itambuliwe, itekelezwe na kusimamiwa na Halmashauri za Wilaya husika na siyo ofisi za Kanda.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi ambao kwa sasa wanautumia, ni mfumo mzuri endapo utasimamiwa vizuri. Kwa sasa mfumo huu unazo changamoto mbalimbali ambazo zikishughulikiwa, zitauboresha na kuwanufaisha wakulima. Mfumo wa stakabadhi ghalani kwa sasa unalalamikiwa sana na waananchi kwamba hauna nia njema hususan katika msimu unaoendelea sasa wa ufuta Lindi na mtwara. Bei dira zinazotolewa na vikosi kazi katika Mikoa husika ni mojawapo ya kikwazo kwa mafanikio ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, inaelekea bei dira zinapangwa huwa hawalinganishi na bei soko na bei za kimataifa. Kwa mfano, msimu huu wa ufuta, bei dira kwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni Sh. 1,000/= kwa kilogram moja, wakati bei ya wanunuzi binafsi ni Sh. 1,500/=. Hali hii inawafanya wananchi wakatae kuuza mazao yao katika Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa kuwa wanaona mfumo wa Serikali unawapunja. Nashauri Serikali kupitia Wizara husika ya Kilimo, Chakula na Ushirika ikasaidia kwa

kutoa mwongozo wa namna ya kupata bei halisi za mazao kwa kulinganisha bei za soko na bei za soko la kimataifa.

Wizara iwape uwezo vikundi kazi *(Task Force)* zinazoweka maoteo ya bei ya mazao kwa msimu husika, kwa kuwa ni dhahiri kabisa kuwa wanunuzi binafsi wanakuwa wanafahamu kuwa bei ya Soko la Kimataifa la mazao hayo. Pengine wanaopanga bei za mazao Mikoani wanapaswa kupewa mwongozo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linalolalamikiwa ni ruzuku za pembejeo. Mwaka 2011/2012 Serikali iliimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Bado zipo changamoto zinazoikabili. Kwanza, ucheleweshaji wa pembejeo za kilimio hususan mbegu huwa zinachelewa kuwafikia wakulima, kwa mfano mbegu bora kwa wakulima ambao msimu wa upandaji unatakiwa uwe Januari, mbegu zinakwenda Aprili. Madawa ya mimea kwa mfano dawa za kupulizia mikorosho *(sulphur)*, wakati wakulima wa korosho wanahitaji dawa hizo kabla ya mwezi Juni, mpaka sasa, tarehe ya leo madawa ya kupuliza mikorosho haijawafikia wakulima japokuwa dawa hizi zinatakiwa zinunuliwe na fedha za mfuko wa wakulima.

Naishauri Wizara ya Kilimo isimamie suala hili kwa ukamilifu ili kuhakikisha Hazina inatoa fedha za kununua pembejeo hizo mapema. Kimsingi, hakuna mfanyabiashara anayeweza kuagiza pembejeo za zaidi ya Shilingi bilioni mbili bila kuwa na uhakika wa kupata fedha kutoka Hazina. Katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa zao la korosho ambalo ndilo zao kuu la

biashara, bado wakulima hawajanufaika kabisa na ruzuku za pembejeo mwaka 2011. Wakulima wa korosho walinunua Mfuko wa *sulphur* kwa Sh. 50,000/=. Mwaka huu bei bado iko juu, Sh. 45,000/= mpaka Sh. 50,000/=. Ni dhahiri pia kuwa wakulima hawawezi kununua madawa hayo kwa bei hiyo, na endapo Serikali ingesimamia vizuri suala la pembejeo za kilimo, lingekuwa na manufaa zaidi kwa wana Mtwara na Mikoa yote inayolima korosho.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ili fedha hizi ziende kusukuma maendeleo ya Watanzania wote kwa ujumla.

**MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na bajeti nzuri, nina maelezo machache katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ya Ardhi ipitie upya mipaka ya Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Baadhi ya maeneo yaliyopo mpakani mwa Mikoa hiyo, yameingia kwenye Mkoa mwingine, mfano, eneo la Pugu Sekondari, lilikuwa Mkoa wa Pwani, lakini sasa lipo Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuwalipa posho na mishahara Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa kwani hawa wapo karibu zaidi ya wananchi na ndiyo wasimamizi wakuu wa fedha zinazokwenda vijijini, na Mitaani ambazo ni nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji wawe karibu na Maafisa Tarafa. Mara nyingi Wakurugenzi wengi katika maeneo mengi huwasahau kuwatumia Maafisa Tarafa na badala yake huwatumia Maafisa Watendaji na Kata pekee. Kuna dhana imejengeka kuwa Afisa Tarafa ni Msaidizi wa Mkuu wa Wilaya na siyo Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuongeza ufanisi bandarini ili meli zinapofika eneo la bandari zisikae muda mrefu kabla ya kushuka mzigo. Ni vyema Serikali ikachukua hatua za makusudi ili ucheleweshaji, kushusha mizigo bandarini usiwepo, kwani kwa hali ya sasa ambayo huchukua takribani mwezi mmoja kwa meli kukaa kabla ya kushusha mzigo. Hii ni gharama kubwa ambayo hatimaye inamwezesha mlaji wa mwisho ambaye ni mwananchi.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 23 na 24 kuna maelezo kwamba Serikali kupitia SUMA JKT inauza matrekta kwa bei nafuu ili wakulima waweze kukopa na hivyo kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Waziri Mkuu: Je, Serikali inafahamu chochote kuhusu *Agricultural Inputs Trust Fund?*

Mheshimiwa Spika, wakulima wengi wa Mkoa wa Arusha waliokopa matrekta kupitia *Agricultural Inputs Trust Fund* na wengi walishindwa kulipa mkopo kwa wakati, hasa walionunua matrekta ya Shilingi milioni 40

kutokana na ukosefu wa mvua za kutoshsa na hivyo kukosa mazao ya kuuza.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha hali ya uchumi wa Taifa, Serikali imesema kwamba ukuaji wa uchumi ulishuka kwa asilimia 6.4 mwaka 2011 ukilinganisha na asilimia 7.0 mwaka 2010 kutokana na ukame.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie utendaji wa *Agricultural Inputs Fund*, kwani wamewadhalilisha wakulima wengi kwa kutaka kuwafilisi mashamba yao na nyumba zao bila kuangalia kwamba wameshindwa kurudisha mkopo kwa wakati kutokana na ukame ulioipata nchi yetu na hivyo wakulima wengi kushindwa kuzalisha kama walivyotarajia.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa maelezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 62 kuhusu madawa ya kulevya, kwamba Serikali imejizatiti kukabiliana na tatizo sugu la usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya na kwamba katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Februari, 2012 kilo 349 za dawa za kulevya za viwandani na kilo 48,227 za bangi na kilo 10,680 za mirungi zilikamatwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu: Je, dawa hizi za kulevya zinapokamatwa huwa zinapelekwa wapi? Kwanini hatujawahi kusikia kwamba kuna utaratibu wowote uliowekwa wa kuziteketeza?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi alivyowasilisha bajeti ambayo kama itatekelezwa, itakuwa chachu katika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe masikitiko yangu kuhusu Serikali, kwamba imekuwa ni kawaida ya Bunge kupitisha bajeti hizi, lakini pesa zinazokwenda kwenye Halmashauri zetu hazifiki hata asilimia 50. Kwa hiyo, mipango mingi ya maendeleo na huduma nyingi za kijamii zinakuwa hazitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali ipitishe bajeti itakayokuwa inaweza kutekelezwa. Ikumbukwe kuwa Halmashauri ndizo zinazogusa maisha ya Watanzania kila siku. Naishauri Serikali ijitahidi kuhakikisha pesa zote zinakwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia kuhusu maslahi ya Madiwani. Kwa kweli nampongeza sana kwa kuona kuna haja ya kuboresha posho za Madiwani, pamoja na kuwapatia vyombo vya usafiri kwa mkopo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukumbusha tena kuwa, asiishie kwa Madiwani tu, pia kuna *charge* ya Serikali kuwaangalia sana Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa hasa katika maeneo ya posho, vyombo vya usafiri pamoja

na namna ya kuwahudumia pindi wanapopata majanga makubwa kama misiba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, huwa hawathamini, na Halmashauri hata pale inapotokea wao wenyewe wakafariki dunia, Halmashauri huwa zinakuwa haziko tayari kuratibu mazishi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikahakikisha pesa zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara, zinapelekwa na zinafika kwa wakati. Eneo hili ni muhimu sana katika ustawi na mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini kumekuwa na kero kubwa sana ya usafiri katika barabara itokayo Kinyamambo ‘C’ hadi Kisusa, na kuna baadhi ya maeneo hayapitiki kabisa kama Kijiji cha Kipanga Kijiji cha Mpangatazala, Kijiji cha Ihimbo.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itatekeleza wajibu wake, watu wetu pamoja na mali zao vitakuwa salama. Vijiji nilivyovitaja hapo juu vinalima mazao mengi sana, lakini mazao haya yanaharibika kutokana na ukosefu wa usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe tamko ni lini tutapata Halmashauri ya Mji wa Mafinga. Vigezo vyote vya kupata Halmashauri tunavyo na vikao vyote vya kikanuni vimeshafanyika.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini, asilimia 80 ya Jimbo langu halina maji safi na salama, Kata ya Mdabulo, Ihami, Mapanda, Kwaha, Mpangatazala, Ihalimba, Ifwagi na Kibengu zenye vijiji 34 hazina kisima hata kimoja na Serikali haionyeshi nia ya kutaka kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, niko tayari kuunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama atanieleza jinsi Serikali ilivyojipanga kutatua tatizo sugu la maji katika Kata hizi.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine inayotaka tiba katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini ni tatizo la dawa na watumishi katika Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, hii ni kero kubwa sana kwa wananchi wetu hasa watoto na akina mama wajawazito. Naiomba sana Serikali ihakikishe dawa na wataalam wa afya wanapatikana kwa wakati, kwani hauwezi kuahirisha magonjwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba sana uangalie Watendaji wa Halmashauri wanaoacha kutekeleza majukumu yao na kuanza kushughulika na siasa.

Mheshimiwa Spika, hii ni kero kubwa sana katika Halmashauri zetu. Pia naiomba Serikali ihakikishe chenji ya rada inafanya shughuli iliyokusudiwa

**MHE. ASHA MOHAMED OMARI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri yenye matumaini makubwa kwa Watanzania. Nami kwa ujumla naunga mkono hoja japo nilikuwa na machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu chenji ya rada, nchi yetu ni ya Muungano. Hivyo, fedha hizo inatakiwa igawanywe pande zote mbili Zanzibar na Tanzania Bara, kuliko zikatumika upande mmoja tu wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maoni yangu.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011/2012 Serikali ilitenga jumla ya Shilingi bilioni 94.02 na hazikuwasilishwa zote kwa wahusika. Napendekeza kwamba kwa kuwa mwaka 2012/2013, Serikali imetenga jumla ya fedha Shilingi bilioni 128.9, naiomba iongeze fedha kwenye bajeti hii kutokana na unyeti wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iharakishe kuenezwa kwa mfumo wa *LGHRS* kwa haraka katika Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara na madeni ya walimu, napendekeza Serikali iandae mkakati madhubuti wa kulipa malimbukizo ya madeni yote ya

Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchi nzima. Mishahara ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ipandishwe ili iwawezeshe Walimu hao kujikimu kimaisha. Serikali iandae utaratibu wa kuboresha na kujenga nyumba za Walimu Mijini na Vijijini, uandaliwe utaratibu wa kuwa na mfumo maalum ambao utawasaidia Walimu kukopa kwa masharti nafuu ili iwasaidie kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa inatumia matumizi makubwa sana ya kiutawala na kiutendaji kwa mamlaka mbili; ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma, ambazo zote zina nguvu sawa na eneo la utendaji ni moja. Napendekeza kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza matumizi katika mamlaka hizi, Serikali iimarishe Mamlaka ya Manispsaa ya Dodoma kwa kuajiri wataalam wa kutosha ili *CDA* ifikie kikomo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, napendekeza kwamba, wataalamu wa kilimo na mifugo waajiriwe na wapelekwe vijijini. Serikali ifikirie kujenga miundiyombinu kutoka vijijini ili wakulima wapate nafasi ya kuuza mazao yao kwa bei nzuri kwa manufaa yao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba, wanafunzi wote wanaosoma na kuhitimu katika Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo, waajiriwe mara moja. Chuo lazima kiwe na wataalamu wake wa kutosha na wapewe mafunzo ndani na nje ya nchi ilii kuwajengea uwezo kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa haraka kwa Jiji la Dar es Salaam, naunga mkono mpango wa Serikali wa *DART*. Naiomba Serikali ifanye utafiti wa kina na kutafuta njia ya kuondoa msongamano wa magari, ajali za barabarani na kuangalia hali ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba Serikali ijenge barabara za juu, ijenge reli za kuzunguka Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, wiki chache zilizopita ulitangazwa uteuzi wa Mabalozi ambao wanashikilia nafasi za Ukurugenzi katika Idara mbalimbali za Wizara ya Mambo ya Nje, nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, uteuzi ule uliozingatia umri, jinsia na taswira ya Kimuungano na nawapongeza mabalozi hao na kuwatakia utendaji mwema, lakini ingependeza zaidi kama kungekuwa na Mkurugenzi japo mmoja pale Wizarani kutoka Zanzibar na isiwe tu yule wa Ofisi ya Zanzibar ndiyo atoke Zanzibar, ila hata pale Makao Makuu ya Wizarani panahitajika Wakurugenzi kutoka Zanzibar kama ilivyokuwa wakati wa Marehemu Mzee Idrisa Abdul Wakil, alipokuwa Mkuu wa Itifaki Dkt. Salim Ahmed Salim, akiwa Mkurugenzi Idara ya Afrika na kadhalika. Bila shaka hii itadhihirisha sura ya Muungano na kupunguza manung'uniko hususan kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, uwiano katika Taasisi za Muungano hasa Wizara ya ulinzi na mambo ya ndani Wizarani, hauko kimuungano. Sidhani kama kuna

Maofisa wapatao watano katika Wizara ya Ulinzi ukiachilia mbali wale Maafisa wa JWTZ na kadhalika na Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Nje, angalau wapo wachache, lakini kutokana na utumishi wao kutumika ndani na nje ya nchi, hali katika vituo vyetu vya Ubalozi havioneshi uwiano ulio sawa, kwani katika Balozi kamili 32 na vituo vidogo vitatu tulivyonavyo na kuongeza idadi na kuwa na vituo (Balozi) 35 watumishi wa kada zote waliopo huko hawazidi 15 ukiondoa mabalozi watatu katika hao 15, Maafisa wa mambo ya Nje tu watano. Hii siyo kwa sababu hawapo, ila hawapangiwi kufanya kazi huko.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hoja ya bajeti ya Waziri Mkuu(Ofisi).

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayotakiwa kutoa majibu ya matatizo na unyonge, umaskini hasa wa Watanzania wengi walioko huko chini na wenye kipato kidogo, hususan wakulima na wafanyakazi na hata wafanyabishara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, Jambo la kwanza, Serikali ijitahidi kuhakikisha fedha zinatengwa kupelekwa katika Halmashauri, Manispaa ambazo ndizo zinagharimu miradi ya maendeleo kwenye Mitaa, Vijiji na Vitongoji inakwenda kwa wakati. Ni muhimu kuhakikisha pia kuwa fedha hizi zinatumiwa kutekeleza au kugharimia miradi hii, kamwe haziishi mikononi mwa Watendaji wabovu na wasiokuwa waaminifu.

Wapatikanapo hawa, basi wachukuliwe hatua ambayo ni mfano kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, hakuna maendeleo yatakayowafikia Watanzania walio wengi kama hatutawagusa na kuwainua katika kilimo, elimu, biashara ndogo ndogo, ardhi na makazi, afya na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, muda umefika sasa kilimo kiwe cha kisasa. Naipongeza Serikali kwa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza na vifaa kama matrekta na kadhalika. Lakini hivi vyote kwa mkulima mdogo ni sawa na *'window shopping'* kwa kuwa masharti na uwezo kwa kuvipata hawana.

Mheshimiwa Spika, naomba masharti ya pembejeo za kilimo pamoja na mashine husika kama *Pump* za maji na matrekta yapungue na yawe rahisi. Lakini pia tuchochee kilimo cha biashara *(commercial farming).* Tukifanya maeneo makubwa ya kilimo cha kisasa cha umwagiliaji na uwekezaji mkubwa, basi wakulima wadogo watafaidika kwa masoko, ujuzi na hata bei bora za mazao yao. Pia Serikali itafaidika kwa kuwa mazao yatasindikwa na kuuzwa nje ya nchi na kusaidia pato la kigeni.

Mheshimiwa Spika, napongeza kazi nzuri ya Serikali kuanzisha Shule za Kata na za Msingi kwa wingi. Muda sasa ni mwafaka kuboresha shule hizi kwa kuzipatia vifaa vya kutosha, madawati, madarasa, walimu wa kutosha na makazi ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, naomba fedha za ziada zilizopatikana kutokana na mgogoro wa rada, maarufu kama chenji ya Rada zielekezwe huko zisaidiane na bajeti iliyopangwa. Hapa uwepo umakini na usimamizi wa dhati.

Mheshimiwa Spika, biashara ndogo ndogo huletwa na biashara kubwa. Kwanza uwepo msukumo wa kusaidia zaidi biashara kubwa ili ziweze kutoa ajira na msingi wa biashara ndogo ndogo. Ofisi ya Waziri Mkuu ihimize kila Manispaa na Halmashauri zitenge sehemu maalum na rasmi za biashara ndogo ndogo. Zijulikane rasmi toka mwanzo na sheria ziwaelekeze walengwa kutumia maeneo haya. Hii itawapa wafanyabishara hawa maeneo maalum, lakini pia biashara zao zitapata urasimu na tija zaidi, Miji itakuwa safi na migogoro kati ya Mamlaka za Miji na wafanyabishara ndogo ndogo hazitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ndiyo msingi wa shughuli za binadamu na ndiyo kichocheo cha maendeleo. Tunajua bajeti yetu siku zote inakabiliwa na uhalifu na upungufu wa fedha. Lakini pia tunaelewa takriban 75% ya mapato ya Serikali yanatokana na shughuli za kiuchumi katika Jiji la Dar es Salaam. Vile vile tunafahamu msongamano wa magari ndani ya jiji la Dar es Salaam hadi Kibaha Pwani ilivyo kuwa kubwa na yanavyopotea mabilioni ya fedha kwa kila siku ijayo. Naomba sana sasa kwa makusudi Ofisi ya Waziri Mkuu ichukue hatua ya kuanza ujenzi wa madaraja ya magari kupita juu na kuongeza upanuzi wa njia za barabara *(overfly, roads, pumps and bridges).* Hata kwa mpango maalum, wananchi wako tayari kusaidia.

Mheshimiwa Spika, suala la makazi na hususan kwa vijana wanaotoka vyuoni na kuanza kazi, ni tete. Uwezo wa kukabili kodi za mwaka na kiasi chake ni mdogo. Hii hupelekea vijana hawa hata kutumia njia mbadala kupata kipato. Hii hushusha tija kazini kwao na kuletea Taifa hasara zaidi. Naiomba Serikali sasa kuwa ni wakati mwafaka kuona ni namna gani kutakuwa na utaratibu *(program)* maalum ya kuanza kufikiri namna ya kuwasaidia vijana wanaoanza kazi kupata makazi na usafiri kwa nafuu na malipo ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, baada ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mwaka 2009 kuna maeneo ambayo uchaguzi ulivurugika na hivyo uchaguzi haukufanyika na vijiji hivyo kukosa uongozi mpaka sasa hivi. Mfano, katika Jimbo la Singida Mashariki, Kijiji cha Kinyamwandyo, Tarafa ya Ikungi, Kijiji hiki mpaka sasa hakina Mwenyekiti baada ya masanduku ya kura kuchomwa na watu wasiojulikana. Kuna maeneo mengine ambayo uchaguzi ulifanyika, lakini Wenyeviti ama walifukuzwa au kujiuzulu wenyewe mara baada ya uchaguzi na vijiji hivi mpaka sasa havina Wawakilishi wao. Mfano ni huu ufuatao:-

Jimbo la Singida Magharibi, Kijiji cha Mdughuyu, Tarafa ya Ihenja, Kata ya Sepuke, pia kuna Kijiji cha Mnyange, Tarafa ya Ihenja na Kijiji cha Iyumbu, Tarafa ya Sepuka.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Singida Mashariki, kuna kijiji cha Mwau, Tarafa ya Ikongi na Jimbo la Singida Kaskazini, Kijiji cha Igauri, Tarafa ya Ilongero. Vijiji hivi vinakaa bila Wenyeviti wa Vijiji na hivyo kufanya utendaji kazi kuwa mgumu. Kwanini mpaka sasa Ofisi ya Waziri Mkuu iko kimya bila kuona umuhimu wa jambo hili?

Mheshimiwa Spika, tatizo la Mikutano ya *Full Council*, kumekuwa na tatizo kubwa la mawasiliano kati ya Wakurugenzi na Wabunge kuhusu mialiko ya Mikutano ya Mabaraza ya Madiwani. Mikutano hii ambayo ni ya muhimu sana, mara nyingi imekuwa ikifanyia aidha Wabunge wakiwa kwenye Vikao vya Kamati za Bunge Dar es Salaam au kwenye Vikao vya Bunge Dodoma. Hii maana yake ni kuwanyima Wabunge kuhudhuria vikao hivi ambavyo ni muhimu kwa maamuzi ya kuendeleza Halmshauri zao na hivyo kuwakosesha kutoa michango yao ambayo ni muhimu sana.

Mara nyingine inawalazimu Wabunge kuacha Vikao vya Kamati au vya Bunge ili waende kwenye *Full Council* maana wanashindwa kujigawa mara mbili. Kwa namna hii, Serikali haioni kuwa Mbunge anashindwa kuhudhuria vikao vyote vya Bunge au Kamati ambavyo ni wajibu mkubwa wa Mbunge? Naomba Serikali ije na majibu na tamko kwa Wakurugenzi ili wawe wanapanga Mikutano isiyoingiliana na ratiba za Bunge, maana hizi ziko wazi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni la Wakurugenzi kuwakataza Madiwani kuondoka na makabrasha yao baada ya vikao hivyo vya Baraza la Madiwani. Hili linatokea sana kila wakati katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Ninavyofahamu na sheria inavyosema, kabrasha ni mali ya Diwani kikao kinapokwisha sasa iweje Mkurugenzi alazimishe Madiwani kukusanya makabrasha hayo na kuyarudisha Ofisini tena kwa amri kali? Serikali itoe tamko hapa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wabunge wa Viti Maalum kukatazwa kuhudhuria Vikao vya Kamati za Fedha na Uchumi, tumekuwa tukilizungumzia sana suala hili. Sheria ya mwaka 1984, inayotaja Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi imeshapitwa na wakati. Tunaomba, irejewe upya, kwani inaleta ubaguzi kati ya Wabunge wa Viti Maalum na Madiwani wa Viti Maalum. Inakuwaje Diwani wa Viti Maalum ndiyo aweze kuingia kwenye Kamati hiyo na Mbunge wa Viti Maalum abaguliwe na sheria hiyo? Tunaomba Waziri wa TAMISEMI alitolee ufafanuzi wa kina jaribio hilo, kwani Wabunge wa Viti Maalum nao ni Wawakilishi wa wananchi kwa upana wake, hivyo ni vyema nao wangepata nafasi ya kushirikishwa kwenye Kamati hizi muhimu kama wanavyoshirikishwa kwenye *Oversight Committees* Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na

Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iangalie upya sera yake ya uwekezaji (WAWEKEZAJI) katika Sekta ya Ujenzi kupitia *TIC*, hasa misamaha ya kodi, kwani hakuna kitengo cha kutathmini vifaa hivyo, hata ndani ya *TRA* hakuna. Pia wakati wa kuuza majengo hayo, kama vile mahoteli yanauzwa katika bei ya soko wakati vifaa vya ujenzi havikulipiwa kodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu ya usafiri kwenye *construction management*, kuna kanuni ya *classification*. Miundombinu yote iliyokwisha jengwa iwe endelevu katika kuikarabati, yaani iliyo *class A,* iendelee kuwa *Class A,* wakati unajitahidi kunyanyua *class* nyingine zilizo chini yake *Class B*, kwenda *A*. *Class C* kwenda *B class D* kwenda *C* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashauri bandari zilizopo na hasa bandari ya Dar es salaam, Tanga na Mtwara zikarabatiwe na vipimo vya ufanisi na kuaminika vipewe kipaumbele, kwani usafiri wa majini ndiyo usafiri ulio rahisi na siyo ghali. Pia uwekezaji katika Reli, barabara na anga uimarishwe katika mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, elimu yetu mifumo yake iangaliwe upya, kwani mfumo tulionao kwa sasa kwa kiasi kikubwa hauzingatii utu wa kumwendeleza mwanadamu. Miongozo ya masomo hasa ya Hisabati na Sayansi katika Shule za Msingi na Sekondari inahitajika kuandaliwa upya iweze kuendana na kasi ya ukuaji wa Sayansi na Teknolojia katika karne ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nishauri uimarishaji wa Kitengo cha Maafa (majanga) katika Ofisi wa Waziri Mkuu hasa kuzuia maafa ambayo husababishwa na binadamu *(man made risk)* katika kuyagundua mapema ili kuweza kukabiliana nayo. Kitengo hiki kiwe tayari wakati wote na kiwe na wataalamu wa kutosha katika kushughulikia maafa ambayo hayatarajiwi kutokea *(Act of God).* Aidha, elimu itolewe kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, warsha na makongamano mbalimbali kuhusu namna ya kujikinga na majanga yakitokea. Pia elimu hii ianze na/au iingizwe kwenye mitaala yetu ya Shule za Msingi na Sekondari hata zile Taasisi za Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri kwa umuhimu wa pekee, janga linalotengenezwa na wanadamu (Watanzania) wachache wasiotakia Taifa letu mema kwa kupandikiza chuki na kulisambaratisha Taifa kwa kuhubiri ukabila, udini, ukanda, ubaguzi wa rangi na kadhalika. Wote wenye nia njema na Taifa letu tuungane kupiga vita janga hili kwa nguvu zetu zote, kwa ustawi na kuimarisha nguzo zetu za Taifa za hekima, umoja na amani.

Mheshimiwa Spika, kwa pamoja tutashinda.

Mheshimwa Spika, napendekeza kuhusu changamoto ya msongamano wa magari katika Jiji la Dar es salaam, kwa kuwa hili ni sawa na janga la Taifa, na kuwa kuwa wakati wa janga inabidi tufanye kazi kwa pamoja *(team work),* ni vyema wanajeshi wetu wa Jeshi la wananchi wa Tanzania wakisaidiana na Wizara

za Uchukuzi na Ujenzi na wote wenye nia njema washirikiane pamoja katika kufufua reli ya kuanzia Ubungo mpaka *station* (kituo cha kati). Pia reli kutoka Pugu hadi Kituo cha Kati ianze kutumika kutoa huduma ya usafiri jijini kwa haraka (sasa).

Mheshimiwa Spika, aidha, usafiri wa majini kwa kutumia meli kuanzia Bagamoyo – Mbweni – Kunduchi – *Mbezi Beach* – Msasani – Bandarini, yote yanawezekana tukishirikiana pamoja kwa kufuata ushauri wa wataalamu.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu Bajeti ya Ofisi yake kwa mwaka 2012/2013. Nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo inaelekeza kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Pamoja na hayo yote, naomba niorodheshwe na kuzungumzia kero mbalimbali zilizopo Wilayani kwangu Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na mambo mengine, inasema kuwa kila Makao Makuu ya Wilaya itapatiwa umeme Mkoa wa Mtwara. Wilaya zake zote zimepatiwa umeme, isipokuwa Wilaya yangu ya Nanyumbu. Mwaka wa fedha wa 2011/2012, Serikali iliahidi kuipatia Makao Makuu ya Wilaya ya Namyumbu (Mangaka) umeme wa kutoka Masasi. Hadi leo hii hakuna hata dalili yoyote wala jitihada zozote zinazoonekana. Ninaomba Serikali kupitia Wizara inayohusika iniambie ni lini Nanyumbu tutapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja kwenye mto Lukwamba, Kata ya Napacho katika Kijiji cha Mpombe ni kero kubwa inayowapata wananchi wa Mpombe, Ndechela, Mburusa na kadhalika. Wananchi wa maeneo hayo wanapata adha kubwa wakati wa masika, kwani wanashindwa kwenda kupata matibabu na kufanya shughuli nyinginezo za kibinadamu. Daraja hili inatengewa fedha kila mwaka, lakini kwanza fedha inayotengwa ni chache na kibaya zaidi haipatikani, hivyo kupelekea kutojengwa kwa daraja hili. Naomba nipatiwe jibu juu ya ujenzi wa daraja hili wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba Serikali itimize ahadi aliyoitoa Rais juu ya ujenzi wa barabara ya kutoka Nangomba mpaka Nanyumbu itakayounganisha na ile itakayojengwa kutoka Mangaka hadi Mtambaswala kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hali ya baadhi ya Shule Wilayani Nanyumbu inatisha, madarasa yamechakaa na mengine yanahatarisha maisha ya wanafunzi. Madarasa ya vijiji vya Mikuva, Napacho, Nandembo, Msinyasi, Liunga, Chivirikiti, Nakole ni baadhi ya Shule zenye madarasa chakavu. Nyumba za Walimu hakuna, vyoo navyo ni tatizo. Madawati hakuna na baadhi ya wanafunzi wanakaa chini. Hivyo naomba fedha za rada zijenge nyumba za Walimu, zitengeneze madawati na zijenge matundu ya choo. Pia kuna uhaba mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Nanyumbu kuna maeneo hayapati huduma ya simu za mkononi, hivyo ninaomba huduma ya simu za mkononi zijenge minara ya simu ili wananchi waweze kupata huduma hii. Maeneo hayo ni kama Likokona, Nakopi, Chivirikiti, Napacho, Lumesule, Nangomba na Marumba.

Mheshimiwa Spika, vijana Wilayani Nanyumbu wamesahaulika. Hawawezeshwi, hawapati mikopo ili waweze kuwa wajasiriamali. Hivyo, naomba wapatiwe mikopo, wapate fursa ya kupatiwa viwanda vidogo vidogo. Hivyo, naomba wakati wa majumuisho, niambiwe Serikali itawasaidiaje vijana wangu wa Wilaya ya Nanyumbu, kwani ni kundi lililokata tamaa.

Mheshimiwam Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii, Serikali imetenga fedha za kujenga Daraja la Mto Mongo Obakima kama ilivyo ahadi ili kunusuru hali ngumu ya wananchi wa vijiji vya Nghanga na Mwasengela Jimboni Kisesa?

Mheshimiwa Spika, kwanini Serikali isiunde Tume haraka sana ya kupitia mikataba ya viwanda na mashamba ambayo hadi leo hayajaendelezwa au kubadilishwa matumizi ili kutaifisha viwanda na mashamba na kuyarejesha Serikalini? (Zoezi la ubinafsishaji).

Mheshimiwa Spika, kwa nini hadi leo bajeti za Halmashauri ya Wilaya zinajadiliwa na kuidhinishwa kipindi ambacho Wabunge wanaendelea na Vikao

vya Bunge kinyume na maelekezo ya Bunge na Serikali? Serikali imechukua kiasi gani kutokana na taarifa mbalimbali za wizi na utoroshaji wa fedha nje ya nchi? *The Global Financial Integrity Report of 2008 of the heading "Illicit Financial Outflow from Africa."* Ilibainishwa kuwa kwa miaka 39(1977-2008), Tanzania ni nchi ya 13 kati ya nchi 20 zinazoongoza kwa utoroshaji na fedha za umma na kuficha nje na kwamba kwa kipindi hicho Tanzania imepoteza Shilingi trioni 11.6 na zimefichwa nje na wafanyabiashara na Watendaji wa Serikali. Hata utafiti uliofanywa na akina Ndikumana unadhibitisha haya.

Mheshimiwa Spika, *report* ya *one billion dollar question (how can Tanzania stop losing so much revenue?)* inaonyesha kuwa Tanzania inapoteza Shilingi bilioni 478 kutokana na *illicit capital flow account* kila mwaka. Katika *report* iliyotolewa na *Swiss Cental Bank* na *Swiss National Bank* kuwa fedha zimefichwa Uswiss na Watanzania, jumla ya Shilingi bilioni 315.5. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia hali hii isiendelee? Je, kuna mkakati gani wa kufilisi *account* hizo na kuzirejesha fedha hizo nchini? Akaunti hizo ni za akina nani? Je, Serikali inafahamu mkakati wa Benki ya Dunia wa kurejesha rasilimali zilizoibiwa? Kwa nini *illicit capital flow* iliongezeka mara dufu katika kipindi cha ubinafsihaji?

Mheshimiwa Spika, Serikali mwaka 2011 iliajiri mtaalamu mshauri wa kuandaa gharama halisi ya kusomesha mwanafunzi Chuo Kikuu hapa nchini *(student unit cost)* ili kuondoa tatizo la utozaji wa ada kiholela. Ni fedha kiasi gani zimetumika kukamilisha

mchakato huo? Matokeo ya utafiti huo yako wapi? Je, sasa *Student Unit Cost (SUC)* hapa nchini ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi za umma kuachwa kwenye Makampuni *(unclaimed funds),* fedha hizi hazijadaiwa na wahusika kwa muda mrefu na wenyewe ambao inakuwa vigumu kuwapata; mfano, faida na akiba za wateja, hisa ambazo hazijadaiwa katika soko la hisa Dar es Salaam, makato ya kisheria ya watumishi aliyeachishwa kazi au mtumishi aliyefariki, lakini mafao ya akiba yake inaendelea kutumwa katika Mifuko ya Hifadhi kama *NSSF* na *HIF*. Kimsingi, kisheria fedha hizi siyo za mashirika ambayo fedha hizo zinakuwa zimewekwa, lakini ni za mtu asiyefahamika *(unknown beneficiaries).*

Je, kwa nini tusitenge Sheria ya Fedha hususan wakati wa kupitisha *Finance Bill* ili kuyataka Mashirika ya Umma na Makampuni kuzisalimisha fedha au rasilimali ambazo hazijadaiwa *(unclaimed assets)* katika *account* maalum kama mapato ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, *CAG* ana uhuru kamili katika mambo ya ukaguzi, na hivyo ni lazima mamlaka inayoshughulikia maoni na mapendekezo yake pia iwe na uhuru kamili ili kuweza kushughulikia taarifa hizo bila kuingiliwa. Tatizo lilipo hivi sasa, Ofisi ya Mwendesha mashitaka Mkuu wa Serikali ipo chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hivyo haiko huru. Je, kwa kuwa ilishakubalika toka mwaka wa fedha 2010/2012 kuwa *DPP* awe na kasma yake, kwa nini hadi leo *DPP* hajateuliwa kuwa Afisa Masuuli? Je, ni lini Ofisi ya DPP, itajitegemea (*fully independent)?*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeridhika wakulima wa pamba, pamba yao kununuliwa kwa bei ya Sh. 660/= kwa kilo ilhali inafahamu gharama za uzalishaji?

Mheshimiwa Spika, kutokana na nia ya Serikali kupunguza matumizi yasiyo na tija hususan kuanzia mwaka 2012/2013: Je, kitendo cha Serikali kuzuia ununuzi na matumizi ya magari ya kifahari kumeliopunguzia Taifa mzigo kiasi gani cha fedha? Maeneo gani mengine ya matumizi yasiyokuwa na tija ambayo Serikali imepunguza na ni kiasi gani cha fedha? Je, kuna haja ya kuendelea kuwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye ukubwa ule ule na idadi ya Watumishi hao wakati majukumu mengi ya Wizara hiyo yanatekelezwa na TAMISEMI?

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuongeza fedha za maendeleo ili kuwezesha utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika mpango wa maendeleo, Ofisi yako imekuwa mfano mzuri wa kupunguza matumizi yasiyo na tija (TAMISEMI). *Programme* 10 (Utawala) *Sub Vote 1001* toka Shilingi bilioni 8.4 hadi bilioni 3.3. *Programme 10* (Sera na Mipango*) Sub Vote 1003*, toka Shilingi bilioni 2.1 hadi Shilingi bilioni 0.9. Je, kwa kuwa Wizara nyingi hazijafanya kazi nzuri, hii iliyofanywa na Wizara yako na kwa kuwa *Finance Bill* italetwa mwishoni, utakubaliana nami kuwa wakati tunapitia Wizara moja hadi nyingine tufyeke fedha zilizolundikwa katika matumizi yasiyokuwa na tija ili kuongeza fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kutimiza ahadi yako ya kuboresha maslahi ya Madiwani. Vipi kuhusu Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji?

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuongoza vyema utekelezaji wa shughuli na mipango mbalimbali ya maendeleo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri waliopo Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya ya kumsaidia Waziri Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Sasa ningependa kuchangia katika masuala matatu. Ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Tanga, Mfuko wa Taifa wa UKIMWI na lishe.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Tanga, Jiji la Tanga linakadiriwa kuwa na wakazi 298,881 *(2010 - Population Projections)* na lina Vituo vya Afya 55, ambavyo pia vinahudumia Wakazi wa Wilaya jirani na Jiji hasa Muheza, Mkinga, na Pangani. Kati ya Vituo hivi, 34 ni vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayowakabili Wakazi wa Jiji la Tanga ni kukosekana kwa hospitali ya Wilaya na jiji la Tanga. Hii imefanya huduma za rufaa Wilayani kutolewa na hospital ya Mkoa Bombo. Kutokuwepo kwa hospitali ya Wilaya kumepelekea kuwepo kwa mlundikano wa wagonjwa na kazi nyingi *(workbload)* kwa hospitali ya Mkoa.

Wahanga wakubwa wa hali hii ni wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, tayari Jiji la Tanga limeshapata na limetenga eneo la ekari 24 kwa ajili ya kujenga hospitali ya Wilaya. Gharama za ujenzi ni Shilingi bilioni 15, kwa mujibu wa *standards* za hospitali za Wilaya zilizowekwa na TAMISEMI. Halmashauri ya Jiji la Tanga tayari limeshatenga Shilingi milioni 100 kwa mwaka fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni kiasi gani cha fedha kimetengwa na TAMISEMI kwa mwaka 2012/2013 kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, ni lini Mfuko wa Taifa wa UKIMWI utaanzishwa? Kwa mujibu wa takwimu, karibu watu milioni 1.2 wanaishi na virusi vya UKIMWI (VVU) Tanzania, na karibu watu 100,000 waliambukizwa virusi vya Ukimwi (VVU) mwaka 2009. Wanawake ndiyo waathirika wakubwa wa UKIMWI. Mwitikio wa wananchi katika kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI na kutoa huduma kwa waathirika kwa kiasi kikubwa ulitegemea na bado unategemea fedha za wafadhili wa nje.

Ni ukweli usiopingika kuwa karibia asilimia 80 ya fedha kwa ajili ya miradi na program ya VVU/UKIMWI, ni za wafadhili wa nje. Wafadhili wa nje wanakaabiliwa na mtikisiko wa uchumi katika nchi zao na hivyo kupelekea kupunguza fedha za ufadhili kwa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati nchi imepunguza maambukizi ya UKIMWI/VVU, bado ugonjwa huu umebaki kuwa ni tishio kwa nchi zetu. Hivyo uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa UKIMWI ni lazima sasa upewe kipaumbele. Wakati wa kuanzisha mfuko huu ni sasa, ni lazima mfuko huu uwe wa wazi, upewe nguvu za kisheria na uanze kufanya kazi haraka sana. Pia ni lazima ufanye kazi kwa kutumia dhana ya *PPP*, kama baadhi ya nchi nyingine Afrika, Kusini mwa Sahara wanavyofanya. Pesa za Mfuko wa UKIMWI zimeweza kupatikana kutoka kwenye kodi za Serikali *(Government taxation* na *corporate social responsibility funds of private sector organizations).*

Mheshimiwa Spika, sekta ambazo tunaweza kuzi-*target* ni kama *oil* na gesi, mawasiliano, *banking and insurance, Aviations and Mantime, food and beverage* na wafadhili binafsi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Muswada wa kuanzishwa Mfuko wa Taifa wa UKIMWI uandaliwe na kupitishwa na Bunge ili tuweze kutatua kero, changamoto mbalimbali zinazotokana na UVV/UKIMWI hasa kwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ni lishe. Nimefurahishwa sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo pamoja na mambo mengine imeonyesha mikakati ya Serikali katika kupunguza tatizo la utapiamlo nchini. Ni kweli hili ni tatizo kubwa sana kwa mujibu wa ripoti ya *demography* na afya ya mwaka 2010 (TDHS 2010), wastani wa watoto 42 katika

kila watoto 100 wa chini ya miaka mitano wamedumaa, kwa Mkoa wangu wa Tanga ni asilimia 49,Dodoma ni asilima 56 na Lindi ni asilimia 54. Pia takwimu zinaonyesha kuwa watoto 47,500 chini ya miaka mitano hufariki kila mwaka kutokana na utapiamlo.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati za lishe zimeanzishwa katika Ngazi ya Taifa na Halmashauri, ningependa kusisitiza kuwa ni vyema sasa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha hali ya lishe nchini zipelekwe kwenye Halmashauri. Pia napendekeza kuwepo au kuanzishwa kwa Kamati za lishe katika ngazi za Kata. Ni vizuri pia Maafissa wa Maendeleo ya Jamii waliopo katika Kata kuhusishwa kwa karibu zaidi katika kuboresha na kuchochea lishe katika sehemu zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa imezingatia vipaumbele muhimu na kuona au kuwaona wanyonge kama waendesha pikipiki maarufu kama boda boda. Napenda pia kupongeza hotuba hii namna ilivyozingatia suala la rasilimali watu hasa Idara ya Afya na Waalimu. Watumishi hawa wakiongezeka, watatusaidia na kuondoa changamoto ambazo zimejitokeza za kuwa na Vituo vya Afya na Zahanati bila Waganga wala Wauguzi, na Shule za Sekondari na Msingi bila kuwa na Walimu jambo ambalo limeshusha ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, *Mwananchi Empowerment Fund* imeweza kutoa Shilingi bilioni 7.3 katika Mikoa ya Dodoma, Lindi, Manyara, Mtwara, Pwani, Rukwa, Ruvuma na Tanga. Fedha hizi ni chache sana, zinatakiwa ziongezwe, kwani huu ni mtaji wa msingi ambao utalikomboa Taifa kwa baadaye wananchi wakijengewa uwezo. Maana yake nchi itakuwa na mapato na changamoto mbalimbali zitakazokabiliwa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotengwa kwenye kilimo, haitoshi, iongezwe na pawepo dhamira ya dhati ya kuimarisha kilimo kujua kuwa kilimo kinaajiri watu wengi na ni fursa ya wazi kabisa. Vijana wakielimishwa kuiona na kuitambua fursa hii ya kazi za kilimo, mitaji itolewe kulibainisha hilo. Pembejeo zinazotakiwa kwa kilimo zitolewe kwa wakati, matrekta yapunguzwe bei na yaende Halmashauri waliko wakulima, siyo dhambi kama wananchi watakopeshwa kwa bei nzuri na mkopo wa muda wa miaka mitano na kuendelea. Masoko ya mazao ya wakulima ya uhakika yatahamasisha kilimo kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri za ujenzi wa barabara nchi nzima, naomba yafuatayo yazingatiwe:-

Kwanza naomba barabara za vijijini ziwe na wakala wa barabara vijijini kama ilivyo maji, umeme *(REA).* Barabara za vijijini ni muhimu, kwani ndiyo zinaunganisha maeneo ya uzalishaji katika Wilaya ya Nkasi na Jimbo la Nkasi Kusini ziko biashara za Kitosi, Wampembe (kilometa 68).

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nkana - Kala (kilometa 67) ina umuhimu wa pekee katika Jimbo la Nkasi Kusini, kwani barabara hizi zinaunganisha kanda mbili muhimu zinazotegemeana, yaani mwambao mwa Ziwa Tanganyika na Ufipa ya Juu. Eneo la mwambao wanakabiliana na vifo vingi vya akina mama na watoto hawana mawasiliano ya simu, barabara hizi ndiyo pekee zinategemewa.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa uchaguzi aliahidi kuzishughulikia barabara hizi ambazo kimsingi, Halmashauri ilishashindwa kwa kukosa fedha, wananchi wasubiri ahadi ya Rais wao.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi ya Benki ya Dunia. Miradi ya Chala, na kijiji cha Kamwanda inasuasua kupita kiasi. Pia maeneo ya Jimbo lote maji ni changamoto kubwa. Pengine utaratibu wa uhakika uweze kutafutwa. Benki ya Dunia katika miradi hii haiwezi kabisa kukabiliana na changamoto zilizopo nchi nzima. Kijiji cha Mpala kiko kwenye mpango katika awamu inayofuata. Tunaomba dosari zinazoonekana katika utekelezaji wa sasa zirekebishwe ili kasi iongezwe. Hapa kuna maradhi ya kuhara na kutapika kila wakati na chanzo ni maji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nkasi haina Chuo cha Ufundi licha ya kuwa na Sekondari zaidi ya 22. Tunaomba Chuo cha Maendeleo cha Chala kiimarishwe na kuwa *VETA*.

Mheshimiwa Spika, hotuba ni nzuri, nami naunga mkono hoja isipokuwa changamoto zifuatazo ziangaliwe:-

Mheshimiwa Spika, mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa, Halmashauri haijapewa wataalamu kubainisha vyanzo vyao vina *strength* kiasi gani *(how potential area)* upo umuhimu wa kutafuta wataalamu kupitia vyanzo vya Halmashauri zetu nchini ili kuweka malengo yanayolingana na *strength* ya vyanzo vilivyopo. Wanaokusanya mapato ya Halmashauri zetu siyo waaminifu, wanaiba sana na nina mifano ifuatayo:-

Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, kuna wizi mkubwa sana wa mapato yatokanayo na ushuru wa vyombo vya uvuvi pamoja na leseni za samaki na dagaa. Mimi pamoja na Mbunge mwenzangu Ali Keissy wa Jimbo la Nkasi Kusini, tulipatiwa risiti na wananchi katika risiti 10 tulizozifanyia kazi tuligundua yafuatayo: Fedha iliyokusanywa ilikuwa zaidi ya Shilingi milioni 2.7.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyoingia Hazina ya Halmashauri ilikuwa takribani Sh. 150,000/=. Ukipiga hesabu Sh. 27,000,000.00 - Sh. 150,000.00 = Sh. 2,550,000.00. Wizi wa ajabu, fedha haziingii kwenye Hazina ya Halmashauri na Wilaya, na wafujaji wapo tu.

Mheshimiwa Spika, pili, vitabu vingi vinavyokusanya ushuru vimepotezwa na wakusanyaji. Hao wakusanyaji bado wanafanya kazi kama kawaida. Naona matatizo kama haya yanahitaji ufumbuzi, wananchi watakata tamaa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Barabara wa Serikali za Mitaa una fedha kidogo na umeshindwa kukabiliana na changamoto zilizopo. Ushauri wangu ni kwamba kuanzishwe Wakala wa Barabara Vijijini. Wakala huyu atafanya kazi vizuri na rasilimali watu waliopo itatumika vizuri. Wahandishi wanakaa, hawatumikii kwa vile hakuna kazi, wamebaki wanyonge huku walio na taaluma kama wao waliopo Serikali Kuu wakitumia utaratibu wao vilivyo, mwisho, huweza kushawishika kirahisi kuanza kushirikiana na Wakandarasi wasiofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, mipango ya MMAM/MMEM/MMES, yote ina malengo mazuri na MMEM na MMES wanafanya vizuri. MMAM bado kabisa. Wananchi wamehamasishwa kujenga majengo, lakini yameshindwa kwisha kwa kukosa msaada walioahidiwa kuwa waazishe majengo na yatamalizika.

Mheshimiwa Spika, Waganga na Manesi hakuna; madawa katika Zahanati, hakuna; Walimu katika Sekondari hii, ni aibu na kukatishana tamaa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kupongeza hotuba ya Waziri Mkuu nimpongeze Waziri wa TAMISEMI na Manaibu Mawaziri pamoja na Watumishi wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, ndani ya hotuba ya Waziri Mkuu, imezungumzia habari ya kuanzishsa Kituo cha Kusaidia kuwakopesha vifaa vya kisasa katika Kata ya Rwamgasa – Geita. Naomba suala hili liwe dhahiri na fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha zipelekwe kwa wakati ili wananchi hasa wachimbaji wadogo wanufaike.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ninaomba Serikali katika bajeti ya mwaka huu ijenge Chuo cha Ufundi *(VETA)* Geita. Maana Wilaya yetu hatuna Chuo chochote cha *VETA*. Hii itawasaidia vijana wetu wanaomaliza Kidato cha Nne. Wilaya ya Geita inazo Shule za Sekondari zaidi ya 30. Hivyo, watoto wanaohitimu Kidato cha Nne ni wengi sana wanahitaji kupata ujuzi katika Vyuo vya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ninaomba Serikalli katika bajeti ya mwaka huu iweke kipaumbele katika kuboreshsa mazingira ya watumishi hasa kwa kujenga nyumba za Walimu na maabara. Vile vile kuwapa posho maalum kwa walio katika mazingira magumu, yaani *(hardship allowance).*

Mheshimiwa Spika, naomba waratibu wa elimu wapewe usafiri hata kama kwa kukopeshwa pikipiki, itawawezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaunga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mipango mizuri ya kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye jambo lifuatalo ili kuleta udhibiti wa fedha zinazokwenda katika Halmashauri:-

Kwanza, kuanzishwa kwa *financial communication protocol* ambayo malipo yote yaliyofanyika, mikataba iliyoingia na *Bank reconciliation* kwa kila mwezi zitumwe kwa Mwenyekiti wa Halmashauri, Mbunge wa Jimbo na kwa Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizo ziandaliwe na *DT*. Taarifa hizo zitasaidia kufanya udhibiti wa karibu kwa kila mwezi, hivyo itasaidia sana kulinda upotevu wa fedha za Serikali. Yakifanyika haya, fedha za Serikali zitakuwa katika udhibiti mzuri na hivyo kuepusha ubadhirifu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri Mkuu, Waziri wa nchi na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba zao walizoziwasilisha vizuri. Napenda kuanza kwa kusema kuwa siungi mkono hoja hii. Sababu zimetajwa kwa ufasaha katika hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Mchango wangu hapa utahusu kusisitiza au kushadidia yale ninayoona kuwa ni muhimu yazingatiwe na yatekelezwe haraka.

Jambo zito kabisa ambalo Serikali imezembea kulisimamia ni *propaganda* za udini, ukabila na ukanda. Siku hizi ni jambo la kawaida kumsikia Kiongozi wa CCM au Serikali, au dini akishiriki katika *propaganda* za namna hii hasa kwa lengo la kuvichafua Vyama vya Upinzani au kuichafua dini nyingine.

Mheshimiwa Spika, waasisi wa Taifa hili, walijenga misingi mizuri ya Utaifa na utangamano. Walipinga kwa nguvu zote ubaguzi kwa misingi ya udini ukabila na ukanda kwa kuchukua hatua za kuanzisha asasi na Programu za Kitaifa ambazo zilisaidia katika ujenzi wa msingi imara ya utaifa na uzalendo. Lakini kwa miaka 15 hivi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa pande zote mbili, imeshindwa kusimamia kwa uthabiti na umakini wa kutosha masuala haya. Baya zaidi, baadhi ya viongozi (baadhi ya Wabunge na Wawakilishi na hata Mawaziri) hushiriki katika *propaganda* chafu za udini, ukabila na ukanda, dhidi ya Vyama na dini nyingine. Serikali inapaswa kuchukua hatua kusimamia suala hili. Jambo la pili nitakalozungumza, linahusu fedha ya rushwa ya rada.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaotaka Serikali iwachukulie hatua wale wote waliohusika na rushwa hii ya ununuzi wa rada. Maswali ninayotaka Serikali iyajibu ni haya: Kwa nini, hadi sasa wahusika hawajachukuliwa hatua? Ni lini Serikali itawafikisha Mahakamani na hata kuwafilisi akaunti zao za nje? Kuhusu matumizi ya fedha hii, siyo busara kuitapanya kwenye mambo mbalimbali.

Itumike kwa jambo moja tu ili matumizi yake yalete tofauti.

Mheshimiwa Spika, mimi napendekeza fedha yote itumikie kujenga nyumba za Walimu katika Shule za Vijijini, hasa vijiji vilivyo pembezoni ambako Walimu hawapendi kwenda kufanya kazi kwa sababu hakuna nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu linahusu usambazaji wa pembejeo kwa njia ya vocha. Mfumo huu haujafanikiwa kwa kiasi kikubwa. Mfumo kwa kiasi kikubwa umechakachuliwa, unaishia kuwanufaisha baadhi ya Maofisa na mawakala waliopewa kazi hiyo. Wakulima wengi, mathalan wa Jimbo langu, wamekuwa wakihangaika kupata pembejeo hizo na wanapozipata, bei huwa ni kubwa sana hata wakulima wengi kushindwa kumudu bei ya pembejeo hizo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe maelezo kuhusu mauaji ya albino yaliyojitokeza hivi karibuni kule Arumeru Arusha.

Mheshimiwa Spika, suala la gesi kuingizwa katika mikataba kabla ya sera na sheria kuundwa, halikubaliki na wananchi wa Kusini. Tunataka mikataba yote ifike Bungeni, tuone uhalali wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe ufafanuzi kuhusiana na mabilioni ya Shilingi yaliyokutwa katika Benki za nje ya nchi, zikihusishwa mikataba ya gesi.

Mheshimiwa Spika, faida gani itapatikana kutokana na upatikanaji wa gesi na Mikoa ambayo haijaingizwa katika gridi ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe ufafanuzi kuhusiana na Mpango wa *SAGCOT*, kutohusisha Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, au Mikoa hiyo imeondolewa ukanda wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe ufafanuzi kuhusu umeme wa KV 133 katika Mikoa ya Kusini kwa ajili ya maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itoe ufafanuzi juu ya vifaa vilivyoharibika zikiwemo *X-Ray* na *Ultra sound*, lini vitapatikana au kurekebishwa? Pia ukosefu wa madaktari bingwa ikizingatiwa kuwa hospitali hiyo imepandishwa hadhi ya kuwa ya Rufaa, pia ukosefu wa wataalam wa kutoa dawa za usingizi katika hospitali hiyo, motisha kwa wafanyakazi na kuhusisha Ofisi ya *RAS* na malipo ya ununuzi wa madawa, chakula na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lini ukarabati wa Ofisi ya Mnyororo Baridi utakamilika ikizingatiwa kuwa hapo ndipo chanjo zote huhifadhiwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Manispaa ya Lindi, ambayo imepandishwa hadhi tokea Julai, 2010,

mpaka sasa Manispaa hiyo imekua ikipokea mgao wa bajeti, ule ule uliokuwa wa Halmashauri ya Mji ambayo ilikuwa na Kata 13 na sasa kuna ongezeko la Kata tano. Serikali itoe ufafanuzi kuhusu fedha za maendeleo na matumizi ya kawaida ili kukidhi matakwa ya Manispaa.

Mheshimiwa Spika, pia kuna nafasi nyingi zinazoendelea kukaimiwa kwa muda mrefu. Kwanini Serikali isiwapandishwe vyeo waliopo au kuwaleta wenye sifa za kuweza kuziba mapengo hayo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi, Serikali iliunda Tume kuratibu mashamba yote ya mkonge. Ni lini taarifa hiyo itakuja Bungeni?

Mheshimiwa Spika, kuhusu magari mabovu aina ya *Toyota Land Cruiser,* (maarufu kama vuvuzela) ambayo hayakuwa na viwango vya ubora, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na kuagiza magari hayo ukizingatia katika Mkoa wa Lindi, gari aina hiyo ya *RC* na la *RAS* hivi sasa yamekufa?

Mheshimiwa Spika, Stakabadhi Ghalani haimsaidii mkulima mdogo, kwani wakulima hukopeshwa na kulipwa kwa awamu tofauti, takribani mara tatu. Hii humfanya kushindwa kulipa karo za shule na huduma nyingine. Neno hili libadilishwe, badala ya “Stakabadhi Ghalani” iwe “Malipo Ghalani.”

Mheshimiwa Spika, Ikama ya walimu katika Shule za Msingi, fedha kidogo za *Capitation,* Walimu kukaa vituo vya kazi muda mrefu, Walimu kutopata nafasi za

kujiendeleza kwa wakati, waliojiendeleza kutobadilishwa kazi au kupandishwa vyeo au kuongezwa mishahara na kadhalika, hayo ni matatizo katika Jimbo la Lindi Mjini. Serikali itatoa ufumbuzi gani kuhusiana na matatizo hayo?

Mheshimiwa Spika, Serikali kutumia Benki moja katika fedha za Halmashauri kunazuia Halmashauri kuwa na uhuru kwa kuendesha akaunti katika hali ya ufanisi kwa vile fedha zinaibiwa kwa wafanyakazi wa Halmashuri kushirikiana na wafanyakazi wa benki.

Mheshimiwa Spika, benki inayotunza fedha za Halmashauri haitoi riba yoyote katika fedha hizo. Kama benki ingetoa riba ingekuwa chanzo kimojawapo cha mapato ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha walitangaza zabuni ya mabenki kutoa huduma kwa Serikali, lakini zabuni ilikuwa na kigezo cha benki kutoa huduma kwa Serikali katika Wilaya zote badala ya kugawa maeneo au aina ya huduma ambazo benki zingechagua kutoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itengue zabuni iliyotangazwa awali kati ya mwezi Machi na Aprili, 2012 na itangazwe upya.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri aliyoitoa ambayo imeaonesha matumaini makubwa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hotuba hii ningeomba Serikali itoe tamko kuanzia sasa kuwa katika shughuli zozote za Serikali ambazo zinajumuisha wananchi au kushiriki kwa wananchi kuwe na tamko la kuhimiza wananchi kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, iwe ni utaratibu kwenye mikusanyiko yoyote ya watu, suala hili liwe linazungumziwa kabla ya kuanza kwa sherehe au shughuli yoyote, vilevile hata viongozi wanapokwenda kufungua au kufunga shughuli yoyote msisitizo uwekwe kwa watu kulipa kodi. Lakini zaidi ya yote, ni suala la muhimu la wananchi licha ya kulipa kodi, vile vile wahimizwe kudai risiti.

Mheshimiwa Spika, kudai risiti iwe ni kauli mbiu ya Serikali, kwani kodi za wananchi zitathibitika kuwa zimeingia kwenye Mfuko wa Serikali. Kutokudai risiti, maana yake ni pesa zote kwenda kwa wafanyabiashara na Serikali kupoteza mapato ambayo yangerudi kwa wananchi na kuleta maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba kutoa ushauri wangu katika maeneo manne.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu katika Halmashauri zetu ni matatizo makubwa sana. Natoa ushauri kwako ili kutatua matatizo ya Walimu wa Shule

za Msingi na Sekondari kwamba, ingekuwa vizuri suala la elimu lirudi Wizarani moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, matatizo yamekuja kuongeza gharama au madeni ya Walimu yataongezeka kila mara. Kwa sababu malumbano yametokea kati ya Viongozi wa Halmashauri, hasa Sekta ya Elimu huchangia sana kuongezeka madeni kwa kutoa uhamisho na visasi au maslahi.

Mheshimiwa Spika, dhamira nzuri ya Serikali ya Chama chetu cha Mapinduzi ni nzuri, lakini awamu iliyopita, suala la pembejeo lilileta ubadhirifu wa hali ya juu sana iliyochangiwa na mawakala wenye tamaa. Wizi huu au ubadhirifu huu ulitokea pia Wilayani kwetu Kilosa. Natoa ushauri kwa Serikali kuwapa au kuwatumia *SACCOS* za Kata zenye uwezo au vikundi vya wakulima, kwa mfano, wakulima wa miwa wa bonde la Ruaha ambao ni wakulima wazuri na ni tegemeo kwa kiwanda cha sukari cha Iloko.

Mheshimiwa Spika, vikundi hivyo vina uwezo na wanajielewa wenyewe kwa wenyewe, muda mwafaka wa pembejeo na watalengwa wahusika moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yangu kwa kuweza kutuchimbia visima hadi sasa kwa kupitia msaada wa Benki ya Dunia. Tumechimbiwa visima, tunashukuru. Lakini cha ajabu, tulitaka watumalizie baada ya uchimbaji na kutukabidhi ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. Majibu tuliyopewa kuwa awamu ya pili haitaanza mpaka wamalize

uchimbaji kwa Wilaya yote, ndiyo waanze awamu ya pili ya upimaji na ujenzi wa *pump* na mengine.

Mheshimiwa Spika, vijiji vyetu tayari vimeshatoa au kuchangia pesa za asilimia 2.5 ya fedha na mradi huo toka muda mrefu sana. Naomba Wizara itoe amri kuwa baada ya uchimbaji tu, waanze ujenzi na kukabidhi kwani inaweza kuleta hasara iwapo itajifukia au kuweza kuhujumiwa na watu wasiopenda maendeleo.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana ni bomu kubwa kwa Serikali yetu. Natoa ushauri kwa Serikali yetu kutenga maeneo kwa ajili ya kilimo na pia kuwawekea dhamana kwa kukopeshwa zana za kilimo na pembejeo pia. Serikali yetu imeweza kutudhamini magari Wabunge wote, nadhani kwa mfumo huo huo ni vizuri ikawadhamini vijana wenye nia ya kujiajiri na naamini wataweza kulipa madeni hayo.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majukumu ya Wizara hii ni utekelezaji wa malengo ya *millennium* kuwapunguzia wananchi umasikini wa kipato cha chakula.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote tunaishi, tunafanya kazi kwa kuwa na maji. 'Maji ni Uhai'. Napendekeza kuwa, tuwekeze kwenye maji ili Watanzania wapate fursa ya kufanya kazi za maendeleo. Mpango wa *WSDP* toka mwaka 2006 - 2025 ambapo ulianza rasmi mwaka 2007 - 2025 kuweza kufikia asilimia 90 kwa vijijini na 95% maji mijini kwa kipindi cha *millennium* 2015, ilitakiwa kutolewa *USD*

3,360,000 kwa miaka 19 ambapo kila mwaka *YSD* 176,842.1 lakini sasa hivi utekelezaji huo haupo.

Mheshimiwa Spika, je, tutaweza kufikia lengo hilo la kupata maji? Serikali inatakiwa kuweka kipaumbele Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali sasa kuelekeza nguvu zake katika ujenzi wa reli ili kuondokana na kero za usafirishaji wa mizigo na kupunguza gharama za usafiri wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, magari makubwa yenye uzito mkubwa huharibu barabara, ndiyo maana kila kunapotengenezwa barabara zetu kwa muda mfupi huharibika. Hivyo ujenzi wa reli utapunguza kuharibika kwa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijatenga fedha za upimaji wa ardhi kwa ajili ya ufugaji. Je, tatizo la wafugaji wanaohamahama litakwisha lini kama maeneo yao hayajapimwa?

Mheshimiwa Spika, katika randama kunaonyesha hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa malambo, josho na dawa kwa ajili ya wafugaji wanaohamahama. Je, hawa wafugaji wapo nchi gani? Siyo sehemu ya mapato katika nchi hii?

Mheshimiwa Spika, watumishi wengi wanadai maslahi yao na Waziri kila mara anasema wameanza kulipa. Je, wale Afisa Watumishi wanaoshindwa

kutekeleza maagizo ya Serikali na Watumishi wanateseka, kwa nini wasichukuliwe hatua?

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia zote. Pia nampongeza Mheshimiwa Daktari Kikwete kwa G8 kufadhili *SAGCOT,* hongera sana.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igalula lina skimu moja ya umwagiliaji, Loya kati ya Kata 10. Miswaki skimu imekufa na iliyopo haiendeshwi kitaalam hivyo tija iko chini sana. Serikali ifufue skimu hizi na kuanzishwa nyingine Kizengi, Goweko, Nsololo, Igalula kwani maji yapo masika na hayako kiangazi.

Mheshimiwa Spika, pembejeo zinachelewa kufika Igalula, - Hazina ihakikishe *export levy* kutoka pesa za pembejeo (mbolea, madawa na kadhalika) kwenye vyombo vya Serikali na siyo Mfuko wa Pembejeo kwa mfano *TFC* ili mbolea ya ruzuku iwahi kuwafikia wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Goweko tangu 2009 iliahidiwa bwawa na upembuzi yakinifu kwa mahitaji ya Benki ya Dunia, je ilikamilika? Bwawa litajengwa lini? Bwawa litoe maji kwa matumizi ya binadamu, mifugo, umwagiliaji na ufugaji samaki.

Mheshimiwa Spika, asilimia mbili za tumbaku wakulima Igalula wanasubiri malipo, ni vyema kukawa na Mfuko ili kama bei itashuka wapate bei iliyoboreshwa kama *STARBAL* (kahawa). Mfuko pia

usaidie wakulima wa pembejeo kwa ruzuku kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, trekta umoja katika vijiji wakopeshwe na malipo wakati wa mavuno. *SACCOS* zigharamie mafunzo na matengenezo ya trekta hizo.

Mheshimiwa Spika, Kata 10, Vijiji 51, Jimboni Igalula ni vijiji vitatu tu ndivyo vina maji ya visima. Maji yaje, visima vyote vya Jimbo la Igalula na kila mtumiaji atozwe na fedha zilipwe baada ya maji kuwepo.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa vyanzo vya maji ni muhimu. Hivyo sheria ndogo ndogo zisimamiwe ili kilimo, mifugo mazingira na afya za wananchi ziimarike. Visima vitano vya Benki ya Dunia bado hata kimoja kuchimbwa. Tunaomba hivyo vikamilike kwani wananchi wamechangia lakini maji bado.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Umeme *(REA),* vijiji vimo kwenye ilani ya CCM 2010 – 2015 na mpango wa umeme vijijini 2010/2011. *NEMSIS* (USA) Kampuni ya Umeme wamesaini Mkataba na *REA*? Vijiji vinasubiri umeme mwaka huu wa fedha; Goweko, Imalakaseko, Igalula, Kigwaa, Kigwa B. Naomba bajeti hii utekeleze ahadi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mifugo, Mheshimiwa Rais Daktari Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 27 Oktoba 2010 katika Vijiji vya Ikolamnsimba, Isikizwa, Uyui, Tabora alitoa ahadi kwa wananchi wa Igalula na Tabora Kaskazini kuwa kutakuwa na mpango wa kupanda nyasi katika baadhi ya maeneo kwa ajili ya kulisha

mifugo. Je, mpango huu uko katika hatua gani za utekelezaji katika Jimbo la Igalula. Hii itapunguza wafugaji kuhamahama kutafuta maji na malisho. Idadi ya Mifugo ni kutoka Mwana, Shinyanga, Geita, Simiyu ni kubwa sana. Uwezo wa maji na malisho ni mdogo, wageni wetu wafugaji wanalima pia. Misitu asilia imekatwa sana vyanzo vya maji vimetoweka, mvua zinatoweka kutoka 1000mm hadi 250mm (2012) ukame unalikabili Jimbo na hivyo uhaba wa chakula. Mifugo inaharibu sehemu oevu na chepechepe za mbuga za Nsololo, Kawekapina, Nyahua, Simbadamalu, Mwamakoyesengi, Myenze, Lutende zimekauka, mpango mtambuka ni muhimu kutatua tatizo hili la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mazingira, jitihada zifanyike kushirikisha Wizara ya Mazingira (Ofisi ya Makamu wa Rais), Mifugo na Uvuvi, Kilimo, Chakula na Ushirika, Maji na Umwagiliaji, Maliasili na Utalii na TAwala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuokoa misitu, vyanzo vya maji, ardhi oevu na ya kilimo, umwagiliaji. Mpango wa matumizi bora ya ardhi uwepo kila Wilaya na kuratibu matumizi endelevu ya rasilimali hizi, maji, ardhi, misitu, samaki na wanyama ili wananchi watumie fursa hizi kujikomboa kutoka lindi la umaskini na kuyahifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, biashara ya hewa ya ukaa *(carbon credit),* Ofisi ya Makamu wa Rais isaidie kutayarisha maandiko.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, fedha za maendeleo katika bajeti ya 2011/2012

zilizoifikia Wilaya ni asilimia takriban 30 tu. Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ulisuasua. Jitihada ziongezwe ili bajeti hii itekelezwe katika Afya, maji, barabara, mikopo, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Korido ya Kati ya Miundombinu *(Central Infrastructure Corridor)*, naipongeza Serikali kutenga fedha na barabara za Tabora na hasa Tabora – Itigi, naomba barabara ya Nyahua–Chaya–Itigi kilomita 89, tayari kuna wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, Korido ya kati ina Reli, barabara, mkongo wa mawasiliano na inahitaji bomba la gesi ili Serikali ilete nishati hii itumike kwenye matumizi mbalimbali yaokoe msitu na tufuge nyuki tupate asali bora na kuuza *honey king* Kibaha na nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Afya, tunaomba Hospitali ya Wilaya yetu haina hata *DDH*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala, ombi la Wilaya ya Igalula, mchakato wa kuomba Wilaya umejadiliwa na *WDCs* zote na kupelekwa *DDC* tunakamilisha utaratibu kuwasilisha *RCC*. Igalula inaomba Kata jirani nne kutoka Tabora Kaskazini (Jimbo) ili wilaya mpya iwe kamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, Idara ya Ukaguzi haina rasilimali za kutosha hivyo kushindwa kufanya ukaguzi wa shule zetu. Idara hii haina magari wala mafuta. Vile vile hosteli, maabara na nyumba za walimu bado ni tatizo kubwa katika Jimbo la Igalula, tupate ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waheshimiwa Madiwani, Mheshiwa Waziri Mkuu hongera kwa kuongeza posho za Waheshimwa Madiwani kwani zimekuja wakati mwafaka. Niliomba hili tarehe 21/6/2012, nilipochangia katika bajeti ya Serikali. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imethibitisha hilo, nimefarijika sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli na bandari uk. 41). Reli ya kati ijengwe kwa *PPP* na kuunga bandari ya Dar es Salaam. Taarifa haitamki kuhusu ujenzi wa gati 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam. Nchi nane Zambia, Malawi, Uganda, Rwanda, Burundi Mashariki, DRC, Southen Sudan, Zimbabwe zinategemea Bandari ya Dar es Salaam. Gati hizi zijengwe kwa utaratibu uliowekwa na *TPA* na Bodi yake ili tupokee meli kubwa na kuipiku Bandari ya Mombasa. Fedha hizo za ziada zitajenga Mwambani (Tanga) Mbegani (Bagamoyo).

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kitengo cha wataalam walikuja kufanya *survey* ya kusambaza umeme Vijiji vya Wilaya ya Kaliua, waliona inawezekana umeme unahitajika sana, kwa ari waliyonayo wananchi ya kujiletea maendeleo. Naomba sana Wizara itimize ahadi hii ya utekelezaji katika kutuleta umeme. Ripoti iko *REA* yenye kuainisha Vijiji vyote vya Wilaya hii.

Mheshimiwa Spika, suala la hifadhi ni janga kwetu, wavamizi wamehamasishwa kisiasa, matokeo yake

misitu imekwisha, mvua zimepungua sana. Naomba zoezi la kuwaondoa wavamizi hawa liwe endelevu. Wote waondolewe, mipaka iwekwe ya kueleweka na ionekane. Baada ya hapo ulinzi uwe wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha tumbaku, naomba lisimamiwe na Serikali na ndiyo iwe yenye kutoa miongozo badala ya kuwaachia wazungu hawa waliomo katika biashara ya tumbaku.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ndiyo iamue nani alime na nani asilime, bei ipangwe mapema na huduma za ugani ziongozwe.

Mheshimiwa Spika, mazao mbadala ya biashara kwetu Urambo Magharibi ni mahindi na pamba, lakini huduma zake za ugani ni hafifu sana. Naomba hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, suala la maji ni suala la kufa na kupona, naomba Wizara ilete watalaam kupima maji ili tuwe na uhakika. Tunapochimba visima mkoani mwetu. Mara nyingi tumepata wafadhili wa kutusaidia maji, lakini wamekatishwa tamaa na visima visivyo na maji au kukauka baada ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya bila Halmashauri ni Wilaya butu, naomba sana Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ipatikane haraka sana na tuletewe Mkurugenzi mahiri.

Mheshimiwa Spika, *TASAF* wametudanganya kwenye ufadhili wa mkandarasi wa ujenzi wa shule

katika Kijiji cha Kasna, upate Kata ya Igogola tangu 2007 hadi leo. Naomba fedha hizi zipatikane ili kuwatia moyo wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, naomba taasisi ya fedha *SCULLT* iwajibishwe kwa kutowapatia wananchi wa Kameje kupitia *SACCOS* yao ya Chemchem. *SACCOS* hii walijichangisha milioni 27, leo mwaka huu wa tatu hawajapewa chochote. Naomba wapewe mikopo na fedha yao iwe imeongezeka na kuzingatia riba.

Mheshimiwa Spika, umeme umetokea urambo kuja Kaliua kupitia Vijiji vya Usindi na Isanjandugu. Vijiji hivi umeme umepita juu tu, inasikitisha. Naomba vijiji hivi vipatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hiyo kuwasilisha kero mbalimbali za Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero pamoja na kupewa kipaumbele kuwa ni Wilaya ya Kilimo Kwanza, lakini barabara hazipitiki kwa urahisi na kupelekea gharama za nauli kuwa kubwa kwa wananchi na mazao wanayosafirisha.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero zipo Kata, vijiji vingi havina maji safi na salama. Serikali ilipokea ombi kutoka Halmashauri kuendeleza mradi mkubwa wa maji ambao chanzo chake ni Mto Limemo Kiburubutu ili kufanya pembuzi yakinifu kujua gharama

halisi ya mradi ambapo ziliombwa Sh. 508,000,000 na wakapewa 5.6 milioni ambazo hazitamaliza hatua ya mwanzo na kuja gharama halisi za mradi. Hivyo, mradi upate pesa za kumalizia ili wananchi wa Mji Mdogo wa Ifakara waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ningependa Serikali itoe ufafanuzi kuhusu mageti ya ushuru wa mazao kila Kata na kuwatoza wakulima ushuru ingawa lipo tamko la Waziri Mstaafu Brigedia Ngwilizi, Tamko Na. 230 la mwaka 2002 na kuanza kutumika Mei Mosi, 2002 ambayo ilifuta ushuru wa mazao kwa wakulima. Je, kwa nini Halmashauri itunge Sheria Ndogo na kuwatoza ushuru wakulima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Halmashauri kukusanya mapato kwa kuwatesa wakulima ni vyema, Serikali ikahimiza Halmashauri kutafuta vyanzo vingine vya mapato ambavyo si kero kwa wananchi katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tulipitisha Sheria katika Bunge hili la kuruhusu Halmashauri kukusanya ushuru wa leseni, nasisitiza Serikali ipeleke haraka maelekezo ya ukusanyaji mapato hayo ya leseni ili kuongeza kipato cha Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie baadhi ya kero ya Wilaya ya Mvomero. Katika Makao Makuu pale Sokoine kabla ya kuwepo, wananchi waliokutwa pale wamenyang’anywa maeneo na hawajalipwa kwa kiwango kinachostahili, nashauri Serikali iangalie upya

malipo ya wakazi hao ili waondokane na mateso wanayopata.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mvomero kuna matumizi mabaya ya pesa za walipa kodi kwa kukodi basi la kupeleka watumishi ofisini kila siku kwa Sh. 300,000/=, hatua zichukuliwe haraka kupata gari la Halmashauri na si kukodi, wapate hata gari la mkopo.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Embeti, kulikuwa na kiwanja cha mpira kimebadilishwa matumizi na kujengwa Kiwanda cha Kukamua Alizeti na Nyumba ya Kuhifadhi Nyanya. Nashauri Serikali ishughulikiie suala hilo na matumizi ya awali yarejeshwe.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji Kiwanda cha Sukari, Mtibwa ni kero kwa wananchi. Viwango anavyolipa mwekezaji kwa wakata miwa vinatofautiana sana na wakatisha miwa (makandarasi) ambao si wa kiwanda. Mwekezaji analipa Sh. 3,800/= kwa siku, mkandarasi nje ya kiwanda na ni mashamba yaliyo mbali na kiwanda anawalipa wakataji Sh. 7,000 kwa siku. Je, tukisema wawekezaji wamekuja kutunyonya tunakosea?

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi mwekezaji huyo kwa wafanyakazi wa kiwandani wenye mktaba hutoa malipo duni na mfanyakazi amepangiwa kuumwa mwisho siku tatu zikizidi yeye hatambui.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tarehe 24 Juni 2012, wakata miwa waligoma na kutaka waongezwe malipo na marekebisho ya mkataba. Matokeo yake

Askari Polisi walileta na kulazimisha wakakate miwa kwa kupigwa mabomu ya machozi. Kwa hali hii maisha bora kwa wananchi wa kawaida yatawezekana? Je, kwa nini wawekezaji wanaachiwa kudhulumu wenyeji?

Mheshimiwa Spika, kuna shamba la ekari zisisopungua elfu moja na zaidi lililoko Kata ya Embeti, Kijiji cha Embeti ambalo linalalamikiwa na wananchi kuwa la kigogo mmoja ambapo anasingizia ni mali ya Kanisa. Shamba hilo linahitajika na wananchi kwa kulima mpunga kwani hawana mashamba. Mmiliki huyo amelima kidogo miwa na kuacha pori ambalo halitumiwi na wananchi hawana mashamba mengine. Nashauri Serikali iende kutoa maamuzi magumu kwa manufaa ya watu wengi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero katika Wilaya ya Kilosa, Jimbo la Kilosa kati, wahanga wa mafuriko ya Kilosa mpaka leo hawajui hatima yao kwani wametelekezwa bila msaada wala taarifa kamili kuhusu ahadi zilizotolewa za kujengewa nyumba. Hivi sasa Viongozi wa Serikali wa Wilaya wanakwenda kung'oa mabati na bila maelezo yoyote na hayajulikani wanakopeleka. Hivyo, wakati umefika wa Serikali kutoa maelezo ya kutosha kuwa wahanga hao ili wajue mwisho wa kukaa katika makambi ambapo ni kama wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilosa inayo migogoro mingi ya ardhi inayutokana na baadhi ya vigogo kujitwalia ardhi kubwa na kukodisha wananchi kwa kilimo kwa mwaka ekari Sh.15,000/= matokeo

hayo ni mabaya kwa nchi yetu, napenda Serikali ione njia nzuri ya kunusuru hali hii.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Parakuyo ambapo kinapakana na Hifadhi ya Mikumi pia shamba la kigogo mmoja lililopo eneo la Mkata ambapo kuna njia ya miaka yote kabla hata ya kuuziwa Kigogo huyo, ng'ombe hupita kwenda kunywa maji bwawani, kwa kuwa ng'ombe walishazoea kupita njia hiyo. Hivi sasa walinzi wa shamba hilo hukamata ng'ombe wanaopita njia hiyo na kutoza faini ya Sh. 10,000/= kwa kila ng'ombe na hakuna shughuli nyingine yoyote ya kimaendeleo inayofanywa kwenye shamba hilo isipokuwa kukusanya faini kwa ng'ombe. Huyo mwekezaji hana faida yoyote, ni vyema Serikali ikachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wa Parakuyo wanazidi kuwa maskini kwa kila uchao, ng'ombe wao wanapigwa risasi na Askari wa Wanyamapori *(TANAPA)* wa Mbuga ya Mikumi.

Mheshimiwa Spika, hali inayoendelea katika Kijiji cha Parakuyo ni mbaya, taarifa ya uhakika katika kipindi cha Mei na Juni, 2012 hadi tarehe 28 Juni 2012, idadi ya ng'ombe waliopigwa risasi na Askari wa *TANAPA* imefikia... Hali hii haivumiliki na inaashiria kutoka vurugu, mapigano na kuuawa watu kama ilivyotokea Ulanga mwaka huu. Hivyo ni bora kunusuru maisha ya watu, nasema hayo na ushahidi upo na vielelezo vimekabidhiwa kwa Naibu na Waziri wa Maliasili na Utalii tarehe 19 Juni 2012. Hivyo, wananchi wanataka viongozi wa Serikali kwenda kujionea hali halisi na kupata ufumbuzi mapema.

Mheshimiwa Spika, migogoro mingi ya Ardhi inasababishwa na baadhi ya watendaji wa Serikali wa ngazi mbalimbali kutaka kujilimbikizia mali kinyume na sheria na ubnafsi uliojaa mioyoni mwao, hivyo, kusababisha mapigano ya wakulima na wafugaji na kuleta umaskini.

Mheshimiwa Spika, pia migogoro inasabishwa na uzembe wa Serikali kuendesha zoezi la upimaji ardhi wa haraka hasa maeneo yenye migogoro kwa kutaka kuleta amani. Tumesema sana, tumeshauri sana, lakini hatua hazichukuliwi, ifike wakati sasa wa kumaliza migogoro kwa kupima ardhi na kuboresha maeneo ya wafugaji kwa kujenga miundombinu na kutoa mafunzo ya ufugaji wa kisasa ili wasitangetange. Nashauri maeneo yote yenye migogoro ya wafugaji na wakulima Mkoa wa Morogoro yafikiwe kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Wilaya ya Morogoro Vijijini. Katika Kata ya Bwakila chini kuna tatizo kubwa la ukosefu wa eneo la kujenga Zahanati, Kituo cha Afya, Soko, Kituo cha Polisi na huduma za kijamii kutokana na shamba kubwa lililokuwa la *Tanzania Cotton Company* kuwepo katikati ya Mji wa Kata hiyo. Jitihada mbalimbali za Viongozi wa Kata zimefanywa za kutaka shamba hilo kurudishwa kwa Serikali ili viwanja vipimwe lakini hazijazaa matunda kutokana na baadhi ya Viongozi kushindwa kuchukua maamuzi ingawa hati ya umiliki wa Kampuni hiyo ya Pamba kuisha muda wake wa umiliki na vielelezo vipo. Hivyo, nashauri Serikali inusuru hali hiyo kwa maendeleo ya Kata.

Mheshimwa Spika, Kata ya Bwakila chini inayo migogoro ya wakulima na wafugaji inayosababishwa na baadhi ya viongozi kuruhusu mifugo iendelee kuingizwa usiku hali wakijua ardhi haitoshi. Nashauri hatua za haraka zichukuliwe kunusuru migogoro.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kero ya Wilaya mpya ya Gairo. Wananchi wa Gairo miaka yote wana shida ya maji, huishi kwa kununua ndoo ya lita 20 kwa Sh. 1,000. Kulikuwa na mradi mkubwa wa maji, lakini hadi sasa haujulikani umeishia wapi. Naishauri Serikali, uboreshaji wa Makao Makuu ya Wilaya uanzie na upatikanaji wa maji safi na salama hapo Gairo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kero za utawala Bora wa Kidemokrasia, utawala bora ni vizuri ukatekelezwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa katika Vijiji na Kata nyingi hapa nchini zipo nafasi za wazi za Kata (Udiwani), Vijiji (Wenyeviti), Vitongoji na wajumbe wa Serikali ambazo zimechukua muda mrefu bila kufanyika chaguzi hizo na kusababisha kuzorota kwa maendeleo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mikumi, Kata ya Ruaha, Kijiji cha Ruaha, wananchi baada ya kugombana na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji kuhusu makusanyo ya fedha za Kijiji na kukubali kuzitumia binafsi hivyo kulazimika kujiuzulu uongozi. Baada ya kujiuzulu kwa mujibu wa Sheria, uchaguzi unatakiwa

kufanyika ndani ya siku 60, sasa imepita miaka miwili (2) bila uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi baada ya kufuatiliwa sana aliitisha uchaguzi mara ya kwanza na kusitisha. Mara ya pili aliitisha uchaguzi uliokuwa ufanyike tarehe 27 Mei 2012; wagombea walishateuliwa, wananchi walishajiandikisha kupiga kura, kampeni zilifanyika. Lakini cha kusikitisha Kaimu Katibu Tawala wa Kilosa aliandika barua ya kusitisha uchaguzi huo bila sababu. Wananchi waliona wameonewa na kunyimwa haki na kutokea fujo.

Mheshimiwa Spika, baada ya vurugu kutokea, wananchi walikamatwa siku hadi siku kuanzia mwezi Mei mwishoni hadi Juni hii na hata walikuwepo wagombea kupitia CHADEMA wa Kijiji na Kitongoji walikamatwa na kubambikiwa kesi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamatwa wagombea wa CHADEMA hivi sasa Serikali imetangaza kuanza kuandikisha wapiga kura upya na uchaguzi ufanyike. Je huu ni utawala bora? Nani anaweza kuvumilia vitendo vya kupora haki, vitisho na kulazimisha wananchi wachaguliwe chama au viongozi? Nani atakayerudisha gharama za mazoezi yote yaliyopita na hili la sasa lililotangazwa? Ifike mahali, viongozi wamuogope Mungu.

Mheshimiwa Spika, nashauri uchunguzi wa kina ufanyike na wote waliosababisha mgogoro katika Kijiji cha Ruaha wachukuliwe hatua na wananchi waachwe wachague viongozi wao. Ahsante.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Utekelezaji, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini katika mwaka 2012/2013. Pamoja na Serikali itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mipango ya miradi ya maendeleo ikiwemo matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfumko wa bei ni ishu kubwa katika nchi yetu na kukua kwa uchumi ukiongezeka katika ukurasa wa nne na tano. Hali ya uchumi inapaswa Serikali kuwa makini kwani kukua kwa uchumi wakati watu wake waadhirika na hali hiyo, sioni sababu kwa nini tufike kuyumba wakati vyanzo vya uchumi tunavyo, tunachotakiwa tutafute wataalam ambao tunao hata hapa nchini tuna maprofesa wa kilimo wanaweza kututengenezea mabwawa ya maji kwa ajili ya mashamba ya umwagiliaji itatusaidia kupunguza suala la vyakula hata mabwawa ya kutunza maji kwa ajili ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo. Mkulima analima kutumia nguvu zake lakini ikifikia wakati wa kutoa mazao shamba anakutana na mageti na kutozwa ushuru, akifika sokoni anatozwa ushuru. Haitoshi si sehemu zote zinapata vocha ya pembejeo kwa bei nafuu au mbegu bora za mazao kama ilivyoelekezwa. Mwananchi huyu akishauza mazao hayo anakuja kulipa kodi ya maendeleo, ada ya watoto wa shule, vitu bei juu, mazao yenyewe

analima lakini hana uhakika wa soko, anauza wapi na wapi alime zao gani la kumpatia kipato cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, yapaswa sasa Serikali iondoe manunguniko na wananchi kwa kuwapatia soko la mazao kwa kila moja ya zao ili wawe na uhakika wauze bei gani. Kushuka kwa uchumi au kupanda ni Serikali yenyewe kujipangia vitu bila mpangilio na kuwabebesha wananchi mzigo na wala haileta tija kupandisha bidhaa kwa ajili ya pato la Taifa wakati wananchi wake hawana uhakika wa mlo mmoja kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, TAMISEMI ina mipango mingi, imezidiwa nguvu na ipo chini ya Waziri Mkuu kwa nia ya kuwa na ufanisi. Kwa sasa suala la elimu linashuka na Halmashauri kushindwa kusimamia suala hilo vizuri. Sasa kitengo cha elimu kiondolewe Halmashauri na kiwe kitengo maalum.

Mheshimiwa Spika suala la uwekezaji ni moja ya matumizi mabaya ya ardhi na linasababisha migogoro ya hapa na pale kwani watendaji wa ngazi za chini kuja juu wanataka kuwa na uwekezaji wao na hawa wanaowekeza, wanawalaghai Viongozi wachache wa Vijiji kuingia mkataba bila wengine kujua.

Mheshimiwa Spika, hayo yametokea Wilayani Kondoa na mwekezaji aitwaye *ENCE* kwenye Kata ya Kisese eneo la Atta. Imefikia mahali mwekezaji anakosa huruma na wenyeji wake kuwatendea unyama wa kumwaga sumu ya kukausha mimea na kusababisha madhara kwa wananchi wa karibu na

eneo hilo. Yapaswa tuwe waangalifu zaidi ya watu wanaotaka kuwekeza kwetu kwa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, usalama wa nchi uko mashakani kwani kama askari wetu hawapo makini kulinda mipaka yetu na mageti wamegeuza kama mradi, Serikali inapaswa kuliangalia kwa macho mawili, tusijitie aibu, nchi ya amani ikawa kisiwa cha machozi. Hili ni angalizo kwa mfano sisi sote kama Serikali tumeshuhudia hapa Dodoma kuletwa watu mpaka hapa, huenda ni makusudi au uzembe, vinginevyo rushwa iko wazi kabisa hiyo.

Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha kwa nini Serikali isiboreshe shule, nyumba za walimu, walimu wa kutosha mashuleni ili kupunguza kelele za upungufu wa walimu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka masuala muhimu yatekelezwe.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa Mbunge. Pili, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa kusema kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivi sasa imeingiwa na balaa ya Uamsho ambao hauna muda wala saa ya kufanyika kwa mambo hayo. Ilipotokea fujo hizo kwa mara ya kwanza Jeshi la Polisi lilishindwa kufanya kazi

zake kama ilivyotakiwa kutokana na ukosefu wa vitendea kazi kama gari, mafuta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Jeshi la Polisi, Zanzibar lipatiwe vifaa vya kutendea kazi kama inavyotakiwa na sio kushitukia tu kama zima moto, kwani suala la vurugu kwa Zanzibar ni la kawaida sio la muda mfupi, kwani watu wanashawishi vijana wenye umri wa miaka kumi na nane ili wafanye fujo kwa maslahi yao na siyo kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala la ulinzi kwa upande wa Zanzibar lipewe kipaumbele kwa asilimia kubwa sana ili kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naendelea kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja huku nikijiaminisha kuwa hakuna Tanzania bila Zanzibar. Kwa hiyo, kilichotokea kwa Waziri Mkuu kutohusisha chenji ya rada na upande wa pili wa Muungano ni hali halisi ya binadamu yoyote ambaye inaweza kumtokea aidha, kusahau au kukamilisha ubinadamu wake kwani ukamilifu wa binadamu ni mapungufu yake na binadamu anayejiona amekamilika, huyo ndiyo mpotevu kabisa kwani sifa hiyo anayo Mwenyezi Mungu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Muungano kuna masikitiko kidogo kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa mwaka 2011/2012 vikao 14 vimefanyika. Huu ni wastani wa kila siku 25 kufanya

kikao kimoja na kulikuwa na hoja kumi na tatu, huu ni wastani wa kila kikao kimoja kwa hoja moja. Kwa mshangao mkubwa sana kutokana na maelezo yaliyokuwepo kwenye hotuba hii ni mambo mawili tu ndiyo yaliyopatiwa ufumbuzi ambayo kwa Wazanzibar sio mambo ya msingi kabisa. Hivi kwa vikao 14 vya mwaka mzima na kutumia fedha za Watanzania walio masikini hivi hamuoni kuwa huu ni mzaha kwa Wazanzibar pamoja na ufujaji wa fedha za walipa kodi?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, waelewe kuwa hakuna Muungano usio na matatizo mahali popote duniani na mwisho wa matatizo ndiyo mwisho wa ulimwengu.

Mheshimiwa Spika, tusiogope kutoa maamuzi ili wananchi watuelewe, ni lazima kutatua kero hizi kila zinapojitokeza tena kwa wakati husika ili tupate muda wa kutatua matatizo mengine ambayo yanaendelea kila ulimwengu unavyokuwa kwani haya mabadiliko ndiyo changamoto za maisha yetu ya kila siku. Sasa usipoyapatia majibu ni sawasawa na kukimbia kivuli chako mwenyewe jambo ambalo haliwezekani.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha Waziri Mkuu pia kiligusia ajira na kilimo. Kuhusu suala hili naishauri Serikali kwa sasa ni wakati mwafaka wa kuelekeza nguvu kwenye kilimo hususan cha biashara kama sukari, pamba, korosho, tumbaku na kujielekeza kwenye Viwanda vidogo vidogo ambavyo vitamilikiwa na wakulima wadogo wadogo wenyewe kwa

kuongeza thamani ya mazao yao na kuweza kuuza kwa tija nje ya nchi. Tukifanya hivi tutakuwa tumetengeneza ajira za uhakika kwa vijana wengi na kupunguza wimbi la kuhamia mijini kwa kutafuta ajira.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mawasilisho mazuri. Aidha, nawapongeza Mawaziri wote wa nchi pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Pili, hali ya Mkoa wa Kilimanjaro ni mbaya sana au itakuwa mbaya sana mwaka huu kwa suala la chakula kwani Wilaya karibu zote zimekumbwa na ukame. Naomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ianze kufanya matayarisho maana mahitaji yatakuwa mengi makubwa. Tatu, naungana na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Kilimanjaro kuiomba Serikali ione jinsi Halmashauri zinazopakana na Mlima Kilimanjaro zitakavyopata angalau sehemu ya makusanyo yanayofanywa na *KINAPA* ambayo peke yake inaingiza zaidi ya 50% ya mapato yote ya *TANAPA*. Hoja ni ile ile kama inayozifanya Halmashauri zenye migodi kunufaika na sehemu ya mapato ya migodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nne, wakati wa kampeni za 2010, Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa barabara ya Kiboriloni – Kikarara – Tsuduni – Kidia Moshi vijijini) yenye urefu wa kilomita 19.8 itawekwa lami. Kwa vile huu ni mwaka wa pili ahadi hii ni ya 2010 – 2015, naomba Waziri wa Ujenzi alizingatie katika bajeti yake kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tano, suala la ujumla la kuondoa *VAT* kwenye uzalishaji wa ndani wa nguo *(textiles)* litasaidia sana nchi yetu. Nikumbushe tu kuwa Tume iliyounda Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya kuimarisha viwanda vya nguo iligundua kuwa endapo *VAT* itasamehewa, nchi itapoteza shilingi bilioni moja tu. Hata hivyo, uamuzi huo utaongeza *foreign direct instruments,* utaongeza ajira na utaokoa fedha nyingi za kigeni tunazotumia kuagiza nguo nje. *Combination* hii itatuongezea zaidi ya shilingi bilioni moja, achilia mbali utulivu utakaotokana na ongezeko la ajira.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kuokoa muda na ili hoja izingatiwe, naomba nitoe mchango wangu kwa muhtasari. Naungana na ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, mimi ni Mjumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza Katibu Tawala wa Mkoa *(RAS)*, Wakurugenzi na Watendaji wa Halmashauri za Wilaya na Jiji kuwa mamlaka ya nidhamu kwa ajili ya watumishi wa ngazi ya chini, Madiwani wavuliwe mamlaka hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *Local Government* Namba 8 (Jedwali) itamke wazi namba ya Wajumbe wa Kamati za Kudumu, fedha za wananchi zinatumika vibaya kuundwa Kamati kubwa hadi 14 (Kamati ya Fedha na Uchumi) ambayo hukutana kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi mbaya wa fedha za Halmashauri ukomeshwe. Pamoja na Sera ya *D by D*. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ifanyie kazi hiyo. Aidha, muhimu

sana Serikali kuboresha mfumo wa utoaji vocha za pembejeo.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo zitumwe mapema, ucheleweshaji wake unapandisha bei ya miradi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile posho ya Madiwani, imepandishwa kufikia shilingi 250,000, sasa wahudhurie ofisini kama watumishi wengine ili wasimamie miradi kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kazi na mipaka ya Mwenyekiti wa Halmashauri na ile ya *DC* ijulikane kuzuia kuwaingilia watendaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho Ofisi za Wabunge Jimboni zipatiwe watumishi hasa Katibu *(Secretary)* na Msaidizi *(Personal Assistant)* ili kumsaidia Mbunge kutekeleza kazi zake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikabidhi ardhi yote kwenye Miji na Makao Makuu ya Halmashauri kwa *Local Government*.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, maslahi ya Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji, ni kwa nini Serikali imekaa kimya katika suala hili muhimu mbali na ahadi yake katika kuhitimisha Bunge la Bajeti mwaka jana (2011)? Serikali iliahidi kuanza kutoa maslahi kwa Madiwani kuanzia mwezi Februari, 2012 na Wenyeviti wa Vijiji kuanzia Julai, 2012 lakini imekuwa

kimya hadi leo hii na kutoweka kwa bajeti ya 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, kwa nini Serikali haijatenga fedha kwa ajili ya hospitali hii inayojengwa na Halmashauri na fedha ya Serikali kuu, hadi sasa imebaki kuwa gofu kwa sababu tangu Serikali itoe fedha kwa mwaka 2008/2009 kiasi cha shilingi milioni 200, haijawahi kutenga fedha yoyote na hii kusababisha ujenzi kusimama. Je, Serikali inasema nini juu ya hospitali hii?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (Mwalimu Nyerere *Medical Centre)*. Imetengewa fedha kidogo shilingi billioni 2.1, ni kwa nini ujenzi wa hospitali hii umetengewa fedha kidogo kiasi hicho Shilingi 2.1? Gharama ya makadirio ya kuendeleza ujenzi huo kwa awamu ya kwanza ni shilingi bilioni 13, kwa mwenendo huo itachukua miaka mingi kukamilika. Je, Serikali iko tayari kuangalia suala hili upya na kuongeza bajeti ili kuharakisha utekelezaji wa ahadi ya Rais ili pia kulinda na kumuenzi marehemu Baba wa Taifa kwa vile jina la hospitali hiyo (Mwalimu Nyerere *Medical Centre*) ni kutoa heshima kwa Mwalimu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutokuwa na usajili wa vijiji na migogoro ya mipaka katika maeneo mengi nchini, kwa vile mwaka 2009 Serikali ilitoa kibali cha kuanzisha vijiji lakini havijasajiliwa; ni kwa nini Serikali haijatoa usajili katika vijiji vingi nchini?

Mheshimiwa Spika, je, kwa nini Serikali haijatoa majibu sahihi na kuelekeza mkoa kutekeleza katika ugomvi wa mpaka kati ya Wilaya ya Serengeti na Wilaya ya Bunda? Mpaka katika Wilaya hizi mbili (Serengeti na Bunda) katika eneo la Remung'orori (Metola) - Serengeti na Mekomariro (Bunda) umepimwa na Mkoa wa Mara kinyume na utaratibu na kuzua ugomvi huo ambao mkoa umeshindwa kuumaliza kwa sababu ndiyo umesababisha kutokana na watumishi wa Mkoa na Mkuu wa Mkoa aliyestaafu. Hatua za haraka zichukuliwe katika hili.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa vitambulisho vya uraia kutokana na uwepo wa wahamiaji haramu na wahamiaji holela, wengi nchini hususan Mikoa na Wilaya za mipakani ikiwemo Serengeti ni vyema Serikali isitishe zoezi hili muhimu, kwa nini Serikali isifanye operesheni ya kuwaondoa wahamiaji hao kwanza? Bila ya kufanya hivyo wahamiaji wengi watapewa vitambulisho vya uraia, Serikali haioni bila kufanya hivyo itakuwa hatari kwa Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, kuzagaa kwa silaha haramu na kuongezeka matukio ya uhalifu, kwa vile nchi yetu imezungukwa na nchi nyingi hata kuliko nchi yoyote katika Afrika na nchi nyingi haziko salama na hazina utulivu, mfano, Kenya silaha haramu mikononi, inakadiriwa kuwa laki tano, Burundi laki mbili kwa makadirio hayo tu kwa nchi mbili jirani zetu. Je, nchi ina mpango gani kukabiliana na hali hii?

Mheshimiwa Spika, ugatuaji wa madaraka kwenda Wilayani (Halmashauri), kwa vile hali ya

ugatuaji bado haijakaa sawa na kusababisha usimamizi na ufuatiliaji umekuwa hafifu, mfano, katika Elimu, Afya na Idara nyingine. Je, ni kwa nini Serikali isiangalie upya utaratibu huu pamoja na kurejesha vyanzo vya mapato, makusanyo katika Halmashauri na Halmashauri zichangie Serikali Kuu kama ilivyo katika nchi nyingine duniani zenye mfumo huu. Pia ni vyema kuanzisha Naibu Waziri wa Afya, TAMISEMI kwa sababu kuna usimamizi hafifu sana katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, Mji Mkuu kuhamishiwa rasmi Dodoma, kwa vile uamuzi huu wa kuhamishia Makao Makuu, Dodoma ni wa miaka mingi (34)na bado suala hili halijakamilika kwa nini Serikali haijatoa kauli kushindwa kutekeleza hili? Kwa nini Wizara nyingi zimejenga maghorofa makubwa Dar es Salaam, baada ya uamuzi huu? Mfano, Maliasili na Utalii; Ofisi ya Rais, Utumishi; Maendeleo ya Jamii na kadhalika. Majengo yote ya ghorofa makubwa yangeweza kujengwa Dodoma kama Ofisi ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walivyofanya. Vinginevyo Serikali igawe kuhamisha makao makuu, Bunge iwe Dodoma; Mahakama iwe Arusha na Biashara iwe Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya kuwa na ofisi mbili mbili za Wizara na nyumba za kuishi inatia hasara Taifa ni vyema kasi ya kuhamisha Makao Makuu iongezwe kwa sababu hata bajeti ya mwaka 2012/2013 iliyotengwa ni ndogo sana.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, juhudi ambazo Serikali inachukua kuboresha wakala

kusimamia kilimo ni muhimu sana. *Approach* ya wakulima wadogo *outgrowers scheme* kushirikiana na wawekezaji ni ya kupongeza. Hata hivyo, nani msimamizi wa hii mikataba ya *outgrowers scheme*? Itabidi Serikali iunde wakala wa kusimamia mikataba ili kulinda maslahi ya wanyonge.

Mheshimiwa Spika, Kiwira, suala ka Kiwira limekuwa linaibuka na kuzama kwenye mijadala ya Bunge. Ukweli ni kwamba, mwekezaji *Tanpower Resource* hapaswi kulipwa chochote kabla hajaeleza alitumiaje mikopo aliyopewa kutoka *CRDB, PPF, NSSF*. Serikali kutenga shilingi bilioni arobaini kulipia madeni ya Kiwira ikiwemo kuwalipa *Tanpower*. Nadhani sio uamuzi unaozingatia maslahi mapana ya Taifa. Kama Shirika la Umma, *NSSF* walitaka kubadili madeni yao kuwa mtaji na kushirikiana na *STAMICO* kuendeleza mgodi. Naomba Serikali itazame upya jambo hili. Kutumia shilingi bilioni arobaini, kulipa madeni wakati *NSSF* ilikuwa tayari kuendeleza, sio uamuzi bora. Nashauri jambo hili litazamwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kabulo; katika suala la Kiwira, suala la Kabulo lina uzito wa kipekee, Mlima Kabulo wenye leseni tofauti na ile ya Kiwira ulikuwa unamilikiwa na Shirika la *STAMICO*, kwa kutumia dola milioni sita, *STAMICO* walifanya utafutaji *(exploration)* kwenye eneo hilo na kugundua mashimo mengi sana ya makaa ya mawe. Tarehe 19 Desemba, 2005, siku moja kabla ya Rais Kikwete kula kiapo, Waziri wa Nishati na Madini alitoa leseni ya eneo la Kabulo kwenda Kampuni ya *Tanpower Resource* ambayo ilikuwa inamilikiwa na Waziri huyo. Tarehe 24 Agosti,

2011, Waziri wa Nishati aliidhinisha mgodi huu kuuzwa kutoka *Tanpower* kwenda kampuni nyingine yenye wana hisa wengi kutoka Australia.

Mheshimiwa Spika, bila Kabulo hakuna Kiwira. Wanaouza Kabulo wana lengo la kuwa wagavi kwa mgodi wa Kiwira. Hii inathibitishwa na mkataba ambao *Tanpower Resouce* waliingia na *KCPL* wa kuuza makaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya *POAC* imelifanyia kazi sana suala la Kiwira. Tafadhali simamisha uamuzi wowote unaondelea ili kuisikiliza Kamati na kupata uamuzi bora.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu nikianzia na maboresho ya Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika sekta ya fedha hayatokani na ongezeko la mabenki na matawi isipokuwa hutokana na idadi ya wanaokopa. Ni imani yangu kuwa mafanikio katika sekta hii yatatokana na idadi ya Watanzania waishio vijijini kupata uwezo wa kukopa. Vile vile sekta hii itafanikiwa na kuwanufaisha Watanzania endapo mabenki yataondoa urasimu uliopo sasa hivi unaomtaka mkopaji kuwa na dhamana jambo ambalo linanyanyapaa Watanzania wenye kipato kidogo hasa wale wa vijijjini.

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa ya mabenki nchini hasa yale yanayomilikiwa na wageni yamekuwa yakitoza riba ya juu sana na kusababisha kushuka

thamani ya mikopo kutokana na kushuka thamani ya fedha yetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iwawezeshe Watanzania kwa kujenga viwanda hasa vijijini kuwekeza kwa njia ya viwanda vijijini kutawasaidia Watanzania wengi walio vijijini kupata ajira na hatimaye kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu 2012/2013. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kupata Wakuu wa Wilaya ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao naamini wana upeo mkubwa na ni wachapa kazi jinsi nilivyowasikia kwenye vyombo vya habari, wakitoa michango yao katika semina elekezi waliyofanyiwa Dodoma, mara tu baada ya uteuzi wao. Hakika naamini watatekeleza vyema majukumu yao na kuwaondolea wananchi kero katika upatikanaji wa huduma za jamii wakishirikiana na wananchi katika kudhibiti mapato na matumizi kwa maendeleo na manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya Bajeti ya mwaka 2012/2013 ambayo inadhamiria kuboresha maisha ya wananchi hasa wanaoishi vijijini. Lengo la kuimarisha sekta ya kilimo ni mkakati tosha wa

kuinua pato la wananchi walio wengi na hatimaye kondokana na umasikini, ujinga na maradhi. Aidha, bajeti hii ni bajeti nzuri yenye mipango mizuri na kwa uhakika inalenga kuboresha huduma muhimu za kijamii na uchumi kama miundombinu, afya, barabara, elimu, maji safi na salama, utawala bora, usawa katika kutoa huduma, kutoa msisitizo katika Sera ya Kilimo Kwanza na mipango mingine mingi ya kuharakisha maendeleo kwa wananchi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ambavyo Serikali imekuwa ikiwajibika kikamilifu katika kuondoa kero za wananchi, kusimamia haki na utawala bora pamoja na kupiga vita adui rushwa, naamini mipango yote iliyoainishwa ndani ya bajeti hii itatekelezwa ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka jana ilikusudia kuimarisha kilimo kuwakomboa Watanzania wengi ambao uchumi wao unategemea kilimo. Pamoja na mipango mizuri ya kuendeleza kilimo kama *(ASDP)* azma ya kilimo kwanza, mpango wa ruzuku kwa wafugaji, uanzishwaji wa Dirisha la Kilimo katika Benki ya *(TIB)* na Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini *(SAGCOT)* na mingineyo. Naipongeza sana Serikali kwani kulikuwa na jitihada za wazi za kusimamia mipango hii kikamilifu. Wananchi walielimishwa namna ya kilimo bora, walishirikishwa katika kupanga mipango ya maendeleo yao pamoja na umuhimu wa kutunza ardhi yao kwa kizazi kijacho. Wananchi wengi hasa wakulima walipata elimu iliyowawezesha kufaidika na mfumo wa stakabadhi ghalani ambapo waliweza kujenga ghala za kuhifadhia mazao mara tu baada ya

kuvuna, hivyo kuwa na uhakika wa ubora wa mazao yao na akiba ya chakula.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nyingi na mafanikio, kuna maeneo ya kuimarisha zaidi na hasa kuongeza bidii ili kufuata kasi na hatua za maendeleo wanazopiga. Nchi ziwe na sheria ya ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma, inaweza kuharakisha maendeleo. Kwa mfano, katika sekta ya miundombinu Serikali inaweza kukaribisha wabia binafsi katika kuendesha wenzetu wa Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla. Hii ni pamoja na kuimarisha miundombinu bila kutumia gharama kubwa za Serikali kwa kutumia mfumo wa ubia wa *PPP*. Kufanya jitihada za kuimarisha kilimo kwa kufungua mashamba makubwa kwani kwetu ardhi si tatizo.

Mheshimiwa Spika, tunao vijana wengi sana ambao hawana kazi endapo Serikali itawahakikishia ushirikiano na msaada katika matrekta, pembejeo na mbegu bora na usimamizi thabiti, nina imani vijana hawa wataikomboa nchi yetu katika umaskini. Vijana hawa wanaweza kuwekwa katika mfumo wa vikosi vya uchumi kama ilivyo JKT, lakini wakapewa majukumu ya kilimo, ufugaji wa nyuki na hata samaki. Vijana hawa ni nguvu kazi ambayo inapotea bure na ndiyo maana wengi wamejiingiza katika vishawishi vya uhalifu na madawa ya kulevya kwani wamekata tamaa. Tuige mfano wa Mkoa wa Kigoma ambapo wamewawezesha vijana waliokuwa wamekata tamaa na wengine walikuwa vibaka, lakini sasa ni vijana ambao wamerekebishika na mpango huo umeonesha tija na pato kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango mizuri ya kuendeleza viwanda ningependa kushauri kuwa Serikali iweke vivutio katika viwanda vile vitakavyoongeza thamani katika mazao yetu. Wananchi wa Kibaha Vijijini ni wakulima hodari wa matunda, mboga, mahindi na pia ni wafugaji na wavuvi. Kama watapatikana wawekezaji ambao watajenga viwanda vya kusindika mboga, samaki na nyama vinaweza kutoa ajira kwa vijana na kutoa soko la uhakika kwa wakulima. Viwanda hivi vitaharakisha maendeleo ya Jimbo la Kibaha Vijijini na kuongeza uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya ndani vitakuwa havina maana kama vitazalisha kuuza nje, lakini soko la ndani lisiwepo. Kuna tatizo kubwa la wananchi kuthamini bidhaa za nje na kudharau bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na viwanda vyetu. Huu ni ugonjwa unaodidimiza uchumi wa nchi. Naishauri Serikali iweke mikakati ya kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kupenda kilicho chetu. Suala hili liwekewe kampeni kama kampeni za chanjo, sensa na kadhalika ikibidi jambo hili liwe kaulimbiu na ujumbe wa Rais katika mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilitoa mawazo mengi ambayo yamezingatiwa katika mipango ya bajeti hii ya mwaka 2012/2013, sina shaka kutakuwa na usimamizi mzuri katika utekelezaji wake. Napenda nimalize kwa kusema kwamba, mambo yote mazuri yaliyoko katika hotuba ya bajeti ya Waziri mkuu yamezingatia kumkomboa mwananchi kutoka katika

hali duni na kuwa katika hali bora pia kumwondolea kero za upatikanaji wa huduma za msingi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Ofisi ya Waziri Mkuu imewasilisha taarifa ambayo bado haiwezi kukidhi matakwa ya wananchi kwa uhakika. Kiasi cha Sh. 108,271,972,000; Sh. 222,276,872,000 kwa ajili ya maendeleo katika Ofisi ya Waziri ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Sh. 26,724,449,000 kwa ajili ya maendeleo ya Ofisi ya Wakuu wa Mikoa yote nchini. Aidha, Halmashauri zote zinaombewa Sh. 3,279,800,075,000 ambapo kati ya fedha hizo Sh. 2,735,646,117,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 544,153,958,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Ofisi ya Bunge imetengewa Sh. 113,220,653,000 ambapo Sh. 111,585,653,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 1,635,000,000 kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ukifanya mchanganuo bado unaona ni namna gani fedha za maendeleo zinatengwa kidogo Serikalini huku matumizi yakiendelea kubaki makubwa. Naishauri Serikali iepukane na suala la kuongeza matumizi kila mwaka kwa kuwa kuongeza matumizi bila sababu za msingi ni utovu wa nidhamu katika matumizi ya fedha za umma. Ukifanya uchambuzi wa kina utabaini kuwa zipo fedha nyingi ambazo zinatumika kwa ajili ya kulipana posho Serikalini bila kujali Serikali inakusanya mapato kiasi gani kupitia vyanzo vyake kwenye Halmashauri na kwingineko kupitia *TRA*.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali iueleze umma wa Watanzania kupitia Bunge ni lini itapunguza hizi posho ambazo siyo za lazima ili fedha hizo zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo. Kwa mfano, posho za mavazi, zinaweza kuondolewa katika baadhi ya maeneo ili kuokoa fedha nyingi zinazopotelea huko kwa kuwa hata Watanzania wanaoishi mijini na vijijini wafanyakazi na wasio wafanyakazi wa Serikali baadhi hawalipwi posho za mavazi. Kwa mfano, ni lini mwalimu alilipwa posho ya mavazi pamoja na kuwa mshahara wake ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, inatupasa tujiulize ni sababu gani zinaifanya Serikali kuwapatia baadhi ya wafanyakazi posho za mavazi huku ikiwaacha wengine. Tunasema kuwa Serikali inawabagua watu wake hasa wafanyakazi kwa kuwapatia baadhi posho za mavazi na kuwaacha wengine. Serikali ikifanya hivyo itaweza kuokoa fedha nyingi. tunashauri posho za mavazi zibakie kwa Askari wa Majeshi yote, Majaji na Mahakimu, pamoja na watumishi wa sekta ya afya yaani Madaktari na Wauguzi , ambao kimsingi uhitaji ni mkubwa ili kuwatambua. Kada nyingine za watumishi wa umma wa mikataba na wale wa kudumu wote tufute posho za mavazi ili kuokoa fedha zinazotumika huko. Ni ajabu kumnunulia Rais mavazi, Waziri Mkuu, Mawaziri na Wabunge na kadhalika. Wanapokwenda nje ilhali angalau wao kipato chao kinawawezesha kununua mavazi huku Serikali ikiwa haiwajali Walimu na Watanzania wengine wasiokuwa na uwezo mzuri kimaisha.

Mheshimiwa Spika, mapato katika Halmashauri zetu, Serikali inapoteza fedha nyingi sana kutokana na uzembe wa baadhi ya watumishi katika Halmashauri zetu, kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu imeingia mkataba na kampuni moja inayojishughulisha na masuala ya utalii ambapo kupitia mkataba huu utakaodumu kwa miaka 30, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu itakuwa ikinufaika kwa kupata mgao wa fedha kiasi cha shilingi milioni 347 tu kwa mwaka mzima, kupitia uwekezaji utakaofanywa na Kampuni ya Muwala *Trust Limited* ya Mjini Arusha. Inatupasa tujiulize, hivi ni sahihi kukubali kumpatia mtu au mwekezaji kuendesha shughuli za utalii kwa miaka 30 na kwamba mwekezaji atakuwa na haki ya kuendelea kulitumia eneo hilo kwa miaka 30 mingine baada ya miaka 30 ya kwanza kumalizika.

Mheshimiwa Spika, hainiingii akilini hata kidogo, kuna uwezekano mkubwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kuwa wamenunuliwa na Kampuni hiyo ya Muwala, hii ni kwa sababu mkataba wa miaka 30 ni wa muda mrefu. Hauna tofauti na mikataba ya akina Chifu Mangungo wa Msovero huko Morogoro katika zama za ukoloni hususani zama zile za Wajerumani. Hivi kweli Serikali inakubali kumpatia mtu kuwekeza kwa miaka 30 ambapo kampuni itakuwa inamiliki eneo lenye ukubwa wa hekta 157,510.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni wazi kwamba wananchi wa Wilaya ya Kasulu waliokuwa wakilima katika eneo hilo na kufukuzwa kama mbwa na Serikali walikuwa wanajua ni nini wanataka kufanya kwa maslahi ya wachache na sio wengi. Hivi ni kweli

kwamba tukifanya uchambuzi wa kiuchumi *(Economic Analysis)* ni sahihi kwa eneo hilo kutumika kwa shughuli za utalii halafu Halmashauri ipatiwe mgao wa shilingi milioni 347 tu kwa mwaka mzima? Wakati sekta ya utalii ikiwa inaelekea kuongoza kwa pato la Taifa, leo Halmashauri inakubalije kuthamini Mwekezaji na kuwasaliti wakazi wa Kasulu na Taifa kwa ujumla kwa kukubali kulipwa kiasi kidogo cha fedha kinachoainishwa hapo juu.

Mkataba huo unasema kama ifuatavyo katika vifungu vya 5.2.1 kuhusu muda wa mwekezaji kulitumia eneo hilo na 8.0 katika 8.1 - 8.3 kuhusu malipo kwa ajili ya kuendesha shughuli katika eneo hilo. Nanukuu: "5.2.1: mwekezaji atakapokuwa na haki zisizo za asili kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu atasimamia eneo hili kwa kipindi cha miaka thelathini kukiwa na haki ya kuongeza kipindi kingine cha miaka thelathini ya mkataba huu kama zitakavyokubaliana pande zote katika mkataba huu. Kila baada ya miaka mitano pande zote katika mkataba huu zitakaa kuangalia vipengele vya mkataba huu na kama kuna eneo lolote la kurekebisha au upungufu wowote utafanyiwa kazi na pande zote katika mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo kwa ajili ya kuendesha shughuli katika eneo hili. Mwekezaji kwa kushirikaina na meneja atasababisha kuanzishwa kwa Mfuko wa Dhamana ambao utatoa fedha zitakazotumika kwa ajili ya kuilipia Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ambapo itakuwa ikilipwa kiasi kinachokaribia au kupungua cha shilingi za Kitanzania milioni mia tatu na arobaini na saba kwa mwaka kwa

uwekezaji huu. Kampuni hii itaaanza kulipa kiasi cha shilingi za Kitanzania milioni mia moja ambapo kiwango hicho kitakuwa kikipanda kila mwaka hadi kufikia kiasi kilichotajwa hapo juu kama pato litakalotokana na Mfuko wa Dhamana utakaoanzishwa na Kampuni ya Muwalla *Trust Limited* kwa ajili ya haki ya moja kwa moja ya matumizi ya eneo hilo na rasilimali zilizopo katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na kupewa haki zisizo za asili za matumizi ya ardhi kama zilivyoanishwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji na 5 ya Mwaka 1999 katika vifungu na. 32(1),(2), (6) (c), (9) na (10) vya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (R.E 2006) kama ilivyofanywa marekebisho mara kwa mara. Kiasi hicho kitakuwa kinaongezeka kutokana na kuongezeka kwa dhamana ya Mfuko huu wa Udhamini.

Mheshimiwa Spika, mkataba huo unaendelea kueleza kuwa katika vifungu vifuatavyo:-

8.2: Fedha hizo zitakuwa zikigawanywa katika mfumo ufuatao:-

8.2.1: Asilimia kumi na tano zitatakiwa kutumika na Wilaya kwa kushirikiana na wadau wa maliasili kwa ajili ya kuliimarisha eneo hilo na ulinzi wa maliasili zake;

8.2.2: Asilimia hamsini kwa ajili ya Wilaya na ambazo zitaelekezwa katika huduma za jamii kama elimu, afya, kilimo, na mikopo midogo;

8.2.3: Asilimia ishirini na tano kwa ajili ya Vijiji vya Kagenrankanda na Mvinza kwa ajili ya kuwezesha miradi ya maendeleo;

8.2.4: Asilimia kumi kama akiba ya Wilaya; na

8.3: Mwekezaji atakuwa anamlipa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ada na malipo mengine yoyote kama itakavyofafanuliwa katika sheria na kanuni mbalimbali zinazotawala maeneo ya ranchi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, inatupasa tujiulize maswali mengi kuhusu mkataba huu na kisha tupate majibu isije kuwa kama ilivyo katika mikataba ya madini ambapo unakuta kampuni za madini zinalipa dola za Kimarekani laki mbili tu kama mrahaba katika Halmashauri zetu kwa mwaka, kiasi ambacho ni kidogo mno kikilinganishwa na makampuni ya mafuta yanayo-*supply* mafuta migodini ambayo hulipa kiasi kikubwa zaidi ya makampuni yenyewe ya madini. Aidha, masharti yalilyomo katika mkataba huu ni makali sana kwa wananchi, upo uwezekano wa kuja kushuhudia mauaji ya wananchi kwa kuwa wananchi watazuiwa kuingia katika eneo hilo na baadhi ya vijiji vimo ndani ya eneo linalotajwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina budi kuepusha migogoro na wananchi wake, kwa mfano Serikali inapata kigugumizi gani kuleta Muswada Bungeni utakaosaidia Taasisi na Halmashauri zote nchini kuwa na fursa ya kuanzisha makampuni ya kibiashara yatakayoweza kufanya shughuli mbalimbali na hivyo

kuiwezesha Serikali kujipatia fedha nyingi badala ya kutegemea kila wakati wawekezaji? Kwa mfano, upo uwezekano mkubwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ikaanzisha shughuli za utalii katika eneo hilo na fedha zote zikabakia katika Halmashauri yetu. Serikali inashindwa nini hadi kila kitu inakuwa ni mwekezaji, mwekezaji? Tunahitaji ufafanuzi katika hili, hata sera ya *PPP* inaweza kuwa na malengo ya kuwanufaisha wachache huku wengi wakibakia kufanywa watwana wa wamiliki wa makampuni ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini tunazo teknolojia nyingi ambazo tukiamua kuzitumia vizuri zinaweza kuliingizia Taifa fedha nyingi na kuepusha kupeleka fedha zote kwa wageni. Kwa mfano, pale Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Dar es Salaam wanazo teknolojia mbalimbali kama vile za ujenzi wa barabara, taa za barabarani, kufanya magari yatumie gesi badala ya mafuta, wanapiga hatua katika teknolojia ya kompyuta hususan katika *Graphics and Designs*. Pale Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* wanazo teknolojia mbalimbali kama kupiga kura kwa kutumia mtandao wa kompyuta: ni kijana mdogo wa chuo cha *IFM* aliyegundua teknolojia hiyo na kuanza kutafutwa na watu wa nje, sisi Watanzania tunalala.

Mheshimiwa Spika, hayo ni baadhi ya mambo machache ambayo iwapo Serikali ikikubali kuleta sera Bungeni pamoja na sheria ya kuruhusu Taasisi zote za Serikali kuruhusiwa kuanzisha makampuni ya kibiashara kama ilivyo China, tunaweza kupiga hatua kubwa sana kimaendeleo kuliko kila wakati kuagiza kila kitu au mambo mengi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hakika Bunge na Serikali vikiamua kuruhusu kuanzishwa kwa makampuni ya kibiashara yatakayomilikiwa na Serikali moja kwa moja na Serikali ikaacha kabisa mtindo wa kuzipatia kazi kampuni za nje zinazotengeneza faida za kupeleka kwao, tutakuwa tumetatua tatizo la ajira lakini pia Taifa hususan Serikali yetu kubaki na fedha nyingi nchini. Kwa mfano, hivi sasa hakuna sababu ya kuwapatia watu binafsi na makampuni yao wakati wataalam kama vile wa barabara wapo pale *DIT* ambao Serikali haiwaruhusu kuanzisha makampuni ya biashara, pale wapo wataalam.

Mheshimiwa Spika, Taasisi kama ile ikiruhusiwa itaweza kutengeneza faida na kulipa kodi Serikalini, lakini pia itaweza kuipunguzia mzigo Serikali yetu katika suala zima la kupatiwa ruzuku hii inapaswa kuwa hivyo hata katika taasisi nyingine zenye ujuzi na teknolojia fulani ambazo zinaweza kuuuzwa ndani na nje ya nchi. Tunaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni kwa nini isiruhusu Halmashauri zetu na taasisi mbalimbali kuanzisha makampuni na kisha kazi zote zikafanywa na taasisi hizo ili kuepusha gharama kubwa?

Mheshimiwa Spika, Serikali kukataa wazo hili basi ni wazi kuwa kuna mkono wa makampuni yanayozuia utekelezwaji wa wazo hili, yaani serikali inaweza kuwa na watendaji Fulani wenye kufanya maamuzi ambao wamenunuliwa kwa kuwa siyo baya hata kidogo. Vile vile serikali inatakiwa kuchukua hatua za haraka katika kuhakikisha mtandao wa reli hapo nchini unaimarishwa ikiwa ni pamoja na bandari. Hii ni kwa sababu sekta ya

usafirishaji pekee ikisimamiwa na kuimarishwa vizuri hapa nchini inaweza kulifanya Taifa kupata zaidi ya shilingi tirioni 10 kwa mwaka, bado hatujagusa madini, utalii, viwanda, kodi za wafanyakazi, bado hatujagusa kodi za biashara mbalimbali kama vile vinywaji vikali na baridi, sigara, mazao ya chakula na biashara. Pia kudhibiti misamaha ya kodi ambayo siyo ya lazima kama ilivyo hivi sasa kwenye madini, makampuni ya simu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawajibika kuchukua hatua za haraka kuyaingilia Makampuni ya Simu na kuyadai kulipa kodi ikiwa ni pamoja na kujisajili katika Soko la Hisa Dar es Salaam kwa kuwa kutokujisajili hapa nchini ni njia mojawapo ya wao kukwepa kulipa kodi *(Dar es Salaam Stock Exchange Market)*. Aidha, yapo mazingira makubwa yanayodhihirisha kusuasua kote katika kuboresha Shirika la Reli hapa nchini kumechangiwa na baadhi ya wafanyabiashara wa malori ambao hawataki kuona reli ikifanya kazi vizuri ili wao waendelee kufanya biashara ya usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani tukaendelea kuwakumbatia watu hawa ambao wakati mwingine wanakwepa kulipa kodi, inatupasa kama Taifa kurejesha usafiri wa reli kwa nguvu na kwa kasi ya ajabu ili kujenga heshima ya Serikali, ni aibu kwa Taifa kubwa kama letu kushindwa kuendesha kilomita za reli nchi nzima zisizozidi kilomita 2,600. Hiki ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na kile cha China ambacho ni zaidi kilomita 91,000 na wana mpango wa kuongeza hivi karibuni hadi kufikia zaidi ya kilomita 200,000.

Mheshimiwa Spika, kimsingi ni aibu, tunazidi kupigwa gepu na Mataifa ambayo wakati tunapata uhuru hali zetu kiuchumi tulikuwa sawasawa nao, kwa mfano, China, Korea, Malaysia, Indonesia, Singapore na kadhalika. Je, ni wapi tumekosea? Jibu ni rahisi sana, tumekosea kwenye kuheshimu hayo niliyoyajadili katika *paper* hii.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, inatupasa tuanzishe sheria ya kushughulika wahujumu wa uchumi kwa kuwa ni watu hatari sana katika maisha yetu ya kila siku, sheria hiyo inabidi iwe mahsusi kwa ajili ya kuwanyonga hadharani watu wote wanaohujumu uchumi wa nchi yetu na wahujumu ni akina nani? Ni wale wote wanaotumia nafasi za umma na binafsi vibaya kwa maslahi yao wenyewe. Hawa wanapaswa kunyongwa hadharani tena kwa mashine maalum au vinginevyo hata kwa kutumia risasi mbele ya watazamaji, kesho mtu yeyote akishuhudia fulani kanyongwa hadharani kwa risasi hawezi tena kurudia au kutenda kosa kama lile lililomfanya mwenzake anyongwe. Hii itaweza kuwa njia rahisi ya kukomesha tabia hii. Adhabu hii itapaswa kutolewa baada ya Mahakama kumtia hatiani mtuhumiwa, tusiogope Taifa linaangamia kutokana na majanga ya kulea wahujumu wa uchumi. Kulipuuza wazo hili ni ishara kwamba Serikali inawakumbatia wahujumu wa uchumi na inajua sababu za kukataa wazo hili.

Mheshimiwa Spika, maneno haya yanatoka moyoni kabisa na nitafurahi sana iwapo Serikali inaweza kutafakari kwa kina hasa ikijaribu kuepuka mtazamo kuwa kumnyonga mtu yeyote ni kinyume

cha haki za binadamu. Kuishi katika mtazamo huo ni upofu wa makusudi kwa kuwa mtu yeyote anayehujumu uchumi wa nchi yake na hivyo kusababisha wananchi kukosa huduma na maendeleo yao muhimu, huyo ndiye mtu wa kwanza asiyeheshimu haki za binadamu kwa kuwa huduma bora na safi za afya, elimu, usafiri, kuepukana na deni la Taifa vimesababishwa na wahujumu wa uchumi. Je, kuna sababu ya kuwalinda watu wa aina hiyo. Jibu ni rahisi, hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha na nategemea Serikali itachukua hatua. Siungi mkono hoja iwapo Serikali haioneshi njia mbadala na ambazo ni *serious* katika kutatua changamoto tulizonazo.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na yenye kutoa matumaini kwa Watanzania. Hata hivyo, nina maoni yafuatayo ili kuboresha utendaji wa Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matatizo ya ardhi; kwa muda mrefu sasa kumekuwa na migogoro mingi baina ya wakulima na wafugaji pamoja na wananchi wanaozunguka Hifadhi za Taifa na mara nyingi kusababisha vifo. Tatizo hili litazidi kuwa kubwa kutokana na ukweli kwamba idadi ya watu na mifugo inazidi kuongezeka na hivyo mahitaji ya ardhi kuzidi kuwa makubwa. Naishauri Serikali iweke mikakati endelevu ili kuleta suluhisho la kudumu katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za watumishi wa Halmashauri. Kwa miaka kadhaa sasa ajira mbalimbali za Halmashauri ikiwa ni pamoja na madereva, wahudumu na kadhalika zimekuwa zikifanywa na Idara Kuu ya Utumishi na kuleta usumbufu mkubwa. Je, isingekuwa busara ajira hizo za ngazi ya chini zikafanywa na Halmashauri zenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukosefu wa Watendaji wa Vijiji na Kata; Watendaji wa Vijiji na Kata ndiyo wasimamizi wakuu wa maendeleo katika Vijiji na Kata. Kwa bahati mbaya sana Vijiji vingi na Kata hazina Watendaji. Serikali inasema nini kuhusu upungufu wa viongozi hawa muhimu?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda sana kutoa shukurani zangu za dhati kwa nafasi hii ya kuchangia. Katika hotuba ya Bajeti tuliona kuna sehemu nyingi sana za ukusanyaji wa mapato ya Serikali, lakini kama hakuna nidhamu katika matumizi na upangaji wa mipango isiyohusisha vipaumbele vya wananchi yote ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, mipango mingi ya maendeleo inayopangwa na Viongozi wa Serikali ambao hawakutokana na wananchi ni kazi bure. Mfano mdogo ni utekelezajji wa maendeleo katika Mkoa wa Kagera, kuna chumba cha kulaza wagonjwa katika hospitali ya Mkoa wa Kagera ambacho chumba hicho tayari kimekamilika na hakijaanza kutumika kwa muda wa mwaka mzima sasa na sababu ya kutotumika ni

ukosefu wa fedha milioni 128 kwa ajili ya kununua vifaa tiba, vitanda na magodoro. Cha ajabu sekretarieti ya Mkoa wa Kagera haikukaa na kutafakari juu ya umuhimu huu na kuamua kuanza kujenga ofisi mpya ya Mkuu wa Mkoa nje ya mji kwa gharama ya zaidi ya bilioni kumi, huku walipa kodi wanaachwa wakijifungulia porini au barabarani wakitafuta hospitali.

Mheshimiwa Spika, kama tutaendelea na kuwa na viongozi wa aina hii, basi nafasi hii ya watu walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu itakuwa hatarini katika maoni ya Katiba mpya. Wakuu wa Mikoa ni vizuri leo wapo hapa na japo hawataweza kabisa kusoma rai yangu hii, basi ni vizuri Ofisi ya Waziri Mkuu, ikatoa waraka kwa wakuu hawa na kuwaelekeza jinsi ya kuratibu maendeleo yanayopendekezwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimeona kuna ongezeko la posho kwa Madiwani, ni jambo jema sana na kwa kweli nalipongeza, lakini kuongeza mishahara na posho bila kupambana kwa dhati na mfumko wa bei, ni kazi bure kabisa.

Mheshimiwa Spika, gharama nyingi kwa mbolea na sukari na mchele vimekuwa vikipanda bei bandarini kwa ajili ya urasimu na wingi wa *Reguratory Authorities* ambazo haziko pamoja *(not under one roof)* pale Dar es Salaam ambazo bado hata utendaji wao wa kazi sio wa pamoja wenye nia njema. Lakini unaongeza tu gharama kwa mlaji wa mwisho. Kwa mfano, *Regulatory Authority* mojawapo ni *SUMATRA*, ambao ndiyo wanaosimamia *ICD* (watunzaji wa makontena kwa niaba ya bandari). *SUMATRA* wamekuwa

wakikimbizana na daladala huku wakiacha hizi *ICD* zikijiongezea gharama zilizojificha *(hidden charges)* ambazo zimepelekea uongezekaji wa bidhaa zinazoingia nchini na kuwa ghali kwa mlaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji; hakuna Mbunge hata mmoja ambaye anaweza leo kusimama hapa Bungeni akajivunia kuwa Jimboni kwake kuna maji safi na salama kwa gharama nafuu na yanayopatikana kwa muda wote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa maji unapunguza sana gharama kwa Serikali. Hili nimeliona katika Mkoa wa Shinyanga kabla na baada ya mradi mkubwa wa maji na matokeo yake ni kama ifuatavyo:-

(1) Magonjwa ya mlipuko yamepungua sana na gharama ya matibabu imepungua.

(2) Ufaulu wa wanafunzi katika shule za misingi na sekondari umeongezeka.

(3) Bei ya mboga na matunda imepungua na upatikanaji wake ni rahisi na afya ya watu hawa imeimarika.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa miradi ya maji ambayo ipo kwenye utaratibu basi kasi ya utekelezaji iongezeke ili kupunguza mzigo mkubwa wa uagizaji wa madawa.

(4) Pia uzalishaji uliongezeka maana baada ya maji kupatikana na kupungua kwa magonjwa watu wengi walikuwepo mashambani na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, nategemea yote niliyoeleza yatafanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi. Mungu Ibariki Tanzania.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuongeza kiwango cha malipo ya posho kwa Madiwani, naamini kabisa ongezeko hilo litasaidia kuboresha utendaji wa Madiwani katika maeneo yao na kusimamia miradi ya maendeleo na kupunguza kero mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, natoa masikitiko yangu kwa Serikali kushindwa kutekeleza mpango wa dhamana ya umeme ambapo Bunge lako Tukufu lilipitisha shilingi bilioni 408, *TANESCO* iweze kukopeshwa, lakini cha kushangaza hadi sasa *TANESCO* hawajapewa *guarantee* na Serikali, matokeo yake *TANESCO* imekuwa ombaomba kwa makampuni ya wahindi yanayouza mafuta ili wapewe mafuta kwa mali kauli.

Mheshimiwa Spika, hii inalipunguzia *TANESCO* heshima yake na kupunguza heshima kwa Serikali yetu. Aidha, vigezo vinavyotolewa vya *TANESCO* kutokupewa dhamana havina msingi na vinaonesha ubabaishaji mkubwa kwa baadhi ya watendaji wa

Serikali hasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, mfano Mwanasheria Mkuu anasema *TANESCO* hawajapewa *guarantee* kwa sababu baadhi ya vipengele kwenye mkataba vinatakiwa kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, hii siyo sahihi kabisa kwani tafsiri ya vipengele kwenye mkataba inachukua zaidi ya mwaka mmoja sasa. Cha kushangaza zipo Taasisi za Serikali zilishawahi kupewa *guarantee* kwa mkataba sawa na huo mkataba wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba kabla ya kumaliza kujadili hii bajeti, Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze kwa nini Serikali inakataa kutoa *guarantee* kwa *TANESCO* hadi sasa na kupewa kauli na azimio la Bunge lililopitishwa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa daraja la Kilombero. Daraja la Kilombero liliahidiwa kujengwa tangu mwaka 2005, kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Hadi leo hakuna ujenzi wowote unaoendelea wakati ujenzi utagharimu zaidi ya bilioni 50 ambapo hadi sasa Serikali imetangaza tenda tu; je, ujenzi huo utakamilika lini? Kitendo cha Serikali kutenga bilioni moja kwenye bajeti itachukua miaka hamsini kujenga daraja hilo. Hii haitawasaidia wananchi wa sasa na mpango wa *SAGCOT* hautatekeleza kwani wananchi watalima na kuvuna mazao ya kutosha, lakini miundombinu ikiwemo Daraja la Kilombero kutokamilika, mazao yataishia kuharibika na kuwaongezea wananchi wa Kilombero na Ulanga umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba nipewe majibu kutokana na hoja zangu hapo juu. Naunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, napenda nami kuchangia kwenye bajeti ya Waziri Mkuu, naanza kwa kusema kuwa katika Bajeti ya 2011/2012, Serikali ilieleza kuwa itaongeza uzalishaji kwenye sekta ya kilimo, lakini matokeo yake bajeti iliyopangwa ni asilimia 2.92 ambayo haikukidhi haja na matokeo yake hakuna kilichozalishwa na maisha yamezidi kuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilisema katika bajeti yake ya mwaka 2011/2012, kuwa itashughulikia wafanyakazi hewa lakini katika bajeti ya 2012/2013, Waziri hakutaja chochote na wala kwenye bajeti ya Waziri Mkuu haikuzungumzia chochote. Je, Serikali haioni kuwa ahadi wanazozitoa wanashindwa kuzifanyia kazi na matokeo yake Serikali inashindwa kutekeleza ahadi wanazozitoa kwa wananchi na wananchi wanakosa imani na Serikali na Serikali inaendelea kupata hasara kwa kulipa wafanyakazi hewa na wananchi wanaendelea kukosa madawa na maisha yanazidi kuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisema katika bajeti ya mwaka 2011/2012 kuwa, watafufua umeme Nyakato-Mwanza *megawatt* 60, lakini hakuna umeme uliofufuliwa mpaka leo hii. Tunazungumzia bajeti ya mwaka 2012/2013, suala hili halikutajwa tena kabisa yaonekana wazi kuwa hili halikuwezekana.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa pale Serikali inaposhindwa kutekeleza ahadi walizozitoa ni vyema kulieleza Bunge kuwa suala hili halikutekelezeka kwa sababu na wakazieleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kuweka msukumo kwenye malengo ya *millennium*. Kwa kuwapunguzia wananchi wake umasikini wa kipato na pia kwa kushirikiana na asasi zisizokuwa za Kiserikali kwa kuwapatia wananchi wake vyandarua ili kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie kuhusu Shirika la Nyumba *(NHC)*. Shirika hili linastahili sifa kwa kufanya kazi kubwa ya kuwapatia wananchi makazi ya kudumu kwa kuwajengea nyumba na kuwauzia, lakini jambo la kusikitisha kuwa Serikali inatoza *(VAT)*. Matokeo yake nyumba hizi zinakuwa ni ghali sana na wananchi walio wengi wanashindwa kununua nyumba hizi na zinanunuliwa zaidi na wafanyabiashara na mafisadi tu. Wananchi walio wengi ambao ni wafanyakazi au wakulima ambao kipato chao ni kidogo wanashindwa kununua nyumba hizi.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nipongeze kwa hotuba nzuri ya bajeti kwa kutenga karibu kwenye maeneo mengi muhimu. Hata hivyo, pamoja na kupongeza hatua ya Serikali ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala ikiwemo Wilaya ya Busege na Mkoa wa Simiyu, napenda kuitaka Serikali iteue haraka Wakurugenzi, Watendaji wa Wilaya ili Wilaya

hizo ziweze kuanza kazi kikamilifu na kupanga mipango yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Busega kuna Kijiji cha Lamadi ambacho wakazi wake wanakadiriwa kufikia elfu arobaini, lakini bado hakijapata mamlaka ya mji mdogo. Ningependa kujua ni lini kijiji hiki kitapata hadhi ya mji mdogo ili uweze kuwa na mipango yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mpango wa muda mrefu wa kuupatia maji Mji Mdogo wa Lamadi tangu enzi za Profesa Mwandosya, lakini pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Jakaya Mrisho Kikwete aliwathibitishia wananchi katika mkutano wa hadhara, lakini pia uko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Mradi huu bado haujapangiwa fedha. Mradi huu sasa unakuwa rungu la kisiasa kwa Vyama vya Upinzani dhidi ya CCM. Naomba Serikali ichukue hatua haraka.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Busega kuna madini mengi yaligundulika ikiwemo Nickel na Dhahabu, wawekezaji sasa wameanza kununua viwanja na mashamba ya wananchi kinyemela bila elimu ya kutosha kwa wananchi na hivyo wanalipwa bei duni. Haya yanatokea katika Kata ya Ngasamo ambapo kampuni ya *Red Nickel* inawekeza. Lakini pia katika Kijiji cha Nyangiko watu wamepokonywa mashamba kwa bei ya dezo, hii itatuletea umaskini wa kutupwa. Tunawahitaji wawekezaji wa madini, lakini

tunapenda kuwepo na gawio sahihi kwa wananchi wanaoachia mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa baada ya Mkoa wa Simiyu kuanzishwa, Mkoa huu unapaswa kuuunganishwa kwa lami na mikoa inayopakana ikiwemo Mwanza (barabara ya Bariadi, Nyashimo), Singida (barabara ya Bariadi, Meatu, Sibiti). Tunaomba barabara hizi ziingizwe kwenye mpango wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Simiyu hauna chuo chochote cha elimu ya juu au ufundi. Naomba Serikali iboreshe mpango wake wa kuanzisha vyuo vya *VETA* ili angalau Bariadi, yalipo Makao Makuu ya Mkoa pajengwe chuo cha *VETA,* hivyo hivyo, vituo vya *SIDO*. Hizi taasisi mbili ni muhimu sana katika kujenga ajira, ujasiriamali na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa makusudi na huku wakijua wameamua kuinyonga ili ife, *NARCO*. Hili ndilo Shirika pekee la kibiashara katika Wizara hii, linayo rasilimali ya ardhi kubwa ili kuweza kuzalisha mifugo kibiashara na kuliletea Taifa mapato na kuongeza ajira. Hata hivyo, hili litawezekana kama kutafanyika uwekezaji wa kimkakati kwenye shirika hili. Licha ya kuwa kwenye *receivership* na kwa zaidi ya miaka kumi, lakini Wizara haitaki kuwatengea fedha bilioni kumi tu wanayohitaji kama dhamana ili waweze kukopesheka na taasisi za fedha. Wizara ya Mifugo wana dhamira gani? Zipo nyaraka zinazoonesha kukosekana kwa dhamira ya Wizara kulijenga Shirika hili. Hii ikemewe,

vinginevyo watendaji hawa wataumbuliwa maana vielelezo vipo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba ya Waziri Mkuu imeelekeza kila sekta na shughuli zake. Nianze na suala zima la ukuaji wa uchumi; pato hili la Taifa limekua 6.4 mwaka 2011 ukilinganisha na asilimia 7.0 mwaka 2010. Inaelezwa uchumi huu umekua nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa asilimia 5.1, kiwango kilishuka na kikadhihiri ukame ambao uliudhi pia kilimo, kuenezwa nchini na pia mfumko wa bei kupanda unaonekana bila mafanikio. Pamoja na wataalam ikamilishe miezi sita na 18 kupata matokeo ya hatua zilizochukuliwa na kupata matumaini ya bei ikipungua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali bila kuchukua hatua za uangalizi zaidi za kujiwekea akiba ya maji mengi kwa ajili ya umeme, mashamba mengi yawe ya umwagiliaji, mfumko huo wa bei hautashuka kamwe kwani mpaka sasa Tanzania kila kitu ni uchumi, ni kwa nini tusitumie uchumi wetu vizuri na kuwanufaisha wananchi wake na kuwapa unafuu wa bei ya vyakula.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sensa na makazi 2012. Ni kipaumbele cha pekee katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2012/2013. Inanipa shida pale Serikali inaposema kutenga maeneo ya kuhesabia watu inagharimu, jambo ambalo mwananchi atakuwa pale pale kwa nini ifanyike hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inapenda kuwekeza ili kuongeza kipato, hali hii itatugharimu sana kwa sababu wananchi bado wana tatizo kubwa la ardhi, wanapohamishwa kwa ajili ya mwekezaji. Wananchi huwa hawashirikishwi katika maamuzi ya ardhi hasa vijijni, hasa linapokuja suala la mwekezaji hali hii imepelekea watu wachache kuuza ardhi ya vijiji kinyume cha utaratibu wa sheria. Mfano, ni uwekezaji wa *NAPCO, NARCO* katika Mikoa ya Morogoro na Arusha hata huko Kondoa mwekezaji aitwaye *ENCO* na kadhalika. Hii yote inapelekea machafuko na kupelekea maisha ya watu kupotea kuwa kama wakimbizi katika maeneo yao, hasa wanapokuja kudai haki zao.

Mheshimiwa Spika, mfumo mbaya wa utoaji ardhi kwa mwekezaji katika maeneo mengi Tanzania ardhi inapochukuliwa na mwekezaji mwananchi ana kosa kila kitu na hawi na sehemu ya uwekezaji au umiliki wa ardhi hiyo. Kwa wenzetu kama Angola, ardhi hiyo inapowekezwa ni sheria lazima na mwananchi aliyechukua eneo lake awe na hisa na mwekezaji huyo.

Mheshimiwa Spika, wawezeshaji katika nchi yetu nao tuwaangalie. Pamoja na juhudi za Serikali, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(Mwananchi Empowerement Fund)* katika mikoa ukiwapo wa Dodoma kwa ajili ya zana za kisasa za pembejeo na kilimo cha umwagiliaji wa kisasa. Je, eneo umeelekeza maeneo wakulima walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi Serikali imekuwa inakiuka sheria na taratibu katika kuchukua ardhi toka kwa wananchi. Maeneo ambayo Serikali imekuwa ikitangaza kama hifadhi, mbuga, msitu wa Taifa au urithi wa dunia, wananchi wamekuwa wakinyanyasika kwenye malipo au kuhamishwa maeneo hayo. Mfano, mgogoro wa kondoa wa askari wa *GRV* na wakulima na viongozi wao wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama kwa kuwa tayari bajeti ya Waziri ni ndogo mpaka sasa kwani imefanikiwa kuchukua vijana 20,000 kwa wakati mmoja pamoja na mujibu wa sheria. Je, hao wote wanapopata nafasi na nyumba zao za kukaa wameziandaa au akitoka kwenye mafunzo anakwenda kaa nyumba moja tatu mpaka nne? Je, Serikali itakuwa inatoa ajira bila mafunzo, haileti tija.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii mpaka Serikali ipange bajeti yake vizuri kwa wakulima, afya, elimu, usalama na mwisho wawekezaji wawatoe.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika eneo la fedha za maafa ya mafuriko katika Jimbo la Mpwapwa, sambamba na mafuriko yliyotokea Mkoani Dar es Salaam yaliyotokea msimu wa mvua za masika uliopita 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mpwapwa lilikumbwa na janga hilo la mafuriko yaliyoharibu miundombinu ya barabara nyingi na sehemu kubwa ya mto mkubwa unaopita katikati ya Mji wa Mpwapwa, pamoja na madaraja kadhaa (Gulwe, Godegode, Chisalu, Tambi,

Mwenzele na Mlembule). Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa walitoa ripoti ya maafa ya mafuriko hayo na kuomba msaada wa fedha kutokana na mafuriko hayo. Taarifa hiyo ilitumwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa na nakala kupelekwa Wizara ya Fedha, fedha iliyokuwa inaombwa ilikuwa ni kusaidia kurejesha miundombinu ya barabara zilizoharibiwa na mafuriko. Hadi hivi sasa hakuna kiasi chochote cha fedha kilichotolewa kusaidia kurejesha miundombinu ya barabara zilizoharibiwa na mafuriko hayo.

Mheshimiwa Spika, je, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa; itasaidiaje kwa kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa iweze kurejesha miundombinu iliyoharibiwa bila ya kuathiri bajeti iliyopangwa ya mwaka 2012/2013?

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kwa kuwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Daktari Mgimwa); Naibu Waziri Mheshimiwa Saada Mkuya na Naibu Waziri Mheshimiwa Janeth Mbene, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa bajeti yao nzuri hususan kwa kukubali hoja na ushauri wa Wabunge mfano, kuondoa *VAT* kwenye pamba na nguo za pamba. Vile vile kuondoa kodi kwenye biashara ya bodaboda yaani pikipiki na mengine mengi. Nimalize kwa kumpongeza Mheshimiwa Daktari Mgimwa kwa kujibu hoja kwa kutumia taaluma yake vizuri sana pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Saada Mkuya, Mungu awatie nguvu na afya ili waweze kutekeleza majukumu yao barabara.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa imani endapo sitampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri Naibu Mawaziri walioko chini ya Ofisi yake, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI, Mungu awatie nguvu na afya njema na maisha marefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara ya Watumishi, natambua juhudi za Serikali za kuendelea kufanya mazungumzo na Vyama vya Wafanyakazi ili kuleta mahusiano mazuri kwa lengo la kuleta ufanisi katika majukumu ya wafanyakazi ya kila siku. Pamoja na majadiliano yote bado sijaona ongezeko la kuridhisha juu ya kuinua vipato vya wafanyakazi, mfano, bajeti hii ya 2012/2013 kima cha chini kama sijakosea ni shilingi 170,000.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano wa Mwalimu wa Dar es Salaam, mshahara huu wa shilingi 170,000 utatumika kwa gharama ya usafiri wa daladala tu kwani walimu wengi wanapanda daladala mbili hadi tatu asubuhi na anaporudi ni vivyo hivyo. Kwa hiyo, bado ninaisihi Serikali kuendelea kuona uwezekano wa kuongeza mishahara ya watumishi na kima cha chini iwe shilingi 250,000. Hii itasaidia sana kuwatia moyo watumishi kufanya kazi kwa ufanisi pia kupunguza utoro na rushwa katika maeneo mbalimbali ya kazi. Nasubiri ufafanuzi wa Serikali wakati wa kujibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa hospitali ya rufaa Singida, napenda kuendelea kupongeza juhudi za viongozi na watendaji wa Mkoa wa Singida kwa kuendelea kusimamia miradi ya maendeleo Mkoani Singida vizuri ukiwemo mradi wa ujenzi wa hospitali ya rufaa Mkoani Singida. Ni ukweli usiofichika kuwa, juhudi kubwa imetumika kufikia hapo ujenzi ulipo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na serikali kututengea mwaka huu shilingi bilioni 1.8, ikumbukwe ombi la Mkoa ilikuwa shilingi bilioni 3.8, hivyo ombi letu halikutazamwa kabisa. Naomba sana Serikali kulichukua ombi hili kwa umuhimu wa pekee kwani majengo ambayo yanajengwa sasa tukipata bilioni mbili hayo majengo yatamalizika na hospitali itafunguliwa, jambo ambalo litaokoa vifaa tulivyopata kwa wahisani visiharibike na wale Madaktari ambao wako tayari kuja kufanya kazi watakuja ili wasibadili nia. Naomba sana sana Mheshimiwa Waziri Mkuu asikie kilio cha Wanasingida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu soko la alizeti Singida. Napenda kuupongeza Uongozi wa Mkoa wa Singida chini ya Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Daktari Parseko Kone kwa kufufua Ushirika kwa kupata Vyama 81 ambavyo tayari vimewezeshwa na Mabenki ya *CRDB* na *NMB*. Ni ukweli usiofichika, wakulima wamekuwa wakipunjwa sana na wanunuzi wa kati, nayapongeza mabenki haya kwa uamuzi wake wa busara wa kuviinua Vyama vyaU kwa kuvipa fedha za kununua mazao ya alizeti.

Mheshimiwa Spika, napenda kumuunga mkono Mkuu wa Mkoa wa uamuzi wake wa kupiga marufuku

walanguzi kwenda kwa wakulima kununua alizeti bali wote wanaotaka kununua waende kwenye Vituo vya Vyama vya Ushirika washindane bei anayetoa bei kubwa ndiye anunue. Tusitoe mwanya wa kwenda vijijini watawapunja wakulima kwani wengi wao hawatajua kuwa bei gulioni imepanda na Serikali itashindwa kupata takwimu tutaendelea kuitwa maskini wakati umaskini wa kupindukia haupo. Bado soko huria lipo bali biashara ifanyikie gulioni na magulio yako huko huko vijjijini. Mfano, leo bei ya kilo ya alizeti ni shilingi 700 kutoka shilingi 500, lakini wanunuzi wadogo wadogo walikuwa wananunua shilingi 250 hadi 300.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa UKIMWI; napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Daktari Fatuma Mrisho kwa uongozi wake makini ambao umefanya watendaji wa *TACAIDS* kufanya kazi vizuri kwa lengo la kupunguza UKIMWI kwa kiasi kikubwa. Ni ukweli usiofichika Daktari Fatuma Mrisho ni makini, mwadilifu na ameifanya taasisi hiyo kuwa na watendaji wenye nidhamu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kumwongezea muda wa kufanya kazi kwani ana nguvu na juhudi ili aendelee kulisaidia Taifa hili katika kupambana na janga la UKIMWI. Namwomba aendelee kujenga mazingira rafiki na wanawake wanaofanya biashara ya ngono ili waache tabia hiyo ya kuaibisha jinsia yetu.

Baada ya pongezi niende kwenye mada kuwa sasa wakati umefika Serikali kuanzisha Mfuko wa UKIMWI na Serikali ieleze namna uchangiaji utakavyokuwa ili kila mwenye nia achangie ili kufanya

maandalizi ya kujitegemea endapo wahisani wataacha kutoa msaada.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja nikitegemea kujibiwa.

**MHE. NAMELOK E.M. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Waziri Mkuu kwa uongozi wake mahiri, pia nawapongeza Mawaziri na Watendji wote kwa kazi nzuri wanayofanya kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kuongoza sekta zote zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, napongeza Serikali kuweka kiwango cha chini cha kipato kwa wafanyabiashara kitakachotozwa kodi ya mapato, ili uamuzi huu uwe na manufaa kwa wananchi wote nashauri kuwa Serikali iweke kiwango cha chini cha mapato kwa wakulima ambacho kitatozwa kodi. Watendaji wa Serikali za Mitaa wamekuwa wakiwatoza kodi wakulima fedha nyingi sana kwa mazao hata kabla ya kuuza. Hii imekuwa kero kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango wa kuendeleza kilimo cha mpunga na miwa kwenye mabonde, yalioainishwa. Vile vile nashauri kuwa mabonde madogo madogo yaliyomo kwenye mikoa yote nchini yatumike kwa kilimo cha umwagiliaji kadiri itavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu akiba ya fedha za kigeni. Tumeona hali ya akiba ya fedha za kigeni si nzuri, yako manunuzi ya bidhaa toka nje ya nchi ambayo yangeweza kuepukika na hivyo kulinda akiba ya fedha zetu. Baadhi ya bidhaa hizo ni pamoja na uagizaji wa fedha za kigeni *(cash foreign exchange)* ambazo huuzwa kwa watu watokao nchini kwenda nje ya nchi kwa shughuli mbalimbali. Kwa vile hivi sasa karibu benki zote zinatoa kadi zinazoweza kutumika nje ya nchi, Sheria ya Taasisi za Fedha irekebishwe nchini, vilevile wafanyakazi wa taasisi wanaoagiza bidhaa wanatakiwa kutumia *letter of credit* badala ya kuhamisha fedha.

Mheshimiwa Spika, jamii ya wafugaji ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii itoe utaratibu wa kipekee kwa jamii ya Ngorongoro juu ya kupata mapato yatokanayo na utalii ikiwa ni pamoja na kuiwezesha jamii kupata njia mbadala kwa ajili ya chakula baada ya kusimamishwa kulima. Serikali iwasaidie wafugaji wa mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuboresha mifugo yao, ili kuondokana na umaskini wa kutegemea misaada,. Uboreshaji wa mifugo ni pamoja na kuwawezesha kuboresha masoko ya mazao ya mifugo na kuboresha mbegu ya mifugo.

**MHE. JOSHUA S.M. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, fidia za ardhi kwa wananchi waliokuwa wamiliki wa maeneo yaliyochukuliwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vipya katika maeneo maalum ya uzalishaji *(EP2)*. Eneo la Mahula kwenye Kata ya King'ori, Wilayani Arumeru wananchi waliokuwa wanamiliki

ardhi hii, hakuna aliyelipwa fidia mpaka sasa. Ni lini fidia italipwa na kwa *(rate)* kiwango kipi? Wananchi wanataka kufahamu ni lini hasa *(when exactly)* watalipwa fidia na kama bado Serikali haipo tayari ni kwa nini suala hili liliharakishwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kugawa Wilaya; kwa miaka mingi Wilaya ya Arumeru imeombewa kugawanywa kuwa Wilaya mbili kiutawala, Wilaya hii ni kubwa na idadi ya watu ni kubwa mno. Kumekuwa na changamoto kubwa sana kiutendaji na hivyo kupunguza ufanisi. Napenda kufahamu kama miongoni mwa Wilaya mpya 25 Arumeru imegawanywa ili kuanzisha Wilaya ya Enaboishu au la na Serikali ina mpango gani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu utatuzi wa migogoro kati ya Hifadhi ya Arusha na wananchi wa Arumeru Mashariki. Kumekuwepo na migogoro kati ya wananchi wa Kata za Ngarenanyuki na Leguriki, kupelekea mauaji ya wananchi wawili kwa risasi na wengine kujeruhiwa. Serikali imechukua hatua gani kwa nini familia za marehemu hazijalipwa fidia na kwa nini mpaka leo wananchi wa Leguriki hawajalipwa fidia kwa mazao yao kuharibiwa na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja nikipatiwa majibu stahiki.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Peter Pinda kwa hotuba yake nzuri kuhusu mapitio na

mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali kwa jitihada zake za kutatua matatizo mbalimbali kama ujenzi wa kiwanja cha ndege, unaendelea ujenzi wa gati unaokaribia kumalizika na kutupatia shilingi milioni mia tatu za ahadi ya Rais kwa ajili ya ujenzi wa tuta la barabara zilizotokana na ziara yake mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara ya lami takribani kilomita 16 kutoka Kilindoni – Utende ambalo tathmini ilishafanyika mara tatu, lakini bado halijapatiwa ufumbuzi. Imekuwa tatizo kwa Wanamafia kutokana na kushindwa kuendeleza majengo na mashamba yao kuhofia ujenzi huo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze ni lini barabara hiyo ujenzi wake utaanza?

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu; shule zetu hasa za msingi zinakabiliwa na tatizo kubwa sana la walimu lililotokana na kutopangiwa walimu wa ajira mpya kwa kipindi cha miaka mitatu sasa. Tunaiomba Serikali kuliangalia mipango yake na hasa ukizingatia walimu wengi wamekuwa wakijiendeleza na kuziacha shule zikiwa hazina walimu. Aidha, tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa nyumba na madarasa kwa shule za sekondari lakini walimu wanafanyakazi katika mazingira magumu yatokanayo na ukosefu wa umeme. Kiasi cha nyumba zipatazo 20 katika shule za Baleni, Micheni, Bweni na Kirogwe hazina umeme ambao inaonekana suluhisho lake ni kufunga *solar power*. Tunaiomba

Serikali kutupatia kipaumbele cha kipekee kulingana na hali ilivyo Mafia.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona Mheshimiwa Waziri kuandaa mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi za Shule au kutumia mamilioni ya fedha kwenye *UMISSETA*, wakati mipango iliyo wazi kutatua tatizo hilo haipo. Nani atasimamia michezo ikiwa walimu wanahama Mafia kutokana na kukosa umeme? Bodi zitamsimamia nani ikiwa hakuna Walimu kutokana na kukosa umeme.

Mheshimiwa Spika, najua namna ya matumizi ya fedha za *TASAF*, naishukuru Serikali kwa kutumia fedha hizo kukabiliana na kero za Taifa, lakini naomba Halmashauri ya Wilaya ya Mafia iruhusiwe kutumia fedha hizo ili wananchi waibue miradi ya kuweka *solar power* katika nyumba za walimu au Mheshimiwa Waziri Mkuu atuambie namna ambavyo bajeti yake ilivyojipanga kutatua tatizo hilo la umeme kwenye nyumba za walimu Mafia na katika Idara zingine kama Afya na Kilimo, Vijijini Mafia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi mengineyo *(OC);* Wilaya ya Mafia imekuwa ikitegemea kiwango kidogo sana cha fedha, mfano, mwaka 2012/2013 ni Sh. 748,320,000 ambazo kwa jiografia ya Mafia fedha hizo hazitoshi kwa kuwa usafiri unaotambulika Kiserikali ni ndege, Mafia *to* Dar es salaam, kwa *go and return* kiasi cha shilingi 300,000 hali inayopelekea fedha za *OC* kuishia kwenye safari za watumishi na kusababisha Halmashauri kushindwa kujipatia au kutoa huduma

zingine. Naiomba Serikali kujaribu kutatua tatizo hili kwa kuongeza fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la uvuvi ambalo ndiyo mhimili wa kipato cha wananchi wa Mafia. Serikali katika bajeti yake ya 2011/2012 ilijikita sana kuboresha ulinzi wa maeneo tengefu ya Bahari na kuanzisha au kuendeleza mabwawa ya samaki hali ambayo haikusaidia kuinua pato la Taifa lililokuwa asilimia 1.4 tu. Mwaka 2012/2013 bado mipango ni hiyo hiyo ambayo Wilayani Mafia sijaona bwawa lolote la samaki badala yake Wanamafia wamekuwa wakichomewa moto zana zao za uvuvi kama vile nyavu, boti na kupelekwa Mahakamani. Hali hii imechochea chuki dhidi ya Serikali ambayo bado haijapeleka mbinu sahihi za kuendeleza uvuvi Wilayani Mafia. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ajue kwamba, wananchi wa Mafia maisha yao yanategemea shughuli za uvuvi. Kwa hiyo, utueleze mipango ya Serikali katika kuinua sekta hiyo Mafia.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai kwa kila binadamu. Kimsingi Mheshimiwa Waziri Mkuu naishukuru sana Serikali katika kusaidia kutatua kero ya upatikanaji wa maji kwa kujenga visima 946 kwenye Halmashauri 84 ikiwemo Mafia.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyotoa mwaka 2010 ili kutatua tatizo hilo la maji katika visima vya Chole na Juani (Mafia) bado Serikali haijatekeleza. Nilijaribu kupeleka mitambo ya kuchimba visima, lakini ilishindikana kutokana na ardhi yake kuwa ngumu. Mheshimiwa Rais akaahidi kuvusha

kupeleka maji kutoka Wilayani. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze je, Serikali itaanza lini kutekeleza ahadi hiyo?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali katika juhudi zake za kuboresha miundombinu ya maji ikiwemo mitambo *(machine)* kama ilivyoelezwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini naomba aje Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, inakabiliwa na tatizo la uchakavu wa mitambo na miundombinu mibovu ya maji hali ambayo imeshindikana kutatuliwa na Halmashauri. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze mikakati iliyopo ndani ya bajeti yake ili kutatua suala hilo Mafia.

Mheshimiwa Spika, napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja na nashukuru kwa kuniwezesha kuchangia. Ahsante.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme katika Mkoa wa Lindi; umeme hautoshelezi mahitaji ya viwanda, uliopo ni *kv* 33 na mahitaji angalau *kv* 133. Umeme katika Mkoa wa Lindi si wa uhakika unakatika mara kwa mara, ni wa njia moja hitilafu ikitokea Masasi hadi Lindi umeme unakatika, tupate ufumbuzi wake sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kukipa Kitongoji cha Ruvu hadhi ya kuwa Kijiji, kwa sababu kimekidhi masharti yote yanayotakiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja la Mchinga, tulikubaliana katika Bunge hili kupitia majibu ya Serikali hapa Bungeni kuwa Serikali imekubali ombi maalum la

kuipatia Halmashauri ya Lindi fedha Sh. 380,294,000 kwa ajili ya kujenga Daraja la Mchinga, nataka kufahamu fedha hizo ziko fungu gani katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa stakabadhi ghalani, malipo ya pili yanachelewa sana, tunaomba maelezo kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha hotuba nzuri Bungeni. Ninayo machache ya kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini, naipongeza Serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* kwa kupeleka umeme Vijiji vya Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi, Ihembe I na Ihembe II. Japo mradi huu haujakamilika, lakini juhudi za kuukamilisha zinaonekana na naomba ziendelee. Mradi huu umeviacha Vijiji vya Rukale, Misha, Ruhita, Rubale na Kibogoizi. Naomba Serikali ijitahidi kufikisha umeme katika vijiji hivi kwani viko karibu sana na nguzo zilikopitia, wananchi wa Vijiji hivi wasiposaidiwa watasononeka kwa kuangalia kutoka vijiji jirani, pia umeme huu umekikwepa Kijiji cha Omurusimbi, Ihanda, Rukole, Chonyonyo na Rularo. Vijiji vyote hivi vinapakana hivyo, ni rahisi sana kuvifikia, naomba mradi huu wa umeme vijijini uangalie eneo hili kwani umbali uliopo ni kutoka nguzo zilikofikia, ni kati ya

kilomita mbili hadi ishirini tu, hivyo ni rahisi kuviunganisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi ya Rais. Alipotembelea Wilaya ya Karagwe wakati wa kampeni za mwaka 2005-2010, aliahidi kupeleka umeme katika maeneo ya Tarafa ya Binyonza. Ikiwemo Vijiji vya Kamagambo, Kiruruma, Nyakagoyagoye hadi Nyakaiga, pia ahadi hii ilihusishe wananchi wa Vijiji vya Chamuchuz, Kijumbura, Kaiho, Kanywamagana, Chabuhora, Kayungu, Bukangara, Kandegesho na Ahakishak.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi vinaonekana kama ni vingi, la hasha vijiji hivi vyote ni rahisi sana kufikisha umeme katika vijiji vyote hivi na kwa gharama nafuu. Wananchi wa vijiji vyote hivi wanasubiri kwa hamu sana ahadi ya Mheshimiwa Rais na kwa kuwa ahadi hii iliahidiwa mwaka 2010, wananchi wanashangaa ni lini mradi huu utaaanza na kukamilika. Je, Bajeti ya 2012/2013, imetenga fedha kwa ajili ya mradi huu? Serikali ijitahidi mradi huu uanze ndani ya mwaka huu wa fedha na kukamilika. Naiomba Serikali inipe majibu mazuri katika kujumuisha.

Mheshimiwa Spika, maji, katika mamlaka ya Mji Mdogo wa Kayanga Wilayani Karagwe ni tatizo kubwa sana. Mamlaka ya Mji huu wa Kayanga una miji midogo miwili inayokuwa kwa kasi sana nayo ni Kayanga ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe na Mji wa Omurushaka ambao ni mji mdogo wa biashara na makazi ya watu. Miaka ya 1960 na 1970 Mji wa Omurushaka ulikuwa na maji safi ya

bomba kutoka chanzo cha maji Charuhanga. Yapo matanki makubwa mawili ya maji, ni makame, lakini mazima ila maji hayaingii kwa nini miundombinu yote iliharibika.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imeshapeleka umeme kwenye chanzo cha maji kwa gharama ya milioni themanini na chanzo cha maji kimesafishwa kwa gharama karibu shilingi milioni kumi na sita kutokana na uhaba wa fedha kwenye Halmashauri ya Karagwe. Mradi huu umeshindwa kukamilika, huu ni mwaka wa tatu.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Omurushaka haupati hata tone moja la maji kwa miaka zaidi ya arobaini sasa na Mji wa Karagwe umepata maji chini ya asilimia 50, tayari nimeshamuandikia barua Katibu Mkuu Wizara ya Maji na uongozi wa Halmashauri ya Karagwe ukiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ulishaonana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na kusaidiwa fedha asilimia themanini ya mradi mzima wa maji ya Omurushaka. Nashukuru ahadi hii, bajeti nzima ni kati ya shilingi za Tanzania bilioni moja na nusu (Tshs.1.5 bn) naomba fedha hizi zitolewe katika mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, haya maombi ya maji ya Kayanga na Omurushaka ni ya Mji Mdogo wa Kayanga tu, lakini Jimbo la Karagwe zima na Kata zake 22 wanahitaji maji kwa ajili ya binadamu, mifugo na kilimo. Serikali itenge fedha za kutosha kuchukua maji toka vyanzo vingi tulivyonavyo toka kwa Mwenyezi Mungu kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Kajunju, Ziwa

Burigi, Ziwa Nyakakika, Ziwa Kaberenge na Mto Kagera. Serikali ifanye maamuzi magumu kwa kuleta maji Karagwe kama ilivyofanya Kahama.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema yote anayonijalia katika kutenda na kumudu kazi hii muhimu ya kuwakilisha wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi na Watanzania kwa ujumla. Napenda kuchukua fursa hii kuchangia hoja ya wahamiaji haramu katika Mkoa wa Kagera na Jimbo la Biharamulo Magharibi likiwemo suala hili limeshughulikiwa kwa kipindi cha nyuma, lakini sio kwa ujumla na ukamilifu wake. Limekuwa jambo la kusikitisha kuona wahamiaji hawa sasa wanakuwa na mamlaka ya kufanya fujo, kufanya vurugu na uharibifu mkubwa na mali za wazawa na muda mwingine hata kusababisha ulemavu na vifo kwa wazawa! Hali hii haikubaliki na hatua za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kulinda amani na utulivu wa wananchi wazalendo na wapenda amani.

Mheshimiwa Spika, umekuwa sasa ni utaratibu wa kawaida kwa hawa wahamiaji toka nchi ya Rwanda ambao sasa wameenea sehemu nyingi za Mkoa wa Kagera, hususan katika Wilaya ya Biharamulo wakifanya zaidi shughuli za ufugaji na uharibifu mkubwa wa mazingira! Jambo la kuhuzunisha ni pale wafugaji hawa wanapoharibu mashamba ya wakulima na hatimaye kuwapiga na muda mwingine kutoa lugha za kejeli na matusi kwa wazalendo wakijua kuwa dhahiri wanatumia utajiri wao wa mifugo kutoa hongo na hivyo kupoteza haki ya mwananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali ifanye uchunguzi wa kina kuhusu hawa wahamiaji haramu. Serikali itumie vizuri vyombo vyake vya kiuchunguzi ili kufanikisha kupata idadi ya hawa watu ili warudishwe kwao. Utaratibu mzima ufanyike kupitia Idara ya Uhamiaji, Usalama wa Taifa na hata Jeshi la Polisi wahusishwe na wawezeshwe ili kuanikisha zoezi hili kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia idara husika, Balozi zetu za nchi za nje, zifanyike taratibu za kidiplomasia ili kusudi hawa wahamiaji pindi watakaporudishwa kwao wasipate nafasi ya kurudi tena na kuleta usumbufu kwa wazalendo. Serikali ifanye mipango ya makusudi ili kurudisha ulinzi uliokuwepo miaka ya nyuma kwa maeneo ya mipakani kwani utulivu na amani vilitawala, lakini baada ya kuhamisha kambi za Jeshi la Ulinzi wa wananchi toka maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na *RADOR* iliyokuwepo Biharamulo, hali imekuwa tofauti kabisa na kufanya mipaka yote kuwa vichochoro vya hawa wahamiaji haramu pamoja na mifugo yao kupita kila kona wanapotoka.

Mheshimiwa Spika, vile vile Askari wa Wanyamapori nao wamekuwa wakifumbia macho suala hili kwani huko msituni ni dhahiri wanakutana na hayo makundi ya wahamiaji pamoja na mifugo yao. Kwani wanakopita ndiyo ofisi za hawa wanyamapori ziliko.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai yangu, wote tafadhali tuliangalie kwa urefu na upana wake. Hili ni tatizo

kubwa sana kwa maendeleo ya mkoa wa Kagera na jimbo la Biharamulo kwa ujumla. Naomba mamlaka zinazohusika ziangalie suala hili kwa umakini sana. Zoezi hili lizingatie yale mapungufu yaliyojitokeza kipindi kile kusudi muda huu zoezi hili liwe la ufanisi mkubwa na amani irejee.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia juu ya huduma kwa watu wenye ulemavu (huduma za jamii). Tunao wananchi walemavu (viziwi na mabubu) wananchi hawa wasio na uwezo wa kuwasiliana vizuri waendapo hospitali, pindi wanapoumwa huwa hawapati haki yao ya kimsingi ya kupata huduma za afya kwa umakini wakutanapo na watumishi wa idara ya afya. Kiziwi na Bubu anapofika hospitali akiumwa hukutana na Wauguzi, Waganga, Madaktari, Mafundi Sanifu, Maabara, Mafundi Sanifu Madawa, Mafundi Sanifu Mionzi.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo yote kiziwi na bubu anapofika mawasiliano ni sawa na sifuri. Natoa rai yangu kwamba katika mafunzo yote yanayowahusu wanataaluma wa makundi nilioutaja hapa juu wafundishwe lugha maalum ya vitendo na hii lugha ijumuishe katika mitaala yao ili wataalam hawa watakapoijua lugha hiyo basi wananchi wenzetu walemavu (Viziwi na Mabubu) watapata huduma kwa uhakika na umakini kwa kuwa mgonjwa mlemavu huyo atawasiliana na mtaalam moja kwa moja na maelekezo ya matumizi ya dawa na huduma nyingine atayopata kwa uhakika, hapatakuwa na madhara

yoyote kwani ataweza hata kuuliza swali na kupata jibu direct kutoka kwa mtaalam.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia kuwa, wataalam wa Idara ya Afya Mazingira *(vector control)* watilie mkazo wa elimu ya afya kwa wananchi juu ya kutokomeza mazalia ya mbu, usafi wa mazingira. Elimu hii ikitolewa kwa wananchi ufuatiliaji ukafanyike, baada ya muda hapatakuwepo na mbu, maana mazalio hayatakuwepo, hapatakuwa na ulazima wa kununua vyandarua na hata madawa ya kutibu malaria hayatakuwa na umuhimu wa kununuliwa, ugonjwa wa malaria utatokomea. (Ugonjwa huu ndiyo unaongoza hapa nchini na hivyo vifo vitokanavyo na malaria havitakuwepo tena). Fedha ambazo zingenunulia *anti-malaria and the accessories*) na vyandarua zitafanya *intervention* za kupunguza vifo vya watoto wachanga na vinavyotokana na uzazi *(MDGS)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji; wananchi wa Rukwa wana tatizo kubwa la maji pamoja na kwamba wamezungukwa na Ziwa Tanganyika na Rukwa lakini wana mto mkubwa wa Luiche na maporomoko makubwa ya maji ya Kalambo na Kate.

Mheshimiwa Spika, kama vile vijiji vingi vya Wilaya ya Bagamoyo wanavyonufaika na Mto Wami, Mto Ruvu, lakini kama vile wananchi wa Shinyanga wanavyonufaika na Ziwa Victoria, naiomba Serikali ya CCM, ifanye kila jitihada wananchi wa Rukwa wapatiwe maji kutoka katika vyanzo nilivyotaja hapo

juu ili wanufaike kama wenzao wa Shinyanga na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana kwa bajeti nzuri yenye matumaini. Nataka nichangie suala la mikutano ya mara kwa mara inayofanywa na Halmashauri za Wilaya, ALART; Ofisi za Kilimo; Ofisi za Walimu Wakuu wa Sekondari na Afya - Madaktari wa Mikoa. Mikutano inayofanywa na hao hapo juu ya kila mwaka husababisha idara zao kurudi nyuma katika maendeleo. Ni afadhali wafanye kila baada ya miaka mitatu na minne. Pesa nyingi hutumika katika mikutano hiyo, badala ya nguvu za kazi, mikutano ipunguzwe na sikukuu zipunguzwe pia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Mahakama ya Wlaya ya Ruangwa, mpaka leo haijajengwa, ipo ya zamani tu, tena Mahakama ya Mwanzo. Wilaya ya Ruangwa hakuna Magereza ya Wilaya, tunaomba tusaidiwe.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege wa Lindi umeachwa kabisa. Uwanja ule ni maarufu sana, ulianza wakati wa vita ya II (1939) una *runway* (6) umetumika wakati wa vita vya ukombozi wa Afrika ya Kusini, pia ukombozi wa Msumbiji na vita vya ukombozi wa nchi mbalimbali za Afrika, zikitua ndege kubwa kubwa, lakini sasa uwanja huo hata *Presicion Air* haitui,

kwa hiyo, tafadhali sana tunaomba uwanja wa ndege wa Lindi ufufuliwe.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Lindi, ilikuwa ndiyo mkombozi wa Lindi. Ajira kwa vijana zilikuwa zinapatikana, lakini sasa bandari hii haifanyi kazi. Tunaomba Bandari ya Lindi ifufuliwe.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, hongera kwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana ni muhimu sana na hasa kwa sasa wakati maelfu ya wanafunzi wanamaliza elimu ya msingi na sekondari, lakini wengi wao hawaendelei na elimu ya juu. Ili kuongeza mafunzo ya ufundi wapate kujiajiri na kuajiriwa, Serikali imefikia hatua gani katika kuviwezesha vyuo vya maendeleo kutoa elimu ya ufundi? Tume iliyoundwa ya kuwezesha *VETA* kusaidia Vyuo vya Maendeleo ilitoa mapendekezo gani katika kuwezesha hilo?

Mheshimiwa Spika, kwa nini nchini mwetu *dollar (USD)* inatumika katika biashara? Hatua hii haichangii kushusha thamani ya shilingi yetu? Je, Serikali kwa hili inasemaje?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu Kambi ya Jeshi la Alikhamis *Camp* Wawi. Pamoja na kwamba tunathamini mchango mkubwa unaotolewa na vyombo vyetu vya ulinzi, lakini naomba suala la kambi kuwa karibu na maeneo ya wananchi liangaliwe upya hasa katika

maeneo ambayo ardhi ni ndogo sana. Leo wananchi wa Wawi baada ya kuwa na Kambi za Jeshi, Polisi, JVZ, hawana ardhi ya kulima tena, kwa hiyo, ni vyema hili likaangaliwe kwa haraka. Aidh,a mesi ya Jeshi iliyoko Mji wa Chini karibu na Msikiti, Majumba inawakera sana waumini na wananchi. Naomba ihamishwe haraka.

Mheshimiwa Spika, tunathamini juhudi za Serikali katika kutafuta wawekezaji ila tunaomba tathmini ya kina ya aina ya wawekezaji na kiasi halisi walichoelekeza sio kile kilichoandikwa ndani ya mchanganuo wa biashara tu hivyo hivyo ajira walizosema watatoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilete orodha ya miradi ya *PPP* ambayo imepewa wawekezaji ambayo inatakiwa kupewa wawekezaji na utaratibu wa wazi wa kuwapata hao wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, suala la mgao wa rasilimali ufanyiwe *study-cash distribution system* ili wananchi wafaidike na rasilimali na pia tuangalie upya ule mchango wa *USD* 200,000 zinazotolewa, ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, leo tunazalisha *gas*, lakini wananchi hawafaidiki, ni vyema utaratibu wa mgawano wa rasilimali na maandalizi ya wataalam ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, nashauri Serikali izipe majukumu Wilaya zote mbali na kiasi cha nafaka

na tani milioni kumi na moja za sasa wazalishe mchele tani milioni tano hadi 2015 zigawiwe kila Wilaya na mahindi tani 3,000,000 ziada zaidi zinazozalishwa sasa. Hii ndiyo njia ya kupunguza mfumko wa bei kwa asilimia 24 ya jumla ya mfumko wa bei. Pia tuondoe vizuizi vya kuzuia wakulima wasiuze mazao yao wanakotaka, jambo ambalo linawadhalilisha sana wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakulima wa pamba na korosho. Nashauri wakulima wa korosho wasaidiwe kwa Serikali kuzungumza na wamiliki wa Viwanda vya Korosho, matatizo yake yawekwe ili yatatuliwe waweze ku-*process* korosho ili thamani ya korosho ipande na wakulima wafaidike. Aidha, suala la kuitaka *NDC* na Mifuko ya Jamii ianzishwe Viwanda vya Nguo, Nyuzi, kungoja wawekezaji tutachelewa sana, ni vyema tukakodisha *management* kuliko kuendelea kungoja wawekezaji. Kenya wamefanikiwa kwa kuwa na Viwanda vingi vya Nguo na Nyuzi.

Mheshimiwa Spika, ajira imekuwa ni tatizo sugu, nashauri vijana wanaomaliza masomo, tokea mwaka wa mwanzo wakabidhiwe maeneo yao na aina ya kilimo wanachotaka kulima baada ya kumaliza masomo, hivyo hivyo kwa wafugaji, wavuvi na kadhalika. Kwa njia hii tutakuwa tumewaandaa vijana wetu wajiajiri badala ya kungojea ajira ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi, mzee wangu alikuwa Kadhi, amefanya kazi ni Jaji Ramadhani, Lipiki, Mapigano na hakuna hata mmoja alisema kuwa kuna tatizo la kuwa na Mahakama ya

Kadhi. Hata Jaji Mkuu amesema hivyo. Naomba tulimalize hili lisilete mgogoro. Mwanasheria Mkuu alikuwa marehemu W. Jurado, mbona hakuna tatizo lolote? Nashauri, kutokana na vuguvugu lililopo la kisiasa jambo hili linaweza kuleta fukuto likipuuzwa na kusikilizwa watu wasio na hoja ila hofu tu ya kuogopa kivuli chao.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Bunge, ni vyema Serikali ikaharakisha Mfuko wa Bunge ili Bunge liweze kujipangia ratiba zake hasa za kuziwezesha Kamati kufanya kazi ya kuishauri Serikali na pia kuiwajibisha Serikali pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko, Serikali iache utaratibu wa kuwazuia wakulima kuuza mazao yao wanakotaka, iwaachie wauze kama tunavyoviachia viwanda kuuza bidhaa zao wanakotaka. Kuwazuia wakulima ni kudumaza kilimo na kuwadumaza wakulima, soko huria liwe kwa wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti, Serikali isimamie utekelezaji wa bajeti, kunahitajika nidhamu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi wa viwanda vyetu, vipo viwanda vinazalisha kuliko mahitaji yetu kwa mfano, viwanda vya *Lubricant*, lakini makampuni ya migodi bado inaagizia nje – urari wa biashara yetu unaathirika. Serikali itathamini viwanda vinavyozalisha bidhaa za kutosheleza mahitaji yetu ili tuweke kodi kubwa kwa bidhaa zinazotoka nje. Aidha, makampuni yanayokuja kuwekeza hasa udini ambayo yapo si chini

ya 260, mengine yanafanya biashara ya Machinga. Je, Machinga wetu wanafanya kazi gani yachunguzwe na wakati umefika wa kila mwekezaji kuweka *Bond cash* ya *USD* 100,000 kwa kipindi cha miezi sita na ndipo aruhusiwe kuwekeza kwa mtaji atakaoingiza . Kule Uchina huu ndiyo utaratibu wao katika kulinda ajira za wamachinga wao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi yake na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika maboresho ya sekta ya fedha, Serikali haina budi katika kusimamia kiukamilifu makusanyo ya pato la Serikali kupitia *TRA* na Taasisi zingine. Tanzania bado tunahitaji jitihada za dhati katika zoezi hili kwani bado walipa kodi wengi hawalipi kama inavyostahili, hivyo kwa kiasi kikubwa kuikosesha Serikali pato kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali watumie uzoefu wa zoezi la sensa ya watu na makazi katika kuboresha na kuharakisha zoezi hilo la vitambulisho vya Taifa na anwani za makazi. Vitambulisho vya Taifa vikitumika vizuri vinaweza kusaidia *TRA* kufuatilia walipa kodi wote nchini, hivyo kutatua changamoto ya ukwepaji wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Taifa bado linakabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa mfumko wa bei hasa kwa chakula (mchele, sukari, unga na kadhalika), ambako kunaathiri sana wananchi wa kawaida. Suluhisho la mfumko wa bei kwa vyakula ni kuongeza uzalishaji katika kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji. Serikali katika kukabiliana na tatizo la chakula tayari wameweka mkakati huo kupitia kilimo kwanza na kutenga maeneo maalum katika kilimo cha umwagiliaji katika bonde la Kilombero na mengineyo hili nalo limeainishwa katika mpango wa *SAGCOT*. Pamoja na mikakati hii ya kuendeleza kilimo ili kukabiliana na uhaba wa chakula, lakini bado naona Serikali katika bajeti hii 2012/2013, haijatenga fedha za kutosha katika kuteleza kilimo hiki cha umwagiliaji katika bonde la Mto Kilombero.

Mheshimiwa Spika, Wakazi wa Wilaya ya Ulanga tangu uhuru wamekuwa na kilio na kero ya Daraja la Kilombero. Pamoja na ahadi za Serikali tangu 2005 kwamba itaanza na ujenzi wa daraja la Mto Kilombero. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awahakikishie wananchi wa Ulanga ni lini hasa daraja hilo litaaanza kujengwa? Daraja hili litaharakisha na kuchochea kilimo katika Wilaya ya Ulanga ambayo ndiyo wilaya kubwa inayotoa mchango na kuzalisha mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, tufute ushuru wa mazao kwa wakulima, wanakwenda kuuza mazao madogo madogo, wanaanzia kutoa

ushuru kwenye vizuizi *(barrier),* wanatoa ushuru huko magulioni. Wakulima hawa ni watu maskini sana, kwa nini tunawatesa kwa kuwatoza kodi?

Mheshimiwa Spika, hii ni kero kubwa kwa wananchi wetu. Tuwaondolee kero hii, mtu huyu anapopeleka ndizi au mananasi kuuza gulioni, anakuwa amelenga akiuza anunue chumvi, mafuta ya taa na alipe michango ya shule na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sio mfanyabiashara huyu na tunaposema kuwa kodi hizi watoe wafanyabiashara hawa hawatatoa bila kwanza kuwatoza wakulima hawa. Jambo hili tuliangalie sana na tuwaonee huruma wakulima wetu maskini.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, napenda kuunga mkono hoja ya bajeti ya Waziri Mkuu kwa kuwa Serikali yetu imekuwa sikivu sana na inasikiliza shida za wananchi wake na pia inapokea ushauri unaotolewa na viongozi wake.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Matumizi ya fedha za maendeleo na Ripoti ya *CAG*. Msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Saalam na Mfumko wa bei ya vyakula.

Mheshimiwa Spika, katika matumizi ya fedha za maendeleo, naomba Serikali ifanye juhudi za makusudi katika kusimamia fedha za shughuli za maendeleo,

fedha hizi mara nyingi utendaji wa Serikali hawatekelezi wajibu wao katika matumizi kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kuwapatia kazi wakandarasi wasio na sifa ambao hujenga majumba yasio na viwango na barabara zisizo na viwango.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi yanayajengwa katika Mkoa wa Dar es Saalam, mengi hayana viwango vya Kimataifa. Mfano, nyumba nyingi zinazojengwa hazina viashiria unapotokea moto. Baadhi ya nyumba zinazojengwa pia hazina huduma ya walemavu, hazina sehemu ya kupaki magari, pia hazina uimara. Hali hii imeonekana katika Ripoti za *CAG* zichukuliwe dhidi ya waovu wote.

Pili, ni kuhusu msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Katika Jiji la Dar es Saalam unazidi siku hadi siku kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo sehemu muhimu ya uchumi wa Tanzania, lakini vitendo vya wananchi kutofika kazini kwa wakati vinasababisha uchumi wetu kuyumba.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam tuna Bandari, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, Makao Makuu ya *TRA* pia kuna sehemu inayoshughulikia usafiri wa kutoka Zanzibar - Dar es Salaam, Zanzibar - Pemba. Foleni za Dar es Salaam zinawatesa wengi, si wakazi wa Dar es Salaam tu ni pamoja na wageni wote wanaoingia Dar es Salaam.

Tatu ni mfumko wa bei ya vyakula; wananchi wetu wana hali ngumu ya maisha kutokana na kupanda

kwa bei ya vitu na hasa vyakula kama mchele, unga na sukari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kujitahidi katika kudhibiti hali hiyo lakini hali ni bado ngumu, kutokana na uhaba wa mvua uliotokea mwaka huu. Serikali ni vyema ikajiandaa mapema kwa kuagiza chakula kutoka nje ya nchi ambavyo vitapoza makali ya mfumko wa bei za vyakula kwa wananchi wa kipato cha chini. Ingefaa tukaiga wenzetu Zanzibar kwa kununua chakula kwa wingi mfano, mchele na sukari ili kudhibiti mfumko wa bei kama walivyofanikiwa wenzetu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake nzuri ya Bajeti ya Ofisi yake ambayo imezingatia mambo mbalimbali yenye makusudio ya kuleta maendeleo nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote waliopo katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na TAMISEMI na masuala ya Walimu. Tatizo la walimu na mishahara yao na madai ya kila siku sasa limekuwa sugu. Walimu wamekuwa wakilalamika kistaarabu sana. Wamekuwa wakidai madeni yao huku wakifanya kazi, lakini sijui Serikali imelichukuliaje suala la Walimu. Sitakubaliana

na lolote mpaka Serikali itoe kauli yake kwa Walimu. Mwalimu ni mtu muhimu sana, huwezi kuwa Daktari bila kupita kwa Mwalimu na huwezi kuwa Hakimu mpaka upite kwa Mwalimu. Cha kushangaza, makundi yote muhimu yanapewa posho kasoro Mwalimu tu.

Mheshimiwa Spika, nataka majibu kutoka Serikalini kwa nini Mwalimu hastahili kupewa posho ya mazingira magumu? Kwa nini Mwalimu asipewe posho wakati wanafanya kazi katika mazingira hatarishi. Walimu wanapigwa na wanafunzi mpaka majeruhi lakini hawana bima ya maisha.

Mheshimiwa Spika, Walimu wanafanya kazi shuleni kwa masaa nane, lakini wana kazi ya kuandaa masomo na kusahihisha kwa masaa kumi na mbili. Serikali itambue kazi za Mwalimu na muda anaotumia.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi iliangalie suala la Walimu kwa moyo wa huruma na uungwana mkubwa sana kwa kuwa wamekuwa watulivu sana kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya Walimu nataka nichangie malalamiko yangu juu ya Serikali yetu kuwanyima fidia waliobomolewa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara ya Kilwa (nina-*declare interest*).

Mheshimiwa Spika, nimeandika barua nyingi Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kupeleka taarifa nyingi za kuonesha wananchi waliolipwa si sawasawa, walengwa hawajalipwa na hali ya wananchi ni tete. Sikupata ushirikiano wowote na wananchi wanaichukia

Serikali yao na hapo hapo wale wasiostahili kulipwa na wakalipwa kupitia Mahakama wanadai tena nyongeza na Serikali kwa kukosa ushirikiano inaweza kuwalipa tena.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia suala la fidia ya Kurasini, wananchi wa Kurasini wamesimamishwa kuendeleza majengo yao kwa muda mrefu. Wananchi hawa hawakopesheki na hawajui ni lini watapata tamko la Serikali au walipwe au waachwe?

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niishauri Serikali yangu sikivu ya CCM, kwa kuwa wananchi wale kwa muda mrefu wamewekwa rehani na Serikali, ni vyema kama Serikali imeshindwa basi itafute mwekezaji mzuri ambaye anaweza kuwalipa vizuri wananchi wale watoke, waende wakatafute maisha kwa kujenga makazi mapya katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Kurasini ni eneo zuri sana kwa nini tunaacha eneo muhimu sana na wananchi wamekubali kupisha kufanyia shughuli za maendeleo. Serikali itafute fedha hata kwa kukopa eneo lile linalipa.

Mheshimiwa Spika, naomba mipango ya Mji wa Kigamboni nayo iharakishwe kwa kuwa wananchi wa Kigamboni wengine hawana hata umeme na *TANESCO* wanashindwa kupeleka miradi ya umeme kwa kuwa hawajui miundombinu ya barabara itapita wapi? Wasije kufanya kazi ya hasara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa sana linaloikabili Serikali yetu ni mapato madogo yasiyoweza kukidhi matumizi yetu. Halmashauri ndiyo inaweza kuwa jibu la matatizo hayo, kwa sababu ndiko chanzo kikuu cha mapato yetu, ikiwa yatasimamiwa vizuri na watu waadilifu. Ni kupitia Manispaa zetu ndiyo mapato mengi yamekuwa yanapotea.

Mheshimiwa Spika, nashauri Madiwani na viongozi wa Serikali za Mitaa wapewe majukumu na malengo ya makusanyo vile vile wapewe madaraka zaidi ya kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato. Yawepo Mabaraza ya Kata na Mitaa yatakayosimamia upatikanaji wa mapato yaliyopangwa ili kuwapa motisha na kuongeza mapato. Kata na Mitaa ipewe asilimia ya makusanyo kama Mtaa asilimia kumi na Kata asilimia kumi na iliyobaki ndiyo ipelekwe kwenye makusanyo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na motisha hiyo pia wapewe mishahara kwani kwa mtindo huu watajilipa wenyewe. Hii ni pamoja na kuongeza mapato, lakini pia itachochea maendeleo kwa kutumia asilimia zao kufanyia maendeleo muhimu kama kufanyia matengenezo barabara, zahanati, kununua madawati na mengineyo kadiri watakavyoona wao muhimu. Kuwe na chombo ndani ya Manispaa ambacho kitafuatilia na kukagua mapato na matumizi. Wananchi wataona wanamiliki maendeleo yao na wataona haja ya kutunza na kukuza mapato yao. Ni

mapato mengi sana ambayo yanaingia kwenye mikono ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji na uwezeshaji, sera ya uwekezaji na uwezeshaji bado haijaweza kuonekana kwenye jamii jinsi inavyoweza kumnufaisha mwananchi wa kawaida. Ni ukwelil kwamba wengi wa vijana na wanawake wameachwa nyuma na wala hawajui ina faida gani kwao na kwa kweli wengi bado wanahangaika sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa na elimu ya kutosha na makundi hayo mawili ya vijana na wanawake ni lazima waone umuhimu na uelewa wa sera hii na kwa jinsi gani wanaweza kupata uwezeshaji. Hii ni kweli hata kwa ambao tayari wanayo miradi, lakini hawajui ni jinsi gani wanaweza kukuza mitaji yao ili biashara zao ziwe za kuwaendeleza na siyo za kula tu. Wengi wa hawa, makundi mawili mjini ni wafanyabiashara na wafugaji wa kuku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwingiliano wa Wizara ya Afya, Elimu na TAMISEMI, kuna mkanganyiko mkubwa sana kwa Afya na Elimu kuwa na Wizara mbili zisizokuwa na mawasiliano ya karibu kuhusu kazi zao. Serikali inahitaji kukaa chini na kuangalia ni jinsi gani itajipanga upya kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu amani na usalama; ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi, amani ni lazima iendane na usawa. Hali ilivyo sasa siyo sawa, na inahitaji hatua za haraka na umakini, kuhakikisha usawa wa kijinsia, kielimu, kidini, kikabila. Ni jambo la

kawaida kuingia kwenye Ofisi ya Serikali na kukuta viongozi wa juu wote ni kutosha mkoa mmoja, wa dini moja na bila kujali hata jinsia. Ni tabia iliyozoeleka sasa kualikana kwa Majimbo watu wanaotokea mkoa mmoja. Kukusanya fedha kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa wao wakati wao ni wakazi wa Jijini Dar es Salaam, ni vipi uache shule ya Ilala haina madawati halafu wewe mkazi wa Ilala unafanya harambee ya Shule ya Mufindi. Tunatengeneza matabaka, hivyo wananchi wazaliwa wa Dar es Salaam wanaona wao ni matofali ya kupandia wengine kutengeneza makwao.

Mheshimiwa Spika, naomba hali hii itupiwe macho.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, uhaba wa chakula na njaa, katika Jimbo la Mbozi Magharibi, Wilaya mpya ya Momba hususan Tarafa ya Kamsamba yenye wakazi wasiopungua 60,000, kuna hali mbaya sana ya chakula mwaka huu. Hali hiyo ilitokana na ukame wa kutisha uliotufika wananchi wa Momba baada ya wananchi kupanda mazao yao na kukauka kutokana na ukame. Hivyo basi, wananchi kwa mwaka huu hawajavuna chochote na mpaka sasa bei ya chakula ipo juu sana mfano, debe la mahindi ni shilingi 13,000 ilihali msimu kama huu wa mavuno bei ya chakula huwa chini sana. Hivyo basi, mheshimiwa Waziri Mkuu tunaiomba ofisi yako kupitia Kitengo cha UKIMWI na Maafa, kikafanya tathmini katika Wilaya ya Momba ili kupitia hifadhi ya chakula, Taifa tupate msaada wa kununua kwa bei nafuu kwa ajili ya

wananchi hawa kwa maana hali ya huko ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji safi na salama, katika miaka ya 1995, Tarafa ya Kamsamba yenye Kata tano pamoja na Tarafa ya msongamao yenye Kata mbili walipata mradi wa maji ambao ulitarajiwa kufadhiliwa na Shirika la *DANIDA*. Mradi huo ulitakiwa kusambaza maji toka Ziwa Rukwa na kuelekezwa katika Kata hizo saba.

Mheshimiwa Spika, mchoro wa mradi huo upo na ulikamilika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhifadhi na kuukamilisha mradi huo ili kuondoa kero hiyo ya maji kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005, Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliwaahidi wananchi wa Mji wa Tunduma kuwa watapatiwa maji safi na salama. Eneo la Tunduma ni eneo lenye wakazi wasiopungua 100,000 sasa na ukuaji wake ni wa kazi sana. Je, miradi mingi iliyo katika karatasi (kimaandishi) itakamilika lini? Naomba Ofisi yako itusaidie kuokoa hali mbaya ya maji katika mji huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha tena katika kipindi kingine cha bajeti. Mchango wangu upo katika maeneo yafuatayo ya ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara, misingi ya kutengeneza mishahara yetu inafanya mishahara ya wafanyakazi *(private/public)* kuwa ni midogo sana. Haifanyi mfanyakazi kuwa na uhakika wa kufika mwisho wa mwezi na kukidhi mahitaji muhimu. Hii ni kwa wote. Wafanyakazi ngazi za chini kati na juu, lakini viwango hivyo haviheshimu majukumu na wajibu pia, kama watendaji wakuu wa baadhi ya mashirika wanapata mshahara mkubwa kuliko Waziri wao, hali hii ya udogo wa mishahara inachochea rushwa, lakini pia inafanya kazi ionekane si muhimu. Naomba sana jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji, naona mkazo upo kwenye fedha zaidi, napendekeza tuwe na program zinazotilia mkazo katika kubadilisha ufahamu wetu ili kujenga msingi wa kujitegemea kuwajibika. Watu wana wanawajibika kwa hali walizonazo na wanao wajibu wa kutoka hapo. Serikali ionekane inawawezesha vijana hasa wanaomaliza *VETA* kwa kuwa na *(guarantee bank)* na kuwapa tenda za ujenzi (umeme, matofali na kadhalika).

Mheshimiwa Spika, kuhusu safari nyingi za *DEDs*, Wakurugenzi wa Halmashauri hawakai ofisini, mara nyingi utakuta watu wanaokaimu tu, mara nyingi mno wanaoitwa Dodoma, Dar es Salaam, Morogoro. Lini watasimamia rasilimali na maendeleo Wilayani. Utafiti ufanywe pengine wanaokuwa Wilayani kwa robo mwaka tu. Tutumie *advantage* ya *internet* kwa mawasiliano, hakuna sababu ya kusafirisha watu. Kama hatutarekebisha, basi nadhani mawazo ya Madiwani yatazuia safari hizo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbinga Mashariki, uwekezaji, tathmini ya ardhi ya wananchi. Misingi ya tathmini katika Halmashauri pengine si mizuri na hivyo wananchi wanapata fidia ndogo na hailingani na hela halisi ya maisha. Hii inasababisha malalamiko mengi na inawakatisha tamaa wawekezaji, pia naendeleza jambo hili lichunguzwe na tuwe na mwongozo bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunao mradi wa *Tancoal*, viwango vilivyolipwa kama ushuru wa Halmashauri ni vidogo, hebu tupewe pia mwongozo mzuri zaidi, lakini pia kijiji husika lazima kipewe asilimia fulani. Naomba Waziri wa Mkuu atoe maelekezo kijiji kinalipwa kiasi gani katika mradi huu wa makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, mradi huu haujatajwa kabisa katika hotuba ya Waziri Mkuu, lakini ni mradi wa kwanza nchini wa uchimbaji mkaa na yapo matumizi ya kuzalisha umeme *MW* 400. Ni kwa nini mradi huu hautajwi. Haukutajwa na Waziri wa Fedha na mipango pia. Je, Serikali haitambui mradi huu? Naomba Waziri Mkuu afanye ziara katika mradi huu mara baada ya kumaliza Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara ya mahindi, mwaka jana wananchi wa Jimbo la Mbinga hasa wakulima wa mahindi walipata tabu ya kuuza mahindi yao. Napenda kujua mwaka huu kuna mpango gani? Naomba majibu tena ya maandishi, tumeomba pia kujengewa soko kule Kigonsera, nini majibu ya maombi hayo.

Mheshimiwa Spika, malipo ya wana ushirika wa Mbinga shilingi milioni mia nne. Hili jambo ni la siku nyingi sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu analijua vyema. Ni lini wakulima hawa watalipwa na ni lini pia lile deni la *NBC* karibu shilingi milioni mia saba litafutwa kama yaliyofutwa madeni ya Vyama vya Ushirika vingine. Naomba pia majibu ya maandishi. Lakini upo mpango gani wa kukabidhi mali za *Mbicu* wa *Mbifua* baada ya wana ushirika kulipa deni kwa kampuni binafsi *(golden impex)*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja.

Pili, chenji ya Rada kwa maelekezo ya Serikali ni kwamba, fedha hizo zitapelekwa katika sekta ya elimu, hivyo, kwa kuwa fedha hizi zinahusu pande mbili za Muungano. Nashauri Zanzibar ipatiwe fungu lake kwa kupewa madeski (vikalio) kwani shule nyingi za Zanzibar hazina vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Muungano, kwa muda mrefu tatizo la mapungufu ya muungano limekuwa likizungumzwa na Viongozi au Watendaji wa Serikali wa ngazi za juu tu bila wananchi husika kupata taarifa. Hivyo, nashauri kuwa wakati umefika kuwaarifu wananchi kupitia masuala yaliyofikiwa katika kuboresha Muungano ili wapate kuelewa, aidha taarifa hizo zitolewe kupitia mikutano ya hadhara, vyombo vya habari, (*Radio* na *TV*) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Kiongozi Mkuu katika Serikali ya Muungano. Nashauri atenge muda na afanye ziara ya kikazi Kisiwani Zanzibar ili kuzidisha upendo kwa wananchi wake na naomba katika ziara hiyo afike katika Jimbo langu la Bububu.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu bajeti inayojumuisha Tawala za Mikoa ikiwemo Mkoa wa Dodoma. Sote tunajua kwamba Ofisi ya Mkoa wa Dodoma iliungua moto na kuteketea. Hivyo, ujenzi wa ofisi hii ulishaanza katika eneo lililotengwa kwa ajili hiyo. Ujenzi huu unasuasua sana kwa kukosa fedha za ujenzi kiasi cha fedha shilingi bilioni tano aliyotoa Waziri wa Fedha, ni kwamba fedha hizo zingepatikana 2011/2012 ili kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu hatuoni fedha yoyote kutamkwa au iliyotengwa kwa ajili hiyo. Je, ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Dodoma utaendelezwa katika bajeti ya mwaka 2012/2013 na ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili hiyo?

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano, naipongeza Serikali kwa kuendelea kudumisha Muungano na kufanya juhudi za makusudi ili kero za mambo ya Muungano zipatiwe ufumbuzi na wananchi

wa nchi mbili hizi waweze kuishi bila ya kubughudhiana.

Mheshimiwa Spika, nashauri ingawa viongozi wetu wanafanya juhudi kubwa na vikao vinafanyika na baadhi ya kero zinapata ufumbuzi, lakini ipo haja kwa Bunge hili kujua mazungumzo hayo yanavyoendelea hatua iliyofikia na nini hatima yake. Haja hii itatusaidia sisi Wabunge kujua kwa kina kinachoendelea na pia kusaidia kuwatuliza wananchi juu ya jazba waliyonayo kutokana na kupata maelezo yanayowapotosha hasa kutoka kwa Wapinzani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ulinzi na usalama, nchi yetu imeendelea kuwa ya amani na utulivu ingawa yapo matokeo yanayojitokeza ya kuashiria uvunjifu wa amani. Naishauri Serikali isiwe na huruma na ichukue hatua mara moja pale mmoja wetu anapotumia uhuru wake na kuhatarisha uhuru wa wengine.

Mheshimiwa Spika, vikosi vyetu vya ulinzi vinafanya kazi nzuri na viko tayari kuilinda kuitetea na kuiendeza nchi yetu, lakini vinakabiliwa na matatizo yafuatayo (Kamati yetu ya Hesabu za Serikali tulitembelea Makambi ya Ihumwa Dodoma na Shirika la Mzinga Morogoro):-

Uhaba wa fedha ambao unakwamisha mazoezi ya vitendo kwa majeshi yetu na vijana walioko mafunzo, pamoja na vifaa.

Mheshimiwa Spika, vile vile uhaba huo wa fedha umeendelea kuathiri vifaa muhimu vya kijeshi ambavyo vimekosa maeneo stahiki ya kuvitunza na kuvifanyia mazoezi kwa wakati ili kuvipa uimara na kuwa tayari kwa jeshi na vifaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua ya kuwahamisha wananchi waliohamia maeneo ya Jeshi ikiwemo Dodoma, sehemu ambayo jeshi wameiandaa kwa mazoezi ya milipuko.

Mheshimiwa Spika, kuliendeleza Shirika la Mzinga. Shirika hili limebobea katika utaalam wa kila fani, Serikali ikiliwezesha kwa kulipia fedha za kutosha litaweza kujiendesha na kuzalisha bidhaa mbalimbali ambazo zinahitajika kwa wingi na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, kuliwezesha Jeshi kimafunzo na kivifaa ni kujihakikishia amani na utulivu katika nchi yetu na kuwafanya wananchi waweze kufanya kazi ili kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kusema naunga mkono bajeti hii. Naunga mkono kama Wanamsalala walivyoniagiza kwa matarajio kwamba kuanzia sasa na siku za usoni, Serikali itatumia bajeti hii na zingine zijazo kujibu changamoto za umaskini Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumzia masuala ya uchumi wa Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla,

naomba niifikishie Serikali (TAMISEMI) maombi yafuatayo kutoka kwa wananchi wa Msalala:-

Kwanza, kwa kuwa ni ukweli usiopingika kwamba Kahama hivi sasa ni Wilaya kubwa kuliko Wilaya zote nchini kwa kuwa na wananchi zaidi ya 1,100,000, Vijiji zaidi ya 300 na Kata 55 na kwa kuwa tayari vikao vya Wilaya na Mkoa vilipendekeza toka 2010 kuanzishwa kwa Wilaya mpya mbili za Msalala na Ushetu kwa kuigawanya Wilaya ya Kahama na kwa kuwa tayari Serikali ilikubali maombi hayo, japo si kwa ukamilifu wake, kwa kuanzisha Wilaya ya Ushetu, tunaiomba tena Serikali yetu iangalie kwa huruma wananchi wa Kahama na ikubali kuigawanya Wilaya hii kuwa Wilaya tatu kama ilivyopendekezwa awali.

Pili, kwa kuwa tayari Serikali imekubali kuanzisha Halmashauri tatu za Msalala, Ushetu na Kahama mjini kwa kuigawanya Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, tunaomba iruhusu Halmashauri hizo zote kuanza kazi mwaka huu wa fedha 2012/2013 badala ya kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Kahama pekee na kuziacha zingine mbili za Msalala na Ushetu zifuate baadaye.

Tatu, kwa kuwa Kahama sasa tayari kuna Halmashauri tatu japo mbili za Ushetu na Msalala hazijaanza, lakini Halmashauri ya Mji wa Kahama itaanza Julai Mosi, 2012, tunaomba Serikali, kupitia Tume ya Uchaguzi iruhusu kuanzisha Jimbo jipya la Uchaguzi la Kahama Mjini,kwani kwa muundo wa sasa, Wabunge wawili wa Msalala na Kahama wanahudumu Halmashauri mbili kila mmoja.

Nne, kwa kuwa mtandao wa barabara za Wilaya ya Kahama unaotambulika TAMISEMI ni mdogo sana, yaani kama kilomita 460 pekee wakati mtandao halisi ni zaidi ya kilomita 1600, tunaiomba TAMISEMI ifanye utambuzi mpya wa Barabara za Wilaya na hivyo kuongeza bajeti inayohudumia barabara za Wilaya Kahama.

Mheshimiwa Spika, baada ya maombi hayo ya Wanamsalala kwa TAMISEMI, sasa naomba kufikisha maombi mengine ya Wanashinyanga na Wanamsalala yanayohusu Wizara zingine na Serikali kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kuna *contradiction* kubwa sana ya utajiri wa mkoa na maendeleo katika Mkoa. Kwa taarifa tu Mkoa wa Shinyanga una sifa zifuatazo:-

(1) Una idadi kubwa ya wananchi kuliko mkoa mwingine wowote. Watu ni nguvu kazi, ambayo ingekuwa *productive* kama wanavyoitumia Wachina, Shinyanga ingekuwa na utajiri mkubwa wa kipato kwa wananchi wake;

(2) Mkoa unaongoza kwa uzalishaji wa madini ya almasi na dhahabu;

(3) Mkoa unaongoza kwa uzalishaji wa pamba;

(4) Mkoa unaongoza kwa idadi kubwa ya mifugo; na

(5) Ni miongoni mwa Mikoa mitatu inayozalisha tumbaku kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa zote hizo, Mkoa una sifa mbaya zifuatazo:-

(1) Mkoa unaongoza kwa mauaji ya *Albino*;

(2) Mkoa na Kanda inayoongoza kwa mauaji ya vikongwe kwa imani za ushirikina.

(3) Mkoa umekuwa wa mwisho mtihani wa darasa la saba miaka mitano mfululizo.

(4) Mkoa unaongoza kwa uwiano mbaya kati ya idadi ya shule za msingi na shule za sekondari.

(5) Mkoa unaongoza kwa uwiano mbaya kati ya idadi ya walimu na wanafunzi.

(6) Mkoa unaongoza kwa uwiano mbaya kati ya idadi ya shule za *O level* na *A level*.

(7) Mkoa unaongoza kwa kuwa na uwiano mbaya kati ya idadi ya shule na idadi ya shule za bweni.

(8) Mkoa unaongoza kwa kuwa na uwiano mbaya kati ya idadi ya shule za sekondari na shule za sekondari zenye umeme.

(9) Mkoa unaongoza kwa kupata njaa na kuhitaji msaada wa chakula kila mwaka.

(10) Mkoa unaongoza kwa kuzalisha wakimbizi wa ndani kwa jina la wafugaji.

(11) Kutokana na ukweli huo, it is no wonder kwamba mkoa unaongoza kwa kuwa na uwiano mbaya kati ya idadi ya watu na idadi ya viongozi kwenye nafasi za maamuzi za kisera na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hali hii haifai na haipaswi kuachwa iendelee. Naomba Serikali, kuanzia bajeti hii, ianze kujibu hii human *development paradox in* Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iujengee uwezo Mkoa wa kunufaika na rasilimali zake, yaani watu, mifugo, mazao, madini na kadhalika kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, elimu, kwa kuwa msingi wa umaskini wa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ni ukosefu wa elimu, Serikali iweke msukumo katika elimu kwa Mkoa wa Shinyanga kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kwa kutoa fedha zote za chenji ya rada kuendeleza elimu Shinyanga kwa kukamilisha majengo ya nyumba za walimu, mabweni, umeme, vitabu na maabara. Kwa mfano, Jimbo la Msalala pekee lina maboma 200 ya nyumba za walimu na maboma 250 ya vyumba vya madarasa toka 2004 wakati wa mradi wa MMEM! Maboma haya hivi sasa

yanabomoka na wananchi wamegoma kuchangia miradi mingine mipya ya elimu kwa kudai kwamba nguvu zao zilizotumika kujenga maboma hayo zinapotea bure bila Serikali kukamilisha miradi hiyo.

(b) Kuongeza bajeti ya elimu kwa Mkoa wa Shinyanga kwa kuhakikisha ahadi ya kujenga *VETA* kila Wilaya, hasa Kahama ambayo ina migodi miwili mikubwa ya Buzwagi na Bulyanhulu, lakini wananchi wake hasa vijana hawapati kazi kwa kukosa utalaam na ufundi.

Pili ni madini:-

(a) Mikataba ya Madini *(MDA)* iwekwe wazi na zipitiwe upya ili kama Taifa tunufaike. Mikataba hii imekuwa ikilalamikiwa sana.

(b) Serikali iruhusu Mkoa kunufaika na rasilimali zake za madini kwa kukubali mapendekezo ya Tume ya Bomani ya kugawa mrahaba kati ya Serikali Kuu na Wilaya ulipo mgodi kwa uwiano wa 60 kwa 40 kama ilivyotoa kipaumbele na ilivyoruhusu wananchi wa Lindi na Mtwara kupatiwa umeme wa gesi kwanza kabla ya wengine.

(c) Halmashauri ziruhusiwe kutoza *service levy* toka migodini kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Msimamo huu wa kutoruhusu *Service levy* kutozwa migodini

umeipotezea Kahama zaidi ya US$ 8,000,000 tokea mgodi wa Bulyanhulu ulipoanza uzalishaji rasmi mwaka 2001 na US $ 1,200,000 tokea mgodi wa Buzwagi ulipoanza uzalishaji mwaka 2008. Kwa wastani, kwa Kahama kulipwa US $ 400,000 tu kwa mwaka kutoka migodi hii miwili kama *consolidated local levies* badala ya *service levy* ambayo ni *0.3 percent of gross turnover*, Kahama inapunjwa zaidi ya US$ 2,100,000. Aidha, kwa kuwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 imeruhusu Halmashauri kutoza *service levy* toka 2010, Serikali inaombwa iruhusu Kahama kutoza ushuru huo *retrospectively* na hivyo ipatiwe chenji yake yaani US$ 4.2 m za miaka miwili toka 2010.

(d) Serikali iendelee na juhudi za kutatua migogoro kati ya wananchi na wawekezaji wanaovuna rasilimali za Shinyanga hasa madini.

(e) Naomba Serikali ilipatie ufumbuzi tatizo sugu la wachimbaji wadogo kukosa maeneo ya kufanyia kazi.

(f) Serikali kwa kushirikiana na mgodi wa Bulyanhulu imalize mgogoro wa fidia ya wananchi waliohamishwa kupisha mgodi wa Bulyanhulu mwaka 1996 kwa kuwalipa wadai.

Tatu ni kilimo, kwa kuwa Shinyanga inapata mvua za kutosha lakini kwa muda mfupi, Serikali isaidie

kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Mabonde ya Chela, Ntobo, Bulige, Kabondo na Ngogwa (Jimbo la Msalala) na Mwakitolyo na Salawe (Jimbo la Solwa) yanafaa kwa kilimo cha mpunga na yanaweza kulisha Mkoa mzima wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mtemi Nkumbi, la kupanua *scheme* ya umwagiliaji ya Chela litekelezwe sasa. Ni aibu kwa Shinyanga kutokuwa na *scheme* hata moja ya umwagiliaji yenye kufikia shilingi bilioni moja. Aidha, ni aibu kwa kuufanya Mkoa wa Shinyanga kuwa *permanent food dependent*. Nguvu kazi kubwa iliyoko Shinyanga inapotea bure na hii ni hasara kwa Taifa.

Nne ni viwanda, Serikali ianzishe viwanda vya kuongeza thamani kwa mazao yanayozalishwa Shinyanga hasa pamba na mifugo. Hivyo, Serikali ianzishe au iwezeshe kuanzishwa Viwanda vya Nguo na Nyama shinyanga. Si haki kwa wafugaji wa Shinyanga kuendelea kutangatanga na mifugo yao mingi kwa kukosa malisho bila kuwasaidia kupata soko la uhakika la mifugo yao. Ni aibu kwa zao la pamba kuendelea kuwa zao la wafanyabiashara kutajirika huku bei ikiporomoka kila mwaka. Tunaomba Viwanda vya Nguo na Mafuta ya Pamba Shinyanga.

Tano ni miundombinu na maji; Serikali ianze kutekeleza miradi mikubwa ya miundombinu ya maji, umeme na barabara ili kuchochea maendeleo Shinyanga kwa kutekeleza kwa kipaumbele miradi ifuatayo:-

(i) Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kwenda Kagongwa na Isaka na vijiji vitakavyopitiwa na bomba hilo vya Mondo, Penzi, Banhi, Mwalugulu, Gembe, Sungamile, Kishima, Kagongwa, Iponya, Isagehe, Malenge, Sangilwa, Mashigini, Mwakata, Itogwanholo, Isaka Stesheni na Ntungulu uanze mwaka huu;

(ii) Ahadi ya kuwapatia maji wananchi waishio jirani na bomba kuu la maji toka Ziwa Victoria, kwa umbali usiozidi kilomita 12, Vijiji vya Kabondo, Mwanase, Magobeko, Izuga, Matinje, Nduku, Busangi, Mhama, Bulige na Butegwa itekelezwe mwaka huu;

(iii) Mradi wa ujenzi wa barabara ya Lami kuunganisha Kahama na Geita uanze mwaka huu. Nasikia Mgodi wa Geita wamekubali kugharamia ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami upande wa Geita. Naomba Serikali izungumze na kukubaliana na *ABG* ili nao wagharimie ujenzi wa barabara hiyo upande wa Kahama. Kubalianeni mtakatana kwenye kodi na mrabaha siku za usoni;

(iv) Miradi ya Umeme Vijijini, ambayo maombi yalishapelekwa *REA* toka 2010 itekelezwe. Miradi iliyoombewa kwa Jimbo la Msalala ni kupeleka umeme vijiji vya Busangi, Nyamigege, Nyambura, Ngogwa, Ngaya, Bulige, Chela na Ntobo; na

(v) Mradi wa Umeme kwenda Bukombe kupitia Vijiji vya Lunguya, Shilela, Ikinda, Nyikoboko

na Segese vilivyoko Jimbo la Msalala nao uanze mwaka huu maana umeahidiwa toka 2004 (enzi za Awamu ya Tatu).

Mhe Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana tulijitahidi sana kutoa nafasi kadiri iwezekanavyo kwa wale ambao walikuwa hawajachangia hata mara moja. Waliochangia mara mbili hakuna hata mtu mmoja aliyepata nafasi. Walibaki wachache, lakini mkumbuke kwamba, tumeanza kujadili hoja kuanzia Jumatatu mpaka jana. Sasa tukisema tuendelee kujadili wenyewe tutajijibu wenyewe. Tulifikiri kwamba, leo tuanze na Mawaziri angalau ku-*clear* sehemu mbalimbali ambazo walifikiri kwamba wangejibu, tunawapa muda kidogo halafu baadaye tutaendelea. Waziri Mkuu mwenyewe atajibu saa za jioni.

Kwa hiyo, kwa sababu hiyo basi, nitaanza na Naibu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, atafuatiwa na Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Prof. Muhongo, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa fursa hii uliyonipa ili niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri. Pamoja naye niwapongeze sana Waheshimiwa

Mawaziri wa Nchi na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kazi nzuri kabisa ambayo wamekuwa wakiifanya kutumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja kadhaa ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge, zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Baadhi ya hoja hizo tutazijibu leo lakini nyingine tutajibu mwezi ujao wakati wa kuwasilisha Hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze na hoja ya Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, ambaye alizungumzia suala la ardhi ya wananchi kule Rufiji kwamba imechukuliwa na *RUBADA* na kugawiwa kwa wawekezaji. Tumefuatilia suala hili na kubaini kwamba ni kweli *RUBADA* iliandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika vijiji kadhaa huko Rufiji. Ilipowasilisha taarifa hizo kwa Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi, Tume ilionelea ni vyema kwanza ihakiki upya kabla ya kuidhinisha mpango ulioandaliwa na *RUBADA*. Kwa hiyo, Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi bado inaendelea na zoezi hilo la kuhakiki mpango huo na baada ya kukamilika ndipo ugawaji ambao utakuwa umefanyika utathibitishwa au hapana.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, kuhusiana na utoaji wa hati miliki za kimila katika Wilaya ya Chunya. Hoja ilikuwa kwamba, kutokana na kutokuwepo kwa Afisa Ardhi Mteule, imesababisha Wilaya hiyo kushindwa

kutoa hati miliki za kimila na hivyo kuathiri wananchi kwa kutokuwa na miliki juu ya ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, nilipenda niseme kwamba, taarifa zilizopo zinaonesha kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya iliwasilisha mapendekezo ya kuteuliwa Afisa Ardhi Mteule lakini baada ya uhakiki wa taarifa za aliyependekezwa, ilionekana kwamba hajakidhi vigezo vinavyotakiwa. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya imeelekezwa kwamba, iwasilishe mapendekezo mengine ili Afisa huyo aweze kuteuliwa. Ningemwomba sana Mheshimiwa Mbunge atusaidie kuhimiza Halmashauri kwamba, iharakishe kuwasilisha mapendekezo hayo ili uteuzi uweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, tunayo hoja ya Mheshimiwa Zainab Kawawa, tunamshukuru sana kwa ushauri aliotupa ambapo alishauri kuwa hati miliki za kimila zitambuliwe na kutumika kuthamini mikopo. Hoja hii pia imechangiwa na Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Shabiby na tungependa kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, mashauri yanayoendelea baina ya Wizara ya Fedha na Wizara yangu ya namna ya kuhamasisha na kuhimiza Benki mbalimbali zitambue hadhi ya hati miliki za kimila na hivyo kuweza kuzikubali kama dhamana kwa mikopo itakayotolewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida jambo lolote linapoanza watu huwa na wasiwasi na ndivyo ilivyo kwa vyombo vya fedha kwamba baadhi bado vina wasiwasi juu ya hati miliki za kimila. Ningependa nitumie fursa hii kuwahakikishia wamiliki wote wa Benki

kwamba, hati miliki za kimila zinatolewa kwa Mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Namba 5) ya Mwaka 1999 na zina hadhi sawa na hati inayotolewa kwa ardhi ya ujumla, yaani ardhi ya kawaida inayotolewa chini ya Sheria Namba 4 ya Mwaka 1999. Zaidi sana ningependa kuwahakikishia kwamba, hati miliki za kimila zina hadhi zaidi kwa sababu yenyewe haina ukomo. Ukipewa haina kusema ikifika miaka 99 ardhi ile inarudi kwa Serikali, hapana ukishamilikishwa ni ya kwako. Sana sana kwa mujibu wa Sheria na Sera inaelekezwa kwamba, ardhi iliyomilikishwa kwa mujibu wa Sheria hiyo kwa maana ya hati miliki za kimila, haitauzwa kwa wageni. Kwa hiyo, ardhi ile inakuwa salama zaidi kuliko hata ardhi ya kawaida ambayo imemilikishwa kupitia Sheria Namba 4 ya Mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, lipo suala lililoulizwa na Wabunge wa Dar es Salaam nalo linahusiana na mustakabali wa Mji Mpya wa Kigamboni na Wakazi wengine wa Dar es Salaam, ambao maeneo yao yamewekwa katika mpango wa kuendelezwa upya. Hili ni pamoja na eneo la Kurasini. Ningependa kueleza ifuatavyo:-

Kwamba, Serikali imeshughulikia kwa kiasi kikubwa sana kero za Wananchi wa Dar es Salaam. Nikitoa tu mifano jinsi tulivyoshughulikia, Serikali hivi sasa katika Bajeti hii ambayo itaanza kutumika tarehe Mosi Julai, imetenga fedha za kutosha kulipa fidia kwa Wananchi wa Kurasini ambao eneo lao litachukuliwa kwa ajili ya kuwekeza chini ya usimamizi wa *EPZ*. *(Makofi)*

Vile vile kwa upande wa Kigamboni, kabla sijatoka Kurasini kuna eneo ambalo tunajenga Daraja la Kigamboni, tayari uthamini umekwishafanyika na Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* wanakamilisha taratibu za kuwalipa wahusika fidia katika eneo hilo. *(Makofi)*

Upande wa Kigamboni, ningependa kuwajulisha Wabunge wenzangu wa Dar es Salaam na Wananchi wa Kigamboni kwa ujumla kwamba, Serikali imekwishachukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi ambao watatakiwa kupisha ujenzi wa miundombinu na huduma za jamii. Vile vile Serikali imeidhinisha uanzishwaji wa Mamlaka ya Kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni. Tunatarajia kwamba, taratibu zitakapokuwa zimekamilika, mapema mwaka huu wa fedha unaoanza kwa maana ya mwezi Julai, Agosti na baada ya Bodi ya Chombo hicho kuteuliwa, basi Chombo hicho kitaanza kazi na taratibu zote za maendelezo ya Mji huo Mpya zitasimamiwa na Wakala huyo. (*Makofi*)

Ningependa pia kusema kwamba, moja ya kero ambazo zilikuwepo kwa mfano, kwa upande wa Wananchi wa Kurasini na maeneo mengine ya Dar es Salaam, ilikuwa ni malalamiko juu ya fidia kuwa ndogo. Serikali kupitia Wizara imehuisha viwango vya fidia ambavyo mara vitakapokuwa vimeidhinishwa na Serikali vitaanza kutumika. Tunatarajia kwamba, wale ambao watalipwa fidia, sasa viwango vipya vitatumika baada ya Serikali kuidhinisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda unanikimbia, kuna suala ambalo Mheshimiwa Halima Mdee alilizungumzia kuhusiana na kodi ya ardhi inayotozwa kwa mashamba kwamba ni shilingi 200. Ningependa kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, viwango hivi vimehuishwa na kuanzia mwaka ujao wa fedha viwango vipya ambavyo tayari vimewasilishwa kwa Waziri wa Fedha ili aridhie, vitaanza kutumika na kwa sababu hiyo lile suala la labda pengine viwango vidogo vya ushuru huo kuwa ni kichocheo cha watu kujitwalia ardhi na kuhodhi, pengine itasaidia kupunguza. Viwango vitakavyowekwa havitakuwa vikubwa sana vya kuumiza wakulima wa kawaida hapana.

Mheshimiwa Spika, kuna alilolizungumzia Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, ningependa kumshukuru sana kwa mchango wake mkubwa kwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa, kwa kujenga nyumba kwa ajili ya Watanzania. Tunamshukuru sana yeye na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa ushauri na maelekezo mema wanayotoa kwa Shirika hilo na Sekta ya Ardhi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, ambayo alisema kwamba lipo tatizo la kuingiliana baina ya Hifadhi na vijiji kadhaa kule Mpanda, ambavyo alivitaja Vijiji vya Kasekese, Kapalamsengo, Sebwesa, Kungwi, Vikonga na Kaseganyama kwamba, maeneo hayo yameingiliana

na kumekuwepo na mgogoro baina ya Hifadhi na Wananchi wa Vijiji hivyo. Ningependa kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Hifadhi zote za Taifa huanzishwa kwa mujibu wa sheria na zinapoanzishwa Taarifa ya Serikali (*Government Notice),* inayotoa taarifa ya kuanzishwa kwa Hifadhi yoyote inayohusika, huainisha mipaka ya Hifadhi hiyo. Kwa msingi huo, wito wangu ni kwamba Hifadhi za Taifa, yaani Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA),* ishirikiane na Serikali za Halmashauri zinazohusika kuhakikisha kwamba, wanahakiki mipaka hiyo na kuweka alama ili kuepuka migogoro kwa siku zijazo.

Wizara yangu itakuwa tayari kama Mpimaji Mkuu wa Ardhi hapa nchini kutoa msaada wakati wowote utakapokuwa umehitajika.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa Kalogeris, Mbunge wa Morogoro kwamba, ujenzi wa Bwawa la Kidunda umechelewa sana kutokana na Mthamini Mkuu wa Serikali kuchelewesha kuidhinisha na kurejesha taarifa ya uthamini iliyofanywa katika eneo hilo. Ningependa kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli uthamini umefanyika na baada ya kukamilika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na inaonesha kwamba wananchi wapatao 300 wa eneo hilo wataathirika lakini taarifa ya uthamini bado haijakamilika na haijawasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali. Hivyo, leo nimeagiza kwamba, Mthamini wa Mji wa Manispaa ya Morogoro, Bwana Lioba, akamilishe taarifa hiyo mapema iwezekanavyo na kuwasilisha kwa Mthamini Mkuu wa Serikali iweze

kuhakikiwa na baadaye kuidhinishwa na hatua za kulipa fidia ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ya Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, nimekwishalielezea hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hoja nyingine tutajibu baadaye, naomba nikushukuru sana na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mtajibu tena Wizara zenu zitakaposoma hotuba.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kufurahia michango mingi ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge; mengi sana tumeyazingatia na majibu mengi mtayapata kwenye Hotuba yangu ya tarehe 24 wakati nawasilisha hapa.

Mheshimiwa Spika, labda niongee machache ni kwamba, wengi sana wameongelea suala la gesi, imeonekana kwamba kuna wasiwasi huenda tutapoteza hatujajitayarisha. Kama nilivyoeleza hapo mwanzoni ni kwamba, Sera inatengenezwa na Watanzania na kama nilivyotoa ahadi itajadiliwa kwa undani sana na Watanzania na vile vile tutakwenda mpaka Lindi na Mtwara, wakazi wa kule na wao waweze kuchangia. *(Makofi)*

Mambo yakienda vizuri, kabla ya mwisho wa mwaka huenda tutaleta Muswada hapa Bungeni ili tuweze kuhakikisha tunapata faida kutokana na gesi

yetu hii. Mengi sana kuhusiana na gesi nitaeleza tarehe 24.

Mheshimiwa Spika, labda kitu cha muhimu sana cha kuwaeleza ni kuhusiana na tarakimu ambazo zilikuwa zinatolewa, sasa ni vizuri niwapatie tarakimu ambazo ni za uhakika zaidi. Ni kwamba gesi ambayo tumeipata hadi leo ni ujazo wa futi trilioni 26.99, yaani *26.99 trillion cubic feet.* Sasa kuna *formula* ya kutumia kutoa gesi kwenda kwenye mapipa ya mafuta, ukitumia hiyo ambayo ni ya Kimataifa inaonesha kwamba, hiyo gesi ya kiwango hicho ni sawa sawa na mapipa ya mafuta bilioni 4.86. Sasa ukichukulia bei ya pipa moja kwa sasa ni dola 86, ninamaanisha gesi yetu ina thamani ya Dola za Marekani bilioni 417.81, ambayo ukichukulia dola moja sawa na shilingi 1500 ni trilioni 626.71. Hiyo ni thamani kabla hujatoa fedha walizozitumia kutafuta hiyo gesi na baadaye kuja kuizalisha. Mpaka hivi sasa mitetemo imefikia bilioni 637.79 ya hayo makampuni yaliyotumia. Uchimbaji wa visima ambavyo niliwaeleza kisima kimoja kinatumia fedha nyingi sana ni kati ya Dola za Marekani 100 mpaka 150. Sasa hadi kufika leo hii wametumia Dola za Marekani 840. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hapo nitakuja kuwaeleza faida nyingi sana ambazo tutazipata kwenye Hotuba yangu ya tarehe 24.

Kingine kilichoongelewa nadhani kidogo kwa hisia kali sana ni kuhusu Kiwira na Kabulo. Kwanza kabisa, ukiwa unajadili mambo ya Kiwira na Kabulo ni vizuri ukatenganisha, hii ni Migodi ambayo ipo mbalimbali, ni Migodi miwili tofauti. Ukiwa hapa niliposimama kwamba ndiyo Kiwira ambayo inakisiwa kuwa na tani

kama 35.4 milioni za makaa ya mawe, kilomita nane Kusini ya Kiwira ndiyo upo Mgodi wa Kabulo ambao nadhani ndiyo mkubwa una tani milioni 50.94. Kulia kwake ndiyo kuna Mgodi wa Ilima ambao wenyewe ni mdogo una tani 280,000. Kwa hiyo, ukilichukua eneo lote hilo hapo, lina makaa ya mawe mengi sana. Sasa *STAMICO* ilikuwa ndiyo inashughulika na Kiwira hata mimi nilipokuwa Mwenyekiti wa Bodi kabla ya mwaka 2005, umeme uliokuwa unazalishwa ulikuwa *megawatt* kumi wakati huo, ukashuka mpaka tano, ikafika wakati *TANESCO* ikasema haiwezi kununua umeme wa Kiwira kwa sababu in mwingi sana.

Kwa hiyo, mengi yamefanyika, baadaye *STAMICO* ikashindwa kuiendesha Kiwira, halafu Serikali ikauza huo Mgodi kwa *Tanpower Resources Limited* mwaka 2005 na mauzo ilikuwa ni kwamba, hii Kampuni ya Tanpower ichukue asilimia 70 na Serikali ibaki na asilimia 30. Mengi yalifanyika hapo ambayo vile vile nitawaeleza kwa undani sana siku hiyo ya tarehe 24. Ukweli ni kwamba, hata hiyo kampuni ilishindwa kuendesha Kiwira na cha kuongezea ni kwamba, ilikopa fedha kuendeshea Kiwira na mthamini wa mkopo huo ilikuwa ni Serikali na kufikia Novemba, 2011, mkopo na riba yake ni kama ifuatavyo: Mkopo wa kutoka *NSSF* ni bilioni 16.5, mkopo kutoka *PSPF* ni bilioni 11.09 na mkopo kutoka *CRDB* ni bilioni 4.65. Kwa hiyo, jumla ya mkopo hadi kufikia Novemba 2011 ni bilioni 32.24.

Sasa iwapo Serikali inataka kuuchukua huo Mgodi, inabidi ichukue na madeni. Vile vile nitakuja kuwaeleza kwa nini tumetenga shilingi bilioni 40 kwa ajili ya

kufanya Kiwira iwe mikononi mwa Serikali moja kwa moja. Mnaweza kuona tu mkopo wa Kiwira kutoka kwenye Mabenki upo kwenye kiwango hicho cha bilioni 32.24. Hiyo Kiwira ikaja kuuzwa na huyu *Tanpower* akawauzia Kampuni inayoitwa *Tanzacoal East Africa Mining Company Limited* ambayo ni Kampuni Tanzu ya *Intra-Energy* ambayo vile vile inaendesha ile ya Ngaka. Hapo napo mengi nitawapatia siku ya tarehe 24.

Mheshimiwa Spika, sasa kutokana na hivyo, *NSSF* iliomba kuendesha huo Mgodi wa Kiwira kwa sababu yenyewe ndiyo imetoa mkopo mkubwa, ikasema iuziwe kwa dola moja kusudi walipe wadeni wale wengine ichukue huo mkopo. Kwa hiyo, ikaitafuta kampuni moja inayoitwa *City Energy and Infrastructures Limited* ambayo Makao yake Makuu yako Dubai na India, lakini wataalamu wa kila upande walipoenda kuihakiki hii kampuni kati ya tarehe 18 na 27 Septemba mwaka jana, ikakutwa kwamba hii kampuni haikuwa *registered* popote pale, baadae ikaja kuwa *registerd.* Kwa hiyo, ndugu zangu nataka kuwaeleza unapomsikia mtu anaongea Kiwira lazima ujue anaongea akiwa upande upi, mambo ni mengi sana ya Kiwira.

Niwaambie tu kwamba, nimeagiza Wadau wote wa Kiwira, tutakaa kikao cha pamoja hivi karibuni kwa siku nne, tano, zijazo, kila mtu aje na makabrasha yake tongee kwa uwazi kabisa tujue nani ni nani. Nimeomba tuifanye hiyo kabla ya Hotuba yangu ya tarehe 24 kusudi nikija kuwaeleza hapa, niwaeleze vitu vya

uhakika siyo vya kwenda mbele, nyuma, mbele, nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wameongelea Mgodi wa Kabulo kwa nguvu sana ambao upo Wilaya ya Ileje. Nimewaambia ni kilomita nane tu Kusini mwa Mgodi wa Kiwira na katikati kuna Mto, kwa hiyo, ukitaka kuwa mzalishaji mkubwa ukiwa una *plan* nzuri lazima ununue zote za Kiwira, Kabulo na Ilima. Hizo ni mbinu za uwekezaji. Hii Kabulo nayo ilikuwa ya *STAMICO,* ambayo nayo baadaye ilipewa hiyo Kampuni ya *Tanpower Resources* ya Tanzania ambayo nayo baadaye ikaja kuuza, bei yake sijaielewa sawasawa, vile vile nitawaeleza kwa undani tarehe 24 mambo yalivyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo hali ya Kiwira na Kabulo; kuna mambo mengi sana, nawahakikishia kwamba nitakapokuja hapa tarehe 24 tutakuwa na mwafaka wa kusonga mbele na huu mjadala, sasa tutakuwa tunaongelea uzalishaji wa makaa ya mawe. Isipokuwa nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wengine popote wanaponisikia, kampuni mnazozileta kwamba ziwe ubia na Mashirika yetu ya Umma, msilete kampuni ambazo siyo za uhakika kwa sababu hazitapita wala hazitaruhusiwa kufanya biashara katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee umeme vijijini. Wengi sana wameongelea umeme vijijini tunafurahi, lakini nataka kuwahakikishia kwamba, toka *REA* ianze mwaka 2007, imefanya mambo mengi sana na katika Hotuba yangu vile vile nitawagawia Ramani ya

Tanzania ikionesha wapi umeme umewekwa na *REA.* Vile vile mtapata orodha ya Vijiji vya Mikoa na mkipenda mtapata majina ya vijiji ambapo *REA* imeweka umeme. Kwa hiyo, tutakuwa tunaongea vitu vya uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TANESCO*, nadhani sasa hivi mnaona kidogo tunaendelea vizuri, umeme haukatikikatiki kama hapo awali na kama nilivyowaeleza, ikiwa tuna wataalamu na zaidi ya miaka miatano, kumi tunaingia kwenye mgao kila mwaka, inaonesha ubunifu sasa wa hao ndugu zetu kwenye *Management* labda kidogo umefikia kikomo. Nataka kuwahakikishia kwamba, umeme hautakatika au mgao hautatokea, tutajitahidi kwa njia zote hizo. Mmeona waliokuwa hawajafungiwa umeme, wamefungiwa na ile tarehe ya mwisho tuliyoiweka kwamba *TANESCO* lazima iwe imewafungia siyo ya mzaha, kama hamjafungiwa tuelezeni.

Mwisho kabisa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hiyo ndiyo kengele ya pili.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, haya. Mimi nawaombeni wote tuunge hoja mkono. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Viongozi wote, kwa hotuba nzuri waliyotuwekea Mezani na moja kwa moja naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii kutoa ufafanuzi kidogo kwa baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza kwenye Sekta ya Kilimo. Kwa kuwa hoja zilikuwa nyingi kweli kweli, mimi nimeona afadhali niziweke kwenye kongani kwa sababu hata nikisema nimtaje mmoja baada ya mwingine sitaweza.

Naomba nianze na suala la ruzuku ya pembejeo kuwahishwa kwa wakulima. Kwanza, naomba niseme hakuna biashara inayofanywa na Serikali ya kupeleka pembejeo. Pembejeo zote zinapelekwa na wafanyabiashara isipokuwa ndani ya pembejeo zile kama mbolea ambazo wafanyabiashara wanakuwa wamepeleka, ndimo humo kunakuwa na pembejeo ambazo zinapata ruzuku. Kwa hiyo, ile dhana ya kwamba Serikali ndiyo inapeleka zile pembejeo, nilitaka kwanza niliweke sahihi hili. Tunachokifanya sisi ambacho tunaweza tukaambiwa tumekichelewesha ni kupeleka *voucher* kwa wakulima kuzisambaza ili wale ambao wanapata fursa hiyo waweze kuzitumia. Kwa hiyo, kubwa hapa ni kuwahisha zile *voucher* za pembejeo. Sasa kumetokea matatizo mengi katika mfumo ambao tumeutumia msimu ulipita, lakini tumejitahidi kutafuta njia za kuwahisha *voucher* hizi na pembejeo ziwafikie wakulima. Mfumo mmoja ambao wengi wameupenda hasa Wakuu wa Mikoa

wanaosimamia zoezi hili ni wa kutumia Taasisi na Vikundi vya Ushirika kuweza kukopa kwenye Mabenki ili waweze kujipatia.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unatupa matatizo kidogo tu kwamba unahitaji maandalizi ya muda mrefu. Ili vikundi hivi viweze kukopa kwenye Benki, Mabenki yana masharti yake yanahitaji vikundi vilivyosajiliwa, vikundi vinavyokopesheka, vikundi vyenye *accounts* ambazo zimekaguliwa. Sasa utakuta vikundi vingi tulivyonavyo havina uwezo wa kukidhi matakwa haya ya Benki. Kwa hiyo, mfumo huu pamoja na uzuri wake, tumeona tutumie karibu mwaka mzima huu kuviandaa vikundi hivi ili msimu unaofuata viwe tayari. Kwa hiyo, kwa msimu huu tumeamua kwamba, tutatumia mfumo wa *voucher,* lakini tutauboresha kwa maana ya kwamba sasa hatutakuwa tena na mawakala ambao watateuliwa na Serikali au mawakala watakaoteuliwa na kabati zile. Mawakala watateuliwa moja kwa moja na makampuni ya mbolea, yaani kampuni zitakazopeleka pembejeo, zitapeleka pembejeo moja kwa moja mpaka Vijijini na ndizo zitakazohusika kuteua mawakala wake. *(Makofi)*

Sasa zipo faida ambazo tutazipata kwa kutumia utaratibu huu; kwanza, tutaondoa ule utaratibu ambao mawakala walikuwa wanaweza kuelewana na wakulima na wafanyabiashara wengine wakatuibia fedha, njia hiyo na fursa hiyo hawatakuwa nayo; pia tutapata fursa ya kuweza kuwahisha pembejeo; na zaidi ya hapo kwa kuwa tutatumia makampuni kama *TFC,* ubora wa pembejeo utakuwa mzuri maana itakuwa rahisi wao wenyewe watawajibika kwanza

kwa kufikisha mbolea ile, halafu pia watawajibika kwa ajili ya ubora wa pembejeo inayopelekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba hilo niliachie hapo, nije kwenye suala la Mbolea ya Minjingu. Kwa kweli suala hili pia limezungumziwa na sisi tunaona ipo haja kama tuna rasilimali ambayo iko hapa hapa kwetu Tanzania, basi Mbolea ya Minjingu tutaendelea kuitumia na kwa bahati nzuri tumeifanyia kazi. Hivi sasa mbolea ile tumeiboresha au wameiboresha, baada ya utafiti inatoa mbolea inayoitwa Minjingu Mazao. Mbolea hii ina thamani kabisa sawa na *DADP,* pamoja na kwamba viwango vya kutumia vinatofautiana. Kwa hiyo, tutakachofanya ni kusisitiza matumizi ya Mbolea hii ya Minjingu, lakini kwa kutumia utaratibu huo huo wa kuifikisha kwa wakulima niliyowaelezea hapo awali.

Mheshimiwa Spika, nilipenda pia nieleze kuhusu suala lingine ambalo tunataka kulishughulikia kwa bidii kabisa ni kuhakikisha kwamba tunahamasisha Sekta Binafasi ili zitujengee viwanda vya mbolea, viwanda vitakavyotumia gesi hii ambayo tunaizungumzia, viwanda ambavyo vitatumia hii *Minjingu Rock Phosphate* ambazo ndizo rasilimali tulizonazo hapa Tanzania. Kwa hiyo, siyo tu wawekezaji kutoka nje, Wizarani kwangu nimeanza mazungumzo na mifuko yenye fedha, sasa mazungumzo haya yanaratibiwa na Naibu Waziri, yeye ni mahiri kweli kweli katika eneo hili na Katibu Mkuu, kuangalia uwezekano wa kupata fedha na wafadhili wanaoweza kusaidia wawekezaji ambao wapo tayari kuwekeza katika Sekta hii ya Kilimo

hata hapa ndani. Kwa hiyo, mazungumzo hayo tumeanzisha na yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie changamoto za masoko. Wengi wamezizungumzia hususan Mheshimiwa Zambi. Baada ya hapo, naomba nizungumzie suala la korosho. Suala la korosho ni kama tunaelekea kulimaliza. Tulikuwa na tatizo la korosho zilizobaki Tunduru na Koreku kule *Coast Region* kama tani 13,000. Tatizo lililokuwepo huko lilikuwa siyo suala la kupata mnunuzi, sisi tumekubali sasa tumeamua kuweka ushindani. Kwa maana ya kwamba, waje wengine wanaoweza kuingia katika soko, kuongeza ushindani badala ya kuwa na ukiritimba wa wanunuzi wachache. Baada ya kufanya hivyo, korosho imenunuliwa kwa kiwango cha kutosha, isipokuwa hiyo iliyobaki Tunduru na Koreku ambayo ilikuwa takriban tani 13,000. Leo hii nimefuatilia, naomba niwataarifu Wakulima wa Korosho kwamba, suala hili lilikuwa na utata, utata ulikuwa huyu mnunuzi ambaye yuko tayari kuinunua, anachotaka yeye ni korosho apelekewe bandarini.

Suala lilikuwa utata wa kusafirisha kutoka kwenye maghala mpaka bandarini. Tumezungumza vizuri na Mwenyekiti wa Bodi, Mama Anna Abdalah, tumelifikisha mahali pazuri na hivi sasa nimemwita huyo mnunuzi mwakilishi alikuja juzi na amenihakikishia kwamba, tatizo lilikuwepo la kufungua *letter of credit* ili kumuwezesha mnunuzi huyu kuendelea, hilo sasa limekwisha. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba, tatizo hili litakuwa limepatiwa ufumbuzi ndani ya wiki hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la kahawa. Suala la kahawa nalo limeleta mazungumzo mengi hapa ndani, lakini sisi *bottom line* tunachokisema, tunataka kahawa isindikwe ili mkulima auze kahawa yenye thamani. *(Makofi)*

Sasa kwa kufanya hivyo, tunachohitaji ni kwamba, tuwe na wakulima wanaoweza kusindikiza wasindike, vikundi visindike, vyama vya ushirika visindike, lakini pia hata watu binafsi ambao wanaweza kusindika kama wana uwezo huo, basi tunataka nao waweze kusindika. Tunachokihitaji hapa ni kuweka mazingira ambayo huyu msindikaji mkubwa hatakuwa na nafasi ya kumnyonya mkulima, ampe bei nzuri na hasa kwa kuhakikisha kwamba kahawa ile imesindikwa. Kwa hiyo, tunachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, vikundi vyenye *CPUs,* zile mashine za kukoboa kahawa, vitaendelea kuimarishwa katika maeneo haya ili hatimaye mkulima huyu aweze kupata ubora wa kahawa unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kuacha kuzungumzia suala lililojitokeza kuhusu Bodi ya Kahawa kwa sababu limezua hisia kubwa sana. Naomba niseme kwamba uteuzi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA**: Hiyo ni kengele ya pili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika, ilikuwa ya kwanza.

**SPIKA**: Pole sana ni ya pili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kupata nafasi hii.

**SPIKA:** Huyu mtamwona tutampigia baada ya dakika tano tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia Hoja ya Waziri Mkuu, moja kwa moja nijielekeze katika hoja iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nayo ni hoja ya Kero za Muungano na kwamba, muda wote huu ni kero mbili tu ambazo zimepatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, tunapokaa Vikao vya SMZ na SMT, *reference* yetu kubwa ni hoja 13, kama zilivyoibuliwa na Tume ya Shellukindo Mwaka 1996. Katika kero hizi 13 ni kwamba, kero saba tayari tumeshazimaliza na siyo kero tena na kwa hiyo, tunafanyia kazi kero sita. Kuna kero ambazo zimejitokeza hapo katikati ikiwemo hii ya umeme, ambayo imejitokeza mwaka 2008, lakini pia kero ya Mfuko wa Jimbo. Kero hizi mbili nazo pia tumeshazifanyia kazi na kufanya kero zilizofanyiwa kazi

kuwa ni tisa ambazo utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu, uwezo wa Zanzibar kujinga na *Maritime Organisation* na kufanya biashara na meli za nje, mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada na mikopo ya kibajeti, masuala ya mikopo ya *IMF,* msamaha wa *Multilateral Debt Relief Initiative,* Zanzibar kukopa nje na ndani ya nchi, Miradi ya Maendeleo ya Zanzibar kupelekwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na uvuvi kwenye Ukanda wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, hayo yote tumeshayafanyia kazi na tumemaliza.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo yapo katika hatua mbalimbali ni Hadhi ya Zanzibar kushiriki katika mambo au Taasisi za Nje, Ushirikiano wa Kimataifa, ambao tayari mwongozo umeshawekwa, tunasubiri kikao cha SMT–SMZ kuuthibitisha na kuupa baraka uendelee kutumika. Suala lingine ni ajira katika Taasisi za Muungano, ambapo Mawaziri wa Sekta za Utumishi wa Umma wameshakaa, wameshakubaliana mambo kadhaa, tunasubiri Kikao kuthibitisha. Masuala ya mgawanyo wa mapato ya Benki Kuu na Hisa za Zanzibar katika Sarafu ya *East Africa* na suala la Ripoti ya *GFC.* Haya kama mlivyosikia, timu mpya iliyoingia Wizara ya Fedha itayafanyia kazi. Nami nina imani nao na ninaamini watayafanyia kazi kwa haraka ili tuondoe utata uliopo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kodi ya Wafanyakazi wa Taasisi za Muungano wanaofanyia kazi Zanzibar na kodi ya zuwio. Hili tunatarajia

tutakapopitisha *Miscellaneous Ammendments* na ile *Bill* ya Fedha, hili nalo tutakuwa tumelimaliza.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mafuta na gesi ambalo kama Waziri Mkuu alivyosema, Serikali upande huu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawana utata na hilo ila tunafuata *formalities* kulitoa kabisa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili. Hapa nataka ninukuu kauli ya Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya kwamba, hili nalo wanalifanyia kazi na litakwisha mara moja.

Mheshimiwa Spika, umenipa dakika tano, naomba kuunga mkono Hoja ya Waziri Mkuu na mengine nitajibu kwenye Hotuba yetu ya Bajeti. Asante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Nitumie pia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunirudisha kwenye nafasi ya awali ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Nami ninamuahidi kutumikia katika nafasi hii kadiri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha.

Mheshimiwa Spika, natumia pia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mizengo kayanza

Pinda, Waziri Mkuu, kwa uwezo mkubwa, busara za kutosha, kwa kuiongoza vizuri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na kwa ufanisi mkubwa zaidi. Pia, namshukuru sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge wa Mtwara, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa ushirikiano mzuri anaotupa kwa ajili ya kuimarisha uwajibikaji ndani ya (TAMISEMI), bila kumsahau Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, Naibu Waziri (TAMISEMI), kwa ushirikiano anaonipa wakati wote na ushauri na kuweza kufanya kazi zetu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Katibu Mkuu, Bwana Hussein Katanga na Naibu Makatibu Wakuu, Bwana Alfayo Kidata na Bwana Jumanne Sajin, Naibu Katibu Mkuu wa Elimu, kwa ushirikiano mkubwa wa kiutendaji wanaotupa. Kwa nafasi hii namshukuru pia Mama Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na Wajumbe wote wa Kamati hiie, kwa ushauri juu ya masuala mbalimbali ya elimu. Vilevile nawashukuru Watendaji na Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika kufanikisha kuiandaa bajeti hii na mambo mengine yote yanayotupelekea kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kusahau napenda pia kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Ruangwa, walionipigia kura na kuniamini, kwa ushirikiano wao mkubwa kabisa wanaonipa. Nami nataka kuwahakikishia bado niko imara, tutaendelea kuwa pamoja katika kujiletea maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ambazo zimejikita katika maeneo machache, pamoja na michango iliyokuwa mingi, kama ifuatavyo:-

La kwanza, naomba nizungumzie kidogo juu ya upungufu wa walimu katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mchakato wa ajira ili kuboresha upatikanaji wa walimu katika maeneo yetu. Nataka nitoe taarifa tu kwamba, kufikia Disemba 2011, tulikuwa na walimu wa shule za msingi 167,904, kati ya 214,468 wanaohitajika. Pia, tuna walimu 44,574 wa sekondari, kati ya walimu 81,800 wanaohitajika. Kufikia Januari au Februari mwaka huu, Serikali iliajiri walimu 24,427 ambao wamejigawa katika maeneo yafuatayo: Walimu wa elimu ya msingi 11,235 na walimu wa sekondari 13,192 ambapo wenye shahada walikuwa 7,189 na stashahada ni 6,003.

Mheshimiwa Spika, hawa wote wamesambazwa kwenye maeneo yetu na bado Serikali inao mchakato wa kutosha wa kuajiri walimu wengi zaidi ili kutosheleza mahitaji ya walimu kwenye maeneo yetu. Tukiongeza Walimu wa Vyuo ambao pia waliajiriwa chini ya Wizara ya Elimu na Shule za Mazoezi, wanafanya jumla ya walimu wote ambao wameajiriwa katika kipindi hiki kuwa 25,000.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tuna upungufu wa walimu wa shule za msingi kwenye TAMISEMI 33,636 na

upande wa Sekondari walimu 24,034. Kama Serikali, tutaendelea kuajiri msimu ujao walimu hawa, tunaamini ajira zao katika awamu mbili zijazo tunaweza tukawa tumefikia angalau asilimia 85 kupunguza upungufu wa walimu kwenye maeneo tuliyonayo kwenye shule zetu. Kwa hiyo, suala la upungufu wa walimu, tunaendelea kuliratibu vizuri na Serikali ipo imara katika uajiri tuweze kuongeza idadi ya walimu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo Waheshimiwa Wabunge wameonesha kwamba lina matatizo ni mkakati wa kuboresha miundombinu kwenye shule zetu za sekondari kwenye maeneo ya madarasa, nyumba, maabara, *hostels,* lakini pia hata matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kwamba, Serikali inaendelea kutenga fedha za uboreshaji wa miundombinu hiyo kwa ajili ya kuboresha shule zetu za msingi na sekondari. Kwa mfano, Mwaka wa Fedha 2011/2012, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), ilitenga na kutuma fedha kwenye Halmashauri zetu, shilingi bilioni 30 kwa ajili ya nyumba 614, madarasa 187, maabara 127, matundu ya vyoo 1,916 na kununua madawati kwenye shule zetu mbalimbali 185,218.

Mheshimiwa Spika, tulitenga shilingi bilioni 20.8 kwa ajili ya kukarabati shule kongwe ambazo sasa hivi zinaonekana zimechakaa miundombinu yake. Tulitenga shilingi bilioni 3.2 kati ya hizo ili pia kuweza kufanya kazi hiyo kwenye shule ambazo tumezigawia. Pia kujenga maabara nyingine kwenye Shule hizi za

Kata tulitenga shilingi bilioni tatu na kujenga *hostel* tulitenga shilingi bilioni 14.6. Huo ndiyo mkakati wa kuboresha miundombinu mbalimbali kwenye shule zetu. Hata hivyo, Mwaka huu wa Fedha, tumetenga jumla ya shilingi bilioni 56.3 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu mbalimbali katika shule 264 ili kukabili uchakavu, lakini pia upungufu wa miundombinu unaokabili kwenye Shule zetu za Kata.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, walijadili sana juu ya madai mbalimbali ya walimu, lakini pia suala la stahili mbalimbali za walimu. Serikali, inayo azma ya dhati na katika hili nataka niwaambie walimu kwamba, Serikali inayo azma ya dhati ya kuondokana na madeni ya walimu. Tunao utaratibu ambao tunautumia wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambao wakati wowote mwalimu anapokuwa na jambo lolote la kiutumishi, Mkurugenzi kwenye Mamalaka ile, huwa anaweza kuratibu malipo yake.

Tumeagiza kabisa kwamba, mwalimu anapopata shughuli yoyote ya kikazi, anapokwenda likizo, anapopata uhamisho, ahamishwe kukiwa kuna malipo ili kuondokana na madeni ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni uhakiki wa madeni pale yanapokuwa mengi. Kazi hii tumeshaifanya kipindi kilichopita mwaka jana, ambayo pia tumeendelea kuyalipa mpaka mwezi huu. Katika hili, ingawa watu wengi wanalalamikia kutokuwa na takwimu kamili, nataka nieleze hili ili watu wajue kwamba, uhakiki wa kipindi kilichopita, tulibaini kuna madeni ya shilingi bilioni 52. Bilioni 52 hizi ni zile za

Wizara ya Elimu na TAMISEMI. Bilioni 52 hizi zilikuwa zinalipa *arreas,* kwa maana ya maeneo ya mishahara, lakini na posho mbalimbali ambazo zilikuwa zimejitokeza kwa maana ya matibabu, masomo, likizo, uhamisho; hiyo nilikuwa na maana ya posho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), ilitengewa bilioni 44. Kati ya hizo, bilioni 19.2 zilitumika kulipa maeneo haya ya posho kama ambavyo nimeyaeleza na bilioni 25.6 ni yale ya *arreas* ambayo yanalipwa na Hazina moja kwa moja na yanatumwa kwenye mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, napenda niwape taarifa kwamba, malipo yote yanayotoka Hazina na yale yote ya TAMISEMI, mpaka tulipokutana na Kamati ya Huduma za Jamii, mwezi huu tarehe 12, nadhani tulikuwa tumeshalipa bilioni 17, zilikuwa zimebaki bilioni mbili na Halmashauri chache zilikuwa hazijaweza kulipa. Ahadi ya Halmashauri zile, kufikia kesho tarehe 30 Juni, 2012, watakuwa wameshakamilisha na taarifa tutazipata na tutakuja kuwahabarisha Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hizi *arreas* watu wa Hazina nao walituhakikishia kwa sababu wao ndiyo wanalipa moja kwa moja kwenye mishahara. Kwamba, ifikapo Juni 30, watakuwa wameshakamilisha. Kwa hiyo, ulipaji huu wa kawaida, ambao unashughulikiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, unaendelea vizuri. Pia kuna suala la mishahara ambayo walimu wengi wapya wamekuwa hawalipwi; lakini tumeeleza mara nyingi na Waziri wa

Utumishi, atakuja kueleza kwenye taarifa yake, jinsi ambavyo sasa tuna-*practice* ule utaratibu wa ulipaji kwa kutumia mtandao, ambao upo sasa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna suala la utofauti wa mishahara ambayo imezungumzwa mara nyingi. Ninamshukuru Naibu Waziri wa Elimu, aliwahi kueleza hapa kwamba, ipo *message* inazunguka nchini ambayo inapotosha walimu. Nami ninalirudia hili ili walimu wajue kwamba, ujumbe unaopita ni wa uwongo; unaoonesha kwamba, viwango vya kulipwa vya walimu na watumishi wengine, walimu wanalipwa chini kuliko watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie kwamba, kada ambayo inatuzidi kwa mshahara ni ya Afya peke yake. Sababu ya kutuzidi ni kwa *nature* ya kozi zenyewe, ile miaka ya kusoma kozi ndiyo inatofautisha hilo, lakini *risk* za mahali pa kazi hiyo ndiyo inasababisha kutuzidi. Mishahara halisi ni kama ifuatavyo: Wenye Elimu ya Cheti, *basic* yake ni shilingi 244,400/=, Afya wanaotuzidi ni shilingi 290,000/=, lakini Sekta nyingine kama Kilimo, Mifugo, Utawala na Uhasibu ni shilingi 221,000/=, utakuta wapo chini.

Mheshimiwa Spika, ngazi ya stashahada, mwalimu shilingi 325,700/=, Afya wanatuzidi kwa shilingi 472,000/=, lakini Sekta nyingine zote wanalipwa shilingi 300,800/=. Wakati mtu wa Shahada wa Ualimu anaanza na shilingi 469,200/=, wa Afya peke yake anatuzidi kwa shilingi 682,000/=, lakini kada nyingine zote hizi za kilimo, mifugo na nyingine ni shilingi 446,000/=, utakuta kwamba, zipo chini. Hii ndiyo taarifa

rasmi. Kwa hiyo, nawasihi walimu msikubaliane na *message* ile. Serikali inayo nia ya dhati kabisa ya kuboresha mishahara na hata Mheshimiwa Kiongozi wa Serikali, amewahi kutoa taarifa mara nyingi kwa walimu na amewahi kuzungumza na Chama cha Walimu juu ya nia ya Serikali kuboresha mishahara. Kwa hiyo, nawasihi endeleeni kufanya kazi yenu, Chama cha Walimu tutaendelea kuzungumza nao, kama kuna jambo litajitokeza tunaweza pia tukalifanyia kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda ni mfupi, naomba nimalizie kwa kueleza lile ambalo Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakililalamikia juu ya mfumo wa upelekaji wa fedha za elimu kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, utumaji wa fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni wa Kisheria. Tunajitahidi kuzipeleka kama inavyotakiwa zile za Mpango wa MMEM na za Mpango wa MMES ambazo tayari maeneo mengi huwa zinapelekwa na ukaguzi unafanyika na ufuatiliaji upo. Kwa hiyo, ninataka niwasihi Waheshimiwa Wabunge kwamba, utumaji wa fedha hizi kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, unaenda kama ambavyo tumejipangia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda hautoshi na bado Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), inaendelea na uboreshaji wa taaluma kwenye maeneo yetu kwa kupeleka vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ambavyo pia tunavitumia; na sasa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na *SIDA,* tumetenga shilingi bilioni 30 kwa

ajili ya kununua vitabu. Pia kwa taarifa ambazo nimezieleza hapa awali, ununuzi wa madawati, uboreshaji wa miundombinu; hii yote ni katika kufanya utoaji wa taaluma kuwa rahisi zaidi ili kumuwezesha mwalimu kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, nikiwa najua kwamba muda haunitoshi, naomba niseme kabisa kuwa naunga mkono hoja hii na ninamkaribisha Naibu Waziri mwenzangu, aweze kuendelea. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwepo hapa na afya njema. Zaidi, nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye kwa mara nyingine tena ameonesha imani kubwa kwangu na kunirejesha katika nafasi yangu hii ya Unaibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na kusema ahsante. Ninachoweza kufanya ni kujaribu kwa kadiri Mungu atakavonijalia, kuhakikisha kwamba, ninatekeleza majukumu ambayo amenikabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye ndiyo Kiongozi wetu wa Wizara na ndiye mwenye dhamana. Ninashukuru na ninajivuna moyoni kwamba, ninafanya kazi chini ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nasema ahsante kwa maelekezo yote ambayo amekuwa anatoa kwangu na ninataka nimthibitishie kwamba, bado nitaendelea kushirikiana na yeye kwa unyenyekevu mkubwa na kwa utiifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru pia dada yangu, Mheshimiwa Hawa Ghasia, ambaye tumekaa kwa muda mfupi sana tuliokaa naye, ametuelekeza vizuri, ametupa maelekezo mazuri na ushauri mzuri. Tunafanya kazi kwa uhuru kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nikuthibitishie kwamba, nitaendelea kusaidiana sana na ndugu yetu, dada yetu, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge wetu wa Mtwara Vijijini ili tuweze kuleta ufanisi katika Wizara yetu. Huyu aliyesimama hapa ninamwita pacha, ni pacha wangu; tunafanya nae kazi kwa karibu sana; Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Tunashirikiana vizuri na tunafanya kazi kwa karibu sana, wakati mwingine wala hatujui huu utaratibu wa *Local Government* na Elimu. Napenda kumshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wananchi wangu wa Jimbo la Siha, ambao ndiyo walionipa dhamana ya kuja mpaka hapa na kusimama na kuweza kuteuliwa kwa nafasi hii. Nataka niwaambie Wananchi wa Siha kwamba, nawapenda sana. Kila wakati moyo wangu na akili yangu, inawafikiria sana Wananchi wa Siha na wala wasiwe na wasiwasi, yale yote ambayo wanataka tuyafanye katika Jimbo letu la Siha, tutaendelea kuyafanya. Namshukuru mke wangu

Grace Mwanri na watoto wangu wote, ambao kwa muda wote wamekuwa wananivumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na wewe Mheshimwia Spika, usije ukasema mbona sikukutaja hapa, ahsante sana kwa namna unavyotuelekeza vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi naridhika tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sasa najua muda wangu utakuwa mfupi sana. Watu wamezungumza mambo mengi sana hapa. Nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, Waziri wangu atakuja kuzungumzia mambo makubwa. Mimi nitayasema yale ambayo tumekubaliana niyaseme, lakini hakuna jambo lolote ambalo mmelizungumza hapa ambalo hatutalichukua kwa uzito mkubwa na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tutajibu mambo machache sana hapa kama alivyosema Mheshimiwa Majaliwa, lakini mambo mengi sana tutakwenda kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, naomba niwaombe sana sana, wala tusivutane hapa kwa sababu sisi tunachohitaji ni hizi hela twende tukafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati aliposimama, Mheshimiwa Pindi Chana, moja ya mambo ambayo ameyazungumza hapa kwa uzito mkubwa ni kwamba, baadhi ya Halmashauri hazifanyi Vikao vyake vya Kisheria. Kamati inashauri kwamba,

jambo hili liangaliwe kwa makini ili Vikao vifanyike kwa wakati na Waheshimiwa walipwe haki zao kama inavyostahili na kwamba, kuna Chaguzi ndogondogo ambazo zimekuwa zinatokea lakini hazifanyiki.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwa kifupi tu hapa kwamba, kama mnavyokumbuka, mwaka jana ile *General Purpose Grant* ilikuwa imeondolewa na Serikali. Kama mlivyomsikia Mheshimiwa Waziri wangu aliposimama hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, *General Purpose Grant* imerudi kwenye bilioni 63. Hizi ndizo zinatusaidia kufanya shughuli zote hizi ambazo tunazizungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka nikithibitishie Kikao chako kwamba, baada ya kurudi hii *grant* sasa na hata zile fedha amezizungumzia, tuna uhakika vikao vyote vitafanyika kwa taratibu zilizowekwa. Kwa hiyo, hatuna tena tatizo la kusema watu watakwenda kwenye Mkutano wakakopwa vikao na kwamba hawatalipwa haki zao na anasisitiza pia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati kuwa elimu kwa ajili ya mafunzo ya Madiwani itolewe.

Mheshimiwa Spika, umetusikia tukizunguka nchi nzima, mwanzoni alianza Mheshimiwa Mkuchika ambaye yuko hapa, alianzisha mafunzo ya Madiwani yaliyofanyika Mtwara yalifunguliwa na mimi nilikwenda kukamilisha kule Korogwe na tunaendelea hivyo hivyo Madiwani wote wamepata mafunzo yale wamefanya kazi ile na bado tunaendelea na mchakato. Nilitaka nikuthibitishie kwamba, tutaendelea kufanya kazi hiyo kwa karibu sana, tunacho Chuo chetu cha Hombolo

pale tumezitaka Halmashauri zipeleke Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Watendaji wetu waende kule. Kwa hiyo, hili halina matatizo kabisa.

Kuna rai hapa kwamba, Kamati ya Fedha, Mipango, Uchumi na Utawala katika kila Halmashauri zijengewe uwezo ili kuweza kusimamia Miradi hii kwa ukamilifu; hilo tunalifanya katika Programu ambayo nimeizungumzia. Ipo rai pia inayosema kwamba, uandaliwe utaratibu utakaoziwezesha Kamati zote za Kudumu za Halmashauri kukagua Miradi mbadala ya kuitegemea Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala tu.

Naomba nifafanue kidogo hapa; kinachosemwa hapa ni kwamba, zipo Kamati tatu pale, kila Kamati iende kule kwa ajili ya kukagua Kamati zile zinapoundwa. Mwenyekiti wa kila Kamati aliyeko katika Halmashauri anaingia katika Kamati hii ya Fedha tuliyoizungumza hapa. Ndani yake Mwenyekiti wa Halmashauri anateua Madiwani wengine wawili ambao wanajiunga katika Kamati hii. Kamati hii inayozungumzwa hapa inakutana mara moja kila mwezi. Sasa kinachosemwa hapa ni kwamba, ruhusu sasa na zile Kamati nyingine nazo ziwe zinakagua Miradi kwa sababu hii ndiyo Kamati ambayo inaangalia mambo ya Miradi, kusimamia mambo ya *value for money* yote yanafanyika kule.

Mheshimiwa Spika, uwezo wetu kwa sasa hivi ni mdogo, ukiruhusu zile Kamati zote zifanye pale, ukasema watalipwa *allowances* na kila kitu, gharama zake ni kubwa sana. Tulichofanya kama TAMISEMI, tunaweka utaratibu ambao utamfanya Diwani pale

alipo katika Kata yake aweze kukagua Miradi iliyoko katika Kata yale na kupata hiki ambacho kinakusudiwa kufanyika hapa. Pale Halmashauri wanapofikiri kwamba ipo haja sasa ya kufanya hivyo kwa maana ya Madiwani wote, watafanya hivyo kupitia kwenye Kamati tuliyoizungumza ya Fedha, Utawala na Mipango. Kama kuna jambo la kuripoti katika zile Kamati nyingine, hawa wataripoti kupitia Mjumbe mmoja mmoja ambaye amechukuliwa kuingia katika Kamati hii ambao ni Wenyeviti.

Mheshimiwa Lekule Laizer, alizungumzia mgawanyo wa fedha za Serikali unazifanya Halmashauri nyingine kupata fedha kidogo na ambazo wakati mwingine hazipatikani. Nataka niseme kuwa, utaratibu tunaotumia sisi wa Bajeti ni wa *Cash Budget* na mapendekezo yote ya hela zitakazotumika katika Halmashauri yanaanzia kwenye Halmashauri yenyewe, unachofanya unawapa *ceiling* tu. Tuna kitu kinaitwa *opportunities and obstacles to development* ndicho kigezo kinachotumika. Kwa hiyo, kwa vile fedha tulizonazo ni kidogo, wanaopanga kipaumbele ni Halmashauri yenyewe inayohusika. Ikifikiri kwamba kisima cha maji hapa ni muhimu kuliko kuwa na darasa, wataelekeza kule kwenye kisima cha maji.

Wakifikiri barabara hii ni muhimu kwa uchumi pale watapeleka pale, wakisema ni hospitali watapeleka pale na vipo vigezo ukiangalia katika *Constituency Development Catalyst Fund,* ule Mfuko wa Wabunge ambao tunautumia hapa, mle ndani tunaangalia pia kiwango cha umaskini, uwezo na *population*. Huwezi kufanya upendeleo wowote hapo, kwa sababu kila

Halmashauri imewekwa katika huo utaratibu na mwisho wa siku wanapewa *ceiling,* wanaweza wakaambiwa mwaka huu m-*maintain* bajeti ile ile kama ya mwaka jana au mwongeze asilimia kumi. Wazo hilo la kwamba kunaweza kukatokea upendeleo, utapendelea wapi!

Unaweza ukaangalia mwenzako kwa maji akaonekana yuko chini, lakini katika Halmashauri kwa mfano Nkasi, Mheshimiwa Keissy anazungumzia habari ya maji hapa ukakuta ame-*reflect* maji ukukata maji ipo juu. Sasa ukiangalia unasema mbona wenzangu wa kule Newala nimeona wao wako chini na mimi mbona ya kwetu ipo juu na nini ni kwa sababu hizi *proposal* zinatokana na Halmashauri zilizoweka. Kwa maana ile *theory* ya *Decentralization by Devolution (D by D)*, kupeleka madaraka kule na kupeleka *resources* na vitu vingine katika Halmashauri.

Hapa ipo rai imeletwa na Mheshimiwa Silinde, Serikali ijaze nafasi wazi zilizoachwa katika Serikali za Mitaa, Vitongoji na kadhalika. Nataka niseme mambo yafuatayo: Kwanza, hizi nafasi kumi sasa hivi na Wabunge mjue, zile za Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji, mtakumbuka wote hawa walikuwa wanakwenda mpaka Utumishi na Mheshimiwa Kombani atakaposimama hapa atazungumzia habari hii. Nina hakika kwamba, Waziri wangu yuko *competent* sana na jambo hili, kwa sababu ndiyo wamekuwa wanalisimamia. Tumerudishiwa zile nafasi tena kupitia rai yenu ambayo mmekuwa mnatoa, wale Watendaji, Walinzi, zile kazi za pale, madereva na nini, zote zimerudi katika Halmashauri. Mwenyekiti wa

Kamati ya Ajira ndiye atakayekuwa anasimamia mambo haya.

Hii imetokana na kwamba, tunashukuru Serikali imeruhusu *General Purpose Grant* imerudi kule. Kwa hiyo, hili linalosemwa hapa hivi sasa hamtaona linajitokeza tena, kwa sababu mtakachohitaji ni kupata kibali cha kusema kwamba ajirini kiasi hiki kwa sababu hutawaacha wakaajiri wenyewe wanavyotaka; itasema Waziri mwenye dhamana atasema pia muajiri Watendaji wa Kata kiasi hiki na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba niende haraka kidogo, nasikia kengele ya kwanza imeshagongwa. Baadhi ya Vijiji na Kata havina Watendaji, hiyo nimeishaijibu; utaratibu wake ni huo sasa hivi mtusaidie kupitia kwa Makatibu Tawala wa Mkoa, tumeshawaelekeza tayari kwamba, majina yale yapatikane na mseme akina nani mnawapendekeza kwenye nafasi zile, wao watakuwa wanasimamia shughuli hizo. Kuna rai hapa kwamba, Wenyeviti wa Vijiji nao wapewe *allowances* na walipwe posho kama walivyo; tunafanya hivyo na nataka niwaambie Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji, kwanza kabisa, kama Serikali tunawashukuru kwa kazi kubwa wanayofanya katika maeneo ya kazi. Tumezungumza, Shule za Kata na Zahanati zinajengwa kule. Miradi yote iliyoko kule wanaofanya kazi ile ni Wenyeviti wetu wa Vijiji na Wenyeviti wetu wa Vitongoji, wanafanya kazi kubwa sana. Tulichoelekeza, kila Halmashauri tunawapelekea kitu kinachoitwa *capacity building grant* inakwenda pale asilimia 20, tunataka tuirudishe kwenye vitongoji itumike. Hii *grant*

ninayoizungumzia hapa, asilimia 20 tunarudisha kitu kinachoitwa *compensation,* zile hela tunazozirudisha kwa ajili ya kodi ambazo zilikuwa na kero kama vitumbua, maandazi, nyanya, mchicha, zile ndogo ndogo nazo Serikali ina-*compensate.*

Tunazitaka Halmashauri zihakikishe kwamba, hicho kinachokwenda kama fidia, asilimia 20 inarudi kijijini ili waweze kuwalipa posho zao Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji kidogo kidogo kulingana na uwezo. Wakati huo huo tunatakiwa tuimarishe mapato yetu ya ndani kwa maana ya *home resource* ili tuweze kufanya shughuli zetu. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelekezo ya Serikali kwamba, Wenyeviti wa Vijiji tuwaangalie kwa sura hiyo ambayo nimeieleza hapo.

Maafisa Tarafa wanasimamia shughuli za maendeleo hawatambuliwi; naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kusema kwamba, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hawezi kukataa kumtambua mtu anayeitwa Afisa Tarafa. Afisa Tarafa ni mkono wa kuume wa Mkuu wa Wilaya katika Wilaya inayohusika, ni sehemu ya *Central Government*. Sasa tumesema wataingia kwenye Kamati na wataingia pia katika Baraza na kama kuna Mbunge yeyote ambaye ana habari, kuna Afisa Tarafa anakataliwa asiingie katika Vikao vya Halmashauri atupe jina la huyo Mkurugenzi ili tuweze kuchukua hatua. Haya ni maelekezo ya Serikali kwa ajili ya kuimarisha ufanisi katika *level* ya Tarafa.

Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, amezungumzia tatizo la maji pale

kwake. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Keissy, kwa kulileta suala hili kila wakati. Katika Bajeti ya Mwaka 2012 na 2013 tumetenga shilingi milioni 100 ili ziweze kutusaidia kuondokana na tatizo la maji lililoko pale. Ujenzi wa Vituo vya Afya unaendelea.

Mheshimiwa Kiwelu na Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro, wamesimama hapa wamezungumzia sana Hospitali ya Mawezi. Nataka nikwambie maelekezo yako yalitekelezwa, tulikwenda mpaka kwenye Hospitali hii na Mkuu wa Mkoa yuko hapa na *RAS* wako hapa wanasikia na Mheshimiwa Kiwelu yuko hapa, utakaposimama usizuie shilingi hapa kwa sababu tulikwenda mpaka kule. Nakuomba dada yangu tafadhali, Mkuu wa Mkoa kupitia ile ziara anayoifanya ametenga shilingi milioni 744 zimewekwa hapa, najua hazitoshi wanahitaji bilioni 13 kwa sababu ya ile wodi wanayoizungumza na kadhalika, lakini hizo ndizo jitihada zilizofanyika, ninawaomba sana mtupitishie.

Jengo la wazazi nalo linahitaj karibu shilingi bilioni 13; ni hela nyingi, tulisema ikiwezekana tutafute na wahisani kutoka nje waweze kusaidia. Sasa kuna Mradi ule wa Kimile na Kakunyu, iliyoko katika Wilaya Misenyi, nayo tumeanza. Wanavyozungumza hapa ni namna ya kusaidia Miradi ile, wananchi wanatakiwa wafanye hivyo ama wapewe hela au wakati mwingine wafanye kwa mikono yao wenyewe.

Maafisa Tarafa wa Mkoa wa Kagera walipwe stahili zao, tumehakikisha kwamba watalipwa na tumeshawawekea utaratibu ambao unaondokana na

hilo tatizo. Hoja hii ililetwa na Mheshimiwa John Charles Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Wakurugenzi wa Halmashauri watumike katika kuwatambua wakulima wanaokopeshwa matrekta. Tumesema tumeagiza Halmashauri, ndugu yetu Shabiby najua ni mfanyabiashara, ukiliachia trekta tu hivi hivi bila kuwa na dhamana yoyote pale au bila kuwa na *security* yoyote pale, itakuwa ni kitu cha ajabu, atakwambia mimi natoka hapa nipo karibu na Msikiti, chini ya Kanisa pale kwenye mfereji, ukikata kona hivi utakuta Bendera ya CCM, ukienda chini yake ndiko ninakotoka, itakuwa ni ngumu sana kuweza kufuatilia hela hizo zitakuwa zimepotea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kusema naunga mkono hoja iliyoletwa hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuiongoza nchi yetu kwa hekima na busara kubwa sana. Napenda pia kuwashukuru wapiga kura wangu na Wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Viongozi wa Mkoa wa Mtwara,

wakiongozwa na Mkuu wetu wa Mkoa wa Mtwara. Napenda pia kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuujalia Mkoa wa Mtwara na Lindi, rasilimali ya gesi nyingi sana ambayo imeongeza mvuto sana, si tu kwa wawekezaji bali pia na wanasiasa wote. Wenyewe ni mashahidi ndani ya Bunge hili, kila anayesimama asipoutaja Mkoa wa Mtwara, anaona kama hajakamilika kuwa Mbunge ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Napenda pia kuwahakikishia Wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi kwamba, mnao Wabunge wenu makini na ambao wanaitetea Mikoa yenu kwa uadilifu mkubwa sana na wala hatuhitaji msaada kutoka kwa Wabunge wa Mikoa mingine ambao hata kwenye Mikoa yao bado wanayo matatizo mengi ya kuyazungumzia lakini wanapoteza muda mwingi kuzungumzia Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Napenda niwaambie Wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwamba, wawe makini wasidanganyike na wanasiasa, siasa chafu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda nirudi katika hoja ambazo zipo mbele yetu. Hoja ya kwanza ambayo imezungumziwa na Waheshimiwa wengi sana ni suala la ubadhirifu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunachukua hatua za dhati

kabisa kuhakikisha tunakabiliana na tatizo la ubadhirifu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika hotuba yangu nimeonesha Wakurugenzi wangapi na Wakuu wa Idara wangapi ambao tayari tumeshawachukulia hatua. Napenda niwahakikishie kwamba, sasa hivi tayari tumeiwezesha Mikoa na Wilaya kupitia vikao vya kazi ambavyo tumevifanya Dodoma na kupitia mafunzo ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Tumewawezesha na tumewapa majukumu ya kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kwamba, zinatekeleza wajibu wake. Tumewaambia Makatibu Tawala wa Mikoa watawajibika pale ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeenda kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu na wao kutokuwachukulia hatua zinazopaswa. Kwa hiyo, napenda nikuhakikishie kwamba, tupo makini, tupeni muda tutahakikisha kila mbadhirifu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa tunamchukulia hatua stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia limezungumzwa suala la watumishi wabadhirifu kuhamishiwa katika maeneo mengine. Napenda nikuhakikishie kwamba, siyo Sera yetu kuhamisha watumishi wabadhirifu. Tumezielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa kuwachukua hatua pale ambapo watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wameenda kinyume na taratibu. Pale inapotokea bahati mbaya tumemhamisha mtumishi bila kufahamu kwamba anayo makosa katika eneo lake, tukipewa taarifa mara moja tunawarudisha katika maeneo yao ili waende wakachukuliwe hatua. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kama mnao ushahidi kwamba kuna mtumishi tumemhamishia eneo lingine baada ya kuwa amefanya ubadhirifu katika eneo lake,

tupeni taarifa tutamrudisha na hatua pia tutawachukulia.

Mheshimiwa Spika, lipo suala ambalo ningependa nilizungumzie pia kwamba, Mbunge wa Nyamagana, Mheshimiwa Wenje, ameshangaa uwepo wa Wakuu wa Mikoa katika Bunge letu hili. Kwanza, nimesikitika jinsi alivyowadhalilisha Wakuu wa Mikoa kupitia mchango wake ambao aliutoa wakati anachangia kwa kusema kwamba, wanapigwa tu na viyoyozi hapa. Mimi binafsi nimesikitika na napenda nimwombee radhi kwa Wakuu wa Mikoa kwa sababu mimi ndiye niliyewaalika Wakuu wa Mikoa waje wahudhurie hapa na siyo kwamba wamekuja kupigwa na viyoyozi kama ambavyo amesema; wanayo kazi, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge ni mashahidi kwamba katika Kamati ile Wakuu wa Mikoa ndiyo waliowasilisha Bajeti ya Mikoa yao. Wao wenyewe ndiyo waliojibia hoja zote zilizotolewa katika mikoa yao, kwa hiyo, hoja zote mnazozitoa hapa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala ambao wapo pale juu ndiyo ambao wanatupatia sisi majibu ambayo tunawapatieni ninyi.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa TAMISEMI, Manaibu wake na Mheshimiwa Waziri Mkuu, siyo maghala ya kutunza kumbukumbu zote zilizopo katika Mikoa yetu. Kwa hiyo, maswali yanayoulizwa na taarifa ambazo Waheshimiwa Wabunge wanazihitaji, tunazipata kupitia kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala ambao wako pale juu na pia wanayo haki ya kupata viyoyozi hivyo ambavyo ninyi mnapepewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Wakuu wa Mikoa kuwepo ndani ya Bunge hili hatukulianzisha sisi TAMISEMI, sasa hivi ni suala ambalo lilikuwepo tangu Uhuru, tena kipindi hicho walikuwa na hadhi ya Wabunge kama sisi na walikuwa wanaingia ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, wale vijana ambao wameingia juzi Bungeni ambao walikuwa wameomba mwongozo kwamba wamedhalilishwa, napenda tu niwafahamishe kwamba, hii ilikuwepo tangu enzi za Uhuru, Wakuu wa Mikoa kuhudhuria katika kikao hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na Kamati zetu ambazo zinatushauri. Nipende kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hoja zote ambazo wamezitoa tutazifanyia kazi na zile ambazo sitaweza kuzitolea majibu hapa, wawe na uhakika kwamba watapata majibu yao kwa maandishi kabla Bunge hili halijaahirishwa.

Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, alitoa angalizo hili, pia ni la Kamati yake kwamba tusijisahau, Hati Safi isiwe kigezo kwamba mambo ni shwari katika Halmashauri zetu. Upo uwezekano katika baadhi ya Halmashauri wanapata Hati Safi lakini Miradi inatekelezwa kinyume na chini ya viwango.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Pindi Chana na Kamati yake kwamba, angalizo lake tunalitekeleza na pia kama nilivyotangulia kusema, tumezielekeza Sekretarieti za

Mikoa kusimamia utendaji kazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pale ambapo wanaona kwamba utekelezaji wa Miradi au utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa upo chini ya kiwango, wanao uwezo kisheria wa kuzichukulia hatua Mamlaka hizo kupitia Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa ni kuhusu ushauri wa Kamati kwamba, wafanyakazi wanakopa kupita kiasi na hivyo kuwafanya baadhi yao mwisho wa mwezi kutoka patupu. Pia suala la makampuni kuwahadaa watumishi na kukopa bila waajiri wao kufahamu. Napenda kumhakikishia kwamba, ofisi yangu imezielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kwamba, makampuni yanakopesha watumishi kwa ridhaa ya waajiri, yaani Halmashauri husika. Pia tumewaelekeza kutumia au kutekeleza Waraka wa Utumishi wa tarehe 19 Machi, 2009 na mwingine wa mwaka 2012, ambao umeelekeza kwamba, mtumishi asikope zaidi ya theluthi moja ya mshahara wake. Kwa vile sasa hivi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imegatua mfumo wa kuwaingiza watumishi katika *payroll* kwa kutumia Lawson, Toleo Namba Tisa, ambapo sasa hivi makato yote ambayo mtumishi anakatwa, yanafanywa na mamlaka za ajira. Tuna uhakika kabisa kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na uhakika kwamba, mtumishi hakatwi zaidi ya kile ambacho kimeelekezwa na Waraka wa Utumishi.

Pia tunawaomba makampuni yote ambayo yanatoa mikopo kwa watumishi, wahakikishe kwamba kabla ya kumkopesha mtumishi, basi anahakikisha

kwamba anapata ridhaa ya mwajiri wake na kama atafanya hivyo, lolote litakalotokea mwajiri hatawajibika kwa mikopo ambayo imetolewa nje ya ridhaa ya mwajiri.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, alipenda kufahamu kwamba wale Wajerumani wanaokuja kufunga Mifumo ya Kompyuta katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, wanakuja kufanya nini wakati tunazo Kampuni za Wazawa ambazo zina uwezo wa kufanya kazi hizo. Pia alipenda kufahamu hiyo kazi wanafanya bure au nani atawalipa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie kwamba, katika jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaongeza makusanyo yake, wadau mbalimbali walijitokeza katika kuisaidia Serikali. Miongoni mwa wadau hao ni Wajerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo la *GTZ*. Katika kuboresha mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, eneo la kodi ya majengo, hawa wenzetu Wajerumani waliamua kuzisaidia zile mamlaka ambazo zimejitaja, yaani Majiji na Manispaa ya Kigoma Ujiji na Manispaa ya Mtwara Mikindani. Kwa hiyo, hawa Wajerumani wamekuja kutusaidia, hatuwalipi na wala hawachukui kazi za wazawa. Hadi hivi sasa tunapozungumza, tayari Wajerumani wamewasaidia Manispaa ya Mtwara Mikindani katika kufunga Mfumo wa Kompyuta kupitia *University Computing Centre.* Kwa hiyo, hawa Wajerumani wanatumia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hawafungi wenyewe isipokuwa wao wanatoa msaada tu, wanaziwezesha hizi

Mamlaka kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kufungiwa huo mtandao. Kwa hiyo, napenda nikuhakikishie kwamba, Wajerumani hawakuja kuchukua kazi za Watanzania, kazi za Watanzania zipo na wanatumia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, alitaka Serikali itoe kauli juu ya kusimamishwa kwa Uchaguzi wa Vijiji, Vitongoji na Serikali za Mitaa. Napenda nimhakikishie kwamba, suala la kujaza nafasi katika ngazi za Vijiji na Vitongoji ni la kisheria. Sura Namba 287 na 288 ya Sheria za Serikali za Mitaa na Kanuni za Uchaguzi za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2009, zinatamka kwamba nafasi zijazwe ndani ya siku 60. Pia ninataka kumhakikishia kwamba, lile lililotokea Mwanza ni la kuhakikisha hizi chaguzi hazigongani na si la Tanzania nzima kama alivyotaka kusema au kutaka kuwahakikishia Watanzania. Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ulifanyika mwaka 2009, sasa hivi kinachofanyika ni kujaza nafasi tu katika baadhi ya maeneo. Baadhi ya Mikoa walishajaza hizo nafasi. Kwa hiyo, alichofanya yule Mtendaji kwa niaba ya *RAC* katika Mkoa wa Mara ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, Chaguzi za Chama cha Mapinduzi, ambacho ni Chama kinachotawala na uchaguzi wa kujaza nafasi ambazo ni chache sana hauingiliani.

Pia Kamati yetu kupitia Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati, alitaka kupata ufafanuzi wa vikwazo vinavyosababisha Mradi wa *DAT* usikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, vikwazo vilivyokuwa vinasababisha Mradi wa *DAT* usikamilike kwa wakati vimeshapatiwa ufumbuzi hasa baada ya kesi ya eneo la Gerezani kumalizika na Serikali kutoa kiasi cha shilingi bilioni 12.03 kulipia fidia kwa maeneo yote yaliyokuwa yamebakia kwenye awamu ya kwanza. Aidha, katika utekelezaji wa awamu wa pili na ya tatu, Serikali itahakikisha kuwa changamoto zilizojitokeza kwenye awamu ya kwanza zinatafutiwa ufumbuzi kabla ya ujenzi wa miundombinu kuanza.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na suala ambalo lilitaka Serikali itoe taarifa juu ya utekelezaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam, ambayo ndiyo hiyo *DAT* niliyoilezea, Mradi ambao umechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, Serikali imezifanyia kazi changamoto zote zilizokuwepo katika Mradi huu na utekelezaji wa Mradi sasa unaendelea vizuri kwa kujenga miundombinu katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Barabara Kuu kutoka Kimara mwisho hadi Kivukoni inategemea kukamilika ndani ya miaka miwili kuanzia Machi 2012 hadi Februari 2014 na hivyo mabasi ya usafiri wa haraka kuanza kazi. Ujenzi wa Barabara ya Magomeni - Moroko na Fire - Gerezani inaendelea na itakamilika Februari, 2015. Usanifu wa awamu ya pili na ya tatu ya Barabara za Kilwa na Nyerere umekamilika na ujenzi wa miundombinu yake unatarajiwa kuanza

Mwaka wa Fedha 2013/2014 na kukamilika mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Silinde aliitaka Serikali ianzishe Mamlaka ya Maendeleo Vijijini ili isimamie maendeleo vijijini. Uwepo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa umetamkwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 145 na 146. Serikali inatekeleza dhana ya maendeleo vijijini kupitia Sera yake ya Maendeleo Vijijini ya Mwaka 2003, ambayo inatilia mkazo ushirikishwaji wa wananchi katika kujiletea maendeleo. Kupitia Sera ya Upelekaji wa Madaraka kwa Umma, Serikali za Mitaa zinaendelea kuwashirikisha wananchi katika kuamua na kutekeleza shughuli zao za maendeleo. Aidha, kama njia ya kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali, hakuna haja ya kuanzisha mfumo mpya wa mamlaka mpya kama ambavyo nimetangulia kusema. Mfumo uliopo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa unatosheleza na Chama chetu cha Mapinduzi tunaona unafaa labda kama itatokea na ninahisi haitaweza kutokea, Chama cha Mheshimiwa kikishika madaraka basi mfumo huo utaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mbunge wa Temeke na Mheshimiwa Zarina Madabiba, Mbunge wa Viti Maalum, walizungumzia suala la kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam na pia kuomba uwepo wa *ring roads.*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza msongamano katika

Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na ujenzi wa *ring roads* kama ifuatavyo:-

Kwanza, Ubungo – Kigogo – Kawawa Road – Round About ambayo ni sawa na kilomita 6.4, Kigogo – Round About – Msimbazi Valley – Jangwani – Twiga Junction kilomita 2.7 na Jet Corner – Buza – Davis Corner kilomita 10.3. Mikakati mingine ya kupunguza msongamano ni pamoja na upanuzi wa Barabara ya New Bagamoyo, Mwenge – Tegeta, ujenzi wa Barabara ya Sam Nujoma, upanuzi wa Barabara ya Nelson Mandela, upanuzi wa Barabara ya Morocco - Mwenge, ujenzi wa Barabara ya Kawe TPDF Range, utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka ambayo nimeshaelezea utekelezaji wake ulivyo na hatua ambayo tumefikia na pia kuanzisha usafirishaji wa reli na majini ambayo ni sehemu ya kazi za Wakala wa *DATS.* Pia ujenzi wa *fly over* nao kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiuelezea ni mojawapo ya mikakati ya kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, ambapo Mheshimiwa Waziri husika atakapofika atalielezea zaidi suala hili lipo katika hatua gani.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napenda niishukuru familia yangu, nikianzia na wazazi wangu; Mzee Abdulrahman Mohamed Ghasia na Mama yangu Kashu Balozi, kwa malezi mema kwangu. Pia nawashauri wazazi wengine waendelee kutulea watoto wao tuliopo ndani ya Bunge hili Tukufu ili tuendelee kuwa na mwenendo mwema na hivyo kuendelea kuwajengea heshima wazazi wetu. Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wanangu

nikianzia na mwanangu Inna, Hussein, Asia, Seif na Nasra. Mwisho, namshukuru mume wangu mpenzi Mr. Yahya Ally Muhata, kwa kunivumilia muda wote na pia kuchukua jukumu la kuwa mlezi wa familia yetu kuwalea watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maelekezo ambayo anatupatia katika ofisi yetu. Pia nawashukuru Makatibu Wakuu, nikianzia na Mheshimiwa Hussein Katanga - Katibu Mkuu TAMISEMI na Manaibu wake nikianzia na Bwana Jumanne Sagini na Bwana Alphayo Japani Kidata, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Pia nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Madiwani wote na Mabaraza ya Madiwani, kwa ushirikiano ambao wananipatia katika kipindi kifupi. Nami nawaahidi ushirikiano na pia nawashukuru Manaibu wangu wote; Bwana Mwanri na Bwana Majaliwa, kwa ufafanuzi na pia ushirikiano wanaonipatia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa ufafanuzi huo na sasa namwite Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, ninampa dakika 30, atafuatiwa na Mheshimiwa William Lukuvi, ninampa dakika hizo hizo 30.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninapenda vilevile kukushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia

katika majumuisho ya hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nitumie fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa na imani nami katika kusimamia shughuli za uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya sekta binafsi. Namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuiongoza Serikali na kusimamia utekelezaji wa kila siku, lakini pia kwa kutupa maelekezo na ushirikiano wa karibu sana. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza na kumshukuru sana Waziri mwenzangu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa William Lukuvi, ambaye ni ndugu yangu na ninampongeza kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kusimamia shughuli za Serikali Bungeni. Hongera sana. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wabunge walioteuliwa kuingia Bungeni, Waheshimiwa Mawaziri walioteuliwa kuwa Mawaziri wakati wa kashikashi zilizopita. Nawapongeza vilevile Mawaziri wenzangu ambao kwa bahati nzuri tumebakia katika nafasi zetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, akisaidiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kwa kutupa ushirikiano wa karibu na upendo mkubwa sana. Wametoa maoni na ushauri wao wenye mchango mkubwa sana katika kuboresha utendaji wa kazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu hususan uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya

sekta binafsi. Namshukuru Mheshimiwa Chenge na ninawashukuru Wajumbe wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutambua mchango wa Kambi ya Upinzani Bungeni, inayoongozwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai na Msemaji Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Vilevile ningependa kuomba ushirikiano wa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Esther Matiko, kwa kushirikiana naye kama ilivyokuwa kawaida yetu miaka miwili iliyopita. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yenu mizuri na yenye tija wakati wa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Serikali inathamini sana maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na itazingatia ipasavyo maoni na ushauri huo katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa nisifikie hoja ya kila Mbunge, lakini nataka niwahakikishie kwamba, hakuna hata hoja moja ambayo sitaizingatia katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda niwashukuru Wananchi wa Jimbo la Hanang, kwa kuendelea kushirikiana nami katika shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo ya Jimbo letu na hasa ukizingatia kwamba ni chimbuko la Upinzani vilevile. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa mama yangu mzazi na pia familia yangu, ikiongozwa na mume wangu mpenzi, Profesa Joseph Nagu, kwani bila uvumilivu na ushirikiano wao wa karibu, kazi yangu ingekuwa ngumu sana. Napenda pia kuwashukuru

watoto wangu Tumaini, Neema, Deo na wale wote ambao ninawalea.

Vilevile nawashukuru sana Mawaziri, Wabunge, Ndugu na jamaa, Wananchi wa Jimbo la Hanang Mkoa wa Manyara, Singida, Dodoma, Arusha, Mwanza na Mikoa mingine na majirani zangu walionifariji wakati wa msiba wa baba yangu mzazi, Mzee Michael Ndafu Mombo, aliyefariki tarehe 15 Aprili 2012 tukiwa hapa Bungeni katika Hospitali ya Mount Meru Arusha na hatimaye kuzikwa nyumbani Hanang Mkoani Manyara. Nawashukuru sana. Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya baba yangu mahali pema peponi; *amina.*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitoe maelezo ya jumla kuhusu masuala ya uwekezaji, uwezeshaji wananchi kiuchumi na maendeleo ya sekta binafsi. Hii ni kwa sababu inawezekana kama nilivyosema nisimfikie kila Mbunge mmojammoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba, uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi, ni suala la msingi na la lazima katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa lolote. Umuhimu wa uwekezaji ndani hauna mjadala, lakini ili uwekezaji wa ndani uweze kukidhi mahitaji ya Taifa, ni lazima kiwango cha kuweka akiba kiwe cha kutosha ili kuzalisha mitaji ya kuwekeza. Kwa upande wa Tanzania, kiwango cha kuweka akiba ni asilimia 15 tu ya pato la Taifa. Kiwango hiki ni kidogo na hivyo hakiwezi kukidhi mahitaji halisi ya mitaji kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, uwekezaji wa nje hauepukiki, hivyo ni muhimu kuweka vivutio kujenga mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na nje hasa pale ambapo gharama ya uwekezaji na ya biashara ni kubwa sana na kwa kuzingatia manufaa ya uwekezaji, hili ni suala gumu pale ambapo kila mmoja anaona uwekezaji uko labda kwa ajili ya manufaa ya wawekezaji peke yake. Mimi nimepewa kazi hii na ninaamini kwamba, hakuna nchi ambayo inaweza kukuza uchumi wake bila ya kuwekeza. Ni sawasawa na mkulima asipopanda shamba lake hatavuna. Manufaa yanayotokana na uwekezaji ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, kuongezwa kwa fursa hususan za ajira, mapato ya kodi, kuongeza thamani ya bidhaa, fedha za kigeni, teknolojia ya kisasa, menejementi na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ndani cha uwekezaji kitaongezeka endapo tutaongeza kiwango cha kuweka akiba na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Vilevile hatuna budi kujijengea uwezo katika kuandaa na kusimamia mikataba ya uwekezaji ili kulinda maslahi ya Taifa na kufaidika na uwekezaji huo hususan ule unaotokana na mitaji ya nje. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa, wawekezaji wanatimiza masharti yanayoambatana na mikataba ya uwekezaji wao kama vile ulipaji kodi na kuweka mfumo mzuri wa uwajibikaji kwa jamii zinazowazunguka na kwa Taifa vilevile. Uzoefu wa Angola na Norway unatufundisha kuwa makampuni makubwa yanaweza yakachangia maendeleo ya nchi kwa kutumia sehemu ya mitaji yao. Lengo ni

kuhakikisha kuwa uwekezaji unanufaisha wawekezaji wenyewe, wananchi na Taifa kwa ujumla kwa manufaa ya pande zote husika. Kwa sababu hizi ninawaasa Watanzania wenzangu na Waheshimiwa Wabunge tutambue na kuthamini mchango wa wawekezaji wa ndani na nje katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu na siyo kuwatazama wawekezaji wote kama vile ni waporaji. Jambo muhimu zaidi ni sisi kujipanga vizuri, kuboresha uwezo na uzalendo wetu wa kuandaa, kufuatilia na kusimamia mikataba yenye maslahi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2000 hadi Mei, 2012, jumla ya miradi 6,602 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 49 imesajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* ambayo imetoa ajira kwa Watanzania takribani 950,108. Idadi ya wawekezaji wa ndani imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na katika kipindi husika jumla ya miradi 3,345 inamilikiwa na wawekezaji wa ndani ambayo ni sawa na asilimia 51 na inatia moyo sana. Miradi hii ina thamani ya sawa na dola za Marekani bilioni 24.99 ya miradi yote. Miradi inayomilikiwa na wageni kutoka nje ni 1,569 ambayo ni asilimia 24, na miradi ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wa kutoka nje (*joint venture*) ni 1,688 ambayo nia sawa na asilimia 25 ya miradi yote. Tukumbuke kuwa mitaji duniani kote huenda kwenye nchi ambazo zina mazingira wezeshi ya kuwekeza na kufanya biashara. Nilisema mara ya mwisho kwamba, ndege zinatua pale penye uwanja wa ndege, kama hakuna uwanja ndege haiwezi kutua.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji kutoka nje au *foreign direct investment* umekuwa ukipanda mwaka hadi mwaka. Kwa mujibu wa Taarifa ya Dunia ya Uwekezaji ya mwaka 2011, inayotolewa kila mwaka na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo, mitaji ya moja kwa moja *(FDI)* iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 494 mwaka 2005 hadi kufikia dola za Marekani milioni 700. Mojawapo ya sababu zilizochangia kukua kwa miradi hii, ni pamoja na unafuu wa kodi kwa vifaa vya mtaji (*deemed capital goods*). Unafuu unaotolewa ni Ushuru wa Forodha na *VAT* kwa baadhi ya vifaa vinavyohitajika wakati wa kuanzisha miradi ya uwekezaji ambayo kimsingi havipo katika kundi la mitambo (*capital goods by generic descriptions*) ambavyo kiasili havitozwi kodi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, wataalam wa kodi wanashauri kwamba kodi yoyote inayotozwa kwenye mitaji ni kodi mbaya. Tofauti na dhana iliyopo miongoni mwa Watanzania wengi kwamba, wawekezaji wanasamehewa kulipa kodi zote, wawekezaji hulipa Ushuru wa Forodha na *VAT* kwa vifaa ambavyo havijaorodheshwa kama vifaa vya mtaji, Ushuru wa Bidhaa, Kodi ya Zuio kwa huduma mbalimbali, Kodi ya Mapato, Kodi ya Maendeleo ya Ujuzi wa Wafanyakazi. Kodi hizi hulipwa hata katika kipindi cha uanzishwaji wa miradi na hivyo kufanya misamaha ya kodi inayotolewa kuwa ni kiasi kidogo ikilinganishwa na kodi zinazokusanywa au zitakazokusanywa kutoka kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya awali ya utafiti uliofanywa na *TIC* ambayo nitayagawa hapa Bungeni yakihusisha sampuli ya makampuni 42 yaliyosajiliwa na

Kituo hicho katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010 umeonesha kwamba, makampuni haya yaliwekeza mtaji wenye thamani ya shilingi trilioni 1.7. Jumla ya misamaha ya kodi kwa bidhaa za mtaji yenye thamani ya shilingi bilioni 88.8 ilitolewa kwa makampuni hayo. Katika kipindi hicho, kodi iliyolipwa na makampuni hayo baada ya misamaha hiyo iliyotolewa wakati miradi hiyo ilipoanzishwa imefikia shilingi trilioni 1.13 na yanaendelea kulipa kodi bila kuhitaji misamaha zaidi. Takwimu hizi zitakuwa kwenye *Hansard* na matokeo haya nitayagawa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna miradi ambayo iko kwenye sekta zingine. Miradi hiyo haijafanyiwa utafiti na tutaendelea kufanya utafiti huko. Suala la msingi siyo kuondoa misamaha yote ya kodi kwenye uwekezaji, kwani dhamira ya Serikali kutoa misamaha hiyo ni kuvutia mitaji kutoka ndani na nje ya nchi kwenye miradi mipya ambayo isingepatikana bila vivutio hivyo. Kama nilivyoshauriwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba misamaha inayotolewa inahakikiwa ipasavyo na taasisi husika kama *TIC, EPZA*, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kulinda maslahi ya Taifa letu. Aidha, Serikali ina utaratibu wa kuingia Mikataba ya Utekelezaji *(Perfomancce Contracts)* na wawekezaji wakubwa ili kuwezesha ufuatiliaji wa mafanikio yaliyotarajiwa. Natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kushirikiana na Serikali kubaini matumizi mabaya ya misamaha ya kodi ili hatua stahiki zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, Tanzania bado inapokea kiwango kidogo cha mitaji kutoka nje. Kulingana na taarifa ya Dunia ya Uwekezaji ya mwaka 2011 kwa mwaka 2010 jumla ya mitaji yote duniani ilikuwa dola za Marekani bilioni 1,244. Katika mwaka huohuo Tanzania ilipata dola za Marekani 700 kati ya dola za Marekani bilioni 55 zilizokuja Afrika. Hii ni sawa na asilimia 1.27 tu ya mitaji yote iliyokuja Afrika ambayo ni asilimia 0.06 tu ya mitaji yote duniani. Utaona ni kiasi gani kinakuja Tanzania. Afrika ilipokea kiasi cha dola za Marekani bilioni 55 ambazo ni sawa na asilimia nne (4%) ya mitaji yote ya Dunia. Bara la Ulaya lilipokea dola za Marekani bilioni 313, Amerika Kaskazini dola za Marekani bilioni 252, Asia dola za Marekani bilioni 358 (hii ikiwa ni China na India), Amerika ya Kusini dola za Marekani bilioni 86 na Australia dola za Marekani bilioni 32. Kwa hiyo, utaona sisi tunapokea dola milioni 800 peke yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kudurusu Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 na hatimaye Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1977. Changamoto kubwa ya mfumo wa sasa wa misamaha ya kodi umejikita kupima ubora wa wawekezaji kwa kuangalia faida itakayotokana na matunda ya uwekezaji huo badala ya kuangalia mitaji inayofanya uwekezaji huo uwepo. Manufaa yanayotegemewa kutokana na faida baada ya uwekezaji ambayo nimeeleza kuwa ni ajira, malipo ya kodi, mapato ya mauzo ya nje, teknolojia mpya na mengine, hayatabiriki na kwa kiasi kikubwa inategemea ujanja wa mwekezaji. Pia siyo rahisi kupimika na kuyaweka bayana. Tutakachokifanya siku za usoni ni kuweka mikakati ya

kuanza kutoa misamaha kwa kuangalia faida tutakayopata kama sehemu ya mitaji ya uwekezaji kwani hii inatabirika na ni rahisi kupima kama inalingana na misamaha tunayotoa. Mfano, ni utoaji wa hisa zisizolipiwa kwa kutumia rasilimali ya asili, kutengeneza miradi au *corporate social responsibility* (miradi ya uwajibikaji wa muwekezaji) kwa jamii na taifa kama asilimia ya uwekezaji, kununua vifaa vilivyotengenezwa ndani au chakula kinaweza kununuliwa ndani kama asilimia ya mtaji wa uwekezaji, kutumia asilimia kubwa ya bidhaa za uzalishaji kupitia kampuni za Kitanzania na kuajiri Watanzania katika nafasi ambazo sasa hivi zimeajiri wageni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 imekamilika na maandalizi ya msingi ya kuanzisha Kitengo cha Utaratibu wa Masuala ya Ubia (*PPP cordinating Unit*) kwenye Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Kitengo cha Fedha kwenye Wizara ya Fedha yamekamilika. Mapendekezo ya miradi yenye uwezekano wa kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP* yamewasilishwa na tutayafuatilia kwa karibu kwa sababu ndipo hapo tunaweza tukatekeleza miradi ya miundombinu na kuweza vilevile kuondoa gharama za uwekezaji na kufanya biashara Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza uwekezaji, sasa naomba niende kwenye uwezeshaji wa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao. Uwezeshaji wananchi kiuchumi, ni uamuzi wa makusudi unaojumuisha hatua mahsusi zinazochukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuinua uelewa,

ujuzi, elimu ya ujasiriamali na kuwawezesha Watanzania kumiliki rasilimali na kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi. Aidha, uwezeshaji wananchi kiuchumi ni dhana pana ambayo inahitaji wananchi kutambua fursa mbalimbali zinazowazunguka na kuzitumia fursa hizo kujikwamua kiuchumi. Jukumu la Serikali ni kuandaa na kuboresha sera, sheria, kanuni na taratibu ili kumwezesha mwananchi kutumia fursa hizo. Ili kufaidika na matunda hayo, Watanzania wanapaswa kufanya kazi kwa bidii, maarifa na kwa kujituma. Hivyo ni lazima kuwapa wananchi wote fursa sawa ili waweze kujitegemea. Jitihada hizi kama wananchi wataziunga mkono, zitapunguza tofauti kubwa ya vipato ambavyo vipo hivi sasa na vinahatarisha amani yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo, Serikali imetunga Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya Mwaka 2004. Sera ni pana na nzuri, lakini nafikiri tunahitaji kuangalia sheria ambayo inawezesha utekelezaji wa sera ile. Sasa hivi tuna mifuko mbalimbali ambayo inawezesha wananchi. Mifuko hiyo iko mingi, nikiisoma sasa hivi pengine inaweza ikachukua muda. Naweza nikatayarisha hiyo *list* nikawaletea. Serikali imeanzisha mifuko mbalimbali kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Sheria yake, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni chombo cha kitaifa kitakachosimamia, kufuatilia na kuratibu shughuli zote za uwezeshaji wananchi katika sekta zote na katika maeneo yote. Serikali inaangalia uwezekano

wa kuweka baadhi ya Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama ilivyo kwa Zambia ambapo mifuko yote ipo chini ya Mfuko wa *Citizen Empowerment Fund* na hili limeshauriwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada nyingine za Serikali katika kuwezesha wananchi ni kuweka mazingira wezeshi ambayo ni pamoja na kuimarisha uchumi jumla, kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii, kuboresha huduma za Serikali, kuimarisha upatikanaji wa mitaji, kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu, kuboresha na kuimarisha masoko, kuimarisha ushirika na kuhakikisha ardhi inawanufaisha wananchi wa Tanzania. Aidha, Serikali inatekeleza mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Mpango huu umeandaliwa kuiwezesha Serikali kutoa huduma za msingi kwa sekta binafsi na ninapenda kusema kwamba, urasimu unapaswa uwezeshe, urahisishwe na uhamasishe uwekezaji ndani ya nchi badala ya kuukwamisha. Tunajitahidi sana. Hii inatokana na mtazamo (*mind set*) zetu kutokana na uchumi hodhi ambao unaendelea mpaka sasa. Kwa hivyo, kazi yetu kubwa ni kuhakikisha kwamba *mind set* ile inabadilika.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye maendeleo ya sekta binafsi. Serikali imeachana na kuendesha uchumi. Kama hatutakazania sekta binafsi maana yake uchumi wetu utalegalega. Kwa hiyo, moja ya jitihada zinazofanyika Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kuhakikisha sekta binafsi inatekeleza wajibu wake.

Kutokana na utekelezaji wa miradi ya kukuza ushindani wa sekta binafsi, Tanzania imechaguliwa na imekubali kuwa mwenyeji wa mkutano wa Kimataifa ujulikanao kama '*International Smart Partineship Diologue* ya mwaka 2013' unaotarajiwa kufanyika hapa nchini mwezi Mei, mwaka ujao. Mikutano ya aina hii hufanyika karibu kila mwaka na katika nchi mbalimbali ikijumuisha viongozi wa Serikali, wafanyabiashara, waandishi wa habari, vijana, wanawake na sekta binafsi kwa ujumla kukaa pamoja na kuangalia mustakabali wa Taifa lao hasa katika mambo ya kiuchumi na ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kujibu hoja za Wabunge waliochangia katika eneo la uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya sekta binafsi na nina hakika sitawafikia wote lakini naomba nikiri kwamba, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi inayoongozwa na Mheshimiwa Andrew John Chenge (Mtemi) akisaidiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula, imefikia maeneo yote ambayo Wabunge waliyatolea hoja. Kwa hiyo, nitakapokuwa ninajibu hoja za Kamati nitakuwa nawajibu Wabunge vilevile.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza, Serikali ifanye tathmini ya fedha za mikopo inayotolewa kupitia mifuko mbalimbali ili kuona kama malengo yaliyokusudiwa yamefikiwa. Aidha, Serikali iweke msisitizo katika kuhamasisha uwekezaji na uwezeshaji kwenye sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji ambazo zinaajiri na kutegemewa na Watanzania wengi. Hili halina mjadala. Serikali imeanza mchakato wa kutathmini mifuko mbalimbali ya uwezeshaji ikiwa ni

pamoja na kuitaka mifuko husika kutoa taarifa za kila robo mwaka zitakazoainisha kiasi cha mikopo iliyotolewa, idadi ya wananchi waliofikiwa, shughuli au miradi iliyolengwa na mikopo inayorejeshwa. Kiwango cha urejeshwaji wa baadhi ya mikopo iliyotolewa ni cha kuridhisha. Mfano, hadi Aprili, 2012 kiwango cha urejeshaji katika mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kilikuwa asilimia 96. Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kuongeza Ajira au *JK Fund* asilimia 78, *TASAF* asilimia 91, *SELF* asilimia 91.4 na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo asilimia 73. Kwa hiyo, unaona kwamba wananchi wanarudisha mikopo ile na Serikali kwa kushirikiana na mifuko hiyo itajitahidi kutoa mikopo kwa ufanisi zaidi ili wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Kamati yetu ni kwamba, Serikali iimarishe usimamizi wa utekelezaji wa sera, sheria, programu, mikakati na mifuko mbalimbali yenye lengo la kuwawezesha kiuchumi wananchi wengi zaidi wenye kipato cha chini. Aidha, Serikali iwe makini katika kutoa mikopo kwa sekta binafsi kwa kuhakikisha inaelekezwa kwenye maeneo ya wananchi wenye kipato cha chini badala ya kuelekezwa kwa wafanyabiashara wachache. Tunakubaliana na hoja hiyo, ni kweli kwa uwezeshaji unafanyika kupitia sera, sheria, programu na mikakati mbalimbali katika sekta za kiuchumi na kijamii ambapo kimsingi Serikali inaweka mazingira wezeshi kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo. Serikali itahakikisha kwamba mfumo wa sera, sheria, programu na mfuko inazingatia uwezeshaji wa wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, Kamati vilevile ilisisitiza Serikali itoe taarifa kuhusu jitihada zinazoendelea. Serikali inafanya juhudi mbalimbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi na mimi nakiri ni kutokana na kutotoa taarifa, wananchi hawaelewi kwamba wanawezeshwa. Tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunatoa taarifa za kila wakati. Hadi kufikia Aprili, 2012, jumla ya mikopo iliyotolewa kupitia mifuko hii huwezi kuamini ni shilingi bilioni 177.93 maana yake ni trilioni moja na zaidi. Kwa hivyo, kama tungekuwa tunatoa taarifa, fedha hizi zingejulikana na vilevile kufuatiliwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesema kuwa elimu inahitajika kutolewa kwa wananchi wengi ili waweze kushiriki kikamilifu katika ujasiriamali, uwekaji akiba na hatimaye katika kuwekeza. Hilo ni muhimu na tutahamasisha wananchi, tutawaelimisha bila kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, Kamati vilevile imesisitiza hasa Mheshimiwa Devotha Likokola kuwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lianzishe dawati maalum kwa ajili ya kuratibu shughuli za VICOBA. Hili tumelikubali, kwanza tutathmini na tutaona namna nzuri ya VICOBA vitakavyochangia maendeleo ya nchi yetu kwa sababu ndio mwanzo wa wananchi kuweka akiba.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi kupitia kwa Mheshimiwa Andrew Chenge, wameshauri Serikali ihimize uwezeshaji wananchi kiuchumi na Serikali iangalie namna ya kuunganisha mifuko hiyo, hiyo nimeshaelezea.

Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido amesema kwamba Longido fedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi maarufu kama JK hazijawahi kufika Longido. Nataka nimhakikishie na nitampa taarifa kwamba fedha hizi zimefika.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wameniomba nishirikiane nao katika kuwezesha wananchi. Hiyo ni rai ambayo nimeikubali kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mwijage kwa kuniomba kwenda Kagera, nitakwenda na nitaenda katika Mikoa yote ili tushirikiane kuwawezesha wananchi wetu washiriki kikamilifu katika kuanzisha na kuwekeza akiba zao kwenye miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunajua kwamba vijana ni wengi na wenye nguvu na Mheshimiwa Ester Bulaya ameniomba kwamba nisisahau vijana nitafanya hivyo kwa kutambua kwamba vijana ndio nguvu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge Wanawake wametupongeza na kututia moyo Mawaziri Wanawake, ninawahakikishia kwamba hatutawaangusha, tutatenda kazi zetu kwa uaminifu, kwa uadilifu na kutokuwaangusha wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee jambo moja ambalo linahusu Jimbo langu. Kule Jimboni kwangu kuna mashamba ya ngano ambayo yalikuwa chini ya Serikali baadaye tukayabinafsisha na wawekezaji kwa kweli wameanza kuwekeza lakini

hawajafikia matarajio ya wananchi wa Hanang. Kwa hivyo nitajitahidi na nimeshajitahidi wawekezaji wale wamenihakikishia kwamba wataanzisha miradi ya umwagiliaji kwa sababu na wao hawatakuwa wanasuasua kama wakulima wa kawaida. Wamenihakikishia wataanzisha Kituo cha Kilimo au Chuo cha Kilimo ambacho ni cha Kimataifa ili Wahanang wafaidike na wengine waniunge mkono.

Mheshimiwa Spika, vilevile kama Waziri wa Uwezeshaji, nimetoa mfano wa kuwawezesha vijana na makundi mbalimbali ya Hanang nikianzia na kutoa matrekta kwa wakulima, bodaboda kwa vijana, vyerehani kwa kinamama na vingine vitafuata. Nashukuru Wabunge waliokuja kuona mfano Hanang, waliwekwa kwenye luninga na mimi nikafarijika kwa kuona kwamba Hanang ina mchango wa kutoa kupitia kwa Mbunge wao ambaye ni Waziri wa Uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono na namshukuru Waziri Mkuu. *(Makofi)*

## MAJIBU KWA MAANDISHI YA MHESHIMIWA DKT. MARY M. NAGU, WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI) KUHUSU UFAFANUZI WA HOJA ZA WAHESHIMIWA WABUNGE WALIPOJADILI HOTUBA YA BAJETI YA MHESHIMIWA WAZIRI MKUU TAREHE 29 JUNI 2012

Mheshimiwa Spika, Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na napenda

kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika majumuisho ya Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Aidha, niwashukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge. Nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa na imani nami katika kusimamia shughuli za Uwekezaji, Uwezeshaji na Maendeleo ya Sekta Binafsi. Nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo na ushirikiano wake pia ninampongeza Mheshimiwa William W. Lukuvi kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kusimamia shughuli za Serikali Bungeni chini ya Katibu Mkuu P. Lyimo pamoja na Ndugu Charles Pallangyo na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, na Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo. Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi, wakiongozwa na Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, akisaidiwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, wametoa maoni na ushauri wao wenye mchango mkubwa katika kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji. Nawashukuru na kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutambua Mchango wa Kambi ya Upinzani Bungeni, inayoongozwa na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mbunge wa Hai na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu mizuri na yenye tija, wakati wa kuchangia hoja ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu. Serikali inathamini sana maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, na itazingatia ipasavyo maoni na ushauri huo katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake. Inawezekana kabisa nisifikie hoja ya Wabunge wote lakini hakuna hata mmoja ambaye hoja yake sijaizingatia.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Hanang kwa kuendelea kushirikiana nami katika shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo ya Jimbo letu. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa mama yangu mzazi pia familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpenzi Prof. Joseph Nagu kwani bila uvumilivu na ushirikiano wao wa karibu kazi yangu ingekuwa ngumu sana. Vilevile, nawashukuru sana Mawaziri, Wabunge, Ndugu, Jamaa, Wananchi wa Jimbo la Hanang Mkoa wa Manyara, Singida, Dodoma Arusha, Mwanza na Mikoa mengine yote pamoja na majirani zangu wote walionifariji wakati wa Msiba wa Baba yangu mzazi Mzee Michael Mombo Mbafu aliyefariki dunia tarehe 15 Aprili, 2012 katika hospitali ya Mount Meru Arusha na baadaye kuzikwa nyumbani Kate Hanang Mkoani Manyara. Nasema Ahsanteni sana. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu baba yangu mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe maelezo ya jumla kuhusu masuala ya Uwekezaji, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi. Hii

ni kwa sababu inawezekana kabisa nisifikie hoja zote zilizotolewa kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba, uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi ni suala la msingi na lazima katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa lolote Duniani. Umuhimu wa uwekezaji wa ndani hauna mjadala, lakini ili uwekezaji wa ndani uweze kukidhi mahitaji ya taifa ni lazima kiwango cha kuweka akiba kiwe cha kutosha ili kuzalisha mitaji ya kuwekeza. Kwa upande wa Tanzania, kiwango cha kuweka akiba ni asilimia 15 tu ya Pato la Taifa. Kiwango hiki ni kidogo na hivyo hakiwezi kukidhi mahitaji halisi ya mitaji kwa ajili ya uwekezaji. Kutokana na hali hii, uwekezaji wa nje hauepukiki hata kidogo, hivyo, ni muhimu kuweka vivutio kujenga mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na nje hasa pale ambapo gharama ya uwekezaji wa biashara kubwa sana na kwa kuzingatia manufaa ya uwekezaji. Manufaa hayo ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, kuongezeka kwa fursa hususan za ajira, mapato ya kodi, kuongeza thamani ya bidhaa, fedha za kigeni, teknolojia ya kisasa, menejimenti na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ndani cha uwekezaji kitaongezeka endapo tutaongeza kiwango cha kuweka akiba na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Vilevile, hatuna budi kujijengea uwezo katika kuandaa na kusimamia mikataba ya uwekezaji ili kulinda maslahi ya Taifa na kufaidika na uwekezaji huo hususani uwekezaji kutokana na mitaji ya nje. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa wawekezaji

wanatimiza masharti yanayoambatana na mikataba ya uwekezaji wao kama vile ulipaji kodi na kuweka mfumo mzuri wa uwajibikaji kwa jamii zinazowazunguka na kwa Taifa *(corporate social responsibility).* Uzoefu wa Angola na Norway, unatufundisha makampuni makubwa ya uwekezaji yameweza kuchangia maendeleo ya nchi kutumia sehemu ya mitaji yao. Lengo ni kuhakikisha uwekezaji unanufaisha wawekezaji, wananchi na Taifa kwa ujumla kwa manufaa ya pande zote husika. Kwa sababu hizi, nawaasa Watanzania wenzangu tutambue na kuthamini mchango wa uwekezaji wa ndani na nje katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu na sio kuwatazama wawekezaji wote kama waporaji wa rasilimali za Taifa. Jambo muhimu zaidi ni sisi kujipanga vizuri kuboresha uwezo na uzalendo wetu wa kuandaa, kufuatilia na kusimamia mikataba yenye maslahi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2000 hadi Mei, 2012 jumla ya miradi 6,602 yenye thamani ya Dola za Marekani 49 bilioni imesajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* ambayo imetoa Ajira kwa Watanzania wapatao 950,108. Idadi ya wawekezaji wa ndani imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na katika kipindi husika jumla ya miradi 3,345 inamilikiwa na wawekezaji wa ndani ambayo ni sawa na asilimia 51 ambayo ni sawa na Dola za Kimarekani bilioni 24.99 ya miradi yote; miradi inayomilikiwa na wageni kutoka nje ni 1,569 ambayo ni asilimia 24 na miradi ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wa kutoka nje *(Joint Venture)* ni 1,688 ambayo ni sawa na asilimia 25 ya miradi yote.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa mitaji duniani kote kuenda kwenye nchi ambazo zina mazingira wezeshi ya kuwekeza na kufanya biashara. Uwekezaji kutoka Nje *(Foreign Direct Invesment-FDI)* umekuwa ukipanda mwaka hadi mwaka. Kwa mujibu wa Taarifa ya Dunia ya Uwekezaji ya mwaka 2011 inayotolewa kila mwaka na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo *(UNCTAD),* Mitaji ya Moja kwa Moja *(FDI)* iliongezeka kutoka Dola za Marekani 494 milioni mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Marekani 700 milioni. Mojawapo ya sababu zilizochangia kukua kwa Miradi hii ni pamoja na Unafuu wa Kodi kwa Vifaa vya Mtaji *(Deemed Capital Goods).* Unafuu unaotolewa ni Ushuru wa Forodha na *VAT* kwa baadhi ya vifaa vinavyohitajika wakati wa kuanzisha miradi ya uwekezaji ambavyo kimsingi havipo katika kundi la Mitambo *(Capital Goods by Generic Description)* ambavyo kiasili havitozwi kodi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Wataalam wa Kodi wanashauri kwamba kodi yoyote inayotozwa kwenye mtaji ni kodi mbaya.

Mheshimiwa Spika, tofauti na dhana iliyopo miongoni mwa Watanzania wengi kwamba wawekezaji wanasamehewa kulipa kodi zote, wawekezaji hulipa Ushuru wa Forodha na *VAT* kwa vifaa ambavyo havijaorodheshwa kama Vifaa vya Mtaji (*Deemed Capital Goods),* ushuru wa bidhaa, kodi ya zuio kwa huduma mbalimbali, kodi ya mapato, kodi ya maendeleo ya ujuzi wa wafanyakazi (*skills development levy)* n.k. Kodi hizi hulipwa hata katika kipindi cha uanzishwaji wa miradi na hivyo kufanya misamaha ya kodi inayotolewa kuwa ni kiasi kidogo ikilinganishwa na kodi zinazokusanywa au

zitakazokusanywa kutoka kwa wawekezaji. Matokeo ya awali ya Utafiti uliofanywa na *TIC* ikihusisha sampuli ya makampuni 42 yaliyosajiliwa na Kituo hicho katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010 umeonesha kwamba makampuni hayo yaliwekeza mtaji wenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.7. Jumla ya misamaha ya kodi kwa bidhaa za mtaji yenye thamani ya Shilingi Bilioni 88.8 ilitolewa kwa makampuni hayo. Katika kipindi hicho, kodi iliyolipwa na makampuni hayo baada ya misamaha hiyo iliyotolewa wakati miradi hiyo ilipoanzishwa imefikia Shilingi Trilioni 1.13 na yanaendelea kulipa kodi bila kuhitaji misamaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la msingi sio kuondoa misamaha yote ya kodi kwenye uwekezaji kwani dhamira ya Serikali kutoa misamaha hiyo ni kuvutia mitaji kutoka ndani na nje ya nchi kwenye miradi mipya ambayo isingepatikana bila vivutio hivyo. Kama mlivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wengi, jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba misamaha inayotolewa inahakikiwa ipasavyo na taasisi husika (kama *TIC*, *EPZA,* Wizara ya Nishati na Madini na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali), ili kulinda maslahi ya Taifa. Aidha, Serikali ina utaratibu wa kuingia Mikataba ya Utekelezaji "*Performance Contracts*" na wawekezaji wakubwa ili kuwezesha ufuatiliaji wa mafanikio yaliyotarajiwa. Natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kushirikiana na Serikali kubaini matumizi mabaya ya misamaha ya kodi ili hatua stahiki zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, Tanzania bado inapokea kiwango kidogo cha mitaji kutoka nje. Kulingana na

Taarifa ya Dunia ya Uwekezaji ya mwaka 2011. Kwa mwaka 2010 jumla ya mitaji yote ya Dunia ilikuwa Dola za Marekani 1,244 Bilioni. Katika mwaka huo, Tanzania ilipata Dola za Marekani 700 Milioni tu kati ya Dola za Marekani 55 Bilioni zilizokuja Afrika. Hii ni sawa na asilimia 1.27 tu ya mitaji yote iliyokuja Afrika na asilimia 0.06 tu ya mitaji yote ya dunia. Afrika ilipokea kiasi cha Dola za Kimarekani 55 Bilioni, ambazo ni sawa na asilimia 4 tu ya mitaji yote ya dunia; Bara la Ulaya lilipokea Dola za Marekani 313 Bilioni; Amerika ya Kaskazini Dola za Marekani 252 Bilioni; Asia Dola za Marekani 358 Bilioni; Amerika ya Kusini Dola za Marekani 86 Bilioni na Australia Dola za Marekani 32 Bilioni.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kudurusu Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 na hatimaye Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 ili kukabiliana na changamoto zilizopo na kuweka mazingira mazuri zaidi ya kuvutia uwekezaji wa ndani na nje. Changamoto kubwa ya mfumo wa sasa misamaha ya kodi umejikita kupima ubora wa uwekezaji kwa kuangalia faida itakayotokana na matunda ya uwekezaji huo badala ya kuangalia mitaji inayofanya uwekezaji huo uwepo. Manufaa yanayotegemewa kutokana na faida baada ya uwekezaji (kama ajira, malipo ya kodi, mapato ya mauzo ya nje na technlogia mpya) hayatabiriki na kwa kiasi kikubwa inategemea ujanja wa mwekezaji. Pia sio rahisi kupimika na kuyaweka bayana. Tutakachokifanya ni kuweka mikakati ya kuanza kutoa misamaha kwa kuangalia faida tutakayopata kama sehemu ya mitaji ya uwekezaji kwani hii inatabirika na ni rahisi kipima kama inalingana na misamaha

tunayotoa. Mfano ni utoaji wa hisa zisizolipiwa kwa kutumia rasilimali, kutengeneza miradi ya *(Corporate Social Responsibility)*miradi ya uwajibikaji wa wawekezaji wa jamii wa Taifa kama asilimia ya uwekezaji, Kununua bidhaa iliyotengenezwa ndani kama asilimia ya mtaji wa uwekezaji, kutumia asilimia kubwa ya bidhaa za uzalishaji kupitia kampuni za kitanzania na kuajiri Watanzania katika nafasi zilizoajiri wageni kwa muda mahsusi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010, Serikali imekamilisha maandalizi ya msingi ya kuanzisha Kitengo cha Uratibu wa Masuala ya Ubia *(PPP-Coordination Unit*) kwenye Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* na Kitengo cha Fedha *(PPP-Finance Unit)* kwenye Wizara ya Fedha. Mapendekezo ya miradi yenye uwezekano wa kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP* yamewasilishwa katika Kitengo cha Uratibu na yanafanyiwa kazi ili kuainisha inayokidhi vigezo vya Sheria na hatimaye kufanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi ni uamuzi wa makusudi unaojumuisha hatua mahsusi zinazochukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuinua uelewa, ujuzi, elimu ya ujasiriamali pamoja na kuwawezesha Watanzania kumiliki rasilimali na kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi. Aidha, uwezeshaji wananchi kiuchumi ni dhana pana ambayo inahitaji wananchi kutambua fursa mbalimbali zinazowazunguka na kuzitumia fursa hizo kujikwamua kiuchumi. Jukumu la Serikali ni kuandaa na kuboresha

Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu ili kumwezesha mwananchi kutumia fursa hizo. Ili kufaidi matunda ya kukua kwa uchumi, mwananchi mmoja mmoja ana jukumu la kujiendeleza, kufanya kazi kwa bidii na kwa tija. Aidha, ieleweke kwamba uwezeshaji si kumnyang'anya aliyenacho na kumpa asiye nacho; bali ni kumwezesha asiye nacho ili aweze kujikwamua kiuchumi; hivyo ni lazima kuwapa wananchi wote fursa sawa ili waweze kujitegemea. Jitihada hizi kama wananchi wataziunga mkono zitapunguza tofauti kubwa ya vipato ambayo ipo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo, Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004. Sera ya Uwezeshaji imeelekeza kuanzishwa kwa Taasisi za kutekeleza Sera hiyo kama vile Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, popote zilipo Wakala wa Dhamana za Mikopo, Wakala wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara ndogo, Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali, Kituo cha Uendelezaji Masoko, Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Uanzishwaji wa Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeanzisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kwa kuwa Uwezeshaji ni suala mtambuka, majukumu ya msingi ya Baraza ni kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli zote za Uwezeshaji Kitaifa zinazotekelezwa na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta Binafsi. Aidha, Serikali imeimarisha Wakala wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

*(SIDO)* kama Sera inavyoelekeza. Vilevile, majukumu ya Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali yanatekelezwa na Kituo cha Kuendeleza Ujasiriamali cha Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam na majukumu ya Wakala wa Dhamana za Mikopo yanatekelezwa chini ya Benki Kuu ya Tanzania. Mchakato wa kuanzisha Benki ya Kilimo umefikia hatua nzuri, ambapo kwa sasa majukumu yake yanatekelezwa kupitia Dirisha la Kilimo lililofunguliwa kwenye Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*).

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Mifuko mbalimbali kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Sheria yake, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni Chombo cha Kitaifa kitakachosimamia, kufuatilia na kuratibu shughuli zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Serikali inaangalia uwezekano wa kuweka baadhi ya Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama ilivyo kwa Zambia ambapo Mifuko yote ipo chini ya Mfuko wa *Citizen Empowerment Fund.* Hii itarahisisha uratibu na tathimini ya matokeo ya jitihada za Serikali na kuondoa muingiliano wa majukumu na kuwepo kwa Mifuko inayofanya shughuli zinazofanana kwa walengwa wale wale.

Mheshimiwa Spika, jitihada nyingine za Serikali katika kuwawezesha wananchi ni kuweka mazingira wezeshi ambayo ni pamoja na kuimarisha uchumi jumla, kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii, kuboresha huduma za Serikali; kuimarisha upatikanaji

wa mitaji; kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu; kuboresha na kuimarisha masoko; kuimarisha Ushirika na kuhakikisha Ardhi inawanufaisha wananchi. Aidha, Serikali inatekeleza Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini *(Roadmap for Improvement of Business Environment and Investment Climate in Tanzania).* Mpango huo umeandaliwa kuiwezesha Serikali kutoa huduma za msingi kwa Sekta Binafsi kwa kuondoa vikwazo na urasimu unaotokana na Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za Kiutawala zinazokwamisha biashara na uwekezaji nchini. Lengo ni kupunguza gharama na muda unaotumika katika uanzishaji, uendeshaji na ufungaji wa biashara. Urasimu ni dhana ya kuwezesha, kurahisisha na kufanikisha juhudi. Urasimu si dhana ya kukwamisha.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya sekta binafsi. Serikali inaratibu jitihada za kuyaleta pamoja makundi mbalimbali ya sekta binafsi chini ya Taasisi ya Sekta Binafsi (*TPSF)* ili kuwa na sauti moja katika kufanya majadiliano na Serikali. Serikali itaendelea na majukumu yake ya kuweka mazingira wezeshi, kujenga miundombinu ya kiuchumi, kusimamia sheria za nchi na kulinda raia na mali zao. Serikali pia inaendelea na maandalizi ya Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi Tanzania. Aidha, Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya yatatumika katika kubaini mahitaji ya Sekta Binafsi na kufanya tathmini ya gharama za kufanya biashara kwa baadhi ya Mikoa ili uzoefu utakaopatikana utuwezeshe kutambua sababu za kuongezeka kwa gharama za kufanya biashara na

kuwekeza nchini na hatua za kuchukua kupunguza gharama hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Ushindani wa Sekta Binafsi, Tanzania imechaguliwa na imekubali kuwa mwenyeji wa mkutano wa Kimataifa ujulikanao kama *"International Smart Partnership Dialogue 2013"* unaotarajiwa kufanyika hapa nchini mwezi Mei 2013. Mikutano ya aina hii hufanyika karibu kila mwaka ikijumuisha Viongozi wa Serikali, Wafanyabiashara, Waandishi wa Habari, Vijana, Wanawake na Sekta Binafsi kwa ujumla. Lengo la mikutano hiyo ni kupanga mikakati ya kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kuwashirikisha wananchi wa matabaka yote.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika eneo la Uwekezaji, Uwezeshaji na Maendeleo ya Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, iliyotolewa Mhe. Andrew John Chenge (Mb.). Serikali ifanye tathmini ya fedha za mikopo inayotolewa kupitia mifuko mbalimbali ili kuona kama malengo yaliyokusudiwa yamefikiwa ikiwemo wakopaji kurudisha fedha ili wengine wakope. Aidha, Serikali iweke msisitizo katika kuhamasisha uwekezaji na uwezeshaji kwenye Sekta ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji ambazo zinaajiri na kutegemewa na Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza mchakato wa kutathmini Mifuko mbalimbali ya uwezeshaji ikiwa ni

pamoja na kuitaka Mifuko husika kutoa taarifa za kila robo mwaka zitakazoainisha kiasi cha mikopo iliyotolewa, idadi ya wananchi waliofikiwa, shughuli au miradi iliyolengwa na mikopo inayorejeshwa. Kiwango cha urejeshwaji wa baadhi ya mikopo iliyotolewa ni cha kuridhisha. Mfano, hadi mwezi Aprili 2012 kiwango cha urejeshaji katika Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kilikuwa asilimia 96, Mpango wa Uwezeshaji Wananchi na Kuongeza Ajira *(JK Fund)* asilimia 78, *TASAF* asilimia 91, *SELF* asilimia 91.4, na Mfuko wa Pembejo za Kilimo asilimia 73.

Mheshimiwa Spika, kamati imeelekeza Serikali iimarishe usimamizi wa utekelezaji wa Sera, Sheria, Programu, Mikakati na Mifuko mbalimbali yenye lengo la kuwawezesha kiuchumi wananchi wengi zaidi wenye kipato cha chini. Aidha, Serikali iwe makini katika kutoa mikopo kwa Sekta Binafsi kwa kuhakikisha inaelekezwa kwenye maeneo ya wananchi wenye kipato cha chini badala ya kuielekeza kwa wafanya biashara wachache.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa uwezeshaji unafanyika kupitia Sera, Sheria, Programu na Mikakati mbalimbali katika sekta za kiuchumi na kijamii ambapo kimsingi Serikali inaweka mazingira wezeshi kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo. Serikali itahakikisha kwamba mfumo wa Sera, Sheria, Programu na Mifuko inazingatia uwezeshaji wa wananchi wenye kipato cha chini. Aidha, Serikali imeanzisha mifuko mbalimbali inayotoa mikopo au ruzuku kwa wananchi wenye kipato cha chini. Kwa mfano, chini ya Mradi wa Kukuza Ushindani

wa Sekta Binafsi kupitia Programu za Kuchangia Mitaji *(Matching Grants Programme)* na Fanikiwa Kibiashara *(Business Development Gateway);* Serikali imewawezesha wajasiriamali wadogo wapatao 4,500 kwa kuwapa mafunzo ya ujasiriamali na mipango yao ya biashara kushindanishwa. Kati yao wajasiriamali 2,780 walishinda na kupewa ruzuku ya mbegu mtaji. Aidha kiasi cha shilingi bilioni 9.9 zilitolewa kwa washindi hawa hivyo kuwawezesha kuboresha biashara zao, kuongeza kipato, kukuza ushindani wao na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kusisitiza Serikali itoe taarifa kuhusu jitihada zinazoendelea za kuwawezesha wananchi kiuchumi pamoja na jitihada za serikali katika kuongeza wataalam wa mikopo pamoja na usimamizi wa mikopo hiyo ili kuhakikisha inawafikia walengwa. Serikali inafanya juhudi mbalimbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kusimamia mifuko mbalimbali ya uwezeshaji. Mifuko hiyo ni pamoja na *TASAF, SELF*, Mwananchi *Empowerment Fund* (*MEF*), Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira *(JK Fund),* Mpango wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo ya Nje *(ECGS),* Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF)* n.k. Aidha, hadi kufikia Aprili 2012, jumla ya mikopo iliyotolewa kupitia mifuko hii ni shilingi bilioni 1,077.93. Hii inadhihirisha wazi kuwa Serikali imedhamiria kwa dhati kuwawezesha wananchi wake kiuchumi. Aidha, Serikali haitoi mikopo hii moja kwa moja bali inaweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na kuadhamini mikopo hiyo kupitia mabenki na taasisi za fedha. Hivyo, mikopo hiyo hutolewa kwa kufuata

taratibu za benki na Taasisi ya fedha husika. Taasisi mbalimbali zinaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali ambayo yanajumuisha utumiaji mzuri wa mikopo na ulipaji wake. Vilevile, Taasisi mbalimbali za Kifedha zinatoa mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa Maafisa Mikopo ili waweze kusimamia mikopo husika vizuri.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetaka kuwa elimu inahitajika kutolewa kwa wananchi wengi ili waelewe na kushiriki kikamilifu katika ujasiriamali, uwekaji wa akiba, uwekezaji na kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali linaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kujenga tabia ya kuweka akiba na kuwekeza kwenye miradi yenye tija. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaendelea na uhamasishaji, uanzishwaji na uimarishaji wa Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na *SACCOS*. Aidha, Baraza la Taifa la Uwezeshaji likishirikiana na wadau limetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa maseremala, wafugaji nyuki na mafundi wa ushonaji ili kuwaongezea ujasiri wa kuthubutu kuanzisha miradi na kuzalisha bidhaa zenye viwango. Mafunzo kama hayo pia yanaendeshwa na Taasisi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesisitiza hasa Mheshimiwa Devota Likokola, (Mb.) kuwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi lianzishe Dawati Maalumu kwa ajili ya kuratibu shughuli za *VICOBA* (*Village Community Banks).* Kikao cha wawakilishi wa

*VICOBA* kujadili na kukubaliana utaratibu wa pamoja wa usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji wa *VICOBA* kwa lengo la kuboresha usalama wa fedha za wananchi kilifanyika mwezi Septemba 2011. Kikao cha pili cha kuhitimisha mchakato huo kitafanyika kabla ya mwisho wa mwaka 2012 ambapo suala la kuanzisha dawati maalumu pamoja na taratibu zitakazozingatiwa katika kuratibu shughuli za *VICOBA* litafanyiwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi kupitia kwa Mheshimiwa Andrew Chenge (Mb) na Msemaji na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mb). Wameshauri Serikali ihimize uwezeshaji wananchi kiuchumi na Serikali iangalie namna ya kuiunganisha mifuko ya uwezeshaji ili kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuongeza tija kwa wanufaika na fedha zinazotolewa na Serikali kwa mifuko hiyo yote.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuangalia uwezekano wa kuunganisha baadhi ya mifuko ya uwezeshaji ambayo ni midogo midogo na inafanya kazi zinazofanana ili iweze kuwa kwenye mfuko mmoja ambao utakuwa chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Utaratibu huu utapunguza gharama za uendeshaji wa mifuko na utaweza kuwa na tija zaidi kuliko ilivyo sasa. Katika kufanikisha azma hii, mwezi Oktoba 2011 Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliandaa mkutano uliokutanisha mifuko yote ya uwezeshaji. Mkutano uliazimia kuwa uchambuzi ufanyike ili kuunganisha mifuko inayofanya shughuli

zinazofanana na pia mifuko itoe taarifa za utekelezaji kila robo ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer (Mb.) – Longido ametoa hoja kuwa Fedha za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi maarufu kama mabilioni ya JK kiasi cha Sh.250, 000,000/= zilizotolewa kwa Wilaya ya Longido bado ziko Benki hazijatumika. Serikali ieleze ni kwa nini na ihakikishe inawakopesha walengwa fedha hizo mara moja.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi na Kuongeza Ajira *(JK Fund)* zipatazo shilingi milioni 250 zilitolewa kwa ajili ya Wilaya ya Longido. Fedha hizo zinakopeshwa kupitia Taasisi ya *PRIDE TANZANIA Ltd.* ambapo jumla ya Shilingi milioni 110.0 zimekopeshwa kwa *Longido SACCOS* (milioni 50.0) na vikundi vya wanawake (milioni 60.0). Fedha zilizobaki zinaendelea kukopeshwa.

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kuwa Fedha za uwezeshaji shilingi bilioni saba zilizotolewa kama mabilioni ya JK zipelekwe pia Zanzibar. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mheshimiwa Hamad Yusuph Massauni (Mb.)

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu, aya ya 32, ukurasa wa 20 imetajwa kuwa Mfuko wa Mwananchi *Empowerment Fund (MEF)* umetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 7.3. Kwa hiyo, mikopo hiyo haijatolewa chini ya Mpango wa *JK Fund.* Mpaka sasa mikopo hiyo imetolewa kwenye Mikoa tisa chini ya udhamini wa *MEF* kwa benki ya *CRDB* ambayo

imeweza kutoa mikopo mara tatu ya fedha zilizotolewa na Serikali za jumla ya shilingi bilioni 2.2. Kutokana na ukweli kwamba hivi karibuni Benki ya *CRDB* imefungua Tawi Darajani-Zanzibar, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi litaangalia uwezekano wa kupeleka mikopo hiyo Zanzibar pia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles J. Mwijage (Mb), Mheshimiwa Ester Bulaya (Mb) na Mheshimiwa Moza Abedi Saidy (Mb.), wameishauri Serikali iwasaidie wakulima wengi vijijini kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hususan kuwapatia zana za kisasa na pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unaendelea kuwawezesha wakulima na Wajasiriamali wengine hatua kwa hatua katika maeneo mbalimbali ya nchi kutegemeana na Mfuko unavyopatiwa fungu la maendeleo. Hadi Aprili 2012, Mfuko ulikuwa na Shilingi bilioni 2.2 ambazo tayari zimedhamini mikopo ya Shilingi bilioni 7.3 kupitia benki ya *CRDB*. Mikoa iliyonufaika ni Dodoma, Lindi, Manyara, Mtwara, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Singida na Tanga. Kati ya Wajasiriamali walionufaika na mikopo hiyo, 7,187 wametumia mikopo hiyo kwenye zana za kilimo, pembejeo na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege (Mb.) na Mheshimiwa Devotha Likokola (Mb) wametoa hoja kuwa pamoja na Serikali kutoa fedha za uwezeshaji jumla ya shilingi bilioni 7.3 kwa Mikoa 9 ukiwemo Mkoa wa Rukwa, lakini wananchi wa Jimbo la Kalambo hawajanufaika na

fedha hizo. Ni vyema Wabunge wawe wanapewa taarifa sahihi kuhusu utekelezaji wa mipango kama hii kwenye Majimbo yao. Aidha, katika kuwawezesha wananchi kupitia utaratibu wa *VICOBA*, ni vyema Serikali ihakikishe kwamba elimu ya ujasiriamali inaenezwa kwa Mikoa yote hasa kipaumbele kitolewe kwa Mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, mikopo inayodhaminiwa na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi (*MEF*) kupitia benki ya *CRDB* haitolewi kwa utaratibu wa Majimbo bali hupitia Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* au vikundi vingine vya kiuchumi. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu wahamasishe wananchi katika Majimbo yao kujiunga na *SACCOS* au vikundi vingine vya kiuchumi kuwawezesha kuomba mikopo wanayohitaji kupitia benki ya *CRDB*. Aidha, Serikali inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuendelea kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kuanzisha vikundi vya kiuchumi kama *VICOBA*.

Mheshimiwa Spika, hoja imetolewa na Mheshimiwa Andrew John Chenge (Mb.) na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Serikali ifanye utafiti wa kina kuhusu faida na hasara inayotokana na misamaha ya kodi kwenye miradi inayosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali hivi sasa *TIC* inaendelea na utafiti kuhusu misamaha ya kodi kwa wawekezaji waliosajiliwa. Utafiti huu

umetengewa fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 na utakapokamilika taarifa yake itatolewa.

Mheshimiwa Spika, Mheshiniwa Andrew John Chenge (Mb.) na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, amesisitiza Michango ya Wawekezaji kwa Jamii *(Corporate Social Responsibility)* iwekewe kiwango cha asilimia fulani ya thamani ya uwekezaji au faida badala ya kutegemea hisani ya mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali haina Sheria inayowataka Wawekezaji kuchangia maendeleo ya Jamii kupitia Michango ya Hisani kwa Jamii *(Corporate Social Responsibility).* Hata hivyo, tunatambua michango ya makampuni mbalimbali mfano *Barrick Gold Mine, CRDB Bank Plc, TBL, IPP Media, SIGARA, NMB, Twiga Cement* na *VODACOM* na tunahimiza Makampuni mengine kuiga mifano hii kama njia ya kutengeneza mahusiano bora na jamii, kupanua soko na hatimaye kujipatia faida zaidi. Hata hivyo, kama nilivyosema hapo awali, Serikali itafanya utafiti kupata uzoefu wa nchi za Angola na Norway kwa lengo la kushawishi wawekezaji wachukulie suala hili kama jambo la lazima.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya fedha na Uchumi imisisitiza Serikali itenge fedha ili kuwezesha upembuzi yakinifu wa miradi ya *PPP* kufanyika katika ngazi ya Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 pamoja na

Kanuni zake za mwaka 2011 imeelekeza kuwa Wizara, Taasisi na Serikali za Mitaa zina jukumu la kufanya upembuzi yakinifu wa miradi yenye uwezekano wa kutekelezwa kwa mujibu wa Sheria hiyo. Kwa hivyo, ni jukumu la Mamlaka za Serikali kupanga na kuainisha mradi itakayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kufanya upembuzi yakinifu katika Bajeti zake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sylivester Maselle Mabumba (Mb.) ameshauri Serikali iendelee kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na miundombinu ya uhakika ya umeme. Mabenki nayo yawawezeshe wawekezaji wa ndani kwa mikopo ya riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo inatekeleza Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na uwekezaji *(Roadmap for Improvement of Business Environment and Investment Climate in Tanzania).* Mpango huu unaiwezesha Serikali kutoa huduma za msingi kwa sekta binafsi kwa kuondoa vikwazo na urasimu unaotokana na sera, sheria na taratibu za kiutawala zinazokwamisha biashara na uwekezaji nchini. Lengo ni kupunguza gharama na muda unaotumika kuanzisha na kuendesha biashara. Vilevile, Serikali kupitia Wizara zake inazingatia umuhimu wa kuimarisha miundombinu ya kiuchumi kama vile barabara, reli, bandari, usafiri wa anga, mawasiliano, nishati, elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Amina Amour (Mb.) ameshauri Serikali ipime maeneo ya uwekezaji na kuainisha miradi kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na OWM – TAMISEMI imeandaa utaratibu wa kuainisha maeneo ya uwekezaji ili yapimwe kwa ajili ya uwekezaji wa ndani na nje. Hatua hii itategemea upatikanaji wa fedha za kupima ardhi katika kila Mkoa ulioainisha maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Yusuph Masauni (Mb) ameshauri Serikali ifanye utafiti wa kina kuhusu sera na sheria za uwekezaji ili kuhakikisha kuwa hakuna mianya ya upotevu wa fedha kwa kisingizio cha misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika utangulizi, wawekezaji hulipa kodi nyingine zote zikiwa ni pamoja na za forodha na *VAT* kwa vifaa ambavyo havijaorodheshwa kama vifaa vya mtaji (*Deemed Capital Goods).* Kodi hulipwa hata katika kipindi cha uanzishwaji wa miradi na hivyo kufanya misamaha inayotolewa kuwa kiasi kidogo kulinganisha na kodi zinazokusanywa kutoka kwa wawekezaji. Aidha, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi na kufanya utafiti kuhusu umuhimu na kiwango cha misamaha hiyo kwa bidhaa za mtaji kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (Mb.) ametoa hoja kwamba Serikali ifanye tathmini ya kina ya aina ya wawekezaji na kiasi halisi walichowekeza badala ya kile kilichoandikwa kwenye mchanganuo wa biashara tu.

Mheshimiwa Spika, fedha za tathmini hii zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha. Jukumu hili litafanyika kwa kushirikiana na Taasisi ya Takwimu ya Taifa (*National Bureau of Statistics)* pamoja na Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* ina utaratibu wa kutembelea miradi iliyosajiliwa na *TIC* ili kuihakiki kwa kuzingatia mikataba ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hoja imetolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (Mb.) kwamba Serikali ilete Bungeni orodha ya miradi ya *PPP* ambayo imepewa wawekezaji na ambayo inatakiwa kupewa wawekezaji na utaratibu wa wazi wa kuwapata hao wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Kitengo cha Uratibu *(PPP Coordination Unit)* na Kitengo cha Fedha *(PPP Finance Unit)* kama hatua muhimu za utekelezaji wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010. Wizara zimewasilisha katika Kitengo cha Uratibu miradi inayopendekezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Miradi iliyopokelewa ni pamoja na ujenzi wa barabara za Dar es Salaam-Chalinze na Arusha-Himo; ujenzi na upanuzi wa Bandari za Mwanza, Mbegani, Mwambani na Mtwara; ukarabati wa Viwanja vya

ndege vya Mwanza, Kilimanjaro, Mtwara na Arusha; Uboreshaji wa Reli kutoka Dar es Salaam-Isaka na Tanga-Arusha; Ujenzi wa Reli kutoka Arusha-Musoma na Mtwara-Mchuchuma; Ujenzi wa Bandari ya Nchi Kavu *(Kisarawe Cargo Freight Station)* na Ujenzi wa Majengo kwa ajili ya ofisi, Biashara na mabweni kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha. Aidha, baada ya uchambuzi kufanywa na Kitengo cha Uratibu, Wizara zitatakiwa kuandaa na kuwasilisha upembuzi yakinifu kwa mujibu wa Sheria ya *PPP* na Kanuni zake. Taratibu za kutangaza zabuni kwa uwazi na ushindani kulingana na Sheria ya *PPP* na ya Ununuzi wa Umma ili kupata Wawekezaji zitafanyika baada ya Miradi kupitishwa na Kitengo cha Fedha.

Mheshimiwa Charles J. Mwijage (Mb) na Wabunge wengine wengi wametaka Mheshimiwa Waziri wa Nchi ahakikishe Uwezeshaji unafikia makundi mbalimbali katika maeneo yao. Rai hii naipokea kwa moyo mkunjufu na kwa kuanza nimeonyesha mfano katika Jimbo langu la Hanang kuwezesha vikundi mbalimbali kupata mikopo ya matrekta yaliyotolewa na *TIB* kwa kushirikiana na *PASS,* nachukua nafasi hii kuwashukuru pia na mikopo mingine kama pikipiki, vyerehani na vinginevyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza niseme kabisa naunga mkono hoja hii ambayo imewasilishwa hapa Mezani na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kufanya kazi za Serikali na za Kibunge kwa ufanisi. Lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini tena na kunibakiza katika nafasi hii ili niweze kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Namshukuru sana Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo yake na miongozo yake na ushauri wake na kutulea sisi Mawaziri ambao tunafanya kazi chini yake. Tunamshukuru sana na tunafarijika na tunafaidika sana na ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu ambao tuko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Manaibu Mheshimiwa Majaliwa na *caterpillar* Mheshimiwa Mwanri, mimi huwa naliita *caterpillar* hili. Tunashukuru sana lakini pia tunawashukuru watendaji walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu wakiongozwa na Mheshimiwa Peniel Lyimo, Katibu Mkuu na kule TAMISEMI yuko Mheshimiwa Hussein Katanga, lakini na Manaibu Katibu Wakuu na Wakurugenzi wote, kwani bila wao, hata haya tunayoyasoma hapa yasingewezekana. Kwa hiyo tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pia kutokana na majukumu yangu, ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa ushirikiano wake mkubwa sana na uendeshaji bora wa Bunge hili. Naibu Spika, Wenyeviti pamoja na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kisekta,

Wajumbe wa Tume na Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ambapo katika vikao hivyo vyote mimi ni Mjumbe kwa niaba ya Serikali. Nawashukuru sana kwa ushirikiano ambao tumepeana katika vikao mbalimbali na kushirikiana katika shughuli mbalimbali za Kibunge. Lakini naishukuru sana Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa busara na hekima zao kwa kutuwezesha kupitisha bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Vitengo vyao vyote na ushauri wao wote walioutoa, nataka kuwahakikishia kwamba tutauzingatia.

Mheshimiwa Spika, pia kwa utamaduni wa Kibunge, Bunge hili lina sehemu ya Serikali na Kambi ya Upinzani. Kwa nafasi niliyonayo mimi nalazimika kufanya kazi karibu na Kambi ya Upinzani kwa sababu ndio utamaduni wa Kibunge. Kwa sababu hiyo na kwa kufanya kazi, hivyo napata ushirikiano mzuri sana na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mbowe. Namshukuru sana na kwa sababu naye ni Mjumbe wa Tume ya Bunge na Kamati ya Uongozi kwa nafasi yake ya uongozi kama mimi ninavyowakilisha Serikali.

Mheshimiwa Spika, namshukuru vilevile *Chief Whip* wa Upinzani Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Zitto ambaye ndiyo Naibu Kiongozi wa Upinzani Rasmi. Hawa wote nawashukuru kwa ushirikiano na mashauriano kadhaa yanayosaidia katika kuendesha Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi kuliko yote, niishukuru sana Kamati ya Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi. Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ndio imekuwa mhimili wa utendaji wa

Serikali humu ndani. Yale yote tunayoyafanya, tunayoyasema, tunashauriwa kwa karibu sana na Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Tunawashukuru sana kwa sababu sisi wote tuliopo Serikalini tunatekeleza sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa hiyo ni wajibu wenu kutushauri. Hii ni Serikali yenu na ninyi mna wajibu wa kutushauri, kutusema hata kusema lolote ili mradi tu mhakikishe kwamba Serikali inaendelea kuchapa kazi na kutimiza wajibu wake vizuri. Kwa hiyo, naishukuru sana Kamati hii ya Wabunge wa CCM na watu wasishangae kwa sababu ndio utaratibu wa Wabunge kufanya kazi na *caucus* za vyama hata wenzetu wanafanya kazi na *caucus* zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu na wote wanajua kwamba kama *Chief Whip* sitokitoki hapa, miezi miwili na nusu sasa, fikirieni kazi yenyewe hiyo ya kukaa miezi miwili na nusu ilivyo. Lakini hawa jamaa wamekuwa wakinivumilia, mke wangu ananivumilia sana anaitwa Germina Lukuvi, watoto wangu Nobert, Brown na Anifisye wananipa moyo sana, nazungumza nao mara tatu kila siku na wameshanivumilia kidogo kwa sababu kazi hii wameizoea kwa sababu nimeanza tangu mwaka 2000, lakini kidogo napata nafasi ya kuwatembelea na kesho nitakwenda kuwatembelea vilevile. Kwa hiyo nashukuru sana kwa fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda niwashukuru ndugu zangu na wananchi wa Jimbo la Ismani walioniweka hapa tangu mwaka 1995. Hapa sitaki kutoa siri nawafanyia nini maana yake siasa ni

ushindani, lakini wajue yale yote yatatekelezwa. Hawanioni huko lakini hata ninayoyafanya hapa ni kwa heshima yao, bila ya kura zao nisingefika hapa. Kwa hiyo wajue kwamba mimi nafanya kazi zao, najua wanapata matatizo, kuna watu wanapitapita huko wanasemasema hivi na vile lakini nampongeza sana hapa mbele ya Bunge Mwenyekiti wa Kijiji kimoja kinaitwa Makatapora ambaye alimkatalia Mbunge mmoja wa Viti Maalum pale ambaye alilazimisha kufanya mkutano akamwambia mimi ndio Mwenyekiti wa Serikali hufanyi mkutano hapa akakataa. Kwa hiyo, namshukuru sana kwamba ameonyesha ujasiri na kuonyesha kwamba yeye ndio mwenye Serikali. Kwa hiyo yule Mbunge alilazimisha akamsumbuasumbua lakini mwisho wa yote hakufanya mkutano pale kwa sababu Mwenyekiti wa Serikali alimkatalia kwa sababu alikuja bila kibali rasmi cha kufanya mkutano. Sasa nawaomba wote wanaokwenda namna hiyo, wajue zile Serikali za Vijiji ni Serikali kamili, lazima mzitii. Kwa hiyo namshukuru sana Mwenyekiti wa Kijiji cha Makatapora, nitakwenda kumwona hivi karibuni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu, hoja zilizotolewa kwa Waheshimiwa Wabunge ni nyingi na kama utamaduni ulivyo sisi tutajitahidi kama waratibu wa shughuli za Serikali kuhakikisha kwamba hoja zote zile ambazo zimetolewa kwa sekta mbalimbali maana hoja hizi zimetolewa kwa Waziri Mkuu kama mratibu wa shughuli za Serikali. Kwa hiyo, tutahakikisha wenzetu na tumeshawapelekea hoja zote ili wazitumie kujibu katika Wizara zao lakini pia na sisi tunajua hatuwezi kutosheleza mahitaji yote ya

majibu, tutazijibu hoja hizi kwa maandishi vilevile kama watakavyofanya wenzetu Mawaziri wa Kisekta. Kwa hiyo, hakuna hata hoja moja itakayopuuzwa.

Mheshimiwa Spika, yaliyozungumzwa ni mengi na kwa sababu ya muda, nitazungumzia machache kuhusu ucheleweshwaji wa vitabu kuwasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge, kupunguza matumizi ya Serikali, nitazungumzia kidogo Masuala ya Uratibu wa Maafa, Udhibiti wa UKIMWI, Tume ya Uchaguzi, Usajili wa Vyama vya Siasa, Masuala yanayohusu Bunge, Maadhimisho ya Taifa, Dawa za Kulevya, Udhibiti wa Matumizi wa Fedha za Umma, Ustawishaji Makao Makuu na Masuala ya Uratibu wa Shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi nianze kwa kuipongeza tena Kamati ya Kisekta ambayo ilitoa ushauri mwingi sana chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi Chana na Makamu wake. Nataka kuwaahidi kwamba ushauri wote nitauzingatia, lakini jambo moja walilosema ni kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka huu imechelewa kupeleka vitabu. Tunakiri kweli tumechelewa kupeleka vitabu vya hesabu, lakini tuliomba radhi kutokana na sababu mbalimbali ambazo hazikuweza kuzuilika. Tulichelewa na tunashauriana na Mheshimiwa Spika ili ikiwezekana utaratibu huu ubadilishwe kidogo, vitabu viweze kupatikana mapema na mijadala ya bajeti iweze kufanyika mapema sio kwa kukimbizana kama hivi ilivyo sasa. Kwa hilo limefanyika na ni kweli tunakiri, lakini tusingeweza kufanya nje ya utaratibu ule tulioufanya.

Mheshimiwa Spika, lakini hoja ya pili, ilizungumzwa…

**SPIKA:** Vitabu vya Makadirio sio vya hesabu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, vitabu vya makadirio, hizo *Volume I, II, III* na *IV* ndivyo vilivyochelewa.

Mheshimiwa Spika, pili, ilizungumzwa kuhusu gharama za pango, lakini zaidi ilizungumzwa Ofisi mbalimbali za Serikali ambazo zinapanga. Kwetu sisi hasa Tume ya Uchaguzi na Ofisi nyingine ambazo zinapanga, ukweli ni kwamba tunafanya utaratibu wa kuvipatia viwanja Idara mbalimbali za Serikali ili ziweze kujenga lakini kutokana na mpango huu tulionao wa miaka mitano na mpango wa mwaka mmoja, shughuli hizi za ujenzi wa Ofisi haziko kwenye vipaumbele vya awali. Kwa hiyo, kwa muda mfupi huu wa sasa wataendelea mpaka tutakapomaliza ile mipango ambayo tumejipangia katika mpango wetu wa miaka mitano, lakini tunaamini kwamba ipo siku Idara zote hata Idara ya Tume ya Uchaguzi itapata jengo lake.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni maafa, kwamba Idara ya Maafa ijengewe uwezo, Serikali itafute njia mbadala ya kusafirisha chakula kutoka kwenye maghala ya hifadhi ya chakula kwenda kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula nchini na tathmini ya kubaini maeneo yenye upungufu yafanyike. Serikali ihakikishe zoezi la kuwalipa fidia wafugaji walioathirika na ukame Loliondo, Ngorongoro

na Monduli unakamilika. Serikali iboreshe utaratibu wa malipo ya wahanga wa mabomu wa Mbagala hususan kule Mkoani Dar es Salaam. Maelezo ni kwamba Serikali imeshaanza kuujengea uwezo Idara ya Maafa kwa kujenga maghala ya kuhifadhi vifaa katika kanda tano (5) za Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Shinyanga na Dar es Salaam. Vifaa vingi vya maafa vya dharura huwa tunaweka katika maeneo hayo ili kupunguza umbali wa kuchukua vifaa hivyo kutoka Dar es Salaam lakini pia mchachato wa kutunga sheria mpya kuhusu Idara ya Maafa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu Mbagala, Serikali imechukua jukumu la kulipa fidia yote na wale wote ambao walikuwa wanadai fidia ya nne kwa orodha ambayo imefanyiwa tathmini hivi sasa Mkoa wa Dar es Salaam wanalipa. Tumewapa shilingi 2,200,000,000/= wanamalizia kulipa, wale wote ambao hawajalipwa na wale wa Gongo la Mboto nimezungumza nao jana na nimewaahidi kwamba nikirudi Dar es Salaam tutaonana na wote ambao wana madai halali yamehakikiwa yanayohusiana na maafa ya Mbagala na Gongo la Mboto, Serikali itayalipa ili mradi yamehakikiwa na ni malipo halali. Serikali hii haiwezi kudhulumu haki ya mtu, kwa hiyo tutalipa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usombaji wa chakula, Serikali sasa imeanza kuchukua hatua mbadala kusafirisha chakula kutoka kwenye maeneo yenye upungufu kwa kutumia magari ya Jeshi. Zamani tulikuwa tunatumia treni kwenda Shinyanga, tatizo kubwa zaidi ni sehemu ya Shinyanga, ghala la Shinyanga halina chakula kwa sababu hakuna

barabara inayounganisha Rukwa kwenye chakula na pale Shinyanga. Kwa hiyo sasa tumechukua jukumu na bahati nzuri sasa mvua zimekatika pamoja na treni tunachukua na magari ya Jeshi ambayo yametusaidia sana. Tunalipongeza sana Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambao wametusaidia sana kusafirisha chakula kutoka Makambako, Njombe, Mpanda kwenda Arusha, sasa hivi tuna tani zaidi ya 7,000 pale Arusha, lakini pia sasa wameanza safari ya kupeleka chakula Shinyanga ili kihudumie katika ile kanda nyingine. Kwa hiyo, tunachukua jitihada, tunataka kuwahakikishia wenzetu wa Kanda ya Ziwa kwamba tutakuwa na chakula cha kutosha katika eneo lile la hifadhi la chakula.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nataka kuwahakikishia tena wale wote waliopatwa na maafa na kama nilivyosema yaliyofanyiwa tathmini tutayalipa lakini tunaendelea kufanya tathmini. Mwezi wa tatu tumeshafanya tathmini nyingine ya hali ya chakula na hali ikiruhusu, hali ikiwa mbaya na muda ukifika tutawahudumia chakula wale ambao wanahitaji msaada wa chakula kwa sababu kiongozi wetu wa nchi Mheshimiwa Rais alishaagiza kwamba hakuna mtu atakayekufa kwa njaa katika nchi hii. Madhali Serikali ya CCM inatawala, itahakikisha kwamba raia wake hawawezi kufa njaa. Kwa hiyo, tathmini tunayo wakati ukifika na ratiba tumeshapanga ya kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, eneo la UKIMWI, hoja zilikuwa Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya kondomu. Serikali ielekeze mikakati mbadala inayochukuliwa kuendeleza mapambano

dhidi ya maambukizi mapya ya UKIMWI. Serikali ifanye utafiti kujua ni kwa nini baadhi ya watu wanasambaza UKIMWI kwa makusudi. Maelezo ni kwamba Serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu matumizi sahihi ya kondomu kwa kutumia njia mbalimbali. Aidha, programu ya Tuko Wangapi ambayo imeanza hivi karibuni inaelimisha kuhusu madhara ya kuwa na wapenzi wengi. Serikali pia inaanzisha Mfuko wa UKIMWI utakaogharamia shughuli za kudhibiti UKIMWI. Suala hili limeulizwa sana na Mwanaharakati Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. Mfuko huo utatumika kugharamia programu za tiba ikiwemo ununuzi wa dawa, vifaa vya maabara, utunzaji wa yatima, udhibiti wa UKIMWI hususan vijana, udhibiti wa maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kuongeza upatikanaji wa matumizi ya kondomu. Kuhusu kufanya utafiti wa watu wanaosambaza UKIMWI kwa makusudi, ushauri umezingatiwa, hata hivyo hakuna takwimu zinazoonyesha kuwepo kwa matukio ya aina hiyo yaliyofikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la Bunge. Waheshimiwa Wabunge waliochangia eneo hili walikuwa na hoja zifuatazo. Utaratibu wa maswali papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu uboreshwe, muda wa kufanya kazi kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala uongezwe, Ofisi ya Bunge inunue mabasi mapya kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge, Makatibu wa Kamati Bunge wajengewe uwezo, tatizo la maegesho ya magari na upungufu wa kumbi za Mikutano Dar es Salaam lishughulikiwe, Ofisi ya Bunge iharakishe mchakato wa Wabunge kujiunga na Bima ya Afya, Ofisi za Wabunge Majimboni

ziongezwe watumishi, Serikali iharakishe uanzishwaji wa Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kwamba Kamati ya Bunge ya Kanuni inaangalia utaratibu mzuri utakaowezesha Wabunge kuuliza maswali bila usumbufu lakini pia Ofisi ya Bunge inafanyia kazi suala la muda wa uchambuzi wa Bajeti ikiwa ni pamoja na kuangalia upya ratiba za vikao vya Kamati za Bunge. Unaangaliwa pia uwezekano wa kuanzishwa kwa Kamati ya Bunge ya kushughulikia Bajeti. Hili alishasema Mheshimiwa Spika. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Bunge itanunua mabasi mpya manne kwa ajili ya kuhudumia Waheshimiwa Wabunge. Kuhusu tatizo la maegesho ya magari pamoja na upungufu wa kumbi za mikutano  kwa Kamati za Bunge katika Ofisi ndogo ya Dar es Salaam, Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na *NSSF* iko kwenye hatua za harakati za ujenzi wa ofisi mpya za Wabunge Majimboni pamoja na upanuzi wa ofisi ndogo ya Dar es Salaam. Waheshimiwa Wabunge, Tume yenu inaendelea kuzungumza na *NSSF* ili kuona kama upo uwezekano wa kujenga ofisi zote za Waheshimiwa Wabunge kwa mpigo badala ya kujenga ofisi mojamoja inachukua muda mrefu na inachukua fedha nyingi sana. Kwa hiyo mazungumzo hayo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makatibu wa Kamati wanaendelea kupewa mafunzo mbalimbali lakini Ofisi ya Bunge kupitia Tume ya Huduma za Bunge imeanza kufanyia kazi suala la Bima ya Afya kwa Wabunge ambapo mchakato wa kuwapatia Wabunge Bima hiyo umeshaanza. Aidha, Bima ya Maisha kwa

Waheshimiwa Wabunge kufuatia masharti yao ya kazi inashughulikiwa na Tume kwa kushirikiana na Hazina kulingana na Sheria ya Uendeshaji wa Bunge ya mwaka 2008 na taratibu za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge inaangalia uwezekano wa kuwa na watumishi wanne kuanzia mwaka wa fedha ujao kwa Wabunge wote yaani Katibu wa Mbunge, Mpiga Chapa, Dereva na Msaidizi wa Ofisi. Nataka wananchi wajue kwamba kunatofauti kati ya Mbunge na Ofisi ya Mbunge. Mbunge ni Ofisi, Mbunge ni taasisi kama alivyo Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya ana jina lake, Mkuu wa Wilaya ni mtu lakini ana ofisi. Kwa hiyo, Mbunge naye akichaguliwa ni Mbunge ndiyo Lukuvi lakini ana ofisi. Ile Ofisi yenu ile lazima iwe na wahudumu ambao watawahudumia ninyi, mkiwa na barua zenu, mkiwa na maswali waweze kuwajibu, waweze kuwa na watu wa kuwatumia ili mkifika pale hata kama Mbunge hayupo akute kuna watu wanaweza kupokea malalamiko yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Ofisi ya Mbunge nafikiri jambo hili litatekelezwa katika mwaka huu wa fedha ili kuhakikisha kwamba kila Ofisi ya Mbunge inakuwa na wahudumu wa msingi kwa mujibu wa masharti ya Mbunge. Pia mwaka huu wa fedha Serikali imetoa shilingi bilioni 10/- kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa ofisi za Wabunge. Hizi mtaziona kwenye vitabu vya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi, maswali ni kwamba Serikali kuhakikisha Tume inapata maghala

yake yenyewe, Serikali itenge fedha za kuboresha Daftari la Kudumu la Mpigakura, Tume itoe elimu zaidi kwa wapigakura pamoja na vyama vya siasa ili wasifanye fujo wakati wa uchaguzi, Serikali iijengee uwezo Tume ya Uchaguzi ili ijiimarishe hadi kwenye uchaguzi wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, maelezo hapa ni mafupi tu kwamba Serikali itafanyia kazi ushauri na maoni yaliyotolewa na kwa yale yanayohitaji fedha Serikali itaendeleza jitihada za kuipatia fedha Tume. Mwaka huu hatuna fedha nyingi za kuwapa lakini tunataka kufanya mazungumzo ili kuona yale maghala kwa sababu fedha nyingi sana Tume wanatumia kukodisha yale maghala wanapotunza vile vifaa, tunataka kuona kwa sababu yale maghala ni ya Serikali tuone kama tunaweza tukapunguza gharama ya Tume ili fedha zile zikatumika kwa shughuli nyingine. Yale maghala wasiyakodi, waazime, wayatumie, wayatunze ili fedha zile wanazolipa kodi zitumike katika shughuli zingine angalau kuanza kuboresha hili daftari kama zinaweza zikatosheleza. Lakini hilo tunaliangalia, ukweli ni kwamba fedha zinazotakiwa kwa Tume ya Uchaguzi ni nyingi lakini mtakumbuka vipaumbele vya mwaka huu hasa za maendeleo vimemaliza fedha zote lakini tunaendelea na kazi hii ya kuhakikisha kwamba Tume yetu tunaijenga kiuwezo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusu dawa za kulevya, Serikali ishughulikie suala la upungufu wa rasilimali watu pamoja na ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara, Serikali ipanue huduma ya tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya, vita ya dawa za

kulevya itangazwe kama janga la taifa, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na wafanyabiasha wa dawa za kulevya. Maelezo ni kwamba Serikali inakamilisha Sera na Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ambapo kitaanzishwa chombo kipya chenye nguvu na mamlaka ya kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini. Mnajua sasa kuna eneo, Tume iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu lakini Idara ya Polisi vilevile ina Idara inayopambana na madawa ya kulevya. Kwa hiyo, kutokana na uzoefu ambao umejengwa sasa, tunafikiri kwamba vyombo vyote vya dola lazima vishirikishwe lakini tuwe na chombo kimoja tu ambacho kitasimamia masuala yote yanayohusiana na madawa ya kulevya na hili tumepata uzoefu kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais baada ya kuunda *Task Force* ya Vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama ambavyo wanafanya pamoja ili kukabiliana na janga hili na ndiyo maana mnaona kasi ya ukamataji ni kubwa sana. Tumepata heshima ya kimataifa, Marekani na dunia nzima kwa kazi hii kubwa tunayofanya ya ukamataji ya madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo sasa madawa mengi yanakamatwa kwa sababu vyombo vyote vinashirikiana na tunapata taarifa za kutosha. Kwa taarifa yenu, timu hii ya *Task Force* imepewa heshima maalum na Marekani na waliitwa huko kupongezwa baada ya kumkamata gwiji mmoja, mama ambaye alikuwa anatafutwa katika nchi tano ambaye alikuja kukamatwa Dar es salaam kwa msaada na uwezo wa timu hii ya Watanzania wameweza kumkamata huyo mama na kumfikisha kwenye Vyombo vya Sheria. Kwa

hiyo, Tume hii inafanya vizuri kazi ya Serikali, sasa ni kuimarisha lakini tunaomba ushirikiano mkubwa wa wananchi ili kuwafichua hawa watu wote. Lakini pia pamoja na kuimarisha Tume, tunataka kurekebisha Sheria ili mgongano uliopo ndani ya Sheria zetu urekebishwe ili wanaopatikana na hatia hizi wafungwe, kusiwe na *option* ya faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya tisa, maadhimisho ya sherehe za taifa. Hoja hapa ilikuwa kwamba, kuna gazeti moja lilitangaza kwamba sherehe hizi za miaka 50 zimetumia shilingi bilioni 64. Sasa ukweli ni kwamba fedha zilizotumika ingawa tulipanga bajeti ya kutumia shilingi bilioni 30 kwa maadhimisho ya nchi nzima, kwa sababu tulipanga maadhimisho haya yaanze Wilayani, Mikoani na Kitaifa lakini ukweli ni kwamba tumekwenda kutumia shilingi 27.5 bilioni. Kwa hiyo, yale yote mmeyaona yamefanyika kila mahali, hapa, Zanzibar, Dar es Salaam na kila mahali tumetumia jumla shilingi bilioni 27.5. Kwa hiyo, ile ya kwamba shilingi bilioni 64 sio kweli, ni uongo na hata ile bajeti yenyewe tuliyokuwa tumeweka hatukuifikia. Sina muda wa kuwaeleza tumetumia kwa lipi, tutafafanua kwa baadaye na Jumatatu kutakuwa na swali hili na litaulizwa hapa Bungeni. Tuliambiwa tukanushe wakati ule lakini wakati mwingine uongo ukizidi sana si vizuri sana kujiingiza na kukanusha papo kwa papo kwa sababu mwongo ataendelea kuwa mwongo tu, utakanusha leo atazusha kesho. Kwa hiyo ukweli ni kwamba ni shilingi bilioni 27.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhamia Dodoma. Hoja hii imetolewa na Kambi ya Upinzani na namshukuru sana

Mheshimiwa Mbunge wa Dodoma ametoa hotuba yake nzuri sana ya kuunga mkono mpango huu wa kuhamia Dodoma na anathamini sana jitihada zinazofanywa na Serikali hapa za kuharakisha ujenzi wa miundombinu. Ukweli ni kwamba Serikali haijashindwa kutekeleza mpango wake wa kuhamia Dodoma. Hii ni Sera ya Serikali ya CCM, iko ndani ya Ilani, tunakwenda hatua kwa hatua na tulianza tangu mwanzo kutangaza nia lakini kwa hatua tulizopiga sasa tunaenda vizuri. Sehemu kubwa ya miundombinu muhimu inaanza kukamilika. Hivi ninavyozungumza sasa hivi tuna fedha dola za kimarekani milioni 32 ambazo zinafanya kazi ya kuimarisha miundombinu hapa Dodoma lakini pia tumeshafanya mapitio ya *Master Plan* mpya ya Dodoma. Mji wa Dodoma sasa Makao Makuu ya Serikali yatajengwa kati ya Chamwino na Ihumwa. Eneo hilo limeshatathminiwa tayari na *Master Plan* imeshatengenezwa, tuliajiri *consultancy* kutoka Korea ya Kusini, wamekamilisha kazi yake na mipango inaendelea vizuri. Kwa hiyo, mipango hii ya ujenzi ya miundombinu, uongezaji wa huduma unaendelea vizuri sana na ndiyo maana Serikali imeweza kutoa dola hizo zote kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa maji, barabara, mifereji na huduma zingine muhimu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ujenzi wa miundombinu ya elimu kama Chuo Kikuu na yenyewe inaongeza tija na huduma katika Mkoa wa Dodoma. Hata Bunge hili kulijenga hatukujenga kwa makosa. Tulijenga kwa nia hiyohiyo kwamba tungependa mji wa Dar es Salaam ubaki kuwa kitovu cha biashara lakini huduma zingine za Serikali na Bunge ziendeshwe

Dodoma. Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo yanaonekana kwa macho na kila mwenye macho anayaona. Kwa hiyo, nataka kusema kwa ufupi kwamba Sera yetu ya kuhamia Dodoma iko palepale lakini tutaenda hatua kwa hatua, hata Roma wanasema haikujengwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu linahusu kubana matumizi ya Serikali. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia hatua kadhaa ambazo tunakusudia kuzifanya katika kubana matumizi. Mwaka jana tuliahidi kwamba tutaanza kuchukua hatua, Waheshimiwa Wabunge wengi mmeshauri na katika maeneo kadhaa mmesema kabisa hili fanyeni. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo hapa. Sasa haya maelekezo aliyotoa ni sehemu tu ya yale aliyoweza kuyasema lakini ndani ya Serikali kuna maelekezo mengi ameshayatoa yanayoelekeza utaratibu wa kubana matumizi. Eneo moja ni hilo la magari. Huko kwenye kazi ngumu huko wataendelea kutumia zile *hard top* lakini sisi wengine tutaendelea kutumia magari yasiyozidi *CC 3000* ambayo tunafikiri yanatosha. Kwa sababu haya makubwa yanayoitwa *VX* ili likupe nafuu ya matumizi ya mafuta lazima ulipige likimbie zaidi ya kilometa 150 kwa saa ndipo unapata nafuu ya mafuta lakini kwa matembezi ya Dar es Salaam kilometa 60 kwa saa, tunatumia mafuta mengi sana katika miji na hasa kwenye barabara ambazo haziendi kasi sana gari zile matumizi ya mafuta yanakuwa makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ili upate nafuu ya magari yale lazima uende kwa kasi ndiyo matumizi yanakuwa madogo kutokana na injini yake. Maana mengine yana injini zaidi ya *CC 4000* na kuendelea na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu anafikiri gari ya *CC 3000* kwa Waziri kama Lukuvi inamtosha. Kwa hilo tutatekeleza na bahati nzuri Mawaziri wa ofisi yake mwaka huu tutaanza kununua magari hayo ya *CC 3000* lakini hili halitoshi tu kuelekeza hivyo. Maana yake ni kwamba viongozi wote wa Serikali kokote walipo lazima wasimamie hatua mbalimbali za kubana matumizi. Kubana matumizi sio magari tu, kila kiongozi lazima awajibike na bajeti yake kuhakikisha kwamba matumizi yasiyo halali, safari zisizokuwa za msingi, kuna viongozi wa Halmashauri ambao ukiangalia safari zao wanasafiri zaidi na viongozi wa Serikali wanasafiri zaidi kwenda nje ya maeneo yao kuliko ndani ya maeneo yao. Kwa hiyo, hizi zote ni hatua mbalimbali ambazo Mhesimiwa Waziri Mkuu ameshatolea maelekezo ambazo zinaashiria kubana matumizi.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho hapa nizungumzie Vyama vya Siasa. Wameshauri Serikali iongeze bajeti Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Msajili wa Vyama vya Siasa nchini achukue hatua mara moja dhidi ya Vyama vya Siasa na viongozi wake ambao wamekuwa na tabia ya uchochezi katika misingi ya Udini, Ukanda na Ukabila kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa. Kama kuna Chama chochote cha Siasa kinachoonekana kuwepo kwa misingi ya Ukanda Ukabila au Udini kifutwe haraka ili kuepusha Taifa letu na uchafu huu. Kuziwezesha Ofisi za Kanda za Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa na

waratibu watakaoratibu shughuli za Vyama vya Siasa Mikoani ili kuboresha utendaji wa kazi za Msajili.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kwamba Serikali itaendelea kuongeza bajeti ofisi za Vyama vya Siasa ili ziweze kuwajibika vizuri. Serikali inakiri kwamba sehemu ilipo ofisi ya Msajili ni ndogo hivyo ipo katika mchakato wa kutafuta eneo lingine ambalo litakidhi mahitaji yake. Baada ya muundo mpya wa Ofisi ya Msajili kupitishwa waratibu na watumishi katika kila Kanda watapangwa kukidhi shughuli mbalimbali katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itahakikisha kuwa Kanuni na maadili ya Vyama vya Siasa zinafuatwa na Vyama vyote na haitasita kufuta Chama chochote kinachokiuka sheria. Haya maneno ya Tendwa kwamba hatashindwa kufuta Chama chochote kinachokiuka sheria.

Mheshimiwa Spika, yapo maelezo mengi hapa yametolewa lakini siwezi kuyasoma yote lakini wengine hapa walikuwa wanashauri kwamba hivi ni lazima viongozi kama sisi tukashifu, tutukane, tuseme uongo ili tusifiwe? Mimi nasema hapana, ndiyo jibu langu, sio lazima. Sio lazima useme uongo, ukashifu ili uweze kusifiwa lakini pia niwashauri wale wote wenye tabia hizo ambazo zimeelezwa hapa za kufikiria wanaweza kuligawa Taifa hili kwa Udini au Kiukanda, mimi nawashauri waache kwa sababu nchi hii haipo tayari kuwa kama Mali au Sudan. Mimi naomba tujenge misingi mizuri kwa vijana wetu ili Taifa hili lisije kuwa na watu wa kunung'unika, wazushiwazushi, waongowaongo, haifai na hatupo tayari kugawana nchi hii kwa misingi yoyote ile, iwe ya Kikanda au ya

Kikabila, nchi hii imejengwa, Waswahili wanasema usione vyaelea vimeundwa.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwashauri ndugu zangu na wananchi hasa wanachama wa CCM maana wanakuwa wanauliza sana, mbona viongozi wa CCM hamtembei kama wanavyofanya wenzenu? Sisi tuna kazi ya kufanya, sisi ndiyo tunaojenga nchi hii, sisi tunaongoza Serikali, kwa sababu hata hao wanaotembea kwa taarifa yenu matatizo yenu wanakuja kutuambia sisi ndiyo tunakuja kufanya. Tuna kazi ya kufanya ndiyo maana hatuwezi kutembea, mmetupa kazi ya miaka mitano na sisi ndiyo tunafanya kwenye Majimbo yenu. Wacha hao watembee Mtwara, Lindi lakini sisi tunakuja kujenga, tunaweka maji kule Dar es Salaam, tutajenga masoko, ndiyo kazi yetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi ndiyo tunaokusanya kodi, lakini sisi ndiyo tunaotekeleza Ilani yetu, ndiyo maana hamtuoni kwa sababu tuna kazi ya kufanya na ukiona watu wanasema sana jambo fulani, ujue wao ndio wanaofanya. Juzi hapa tulimsikia Kiongozi mmoja wa Upinzani akisema Mawaziri wamesema mahali kwamba Serikali haitatoa maendeleo kwa Majimbo ya Upinzani lakini hawa watu wamekwenda Ngara wenyewe wamegeuza wao wenyewe wanasema mtuchague sisi kwa sababu tunaogopwa na Serikali. Mkituchagua Serikali ndiyo itakuja kutekeleza miradi hiyo, hawa walisema hivi na wanasema vinginevyo. Kwa hiyo, nataka tu mjue kwamba yapo maneno lakini vipo vitendo. Sasa muamue kusikiliza maneno au msikilize vitendo na

vitendo katika nchi hii vinapatikana na vitaletwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawashukuru sana wenzangu Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wenu mliotupa, nataka kuwahakikishieni kwamba yote haya tutayatekeleza lakini nawashukuru sana viongozi wenzetu wa Wabunge wa Upinzani kwa kazi mnayofanya ya kutukasanyia maoni ya wananchi na kutupa tuyatekeleze. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakaporudi tutaanza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, atajibu hoja zake kwa muda mfupi halafu saa kumi na mbili na nusu tutaanza kazi ya Kamati ya Matumizi. Maelezo kuhusu Kamati ya Matumizi nitayatoa tutakapoingia baadaye kwa sababu ni vizuri tukajua hilo kwa sababu ni eneo pia huwa hatufanyi vizuri.

Sasa nina tangazo mahsusi sana ingawa wengine hawapo lakini naomba mnisikilize. Mpambe wa Bunge, *Sergeant At Arms* anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kutakuwa na zoezi la kuweka alama za utambulisho kwenye silaha litakalofanyika leo na kesho tarehe 30. Zoezi hili litafanyika katika Kituo Kikuu cha Polisi hapa Dodoma. Tunaomba Wabunge wote wanaomiliki silaha kutumia fursa hii ili kuweza kuwekewa alama za utambulisho kwenye silaha zao. Tulipendekeza labda tufanyie hapa karibu ikaonekana kiusalama sivyo kwa sababu unaweza usijue zimetokea wapi. Kwa hiyo, mnaombwa nyie wote mnaomiliki silaha muende kule *Police Central* ya hapa Dodoma mkafanye shughuli hiyo. Muda

mliopewa ni leo na kesho, kwa hiyo muende mkafanye hivyo.

Asubuhi nilitangaza na nafikiri hawa ndiyo wanakwaya wenyewe niliowatambulisha walikuwa *basement*. Nafikiri ni wanakwaya 60 kutoka KKKT Mkoa wa Manyara. Naomba wasimame, walipo. Ahsante sana, karibuni sana naona mmesafiri mwendo mrefu, nadhani mnaliombea Taifa hili kuwa na amani ambayo tunaiomba, ahsanteni sana kwa kuja. *(Makofi)*

Halafu kuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondali Buigiri, ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Naona wasichana wachache kutoka Huruma Sekondari, wako wachache sana, simameni hapo mlipo. Haya akina mama wa kesho someni kwa bidii sana. *(Makofi)*

Halafu wale watunza kumbukumbu, Makatibu Mukhutasi 48 kutoka Halmashauri mbalimbali na wenyewe wasimame kama wapo. Ahsante sana, nafurahi kuwaoneni. Wengine siwajui maana sijapewa maelezo yao lakini kwa ujumla wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani, Ndugu Canon Mvinga na mkewe, wako wapi? Watakuja mchana. Tunatarajia kuongeza viti huko nyuma kwa sababu sasa hivi ukumbi wetu hautoshi nadhani kuanzia Jumatatu nafikiri tutakuwa tumeongeza nafasi kubwa zaidi lakini kwa sasa ndivyo tunavyobanana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nisitishe shughuli hizi mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha asubuhi tulitoa nafasi kwa baadhi ya Mawaziri kuweza kujibu hoja mbalimbali zilizokuwa zinatolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, sasa tutamwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kutoa ufafanuzi.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema mpaka leo hii tunapohitimisha majadiliano ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2012/2013.

Kipekee, nikushukuru sana wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kusimamia na kuongoza kwa umakini na uvumilivu mkubwa majadiliano ya Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa njia ya kipekee Waheshimiwa Mawaziri kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mbunge na Waziri

wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri, Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Aggrey Deaisile Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI anayeshughulikia masuala ya elimu, ambao wameendelea kunishauri na kunisaidia katika kufanikisha majukumu ya ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote na watendaji kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii na uwezo mkubwa katika kunisaidia. Niwashukuruni ninyi wote Waheshimiwa Wabunge mliopata nafasi ya kuchangia kwa michango yenu ya kina ambayo kwa kiasi kikubwa imewezesha ofisi yangu kujua maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi zaidi na maeneo ambayo tumefanya vizuri. Katika mjadala huu, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 268 walichangia, Waheshimiwa Wabunge 113 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 155 wamechangia kwa njia ya maandishi na ninaomba uniruhusu niwataje mmoja mmoja kwa majina.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge, Viti Maalumu, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi,

Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mbunge wa Hai, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Msemaji wa Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Anne Kilango, Same Mashariki, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Ally Kessy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini na Mheshiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, Mheshimiwa Kaika Saning'o, Mbunge wa Ngorongoro, Mheshimiwa Hamad Yusuph Masauni, Mbunge wa Kiwajuni, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Lediana Mfuru Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Vicent Joseph Nyerere, Mbunge wa Msoma Mjini, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi,

Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mbunge wa Nyamagana, Mheshimiwa Charles Paul Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mbunge wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mbunge wa Geita, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, Mheshimiwa Mohamed Habibu Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mbunge wa Gairo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Devotha Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalimu, Mheshimiwa Waridi Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki, Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Joshua Samuel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa

Ilemela, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru Kusini, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Vicky Kamata, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mbunge wa Kibiti, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, Mheshimiwa Yusuph Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, Mheshimiwa Anthony Mbasa, Mbunge wa Biharamuro Magharibi, Mheshimiwa Jenista Muhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Al–shaymaa John Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mbunge wa

Chaani, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Namelok Edward Moringe Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, Mheshimiwa Haji Khatibu Kai, Mbunge wa Micheweni, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa viti Maalum, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Susan Limbweni Aloyce Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Joyce Mukya, Mbunge wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri, Mbunge wa Babati Mjini na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi, Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa

Engineer Christopher Chiza, Mbunge wa Buyungu, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, Mbunge wa Makunduchi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI Elimu, Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na uwezeshaji na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Ismani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mbunge wa Kyerwa, Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, Mheshimiwa Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amos Makala, Mbunge wa Mvomero, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ezekiel Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, Mheshimiwa Vicent Joseph Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Profesa Peter

Msolla, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mbunge wa Kwimba, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Sara Masafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Busega, Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Engineer Gerson Hosea Lwenge, Mbunge wa Njombe Magharibi, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Obama, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mbunge wa Koani, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Magharibi, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Moses Joseph Manchali, Mbunge wa Kasulu Mjini, Mheshimiwa Silvester Masele Mabumba, Mbunge wa Dole, Mheshimiwa Moza Abeid Said, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Gregory George Teu, Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Namelok Edward Moringe Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mbunge wa Mafia na Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Dkt. Anthony Gervas Mbassa, Mbunge wa Biharamuro Magharibi, Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum,

Mheshimiwa Margraret Simwanza Sitta, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hamad Rashid Hamad, Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa Dkt. Haji Hussein Mponda, Mbunge wa Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Jason Samson Rweikiza, Mbunge wa Vijijini, Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe, Mheshimiwa Mariam Nasor Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, Mheshimiwa David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, Mheshimiwa Christine Mughwai Lissu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Asha Msimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, Mheshimiwa Joyce

John Mukya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenisini na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Herbet James Mntangi, Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Gooddluck Joseph Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyag'hawale, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijini, Mheshimiwa Amina Nassoro, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nasir, Mbunge wa Korogwe Mjini, Mheshimiwa Benedict Ole–Nagoro, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Innocent Edward Karogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Rajabu Mbarouk, Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Esther Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum,

Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe na Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dkt. Christina Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kwambwa, Mbunge wa Bagamoyo, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, Mheshimiwa Yusuph Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala, Mheshimiwa Engineer Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Mheshimiwa Cecilia

Damian Parreso, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Agnes Elius Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Said Ramadhani Bwanamdogo, Mbunge wa Chalinze, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngondo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Mheshimiwa Asha Mohammed Omar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwanahamisi Kassim Said, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Esther Minza Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Mendrad Lutengano, Mbunge wa Mufindi Kusini, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo na Mheshimiwa Engineer Athuman Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igalula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi, Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Yusuph Nassir Abdallah, Mbunge wa Korogwe Mjini, Mheshimiwa Deusderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, Mheshimiwa Lolesia Jeremia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Susan L. Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela K. Kahigi, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga,

Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Abdulsalaam S. Amer, Mbunge wa Mikumi, Mheshimiwa Rose K. Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Abdallah Sheria Ameir, Mbunge wa Dimani, Mheshimwia Said Mussa Zuberi, Mbunge wa Fuoni na Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, Mbunge wa Moshi Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa majina yamechanganywa sana lakini mtatuwia radhi, kuna maneno mengine tumeyachanganya kidogo. Kuna moja hapa amenisahihisha anasema umekosea kunitaja jina siyo Amina Amour ni Amina Mohamed Mwidau, nakubali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimetaja majina, naomba sasa nitoe tu shukrani za jumla kwa Waheshimiwa Wabunge. Idadi ya wachangiaji ni kubwa, hii inaonesha dhahiri jinsi ambavyo Wabunge mnavyoweka umuhimu katika majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake. Kwenu ninyi wote, nasema ahsanteni sana. Michango na hoja, ni nyingi, Mawaziri na Manaibu Mawaziri wamejaribu kujibu baadhi lakini bado zimebaki nyingi hoja ambazo hatutaweza kuzijibu kutokana na muda. Napenda kuwaaidini kwamba tutajitahidi kuziandika zote na kuziwasilisha kwenu ili muweze kuona majibu yetu ni nini.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Wabunge wote kwa jinsi mlivyochambua kwa kina utekelezaji wa shughuli za Serikali. Hii ni dalili kwamba Bunge hili lina Wabunge wanaojali

maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla. Niwashukuru wote walioonesha mafanikio ambayo tayari yamepatikana katika utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya Serikali. Vilevile niwashukuru wale wote mlioonesha miradi na shughuli ambazo Serikali haijatekeleza kwa ufanisi uliotarajiwa. Kwangu mimi, michango yote itatusaidia sana katika kufanya vizuri zaidi kukabiliana na changamoto zinazowakabili wananchi. Aidha, michango hii mizuri, imetusaidia sana kufahamu kwa kina mambo mengi ambayo wananchi wetu wanategemea kutoka kwa Serikali yao. Nataka niwaahidi wote waliotupongeza kwa kazi nzuri tuliyoifanya. Hata hivyo, hatutabweteka na pongezi hizo bali zitakuwa chachu ya kutuwezesha kufanya vizuri zaidi. Kwa zile changamoto zilizotolewa, ninawahakikishia tumezisikia na tutazifanyia kazi. Ninachokiomba, ni ushirikiano wenu, nasi tutafanya tuwezalo katika kutekeleza yote ambayo mmetushauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(9) inayohusu kujadili bajeti za Wizara, nichukue nafasi hii sasa kujibu na kufafanua baadhi ya hoja zilizotolewa na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ambalo nataka kulitolea ufafanuzi ni suala linalohusiana na fedha za Rada. Eneo hili limechangiwa na Wabunge wengi kwa hisia tofauti lakini kwa nia njema sana. Baadhi ya wale waliochangia ni pamoja na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Michael Lekule Laiser, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Ally Keissy

Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mn'gong'o, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mbunge wa Viti Maalum na wengine ambao pengine sikuweza kuwakumbuka harakaharaka.

Msheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano (*Memorandum of Understanding*) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwakilishwa na Wizara ya Fedha na Serikali ya Uingereza, Ikiwakilishwa na *DFID*, *BAE Systems* na *SFO*) iliyosainiwa mwezi Machi, 2012 kuhusu matumizi ya fedha za fidia ya Rada. Sehemu ya II, Kifungu Na.10 cha makubaliano hayo, matumizi ya fedha hizo yanalenga kuimarisha uendeshaji wa Elimu ya Msingi ambapo asilimia 75 ya fedha zitatumika kununua Vitabu vya Kiada, Viongozi vya Walimu, mihtasari na miongozo ya mihtasari, aidha, asilimia 25 itatumika kununua madawati. Hayo ndiyo makubaliano yaliyofikiwa rasmi na kuwekwa saini na pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, msingi wa makubaliano ya kununua vitabu ni kwamba, kwa sasa kitabu kimoja hutumiwa na wanafunzi wasiopungua kumi kwa wastani. Uwiano huu ni mbaya kwa kuwa mwanafunzi hapati fursa ya kutumia vitabu katika maisha yake ya shule. Walimu pia hawana mihtasari na vitabu vinavyowaongoza kufundisha. Matokeo ya hali hii ni

kwamba wanafunzi wengi huhitimu Elimu ya Msingi bila kupata kwa ukamilifu stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na hivyo kutofanya vizuri kwenye mitihani yao ya Darasa la Nne na Saba. Iwapo fedha hizi zitatumika kununua vitabu, tutakuwa na uhakika wa kuwa na uwiano mzuri wa vitabu hasa kwa masomo ya msingi (*core subjects*) yaani Hisabati, Kiswahili, Sayansi, Kiingereza na Jiografia. Kitabu kimoja, kama tutatumia fedha hii kama nilivyoeleza, kitatumiwa na wanafunzi wawili hadi watatu badala ya watoto kumi. Shule zitaelekezwa kuwagawia wanafunzi vitabu hivyo wakati wakiwa shuleni na nyumbani, Walimu pia watakuwa na uhakika wa kupata muhtasari, miongozo ya masomo na Viongozi vya Mwalimu kwa masomo yote.

Mheshimiwa Spika, Vitabu hivyo vitanunuliwa kutoka makampuni kumi na tatu (13) ya wachapishaji ambapo vitabu vyao viliteuliwa kuwa Vitabu Teule vya Kiada ambavyo ni viwili kwa kila soma. Makampuni hayo ni *Ben Company, Best Deal Publisher, E & D Vision, Education Books Publisher, Jadida, LongHorn, Longman, Macmillan, Mkuki na Nyota, Mture, Oxford, Tanzania Institute of Education (TIE) na Ujuzi Book.*

Mheshimiwa Spika, kati ya makampuni hayo, ni makampuni mawili (2) tu ambayo ni ya nje lakini wanayo matawi hapa Tanzania. Makampuni mengine yanayobaki wamiliki wake ni Watanzania wazawa wa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili lililopangwa kutumia fedha hizi ni madawati. Kadhalika, eneo hili lilizingatiwa kutokana na upungufu mkubwa wa madawati Kitaifa. Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba, karibu nusu ya wanafunzi ambao ni milioni nane (8,000,000) hawana sehemu nzuri za kukalia. Hii ina maana kwamba, kuna upungufu wa madawati takribani 1,500,000 – 2,000,000. Athari za ukosefu wa madawati ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Wanafunzi kushindwa kumudu stadi za kuandika;

(ii) Wanafunzi kuchafuka kutokana na kukaa chini kwenye madarasa yenye vumbi;

(iii) Wanafunzi kupata athari za kisaikolojia kutokana na kukaa chini huku baadhi yao wakiwa na madawati; na

(iv) Umri wa kitabu (*book life span*) hupungua kutoka wastani wa miaka 3-5 hadi chini ya miaka miwili (2) kutokana na kukosa eneo la kuhifadhia vitabu hivyo na kuviweka katika sakafu zenye vumbi au madarasa yasiyo na sakafu kabisa.

Mheshimiwa Spika, iwapo madawati yatapatikana kwa bei nzuri, kiasi cha shilingi bilioni 18.1 zitaweza kutupatia madawati yasiyopungua laki nne (400,000) ikiwa tutaweza kupata dawati moja kwa shilingi 50,000/-. Hata hivyo, madawati imara bei yake haipungui shilingi 100,000/- kwa dawati moja. Kwa madawati laki nne (400,000), tutaweza kuwa na

watoto 1,200,000 watakaonufaika na ununuzi wa madawati.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafakari kuhusu kutumia fedha zilizopatikana kujenga nyumba za Walimu. Uchambuzi unaonesha kuwa, kwa wastani wa shilingi 12,000,000 kama gharama ya nyumba moja, fedha hizo zinaweza kutupatia nyumba 6,000. Kwa idadi ya Shule za Msingi 16,000 zilizopo, hata kama tutaamua kujenga nyumba moja kwa shule moja, bado tutakuwa na shule 9,000 ambazo zitakosa mgao wa nyumba hiyo moja. Aidha, umuhimu wa nyumba utawafikia Walimu wachache tofauti na vitabu na madawati ambapo wanafunzi wote na Walimu wote watapata vitabu ambavyo vitarahisisha kazi ya kujifunza na kufundisha. Madawati pia yatawafikia wanafunzi wengi. Hivyo, bado kama Serikali tunaona kuwa ni bora fedha hizo zielekezwe kwenye vitabu na madawati. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za Walimu, madarasa, vyoo na maabara kupitia programu za Kitaifa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazoendelea kupitia *"Local Government Capital Development Grant", MMEM*, *MMES* na juhudi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua. Serikali imechagua kiasi cha fedha hizi kituwezeshe kupata vitabu kwa masomo ya msingi kwa watoto wote na hivyo kutupunguzia kwa kiasi kikubwa tatizo la uhaba wa vitabu kwa wanafunzi. Kiasi kinachobaki cha asilimia 25 kisaidie kupunguza tatizo la madawati. Lakini tunaweza vilevile tukaamua kuzitumia fedha hizi ndogo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba chache za

Walimu na madawati kidogo lakini wakati huohuo watoto wakaendelea kutumia vitabu vikiwemo vya masomo ya msingi kwa uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi takriban kumi. Serikali inaona kuwa uamuzi wake wa kununua vitabu na madawati ili kupunguza upungufu wa vitabu na madawati bado ni uamuzi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha hizi kutumika Tanzania Bara kunatokana na ukweli kwamba ununuzi wa Rada ulifanywa na Sekta ya Mawasiliano chini ya Wizara ya Miundombinu ambayo siyo ya Muungano; na sio Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo ni miongoni mwa Wizara za Muungano. Kwa hiyo, kutokana na maelezo hayo, ndiyo maana fedha hizi zilikuwa zaidi zimelenga kutolewa kwa ajili ya kuhudumia madawati pamoja na vitabu upande wa Bara.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Mahakama ya Kadhi nchini. Wabunge waliochangia hapa ni pamoja na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani pamoja na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, suala la kuanzishwa au kurejeshwa Mahakama ya Kadhi lipo katika hatua nzuri ya utekelezaji wake. Kamati Ndogo iliyoteuliwa na Waziri wa Katiba na Sheria yenye Wajumbe Wawakilishi wa Waumini wa Dini ya Kiislamu na Serikali imeshatoa Taarifa yake ya Kwanza na kutoa ushauri wa namna ya

kuanzishwa Mahakama au kurejesha Mahakama ya Kadhi nchini.

Mheshimiwa Spika, hoja zilizoafikiwa na pande zote mbili ni pamoja na Uanzishwaji au urejeshaji wa Mahakama ya Kadhi chini ya Sheria ya *Islamic Law (Reinstatement) Act, Cap 375* kama ilivyokuwa imerejewa mwaka *2002.* Hoja nyingine ni ile inayohusu masuala saba yatakayoshughulikiwa na Mahakama ya Kadhi ambayo ni Ndoa na Talaka, Mirathi, Wosia, Hiba/Zawadi/Tunu, Wakfu; Malezi ya Watoto na Usuluhishi wa Migogoro ya Kiislamu. Vilevile ni kuwa Mahakama hiyo haitahusika na Mashauri ya Jinai.

Mheshimiwa Spika, katika Kikao cha mwisho cha pamoja kati ya Serikali na ujumbe wa Wawakilishi wa Waumini wa Dini ya Kiislamu kilichofanyika mwezi Machi mwaka huu, Wajumbe waliafikiana kuwa upo umuhimu na dhamira ya kweli ya kuanzisha au kurejesha Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara. Hivyo, ili kuwezesha suala hili liende kwa haraka, kwa kuanzia, ni vyema zikaanzishwa Mahakama za Kadhi katika baadhi ya maeneo machache nchini. Lengo ni kuwezesha umma kulielewa vizuri suala hili kinyume na hisia potofu zilizopo sasa zikihusisha Mahakama ya Kadhi na Sharia (inayohusisha masuala ya jinai) chini ya Dini ya Kiislamu.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho cha mwisho cha Kamati Kuu inayosimamia suala hili, iliamuliwa na pande zote mbili (Waislamu na Serikali) kuwa baadhi ya Wajumbe kutoka upande Waislamu na Serikali wakafanye ziara ya mafunzo katika nchi za India,

Uingereza, Kenya na baadaye Zanzibar ili wakajifunze namna ya kuratibu na kuendesha Mahakama za Kadhi katika nchi hizo ambazo zina Mahakama za Kadhi kwa muda mrefu. Lengo ni kupata uzoefu na kujua njia bora ya kutuwezesha kuanzisha au kurejesha Mahakama hiyo nchini. Ziara hiyo inatarajiwa kufanyika hivi karibuni na kugharamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati Kuu inayojumuisha Viongozi wa Waumini wa Dini ya Kiislamu na Serikali chini ya Uenyekiti wangu, kimsingi imekubaliana kwa kauli moja uanzishwaji au urejeshwaji wa Mahakama hiyo nchini itakayokuwa nje ya mfumo wa Serikali. Aidha, Mahakama hiyo itagharamiwa na kuendeshwa na Waumini wa Dini ya Kiislamu wenyewe. Serikali kwa upande wake hususan katika hatua hizi za awali za kuanzishwa kwa Mahakama hii, itaendelea kushirikiana na Viongozi wa dhehebu hili kwa karibu sana ili kuhakikisha kuwa azma hii inafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni njema na thabiti katika suala hili. Serikali itaendelea kushirikiana na Waumini wa Dini ya Kiislam na Viongozi wake hadi lengo litakapokuwa limefikia tamati. Naomba kutoa wito kwa Jumuiya ya Waumini wa Dini ya Kiislamu nchini pamoja na wadau wengine kuvuta subira juu ya suala hili wakati Serikali na Viongozi wa Dini ya Kiislam wakiendelea kulikamilisha kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni eneo linalohusu zana za kilimo. Eneo hili limechangiwa na Wabunge wengi vile vile, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana,

Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini na wengine ambao pengine sikuwataja

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2012/2013, ukurasa wa 23, Ibara ya 37, Serikali imejitahidi kupunguza bei za matrekta ya SUMA JKT ili kuwawezesha wakulima wengi kupata matrekta. Kwa mfano, baadhi ya bei za matrekta hayo ni hizi zifuatazo; *Farmtrac 60(50 HP; 2wd) Tractor 16,480,952.00, Farmtrac 60DT(50 HP; 4wd) Tractor 23,267,522.00; Farmtrac 70 (60 HP; 2wd) Tractor, 24,212,000.00; Farmtrac 70DT(60 HP; 4wd) Tractor, 30,489,632.00; New Holland 75 HP; 2wd Tractor 31,030,487.00; New Holland 75 HP; 4wd Tractor 38,784,527.00; 12 Disc Mounted Harrow3,901,185.00; 5Ton Non Tipping Trailer 7,705,417.00; Power Tillers with accessories (set) 8,440,000.00, Rotavator with 30 Blades 6,421,467.00; Planter 5,171,186.00; Seed Drill 4,035,161.00* na *Irrigation Water Pump, 5,747,782.00.*

Mheshimiwa Spika, orodha yote hii tutaiandaa na kuisambaza kwa Wabunge wote ili waweze kupata undani wa bei kwa kila eneo linalohusika kama ni *4Wheel Drive* ama *2Wheel Drive*.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya kilichofanyika Dodoma mwezi Mei 2012, viongozi hao walitakiwa kuhamasisha ununuzi wa matrekta. Kufuatia juhudi hizo za kujitangaza kupitia vipindi maalum kama

ilivyoagiza Waziri Mkuu, matunda ya kazi hiyo sasa yameanza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma sasa umenunua matrekta 50 na tayari baadhi ya matreka hayo yako Mjini Songea na nimekubali kwenda kuwakabidhi baadhi ya wakulima watakaokuwa wameamua kukopa matrekta hayo ndani ya wiki moja ijayo. Mkoa wa Tabora wao wameagiza matrekta 25 na tayari 15 yameshafika na wananchi wameanza kununua hayo matrekta. Mkoa wa Morogoro nao umenunua matrekta 25. Watendaji Wakuu Mkoani na Wilaya zake zote wameamua kuchukua matrekta 20 na uhamasishaji kupitia *TCCIA* Kilombero wanaomba idadi ya matrekta 15. Mkoa wa Shinyanga kupitia *Shinyanga Foundation Fund*, wao wameamua kabisa kuanzisha kituo kikubwa pale ambacho kitakuwa na matrekta mengi. SUMA JKT wameeleza kuwa wamepokea maombi mengi kutoka Mikoa mingine, ikiwemo Kigoma, Tanga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana Wakuu wa Mikoa hiyo waliohamasisha na kuanza kutoa msukumo wa ununuzi wa Matrekta ya SUMA JKT. Kipekee kabisa nawapongeza:-

Mheshimiwa Said Thabiti Mwambungu, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma; Mheshimiwa Fatma A. Mwasa, Mkuu wa Mkoa wa Tabora; Mheshimiwa Joel Bendera, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Mheshimiwa Ali Nassoro Rufunga, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga. (*Makofi*)

Vilevile, napenda kuwapongeza Wakuu wa Wilaya wote wanaoendelea kuhamasisha ununuzi wa matrekta kupitia Programu mbalimbali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, bei hizi ni za Kituo cha Dar es Salaam. Bei za Mikoani ni dhahiri kwamba zitaongezeka kidogo kulingana gharama za usafirishaji kutoka katika Vituo hivyo. Hata hivyo, bado ikilinganishwa na matrekta mengi itakuwa bado ni chini na yenye nafuu zaidi. Ili kupata picha kamili kama nilivyosema na namna tulivyopunguza gharama zote hizi basi mchanganuo kamili wa kila kitu tutautoa na kuugawa..

Vilevile, Serikali imeamua kusogeza muda wa urejeshaji wa mikopo ya ununuzi wa matrekta hayo kutoka miaka miwili (2) hadi miaka minne (4) na watapewa *Grace Period* ya miezi sita kabla hujaanza kulipa. (*Makofi*)

Pamoja na hatua hiyo, yapo matrekta mengine yanayonunuliwa na Halmashauri kupitia Programu za *ASDP*, *DADPs* na *DASIP* ambao yanakwenda kwa Vikundi vya Wakulima na wala siyo kwa mkulima mmoja mmoja, Aidha, yale yanayokopeshwa kwa wakulima mmoja mmoja au Vikundi vya Wakulima huwa vinadhaminiwa na Vikundi vyao vya *SACCOs* au *SCULLT*. (*Makofi*)

Vilevile, upo Mfuko wa Pembejeo ambao tangu kuanzishwa kwake umetoa mikopo kwa wakulima

Vijijini kupitia *SACCOS* 341 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 6.7. Mikopo inayotolewa ni pembejeo za kilimo na mifugo, zana za kilimo ikiwa ni pamoja na matrekta makubwa na matrekta madogo (*Power Tillers*).

Mheshimiwa Spika, katika juhudi hizi hizi Serikali pia sasa imekubali kupunguza sana kiwango cha dhamana kulingana kama ni mtu binafsi au ni Halmashauri zetu za Wilaya. Kwa hiyo, kwa upande wa Halmashauri dhamana ile itakuwa asilimia kumi tu ambayo itahitajika badala ya kiwango kilichokuwepo mwanzoni cha karibu asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linalohusiana na suala la kilimo ni suala zima la umwagiliaji. Eneo hili limechangiwa na Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Sylivester Massele Mabumba, ndugu yangu Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale na Mheshimiwa Daktari Haji Hussein Mponda.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo yaani *ASDP*, ina mipango mahsusi ya kuendeleza wakulima wadogo ambapo wananchi wenyewe hushiriki katika kupanga mipango ya maendeleo katika kilimo kwa maeneo wanayoona ni ya kipaumbele kwao. Kila Halmashauri hushirikisha wakulima wake katika mipango na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo kupitia *DADPS*.

Mheshimiwa Spika, hivyo naomba kuziagiza Halmashauri zote za Wilaya kuhakikisha kwamba,

wanahamasisha watu wao vizuri ili waweze kujua kwamba fursa hii iko pale kwa ajili yao wakulima wadogo, waitumie ili waweze kuingia katika kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yote yenye fursa za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuna dhana imejengeka kuwa *SAGCOT* ni mpango wa kuwanufaisha wakulima wakubwa hasa wawekezaji wa Kimataifa na wale wa kati na si kwa wakulima wadogo. Lengo kubwa la *SAGCOT* ni kusaidia wakulima wadogo kwa kutumia mbinu za kushirikisha wakulima wakubwa na wa kati. Mathalani katika eneo la hekta laki moja linalofaa kwa kilimo cha mpunga na linalokaliwa na wakulima wadogo kama litapatikana eneo la hekta elfu tano mpaka kumi, basi atatafutwa mkulima mkubwa ambaye atawekeza katika eneo hilo ambalo ni asilimia tano mpaka kumi ya eneo lote. Teknolojia na huduma za ugani atakazotumia mkulima mkubwa zitatumiwa na wakulima wadogo chini ya Mfumo wa "*Block Farming*".

Mheshimiwa Spika, hii itaweza kusaidia sana katika kukuza na kuendeleza kilimo. Inategemewa kuwa mkulima mkubwa atajenga Kiwanda cha Kusindika Mazao yake na ya wakulima wadogo ili kuongeza thamani. Pia atakuwa ni Soko la Wakulima la uhakika ambako ataweza kuuzia mahindi au mpunga au mazao mengine yoyote. Mfano mzuri ni ule ambao tumeuona pale Morogoro. Kwa hiyo, eneo hili kwa kweli nia yake ni njema na naomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kujaribu kueleza kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivi mkulima mdogo ataweza kulima kwa kutumia zana za kisasa na kuongeza uzalishaji na tija. Mfano ni Mwekezaji wa Kilombero *Plantation (KPL)* ambapo kabla ya uwekezaji wakulima walikuwa wanazalisha tani 1.2 kwa hekta, lakini baada ya uwekezaji wakulima wadogo sasa wanazalisha hadi tani nane kwa hekta. Hivyo Miradi kama *SAGCOT* itawainua sana wakulima wadogo ikitekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni hili linalohusu uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi. Eneo hili Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, wametoa ushauri na mapendekezo kadhaa katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina Sera ya kuzuia mauzo ya chakula nje ya Nchi. Hata hivyo, kunapokuwa na uhaba wa chakula unaotishia usalama wa chakula nchini, Serikali hulazimika kuweka zuio la muda ili kuhakikisha wananchi wake hawakosi chakula. Zuio hilo halihusu mazao ya aina nyingine zote kwa mfano, matunda, mboga na mazao mengine mbali ya nafaka. Zuio hili mara nyingi limekuwa zaidi linagusa zao la mahindi. Aidha, kwa sasa Serikali inaweka mkazo zaidi katika mikakati inayolenga kuzalisha chakula kwa wingi kama suluhisho la kudumu ili Tanzania iwe muuzaji mkubwa wa vyakula kwa nchi jirani na kuinua uchumi wa nchi na kuwanufaisha wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kupunguza kiasi cha hifadhi ya chakula nchini ili kuweza kusaidia wakati na katika maeneo yatakayokumbwa na njaa. Wakulima wanahimizwa kuhifadhi chakula cha kutosha kwa matumizi ya angalau mwaka mzima. Aidha, kwa sasa tunao mpango wa kujenga Masoko ya Kimataifa mipakani ili Tanzania iweze kuuza mazao mbalimbali kwa nchi jirani kama vile nafaka. Mfano, wa Masoko hayo ni Soko pale Himo kwa Mzee Mrema ambapo majaribio ya uuzaji mahindi nje ya nchi yameanza kufanyika. Kwa hiyo, tutaendeleza juhudi hizo kwa nia njema ya kuhakikisha kwamba tunafaidika na utaratibu huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa na Wabunge ni lile linalohusu ununuzi wa mazao ya korosho. Kuhusu zao la korosho changamoto iliyopo kwa sasa ni kuhusu kuongeza thamani ya korosho kwa kuhakikisha kwamba korosho yetu inabanguliwa kabla ya kuuzwa. Kwa kuwa Serikali haijihusishi moja kwa moja na uendeshaji wa viwanda na kwa kuwa Mikataba ya ubinafsishaji wa Viwanda vya Korosho ni ya kisheria, Serikali itaendelea na jitihada zake za kuwapata wawekezaji mahiri ambao watatekeleza wajibu wao inavyotakiwa. Aidha, pale itakapodhihirika kisheria kuwa mwekezaji ameshindwa kuendeleza Kiwanda alichokabidhiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Mauzo, sheria itachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inafanya mazungumzo na Wawekezaji Binafsi kutoka nje na ndani ya nchi kwa lengo la kuwahimiza kuwekeza katika ubanguaji wa korosho hapa nchini. Serikali

inawahimiza wakulima kutumia utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani ili kuwa na uhakika wa soko na bei. Serikali pia inawahimiza wakulima kuwa katika ushirika ambao una nafasi nzuri ya kutafuta masoko na kupata bei nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie kidogo, ni hili linalohusu pamba. Eneo hili kwa kweli lilichangiwa na Wabunge kadhaa na wote wamelizungumza kwa hisia kubwa kwa sababu ni jambo linatugusa wote kwa namna moja au nyingine. Maeneo nitakayoyatoa hapa ni kusaidia tu kuonesha juhudi za Serikali katika kujaribu kupata ufumbuzi wa tatizo la bei ya pamba.

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Juni, 2012 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iliitisha Kikao cha Wadau wa Zao la Pamba ili kujadili Bei Dira ya Pamba kwa msimu wa ununuzi wa mwaka 2012/2013. Lengo la Serikali ni kukamilisha zoezi hili mapema ili kuruhusu kufunguliwa kwa msimu wa pamba. Kikao hicho kilihudhuriwa na wadau wafuatao:-

(i) Chama cha Wakulima wa Pamba *(TACOGA)*;

(ii) Chama cha Wafanyabiashara wa Pamba *(TCA)*;]

(iii) Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba;

(iv) Bodi ya Pamba;

(v) Ofisi ya Waziri Mkuu;

(vi) Wizara ya Viwanda na Biashara; na

(vii) Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Katika Kikao hicho, Wajumbe walijadili na kukubaliana kuzingatia vigezo vya Mkokotoo kama ifuatavyo:-

(i) Bei ya pamba nyuzi ikiwa kiwandani, kwa kutumia *New York Futures* badala ya *A Index;*

(ii) Kiwango cha kubadilishia fedha;

(iii) Bei ya kuuzia mbegu;

(iv) Faida ya Wachambuaji;

(v) Gharama ya Ununuzi wa Pamba Mbegu;

(vi) Gharama za Usafirishaji;

(vii) Riba ya Mkopo wa Benki;

(viii) Mchango wa wakulima kwenye Mfuko wa Wakfu *(CDTF)*; na

(ix) Ushuru wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Maazimio ya Kikao hicho, katika azimio la kwanza Kikao kiliazimia kwamba:-

(i) Bei ya Pamba Nyuzi ikiwa Kiwandani, kwa kutumia *New York Futures* iwe senti 63 za Kimarekani kwa Ratili kwa Dola;

(ii) Bei ya kuuzia mbegu iwe ni Shilingi 300 kwa kilo;

(iii) Faida ya Wachambuaji iwe Asilimia saba;

(iv) Gharama ya ununuzi wa Pamba Mbegu vituo iwe Shilingi 30 kwa kilo;

(v) Gharama ya usafirishaji wa Pamba Mbegu kwenda Kiwandani iwe Shilingi 40 kwa kilo;

(vi) Riba ya Mkopo wa Benki iwe Shilingi sita kwa kilo ya Pamba Mbegu;

(vii) Mchango wa wakulima kwenye *CDTF* uwe Shilingi 20 kwa kilo ya Pamba Mbegu; na

(viii) Ushuru wa Halmashuri upungue kutoka asilimia tano hadi asilimia mbili ya bei ya Pamba Mbegu.

Mheshimiwa Spika, Azimio la pili, Kamati iliazimia Bei Dira kwa kilo ya Pamba Mbegu kwa mkulima bei ya Mkulima itatangazwa na Mamlaka husika kabla ya msimu wa pamba kuanza kwa kuzingatia vigezo mbalimbali tarehe itakapokuwa imesogea ya kutangaza bei dira kwa ajili ya zao hilo.

Mheshimiwa Spika, kubwa hapa ni kwamba hawa wadau wote wanaombwa (ku-*scarifies*) kutoa kwa

maana ya kujinyima katika maeneo mbalimbali ili kuwezesha bei ya pamba ambayo itatumika kama dira angalau iweze kuwa ya juu na isiwe ile inayomuumiza mkulima mdogo. Ndio hasa maana ya jambo hili. Kwa hiyo, matumaini yangu ni kwamba itakapokuwa imefikia tarehe ambayo wamekubaliana sasa, basi wataangalia vigezo na viashiria hivyo vyote kisha watapanga bei kadri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni hili linalohusu mfumo bora wa uuzaji wa zao la korosho ghafi na kujenga Viwanda Vidogo Vidogo. Eneo hili hasa Mheshimiwa Mbowe alilizungumza sana. Nimeona ni vizuri niliseme kidogo kwa ajili ya jambo moja ambalo nafikiri ni la msingi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya *Warehouse Receipts Act* ya mwaka 2005 inayohusu Stakabadhi ya Mazao Ghalani kwa lengo la kumnufaisha mkulima mdogo kwa kumhakikishia bei nzuri ambayo inamwezesha kuweza kuhimili gharama za uzalishaji. Serikali bado inaona mfumo huu wa uuzaji wa korosho kupitia Stakabadhi ya Mazao Ghalani (*Warehouse Receipt System*) ni mzuri. Ni mfumo wa kumsaidia mkulima mdogo. Tatizo ni changamoto zinazokabili mfumo huu ikiwa ni pamoja na wanunuzi wasio waaminifu ambao bado wanapenda kutumia mifumo ya ulanguzi ambayo inawaumiza wakulima wadogo. Matatizo mengine ya bei dira nayo yanachangia katika eneo hili, hasa pale bei ya Soko la Dunia inaposhuka. Kwa sasa Serikali itaendelea kuboresha Mfumo huu kwa kadri itakavyoweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inafikiri kuwa suluhisho la kudumu ni kuwa na Viwanda vya Kubangua Korosho na itaendelea na jitihada zake za kuwapata wawekezaji mahiri ambao watatekeleza wajibu wao ipasavyo. Aidha, Serikali ina mpango wa kusaidia kuanzishwa kwa *Tanzania Commodity Exchange Market* ambapo mazao mbalimbali ikiwemo korosho yatauzwa katika Masoko ya Kimataifa na ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulitembelea nchini Ethiopia kujionea namna mfumo huu unavyofanya kazi vizuri na kwa uwazi na kwa manufaa ya mkulima mdogo. Matumaini yetu ni kwamba haitachukua muda mrefu kabla utaratibu huu haujaanza kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nimeona niligusia kidogo ni migogoro inayojitokeza kati ya wakulima na wafugaji eneo hili nalo limechangia kwa hisia kubwa. Lakini naomba tu niseme kwamba kwa kutumia mfano uliotokea pale Rufiji, katika Kijiji cha Umwe, Ikwiriri, kilichotokea pale siku ya tarehe 19 Mei, 2012 ni kwamba vurugu zilianza baada ya kifo cha Mzee Shamte Seif Mtawagala, aliyekuwa na umri wa miaka 80 kilichosababishwa na vijana wafugaji ambao walikuwa wanalisha mifugo katika shamba lake. Alipojaribu kutaka kuhoji na kutetea mali yake shambani ndipo vurugu hizo zilipoanza na hivyo kusababisha kifo cha mzee huyo na kwa kweli vijana wote na watu wazima waliona kwamba mzee huyo hakutendewa haki. Hivyo, kutokana na vurugu hizo baadhi ya nyumba, maduka, maboma ya ng'ombe na gari moja vilichomwa moto. Vile vile baadhi ya

ng'ombe walikatwa katwa kwa mapanga. Serikali iliingilia kati vurugu hizo na kuzizima asubuhi ya tarehe 21 Mei, 2012.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuhakiki idadi ya mifugo iliyopo, uwezo wa ardhi na malisho kwa ajili ya mifugo pamoja na miundombinu ya mifugo iliyopo ili kuwezesha kupanga matumizi bora ya ardhi, kuandaa miundombinu ya kutosha ikiwa ni pamoja na majosho, malambo na vyanzo vya maji. Zoezi hili limeanza tarehe 23 Mei, 2012 na linatarajiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2012 katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imetoa Mwongozo kwa umma, kwa Watanzania wote kupitia Vyombo vya Habari kuhusu utaratibu wa kuhamisha na kusafirisha mifugo ya kufuga kutoka sehemu moja hadi nyingine. Serikali inaamini Viongozi wa Vijiji na Halmashauri pamoja na Wafugaji wakizingatia mwongozo huo, migogoro inayojitokeza, kama huo wa Ikwiriri, haitakuwepo kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo Serikali kupitia Mipango ya Maendeleo katika Halmashauri (*DADPs*) itaendelea kujenga, kukarabati na kuimarisha miundombinu katika Vijiji na maeneo ya wafugaji ili kuboresha huduma. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi 5,008,285,000 kwa ajili hiyo kupitia *DADPs*. Aidha, kupitia mipango mbalimbali katika Wizara, Halmashauri na Sekta Binafsi, miundombinu ya aina hiyo itajengwa na kuimarishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka nigusie kwa kifupi ni hili linalohusu migogoro ambayo inatokana na kitu kinachoitwa uporaji wa maeneo ya ardhi. Vile vile limezungumzwa na baadhi ya Wabunge kadhaa. Ili kuondokana na migogoro baina ya wakulima na wafugaji pamoja na makundi mengineyo ikiwa ni pamoja na mtu na mtu, inashauriwa kuwa ardhi yote ipangiwe matumizi kisha ipimwe na kumilikishwa watu wote wenye haki juu ya ardhi inayohusika. Ardhi kwa ajili ya ufugaji ipimwe na hati kutolewa ama kwa ushirika wao au Serikali ya Kijiji kinachohusika kama mdhamini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa Halmashauri za Wilaya kuwa watenge fedha kwenye Bajeti zao ili kugharamia upangaji wa matumizi bora ya ardhi kama njia ya kutatua matatizo haya. Wataalam wa Ardhi wa Wizara wahusike kikamilifu kushirikiana na Halmashauri zitakazokuwa tayari kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mkakati wa kuondoa migogoro hiyo kwa kuhakikisha kuwa inaongeza kasi ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 1,300 kila mwaka kuanzia mwaka 2012/2013. Aidha, Serikali inaendelea na mashauriano na washirika wetu wa maendeleo ili kupata fedha za kuunga mkono wananchi au Wilaya zitakazokuwa tayari kutekeleza maandalizi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wafugaji ili waondokane na uchungaji na kufugia

sehemu moja huku wakiboresha mifugo yao. Aidha, Serikali itaendelea kujenga miundombinu ya mifugo ili kupunguza umbali kwa wafugaji kufuata miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu mkubwa ni lazima sasa uwekwe katika uanzishwaji wa Viwanda vya Kusindika Nyama. Eneo hili litatusaidia sana katika kupunguza idadi ya mifugo, lakini vile vile kuongeza au kukuza uchumi kutokana na mifugo yetu. Ni eneo ambalo tutalitilia mkazo mkubwa ili liweze kuwa la mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushauriana ndani na kwa kutumia wenzetu kutoka nje ili kuhamasisha, benki mbali mbali ziweze kutambue hadhi ya hatimiliki kimila, kisheria na zikubali kutoa mikopo kwa Wananchi wenye hatimiliki za kimila kwa kuwa inaweza kuwa ni hati inayoweza kufaa sana kama dhamana kwa ajil ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie kidogo suala la Kigamboni au Mji wa Kigamboni. Eneo hili nalo linatugusa wengi kutokana na mambo yanayoendelea pale. Nimekuwa nikijitahidi kukutana na viongozi na wananchi mbalimbali kwa nia ya kuleta maendeleo ya Watanzania. Ni bahati mbaya kwamba sikukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam kuhusu maendeleo ya Jiji na watu wake. Napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge hao kuwa niko tayari wakati wowote kukutana, wakati wowote tutakapokuwa hapa Dodoma ili kuweza kukaa na kuzungumza matatizo kwa ujumla. Kwa namna ya

pekee itabidi tutazame maeneo yote yanayohusu matatizo ya ardhi katika Jiji letu la Dar es Salaam ikiwemo ujenzi wa Mji wa Kigamboni, eneo la Kurasini na maeneo mengine yote yanayohusiana na makazi ya watu yakiwemo yale ambayo tunasema ni maeneo yenye hali au maeneo hatarishi. Yote haya tukiyafanya kwa nia njema tuna hakika kabisa tutaweza kupata ufumbuzi wa haraka katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo kuhusiana na sekta ya uvuvi, lakini hasa kwa maana tu ya kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali sasa imekwisha kamilisha mpango au programu ya kuendeleza Sekta ya Uvuvi hapa nchini (*Fisheries Sector Development Programme*). *Sector* hii imejumuishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka 2011/2012 hadi 2015/2016. chini ya programu hii, mambo mbalimbali yameainishwa yakiwemo masuala ya uendelezaji wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji, uhifadhi wa rasilimali, matumizi endelevu ya rasilimali pamoja na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, aidha, programu hii inahusisha uimarishaji wa huduma za ugani, utafiti, mafunzo na upatikanaji wa takwimu sahihi za rasilimali ya uvuvi. Pia, Programu imeainisha maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa kila mwaka. Mwisho, kutekelezwa kwa Programu hii kutawezesha kuongeza tija na uzalishaji katika Sekta ya Uvuvi. Aidha, tunatarajia kuimarisha doria za kuzuia uvuvi haramu ambao nao bado unatuathiri kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge sasa kutoka Jimbo la Katavi na wakati mwingine ni vizuri mkaniruhusu yanaposemwa mambo yanayonigusa basi na mimi niseme kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, liko eneo ambalo kila tunapokuwa Bungeni linazungumzwa, rafiki yangu Arfi ana usongo nalo sana, jana nikamwona dada yangu Mallac naye kalivalia njuga kweli kweli eneo hilo, ingawa Mallac alikwenda mpaka Jimboni mpaka kwenye Vijiji vyangu. (*Kicheko*)

Sasa, ah! Tatizo ni pale ambapo wanapokwenda kule wanaacha mambo, wanamsema Pinda, sasa hii ni tabu kweli kweli. Pinda *is nobody*, mimi nadhani kubwa pale ni maendeleo makubwa sana. Lakini kubwa tu niseme kwamba mkienda huko wenzetu basi m-*appreciate* mengine yanayofanyika vilevile. (*Makofi*)

Ndiyo, maana Mallac angalau dada yangu yule angefika kule akasema amefika kule amefurahi sana maana nimejitahidi, nimeweka *solar power* vituo vya afya vyote, zahanati zote, nyumba za waganga wote, nikajitahidi shule za sekondari zote nimeziwasha na *solar*, nikawapa walimu nyumba zao na majengo mengine yote yana *solar power*, lakini dada yangu anachokiona pale ni mbaya sana, ikabidi nipige na picha na kadhalika. Nikasema eh! *Agenda* hii ni ngumu kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sasa hili eneo ambalo linahusu *Agrisol Energy Tanzania Limited*, niliwahi kulisema, naomba nirudie tena, nalisema hili si kwa sababu

mkiwa na jambo au Mbunge akiwa na jambo hawezi kushauri juu ya eneo hilo, hapana. Lakini nataka tu nieleze uhalisia wa jambo lenyewe. Eneo hili, ni eneo ambalo linakaliwa na wakimbizi hivi sasa Katumba na Mishamu. Maeneo haya, yalikuwa ni maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa mujibu wa sheria, ni maeneo ya Serikali. Tuliyatoa katika kukidhi haja hii ya kuweka wakimbizi katika maeneo hayo. Kilichotokea nini?

Mheshimiwa Spika, baada ya nchi ya Burundi kuwa na amani, uamuzi wa Serikali ukawa ni kwamba basi wenzetu mrudi kwenu, ndipo jambo hili likaibuka kwamba sasa hii ardhi tuliyokuwa tumeitoa kama misitu ama tuirejeshe iwe misitu tena ama tuone namna ya kuitumia kwa maana ya kuongeza tija katika udongo au ardhi hiyo. Ndiyo tukaanza kutafakari; mimi, Mkuu wa Mkoa na Wabunge wengine tuliokuwa na nia njema; jamani hii ardhi wakiondoka hawa tunafanyaje? Ndipo ikatokea hiyo kampuni ikasema iko tayari kama tutaridhia kuwekeza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, nikafarijika sana, nikaona pengine ni jambo zuri. Nje ya kambi hizo tunavyo Vijiji 42 ambavyo vinaendelea na shughuli zake. Kwa hiyo, mtazamo ikawa ni kwamba, tukipata mtu mzuri, hawa wote tunaweza tukaona namna ya kuwasaidia wakaona hizo teknolojia, wakaona hivyo vitu vingine pengine tukawa na soko la uhakika kubwa kwa Katavi na kuongeza uzalishaji wa mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatua ya kwanza tuliyoanza nayo ikawa ni kwamba basi we bwana tutiliane *MoU* maelewano hivi, maana yeye alitaka

kuanza na uchunguzi wa udongo maana wenzetu kidogo wamekwenda mbali, hawezi kuanza kulima kama tunavyoanza sisi tunafyeka tu hapana. Wakasema tunataka kwanza tujihakikishie. Kwa hiyo tukakubali. Haya njoo uanze kufanya uchunguzi. Lile jambo tulikwenda kwenye Baraza la Madiwani tukalizungumza, mwisho tukasema ah! Mwacheni afanye uchunguzi, yote mema.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi ule umewachukua mpaka majuzi, walikuwa bado wanafanya ule uchunguzi ili baada ya pale sasa ndiyo tukubaliane eneo gani tunafikiri tuwapeni kwa ajili ya kitu gani. Tulichosema, ni kwamba, sisi kwa mujibu wa sheria zetu leo, ni vizuri ukajua kwamba ardhi yetu sasa hivi mtu akitaka kuweka pale, lazima alipe hiyo kodi ya ardhi ambayo kwa mujibu wa taratibu za sasa ni shilingi 200, ilikuwa shilingi 600, wakatupa ushauri watu wa *private sector*, tukaipunguza mpaka 200. Katavi wote wale ni shilingi 200 kwa heka moja. Ndicho tulichofanya, lakini hatujafika mahali tukaingia mkataba na hawa watu katika uzalishaji wenyewe. Maana ilikuwa ni kwamba tukishamaliza hatua hiyo, tutakapoanza mchakato sasa, ndipo tutaingia kwenye mambo ya msingi, tuone tunapangiana vipi, uwiano utakuwaje, Halmashauri imiliki kiasi gani cha hisa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa hili jambo nimekuwa nalirudia, lakini kila nikiwasikiliza wenzangu naona limepamba moto, utafikiri tumefikia mwisho wakati kumbe jambo lenyewe bado. Sasa nimeona niliseme hili ili wenzangu wa Mpanda wanielewe, maana wasije wakanielewa hapa kwamba mimi nimeuza ardhi,

nimeshawapa *Agrisol* na kadhalika. Hapana hatujafika kote huko, lakini tulifikiri katika hatua hii ya kwanza tuweze kujua nini tufanye.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kidogo juu ya suala hili la uharibifu wa mazingira ya msitu wetu wa Shengena, Mama Anne Kilango Malecela alilisema sana na wote mtakumbuka alivyokuwa amejaribu kulivalia njuga jambo hili kwa nia njema kabisa kwamba Serikali tulijue.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumebaini kwamba kumekuwepo na uchimbaji katika eneo hilo na uchimbaji wake ni wa aina mbili, wanachimba *Bauxite*, wanachimba dhahabu. Sasa uchimbaji ule kama ilivyo kawaida una uharibifu mkubwa sana na nimetazama *DVD* yake kwa kweli ni mkubwa sana. Lakini nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Anne Kilango kwamba alipokuwa amenieleza ilibidi kuchukua hatua haraka sana, nikamuagiza Mkuu wa Mkoa. Mkuu wa Mkoa akapeleka timu, timu ile imefanya kazi nzuri, wamejaribu kuhakikisha kwamba lile eneo halina tena wachimbaji ambao walikuwa wameingia pale kinyume cha sheria na kwa kweli wamejipanga vizuri kuhakikisha kwamba hakutakuwa na watu tena watakaorudi pale na kuendeleza uharibifu.

Tulikuwa na eneo moja ambalo lilitupa wasiwasi sana kwa sababu dhahabu kwa kadri unapojaribu kuipata na lazima utumie madini ya zebaki na kwa kuwa alivyokuwa ameeleza pale, hofu ile na sisi ikatupata. Kwa hiyo, tulichofanya tukachukua maji, tukapeleka kwa Mkemia Mkuu ili atusaidie kuona kama

je, kuna zebaki katika maji hayo ili tuweze kuchukua tahadhari haraka iwezekanavyo katika mtiririsho wake wa maji katika mito yetu. Kwa bahati nzuri majibu tuliyopata kutoka kwa Mkemia amesema hapana, hawakuona dalili ya jambo hilo, lakini ni vizuri tukaendelea kuhakikisha kwamba hakuna uchimbaji tena katika eneo lile kwa sababu hatuwezi kujua ni lini na kiasi gani cha Zebaki kinaweza kikatumika hapo baadaye na hivyo kikaleta madhara makubwa. Kwa hiyo hatua stahiki zilikuwa zimeshaanza kuchukuliwa, lakini kubwa zimechukuliwa kwa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie dada yangu Anne Kilango kwamba, hilo tatizo nadhani kwa sehemu kubwa sasa tutalisimamia vizuri kuhakikisha kwamba halitokei tena. Pia nataka niwahakikishie wakazi wa Vijiji vyote vinavyozunguka lile eneo kwamba tutafanya kazi nanyi vizuri, kuhakikisha kwamba jambo hili linakwenda vizuri. Kama kawaida ya uchimbaji kuna uharibifu wa kila aina, walikuwa katika baadhi ya maeneo wameziba hata mito ili kupata mabwawa kwa ajili kusafisha dhahabu. Kwa hiyo, juzi timu ile ilipokwenda ilibidi ifungue mifereji ile yote ili kuwezesha maji yaweze kutiririka kwenda katika maeneo yanayohusika. Kwa hiyo, nadhani jambo hili kwa sehemu kubwa naweza nikasema kama limekwisha. Niwasihi wananchi wa Same kwamba tuko pamoja na tutajitahidi kuona kwamba jambo hili linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni hili la posho za Madiwani. Naomba tu niseme kwa kifupi, *of course* Wabunge wengi wamelisema, nakubaliana nao na

mimi kama sehemu ya Mbunge najua kabisa kwamba ni eneo moja ambalo linatugusa wengi. Sasa tulichofanya kwa awamu hii, tumeamua kuongeza posho hiyo kutoka 120,000 waliyokuwa wanaipata mpaka 250,000 kwa kila mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tutakachofanya vile vile ni kurekebisha sasa viwango vya posho ambavyo vilikuwa vinaendana na nafasi za Wenyeviti, Mameya wa Manispaa na Mameya wa Jiji kwa sababu na wao walikuwa na viwango tofauti kutokana na posho iliyokuwepo. Lakini azma ya Serikali kwa kweli ni kuona kwamba tuendelee kupanda hiki mwaka hadi mwaka kulingana na uwezo wa Serikali utakavyokuwa unapatikana. Sasa kulikuwa na rai kwamba pengine ni vizuri Madiwani hawa wakaajiriwa kama watumishi wa umma kwa ujumla wake badala ya kutumia mtindo wa posho. Ni wazo zuri na tulishajaribu hata siku za nyuma kuelezwa juu ya jambo hili na mimi nadhani tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, yako mawazo tofauti hapa na pale, tumejaribu kutazama wenzetu nchi mbalimbali ili kuweza kujifunza zaidi, inaonekana wengi bado wanaona ni vizuri mtindo huo ukaendelea kama ulivyo sasa ili waendelee kuwasogeza karibu zaidi na jamii, mkiwaingiza kwenye *schemes* hizi zingine, wanaweza kuonekana wanaji-*distance*, wanajitenga sana na watu wanaowaongoza. Ni watu wanaotokana na maeneo ya wananchi pale, wako nao, wanaishi nao kila siku. Kwa hiyo, ukiingiza dhana ya mwajiriwa, pengine inaweza ikaleta hali ambayo inaweza ikabadili kidogo mfumo wa mtazamo kisiasa lakini vile

vile na kijamii. Lakini ni jambo linalozungumzika, tunafikiri kadri tutakavyokuwa tunakwenda, tutaweza kufanya jambo fulani kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni pensheni ya Wazee. Ni kweli kwamba kwa sasa ni asilimia ndogo sana nadhani kama asilimia nne tu ya Wazee ndiyo tuko kwenye mfumo wa pensheni, asilimia 96 ya Wazee Vijijini huko, kwa sehemu kubwa hawana mfumo wowote wa namna hiyo. Sasa mawazo tuliyonayo Serikalini ni nini? Ni kwamba; moja ni kutazama uwezekano wa kutumia hizi *Pension Funds*, Mifuko yetu ya Hifadhi kuona kama wanaweza wakaja na mfumo unaoweza kusaidia kuweka kitu ambacho ni *sustainable*. Kitu ambacho ni cha kudumu katika kujaribu kutazama namna ya kusaidia eneo hili la Wazee.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tunayo Sera ya Wazee ya mwaka 2003, lakini tulikuwa tunafikiri sasa tuifanyie marekebisho, tuone namna tutakavyoingiza baadhi ya ushauri na mawazo ambayo tunayapata mara kwa mara kutoka kwenu. Kwa hiyo, tutafanya hivyo lakini tutaangalia vile vile namna ya kutumia vyombo hivi vingine ili tuone namna ya kuwasaidia. Sasa upande wa Serikalini huku, tumeshaanza kulitazama jambo hili, lakini tunakwenda hatua kwa hatua. Kwa hiyo, mpaka sasa tulichofanya:-

(i) Tumejaribu kutafuta namna ya kuwatambua wazee yaani *identification* kwa maana ya umri, idadi yao, mahali walipo na nadhani itatusaidia kujua kwa

uhakika tunaanza na wazee wangapi kwa sababu ni jambo la msingi sana;

(ii) Kuangalia miundombinu iliyopo katika Kata na Vitongoji inayotuwezesha kujua kwa uhakika kwamba jambo hili litasimamiwa na kutekelezwa endapo tutaweza kuianzisha pensheni hiyo;

(iii) Kuangalia namna ya kupata na kutunza takwimu na taarifa mbalimbali kwa kutumia sasa TEKNOHAMA ili kurahisisha jambo hili;

(iv) Kuangalia suala zima la *cash transfer mechanism* maana wengi wako Vijijini. Hapa tunaangalia ni miundo ipi itakayotumika, kati ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Benki ya Posta, Matawi ya Benki mbalimbali, M-pesa au tutumie *Mobile Banking* zilizopo na kadhalika. Hili nalo tumeona tuliangalie, tuone namna tutakavyofanya;

(v) Kutazama gharama yenyewe ya Pensheni na hapa tunajumuisha gharama za pensheni halisi pamoja na gharama za usimamiaji na utekelezaji wa suala zima la pensheni hiyo; na

(vi) Mwisho itakuwa *of course* ni suala la vyanzo, tutapata wapi vyanzo vya kuwezesha mpango huo uweze kuwa ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hadi kufikia Juni mwaka huu yako mambo ambayo tulikuwa tumekwishafanya. Tulifanya nini? Mpaka sasa, tuligawa nchi hii Kikanda, kwa hiyo tumechagua Mikoa saba

inayowakilisha Kanda mbalimbali. Mikoa hiyo ni Rukwa, Mtwara, Dodoma, Manyara, Kagera, Pwani na Dar es Salaam. Kwa hiyo, tayari tumetuma madodoso hayo kwenye Wilaya zote kwenye Mikoa hiyo ili kuanza kukusanya taarifa zote muhimu. Tayari kazi hii sasa imeanza katika Mkoa wa Pwani pamoja na pale Dar es Salaam. Hii ni katika kujaribu kutusaidia katika yale maeneo magumu ambayo tunataka tujaribu kupata takwimu zake. Hili ni eneo moja ambalo nimeona niligusie kidogo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nimeona niliseme kidogo tu ni hili la UDA, nini hatima ya UDA. Hoja hii, ilijitokeza katika Bunge la Bajeti lililopita 2011/2012 na Wabunge wengi hasa wa Dar es Salaam walilizungumza sana. Kwa hiyo, nilichofanya baada ya pale, nikamwagiza Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (*CAG)* afanye ukaguzi maalum pale UDA jambo ambalo alifanya na alipomaliza akawasilisha taarifa ile kwangu. Nilipoipata kwa sababu kulikuwa na mambo magumu yamezungumzwa mle, nikaomba ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali akasema kwa kweli yako maeneo ambayo tunadhani yanahitaji sasa uamuzi wa msingi. Sasa kiutaratibu chini ya sheria mliyopitisha hapa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka kamili anapoona kwamba jambo aliloligundua kwa kweli lina kila dalili kwamba ni jinai, kuna kosa la jinai limefanyika, yeye anayo mamlaka sasa ya kumwomba Mkurugenzi wa mashtaka achukue jambo lile na baada ya kuchunguza kupitia taarifa aliyonayo, hatua stahiki

ziweze kuchukuliwa. Kwa hiyo, tumefanya hiyo *process* yote tumeikamilisha na hivi sasa DPP aliamua kwamba baadhi ya watu sasa wafikishwe Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wako watu wamefikishwa Mahakamani kutokana na kazi iliyofanywa na *CAG*. Sasa kwa sababu jambo lenyewe liko Mahakamani pengine naweza nikaishia hapo, lakini maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba matokeo ya shauri hilo, yatatupa vile vile mwelekeo sasa nini hatima ya UDA kwa sababu yako mambo mengi ambayo yanahusika pale. Eh! Muda unakimbia haya.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya suala hili la wakimbizi ambalo nalo lilileta tabu kidogo. Tumekuwa na wakimbizi hapa nchini na baadaye Serikali ilifanya uamuzi wa kuwapa uraia. Taarifa ile ilipofika kwenye Kamati yetu ya Bunge, kidogo wakataka kwa kweli kuelewa kilichotokea ni nini. Kwa hiyo, wakatuomba maelezo zaidi, tukaahidi kwamba basi, hili jambo tutalifanyia kazi ya ziada kabla hatujawaletea tena.

Mheshimiwa Spika, sasa kiutaratibu sisi ndani ya Serikali inabidi mpite kwenye mchakato ule ule, kwa hiyo, jambo hili tumeshafikisha mpaka kwenye Makatibu Wakuu wamelitazama, kilichobaki sasa ni kazi moja tu ya kuwasilishwa kwenye *Cabinet*. Baada ya pale tutaleta hapa. Tunachopeleka kule ni nini? Ni kupeleka lile wazo lililokuwepo la uraia ambalo ndiyo ulikuwa uamuzi kiutendaji, tulikuwa tumeamua kuufanya na baada ya kufanya utafiti wa kutosha.

Sasa Baraza litaelekeza, sasa tuelekee wapi ili tuweze kuja na kauli ya mwisho kupitia Kamati yako ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya mradi wetu wa Kigamboni ambao niliugusia hapo mwanzoni. Suala hili kusema kweli halijapuuzwa hata kidogo sema tu limechukua muda mrefu kidogo kwa sababu ya jambo gumu kidogo kwa sababu lina mambo mengi, kwa hiyo inabidi tulifanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa ninachoweza kusema ni kwamba, kama nilivyosema, tutaanza na Wabunge, ili tuwape undani wa jambo hili vizuri, walielewe, ili na wao watusaidie kulieleza vizuri. Sasa maeneo ambayo mpaka sasa tunajaribu kuyafanyia kazi:-

(i) Kukamilisha uhawilishaji wa viwango vya fidia ya mazao, nyumba na ardhi na kuvitanganza, ili vitumike baada ya kufanya uthamini katika eneo la mradi;

(ii) Kupata fedha za kulipa fidia wananchi watakaoathirika kwa kuhamishwa kupisha ujenzi wa miundombinu na huduma za jamii;

(iii) Kuanzisha Wakala ambaye atasimamia uendelezaji wa Mji Mpya (*Kigamboni Development Agency*); na

(iv) Kupata kibali kutoka Serikalini kutafuta fedha za kujenga Mji Mpya, nje ya fedha za kawaida za

Serikali na kuruhusiwa kuuza *Municipal Bonds* ambazo zilishakubalika, kama njia za kupata fedha za kugharamia mahitaji ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kukumbusha kwamba, zuio ambalo liliwekwa na Serikali kusitisha maendelezo yoyote ndani ya eneo la mradi, hili lilimalizika mwezi Novemba 2011. Hii ilikuwa ni makusudi kwa sababu, baada ya pale tuliona ni vizuri waendelee kwa sababu, mradi wenyewe utakuja polepole. Kwa hiyo, isije tukawa tumeng'ang'ana, tumegandisha watu lakini hakuna kinachoendelea. Lakini na sisi tunaendeleza hii jitihada ili tuweze kwenda na wakati. Kwa hiyo, tunaamini tutafanikiwa kuliharakisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la Jiji letu la Dar-es-Salaam. Hadhi ya Jiji hilo, maana nalo limesemwa na kwa hisia nyingi. Niseme tu kwamba, Jiji la Dar-es-Salaam, limekuwa na matatizo mwengi ya kimuundo na kimfumo. Manispaa zile tatu kwa kipindi kirefu, zilikuwa zikilalamika sana kwamba, Muundo huu hauna tija. Mnakuwa na Chombo pale, lakini hakina eneo, badala yake kinaonekana kama kinaingilia Manispaa zile tatu; mara washike Kituo cha Basi, mara washike Kariakoo, mara washike Makusanyo ya kwenye *Tax,* lakini yale yote yako kwenye Manispaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kilikuwa kilio cha muda mrefu. Kwa hiyo, tukaamua kwamba, basi, hebu tuunde timu ya Wataalam; tukapata Wataalam, *Consultancy,* wakatufanyia kazi, wakaja na mawazo kwamba, pengine tuige baadhi ya nchi nyingine zinafanyaje.

Kwa hiyo, tukafikia mahali tukasema basi, tuchukue eneo moja pale, Ilala, tuipe hiyo hadhi, ili Manispaa zile nyingine zibaki kama zilivyo. Huyu atakuwa na eneo lake, eneo la kukusanya mapato na wenzake wataendelea kuwa na maeneo yao na hakutakuwa na hili li-*Umbrella Organisation,* ambalo wakati mwingine nalo linapata *challenges* nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, timu ile imemaliza kazi. Jambo hili likapelekwa kwa Wadau mbalimbali, tukalizungumza, likarudi Serikalini. Baadaye tukafanya uamuzi kwamba, basi tuvunje lile Jiji, tuipe hadhi hilo eneo.

Mheshimiwa Spika, tulipochukua ule uamuzi, hisia nyingine zikaja kwamba, ahaa, hamjafanya kazi hiyo vizuri, hebu acheni. Bahati nzuri tulikuwa hatujakwenda mbali, kwa maana kwamba, tulikuwa hatujaleta *notice* yoyote hapa kwako Bungeni, ambayo ndio inahalalisha ule uamuzi ambao tunakuwa tumeufanya Kiserikali. Kwa hiyo, tukasitisha lile zoezi. Mambo mengine yakaendelea kama kawaida. Kwa hiyo, Jiji lile tunalolijua likaendelea na shughuli zake, Ilala ikaendelea na shughuli zake, Kinondoni hivyo hivyo na Temeke hivyo hivyo. Hakuna kilichohama, hakuna mtumishi aliyefanya nini, kwa hiyo, ikawa ni kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya uamuzi ule ikabidi tufikirie kwamba, sasa tumefanya hivi, sasa tunafanyaje kurejesha kile tulichokuwa tumedhani tumekiondoa? Kwa hiyo, tukaja tena na *Government Notice* nyingine, ambayo na yenyewe baadaye

ikaonekana nayo hapana, bado hamjaitenda kazi vizuri. Kwa hiyo, juzi hapa baada ya kushauriana sana na Wataalam na Wabunge vile vile, ikaonekana basi, lazima tutoe sasa *Notice* inayofuta vyote viwili, ili ibakie kama ilivyokuwa tangu zamani. Kwa hiyo, ndicho tulichofanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi Jiji la Dar-es-Salaam, kusema kweli ni sawa na kama halikuvunjika. Maana hatukuwa tumekamilisha mchakato wa kuvunjwa kwa lile Jiji. Sasa kumekuwa na yale mawazo kwamba, kwa hiyo, hata Meya aliyekuwepo na yeye hakuwepo kisheria; lakini Wataalam wetu walituambia hapana, kwa vile taratibu zote zilikuwa hazijakamilika, ni sawa kama mlikuwa hamjafikia hatua ya mwisho. Kwa hiyo, hakuna sababu yoyote ya kufikiria hivyo. Kwa hiyo, nataka niwasihi tu Viongozi wa Dar-es-Salaam, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Dar-es-Salaam, basi tulione hivyo na tuendelee sasa kuchapa kazi kama ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo tu juu ya bomba la gesi la Mtwara. Hapa ninachotaka kusema kwa ufupi tu ni kwamba, kama alivyosema Profesa Muhongo, tunayo gesi ya kutosha. Lakini sisi tumejikita zaidi katika mradi huu kwa kujua kwamba, utakuwa na manufaa sana kwetu sisi. Lengo ni kuongeza uwezo wa umeme katika nchi yetu, ilikuwa hasa ndio lengo la bomba hili.

Mheshimiwa Spika, sasa kazi ile, pesa zimeshapatikana na tayari wazo lile la kuanza kujenga

ule mradi limeanza. Sasa yaliyojitokeza hapa ni kwamba, sawa, lakini gesi inatoka Mtwara, inatoka Lindi, mnaipeleka Dar-es-Salaam, sisi tuliobaki hapa tunafaidika vipi na hiyo gesi pamoja na wale wa Lindi na Mtwara? Ambayo ni hoja ya msingi tu, ni jambo la msingi kabisa na nimelikubali.

Mheshimiwa Spika, nilichosema tu ni kwamba, basi hili jambo tutalizungumza tuone ni mahitaji gani yanahitajika pale. Kwa hiyo, tufanyeje ili kuhakikisha bomba hili haliruki tu na kuruka na kupepea na kuwaacha wananchi bila kujali ni nini kinaendelea. Kwa hiyo, tutalizingatia na naamini, tutakwenda vizuri. Lakini kwa ujumla niseme, kwa wana Mtwara na Lindi, nadhani sasa kumekucha na nadhani mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kuteuliwa kwenda Mtwara, Lindi, mwaka 1977 kama Wakili wa Serikali Mfawidhi, ambaye nilikuwa nasimamia Kanda ya Kusini, kwa maana ya Ruvuma, Lindi na Mtwara. Kufuatia uteuzi ule, nilichokipata ni ndugu zangu na marafiki zangu wa Dar-es-Salaam na sehemu nyingine, kunipigia simu kunipa pole na kuniambia kuna nini? Kwa nini unakwenda Mtwara? Umekosa nini? Kwa sababu, ilionekana kama vile Mtwara hakufai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikasema nimepanda hapa, nimeukata, wewe unanipa pole, ya kitu gani tena? Nakwenda kuwa *State Attorney Incharge,* Mungu akupe nini? kwa hiyo, nikaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilivyokwenda kule, mie sijui bwana, labda kwa vile mtoto wa mkulima tabu yake ndio hiyo, nilipaona Mtwara pazuri sana. Nimekuta wana uwanja wa ndege ambao Mpanda, Rukwa, sina. Nikakuta pale kuna kalami ambayo kule nilikuwa sina, nikaona majengo pale mazuri ambayo sikuwa nayo kule Mpanda, kwa hiyo, kwa kweli wala haikunipa tabu. Nikapaona ni pazuri, lakini baadaye nikaja kugundua kwamba, kulikuwa na mambo mengi ya msingi hasa mawasiliano ya njia, barabara ngumu, na kadhalika. Kwa hiyo, nikaelewa kweli maendeleo yalikuwa bado hayajafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kizuri ni kwamba, sasa hivi kumekucha. Nadhani watu wa Mtwara na Lindi, ni kujipanga vizuri na Serikali tutakuwa nanyi kuhakikisha kwamba, hiyo fursa inayoibuka pale, iwanufaishe kweli watu wa Lindi, Mtwara na Kusini kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya msongamano wa magari pale Dar-es-Salaam. Limesemwa na najua linanigusa. Wakati mwingine nikiwa kwenye gari, unaona hata aibu, sababu unajisikia vibaya sana unapoona wewe unasababisha msongamano juu ya msongamano ambao tayari upo, lakini ndio hivyo tena.

Mheshimiwa Spika, lakini kifupi tu niseme kwamba, ule mradi wa mabasi yaendayo kwa kasi, unaendelea vizuri. Tumekopa karibu shilingi bilioni 290 ambazo ni karibu Dola 182 milioni, kutoka Benki ya Dunia. Pale tuna ujenzi wa barabara kwa ajili ya kuweka njia za mabasi yaendayo haraka, zenye urefu wa kilometa

20.9, tunaanza Kimara mpaka Kivukoni. Na matawi mawili kuanzia Magomeni hadi Moroco na *Fire* hadi Kariakoo, pale pana tawi lile. Kwa hiyo, ujenzi wa Vituo vya Stesheni ya Mabasi, vitano vitajengwa, vituo vikubwa 29, vituo vidogo sita na karakana mbili za kuegesha magari, yaani *depots.*

Mheshimiwa Spika, miradi hii ilichelewa kuanza kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo, kutopatikana mapema kwa makandarasi wenye uwezo, lakini hatimaye walipatikana. Miradi yote sasa imeanza kutekelezwa baada ya kuondolewa zuio la Mahakama na kupatikana kwa mkandarasi. Kwa hiyo, sasa tumeanza, tunaendelea vizuri, imani yangu ni kwamba, miradi yote hii itakamilika *on time,* ili angalau tuweze kuwa na fursa ya kuwa na barabara kubwa inayowezesha hiyo kazi kufanyika.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, tutaendelea vilevile na juhudi zetu, maana pale tuna *fly over* moja ambayo, ni lazima tuitafutie suluhu ambayo ni muhimu sana, pale kwenye *junction* ya *TAZARA.* Kwa hiyo, hiyo mazungumzo yake yanaendelea, tukifanikiwa basi na yenyewe itatusaidia kupunguza kiasi fulani msongamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile waliuliza kuhusu *ring roads*. Bado mradi ule upo. Ni suala la fedha, kadri zitakavyokuwa zinapatikana tutaendelea kufanya hivyo kwa kadiri itakavyowezekana. Kwa hiyo, nimeona niliseme hili kwa sababu, ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa vile muda nao umenikabili, naomba niseme, sijui kama nitalimaliza, hili tatizo la kahawa Mbozi. Mheshimiwa Chiza, alijaribu kutaka kuanza kulieleza, lakini muda ukamuishia.

Mheshimiwa Spika, niseme tu hivi kwa ufupi kwamba, nimemsikiliza ndugu yangu Zambi, nimewasikiliza na wenzake waliochangia katika eneo hili. Kubwa nililojifunza kutoka pale ni kwamba, kilio chao ni namna ya kumsaidia mkulima mdogo, aweze kuongeza thamani katika zao lake la kahawa. Ndio jambo kubwa wanalolitafuta. Sasa, uongezaji wa thamani nao nimejifunza kumbe una hatua nyingi kabla hujauza kahawa yenyewe katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kilio chao pale ni kwamba, huyu mkulima mdogo, anapouza kahawa, hata kama ni ile mbivu, isiuzwe kwa bei ambayo ni ya kumlalia au ya kumuonea. Maana wakati ameanza kilio hiki ilikuwa ni 500/= wakati wenzake jirani kule, Mbinga, ni 1,000/=. Kwa uwiano niliopewa, angalau inatakiwa isipungue 1,000/= hata kama ni mbivu, ila lengo kwa kweli ni kwenda katika hatua hiyo nyingine ambayo ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa nimelielewa. Nimejaribu kupitia Sheria ya Kahawa, nimepitia Kanuni za Mwaka 2003, nimepitia Sheria ya 2009, nikapitia Kanuni zile za 2012. Nimejaribu kuona tatizo lililopo pale, ninachoweza kusema ni kwamba, cha msingi ninachokiona kwa ujumla wake, lengo ni namna gani tuthaminishe kahawa ili mkulima aweze kufaidika. Sasa yako mawazo ameyatoa kwamba, pengine

tupige marufuku wale wanunuzi; nakubaliana naye, lakini ni lazima nalo tulipime kwa uangalifu mkubwa sana. Kwa sababu, tunaweza tukafanya hivyo, tukakuta tena tumewanyima fursa hata ile ambayo ingeweza ikapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoweza kushauri tu ni kwamba, sisi atupe nafasi. Kwa vile, bado Bunge, linaendelea, acha tulizamie zaidi, tushauriane na wadau zaidi juu ya jambo hili, tuone ipi itamnufaisha zaidi mkulima, katika mazingira ninayoyaona mimi. Viko vikundi pale, ziko *CPUs* kweli zimejengwa, lakini inawezekana zisiwe nyingi sana.  Pia mkulima naye ni lazima tumsaidie kupata Chama cha Ushirika chenye nguvu, maana bila ushirika huu, sioni atauzaje kwenye Soko la Dunia. Ni lazima tutapita kwenye mikondo ya watu wengine ambao ndio watu wakubwa. Kwa hiyo, hili jambo nadhani tutalifanyia kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili alilolisema ni kuhusu Bodi; muundo wa Bodi na namna ulivyo. Nimekubaliana naye, nimepitia Sheria, nimetazama ni namna gani *Board Members* wanapatikana. Ni kweli, lazima tukubali kwamba, katika orodha na namna walivyopatikana yako maeneo nadhani hatukuwa tumeyatazama vizuri. Kwa hiyo, hili, tutalirekebisha. Tutalirekebisha kwa sababu, kuna vitu ambavyo havikuwa vimezingatiwa kwa namna inavyostahili. Kwa hiyo, katika hili nakubaliananaye na nimeona kwamba, niliseme dhahiri kabisa kwamba, halina tatizo, tutajaribu kuona ni nini cha kufanya.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui kama muda utaniruhusu, niseme lingine moja. Mgogoro wa Wawekezaji kule Kagera. Kule tunayo mashamba ya *NARCO* ya wafugaji, lakini yamekuwa na mgogoro wa muda mrefu sana, lakini sasa nafikiri tumefikia mahali pazuri. Juzi tulikutana, tumelizungumza, yako mawazo mazuri sana ya namna ya kutenganisha na kuwawezesha wananchi wale kuwa na maeneo yao ya uhakika, kuliko ilivyo sasa. Vile vile ni lazima tuhakikishe kwamba, ule utaratibu wa kuleta ng'ombe kutoka nchi jirani kuja kulisha pale, tena kwa gharama, wanatozwa na badhi ya viongozi ambao sio waaminifu kule, tunaupigania sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoweza kusema tu ni kwamba, nataka nikuhakikishieni Waheshimiwa Wabunge wote kutoka eneo lile, hili jambo nadhani limefikia mahali pazuri, sasa tushirikiane tu ili tuone namna tutakavyotekeleza hilo jambo haraka itakavyowezekana na tuweze kuhakikisha linakwenda vizuri. Kwa hiyo, hili nataka niliseme tu kwa kifupi kwa sababu ni jambo linaloeleweka.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nigusie kidogo ni mauaji ya walemavu wa ngozi. Aah, hili eneo bwana ni gumu, wakati mwingine linatia simanzi. Jana Mheshimiwa Kwegyir, vilimshinda na ni kweli ni lazima litakushinda tu kwa sababu, mauaji haya ni ya kikatili mno.

Mheshimiwa Spika, huyu marehemu, mauaji yake yametokea tarehe 26 Mei. Wamepata ile maiti kule Arumeru, Arusha. Alikuwa ni mwanaume

wanamkadiria kati ya miaka 25 mpaka 30, aliokotwa kandokando ya Mto Nambara, amekufa. Akaonekana amekatwa mikono yote miwili, kanyofolewa sehemu za siri na ngozi za usoni zimechunwa.

Mheshimiwa Spika, mwili wake ulikutwa umepasuliwa na kuchukuliwa mapafu. Hali iliyosababisha kuwepo kwa hisia, *strongly, of course* unaweza ukawa mweupe watu wakadhani kwamba, si mlemavu wa ngozi. Lakini baada ya kuona haya yote, ni dhahiri kabisa kwamba, ni wale wale ndugu zetu ambao kila siku wamekuwa ndio walengwa. Sasa jamani, jambo hili kama nchi, kama Taifa, tabu. Unapofikia hatua hii, sishangai kwamba, Mheshimiwa Kwegyir alitoa machozi.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nitoe wito. Niwasihi sana Watanzania na Viongozi wenzangu wote, Madhehebu ya Dini, ndani ya Serikali, sisi Wabunge na wengine wote. Hili jambo ni letu sisi wote, maana ushirikina ni kitu ambacho ni kigumu sana, unakifanyaje? Maana kubwa ni elimu, lakini hatujafika huko. Kama unavyoona mauaji mengi ni ya usiku, katika mazingira hayo, kinachohitajika ni elimu, kinachohitajika ni sisi wote tujitose ku-*fight* kweli kweli, huku kote mnakokwenda. Kila mmoja aliseme kwa njia ambayo itatusaidia kumaliza mgogoro huu *once and for all.*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge. Wengi mmesema sana juu ya amani na utulivu. Nasema chondechonde, wote tulione hili kwamba, ni letu sisi wote. Najua wakati mwingine watu

wanapoona kwenye runinga, wanaona Misri, wanaona Libya, wanafikiri jambo lile ni la faraja; si la faraja hata kidogo, hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watazameni hawa tangu walipofaulu kufanya hayo waliyoyafanya mpaka leo wanavyohangaika kurejesha amani. Tazameni watu wanavyouawa pale bila sababu. Angalieni mali za watu zinavyoharibiwa bila sababu. Si jambo la kuenzi hata kidogo. Uvunjifu wa amani, kukosekana kwa utulivu, kukosekana kwa amani ni lazima wote tuseme, haina nafasi katika Taifa letu la Tanzania, ndipo mtaona ni nini tufanye katika eneo hili. Nawasihi sana na nakubaliana na Wabunge wote kwamba, hili ni letu, tulivalie njuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna fedha huko katika Benki ya Uswis na nimeliona kwenye magazeti na kwenye mtandao. Mheshimiwa Kabwe kasema, Mheshimiwa Mariam Msabaha na yeye alilisema. Tulichofanya, kwa mujibu wa taratibu za nchi hii, maana hili jambo liko nje ya nchi yetu, kwa hiyo, kinachotakiwa hapa ni watu wa TAKUKURU, mnamuarifu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwanasheria Mkuu wa Serikali sasa anaiarifu *Foreign,* Mambo ya Nchi za Nje ili wao sasa *to liason* na Vyombo vinavyohusika kwa lengo la kupata ni nini kimetokea katika eneo hili. Sasa hiyo kazi tumeifanya, kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunapata matokeo ili tuweze kuona tunafanyaje. Kama litakuwa na ukweli, basi hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo, mmetuasa sana juu ya uwajibikaji wa utendaji ndani ya Serikali.

Ndugu zangu nalipokea kwa mikono miwili na nimekuwa nalisema sana. Tutaendelea kulikazia sana ili kuhakikisha kwamba, sisi mliotuamini mkatuweka katika nafasi hizi, uwe Waziri Mkuu, uwe Waziri, uwe Mkuu wa Wilaya, uwe Mkuu wa Mkoa, uwe nani, ni lazima tukubali kwamba, hii ni dhamana tuliyopewa na umma na ni lazima tuhakikishe kweli tunatekeleza yale mnayotuasa.

Mheshimiwa Spika, ubadhirifu, rushwa, matumizi mabaya ya madaraka, usimamizi mbovu wa fedha, ni mambo ambayo lazima tuendelee kwa kweli kuyakemea. Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kupitia Kamati zile tatu, Kamati zile zote za Kisekta, kazi mnayoifanya ni nzuri. Inatusaidia sana ili tuweze kufanya vizuri zaidi. Eeh, wameniambia Mzee, muda umekwisha; alaah, kweli!

Mheshimiwa Spika, basi naomba nimalizie tu kwa kusema kwamba, nawashukuruni sana. Nawashukuruni sana kwa michango yote mizuri. Nawashukuru sana Wapiga Kura wa Jimbo langu la Katavi kule, najua wananivumilia muda mrefu hatuonani, lakini *Inshallah*, muda si mrefu tutawaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirejee kuwashukuru Mawaziri wangu, kwa jitihada wanazofanya kunisaidia. Lakini kwa namna ya pekee niseme kwamba, ninapotembea hapa nchini kuna vitu vinanigusa sana, moja ni la maji na kuna maeneo yamenigusa sana, moja ni Kondoa. Kondoa kuna tatizo la maji la aina yake, sijui wana jiolojia ya namna gani.

Mheshimiwa Spika, sasa pale nina Mradi wa Ntomoko, ulikuwa na sifa kubwa sana. Nimedhamiria kuona kama naweza nikaufufua ule mradi, ili kusaidia jamii yote inayokaa pale. Kwa sababu, ni mradi mmoja ambao hatuwezi kuuacha ukafa bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni pale Orkesmen Simanjiro Makao Makuu, nimekwenda pale mara mbili, tatu sijawahi kuona eneo lenye tatizo la maji kama nililoliona pale. Matumaini yangu ni kwamba, kadri muda utakavyokuwa unakwenda hata ndani ya bajeti hii tuone ni namna gani naweza kusaidia sehemu kama hizi ili kupunguza ile kero kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kwenda Newala, nikakuta nako kuna tatizo *unique* la maji pale, maana mpaka watu wanataka kupigana. Kwa hiyo, ninapopita pita kuna vitu vinavuta hisia zangu, nimeona niliseme hili katika jitihada za kuona tu nini tunaweza kusaidia katika baadhi ya maeneo au kuona namna ya kuweza kuwasaidia zaidi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mama Pinda na leo naona yupo, nafikiri kuwepo kwake kumenipa nguvu kweli, yeye akichungulia hivi napata nguvu kweli kweli. Yeye akichungulia hivi napata nguvu zaidi, kwa hiyo mama nakushukuru sana, nawashukuru watoto na wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono, sasa tutaingia katika hatua nyingine.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea napenda kueleza kwamba Kamati ya Matumizi, kufuatana na kanuni yetu ya 100 imeeleza kwamba mjadala wa jumla kuhusu makadirio na matumizi kwa Wizara utakapomalizika Bunge litaingia katika Kamati ya Matumizi ili kupitisha makadirio ya Wizara husika kifungu cha kifungu. Kwa hiyo, ndiyo kazi ambayo tutaifanya. Lakini wakati huo mnakumbuka kwamba tumekubaliana kutokana na matatizo yetu ya muda na wingi wetu, utaratibu ni kwamba, mnaotaka ufafanuzi tulikuwa tunatumia dakika tano, lakini sasa tutapunguza zitakuwa dakika tatu.

Halafu kuna masuala ambayo ni muhimu hasa neno la kutoa shilingi. Kutoa shilingi kwa kweli ni namna ya kujenga hoja ya kupata muda wa kujieleza kile unachotaka. Kwa hiyo, ukishatoa shilingi yako unaweza kuungwa mkono na wenzio wawili, watatu halafu tunauliza Serikali halafu tunakuuliza wewe mwenyewe. Kama unang'ang'ania shilingi yako tunapiga kura kama umebakia nayo, basi, bajeti itapita lakini itakuwa imeonesha dosari hiyo. Lakini kama wamekushinda wenzio basi na wewe itabidi ukubali.

Waheshimiwa Wabunge kuna eneo ambalo tunafanya makosa, mara nyingi mshahara wa Waziri kwa mujibu wa kanuni yetu ya 101(3) ni maswali kuhusu sera. Pale katika mshahara wa Waziri ukianza kuuliza ile shule yangu hamjajenga, katika kijiji changu maji hamjaleta, siyo madhumuni ya mshahara wa Waziri. Someni kanuni inasema mtauliza jambo mahususi la kisera, sana unaweza kuuliza kuhusu utaratibu wa Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia unakwendaje, ndiyo wakati wake, siyo habari ya maji katika kijiji fulani. Kwa hiyo, someni kanuni ile inasema kabisa kwamba Mbunge ataruhusiwa katika kifungu cha mshahara wa Waziri endapo ataomba ufafanuzi wa suala mahususi la sera na hatazungumzia mambo mawili ya aina hiyo, hiki ni kifungu cha 101(3).

Uzoefu wa bajeti zilizopita Waheshimiwa Wabunge wanauliza ujenzi wa shule katika Kata na Jimbo lake na kutumia mshahara wa Waziri jambo ambalo halikubaliki. Kinachokubalika hapa ni sera ya ujenzi wa shule. Kwa hiyo, naomba sana maana yake tunatumia muda mwingi sana kwenye mshahara wa Waziri kuuliza vitu vidogo vidogo, hatufiki kwenye maendeleo, mara nyingi katika vitabu vya maendeleo hatufiki na Spika anaruhusiwa kuongeza dakika 30 baada ya muda wa kawaida wa kuahirisha Bunge ukifika.

Muda ule ukifika, zikibakia dakika kumi, tunafanya kitu kinaitwa *guillotine, guillotine* ni kwamba tunapitisha vifungu vyote vizima vizima, jambo ambalo kwa kweli hatulipendi, lakini kwa sababu ya kutumia muda vibaya kwenye mshahara wa Waziri, basi tunafikia

mahali kama hapo. Leo hii tutakuwa na vitabu vitatu mikoa, katika mikoa tutapita fungu kwa fungu hatuwezi kuingia kwenye *detail* ya mkoa mmoja mmoja, la sivyo tutalala hapa. Kwa hiyo, hayo ndiyo machache ambayo nilipenda myazingatie Waheshimiwa ili tufanye kazi yetu kwa utaratibu na ufanisi mkubwa sana katika muda tulionao. Kwa hiyo, sasa tunaingia katika Kamati ya matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 25 – WAZIRI MKUU**

Kif. 1001 - *Administration na HR Management...* ... .5,908,141,000/=

**MWENYEKITI:** Nilifikiri mnasimama mshahara wa Waziri, ni 37 siyo hapo, hii ni ofisi binafsi. Mheshimiwa Mbunge hii ni ofisi binafsi, mshahara wa Waziri ni fungu 37 hii ni ofisi binafsi hatuulizi hiyo. Unataka kujua nini?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Naam!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Napenda kupata ufafanuzi katika fungu hilo hilo, siyo mshahara wa Waziri Mkuu, napenda kupata ufafanuzi katika fungu hilo hilo…

**MWENYEKITI:** Sawa!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Ukurasa wa 102, nilipenda kupata ufafanuzi katika *sub vote* 1001 kifungu kidogo cha 220700 ambacho ni cha *Rental Expenses*. Kwenye hiki kifungu kwanza kinaonekana kinapanda kila mwaka, lakini pia mwaka huu ukiachilia mbali mwaka jana kilikuwa milioni 965, mwaka huu ni bilioni 1,312,000,000. Wakati nacheki kwenye randama nikaona kwamba hizi fedha zimetengwa kwa ajili ya kulipia deni na gharama za kukodisha ndege kwa ajili ya safari za kazi. Kwa hiyo, napenda kupata ufafanuzi kwanza kifungu kimechanganywa, wamechanganya *rental expenses* ni milioni 24, lakini vitu viwili vimewekwa pamoja kukodi ndege na *rental expenses,* sidhani kama vilitakiwa vikae sehemu moja, lakini pia Kiswahili chenyewe kimekosewa wameandika kwamba ni kukodisha ndege badala ya kukodi ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nipatiwe ufafanuzi ni deni gani la ndege? Lakini pia hizo pesa kuwekwa kwenye fungu la *rental expenses, is it right* au ilitakiwa iwekwe kwenye *travelling country*.

**MWENYEKITI:** Nani anajibu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uratibu, Sera na Bunge)!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (URATIBU, SERA NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba fungu hilo linahusika na kukodi ndege kwa safari za kikazi. Ndiyo maana limewekwa katika *rental expense,* kukodi ndege na ndege mara nyingi tunakodi ndege za Serikali na ni kweli gharama

zimepanda, kwa sababu hata gharama ya ukodishaji sasa kwa saa zimepanda. Lakini pamoja na hilo mwaka huu tunadaiwa ukodishaji wa ndege za Serikali sh. 560,000,000/= kwa hiyo fedha hizi zitatumika kulipa deni ambalo tayari safari zimeshafanyika. Kwa hiyo, ni ukodishaji wa ndege kwa safari za Mheshimiwa Waziri Mkuu za kikazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 37 – OFISI YA WAZIRI MKUU**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management...* ...4,345,645,000/=

**MWENYEKITI:** Haya wasimame wanaotaka, hautoshi mshahara wa Waziri, nyie vipi! Nianze na Mpina, nawataja kwanza atakayetajwa jina atakaa. Haya tunaanza na Mheshimiwa Rajab.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka Waziri anitolee ufafanuzi jinsi ya Halmashauri kuweza kubadilisha mtindo ulionao wa kutumia benki moja tu hapa nchini. Kwa sababu hata katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilionesha kwamba Halmashauri pamoja na watendaji wa benki walikuwa na mchezo ambao wanacheza wa kuiba baadhi ya fedha. Sasa tulitaka kuwe na uwezo zaidi, kwamba Halmashauri ziruhusiwe kutumia na benki nyingine hususan benki zile ambazo zinamilikiwa

moja kwa moja na Watanzania wenyewe. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anipe kauli juu ya hili.

**MWENYEKITI:** Benki moja ni ipi hiyo?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Benki ya *NMB* pekee yake.

**MWENYEKITI:** Haya naomba wenyewe muwe tayari kujibu, nani? Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo? Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi ni kweli Benki ambayo inatumika na taasisi karibu zote hasa Halmashauri zetu ni Benki ya *NMB* kwa sababu ndiyo benki ambayo imeenea katika wilaya zote za Tanzania. *(Makofi)*

Sasa kuhusu kutumia benki nyingine labda ni suala la kuzungumza na kulitazama.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Miongoni mwa kero na kama alivyoziita Mheshimiwa Waziri Mkuu changamoto za Muungano, ni Mfuko wa Pamoja wa Fedha. Mfuko huu ni kwa mujibu wa Katiba na miaka mingi toka ilipopendekezwa na Katiba karibu miaka 34, Bunge limetunga sheria lakini utekelezaji wake bado. Suala lililobaki ni fomula ya mapato na mgao wa fedha. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, je, tukimpitishia bajeti yake ataweza

kutuhakikishia kwamba suala hili litapatiwa ufumbuzi mara hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Akaunti ya Pamoja ya Fedha, tayari kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waraka umeshajadiliwa na ngazi ya Makatibu Wakuu na upo njiani kwenda katika Baraza la Mawaziri. Baada ya kujadiliwa na Baraza la Mawaziri, utekelezaji utaanza mara moja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee! Mimi nitaitaita tu, msiniulize.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate ufafanuzi kutokana na maelezo ya Waziri Mkuu kuhusiana na suala zima la uwekezaji na hususan *Memorandum of Understanding* aliyoingia baina yake yeye kwa mantiki ya Halmashauri pamoja na *AGGRESOL*. Waziri Mkuu amesema kwamba hayo wamekubaliana katika *feasibility study* peke yake. Lakini ukiangalia vipengele vya hii *Memorandum of Understanding* kuna vipengele vingine ambavyo vinabainisha wazi kwamba Halmashauri pamoja na Mwekezaji wana mipango ya kuingia mkataba wakati tunajua kwamba sheria za nchi haziruhusu kabisa suala la uwekezaji, Halmashauri kuingia mikataba, bali masuala yote lazima yajumuishe Tanzania *Investment Centre*. Sasa kwa kuwa hii *Memorandum of Understanding* ina vipengele ambavyo vinaonesha kama pande mbili zikishindwa kuelewana kutokana na

*terms* ambazo ameziandika hapa watapelekana katika Mahakama za Kimataifa.

Sasa nilitaka Waziri Mkuu atuambie kwa kupitia hili Bunge kwamba, hii *Memorandum of Understanding* ambayo Halmashauri imeingia haina maana na kwamba baada ya hiyo *feasibility study* mchakato wa kisheria kwa mujibu wa sheria za nchi inayohusiana na uwekezaji utafuatwa? Lakini vilevile kwa kuzingatia kwamba mmoja kati ya wabia wa AGGRESOL amejitoa ambaye yeye kazi yake kubwa ya msingi ilikuwa ni kuwasaidia wakulima wadogo wadogo, *status* ya AGGRESOL ikoje? Lakini vilevile atuambie kwa kuzingatia udogo wa maeneo ambayo yanapelekea migogoro baina ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Mpanda, hadhani kwamba ni busara kuacha eneo husika liweze kuendeshwa na wananchi wenyewe kwa msaada wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, kengele ikigonga, imegonga. Kwa hiyo, kila mtu ajipange dakika tatu ni chache, uwe *clear* maana yake ukileta *story* ndefu hakika hupati muda.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Naamini Waziri Mkuu amenielewa vilivyo.

**MWENYEKITI:** Basi ni vizuri ukae chini sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, napenda nimwambie Mheshimiwa Halima Mdee, kwanza ni Mwanasheria anajua maana ya *MOU*. *MOU* siyo msahafu na wala siyo mkataba bali ni makubaliano ya awali. Naomba aendelee kumwelewa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kaongea Kiswahili chepesi, rahisi na kinachoweza kueleweka na mtu yeyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee ni mara moja tu kanuni tumesoma hapa. Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru…

**MWENYEKITI:** Hujasikia nimesema kwamba badala ya kusubiri uitwe mara mbili ni mara moja tu!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nataka kupata ufafanuzi kwa sababu kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu kwamba tukipitisha fedha hizi je, Serikali iko tayari kuwa inatupatia Wabunge taarifa za fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri kila mwezi na fedha ambazo zinakwenda kwenye Mashirika yote ya Umma,? Tuwe tunazifahamu kila mwezi ili tuweze kujua fedha hizo zimekwenda na zinakwenda kutumikaje kwa sababu unakuta Wabunge hatuna taarifa ya fedha ambazo zinakwenda kwenye Halmashauri ili tuweze kufuatilia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI

kila inapopeleka fedha kwenye Halmashauri kila baada ya miezi mitatu inachapa kwenye magazeti. Lakini pili, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo kama alivyo Ndugu yangu muuliza swali anakuwa moja kwa moja Mjumbe wa Kamati ya Fedha, ajitahidi tu awe anahudhuria vikao vya Kamati ya Fedha kwa sababu pale ndipo inapotolewa taarifa ya fedha zilizopokelewa na Halmashauri. (*Makofi*)

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nataka niombe radhi kwa yaliyojitokeza jana kwa Madaktari kwani sivyo ndivyo nilivyokuwa nimeongea.

Pili, nataka kuuliza kwamba, katika mchango wangu nilikuwa nataka kujua hati miliki za wale ambao mashamba yao hayaendelezwi zitafutwa lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ngonyani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati inapatikana kisheria na kwa hiyo kufuta hati napo itafuata mkondo wa sheria na kwa vile ni jambo mahususi katika Jimbo la Mheshimiwa Ngonyani basi mimi na yeye tutakaa na kuangalia na wale wote wanaohusika ili tuone ni nini ambacho tutakifanya.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya amri iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa

wa Singida wiki iliyopita tarehe 20/6 ya kupiga marufuku wanunuzi binafsi wa zao la alizeti kununua kutoka kwa wakulima na badala yake kuelekeza kwamba wanunuzi pekee kutoka kwa Wakulima watakuwa ni Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi ya Mkoa wa Singida *especially* Jimboni kwangu hakuna Vyama vya Ushirika, hakuna *points* ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuuzia alizeti. Kwa hiyo, hii amri imeleta mfadhaiko mkubwa sana kwa wananchi wa Mkoa mzima. Amri inasema kwamba atakayekutwa anauza au ananunua alizeti nje ya utaratibu huu atakamatwa atapelekewa Mahakamani na atafungwa miaka miwili na watu wanakamatwa, wananyang'anywa mali zao na kwa kweli imeleta mfadhaiko mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ninavyofahamu mimi kwanza Mkuu wa Mkoa hana mamlaka ya kisheria ya kutoa amri kama hiyo, sheria ya Tawala za Mikoa haimpi madaraka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, pamoja na kwamba naelewa lengo ni kuondoa walanguzi wanaonyonya wakulima, utaratibu mzuri ungepaswa uwekwe wa kuhakikisha kwamba wakulima wanaoneshwa mahali ambapo watauza alizeti yao, bei itangazwe, watakaokwenda kununua wajulikane lakini hili halijafanyika na matokeo yake kuna *confusion* kubwa, watu wanahangaika na kukosa kujua waende wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze tunafanyaje sisi ambao tunalima alizeti bila msaada wowote, tukishaivuna inapata wajanja zaidi wanaojua namna ya kutuambia tuiuzeje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa *RC* wa Singida ametoa amri hiyo kwa kutaka kuwatetea wakulima wapate bei nzuri kupitia ushirika wao ili wafanyabiashara mmoja mmoja wasiende kwenye shamba moja moja au nyumba moja moja, alikuwa na nia njema kabisa. Najua kuna Vyama vya Ushirika Singida, Singida ni jirani zangu na mimi nilikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, inawezekana kabisa Vyama hivyo vya Ushirika visitosheleze, lakini amri hii ya Mkuu wa Mkoa haiwezi kupuuzwa. Sasa kama kuna changamoto zinazotokana na hiyo amri wananchi na Mkuu wao wa Mkoa wa Singida wataiangalia lakini nia ni njema kabisa na *RC* huyo ndiye anamwakilisha Rais kwenye Mkoa wa Singida na ndiye anayependa wakulima wa Singida ambao ni wapiga kura wa Mheshimiwa Tundu Lissu wapate bei nzuri. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri Mkuu. Ni dhahiri kwamba elimu nchini sasa hivi inashuka kwa kasi kubwa sana na moja ya

changamoto tumekuwa tukisema ni miundombinu, lakini cha kusikitisha pia umakini unakosekana katika sekta hii ya elimu. Juni 2012 wanafunzi wa Shule ya Msingi kwa maana ya darasa la saba Mkoani Mara walifanya mtihani wa hisabati wa *Mock*, lakini cha kusikitisha sana katika maswali 50, maswali 21 yalikuwa yamekosewa na hao wanafunzi walipewa huo mtihani wakafanya na mpaka sasa hivi Walimu wanaendelea kusahihisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana siungi mkono siku zote hasa katika mtihani kwa hisabati kutungwa kwa maana ya *multiple choice* kwa sababu wamewatungia wanafunzi *multiple choices* na maswali yote 21 yamekosewa hayana majibu. Nataka kupata ufafanuzi hao Walimu waliendelea kusahihisha hiyo mitihani licha ya kwamba imekosewa? Pili, hao Walimu waliokuwa na uzembe huu mpaka sasa hivi wamechukuliwa hatua gani? Kwa maana Walimu wanaofundisha shule zote za msingi na waliohusika kutunga huo mtihani.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge ameleta nakala ya mtihani uliofanywa akiwa ameonesha kwamba baadhi ya maeneo hayo yamekosewa na tulichokifanya tumeutuma mtihani ule kwa Afisa Elimu wa Mkoa ili pia akae na delegation yake yaani panel yake ili wapitie upya kwa sababu majibu umeyaweka wewe lakini wao wana *marking scheme* yao. Kwa hiyo, watakuja kututhibitishia, lakini kama ambavyo nimekudokeza mchana kwamba tutakupa taarifa ya matokeo haya.

**MWENYEKITI:** Kumbe mmeongea! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Daktari Augustine Mrema!

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaja kilio cha *Holy Spirit Sisters* ……

**MWENYEKITI:** Hiyo *microphone* iko mbali sana kwa hiyo husikiki vizuri.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nilitaja kilio cha Masista wa *Holy Spirit Sisters* wa Rauya Marangu Moshi, walikuja mpaka hapa Bungeni tukaonana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, tukaonana na Waziri wa Mambo ya Ndani na baadaye akatuelekeza kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio chao ni kwamba wale Masista ni wawekezaji wana shamba Siha, wanafuga ng'ombe wazuri, wanafuga mbuzi, wamejenga Sekondari nzuri sana ambayo hata Rais aliombwa kuja kuifungua. Masista wale wamejenga Kituo cha Afya na sasa hivi wanataka kujenga Kituo cha Kutunza Wazee kikubwa katika Mkoa wa Kilimanjaro. Lakini Masista hawa wamezingirwa au wamevamiwa, sasa katika uvamizi ule Masista wale walihangaika wakaenda Mahakamani……

**MWENYEKITI:** Wamevamiwa na nani?

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Walikwenda Mahakamani wana *Court Order* ambayo nimempatia hata Mwanasheria wa Serikali na Waziri wa Mambo ya Ndani, nimempa pia Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *Court Order* ni toka mwaka 2008 lakini haitekelezwi, hawasaidiwi Masista wale na jana wale wavamizi ambao tayari wameshawazingira wamewaambia mkicheza na sisi tutawabaka. Sasa tunafikia mahali katika nchi hii mpaka Masista wanatishiwa amani, haki haitendeki, *Court Order* wanayo na sisi tumeambiwa na Rais wetu kwamba tuheshimu amri za Mahakama yaani amri za Mahakama ziheshimiwe, sasa tena hii danadana inatoka wapi?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba hebu tusaidie ili wale Masista wa *Holy Spirit Sisters* hiyo amri waliyo nayo watatembea nayo barabarani mpaka lini? Hiyo haki watapata lini? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrema lakini ungeweza hata kwenda kuongea na hao kuliko kutufanya watu wote washiriki wala Masista wenyewe hawajui. Sasa kitu cha maana hapa ni kwamba hivi ikitolewa *Court Order* kinatokea nini baada ya hapo? Nadhani ndiyo swali lenyewe la kisera.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mrema, Naibu Waziri Mkuu Mstaafu jana alinipa hayo malalamiko, lakini kwa kweli ni kesi na kama unavyosema Masista wenyewe wangeweza kwenda hivyo lakini sisi tumeichukua ile kesi na ningejua kama ungeuliza sasa hivi Bungeni labda ningekwambia ungojee mpaka uulize lakini tayari tumeshaanza *process* ya kutafuta hilo jibu sahihi na tutakupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa kuhusu ulipwaji wa madeni na hasa madeni ya ushirika ambayo Awamu ya Tatu ya Serikali yetu ilishaamua kuyalipa. Lakini wapo baadhi ya wanaushirika hawajalipwa mpaka sasa na hasa madeni ambayo yalisababishwa na Chama cha Ushirika na *MBICU* na mwaka jana katika Bajeti ya Serikali tuliahidiwa kwamba pengine katika bajeti hii yangeweza kuwa *considered,* lakini sijaona mwelekeo wowote na hili jambo nililiweka katika mchango wangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Chiza, Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo *Professor*.

**MWENYEKITI:** Utakuwa siku moja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili analoliulizia Mheshimiwa Kayombo kwa kweli ni la muda mrefu na nalifahamu na juzi tumelizungumza hapa. Ninachojua sasa ni kwamba, mchakato ule wa kujua deni lile ni kiasi gani na litalipwaje umekwishafika Hazina na yeye anafahamu na tumelizungumza. Kwa hiyo, naomba tu sasa baada ya kupitisha bajeti hizi tuwasiliane na yeye pamoja na Hazina ili tuone litakavyolipwa maana limeshafika Hazina.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi niliweza kuzungumza juu ya barabara mbili muhimu sana za Nkana Kala na Kitosi Wampembe ambazo mara zote zimekuwa nikiuliza maswali, nimeweza pia kumuona Waziri, nimeweza kwenda kumuona Mkurugenzi wa Barabara Nchini kwani barabara hizi zimekuwa kikwazo sana kwa mashirika ambayo yanajaribu kupunguza vifo vya akinamama na watoto ambavyo vinawabana sana akinamama wa Mwambao na kwenye mazungumzo haya sijaona ufafanuzi wowote tangu nimekuwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hilo nipate ufafanuzi na ufumbuzi wake.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba nitoe ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu amesema amemuona Mkurugenzi wa Barabara Nchini na hii

inaonyesha kwamba barabara husika zinashughulikiwa na Wizara ya Ujenzi na kwenye bajeti yetu tutatoa ufafanuzi wa barabara zote ambazo tumepanga kuzitengeneza mwaka huu ambao ndiyo tunaanza kuujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba aunge mkono ili Waziri Mkuu apate hizi fedha ili tukija kwenye ujenzi basi tutamalizia.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia matatizo ya maji Kondoa na kadhalika na miaka yote nazungumzia matatizo ya maji Namanyere lakini hakugusia kabisa maji Namanyere na yeye ni mwenyeji……

**MWENYEKITI:** Hawakusikii na mimi mwenyewe sikusikii, nadhani hiyo *microphone* siyo nzuri.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Waziri Mkuu katika kuhitimisha amezungumzia matatizo ya maji Kondoa na kadhalika wakati jirani yake Namanyere ndiyo napakana naye hakuzungumza lolote na Namanyere wana matatizo ya maji sijaona na mwenyewe anafahamu, lakini hakuzungumza amekaa kimya, anazungumzia Kondoa na kadhalika. Kusema kweli mimi bila hilo jirani yangu itakuwa ni matatizo makubwa sana, siwezi kuunga mkono hoja mpaka anieleze matatizo ya maji Namanyere. Mwaka jana nilitaka kuleta akinamama basi zima waje kulala hapa Bungeni, ikawa ni matatizo akaniambia, tutakutatulia matatizo ya maji usiwe na

matatizo, naona mwaka huu tena kanilaza hivi hivi. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Lakini hilo swali ndiyo yale ambayo tumekataa kwamba usiulize *specific* lakini naogopa msigombane undugu wenu huko. (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, unajua huyu Bwana ana mambo yake mengi kidogo, kwa hiyo ni lazima tujitahidi kuyasema vizuri.

Mheshimiwa Keissy nilipitiwa tu lakini dhamira yangu ilikuwa ni kutaja vile vile na Nyamanyere kwa sababu nalifahamu sana hilo tatizo lako, kwa hiyo, nipe kamuda kidogo mpaka mwisho wa bajeti, nadhani tutatafuta kila mbinu na najua na bajeti yake ni kiasi gani, angalau uanze tu.

**MWENYEKITI:** Isipokuwa usilete wale akinamama kama ulivyotaka kuleta, maana unataka kuleta balaa kubwa kabisa hapa.  Mheshimiwa Bulaya!

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.  Kwa muda mrefu wananchi wa Mkoa wa Mara wamekuwa na kiu ya ukamilishwaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kwangwa na Wabunge wote wa Mkoa wa Mara tukiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Wassira, Mbunge wa Bunda pamoja na Mkuu wa Mkoa wamekuwa wakilifuatilia suala hili kwa muda mrefu sana na pia nichukue fursa hii kumpa pole Mbunge wa Bunda kwa kufiwa na mama yake, Mungu ampe moyo wa subira ili aweze kuja kulitumikia Taifa.

Mheshimwa Mwenyekiti, mwaka jana tulizungumzia suala la ukamilishaji wa hospitali hii na naamini kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu unalijua na ili tuweze kukamilisha hospitali hizi zinahitajika kama shilingi bilioni 2.5. Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wa Mkoa wa Mara wamekuwa wakipata taabu muda mrefu kwenda hospitali ya Bugando kutokana na huduma duni ambazo wanazikosa lakini ukamilishwaji wa hospitali hii utasaidia matatizo mengi kumalizika kule kule Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, nahitaji *commitment* ya Serikali kuhusiana na ukamilishwaji wa hospitali hii.

**MWENYEKITI:** Suala hilo Mheshimiwa Bulaya kama tulivyosema mambo ya kisera isiwe hospitali *specific*. Mheshimiwa Daktari!

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Esther Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zipo kama ataangalia kwenye vitabu vya Mikoa atakuta kuna billioni 2.1 zimetengwa kwa ajili hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Kikwembe!

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kupata ufafanuzi kwa kuwa, Serikali iliridhia kwa kuanzishwa mikoa mipya ya kiutawala ukiwemo Mkoa mpya wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha orodha ya majedwali yanayoambata na hotuba ya Waziri Mkuu, nikiangalia ukurasa wa 11 katika Mkoa wa Katavi, hakuna Wilaya ya Mlele. Nilikuwa napenda nipate maelezo na pia nifahamishwe kama kuna fungu, ama limetengwa kwenye mafungu mengine, tunaweza tukayapataje ili Wilaya hiyo iweze kujiendesha? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nadhani kwa suala la Mikoa mipya na Wilaya mpya fedha zake za *OC* zimeoneshwa katika Wilaya husika. Lakini fedha za maendeleo ziko Hazina na tumekubaliana sasa hivi mgawo utakuwaje. Kwa Mikoa mipya, najibu la Mikoa ili lisije likaulizwa tena, itapata fedha za maendeleo Sh. 3,503,640,500/= kwa kila Mkoa mpya. Kila Wilaya mpya ipatapata Sh. 2,395,000,000/= na Mlele imo kati ya hizo Wilaya mpya katika orodha yetu ya mgawanyo wa fedha hizo kutoka Hazina.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mwezi Agosti, 2011, Serikali iliwasilisha Bungeni Mpango wa Dharura wa Kuondoa Mgawo wa Umeme Nchini, ambapo kwenye mpango huo zilikuwa zinahitajika Shilingi bilioni 408 kwa ajili ya kugharamia mafuta ya kuendeshea mitambo hiyo. Tunajua sasa ni mwaka mmoja umepita tangu tuupitishe mpango huo wa dharura na Serikali ilitakuwa kutoa *guarantee* kwenye Shirika la Umeme *TANESCO*. Ninachotaka kujua, ni lini Serikali itatoa hiyo *guarantee* ili Shirika la Umeme nchini liweze kujiendesha bila kuwa

na hasara? Kwa sababu sasa wanakopa mafuta kwa kutumia mali kauli.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo Shilingi bilioni 408 ukiipatia *TANESCO* ni sawasawa kama unatupa *glass* ya maji kwenye bahari. Madeni ya *TANESCO* ni mengi na tulipopiga hesabu, ukiwapatia hizo Shilingi bilioni 408 ni kwamba kitakachobaki ni chini ya Shilingi bilioni tatu au nne. Kwa hiyo, sisi kama Wizara, tumefanya mbinu ambazo zinasaidia, sasa hivi hamna mgawo wa umeme, wala umeme haukatikikatiki kama ilivyokuwa hapo awali. *(Makofi)*

**MHE. SELAMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kipindi cha karibuni tumeshuhudia katika Taifa letu wananchi wakipata shida kwa sababu ya njaa, bei ya vyakula imepanda na katika mchango wangu nimezungumza kwamba, bei ya vyakula imepanda na maisha yamekuwa magumu, lakini pia tunashuhudia vijana wengi wanaomaliza Vyuo Vikuu na wale ambao wako Mitaani wakiwa hawana ajira. Wakati huo huo tunashuhudia katika sehemu za *SUMA JKT* kuna matrekta yamekaa pale na kuna uwezekano mengine yakapata pacha. Serikali inaonaje sasa ikiamua kutoa yale matrekta ili kuwapatia vijana katika kila Halmashauri kama utaratibu wa ruzuku ili mradi matrekta yale yaweze kuzalisha chakula cha kutosha na kuleta ajira kwa vijana? Lakini sijapata ufafanuzi wa kutosha katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Seleman Jafo - Mbunge wa Kisarawe, ndugu yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukabidhi matrekta kwa vijana, unatakiwa ufanye kwa wale ambao umewaundia kikundi, na wana uongozi wa aina fulani. Kwa hiyo, ushauri tu ni kwamba akianzia kwake Kisarawe na Waheshimiwa Wabunge wengine, taratibu za Halmashauri zinaruhusu kuunda vikundi vya vijana na kuwawezesha. Kwa hiyo, kitu cha kwanza kinachohitajika kufanyika hapa ni kuwa na vikundi vya vijana na tunayo mifano mingi tu katika Halmashauri na mikoa mbalimbali ambapo kuna vikundi vya vijana ambao Serikali inawasaidia zana za kilimo kwa sababu tayari wapo na wamejikusanya pamoja. Mimi nadhani tungeanzia hapo.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kuna Wizara mbili; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, vilevile kuna Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kutokana na matatizo makubwa ambayo mwaka huu wakulima wa Korosho wameyapata juu ya uuzaji wa korosho zao, nataka kufahamu kutoka Serikalini, ni Wizara ipi ambayo inawajibika kutafuta masoko ya mazao ya kilimo? Kwa sababu kwa tafsiri inaonekana kuwa ni Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Lakini imeonekana kwamba, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko imekuwa haijihusishi sana na kutafuta masoko ya mazao ya biashara.

Je, ni Wizara gani kati ya hizi mbili ambayo *specificaly* inawajibika katika kutafuta masoko ya mazao ya wakulima wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba, wanajaribu kuangalia uwezekano wa Viwanda vya Korosho, vile ambavyo havifanyi kazi ambavyo vinawajibika kufanya, kuvifuta. Sasa nashindwa kuelewa, kwa sababu viwanda hivi vimeuzwa zaidi ya miaka mitano, sasa hivi na havijabangua hata Korosho moja. Ni utafiti gani huo ambao utafanyika ili hali watu hawa hawajatimiza wajibu wao ndani ya miaka mitano?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Wizara ipi inahusika katika kutafuta masoko? Suala la masoko kama nilivyokuwa nalieleza asubuhi hii ni pana kidogo; hata kutafuta namna ya usindikaji ni masuala ya masoko; hata unapowezesha watu kufikisha mazao yao sokoni ni namna ya masoko. Kwa hiyo, hapa kwa kweli ukisema tuweke mstari katikati, ni vigumu kutenganisha Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Viwanda na Biashara. Sisi wote tunahusika kwa njia moja au nyingine. Kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza jana tu au juzi ametoka Ofisini kwangu tukiwa tunatafuta namna ya kutoa korosho iliyoko Tunduru na *Coast Region* kwa lengo la kuifikisha bandarini ili mnunuzi aweze kuichukua. Wote huo ni mlolongo wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona Wizara zote mbili hatuwezi kutupiana mzigo huu, tunafanya kazi kwa pamoja.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami katika mchango wangu wa maneno na maandishi nilitaka kujua kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ni sheria au kanuni ipi ambayo inaipa haki Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kuwahukumu wananchi ambao Halmashauri zao zimepata hati chafu kutokana na makosa ya Serikali yenyewe, lakini vilevile watendaji wabadhirifu kwa kuwanyima fedha ya ruzuku na hatimaye kuwafanya wananchi hao wakakosa maendeleo kutoka katika Serikali yao? Niliomba maelezo sikupewa, lakini naomba sasa hivi nipate maelezo. Kama ni sheria: Je, ilitungwa na Bunge? Kama ni Kanuni, ilitungwa na nani? Ni lini itakuja Bungeni ili tuiondoe ili kusudi wananchi wetu wasipate udhia ambao unasababishwa na watendaji wabadhirifu na Serikali yenyewe kutokuwapa mafunzo watumishi wake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuzipatia mamlaka ruzuku isiyokuwa na masharti, sharti mojawapo ni kwamba, lazima Halmashauri hiyo iwe inasimamia fedha hizo kwa ukamilifu. Hiyo ilikuwa ni katika kupitia mfumo wa maboresho wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri wapo Watendaji wa Serikali, wapo Waheshimiwa Wabunge

na Waheshimiwa Madiwani ambao wanawawakilisha wananchi. Sasa kwanini wanyimwe hizi fedha wakati kuna hayo makosa yaliyojitokeza?

Yale makosa kwa upande mmoja watumishi wanahusika, lakini Madiwani na Waheshimiwa Wabunge wanao mkono wao kwa sababu tunao wajibu wa kusimamia watumishi katika mamlaka zetu. Sisi tumechaguliwa na wananchi tuwawakilishe katika Halmashauri kusimamia Halmashauri zetu. Tunahudhuria katika vikao vya fedha kila mwezi ili kufahamu ni fedha kiasi gani zimeingia na kiasi gani zimetumika. Haiingii akilini kama kweli mtu anaweza akatoa taarifa kwenye Kamati ya Fedha kwamba, bwawa limejengwa wakati halijajengwa na wapo wawakilishi wa wananchi wanaotoka katika maeneo hayo ambao hawajaliona bwawa.

Kwa hiyo, tunafanya hivyo ili kuwafanya Waheshimiwa Madiwani wawe makini zaidi katika kuzisimamia Halmashauri zao, kwa sababu tunao ushahidi kwamba katika baadhi ya maeneo, baadhi ya Madiwani wanashirikiana na Watendaji wa Halmashauri katika kuhujumu fedha za Halmashauri. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Innocent E. Kalogeris alisimama Kutaka kuuliza swali la nyongeza)*

**MWENYEKITI:** Mara moja tu baba yangu, ndiyo utaratibu. Mheshimiwa Mpina!

**MHE.JOELSON L. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nachangia kwa maandishi nilisema kwamba, hizi fedha ambazo zimepatikana Uswizi ni matokeo tu ya utafiti uliofanywa mapema kabisa mwaka 2008 na *global financial intergrity* ambayo ilituambia Watanzania kwa miaka 39 kutoka mwaka 1977 mpaka mwaka 2008 tumepoteza Shilingi trilioni 11.6 zilizofichwa kwenye mabenki kule Ulaya. Sasa ripoti ile ni ya toka mwaka 2008 na Serikali haijawahi kukanusha ripoti hii, na vilevile haijawahi kusema ripoti hii imefanyiwaje kazi. Lakini vilevile hii ripoti ya *one bilion dollar question* yenyewe imetuambia kwamba kila mwaka Tanzaniia inapoteza Shilingi bilioni 478. Sasa ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha tunadhibiti fedha hizi kutoroshwa kwenda Ulaya na namna ya kuzirejesha? Kwa sababu ni muda mrefu, toka mwaka 2008!

Vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anatoa hotuba yake, alisema Serikali imejitahidi kupunguza matumizi yasiyokuwa na tija, na kwa kuwa katika kitabu hiki cha *Volume II* bado matumizi yako mengi ambayo hayana tija. Mheshimiwa Waziri Mkuu anasemaje sasa kuhusiana na kuunda timu mkakati ili tuweze kuzifyeka fedha ambazo hazina tija humu na tuweze kuongezea kwenye shughuli za miradi ya maendeleo tukizingatia kwamba, fedha za miradi ya maendeleo zilipungua?

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Mpina wakujibu lile la mwanzo au la pili? Maana yake unapofafanua ni jambo moja, sasa tuambie wakujibu lipi? Wanalopenda wenyewe?

**MHE.JOELSON L. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibiwe lile la kufyeka zile fedha ambazo zimekuwa *allocated* kwenye maeneo ambayo nakiri kwamba, hazina tija. Naomba ile Tume ili tusaidiane kwa sababu *finance bill* inakuja mwishoni. Sasa ningeomba iundwe Tume mkakati ambayo itaweza kupitia mafungu haya na kutambua kwa kusoma randama ili kuweza kuona matumizi ambayo hayana tija ili fedha hizo tuweze kuziongeza kwenye miradi ya maendeleo.

**MWENYEKITI:** Tumekuelewa. Hiyo ni kuhusu matumizi yasiyokuwa na tija. Nani anajibu? Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge hapa ndani tumejigawa kwenye Kamati mbalimbali na kila Kamati inaamini kazi iliyofanywa na Kamati nyingine. Mafungu yote yaliyomo katika vitabu hivi yamepita katika Kamati inayohusika, yamejadiliwa yakapitishwa na Kamati. Kwa hiyo, nimesimama kutokubaliana na Mheshimiwa Mpina kwamba, kuna mafungu ambayo yamepitishwa ambayo hayana tija kwa sababu mafungu haya yamepitishwa na Waheshimiwa Wabunge wenzake katika Kamati ambazo ni *duly constituted* na Bunge hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka niliyonayo kwa kutumia kifungu cha 28(5)

cha Kanuni ninaongeza dakika 30 kuanzia saa 1.45 usiku halafu mengine tutaangalia baadaye.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakukushukuru kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu aliyoyatoa wakati alipokuwa anajibu hoja nilizotoa hapa Bungeni nikiwa nazungumza. Namshukuru sana. Wakati ule nilisema sitaunga mkono hoja. Ninaomba nilithibitishie Bunge hili kwamba baada ya majibu hayo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niulize kidogo tu kwamba kuhusiana na kahawa ile mbichi au *sherry* ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu anakubaliana kwamba, wananchi wanapunjwa na wananyonywa kwa kahawa yao kununuliwa kwa Sh. 500/=. Lakini pia Sera ya Serikali imekuwa ni kuongeza mazao thamani na hivyo ndivyo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi inavyosema; mazao yaongezwe thamani ili mkulima huyu apate fedha za kutosha. Lakini pia nimemshukuru Waziri Mkuu anaposema suala la kanuni hizo litatamwa kwa undani. Sasa labda Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie itachukua muda gani mpaka Serikali, wataalamu wake na wadau waweze kukaa chini na kubaini kanuni hizo lakini wakihakikisha kwamba hazigongani na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaagiza kwamba, lazima mazao yaongezwe thamani kabla hayajauzwa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Zambi kwa kuunga mkono hoja hii. Lakini pia nataka nimhakikishie kwamba, suala la kutayarisha Kanuni liko katika dhamana yangu na kwa hiyo, baada ya kufikia hapa maelekezo hayo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, tuzamie tuandae Kanuni ambazo hazitaleta migongano tena ya soko la Kahawa. Sasa tutazianza mara moja, lakini siwezi kukwambia kwamba labda ni kesho kutwa, ila nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaanza mara moja. Hivi ninavyozungumza wenzangu wanasikiliza huko waliko.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Wakati wa mchango wangu nilioutoa hapa Bungeni nilizungumzia tatizo la mahindi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwemo ile ya Njombe na Iringa na nikaomba Serikali iweze kutoa fedha za kutosha ili Bodi ya nafaka na mazao mchanganyiko iweze kununua mahindi na hatimaye kinu kilichopo Mkoa wa Iringa kiweze kusaga ili kuongeza thamani ya mazao na pia kupunguza mfumuko wa bei ya chakula. Sasa napenda nipate jibu: Je, Serikali iko tayari kutoa fedha kwa msimu huu ili tuanze kusaga kwa kutumia kinu kilichopo Mkoa wa Iringa na kuleta ajira kwa vijana wetu?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinu cha Iringa tumekiangalia. Kwa kweli ukiangalia kwenye bajeti, Bodi ya nafaka na mazao mchanganyiko haikuwa imepata fedha za

kutosha kuanza moja kwa moja kununua mahindi na kusagisha. Hata hivyo, imepata fedha kwa ajili tu ya kujenga uwezo, kuajiri watumishi ili waweze kufanya kazi hizo. Lakini suala hilo tumeliangalia kwa undani na hatua ambayo tumefikia sasa ni kwamba, sisi wenyewe ndani ya Wizara tutazungumza na *NFRA* tuangalie uwezekano wa kusaidia Bodi hii kwa kuanzia, ili iweze kutusaidia kuanza kazi. Kwa hiyo, hilo tumeshalichukua na tunajaribu kuangalia namna ya kulitekeleza. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo ambalo limeanza kuchukua sura nyingine mpya nalo ni tatizo la Walimu kuanza kujitengenezea makundi ambayo yanapelekea wajiandae kufanya mgomo wa kutokuwafundisha watoto katika maeneo kadhaa ya nchi yetu ya Tanzania. Taswira hiyo imeanza kujitokeza katika vyombo vya habari na maeneo kadhaa yameishaanza kutoa matangazo ya kuwepo kwa mgomo wa Walimu na matangazo haya yamezidi kuchukua kasi na yamekuwa yakiendelea. Walimu hawa wamekuwa wakijipanga kufanya mgomo katika nyakati mbalimbali katika siku zijazo wakidai mambo mbalimbali ambayo yanahusu maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu, sijui Serikali inasema nini na inachukua tahadhari gani katika suala hilo ambalo limeanza sasa kupata picha ambayo na vyombo vya habari vimeanza kulitangaza huku na kule. Kwa hiyo, nafikiri linaweza kama

lisipochukuliwa hatua za haraka likatupa shida nyingine kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu kufahamu, Serikali sasa inafanya nini ili tuweze kufanya suala hili lisitokee na watoto wetu waendelee kufundishwa vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo asubuhi nimeeleza wakati nachangia hoja, ni kwamba suala la uhamasishwaji wa Walimu kugoma ni suala ambalo linaendeshwa na kikundi cha watu wachache kwa lengo tu la kutaka kuvuruga mwenendo wa Serikali hii iliyoko madarakani. Serikali inatambua kuwepo kwa changamoto za ajira ya Ualimu, lakini sisi tumeweza kuziweka vizuri na kwa bahati nzuri sana huwa tunawasiliana kwa karibu sana na Chama cha Walimu kinachowakilisha wao katika kubainisha matatizo yao.

Kwa wakati huu kama ambavyo tumeeleza, uko mzunguko wa taarifa za upotoshaji unaoendeshwa na vyombo mbalimbali ikiwemo na simu na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge Jenista ameeleza, kwamba vyombo vya habari vinaeleza; vyombo vya habari havipaswi kueleza jambo hilo kwa sababu tunayo *forum* ya mazungumzo kati ya Chama cha Walimu na Serikali na tarehe 26 tulishakutana *CMA* kati ya Chama cha Walimu na Serikali kuzungumzia changamoto mbalimbali za Sekta ya Elimu. Kwa hiyo, tunayo matumaini kwamba changamoto zile zitaendelea kujadiliwa na kubainishwa na Serikali inayo

nia ya dhati kutatua matatizo ya Walimu kadri ambavyo yanawasilishwa kwetu.

Nataka nitumie nafasi hii kuwasihi Walimu, vyombo vya habari vinavyotangaza na kuhamasisha jambo hili visiaminike kwa sasa badala yake Chama cha Walimu ambacho kinaendelea kuzungumza na Serikali ndicho kisikike na sisi Serikali kwa sababu tumesema tuko tayari kukaa na walimu kuzungumzia changamoto zetu waendelee kuiamini Serikali yao.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ningeomba kupata ufafanuzi katika mchango wangu wa kuzungumza. Nilizungumzia tatizo la hospitali yetu ya Mkoa wa Kilimanjaro kuhusu chumba cha upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Waziri alinipa majibu, lakini ningependa kuiomba Serikali ione umuhimu wa kutafuta fedha za haraka ili kuweza kunusuru maisha ya wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro hususan akinamama wajawazito ambao wamepoteza maisha kwa kukosa huduma hiyo ya upasuaji na jengo hilo linahitaji Shilingi bilioni 1.8 ili kukamilika na kuanza kutumika. Katika bajeti, tumepewa Shilingi milioni 744 tu. Je, Serikali inasemaje?

**MWENYEKITI:** Katika maswali ya kuuliza mshahara wa Waziri, hilo ni *direct,* lilitakiwa likienda kwenye mpango ndiyo unadai fedha pale.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niendelee kumshukuru Mheshimiwa Grace Kiwelu, safari iliyopita tena alisimama hapa hivi hivi na akatutaka twende kwenye hospitali hii ya Mawenzi na tulikwenda kule na yeye alikuja tukakutana na Uongozi wa Mkoa, tukaangalia matatizo yaliyokuweko pale. Ni kweli anachosema hapa, wodi ile ya akina mama wajawazito inahitaji Shilingi milioni 13. Kwa hiyo, vyovyote vile utakavyofanya, unaona jinsi inavyokuwa ngumu, na *theatre* kama alivyosema, ni hicho kiasi alichosema.

Tulichofanya, kwa maana ya maamuzi tuliyofanya pale, tumeutaka Mkoa wa Kilimanjaro na hata juzi tulikutana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro - Ndugu Gama na *RAS* tukawaambia kwamba, waone uwezekano wa kuingiza; kikubwa sana ni chumba hiki cha kupasulia na ambacho kilifanyiwa kazi. Yale matatizo madogo madogo aliyozungumza pale, tulimwambia Waziri mwenye dhamana wa Ujenzi ili aweze kushughulika na watu wake wale ambao walitufikisha hapo walipotufikisha.

Kwa hiyo, kiasi ambacho kimeweza kutengwa na Mkoa ni Shilingi milioni 744 kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Maoni yetu tumalize kwanza suala la *theatre* pale, ndiyo mawazo tuliyonayo. Halafu pili, tuingie sasa katika suala hili la wodi ya akina mama wajawazito ambao ni pamoja na kutafuta wahisani ambao wanaweza wakasaidia jambo lile, tulilizungumza siku ile. Kwa hiyo, hapa naomba ni-*declare interest* kwamba Mawenzi Hospital, wananchi wa Siha wanatibiwa pale, wakitoka kule Siha

wanapelekwa pale. Kwa hiyo, na mimi mwenyewe ni mdau ambaye napigania sana jambo hili ili liende vizuri. Kwa hiyo, naomba tushirikiane na Mkoa, lakini kiasi kilichopatikana kwa sasa hivi na kwa kweli nimshukuru Mkuu wa Mkoa kwamba kimetengwa kiasi hicho ili tuweze kusaidia pale, liko tatizo, lakini tutaondokana nalo kwa njia hiyo.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hotuba ya Waziri Mkuu nilichangia Sekta ya Muungano, lakini katika ukurasa huo wa 12 aligusia kero mbili ambazo za Muungano zimepatiwa ufumbuzi. Sasa hapa zimekuja kauli mbili, Waziri wa Muungano amesema ni kero saba. Nilitaka sasa nifahamishwe vizuri ili nisiondoe shilingi Mama Tunu akakosa fedha ya maziwa ya watoto? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Maryam ameiuliza na nilitaka kusema labda mchana hakuwepo, lakini kumbe alikuwepo hakufahamu vizuri.

Nimesema hizi hoja zote ni 13 kama zilivyoibuliwa na Tume ya Shellukindo, lakini mpaka mwaka 2011 hoja saba zimeshafanyiwa kazi na mwaka huu wa fedha 2012/2013 tunaomaliza kama alivyoripoti vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu hoja mbili nazo tumezimaliza. Kwa hiyo, jumla ya hoja zilizomalizwa ni tisa. Kuna hoja sita ambazo bado tunazifanyia kazi. Sasa ukichukua tisa na sita siyo 13, ni 15. Hoja mbili ya umeme na Jimbo ziliingia katikati tumezifanyia kazi na

tumezimaliza. Kwa hiyo, zilizomalizika ni tisa na sita tunaendelea kuzifanyia kazi.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimerudisha shilingi ya Mama Pinda apate maziwa ya watoto.

**MWENYEKITI:** Wewe utatoka nje bure.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina jambo dogo tu, nalo ni tatizo la mwingiliano baina ya vikao vya Halmashauri na Mikutano ya Bunge. Mwingiliano huo huwa unatupa shida sana sisi Wabunge tunaotoka mbali na Dodoma na hatuwezi kushiriki kati vikao vya Halmashauri zetu. Serikali inalizungumzia nini? Kwa sababu ni tatizo kubwa sana na hata lile alilosema Mheshimiwa Mkuchika kwamba hizo nyaraka ambazo alikuwa anaziongelea Mheshimiwa Mkosamali kwamba azikute huko, Halmashauri hatazikuta kwa sababu hayuko huko. Naomba ufafanuzi wa Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo analosema Prof. Kahigi ni kweli. Wakati mwingine hutokea kwamba tuko Bungeni hapa na huku unakuta kwenye Halmashauri wanakutana na mambo yanazungumzwa pale unakuta ni mambo ya msingi sana. Rai ambayo ilikuwa imetolewa na maelekezo ambayo tumetoa ni kwa vile ratiba hizi zinafahamika, ratiba zetu za Bunge zinafahamika, tumezitaka Halmashauri zetu kupitia kwa Katibu Tawala wa Mikoa watusaidie kuwaelekeza Wakurugenzi

Watendaji pamoja na Wenyeviti na Madiwani walioko kule kwamba mara nyingi sana wahakikishe kwamba ratiba zile hazigongani. Kwa hiyo, kuna haya maelekezo. Lakini wakati mwingine ikitokea kabisa kuna jambo linataka kupita kwa mfano kuna bajeti inataka kupitishwa sasa, unakuta Mkoa umepitisha, Wilaya hazijapitisha na sisi labda tuko huko, basi katika *emergence* ya namna ile utakuta kwamba Halmashauri zinalazimika kufanya hivyo. Lakini nataka niseme hapa kwamba tumetoa maelekezo hayo kwamba itakuwa ni vizuri kwa sababu Wabunge ni Madiwani na ni sehemu kamili katika Halmashauri ili tuweze kuzioanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kulifuatilia kwa karibu jambo hili.

**SPIKA:** Nami Ofisi yangu tutatoa ratiba ya mwaka mzima ambayo tutaipeleka Ofisi ya Waziri Mkuu kusudi awapelekee watu wanaohusika. Sisi tutatoa ratiba ya mwaka mzima. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia suala zima la chaguzi katika Serikali za Mitaa, lakini bado hili suala limekuwa likipewa majibu mepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo mwongozo haujatoka tu katika Mkoa wa Mara. Kuna vijiji vingi viko wazi, Mitaa iko wazi, Wajumbe wa Serikali za Mitaa wamejiuzulu, maeneo mengine utakuta kwamba Mwenyekiti yuko peke yake, hana Wajumbe na hiyo

Serikali inaendeshwa. Babati Mjini, Babati Vijijini Mkoa wa Manyara, hivyo vijiji vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufahamu kutoka kwa Waziri Mkuu, hizo chaguzi zinaitishwa lini? Maana Wakurugenzi wao wamekuwa wakiwaambia wananchi kwamba hawana *OC* za kuitisha hizo chaguzi. Naomba kauli ya Waziri Mkuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema wakati najibu hoja, kwamba, hivyo vijiji au vitongoji vinatakiwa kufanya uchaguzi ndani ya siku 60. Lakini wote tunafahamu kwamba mwaka huu wa fedha uliokwisha kumekuwa na changamoto sana ya fedha. Kwa hiyo, maeneo mengine imekuwa siyo rahisi kuweza kufanya hizo chaguzi kwa sababu chaguzi pia ni gharama. Lakini tumezielekeza Halmashauri waweke utaratibu katika maeneo ambayo kuna mapengo, basi wafanye uchaguzi. Pia napenda kutoa rai kwa sababu zipo taarifa za usahihi kabisa kwamba wapo baadhi ya watu wanawashawishi baadhi ya viongozi wetu wajiuzulu ili kufanyike uchaguzi wa marejeo. Kwa hiyo, maeneo ambayo watu wamefariki, kwa kweli hayo tutahakikisha kwamba uchaguzi unafanyika, hata kwa kukopa wale wanaosimamia uchaguzi. Lakini pale ambapo tunaona kwamba ni dhahiri kwamba watu wameshiriki kuwashawishi wajiuzulu, basi walioshiriki wakati mwingine tutawashauri watuchangie kuendesha uchaguzi huo.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba sasa ufafanuzi wa mchango wangu wa maandishi ingawaje yote haikupata majibu, lakini naomba tu moja niweze kulisemea kwa sababu ya kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ni kero sana kwa Watanzania wote. Sisi hapa Bungeni wote tunang'aa kwa sababu tunaoga, tunakunywa maji, saa zote tunakunywa maji ya Kilimanjaro, Lakini kuna Watanzania wanaochota maji zaidi ya kilomita 20 na kuendelea. Je, zile fedha ambazo zilikuwa zimetengwa *USD* 3360 ambao ilikuwa ni mpango wa Serikali hii tangu mwaka 2007 ulishaanza? Lakini fedha hizo hazijawahi kutekelezwa kama ilivyotakiwa kwamba kila mwaka angalau itolewe *USD* Shilingi milioni 176.

Namwuliza Waziri Mkuu, leo Shilingi yako mimi nakaa nayo, tuambie ule mpango wa *WSDP* ulikwenda wapi? Watanzania wanapigika, hawana maji na hii Shilingi bilioni 140 ni maji ya Dar es Salaam tu, lakini Watanzania wote vijijini hawana maji, ndiyo maana kila mtu anapiga kelele. Hata wewe kwako hakuna maji huko vijijini. Sasa tunarudi wapi kwa hao wananchi ambao hawana maji? Kwa nini fedha hizi za *EPA*, rada zisielekezwe kwenye maji? Nyinyi mnaelekeza kwenye madaftari, vitabu, kumbe kuna nafasi za watu wengine kuweza kujipatia fedha zao za kula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba hili kwa kweli nipate majibu kwa sababu ni kero kwa Watanzania wote hasa wanavijiji.

**MWENYEKITI:** Sasa hili ndilo la maendeleo. Sasa taabu tupu, mshahara wa Waziri ni sera. Waziri wa Maji, sema, maana nasikia nyie mnang'aa.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna kero kubwa ya maji. Lengo la Serikali ni kwamba inapofika mwaka 2015 katika maeneo ya vijijini wananchi ambao watakuwa wanapata maji watafikia asilimia 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *WSDP* bado unaendelea kutekelezwa. Nadhani katika eneo la vijijini mradi mkubwa ambao umechelewa ni ule wa vijiji 10. Mwaka 2011 fedha zilipelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, lakini hazikutumika kwa sababu utaratibu ule wa kutoa *no objection* kutoka kwenye Benki ya Dunia ulikuwa haukukamilika. Hivi sasa utaratibu huo umekamilika kwa Wilaya 61 na tunategemea mpaka mwezi Agosti, 2012 tutakuwa tumefikia labda Wilaya 70 mpaka 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii ambayo inaendelea, mradi huo umetengewa Shilingi bilioni 81 na kuna wachangiaji wa *WSDP* ambao wameonyesha kuongeza uwekezaji katika eneo hilo. Kwa hiyo, tunategemea kwamba kila Wilaya itaweza kuweka miundombinu kwa ajili ya kusambaza maji katika vijiji vitano kati ya vile kumi.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna suala ambalo linaonekana ni dogo, lakini ni kero sana kwa watu wa Mkoa wa Kigoma na nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu

atoe kauli kwa sababu inaonekana Mawaziri wa Kisekta hawajaliona hili suala, toka Bunge la Tisa tulikuwa tukiliongelea. Ni suala dogo linalohusiana na upatikanaji wa tiketi za treni. Watu wanalazimika kukata tiketi siku hiyo hiyo ya safari na Mkoa wetu ni mkubwa, siyo kwamba watu wote wanakaa maeneo hayo hayo ya mjini kwamba watawahi alfajiri kwenda kupanga foleni waweze kukata tiketi. Wanatoka maeneo mbalimbali, wengine ni watoto wadogo, wengine wajawazito, wengine ni wagonjwa, wengine ni wazee wanalazimika kulala stesheni ili alfajiri waweze kupata tiketi na matokeo yake sasa, tiketi badala ya kuwa Sh. 19,000/= bei ya kawaida, inakuwa bei ya kuruka pale nje anapoona amechoka na ana ulazima wa kuondoka siku hiyo.

Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe tamko kwa sababu naamini hii siyo *Quran* na wala siyo kitu ambacho hakiwezi kubadilika, urudi utaratibu wa zamani ambao tulikuwa tunakata tiketi siku yoyote ili mradi tarehe yako ya kusafiri ikifika unakwenda na tiketi yako na unasafiri.

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba utoe tamko jambo hili liweze kubadilika kwa sababu ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma, ikizingatia treni yenyewe ndiyo hivyo mbovu, lakini na upatikanaji wa tiketi uwe mbovu. Naomba utoe kauli ili jambo hilo liweze kubadilika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa

maelezo juu ya hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mhonga. Bahati mbaya Waziri wa Uchukuzi amekwenda Arusha kwenye Mkutano wa *East Africa.* Lakini jambo hili amelisikia na ameahidi kulichukulia hatua. Hapa kuna mambo mawili. Utaratibu wa ukataji wa tiketi ambao hauna ustaraabu kama alivyosema mwenyewe kuhusiana na foleni zile na kurejesha heshima na utaratibu mzuri wa utaratibu wa safari za treni. Mkuu wa Mkoa Kanali yuko hapa anasikia, lakini nataka nimhakikishie kwamba Serikali imesikia na Waziri ameshajipanga kulishughulikia jambo hili. Nataka nimwombe tu Mheshimiwa Mhonga aamini kwamba Waziri wa Uchukuzi na Serikali itashughulikia jambo hili kwa sababu kama ndivyo linavyofanyika, tunafikiri hata Serikali haifurahishwi na jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba Bunge lirejee, kwa sababu hata nyie mliomba kwa mshahara wa Waziri, sijawamaliza, kwa hiyo, naomba turejee tuongeze muda kidogo.

*(Bunge lilirudia)*

**KUONGEZA MUDA WA KUKAA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuongeza dakika 30 ili tuweze kukamilisha kazi iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuongeza dakika 30 ili tuweze kukamilisha kazi iliyopo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliridhia Mapendekezo ya Kuongeza Muda)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika Mkutano wa Bunge wa Bajeti wa mwaka 2011 kuna suala la kisera ambalo niliuliza kwa Ofisi ya Waziri kupitia mshahara wa Waziri Mkuu kuhusu utaratibu wa fidia kwa wananchi ambao walikuwa wakiishi maeneo ambayo toka wakati wa Mwalimu Nyerere wakiwa na hati za vijiji, utaratibu wa fidia ya ardhi na wakati ule nikaeleza wananchi wa maeneo ya Kisopwa Kwembe na Mloganzila, wananchi 1919 ambao wanatakiwa kuhama kupisha ujenzi wa Chuo cha Muhimbili wakaanza kulipwa fidia ya mali, lakini

hawajawahi kulipwa fidia ya ardhi na mgogoro ulidumu kwa zaidi ya miaka kumi.

Sasa napenda kupata ufafanuzi wa kisera wa Serikali kuhusu fidia ya ardhi ya wananchi kama hawa. Je, watalipwa au hawatalipwa? Nasema hivi kwa sababu tumejaribu njia zote za kiofisi, Waziri Mkuu ofisi yako iliwahi kutoa maelekezo kwa Wizara ya Ardhi mwaka 2010 kushughulikia jambo hili. Mawaziri mbalimbali wamekwenda, Mkutano uliopita wa Bajeti Waziri wa Ardhi aliahidi yeye mwenyewe kwenda kushughulikia jambo hili. Ofisi ya Waziri Mkuu iliahidi kufuatilia na tumeandika barua nyingi sana na hakuna barua iliyowahi kujibiwa hata moja kuhusu jambo hili. Kwa hiyo, naomba kauli tu ya kisera: Je, wananchi hawa watalipwa fidia ya ardhi au hawatalipwa fidia ya ardhi? Ni jambo ambalo vilevile lina ahadi ya Mheshimiwa Rais.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kumjibu Mheshimiwa John Mnyika - Mbunge wa Ubungo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaoishi eneo la Mloganzira ni kweli kwamba wameishi pale kwa miaka kadhaa na kwa kutambua hilo Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 imewalipa fidia ya maendelezo waliyofanya katika eneo hilo. Lakini fidia ya ardhi haijalipwa na sababu ya msingi ardhi ile inamilikiwa kihalali na iliyokuwa *Tanganyika Packers* na kuna hati miliki ya eneo hilo la

*Tanganyika Packers*. Kwa mujibu wa Sheria, huwezi kutoa hati mbili juu ya eneo moja. Kwa maana hiyo, huwezi kumilikisha mtu zaidi ya mmoja katika eneo moja. Kwa sababu hiyo basi, Serikali haitaweza kulipa fidia kwa mtu anayeishi katika eneo ambalo siyo lake. Hata hivyo Serikali inaangalia ni namna gani inaweza ikaangalia uwezekano wa kuwapatia wananchi hawa viwanja eneo mbadala eneo watakalohamia, lakini siyo fidia ya ardhi kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi na maneno pamoja na mambo mengine niliyoyazungumzia kuhusu Mkoa wa Morogoro, lakini nimeona nitake tena ufafanuzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Nilisema kwamba mwaka 2002 aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI wakati huo Brigedia Hassan Ngwilizi alitoa tamko la kufuta kodi ya ushuru wa mazao kwa wakulima na tamko hilo lilianza kutumika Mei Mosi mwaka 2002. Lakini kwa Mkoa wa Morogoro katika Wilaya zake zote ni kilio. Hususan nikichukulia mfano wa geti la Idete. Wananchi, wakulima wa kawaida wanalima mazao katika maeneo mbalimbali, wamewekewa mageti kila Kata. Kwa mfano, geti la Idete wananchi wa Msolwa kule kwenye Kiwanda cha Miwa Kilombero wanalima, Ngeta, Mbungu wanarudisha mazao yao nyumbani. Wakifika pale wanatozwa ushuru na kata mbalimbali za Ifakara. Nataka nisikie kauli ya Serikali na wananchi wananisikia, Mkoa mzima wa Morogoro Serikali inatamka nini? Lile tamko halijufutwa, kwanini Halmashauri zinatunga Sheria kubatilisha lile tamko? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu swali hili la Mheshimiwa Susan Kiwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo analolizungumza Mheshimiwa Kiwanga ni jambo ambalo tumelizungumza. Tumekwenda mpaka kule kwenye Halmashauri kwenyewe kule tumekaa naye na tumekaa na Madiwani tumelizungumza. Hapa mara nyingi sana tumelizungumza. Kwanza nizungumzie haya mageti anayoyazungumza. Mageti haya siyo ya TAMISEMI, ni ya Maliasili na Utalii. Tunachofanya sisi, tuna-*take advantage* kwamba yapo kule na kwa vile Serikali imeweka pale kwa ajili ya kuangalia haya mazao mengine ya misitu yanayopitishwa pale, maliasili wameweka utaratibu huu. Ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba tumekuwa tunakwenda pale na kama *Fusso* inapita pale, imebeba mpunga au mchele, anachouliza pale ni kama limelipiwa ushuru. Kwa mfano, kama wametoka Ulanga wakafika pale kwake watauliza: Je, umelipia? Kama hawana risiti pale, Halmashauri ya Kilombero itatoza ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichosema Mheshimiwa Ngwilizi ni kweli, vile vizuizi viliondolewa pale, kwa maana hiyo, lakini utaratibu ukasema kwamba tutakuwa tunatoza ushuru huo *at source*. Yaani pale wanaponunua au wanapouza. Mazao haya yanayozungumzwa hapa, ukilima mihogo ukajaza

kwenye banda lako, hukuuza kwa mtu, yakabaki pale pale, hakuna ushuru unaolipwa, ni mpaka yanapohama mazao yale kutoka kwa mkulima, yakahamia kwa mfanyabiashara au mchuuzi. Pale ndipo Halmashauri inaposema tulipe cha kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wataalam wa mambo wanasema hivi, ina *financial implications* zake kwa sababu mnunuzi ataiona kama ni *over expenditure,* kwa hiyo, itampunja. Kwa hiyo, Halmashauri hizi ndizo tumeziagiza zijenge Zahanati katika kila kijiji, zijenge Kituo cha Afya na madarasa. Hivi tunavyozungumza hapa, Halmashauri ya Tandahimba kupitia ushuru huo wa mazao inapata Shilingi bilioni 1.9 na kama hapa tutafika mahali kwa sababu sisi tunaheshimu mawazo yanayokuja hapa, tukaamua kwamba tunaondoa, mwelewe *implications* zake kwamba tunamaanisha hicho. Tunauza na mchele huu unavuka unakwenda Sudan, unakwenda Kenya unakwenda maeneo mbalimbali, wenzetu watajengea shule watajengea barabara watafanya kila kitu, na Halmashauri kama haikutoza hapa, kama Njombe pale kwenu hamkutoza, ukienda ukifika Morogoro mchele ule hauna alama, wao watakwambia tuonyeshe risiti, kama huna watatoza. Wakitoza, watatumia zile hela kwa ajili ya Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiwanga tafadhali. Utaratibu wetu siyo huo.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Siyo kweli! Mimi napiga simu.

**MWENYEKITI:** Susan naomba tuheshimiane. Haina maana kupiga kelele, inakuwa kama umepunguza akili zako. Kwanini? Mama, hatufanyi hivyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna haja ya kubadili utaratibu Halmashauri zilete mapendekezo na utaratibu ule nina hakika kwamba utakuja mpaka hapa tunapozungumza. Kwa hiyo, maelezo ndiyo hayo na nimerudia mara nyingi sana kueleza hivi. Mimi sisemi cha kwangu hapa, mimi naeleza utaratibu wa Serikali tu.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru. Hoja yangu ni katika *National Assembly Fund.* Wabunge tuna kazi kubwa katika Majimbo yetu na ngumu sana kuwatumikia wananchi, lakini hatuna ofisi za kufanyia kazi zetu.

Kwa hiyo, hapa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kukarabati jengo la Bunge letu na kujenga nyumba ya Mheshimiwa Spika pamoja na fedha za kujenga Ofisi za Wabunge Majimboni, naomba pawe na marekebisho hapa kwa kutumia Kanuni ya 102 (1). Mafungu haya ya fedha kwa vile hayataathiri madhumuni ya fungu zima hili, naomba ukarabati wa Jengo la Bunge yapunguzwe kwa asilimia 40 na ujenzi wa nyumba ya Mheshimiwa Spika, upunguzwe kwa asilimia 50 ili uongezwe katika kifungu hiki cha ujenzi wa Ofisi za Wabunge ili tuweze kuhudumia wananchi katika kuendeleza Taifa hili. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamis, kufanya hivyo lazima uwe na kifungu kile. Hapa ni kifungu cha mshahara wa Waziri, ni Shilingi bilioni nne tu hapa. Haihusiki hiyo!

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naomba nipatiwe ufafanuzi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka huu kwa utekelezaji wa mwaka 2011, kuna Shilingi milioni 300 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbili za Walimu, Chuo Kikuu Hombolo. Sasa kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ya Mwaka huu, bado inaendelea kueleza kwamba fedha hizi zitatumika. Sasa zitatumika kivipi wakati muda wa kufunga mahesabu ya mwaka umefika na wakati fedha hizi ziliidhinishwa tangu mwaka 2011? Hebu naomba kidogo utufafanulie, zilikwenda lakini hazikutumiwa au vipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia, hizo hela ziko wapi? Tuko katika mshahara wa Waziri. Haina uhusiano na mradi wowote isipokuwa kumwadhibisha yeye huyu kufanya mambo yake. Ndiyo maana tunasema hapa tunatumia sera zaidi kuliko kusema ziko wapi hela? Tungeingia kwenye vifungu pale ndiyo ungesema fedha hizo ziko wapi?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu nilizungumzia suala kubwa lililopo katika Wilaya zote katika Mkoa wa Tabora, suala la

ardhi ambapo ndani ya Wilaya moja tu ya Urambo zaidi ya vijiji 20 wanaambiwa wako kwenye hifadhi maeneo ambayo wamekaa zaidi ya miaka 30 iliyopita na wamekuwa wanabughudhiwa kila mara. Kwa hiyo, wanashindwa hata kutulia kufanya shughuli za maendeleo. Wanakuja maafisa maliasili wanasema, ondokeni, bila kuwaambia wanaondoka kwa utaratibu gani? Wanakwenda wapi? Wanakwenda kufanya nini, wakati wanalima, wanafuga na mambo mengine?

Napenda Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie, wananchi kama hawa ambao wameshindwa kutulia na kufanya kazi zao na kila siku wanasumbuliwa, vijiji vimesajiliwa kisheria na wapo kisheria na wanafanya chaguzi na wana viongozi wao, Serikali inafanya nini kuondoa bughudha hii na kero hii kwa wananchi hawa wa Mkoa wa Tabora na *particularly* Wilaya ya Urambo?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili Mheshimiwa Sakaya alishawahi kuuliza. Nakumbuka aliyewahi kuwa Waziri wa Maliasili, aliwahi kujibu. Naomba nimhakikishe Mheshimiwa Sakaya, jambo hili tumelisikia, tunalitafakari, tusubiri Mheshimiwa Waziri wa Maliasili atakapokuja tutakaa pamoja na Mheshimiwa Mbunge ili tulitafakari na tulizungumze vizuri.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kupatiwa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala la mkakati wa kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Kwa kuwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri haikugusia hata sehemu moja

ambayo inaelezea mkakati wa ugonjwa wa UKIMWI; Mwaka jana mradi huu uliomba upatiwe na ukaidhinishwa Shilingi milioni 216, lakini mwaka huu wa fedha hotuba ya Waziri wa TAMISEMI haikugusia hata kidogo. Je, tuelewe nini? Naomba nipatiwe ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Kwani hakuzungumzia habari ya UKIMWI? Waziri wa Nchi**.**

**WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, ni kwamba UKIMWI unashughulikiwa na sekta mbalimbali na kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu, suala la UKIMWI liko kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Lakini kwa maana ya sisi, akiangalia kwenye hotuba yetu kwenye Shirika la Elimu kule Tumbi Kibaha tumeelezea UKIMWI kama ni suala la kutaja. Lakini kwa maana ya mtu aliyepewa dhamana ya kulisimamia suala hilo, ni Ofisi ya Waziri Mkuu na ndani ya Hotuba ya Waziri Mkuu suala la UKIMWI limezungumzwa na akija Waziri wa Afya atalizungumza.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, napenda nimpongeze na nimshukuru mama yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia kutokana na maelezo yake ya kutaka kudhibiti fedha zetu kwenye Halmashauri na Benki. Lakini kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali Halmashauri zetu kutumia Benki nyingine mbali na *NMB,* na kwa kuwa Wizara ya Fedha imetangaza zabuni kwa mabenki kutoa huduma kwa Serikali ambayo kimtazamo inakinzana na *Procurement Act* ya mwaka 2011, kifungu cha 66 (3): Je, Mheshimiwa Waziri anatoa

tamko gani juu ya zabuni hii? Je, yuko tayari kuifuta kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Kwanza hili suala liliulizwa na Mheshimiwa Rajab, sasa kwa sababu ameingiza habari ya *tender*, basi naomba ujibu.

**WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikusema kwamba nimekubali Mamlaka za Serikali za Mitaa au Serikali kuweza kutumia Benki nyingine. Nilichosema ni kwamba mwanzo tulikuwa tunaitumia sana *NMB* kwa sababu mtandao wake ni mkubwa. Nilichozungumza, tena nilisema suala hilo linazungumzika. Sasa linazungumzika vipi? Kwa vile *tender* ilitangazwa, lengo ni kuhakikisha kwamba kila mtu anakwenda kushindana, sasa atakayeshinda ndiye ataendelea kufanya kazi na Serikali. Suala la mimi kufuta *tender* iliyotangazwa na Taasisi ambayo haiko chini yangu, kwa kweli sina uwezo huo.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nilizungumzia pesa za rada kwa Zanzibar kupata fungu lake. Mheshimiwa Waziri Mkuu amejibu zimepitia Wizara ya Mawasiliano, siyo ya Muungano. Kwa kweli hoja yangu imekuja kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri, kifungu cha (8) ambacho kina mikopo na biashara ya nje, nyongeza ya kwanza ya Katiba. Vilevile kifungu cha 11, usafiri, anga, Posta, Simu, ni mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12 kinahusika na mambo yote ya sarafu na fedha kwa ajili ya mikopo, fedha za Kigeni, usimamizi wa fedha na fedha za kigeni. Sasa hili suala rada iliponunuliwa katika kumbukumbu za *Hansard* sijajua ni Wizara gani, lakini lilizungumziwa, inahusiana na mambo ya Ulinzi pamoja na mambo ya ndege. Sasa haya yote ni mambo ya Muungano. Sasa leo kutoa fedha ya rada ukasema Zanzibar isipate fungu, ni sawasawa na kusema hivi vifungu vyote vya Katiba tunavikiuka, na jambo kubwa zaidi, hadi leo *formula* ya uchangiaji mfuko wa Muungano wa pamoja, haipo.

**MWENYEKITI:** Kengele Imegonga.

**MHE. MOHAMMED H.J. MNYAA:** Kinachotumika ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Naomba ufafanuzi katika suala hili hasa katika hali ya leo ya Katiba Mpya na watu wanavyouliza huko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwana Sheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna ambayo watu hawaifahamu kuhusiana na huu mchakato wa kununua rada. Rada hii haikununuliwa na fedha za Muungano, ilinunuliwa kama ni jambo la Tanzania Bara. Hizi fedha za rada, siyo suluhisho la kila kero na kama zinaweza kutumika Zanzibar siyo kwa sababu zilikuwa zinakwenda kwenye kitu ambacho kinaonekana kama ni jambo la Muungano. Nchi mbili hizi zinaweza kuzungumza zikatumia fedha hizo kwa

njia ambayo zitaelewana, lakini ukweli ni kwamba halikuwa jambo la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa pale utaona kwamba kuna anga na usafirishaji wa anga, lakini rada hii haiku huko. Hayo ndiyo maoni yetu na Mheshimiwa Mnyaa tutaendelea kuzungumza kusudi afahamu historia ya jinsi ile rada ilivyopatikana.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilitaka kujua ni lini Serikali italipa deni la mawakala? Kwani hadi hivi sasa baadhi ya mawakala wameanza kufikishwa Mahakamani na wengine kunyang'anywa dhamana walizokuwa wameziweka baada ya kukopa hela kwenye taasisi za mabenki. Nilitaka ufafanuzi, ni lini Serikali itawalipa mawakala waliosambaza pembejeo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tulimaliza kulipa shilingi bilioni 43 kwa baadhi ya mawakala waliosambaza pembejeo. Baada ya malipo hayo, sasa tumeomba tena Shilingi bilioni 53 na taarifa nilizonazo sasa, ni kwamba *process* inafanywa kuzipeleka benki. Hadi jana nimeambiwa ndani ya wiki mbili fedha hizo zitaanza kulipwa. Kwa hiyo, ninaomba awe na subira, mchakato unaendelea.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, pamoja na mambo mengine, nilimtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu aweke c*ommitment* ya tatizo tulilonalo la ukanda wa Kusini kwa kutokuwa na Hospitali ya Rufaa. Jambo hili ni la muda mrefu na limeleta mgogoro sana na

baadaye Serikali imetuambiwa kwamba sasa wamemaliza na kwamba Hospitali ya Rufaa ingejengwa Mtwara. Katika bajeti iliyopita, zilitengwa pesa kidogo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *fence* na kwa kweli hela hizo zimetumika, lakini hatuoni katika bajeti hii mpango mahsusi wa kuhakikisha hospitali hiyo ya Rufaa inajengwa Mtwara, huku ukitilia maanani kwamba Mji unapanuka, maeneo yale ya Kusini yanapanuka na pengine ni katika kanda chache zenye tatizo hili kutokamilika. Naomba majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira na nia hiyo ya kujenga Hospitali ya Kanda pale Mtwara ipo, ndiyo maana katika bajeti iliyopita fedha za kuanzia kuweka *fence* eneo husika. Mwaka huu wa fedha kwa bahati mbaya sana kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, fedha zilizoweza kupatikana ni Shilingi milioni 400 ambazo tunatarajia angalau zianze zile hatua za awali katika ujenzi huu na tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuwa na Hospitali ya Kanda.

**MHE. MURTZA A.MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliomba kwamba nipate ufafanuzi kwa nini mpaka leo katika maombi yetu maalum ya ujenzi wa barabara kutoka Kipatimo kwenda Mkupera ambayo inayajenga maeneo ya Kandawale kuwa katika kisiwa kwa karibu kipindi cha robo mbili za mwaka na majibu ya Waziri Mkuu na Mawaziri wote sikuona yakianishwa kuhusiana na jambo hilo? Naomba nipate ufafanuzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Hawakusikia vizuri, naomba urudie tafadhali.

**MHE. MURTZA A.MANGUNGU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi tumeleta maombi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Kipatimo hadi Mkupera na sasa ombi hilo liko katika ofisi ya Waziri Mkuu kwa zaidi miaka miwili, hakuna majibu ya kukubaliwa au kukataliwa. Je, tunapata majibu gani kuhusiana na hilo?

**NAIBU WAZIRI TAMISEMI (K.n.y.) WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuwa hii amekuwa akiizungumzia mara kwa mara na imekuwa ikija kama maombi maalum. Maombi maalum ni jambo ambalo tunashirikiana sisi na Wizara ya Fedha kuona uwezekano wa kuzipata hizo hela. Nilikuwa naomba tu kwamba hebu aendelee kutuachia tuone jinsi ambavyo tunaweza kusaidia katika hili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wale wote walioomba kuchukua mshahara wa Waziri Mkuu, wote wamekwisha, na mkiangalia hata kama nimewaomba dakika thelathini ni saa tatu kasorobo na hizi *volume* ziko tatu, kwa hiyo, tunaingia kwenye *guillotine* sasa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*........................ Sh. 930,827,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning ............................Sh.* 5,815,195,000/=

Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*................................ Sh. 268,800,000/=
Kif. 1005 - *Government Communication Unit*.....Sh. 251,523,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit .......Sh.* 259,277,000/=
Kif. 1007 - *Legal Services Unit*.................................. *Sh.* 116,196,000/=
Kif. 1008 - *Management Information System Unit.. Sh.*187,108,000/=
Kif. 2001 - *Civil Affairs and Contingencies ............. Sh.*8,923,941,000/=
Kif. 2002 - *National Festivals*................................... *Sh.*834,347,000/=
Kif. 3001 - *Parliamentary and Political Affairs ........... Sh.*743,193,000/=
Kif. 4001 - *Investment and Private Sector Development ........................................... Sh.*6,872,730,000/=
Kif. 5001 - *Coordination of Government Business.... Sh.* 962,997,000/=
Kif. 7001 - *Government Printer*................................ *Sh.* 4,689,838,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 42 – OFISI YA BUNGE

Kif. 1001 - *Administration and General* ………Sh. 16,708,174,200/=

Kif. 2001 - *National Assembly ……………………. Sh.* 94,887,878,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 56 – TAMISEMI**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management... ..* Sh. 3,286,463,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts ……………… Sh.* 498,813,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning Division ……* *Sh.* 922,655,000/=
Kif. 1004 - *Mgt Information Syst. Division.......... Sh.* 361,581,000/=
Kif. 1005 - *Legal Services Division………………… Sh.* 439,330,000/=
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit ............................ Sh.* 348, 561,000/=
Kif. 1007 - *Government Comm. Unit ................. Sh.* 383,925,000/=
Kif. 1008 - *Procurement Management Unit ..... Sh.* 326,597,000/=
Kif. 1009 - *Infrastructure Development Unit ...... Sh.* 129,197,515/=
Kif. 2001 - *Regional Administration Division ...... Sh.*804,373,000/=
Kif. 2002 - *Local Govent Coordination Div........ Sh.*14,108,870,000/=
Kif. 2003 - *Sector Coordination Division............ Sh.* 933,514,000/=

Kif. 2004 - *Basic Education Coordination Div....... Sh.* 1,546,240,000/=
Kif. 2005 - *Urban Development Division .............. Sh.* 1,545,017,000/=
Kif. 3001 - *Organization Development Div......... Sh.* 9,911,272,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 61 - *ELECTORAL COMMISSION*

Kif. 1001- *Admin. and HR Management* ..........Sh. 2,139,019,000/=
Kif. 1002 - *Planning Monitoring and Evaluation Div....* *Sh.*164,639,000/=
Kif. 1003 - *Finance and Accounts Unit ………………..* *Sh.*244,648,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit ………………………....* *Sh.*178,032,000/=
Kif. 1005 - *Legal Services Unit……………………….....* *Sh.*218,924,000/=
Kif. 1006 - *Procurement MGT &Logistics Unit …………* *Sh.*192,626,000/=
Kif. 2001 - *Election Management Division ……….......* *Sh.*195,820,000/=
Kif. 2002 - *Permanent National Voters Registration System Division....................................... Sh.* 234,692,000/=
Kif. 2003 - *Voters Education Public Inf. Div.………* *Sh.*195,281,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 91 – *ANTI DRUG COMMISSION*

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management..........* Sh. 1,361,470,000/=

*(Kifingu kilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 92 - *TACAIDS (TANZANIA COMMISSION FOR AIDS)*

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management ………* Sh. 151,361,200/=
Kif. 1002 - *Finance, Admn. and Resource Mob.... Sh.* 1,511,688,000/=
Kif. 1003 - *Monit., Evaluation, Research and Mis.... Sh.* 103,985,100/=
Kif. 1004 - *Advocacy, Infor., Education and Com….. Sh.* 73,356,900/=
Kif. 1005 - *District and Comm. Response…………..* *Sh.*525,849,500/=
Kif. 1006 - *Procurement Mgt Unit…………….......... Sh.* 80,055,600/=
Kif. 1007 - *Legal Unit ………………………………. ..... Sh.* 77,097,700/=
Kif. 1008 - *Management Information System ……… Sh.* 48,987,300/=
Kif. 1009 - *Internal Audit Unit …………………………... Sh.* 68,646,000/=

Kif. 1010 - *Special Programmes*…………………….... *Sh.*119,770,500/=
Kif. 1011 - *Government Communication Unit* …….. *Sh.* 38,218,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 27 - REGISTRAR OF POLITICAL PARTIES

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt.…….* Sh. 19,488,941,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MIKOA

## FUNGU 36 – MKOA WA KATAVI

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management*……….. Sh. 731,330,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ……………… " 59,308,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit* ………………………….. " 39,839,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management* ….…….. " 20,992,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Mpanda* …………………………. " 112,336,000/=
Kif. 1006 - *DAS-Mlele* ……………………………. " 193,463,000/=

Kif. 1014 - *Legal Services Sector ………………..* “ 21,246,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Techn.……* “ 1,205,375,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination…………..* “ 97,249,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector ….* “ 86,971,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector……………………* Sh. 56,110,000/=
Kif. 2005 - *Local Govern*t Mgt Services……………. “ 53,694,000/=
Kif. 2006 - Education Sector………………………. “ 135,913,000/=
Kif. 2007 - *Water Services* ……………….…….“ 40,727,000/=
Kif. 3001 - *Reginal Hospital* ……………………….“ 49,549, 000/=
Kif. 8091 - *Local Government* …..……………….. “ 26,600,065,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 47 - MKOA WA SIMIYU

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management ………* Sh. 507,540,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts ……………..* “ 47,302,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit……………………….* “ 22,866,000/=

Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit* ………………… “ 26,310,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Bariadi* ……………………………. “ 218,634,000/=
Kif. 1006 - *DAS-Maswa* …………………………..... “ 189,164,000/=
Kif. 1007 - *DAS Meatu*……………………………… “ 194,860,000/=
Kif. 1008 - *DAS Busega* ……………………………. “ 218,264,000/=
Kif. 1009 - *DAS Itilima*……………………………… “ 195,908,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit* …………………….. “ 21,100,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Techn.*…... “ 34,387,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………..... “ 71,397,000/=
Kif. 2002 - Economic and Prod. Sector…………..“ 114,121,000/=
Kif. 2003 - Infrastructure Sector ………………...“ 75,687,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector*…………………………….... “ 78,924,000/=
Kif. 2005 - *Local Government Services*…………. “ 92,837,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*……………………….. “ 208,286,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector* …………………………… “ 56,422,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ………………………. “ 493,176,000/=

Kif. 8091 - *Local Government Authorities*……… “ 71,656,741,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 54 - MKOA WA NJOMBE

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* …………Sh. 374,432, 000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………... “ 59,101,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit* …………………………… “ 39,895,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit* ………………........... “ 29,895,000/=
Kif. 1005 - *District Admin. Secretary - Njombe*……. “ 336,017,000/=
Kif. 1006 - *District Admin. Secretary - Makete* …… “ 274,934,000/=
Kif. 1007 - *District Admin. Secretary - Ludewa* ….. “ 287,758,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Wanging'ombe......................... Sh.* 239,796,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*..………………………” 57,555,000/=
Kif. 1015 - *Inform. and Comm. Tech*……………...…” 1,676,335,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………………” 110,397,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*………” 100,130,000/=

Kif. 2003 - *Infrastructure Sector* ……………………. " 82,302,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector*………………………………" 70,753, 000/=
Kif. 2005 - *Local Govornt Mget Services*……………" 66,456,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector* ………………………….. " 124,035,000/=
Kif. 2007 - *Water Services* …………………………... " 51,922,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* …………………………. " 388,954,000/=
Kif. 8091 - *Local Government Authorities* ……..... " 59,776,190,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 63 - MKOA WA GEITA

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……… Sh. 668,176,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit* …………. " 53,712,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit* ……………………………" 33,194,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ….. " 17,946,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Geita*……………………………... " 70,000,000/=
Kif. 1006 - *DAS-Bukombe* ………………………… " 70,000,000/=

Kif. 1007 - *DAS Chato* ………………………………... " 70,000,000/=
Kif. 1008 - *DAS Nyang'hwale* ……………………. " 206,062,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Mbogwe*……….........................." 217,486,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit* ……………………." 20,048,000/=
Kif. 1015 - *Information Comm. Tech. Unit*…….. " 34,284,000/=
Kif. 2001 - *Management Support*……………….. " 130,492,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Dev. Support*……….. " 168,044,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Section* ……………." 96,504,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector*…………………………. " 111,102,000/=
Kif. 2005 - *Local Governt Mgt Services*……… " 87,320,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector* ……………………. " 234,389,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector* ………………………….." 72,022,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* …………………..." 89,746,018,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 70 - MKOA WA ARUSHA**

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……… Sh. 2,346,330,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ……………… " 98,781,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………….. Sh. 34,980,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit* .........……………" 38,293,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Arusha* ………………………………" 159,656,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Ngorongoro* ………………………. " 174,445,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Karatu* ………………………………" 86,782,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Arumeru* ………………………… " 178,936,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Monduli* ………………………….. " 102,662,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Longido* ……………………………. " 139,705,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………........" 14,000,000/=
Kif. 1015 - *Infor. and Comm. Techn. Unit*…........….. " 34,577,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Codination*……………….. " 138,800,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*…….. " 205,298,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………… " 171,118,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………... " 85,883,000/=

Kif. 2005 - *Local Government Services* …………… “ 65,237,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector* ……………………………“ 292,537,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector* …………………………..... “ 55,877,000/=
Kif. 3001 - *Reginal Hospital* ……………………….... “ 4,813,362,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* …………………...“ 133,871,224,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 71 - MKOA WA PWANI**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*…...... Sh. 1,155,541,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Units* ………… “ 87,263,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit* …………………….... “ 18,458,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* …… “ 88,183,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Kibaha* …………………………..... “ 189,717,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Mafia* ………………………….…. “ 159,227,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Kisarawe* ………………………….. “ 188, 810,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Bagamoyo* ………………………. “ 259,769,000/=

Kif. 1009 - *DAS - Rufiji*……………………………….. “ 227,507,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Mkururanga* …………………….. “ 205,933,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*…………………….“ 10,000,000/=
Kif. 1015 - *Inform. and Comm. Techn. Unit*……...“ 29,180,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………….. “ 253,337,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* … “ 276,151,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* … “ 276,151,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector* …………………..“ 208,835,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* …………………………… “ 81,702,000/=
Kif. 2005 - *Local Governt Mgt Services* …………“ 60,652,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*………….……….….. “ 196,169,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector* ……………………………. “ 26,758,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….. “ 290,765,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* …………………... ..“ 97,297,104,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 72 - MKOA WA DODOMA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* ………… “ 921,442,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………….. “ 107,194,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*…………………….... “ 47,664,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit*….......…………. “ 37,704,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Kondoa* ……………………………. “ 250,108,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Mpwapwa* ………………………. . “ 201,255,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Kongwa* …………………….……. “ 178,717,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Bahi* ………………………………. “ 205,034,000/=
Kif. 1009 - *DAS Chamwino* …………………….…….. “ 211,304,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Dodoma* ……………………….…. “ 150,264,000/=
Kif. 1011 - *DAS - Chemba* ……………………….……. “ 120,000,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*………………………….“ 29,208,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Techn. Unit*….....“ 40,998,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….“ 197,834,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Prod. Sector* …………….” 202,388,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector* …………………... “ 138,726,000/=

Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………….“ 200,567,000/=
Kif. 2005 - *Local Governt Mgt Services* …………….“ 91,497,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*………………………….“ 293,612,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector* …………………………….... “ 55,027,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………… “ 4,034,978,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* …………………. “ 118,682,179,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 73 - MKOA WA IRINGA

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management*…….…….Sh. 720,562,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………….. “ 139,706,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*…………………….... “ 43,778,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit*…….... “ 41,014,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Iringa* ……………………………….. “ 277,632,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Njombe*……………………………..... “ *0/=*
Kif. 1007 - *DAS - Mufindi* …………………………….. “ 257,256,000/=

Kif. 1008 - *DAS - Ludewa* …………………………….. " 0/=
Kif. 1009 - *DAS - Makete* ………………………………… "0/=
Kif. 1010 - *DAS - Kilolo* …………………………..…." 225,171,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*………………………….. " 26,020,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Techn.* ………..." 77,236,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….. " 179,972,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Prod. Sector* ……………" 277,478,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector* …………………..... " 147,124,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………...." 204,902,000/=
Kif. 2005 - *Local Governt Mgt Services* ……………" 159,520,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*………………………….. " 371,276,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector* ………………………………. " 113,304,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….. " 3,852,589,000/=
Kif. 8091 - *Local Government Authority* ………... " 87,006,875,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 74 - MKOA WA KIGOMA

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……… Sh. 905,572,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*………….. “ 47,000,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………... “ 26,677,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* …… “ 32,000,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Kigoma* ………………………….. “ 273,437,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Kasulu* ……………………………… “ 273,241,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Kibondo* ………………………….. “ 250,941,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Kakonko* …………………………… “ 139,000,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Buhigwe* ………………………….. “ 155,000,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Uvinza* …………………………….. “ 123,000,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………….. “ 2,230,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech* ……… “ 36,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………….... “ 239,840,000/=
Kif. 2002 - *Economic and ProductiveSector* ……“ 256,385,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………….... “ 173,364,000/=

Kif. 2004 - *Social Sector* ………………………... “ 136,154,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* .......“ 112,293,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*……………………….. “ 236,000,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………. “ 14,000,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………… “ 2,170,346,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………………. “ 79,480,564,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 75 - MKOA WA KILIMANJARO

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* …….. Sh. 1,142,238,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………. “ 129,367,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*…………………….. “ 26,927,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* …“ 55,582,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Moshi* …………………………… “ 242,270,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Hai* …………………………….. .“ 206,203,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Rombo* ………………………... “ 199,131,000/=

Kif. 1008 - *DAS - Same* ............................ "
236,187,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Mwanga*............................ "
190,314,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Siha*.................................. "
132,832,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*......................... "
16,112,000/=
Kif. 1015 - *Inform. and Comm. Techn. Unit*......."
31,986,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*.......... ..."
218,468,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ... "
541,121,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*..................... "
191,453,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* .......................... "
16,524,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT.Management Services...* "
42,344,200/=
Kif. 2006 - *Education Sector*........................."
286,589,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*.............................. "
18,951,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ........................."
4,163,050,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ..................."
153,091,354,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 76 - MKOA WA LINDI**

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……... Sh. 1,237,506,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*……………“ 99,980,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………... “ 36,810,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* …… “ 33,668,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Lindi*………………………………… “ 289,444,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Kilwa* …………………………….. “ 225,922,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Liwale*………………………………“ 177,927,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Nachingwea* …………………….. “ 222,488,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Ruangwa* ……………………..... “ 195,916,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*…………………….. “ 32,732,000/=
Kif. 1015 - *Inform. and Comm. Tech. Unit*……….“ 51,667,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………... “ 139,471,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ….. “ 276,499,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*………………….. “ 142,871,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………….... “ 140,073,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* … “ 121,641,000/=

Kif. 2006 - *Education Sector*……………………….. “ 268,889,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*…………………………….. “ 93,517,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….“ 2,314,102,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. “ 61,231,986,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 77 - MKOA WA MARA**

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ………. Sh. 750,651,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………… “ 179,928,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………… “ 61,816,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit* …………….... “ 69,945,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Musoma*………………………….. “ 241,973,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Bunda* …………………………….. “ 240,093,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Serengeti* ……………………….. “ 223,021,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Tarime* …………………………. “ 242,489,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Rorya*……………………………..…“ 256,437,000/=

Kif. 1010 - *DAS - Butiama* ……………………...……“ 120,000,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………….“ 45,903,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech* ………“ 56,225,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………… “ 242,356,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Prod. Sector*……….. “ 253,501,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*………………… “ 157,171,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………….. “ 132,617,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Mgt Services* …………….. “ 118,083,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*…………………..….. “ 262,548,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………….. ..“ 83,130,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………. “ 2,529,694,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………..... “ 119,316,889,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 78 - MKOA WA MBEYA**

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management*……..... Sh. 975,408,000/=

Kif. 1002- *Finance and Accounts Unit* ………….. “ 124,578,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit* …………............ “ 44,951,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit*………………. “ 44,096,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Mbeya* …………………………. “ 215,201,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Ileje* ………………………………“ 183,735,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Kyela*………………………………. “ 150,567,000/=
Kif. 1008 - *DAS- Chunya* …………………………….. “ 218,991,000/=
Kif. 1009 - *DAS Mbozi*………………………………….. “ 247,518,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Rungwe*……………………………... “ 195,557,000/=
Kif. 1011 - *DAS - Mbarali*…………………………….. “ 197,035,000/=
Kif. 1012 - *DAS - Momba* ……………………………... “ 120,000,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………………. “ 8,757,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech* …………. “ 17,172,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*……………... “ 125,878,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*……..... “ 216,329,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………………... “ .138,542,000/=

Kif. 2004 - *Social Sector* ………………………………” 0/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* ……. “ 80,895,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*…………………………..…“ 335,006,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………….“ 51,049,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….“ 1,756,696,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. “ 194,680,565,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 79 - MKOA WA MOROGORO

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……….. Sh. 862,296,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………….. “ 165,399,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*…………………..….. “ 45,636,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ……….“ 51,945,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Morogoro* ………………………….. “ 258,133,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Kilosa* ……………………………….. “ 337,006,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Kilombero* ………………………….. “ 261,648,000/=

Kif. 1008 - *DAS - Ulanga* …………………………..... “ 322,917,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Mvomero*………………………….... “ 259,410,000/=
Kif. 1010 - DAS - Gairo ……………………………….... “ 120,000,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………….... “ 38,059,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech* ………… “ 90,741,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….. “ 180,039,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …… “ 247,407,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….. “ 199,879,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ………………………….... “ 137,544,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services*.…... “ 98,546,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*……………………….... “ 235,740,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*…………………………….….. “ 66,400,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ………………………..…“ 5,445,517,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. “ 146,459,023,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

# FUNGU 80 - MKOA WA MTWARA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* ………. Sh. 1,374,957,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………..... " 31,699,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………... " 13,040,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ……. " 30,125,000/=
Kif. 1005 - *DAS – Mtwara* ………………………….. " 193,034,000/=
Kif. 1006 - *DAS-Newala* …………………………….. " 171,228,000/=
Kif. 1007 - *DAS – Masasi* ………………………….. " 209,826,000/=
Kif. 1008 - *DAS- Tandahimba* ……………………. " 205,047,000/=
Kif. 1009 - *DAS Nanyumbu* ……………………….. " 249,060,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………..... " 26,102,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech* ……..... " 22,939,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………... " 243,873,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector.*….." 154,350,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*………………….. " 143,424,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………….. " 121,412,000/=

Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* …" 44,083,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*……………………….... " 205,001,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………… " 56,457,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ………………………." 2,654,248,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. " 92,896,097,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 81 - MKOA WA MWANZA**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*……….. Sh. 1,034,486,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………. " 140,359,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*…………………….. .." 63,127,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* …... " 59,744,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Nyamagana* ……………………." 219,428,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Sengerema* …………………….. " 281,153,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Geita* …………………………….. " 211,808,,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Kwimba* ……………………..... " 270,596,000/=

Kif. 1009 - *DAS - Magu*.................................. “ 277,078,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Misungwi* .............................. “ 269,481,000/=
Kif. 1011 - DAS - Ilemela ................................ “ 210,853,000/=
Kif. 1012 - DAS - Ukerewe ............................. “ 268,195,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*......................... “ 27,004,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech* ........“ 40,532,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*................ “ 302,495,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ........ “ 218,274,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*......................... “ 171,879,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ................................. “ 133,178,000/=
Kif. 2005 - *Local Government Mgt Services*...........“ 70,255,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*.............................. ” 303,440,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*.................................... .“ 31,482,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ..............................” 3,400,889,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ...................... “ 175,620,378,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 82 - MKOA WA RUVUMA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*.............Sh. 717,469,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*……………“ 142,858,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………… ..“ 61,703,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit* …………….…... “ 76,064,000/=
Kif. 1005 - *DAS – Songea* …………………………..“ 317,257,000/=
Kif. 1006 - *DAS-Tunduru*…………………………….. “ 281,599,000/=
Kif. 1007 - *DAS – Mbinga* …………………………“ 262,226,000/=
Kif. 1008 - *DAS- Namtumbo* ……………………..“ 241,838,000/=
Kif. 1009 - DAS- Nyasa ………………………………“ 230,788,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*………………………“ 27,610,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Techn. Unit*... “ 47,724,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………... “ 166,127,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …. “ 150,403,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*………………….. “ 176,060,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ………………………. “ 79,505,000/=

Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* ... " 99,001,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*.......................... " 271,794,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*.................................." 88,947,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* .........................." 4,165,001,000/=
Kif. 3002 - *Preventive Services*........................ " 58,295,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ........................" 94,386,873,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 83 - MKOA WA SHINYANGA**

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ........... Sh. 1,264,225,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*................. " 136,168,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*............................. " 38,090,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ........... " 50,784,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Shinyanga* ............................. " 236,724,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Maswa* .................................... " 0/=
Kif. 1007 - *DAS - Bariadi* ...................................." 0/=

Kif. 1008 - *DAS - Kahama* …………………………..... “ 222,534,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Meatu*…………………………....…“ 0/=
Kif. 1010 - *DAS - Bukombe* ……………………………“ 0/=
Kif. 1011 - *DAS* - Kishapu……………………………..... “ 194,617,000/=
Kif. 1014 - *Legal Sector Unit*………………………. “ 25,200,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech. Unit*... “ 26,603,,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………….... “ 155,146,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ….. “ 152,935,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………… “ 135,271,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………“ 130,682,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Mgt Services* ……………......“ 81,427,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*……………………….... “ 272,824,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………….. “ 46,300,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….“ 2,707,304,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. “ 85,550,332,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 84 - MKOA WA SINGIDA

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……… Sh. 1,346,253,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*………...…. " 43,272,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………..... " 27,485,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ……..." 36,738,000/=
Kif. 1005 - *DAS – Singida*……………………..……….. " 150,160,000/=
Kif. 1006 - *DAS-Manyoni*…………………………….... " 122,107,000/=
Kif. 1007 - *DAS – Iramba* …………………………….. " 122,107,000/=
Kif. 1008 - DAS- *Ikungi* ……………………………….. " 120,000,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………….. " 6,000,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech*…………. " 16,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….. " 245,455,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ……..." 196,730,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….. " 170,370,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ………………………….. " 141,469,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* ……" 51,000,000/=

Kif. 2006 - *Education Sector*.............................. “ 146,000,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*.................................... “ 40,000,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ...........................“ 2,699,216,000/=
Kif. 3002 - *Preventive Services*......................... “ 48,878,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ........................ “ 72,618,048,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 85 - MKOA WA TABORA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*........ Sh. 1,163,791,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*............. “ 99,854,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*..........................“ 20,084,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit* ................... “ 48,383,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Tabora*................................. “ 182,457,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Nzega*...................................“ 202,443,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Sikonge* ...............................“ 156,790,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Igunga* ...............................“ 187,957,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Urambo* ...............................“ 190,840,000/=

Kif. 1010 - *DAS - Uyui* ………………………..……….” 181,597,000/=
Kif. 1011 - *DAS - Kaliua* ……………………………….“ 189,917,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………….“ 20,280, 000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech*……….... “ 31,147,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*……………. .“ 126,922,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*….... “ 150,033,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………..... “ 141,095,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* …………………………. “ 132,182,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management* ………………“ 72,388,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*………………………….“ 249,666,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*…………………………….....” 39,855,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….. “ 2,695,643,000/=
Kif. 3002 - *Preventive Services*……………………….“ 68,560,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………………..…….. “ 106,299,274,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 86 - MKOA WA TANGA**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* ……….Sh. 2,013,544,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………... " 44,401,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*………………………. " 29,000,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* …..... " 34,000,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Tanga*……………………………….." 75,669,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Kilindi*……………………………... " 109,239,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Korogwe* ………………………… " 101,135,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Lushoto* ……………………….……" 115,042,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Mkinga* …………………………..…" 90,590,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Muheza* …………………………..." 88,513,000/=
Kif. 1011 - *DAS - Pangani* …………………………… " 79,781,000/=
Kif. 1012 - *DAS - Handeni* ……………………………." 104,089,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*…………………..……." 7,000,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech. Unit*….." 14,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*……………." 228,510,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …..." 220,571,000/=

Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………………“ 187,705,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* …………………………..“ 90,968,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* ….“ 145,785,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*………………………..“ 192,689,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………..“ 15,000,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ………………………“ 4,037,428,000/=
Kif. 3002 -*Preventive Services*…………………....“ 30,340,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………………“ 150,365,187,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 87 - MKOA WA KAGERA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* …..... Sh. 2,381,370,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………. “ 30,833,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………“ 34,615,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Mgt Unit* ……..……….. “ 38,654,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Bukoba*…………………………“ 61,995,000/=

Kif. 1006 - *DAS - Biharamulo*……………………….“ 62,607,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Chato* …………………………....“ 0/=
Kif. 1008 - *DAS - Karagwe* ……………………….“ 61,452,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Misenyi* …………………………....“ 61,473,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Muleba* …………………………. “ 61,081,000/=
Kif. 1011 - *DAS - Ngara* …………………………….“ 61,409,000/=
Kif. 1012 - *DAS - Kyerwa* …………………………….“ 120,000,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………….“ 18,676, 000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech*…......“ 49,047,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*……….... ....“ 280,356,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*..… “ 218,860,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….“ 203,106,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ………………………… “ 101,125,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* … “ 69,415,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*……………………..... “ 198,382,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*…………………………….“ 30,572,000/=

Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….“ 2,854,041,000/=
Kif. 3002 - *Preventive Services*………………….... “ 2,854,041,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* …………………….“ 127,628,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 88 - MKOA WA DAR ES SALAAM

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* …….. Sh. 1,015,990,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*……….... “ 82,320,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………“ 35,223,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ….. “ 54,378,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Ilala*……………………………... “ 223,239,000/=
Kif. 1006 - *DAS-Kinondoni*………………………... “ 250,228,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Temeke* ……………………….... “ 247,573,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………. “ 19,209, 000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech*……… “ 46,433,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………“ 196,929,000/=

Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*...... " 158,617,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………… " 191,827,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ………………………. " 55,837,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services* …. " 87,958,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*…………………………" 361,814,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………………" 90,305,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………..……" 252,273,482,000/=

## FUNGU 95 - MKOA WA MANYARA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* …….... Sh. 633,117,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*……………..." 202,670,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*……………………... " 40,900,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ………" 60,602,000/=
Kif. 1005 - *DAS – Babati*…………………………..... " 197,547,*000/=*
Kif. 1006 - *DAS-Hanang*………………………………. " 248,187,000/=
Kif. 1007 - *DAS – Kiteto* ……………………………... " 255,442,000/=
Kif. 1008 - *DAS- Mbulu*……………………………….... " 229,536,000/=

Kif. 1009 - *DAS- Simanjiro*…………………………….... “ 235,640,000/=
Kif. 1014 - *Legal Service Unit*……………………….…. “ 40,020,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comm. Tech*............. “ 44,335,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….. “ 312,454,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*…….. “ 213,113,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………………. “ 162,382,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ………………………….... “ 161,640,000/=
Kif. 2005 - *Local GVT. Management Services*…….. “ 120,691,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector*…………………………. “ 307,742,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………………. “ 52,547,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….... “ 601,210,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………….……. “ 87,381,994,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 36 – MKOA WA KATAVI**

Kif. 8091 – *Local Goverment... ... ... ... ...........*Sh. 8,210,243, 000/=

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 37 – OFISI YA WAZIRI MKUU**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* …….. Sh. 3,500,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*………………….. " 17,360,000/=
Kif. 2001 - *Civil Affairs and Contingencies* ……." 1,827,000,000/=
Kif. 2002 - *National Festivals*…………………… ..." 0/=
Kif. 4001 - *Invest. and Private Sectors Dev't*.... " 18,600,000,000/=
Kif. 5001 - *Coordination of Govern*t *Business*…." 49,960,637,000/=
Kif. 7001 - *Government Printer*……………….... " 500,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 42 - MFUKO WA BUNGE**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* …........Sh. 1,635,000,000/=
Kif. 2002 - *National Assembly*…………………..... " 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

## FUNGU 47 - MKOA WA SIMIYU

Kif. 8091 - *Local Government Authorities*…….Sh. 17,892,207,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 54 - MKOA WA NJOMBE

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*……….…..Sh. 326,261,000/=

Kif. 8091 - *Local Government Authorities*……… " 13,604,156,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 63-MKOA WA GEITA

Kif. 8091 *Local Government*...............………Sh. 19,988,644,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 70 - MKOA WA ARUSHA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*……..….Sh. 619,551,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….. “ 60,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …… “ 38,465,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….“ 0/=
Kif. 2004 - *Social Sector*……………………………..…“ 0/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………………“ 24,248,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital*……………………….. “ 158,523,000/=
Kif. 8091 - *Local Government*……………………...“ 25,710,395,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 71 - MKOA WA PWANI**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*……..….Sh. 50,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….. “ 60,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …… “ 38,484,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….. “ 239,339,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital*……………………….. “ 158,523,000/=

Kif. 8091 - *Local Government*……………….….“ 16,109,665,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 72 - MKOA WA DODOMA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*……… .Sh.2,817,263,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* … “ 48,028,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector*………………………………Sh. 176,591,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………... “ 24,703,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital*……………………….. “ 500,000,000/=
Kif. 8091 - *Local Government*……………………...“ 28,820,460,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 73 - MKOA WA IRINGA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*……...….Sh. 145,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………..….. “ 477,565,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*……. “ 109,965,000/=

Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………………. “ 0/=
Kif. 2004 - *Social Sector*……………………………...“ 170,455,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………...“ 29,929,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital*……………………….“ 0/=
Kif. 8091 - *Local Government Authority*………..“ 15,627,405,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 74 - MKOA WA KIGOMA

Kif.1001 - *Admin. and HR Management*……….....Sh. 574,383,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………....“ 24,703,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …. “ 6,000,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector*…………………………….” 30,000,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital*…………………….“ 222,727,000/=
Kif. 8091 - *Local Government*…………………...“ 30,077,410,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 75 - MKOA WA KILIMANJARO

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……….. Sh. 20,000,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Moshi* …………………………….. " 5,000,000/=
Kif. 1006 - *DAS -Hai* ……………………………….. " 5,000,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Rombo* …………………………. " 5,000,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Same* …………………………. " 5,000,000/=
Kif. 1009 - *DAS - Mwanga*…………………………. " 5,000,000/=
Kif. 1010 - *DAS - Siha*………………………………. " 5,000,000/=
Kif. 1015 - *Information and Comn. Tech. Unit*.... " 18,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………... " 50,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Prodtv. Sector* ………. Sh. 460,404,000/=
Kif. 2003 - *Infrustructure Sector*…………………....." 0/=
Kif. 2004 - *Social Sector* …………………………...." 0/=
Kif. 2007 - *Water Sector* …………………………….." 26,703,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….” 902,694,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………………." 21,062,707,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 76 - MKOA WA LINDI

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……....  Sh. 45,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*……………. " 50,825,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ……. " 58,370,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….. " 283,377,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………." 146,591,000/=
Kif. 2006 - *Education Sector* ……………………….. " 50,000,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………………" 24,703,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………….. " 50,000,000/=
Kif. 3002 - *Preventive Services*……………………..… " 0/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………………. " 13,570,913,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 77 - MKOA WA MARA

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ………..  Sh. 45,000,000/=

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………………“ 60,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …… “ 64,299,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………………..“ 1,193,744,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………….…………“ 146,591,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*…………………...………… “ 24,703,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………......“ 2,240,997,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. “ 27,765,505,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 78 - MKOA WA MBEYA**

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……… Sh. 287,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………….. “ 369,712,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ……“ 86,347,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………………Sh. “ 0/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………“ 0/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………………” 29,929,000/=

Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………... “ 325,140,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* …………………..... “ 35,404,729,000/=

*(Vifingu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yeyote)*

## FUNGU 79 - MKOA WA MOROGORO

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……….. Sh. 620,000,000/=
Kif. 1005 - *DAS - Morogoro* ………………………. “ 10,000,000/=
Kif. 1006 - *DAS - Kilosa* …………………………... “ 5,000,000/=
Kif. 1007 - *DAS - Kilombero* ……………………….“ 5,000,000/=
Kif. 1008 - *DAS - Ulanga* ………………………..“ 5,000,000/=
Kif. 1009 - *DAS Mvomero*………………………….“ 5,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………….. “ 30,594,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Prod. Sector* ………. “ 60,088,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………….. “ 0/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………….“ 146,591,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………….“ 29,929,000/=

Kif. 3001 - *Regional Hospital* …………………….. " 30,000,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. " 26,002,006,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 80 – MKOA WA MTWARA**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* ……….. Sh. 375,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………….... " 25,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Prod. Sector* ………… " 48,103,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*……………………" 0/=
Kif. 2004 - *Social Sector* …………………………" 30,000,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………" 24,703,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* …………………….. " 265,988,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. " 19,166,232,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 81 – MKOA WA MWANZA**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* ………… Sh. 55,000,000/=

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….. “ 39,474,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ……. “ 47,990,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….. “ 406,246,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………“ 158,523,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*…………………………….... “ 29,929,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital*……………………… “ 0/=
Kif. 8091 - *Local Government*…………………….. “ 36,790,787,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 82 – MKOA WA RUVUMA

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……….. Sh. 366,019,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ……“ 68,547,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………... “ 22,000,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………“ 0/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………………“ 24,703,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………......” 0/=

Kif. 3002 - *Preventive Services*…………………….. “ 164,659,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………………. “ 19,104,799,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 83 – MKOA WA SHINYANGA

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……….. Sh. 35,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………….. “ 39,247,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …… “ 52,610,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*………..……….“ 1,222,919,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………“ 170,455,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………………“ 29,929,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………....“ 60,000,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ……………………“ 18,300,141,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 84 – MKOA WA SINGIDA

Kif. 1001 - *Admn. and HR Management* ……… Sh. 205,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*………….. “ 20,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ……“ 33,780,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….. “ 24,703,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* …………………….. ..“ 1,927,881,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. “ 15,450,256,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU - 85 MKOA WA TABORA**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* ………..Sh. 485,242,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*…………. ..“ 30,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …… “ 387,834,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*………………….. “ 29,929,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………” 0/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* …………………….... “ 146,591,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. “ 24,619,793,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 86 - MKOA WA TANGA

Kif. 1001- *Admin. and HR Management* ………. Sh. 274,231,000/=
Kif. 2001- *Planning and Coordination* …………… " 60,574,000/=
Kif. 2002- *Economic and Productive Sector* …… " 88,107,000/=
Kif. 2004- *Social Sector* …………………………….. " 0/=
Kif.2007-*Water Sector*………………………………….. " 29,929,000/=
Kif. 3001- *Regional Hospital* …………………..... " 272,386,000/=
Kif. 8091- *Local Government*…………………….. " 27,778,190,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 87 - MKOA WA KAGERA

Kif. 1001- *Admin. and HR Management* ……….. Sh. 485,500,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*……………....... " 30,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* …..... " 72,310,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*…………………….. " 75,000,000/=

Kif. 2004 - *Social* ……………………..........……………. “ 170,455,000/=
Kif. 2005 - *Local Government Services* …………….. “ 15,818,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………….. “ 29,929,000/=
Kif. 3001- *Regional Hospital*………………………….. “ 50,000,000/=
Kif. 8091- *Local Government* ………………….. “ 27,433,618,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 88 - MKOA WA DAR ES SALAAM

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* ………. Sh. 199,000,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination* ………….. “ 136,567,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ……“ 7,728,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector* ……………………“ 0/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………“ 110,795,000/=
Kif. 2007 - *Water Sector*………………………………” 18,567,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* …………………... “ 23,673,340,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 89 - MKOA WA RUKWA

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management*…….…... Sh. 382,899,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination* ……….……..“ 30,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ……... “ 49,980,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector* ……………….. “ 0/=
Kif. 2007 - *Water Sector*……………………………..... “ 24,703,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital*………………………... “ 134,659,000/=
Kif. 8091 - *Local Government* ………………….. “ 14,276,905,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 91 - TUME YA KUDHIBITI MADAWA YA KULEVYA

Kif. 1001- *Admin. and HR Management*…….. Sh. 1,180,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 92 - TUME YA KUDHIBITI UKIMWI - *TACAIDS*

Kif. 1001 - *Policy, Planning and National*

*Response*......................................Sh. 2,161,835,276/=

Kif. 1002 - *Finance, Admn. and Resource Mobilization* ......................................... " 3,032,137,506/=

Kif. 1003 - *Monitoring, Evaluation, Research and Mis*............................*Sh.* 1,099,361,000/=

Kif. 1004 - *Advocacy, Information, Education and Com* ......................................... " 1,718,260,700/=

Kif. 1005 - *District and Community Response*..... " 3,234,721,171/=

Kif. 1006 - *Procurement Management Unit*....... " 97,001,000/=

Kif. 1007 - *Legal Unit*...................................... " 664,046,325/=

Kif. 1008 - *Management Inf. Systems*................ " 783,378,660/=

Kif. 1009 - *Internal Audit Unit*.......................... " 401,100,000/=

Kif. 1010 - *Special programs*.......................... " 620,241,138/=

Kif. 1011 - *Government Communication unit*... " 1,532,252,224/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 95 - MKOA WA MANYARA**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management* ......... Sh. 646,295,000/=

Kif. 1005 - *DAS – Babati* ………………………… " 13,000,000/=
Kif. 1006 - *DAS –Hanang* …………………………… " 5,000,000/=
Kif. 1007 - *DAS –Kiteto* …………………………… " 76,500,000/=
Kif. 1008 - *DAS –Mbulu* ……………………………" 20,000,000/=
Kif. 1009 - *DAS –Simanjiro* …………………………… " 43,800,000/=
Kif. 2001 - *Planning and Coordination*……………… " 10,000,000/=
Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector* ………" 38,432,000/=
Kif. 2003 - *Infrastructure Sector* ……………………" 24,703,000/=
Kif. 2004 - *Social Sector* ……………………………" 176,591,000/=
Kif. 3001 - *Regional Hospital* ……………………… " 700,000,000/=
Kif. 8091 - *Local Government*…………………… " 17,713,452,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 56 - OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI

Kif. 1001- *Admin. and HR Management* ………..Sh. 250,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy, and Planning Division*………… " 0/=
Kif. 1004 - *Management Inf. System Division* …. " 327,096,000/=

Kif. 2001 - *Regional Administration Div………..* " 0/=
Kif. 2002 - *Legal Govent Coordination Div...…*" 16,014,537,000/=
Kif. 2003 - *Sector Coordination Division……….* " 905,288,000/=
Kif. 2004 - *Basic Educ. Cordination Division……*" 4,779,951,000/=
Kif. 3001- *Organization Development Division…………………..* " 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MBUNGE FULANI:** Mkoa wa Singida hujasoma

**SPIKA:** Waziri wa Nchi, Taarifa

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naambiwa Mkoa wa Singida haukutajwa.

**SPIKA:** Imesomwa.

**MBUNGE FULANI:** Haikutajwa.

**SPIKA:** Imesomwa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa

taarifa kwamba Kamati ya Matumizi baada ya kujadili taarifa ya Mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zilizo chini yake, na yale ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2012/2013, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2012/13 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kwa niaba yenu, kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Waziri Mkuu kwa kazi kubwa waliyoifanya. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge katika siku tano, haya tuliyopitisha, tungependa yaonekane katika vitendo, na hiyo ndiyo itaweza kutoa faraja kwa watu wengi sana. Kama tulivyosema, utaratibu wetu wa kupitisha Bajeti kwa kweli siyo rafiki kabisa, lakini kama tulivyotathmini mwanzoni mwa shughuli yetu hii, tunafikiri ipo haja sasa ya kubadilisha kwamba tuanze mapema kabisa

kushughulikia Wizara zote itakapokuwa inafika tarehe 30 Juni, tunamaliza ile Bajeti kubwa, na kuanzishwa kwa *Budget Office* yetu, nadhani kutabadilisha sana mfumo wa sasa hivi. Kwa kweli tunapitisha, lakini hatukuwa na amani nao kwa sababu sio rafiki hata kidogo. Maana suala la maendeleo lote limepita kwa *gillotine* kitu ambacho hakina afya njema sana.

Napenda kuwapongeza watalaam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zote zinazohusika, na Wakuu wa Mikoa, Ma-*RAS.* tunawaomba kabisa baada ya kupitisha bajeti hii mfanye kazi zinazostahili, mwaka mwingine tukija hapa, Waziri Mkuu awe na nafasi nzuri zaidi kuliko ile aliyokuwa nayo katika mwaka huu.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi tuliyofanya wiki hii, na pale tulipokwaruzana, basi wiki hii tusameheane tuanze wiki ijayo vizuri, maana yake hiyo ndiyo kazi tunayotakiwa kufanya, lakini tuongeze nidhamu ndani ya Bunge letu. Kila mtu akasome Kanuni yake. Leo nilikuwa napitia kifungu kinachohusiana na mawasiliano yetu na vyombo vya habari, vyote, ipo *very clear.* Nayo pia, kwa kuwa kazi yetu ni kuwaeleza wananchi kinachotokea hapa, ni lazima nishukuru Televisheni maana wanatuona vituko vyetu hapa, ingekuwa tunategemea kuandikwa tu, kwa kweli watu wasingetuelewa sana. Maana siku nyingine wanaandika tu. Kama habari ya kuwachambua watu, ukweli huu upo, lakini ukisoma Kanuni yetu hapa tunaweza sisi kuamua magazeti mengine yasiruhusiwe kuja hapa. Lakini bado tunakuwa wastaarabu kwa sababu tungependa sana wananchi wajue na kila mtu aandike kwa

*conciousness* yake, tusiandike vitu kwa sababu tunapenda kuandika.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nataka kutafsiri *Hansard* yangu ya jana, lakini muda umekwisha, tutafanya Jumatatu kuhusu suala alilouliza Mheshimiwa Machali jana. Kwa hiyo, baada ya kusema hivyo, kesho kama nilivyosema, ni wale tu wanaotakiwa kwenda kuweka alama za silaha waende, kesho ni siku ya mwisho.

Kuna Tangazo kutoka Ofisi yangu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sayansi na Teknolojia alipokuwa akijibu swali Bungeni aliahidi kuwaletea Waheshimiwa Wabunge taarifa ya maeneo yasiyo na mawasiliano ili yaweze kufanyiwa kazi. Anawatangaziwa Waheshimiwa Wabuneg kuwa taarifa hiyo tayari imewekwa kwenye *pigeon holes* zenu, hivyo kila Mbunge achukue nakala yake. Nadhani pia mnatakiwa kujaza mahali ambapo maeneo yanu simu hazifiki.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, naomba niahirishe kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.54 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu
Tarehe 2 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*